**2 NOVEMBA, 2023**

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI NA TATU**

**Kikao cha Tatu – Tarehe 2 Novemba, 2023**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, *ndc* – KATIBU WA BUNGE:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatayo ziliwasilishwa Mezani na: -

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST K.n.y MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI (PAC):**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali kuhusu Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Hesabu zilizokaguliwa za Serikali Kuu, Mashirika ya Umma na Kaguzi za Ufanisi kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2022.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA (LAAC):**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa kuhusu Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu

za Serikali kwa Hesabu zilizokaguliwa za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2022.

**MHE. VUMA A. HOLLE - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UWEKEZAJI WA MITAJI YA UMMA (PIC):**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma kuhusu Uwekezaji wa Mitaji ya Umma kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

**SPIKA:** Ahsante sana.

Katibu.

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, *ndc* – KATIBU WA BUNGE:**

## MASWALI KWA WAZIRI MKUU

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Maswali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu. Hata hivyo, leo Mheshimiwa Waziri Mkuu kama ambavyo Kanuni zetu zinaruhusu, atatoa taarifa ya jambo mahususi ambalo ameliandaa kwa ajili ya Taifa letu. Mheshimiwa Waziri Mkuu, karibu. *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Awali ya yote ninamshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema, ambaye ametuwezesha kushiriki Kikao hiki cha Tatu cha Mkutano wa Kumi na Tatu wa Bunge lako Tukufu tukiwa wazima wa afya.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaendelea, naomba niungane na Watanzania wenzangu, kukupongeza sana wewe kwa ushindi ulioupata na kuwa Mwanamke wa Kwanza kutoka Bara la Afrika kuchaguliwa kuwa Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani. Kuchaguliwa kwako kumeendelea kuiweka Tanzania katika ramani ya dunia. Ushindi huu ni udhihirisho wa Wazi wa jitihada za Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambaye anafanya kazi kubwa kuimarisha sauti na taswira ya Tanzania katika medani za uhusiano wa kikanda na kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kuwa, Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari, 2023 zimetoa fursa ya uwepo wa maswali ya papo kwa papo kwa Waziri Mkuu kwa siku ya Alhamisi. Vile vile, Kanuni hiyo hiyo katika kipengele cha 44(4) zimeruhusu Waziri Mkuu kutumia Kipindi cha maswali ya papo kwa papo, kutoa taarifa au ufafanuzi wa suala lolote linalohusiana na shughuli za Serikali na lenye maslahi kwa umma. Kwa msingi huo nimeona ni vema nitumie fursa hii kutoa taarifa kuhusu kuidhinishwa kwa Sera ya Elimu na Mafunzo 2014 Toleo la 2023 la Mitaala ya Elimu ngazi ya Elimu ya Awali, Msingi, Sekondari na Elimu ya ualimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge kwa kuzingatia uhitaji kwa wakati tofauti wamekuwa wakitoa maoni kuhusu umuhimu wa kuwepo mabadiliko katika Sera na Mitaala ya elimu nchini. Hivyo, nimeona ni vema kutoa taarifa hii ndani ya Bunge lako Tukufu kuhusu mabadiliko yanayofanyika katika Sera yetu ya Elimu na ni jambo ambalo lina maslahi mapana kwa taifa letu na kuwa muhimu wa kupata uelewa kutosha kuhusu maboresho hayo.

Mheshimiwa Spika, usimamizi na uendeshaji wa elimu na mafunzo nchini unaongozwa na Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014. Sera hii imegawanyika katika maeneo saba ambayo ni: -

(i) Mfumo wa elimu na mafunzo.

(ii) Fursa za Elimu.

(iii) Ubora wa Elimu na Mafunzo.

(iv) Rasilimali watu.

(v) Usimamizi na Uendeshaji.

(vi) Mfumo wa ugharamiaji na Masuala mtambuka.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Sera hii umebainika kuwa na changamoto mbalimbali zikiwemo Mfumo wa elimu kujikita zaidi kwenye elimu ya jumla na kukosa fursa za elimu mafunzo na

kuzingatia mahitaji, Njia mbalimbali za ujifunzaji kutokidhi kulingana na mazingira. Pia, Mitaala kutokidhi mahitaji ya mabadiliko ya kiuchumi, kijamii, kisayansi na teknolojia. Vile vile, mfumo usiofanisi wa udhibiti na ithibati ya elimu na upungufu wa nguvu kazi. Changamoto hizo zilizaa hitaji la kuboresha Sera yetu ya Elimu ili kukidhi mahitaji ya sasa na wakati ujao.

Mheshimiwa Spika, vilevile maboresho ya Sera hii ni utekelezaji wa maelekezo ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyoyatoa nyakati tofauti kuhusu kufanya mapitio ya Sera za Elimu mwaka 2014 pamoja na Mitaala ya elimu katika ngazi mbalimbali ili ijikite katika kutoa elimu ya ujuzi badala ya elimu ya taaluma pekee.

Mheshimiwa Spika, tarehe 22/4/2021 Mheshimiwa Rais alipohutubia Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alisema, naomba kunukuu "Tutajielekeza katika kufanya mapitlo ya Sera ya Elimu ya mwaka 2014 na kufanya marekebisho kwenye mitaala iliyopo, ili ijielekeze kwenye kutoa elimu ya ujuzi kulingana na mazingira ya nchi na soko la ajira." Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia maelekezo hayo ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Serikali imekamilisha mapitio ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 na kuanda Sera Mpya ya Elimu na Mafunzo ya 2014 Toleo la 2023.

Mheshimiwa Spika, Sera hii mpya imezingatia maelekezo ya Mheshimiwa Rais pamoja na maoni ya wadau mbalimbali wakishirikishwa wakati wa mapitio ya Sera hiyo, ikiwemo Waheshimiwa Wabunge wa Bunge lako Tukufu. Pamoja na uidhinishaji wa Sera, Serikali imekamilisha pia kazi ya mapitio ya mitaala ya elimu katika ngazi ya elimu ya awali, msingi, sekondari na rlimu ya ualimu. Mapitio ya mitaala na *program* mbalimbali katika ngazi ya elimu ya kati na elimu ya juu inaendelea.

Mheshimiwa Spika, vile vile, nitumie fursa hii kutoa taarifa kuwa, kwa sasa Serikali inaendelea na uandaaji wa taratibu za uzinduzi wa sera ya Elimu ya Mwaka 2014 Toleo la 2023. Baada ya kukamilisha taratibu hizo, tarehe ya uzinduzi itatangazwa. Aidha, Serikali inaendelea na maandalizi ya kuanza kwa utekelezaji wa

Sera na Mitaala iliyoidhinishwa kwa kuzingatia kalenda ya utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, mitaala mipya iliyoidhinishwa imejikita katika kuwajengea wanafunzi wetu ujuzi stahiki kwa ajili ya soko la ajira. Kwani, imetoa kipaumbele kwa stadi za amali katika kila ngazi ya elimu.

Mheshimiwa Spika, kiujumla maboresho yaliyofanyika yametokana na baadhi ya changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo mwaka 2014. Pamoja na changamoto hizo kulikuwa na mafanikio katika utekelezaji wa Sera hiyo ikiwemo:-

(i) Kuhuisha mitaala ya elimu ya awali, msingi sekondari, elimu ya ualimu, elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stani na elimu ya Juu kwa nyakati tofauti tofauti.

(ii) Imetoa elimu bila ada kwa shule za awali, msingi na sekondari.

(iii) Imetoa mwongozo wa kuwarejesha wanafunzi waliokatiza masomo kwa sababu mbalimbali na kuimarisha udhibiti ubora wa elimu na mafunzo.

(iv) Kuandaliwa na kutekelezwa kwa mfumo wa tuzo 2015 na kuhuishwa 2022.

(v) Kuandaa na kutekelezwa kwa Mkakati wa ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya Shule za msingi na sekondari wa Mwaka 2022.

(vi) Kununua na kusambaza vifaa vya kufundishia na kujifunzia ikiwemo vya wanafunzi wenye mahitaji maalumu na kuongeza bajeti ya sekta ya elimu kutoka trilioni 4.77 kwa Mwaka 2016/2017 hadi trilioni 5.26 kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, Mabadiliko ya msingi katika Sera ya Elimu na Mafunzoyaliyofanyika. Sera ya Elimu na Mafunzo imefanyiwa

mabadiliko kwenye maeneo kadhaa ikilinganishwa na sera iliyopita. Maeneo yenye mabadiliko ni pamoja na: -

(i) Elimu ya lazima kuwa ya miaka 10 badala ya miaka saba kama ilivyo sasa. Aidha, elimu hiyo ya lazima inajumuisha elimu ya msingi ya miaka sita na elimu ya sekondari ya chini ambayo itatolewa kwa miaka minne. Utekelezaji wa pendekezo hili utaanza kufanyika mwaka 2027 sambamba na kufuta mtihani wa darasa la saba na badala yake kuanza kufanyika kwa tathmini darasa la sita kwa ajili ya kujiunga na elimu ya lazima ya sekondari.

(ii) Kuongeza fursa za elimu ya amali, kwa maana ya elimu ya ufundi na mafunzo stadi. Elimu hiyo ya amali kuanza kutolewa kuanzia kidato cha kwanza.

(iii) Elimu ya ualimu kuanza kutolewa kwa wahitimu kidato cha sita na kuendelea.

(iv) Mafunzo ya ualimu kujumuisha mwaka mmoja wa mafunzo chini ya uangalizi *(internship)* bada ya kuhitimu mafunzo tarajali *(pre -service training)*.

(v) Kwenye upimaji, Serikali itahuisha mfumo wa upimaji na tathmini kwa kuzingatia mahiri zinazohitajika kwa kila ngazi, kwa lengo la kuwa na upimaji endelevu na matumizi ya mbinu mbalimbali za upimaji na tathmini ya maendeleo ya wanafunzi katika kujifunza.

(vi) Upatikanaji wa Vifaa vya vitabu. Serikali itatoa na kusimamia matumizi ya kitabu kimoja cha kiada kwa kila somo katika elimu ya msingi na sekondari ili kufanikisha upimaji wa matokeo ya ufundishaji na ujifunzaji unaofanana.

(iv) Ajira kwa walimu. Serikali itaboresha mfumo wa ajira za walimu, wakufunzi na wahadhiri kwa kuhakikisha kuwa wenye sifa na viwango stahiki, wanapata nafasi ya kuajiriwa.

(v) Vipaji maalumu. Serikali itaweka utaratibu wa kubaini na kuendeleza wanafuzni wenye vipaji na vipawa mbalimbali vinavyojitokeza miongoni mwao.

(vi) Gharama za elimu. Pamoja na kuendelea kutoa elimu bila ada katika elimu ya msingi kwenye shule za umma, Serikali kwa kushirikiana na wadau, itaendelea kuimarisha mfumo wa ugharamiaji wa elimu na mafunzo wenye vyanzo anuai katika ngazi zote. Aidha, Serikali itahakikisha katika taasisi zisizo za umma ada na michango katika ngazi mbalimbali za elimu inazingatia hali halisi ya uchumi, huduma zinazotolewa na taasisi na misingi ya elimu bora endelevu na uwekezaji katika sekta ya elimu.

Mheshimiwa Spika, mgawanyo wa majukumu utafuata sana mifumo ya kitaasisi iliyojengwa kisheria, na kwa kadiri ya utaratibu wa Serikali. Wizara yenye dhamana ya elimu pamoja na taasisi zake, itaendelea kuwa na wajibu wa kusimamia, kuratibu na kuimarisha upatikanaji na utoaji wa elimu na mafunzo nchini.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza majukumu yake, Wizara ina jukumu la kuandaa sheria, kanuni na miongozo ikiwemo uwekaji wa viwango vya ubora wa elimu na mafunzo.

Mheshimiwa Spika, Wizara yenye dhamana ya elimu, pia ina wajibu wa kuandaa mikakati na mipango ya sekta, ikiwa ni pamoja na kutafuta rasilimali mbalimbali kwa ajili ya utekelezaji na kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Sera hii. Aidha, Wizara yenye dhamana na TAMISEMI itakuwa na wajibu wa kuratibu na kusimamia tawala za mikoa zenye jukumu la kutekeleza Sera, kwa kutoa elimu na mafunzo katika ngazi ya awali, msingi na sekondari.

Mheshimiwa Spika, Wizara yenye dhamana na Utumishi, itahusika na upatikanaji wa rasilimali watu. Wizara yenye dhamana ya fedha, itahusika na utafutaji na upatikanaji wa rasilimali fedha. Tawala za mikoa zitasimamia utekelezaji wa Sera na miongozo ya utoaji elimu kwenye mamlaka za serikali za mitaa.

Mheshimiwa Spika, mamlaka za serikali za mitaa zitaendelea na utekelezaji wa Sera na hivyo kutoa huduma za elimu ili kuwafikia walengwa wote. Katika kutimiza azma hiyo, Serikali itaendelea kushirikiana na sekta binafsi, ikiwemo mashirika ya kidini, mashirika yasiyo ya kiserikali na wadau wengine walioamua kuwekeza kwenye elimu katika kuboresha upatikanaji na utoaji wa elimu na mafunzo hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, Hitimisho. Matarajio ya utekelezaji wa Sera hii ni kuimarisha uwezo wa nchi, kuandaa rasilimali watu kutokana na kuwepo kwa mfumo wa elimu ya mafunzo nyumbufu wenye tija na ufanisi na hivyo kuongeza idadi ya wananchi walioelimika na wenye ujuzi, kuendana na mahitaji ya taifa na ulimwengu wa kazi. Vile vile, kuongeza fursa za elimu na mafunzo na kuongezeka kwa matumizi ya teknolojia katika utoaji wa elimu na mafunzo.

Mheshimiwa Spika, marekebisho ya Sera hii yamehusisha wadau wa elimu na mafunzo nchini kwa njia mbalimbali, ikiwemo makongamano, madodoso na vikao kazi. Wadau hao ni pamoja na Waheshimiwa Wabunge kupitia Bunge letu, Wizara, wanafunzi wa shule za msingi na sekondari, vyuo vya kati na juu, kutoka taasisi za umma, sekta binafsi imehusishwa kwa kiasi kikubwa, walimu, wakufunzi na wahadhiri, viongozi wa vyama vya siasa, wazazi na walezi, wadhibiti ubora, taasisi za kidini, mashirika na asasi za kiraia.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya awamu ya sita inathamini sekta ya elimu katika kukuza uchumi wa nchi yetu na kupata rasilimali watu yenye ujuzi na taaluma mbalimbali. Serikali imefanya juhudi kubwa kuibadili sekta hii sambamba na kuboresha na kujenga miundombinu pamoja na shule mpya kwenye maeneo yaliyo na uhitaji zaidi wa shule za msingi na sekondari.

Mheshimiwa Spika, pamoja na ununuzi wa vifaa vya kisasa vya kujifunzia na kufundishia, Serikali imeendelea kuajiri walimu na itaendelea kuajiri walimu na kutoa ruzuku ya uendeshaji. Hivyo, natoa wito kwa wananchi wote kuunga mkono mabadiliko ya Sera hii na kushiriki kikamilifu katika utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, aidha nitumie fursa hii kuziagiza Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Ofisi ya Rais – TAMISEMI, kukamilisha mikakati ya maandalizi ya utekelezaji wa Sera hii pamoja na kusimamia miradi mikubwa ya elimu inayoendelea kutekelezwa kote nchini.

Mheshimiwa Spika, mafanikio ya utekelezaji wa Sera hii na malengo yake, inahitaji ushiriki wetu sote. Pia kwa kutambua umuhimu huo, Serikali itaendelea kutoa elimu kupitia majukwaa mbalimbali kuanzia sasa kwa namna ya kutekeleza Sera hii ili kuwa na uelewa mpana kwa Watanzania. Tutatumia njia mbalimbali namna itakavyoweza kueleweka vizuri bila kuwa na athari katika Mfumo wa Elimu nchini. Hivyo, nitoe rai kwa Wadau wa Maendeleo ya Elimu na jamii kwa ujumla kushiriki katika kutekeleza afua za elimu kwa kuzingatia maslahi mapana ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa sababu bado tuna muda kidogo na kanuni zinaruhusu mtu kukuuliza swali kuhusu hoja uliyoiweka mezani sasa hivi kuhusu jambo ambalo umelizungumzia. Kwa hiyo samahani nikurejeshe tena.

Waheshimiwa Wabunge wawili, watatu nitaruhusu maswali haya, halafu tutatazama kama muda unaruhusu nimeowaona wawili wengine.

Mheshimiwa Shangazi atafuatiwa na Mheshimiwa Husna Sekiboko. Mheshimiwa Shangazi.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa nafasi hii.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwanza nikupongeze sana kwa wasilisho zuri ambalo kwa kweli limekuja wakati muafaka katika kusimamia tasnia nzima ya Sekta ya Elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu ametaja wadau muhimu katika ushirika huu, lakini hadi hivi ninavyozungumza hakuna chombo maalum kinachoisimamia Sekta Binafsi ya Elimu,

hivyo kuwa na sauti ya pamoja pale inapotimiza majukumu yake ya kutoa elimu. Tutakumbuka kwamba shule za Serikali zipo chini ya TAMISEMI na zinapokea miongozo yote kutoka TAMISEMI, lakini Shule za Sekta Binafsi na Vyuo vya Sekta Binafsi na vya Kidini hawa hawana chombo ambacho kinawaunganisha kwa pamoja. Sasa nataka tu kufahamu kwamba ni upi mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba sekta hii nayo inakuwa na chombo ambacho inaweza ikakisimamia? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Shangazi, Mbunge wa Mlalo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Sera yetu ya Elimu imetoa nafasi kutekelezwa kupitia Sekta ya Umma ambayo ni ya Serikali, lakini pia Sekta Binafsi na ndio kwa sababu leo Taasisi za Kidini zimeanzisha shule za msingi, sekondari hata vyuo, mtu mmoja mmoja ameweza kuanzisha shule ya msingi, sekondari na vyuo na wote hawa wako kwenye utekelezaji wa Sera ya Elimu kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, sasa suala la chombo kwa Sera ya Elimu inavyotekeleza, Wizara ya Elimu ndio msimamizi wa sera na yeye ndio anayeshughulikia na udhibiti ubora wa elimu hapa nchini wakati usimamizi wa shughuli za kila siku kwa shule za msingi na sekondari inafanywa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Kwa hiyo matatizo yote na shughuli zote za Elimu ya msingi na sekondari zinasimamiwa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Wanapofanya hivi pamoja na Sekta ya Elimu ambayo inatambua Sekta Binafsi ambayo inafanya kazi ya kutoa elimu nchini inaingia kwenye utaratibu huo huo. Watatekeleza sera ya nchi, lakini pia watakaguliwa kwa mifumo iliyopo nchini, lakini utendaji wa kila siku utaendelea kufuatiliwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa sababu shule zote za msingi na sekondari za sekta binafsi ziko kwenye Halmashauri husika na msimamizi ni Mkurugenzi wa Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo Mkurugenzi na Idara yake ya Elimu wataendelea kufuatilia mwenendo wa utoaji elimu nchini kupitia Idara ya Elimu watakwenda kwenye shule za sekta ya

umma za Serikali watakwenda na kwenye shule za sekta binafsi ili kuona kuwa mwenendo wa utoaji wa elimu unakuwa mmoja na ndio kwa sababu wanafuata ratiba ya Serikali hata Sekta Binafsi, wanafanya mitihani ya Serikali chini ya Baraza la Mitihani pia ni pamoja na Sekta Binafsi.

Mheshimiwa Spika, hii sasa inaweza wakajua sasa sekta binafsi kwamba wanawajibika kwa Mkurugenzi wa Halmashauri husika. Suala la kuwa na chombo maalum cha sekta binafsi kwa kuwa tumesema shule za msingi, sekondari zote zinawajibika kwa Mamlaka ya Serikali za Mitaa hicho ndio Chombo chao ambacho inatakiwa kuripoti matatizo yao, mafanikio yao na kama kuna changamoto nyingine zozote zile wataripoti kwa Wakurugenzi wa Halmashauri. Shule hizo za Binafsi zinakaguliwa na Mkurugenzi wa Halmashauri kupitia chombo cha Wizara ya Elimu cha Udhibiti Ubora tulichokipeleka kwenye Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Spika, hii inafanya uendeshaji wa elimu kwa ujumla wake kuwa hauna matatizo na tumewaruhusu pia Sekta Binafsi kuanzisha umoja wao, watajadili mafanikio yao, watajadili mapungufu yao na watapeleka kwenye ngazi husika za Serikali pale ambapo wanaona kuna umuhimu wa kushirikiana na Serikali. Kwenye maboresho ya Sera hii ambayo leo tunaisoma hapa na kwamba tumeshakamilisha, tunasubiri kuzindua. Sekta Binafsi wameshirikishwa kikamilifu na waliitwa wote hapa Dodoma wamezungumza kwa pamoja, wamekubaliana, wamerudi wakiwa wameridhika na naamini wako Waheshimiwa Wabunge hapa nao wamejikita kwenye utoaji wa elimu na wao pia wanajua kwamba walishirikishwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, nataka niwahakikishie wadau wote wa utoaji elimu kwa Umma kwamba Sera yetu inalenga kufanya maboresho makubwa. Dhamira ya Rais wetu katika kuanzisha mchakato huu, lakini michango ya Waheshimiwa Wabunge imepelekea kukamilika kwa Sera hii na Wadau wa Sekta Binafsi ambao wamechangia, yote inapelekea kwenda kuimarisha Sera hii na iweze kutekelezeka. Kwa hiyo wajibu wetu sasa ni kuipokea na kuanza maandalizi ya kutekeleza Sera hii. Hayo ndio majibu ya msingi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Husna Sekiboko.

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwanza nikupongeze sana kwa Serikali kukamilisha mchakato huu na leo kutuletea rasmi kwamba nchi yetu inakwenda kutekeleza Sera na Mtaala Mpya, lakini Mheshimiwa Waziri Mkuu katika maelezo yako umeeleza kwamba Mtaala huu unakwenda kujikita katika Elimu ya Ujuzi. Hata hivyo, tuna upungufu mkubwa wa vifaa vya kufundishia katika *level* zote *primary, secondary* na Elimu ya kati kwa maana ya vyuo vya kati.

Je, Serikali inajipanga vipi kwenda kuhakikisha kwamba tunapata Makarakana na vifaa vya kufundishia vya kutosha ili kuweza kutekeleza mtaala huu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Husna, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tumeeleza kwamba elimu sasa isiwe ya kitaaluma pekee bali iingize masuala ya ujuzi kwa lengo la wanaomaliza elimu ya msingi hii ambayo imeenda mpaka kwenye sekondari ngazi ya chini, wanapomaliza wawe wana ujuzi ambao wanaweza wakaanza pia kuingia kwenye ujasiriamali moja kwa moja. Sasa Serikali imejipangje kupata vifaa vya kufundishia, tumeeleza kwenye Sera na kwa kuwa Sera itatekelezeka mwaka 2027, bado Serikali itaendelea kutafuta uwezo wa kuanza kununua vifaa na kupeleka kwenye maeneo haya.

Mheshimiwa Spika, sisi sasa tumeanza ujenzi wa *VETA,* Vyuo vya Ufundi, lakini pia tuna Vyuo vya Wananchi *(FDCs)* ambavyo pia vyenyewe vinatoa elimu ya ujuzi. Kwa hiyo kwa kipindi hiki cha mpito tunaanza kuimarisha Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi, Vyuo vyetu vya *VETA* ambavyo wanajenga kila Wilaya kwa lengo la kuanza kutoa ujuzi huku tukijipanga kutafuta vifaa na kupeleka kwenye shule zetu za sekondari. Kama Sera inavyosema mafunzo ya mali na ufundi tutaanza na kidato cha kwanza. Kwa hiyo tuta-*concentrate,* tutaongeza nguvu katika kutoa vifaa na hasa katika kuongeza bajeti na tutaleta maombi

yetu hapa kwenu Waheshimiwa Wabunge, naomba mridhie bajeti zetu ili tuweze kununua vifaa tupeleke sekondari na tutafanya hivyo awamu kwa awamu ili tufikie malengo ambayo tunayakusudia. Hii ndio namna ambayo tunakusudia kuitekeleza ili tuweze kufikia mafanikio, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Joseph George Kakunda.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Ningependa kumuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba hatimaye imehuishwa Sera ya Elimu ambayo ilizinduliwa kwa mara ya kwanza mwaka 2014 lakini mpaka inahuishwa tena haikuwahi kutekelezwa kwa sababu ilikosa nguvu ya sheria. Sasa kwa mahuisho haya yaliyofanyika sasa hivi, je, Serikali imejipanga lini kuleta Sheria ya Elimu mpya Bungeni ili kuyapa nguvu haya mahuisho ambayo yamefanyika?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kakunda, Mbunge wa Sikonge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli hata Sera ya mwanzo tulipokuwa tunatekeleza tulikuwa na Sheria inasaidia, inaongoza utekelezaji wake, lakini kutokana na mabadiliko haya tumegusa maeneo yanayohitaji mabadiliko ya kisheria pia ili Sera hii iweze kutekelezeka; na kwa kuwa tunaelekea kwenda kuizindua na Wizara ya Elimu inaendelea na mchakato wa kusimamia maboresho ya Sera hii mpaka kuzinduliwa na utekelezaji wake, tutaendelea kubaini maeneo muhimu ya kubadilisha Sheria ili tuweze kutunga Kanuni ili ziweze kuwezesha urahisi wa utekelezaji wa Sera hii. Kwa hiyo Wizara ya Elimu imejipanga, inaendelea na mchakato na nimetoa wito hapa na nimeeleza kwamba, bado tunaendelea kutoa elimu kwa njia mbalimbali, kushirikisha wadau wote. Kwa hiyo hii hatua tunayoendelea nayo ya kila hatua itakuwa inabaini kadiri ya mahitaji ya mabadiliko ya sheria na kutengenezea kanuni za usimamizi wa utekelezaji wa sera hiyo, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, swali.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kumuuliza Waziri Mkuu swali la nyongeza.

Mheshimiwa Waziri mmefanya kazi kubwa sana kupunguza miaka kutoka 11 sasa na kuwa 10 kwa maana ya miaka sita na miaka ile minne ya lazima, lakini kuna mzigo mkubwa sana wa masomo mengi kwa watoto wa shule za awali. Je, kuna utaratibu gani ambao Serikali imeuona wa kupunguza idadi ya masomo lakini *quality* ikabaki palepale? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, Mbunge wa Mbeya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Elimu ilipokuwa inatekeleza Sera hii ambayo tunaimalizia muda wake iliaandaa masomo kulingana na uhitaji. Sasa mabadiliko ya sera hii nayo yataangalia mzigo huo na kwa kuwa wadau walishapata nafasi ya kuchangia tunaamini hili nalo walishalisema na Wizara ya Elimu imechukua maoni yote yaliyotolewa na wadau katika kuhakikisha kuwa mzigo huu unapungua na utaratibu ambao upo kwa madarasa ya awali yanayomwandaa mwanafunzi kuingia darasa la kwanza wale masomo yao ni kusoma, kuhesabu na kuandika.

Mheshimiwa Spika, walikuwa wanaandaliwa hivyo kwa kipindi chote cha mwaka mmoja au miwili kulingana na umri wa mtoto. Wanamwandaa kujua kuandika, kusoma na kuhesabu ili aingie darasa la kwanza akiwa anajua kuhesabu, kuandika na kusoma na anapoingia kwa darasa la kwanza, la pili anaanza sasa kuingia masomo ya shule za msingi. Hapa sasa sera na michango ya wadau watakuwa wameshapitia hayo na ushauri upo Wizara ya Elimu, kuona ni masomo yapi yafundishwe kutoka darasa la kwanza mpaka la sita na pia yataangalia uzito na umuhimu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuwa sasa tunawaandaa kwa ajili ya kuingia kwenye mafunzo ya sekondari, lazima watafanya mapitio tena ya masomo haya ili kutoa idadi ya masomo ambayo yataweza kubebwa na kijana huyu wa umri huu ambaye

anasoma mpaka darasa la sita ili kumfanya awe na uelewa mpana na wa haraka zaidi, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Muda wa maswali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu umekwisha, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, *ndc* – KATIBU WA BUNGE:**

## MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA:** Maswali ya kawaida Waheshimiwa Wabunge tutaanza na Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Mheshimiwa Esther Lukago Midimu, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 30

### Ujenzi wa Vituo vya Afya Wilaya ya Itilima

**MHE. ESTHER L. MIDIMU** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga Kituo cha Afya katika Kata za Luguru na Sawida Wilayani Itilima?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa Mheshimiwa Dkt. Festo John Dugange, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Esther Lukago Midimu, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na ujenzi wa vituo vya afya katika kata za kimkakati zenye idadi kubwa ya watu na umbali mrefu kutoka kituo cha karibu cha huduma.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022 hadi Septemba 2023, jumla ya vituo vya afya 348 vimejengwa nchini kote. Kazi ya ujenzi huu ni endelevu hivyo tathmini ya vigezo kwa Kata za Luguru na Sawida itafanyika na kuingizwa kwenye mipango ya ujenzi, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Esther Lukago Midimu, swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER L. MIDIMU:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza. Kwanza kabisa nimpongeze Naibu Waziri kwa majibu mazuri.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kujenga Vituo vya Afya na Hospitali za Wilaya tena nzuri za kisasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kata ya Luguru ni kata yenye idadi ya watu wengi, kituo cha afya kikijengwa Kata ya Luguru kitahudumia Kata ya Sawida na Kata ya Kinamweli. Je, Serikali ina mpango gani wa kuharakisha ujenzi wa kituo cha afya Kata Luguru?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; vituo vya afya vya Mkoa wa Simiyu na hospitali za wilaya tuna upungufu wa vifaa tiba na Watumishi.

Je, ni lini Serikali itatuletea vifaa tiba vya kutosha na watumishi wa kutosha? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, Mheshimiwa Esther Lukago Midimu, kwamba tayari Serikali ilishamwelekeza Katibu Tawala wa Mkoa na Mganga Mkuu wa Mkoa wa Simiyu pia na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Itilima kuwasilisha maombi ya ujenzi wa Kituo cha Afya cha Luguru ili tuweze kuandaa fedha kwa ajili ya kwenda kuanza ujenzi katika kituo hicho cha afya.

Mheshimiwa Spika, pili, Serikali imeendelea kupeleka vifaa tiba pia imeendelea kuajiri watumishi wa sekta ya afya na kuwapeleka katika Halmashauri zetu kote na Halmashauri ya Wilaya ya Itilima ni moja ya Halmashauri ambazo tayari zimepelekewa zaidi ya shilingi bilioni moja ya fedha kwa ajili ya vifaa tiba. Pia imeshapelekewa Watumishi wa Sekta ya Afya na nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kila mara ambapo fedha itapatikana itaendelea kupelekwa kwa ajili ya vifaa tiba, lakini pia Watumishi wataendelea kupelekwa Itilima, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Simon Songe Lusengekile, Mbunge wa Busega, sasa aulize swali lake.

Na. 31

**Ujenzi wa Wodi Vituo vya Afya – Busega**

**MHE. SIMON S. LUSENGEKILE** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga Wodi ya Akinamama, Watoto na Wanaume katika Vituo vya Afya Lukungu - Lamadi na Kiloleli?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Simon Songe Lusengekile, Mbunge wa Jimbo la Busega, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Vituo vya Afya vya Lukungu na Kiloleli ni miongoni mwa vituo vilivyosajiliwa na kuanza kutoa huduma vikiwa na upungufu wa miundombinu ikiwemo Wodi ya Wazazi, Jengo la Upasuaji na Maabara.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutenga bajeti kwa awamu kwa ajili ya ukarabati na upanuzi wa miundombinu inayopungua kwenye vituo vya afya kote nchini vikiwemo Vituo vya Afya vya Lukungu na Kiloleli, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Simon Songe Lusengekile, swali la nyongeza.

**MHE. SIMON S. LUSENGEKILE;** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi kuuliza swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, Kata hizi mbili ambazo nimezitaja na vituo vya afya ambavyo nimevitaja vina wananchi wengi na vinahudumia wananchi wengi sana katika vituo hivi.

Je, Serikali sasa haioni sababu za kuwa na mpango wa haraka ili kuharakisha ujenzi wa wodi hizi ambazo nimezitaja ili wananchi waweze kupata huduma wasisafiri umbali mrefu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, ni kweli Kituo cha Afya cha Lukungu na Kiloleli ni miongoni mwa vituo vya afya ambavyo vinahudumia wananchi wengi sana na kwa kutambua hilo, tayari Serikali imekwishaainisha vituo vya afya vyote ambavyo vina miundombinu pungufu na vinahudumia wananchi wengi ili fedha iweze kutafutwa kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tunaongeza miundombinu ambayo inapungua.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Songe kwamba Kituo cha Afya cha Lukungu tayari kimeingizwa kwenye mpango huo na mara fedha ikipatikana tutahakikisha tunaenda kujenga miundombinu hiyo, ahsante

**SPIKA:** Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso, Mbunge wa Mpanda Vijijini, sasa aulize swali lake.

Na. 32

**Walimu wanaojitolea kupewa kipaumbele katika ajira**

**MHE. MOSHI S. KAKOSO** aliuliza:-

Je, upi Mkakati wa kuwapa kipaumbele cha ajira walimu wanaojitolea katika shule za msingi na sekondari pindi ajira zinapotoka?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso, Mbunge wa Jimbo la Mpanda Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imeandaa mwongozo wa kuwatambua Walimu wanaojitolea katika shule zote nchini. Mwongozo huo umeipa Ofisi ya Rais, TAMISEMI jukumu la kuandaa mfumo wa Walimu wanaojitolea. Kwa sasa mfumo huo unaendelea kuandaliwa, utakapokamilika Walimu watajulishwa ili waanze kufuata utaratibu wa kujisajili katika mfumo huo ili kurahisisha utambuzi wao, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Selemani Moshi Kakoso, swali la nyongeza.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa idadi ya walimu wanaojitolea ni wengi na ajira zinapotoka huwa hawapati nafasi ya kuajiriwa hawa ambao wamejitolea. Halmashauri yangu ina zaidi ya walimu 60 ambao wamejitolea na waliopata ajira wamepata walimu watatu tu.

Je, Serikali haioni kwamba inavunja moyo wale walimu wanaojitolea na wanaopata ajira ni wale ambao wapo mitaani? Tunataka tupate mwongozo sahihi wa Serikali na majibu stahiki kwa wale ambao wanajitolea. *(Makofi)*

Swali la pili, kuna tabia ambayo imejengeka ajira zinapotolewa Halmashauri ambazo ziko vijijini zinapokea watumishi ndani ya miezi mitatu wale watumishi wote wanarudi maeneo ya mijini; Serikali haioni hii tabia ambayo imejengeka ni tabia ambayo inakuja kuua mfumo wa elimu au utumishi wa umma kwenye maeneo ya vijijini? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, kwanza nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali imeendelea kuajiri watumishi wote bila kujali wanaojitolea na ambao hawajitolei. Changamoto ya kuajiri walimu wanaojitolea ilitokana na utaratibu ambao haukuwa rasmi wa kuwasilisha majina ya walimu wanaojitolea. Kwa sababu baadhi ya Wakuu wa Shule wasio waaminifu walikuwa wanatumia fursa hiyo kuingiza majina ya walimu ambao hawajitolei na mara nyingine wanaachwa walimu wale ambao wanajitolea.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua hilo Serikali imeandaa mwongozo mahsusi na imeandaa mfumo ambao walimu wenyewe wataingia *online* kuji-*register,* kujiandikisha kwamba ni walimu wanaojitolea katika shule fulani na Serikali itafanya uhakiki na kuthibitisha kwamba walimu wale wanajitolea katika maeneo hayo. Hii itasaidia mara ajira zinapojitokeza kuona nani amejitolea kwa muda mrefu apate kipaumbele cha kupata ajira hizo. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba hili jambo linafanyiwa kazi *seriously* na Serikali itahakikisha kwamba linakamilika mapema iwezekanavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili kuhusiana na walimu pia watumishi wa sekta nyingine ambao wanapangiwa katika Halmashauri za Vijijini na kuhama, kwenye utaratibu wa ajira kwa mfumo wa kieletroniki kwa sasa, tumeshaelekeza kwamba watumishi wote wa elimu au wa afya wakishaajiriwa kwenye Halmashauri hawatakiwi kuhama ndani ya angalau ya miaka mitatu tangu kuajiriwa. *Unless* kuna sababu ya msingi sana ya kulazimisha

watumishi hao kuhama. Kwa hiyo, nitumie nafasi hii kwanza kuwaomba Waheshimiwa Wabunge wale maeneo ambayo kuna watumishi ambao waliajiriwa maeneo ya vijijini na wamehamishwa kabla ya umri huo tupate taarifa hizo. Tumeshapata Ludewa tumeshapata maeneo mengine, tumeanza kushughulikia na watarejeshwa katika Halmashauri zilezile ili waendelee kutoa huduma kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo hili tunalifanyia kazi, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ile sehemu ya kwanza ya wale wanaojitolea ambao inabidi wapewe kipaumbele, Serikali imeahidi mara kadhaa wakati maswali haya yakijibiwa na upande wa Utumishi na TAMISEMI. Nafikiri ni muda sasa na ninyi mjipangie muda kwamba hilo suala mtalifanya kwa muda gani ili ajira zinapoanza kutangazwa basi tujue kwamba ni ndani ya mwaka, miaka miwili, mitatu itatusaidia, kwa sababu hili swali linajirudia kila wakati ili wanaojitolea wasikatishwe tamaa kuendelea kujitolea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Dkt. John Danielson Pallangyo, Mbunge wa Arumeru Mashariki, sasa aulize swali lake.

Na. 33

**Wananchi kupatiwa ardhi mbadala**

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO** aliuliza: -

Je, upi mkakati wa kuwapa Wananchi ardhi mbadala wanapoondolewa kwenye maeneo yao kupisha uhifadhi na miradi ya mkakati?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Jerry William Silaa, majibu.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. John Danielson Pallangyo, Mbunge wa Arumeru Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri, kunakuwepo na ulazima wa wananchi kuachia ardhi pale ardhi inapohitajika kwa matumizi ya umma. Mahitaji hayo ni pamoja na ardhi ya uhifadhi na ardhi kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya kimkakati.

Mheshimiwa Spika, mfumo wa sheria nchini, umeweka wazi juu ya takwa na haki ya wamiliki wa ardhi kulipwa fidia ya ardhi na maendelezo pale ardhi inapotwaliwa kwa matumizi ya umma. Aidha, sheria inaruhusu fidia hiyo kulipwa kwa fedha taslimu au kupatiwa ardhi mbadala. Pamoja na sheria kuruhusu wananchi kupewa ardhi mbadala pindi ardhi yao inapotwaliwa, wananchi wamekuwa wakipendelea fidia ya fedha badala ya ardhi mbadala ili kuwawezesha kutafuta maeneo mengine wanayoyahitaji. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Pallangyo, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kunipa tena nafasi niulize swali la nyongeza, kwanza nitoe shukurani nyingi kwa majibu mazuri ya Serikali kupitia kwa Waziri wa Ardhi, Mheshimiwa Jerry Silaa ambaye alikuwa Mwenyekiti wangu Kamati ya *PIC*, nimpongeze kwa kuwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali langu majibu yake yapo sawasawa lakini watendaji wakati wa kutekeleza huwa hawaweki bayana sheria inasemaje badala yake wanakuja wanakuambia jamani hili eneo linachukuliwa kwa ajili yakazi hii na hii ya Serikali ninyi mnatakiwa muondoke, mtapata fidia kwa maendelezo ambayo mlikuwa mmefanya.

Je, Serikali haioni sasa kwamba ni muhimu wakati wa kuhamisha wananchi kwenye maeneo yao watoe maelekezo

kwamba watapata nini na nini kulingana na eneo ambalo linachukuliwa *either* kwa uhifadhi au utekelezaji wa miradi?

Pili, kule kwangu nina wahanga wa uhamisho Eneo la Momela, Kitongoji cha Momela wanapaswa wahame kwa ajili ya uhifadhi lakini pia Kata ya Maroroni, Kijiji cha Samaria…

**SPIKA:** Swali lako Mheshimiwa maana naona hayo maelezo ya mwanzo ni mchango. Swali lako?

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Spika, swali langu ni je, Waziri utakuwa tayari kuambatana na mimi tuende tukafanye mkutano uwaeleze wananchi maeneo ya Momela pamoja na *KIA* ambao wanatakiwa wahame, ninakushukuru sana.

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa majibu kwa maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa John Danielson Pallangyo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, naomba kutumia Bunge lako tukufu kuagiza Wathamini wote na Ofisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali kuhakikisha inatoa elimu stahiki kwa wananchi pindi ambapo maeneo yao yanatwaliwa kwa ajili ya miradi mbalimbali ya maendeleo. Wananchi waelezwe wazi takwa la sheria kwa wale wanaotaka kuchukua fedha taslimu kwa niaba ya ardhi yao na kwa wale ambao wanataka kutafutiwa ardhi mbadala.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili, pamoja na kwamba niko tayari kuongozana na Mheshimiwa Dkt. John Pallangyo lakini eneo la *KIA* na eneo la Momela ni maeneo ambayo yanaangukia kwenye vile vijiji 975 ambapo wananchi walikuwa wameingia kwenye maeneo ya hifadhi na wengine wameingia kwenye eneo la Uwanja wa Ndege wa *KIA*. Serikali inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan iliona ni busara kuwafidia kwa yale maendelezo waliyoyafanya, maeneo haya fidia yao wanayolipwa haihusishi ardhi ambayo wamekuwa wakiikalia. Baada ya Bunge hili Mheshimiwa Dkt. Palangyo tutaongozana

pamoja kwenda kutoa elimu kwa wananchi wa Jimbo lako, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Suma Ikenda Fyandomo, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 34

**Uhitaji wa Mwenyekiti wa Baraza la Ardhi Rungwe**

**MHE. SUMA I. FYANDOMO** aliuliza:-

Je, lini Wilaya ya Rungwe italetewa Mwenyekiti wa Baraza la Ardhi?

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Suma Ikenda Fyandomo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi imeendelea kuajiri Wenyeviti wa Mabaraza ya Ardhi ili kuongeza kasi ya kusikiliza na kuamua mashauri ya ardhi. Mwenyekiti wa Baraza la Ardhi la Wilaya ya Rungwe ameteuliwa na kupangiwa kituo tarehe 18 Septemba, 2023 na tayari ameanza kazi. Nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Suma Fyandomo, swali la nyongeza.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, ninaipongeza sana Serikali ya Awamu ya Sita ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwamba ni sikivu sana, kwa sababu niliuliza hili swali la imelitekeleza. Nina maswali mawili ya nyongeza.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuyaelimisha Mabaraza ya Kata ili yasitoe hukumu kwenye mashauri ya ardhi?

Swali langu la pili, katika Wilaya ya Chunya hakuna kabisa Baraza la Ardhi, ukizingatia wananchi wa Chunya wanatoka Kambikatoto, Kipambawe, Mafieko, Bintimanyanga, Matwiga, Luhanga, Ifumbo na Shoga wanakwenda kushtaki mashauri yao kwenye Jiji la Mbeya.

Je, ni lini Serikali itawaepushia shida hiyo wananchi wa Wilaya ya Chunya?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, Mabaraza ya Ardhi ya Kata yameanzishwa chini ya Sheria Sura ya 206 na kupitia Bunge lako Tukufu kwenye Marekebisho ya Sheria Namba 3 ya Mwaka 2021 Mabaraza haya yalipunguziwa nguvu ya kimaamuzi na yanapaswa kufanya usuluhishi ndani ya siku 30 baada ya shauri kufikishwa.

Mheshimiwa Spika, tuliongea na Waandishi wa Habari lakini naomba kutumia Bunge lako Tukufu kuwatangazia wananchi wote kwamba Mabaraza ya Ardhi ya Kata nguvu yake ya kisheria ni kufanya usuluhishi ndani ya siku 30 tokea shauri lifikishwe mbele yake. Baada ya hapo kama usuluhishi utashindwa kufanyika mashauri yawasilishwe kwenye Mabaraza ya Ardhi ya Wilaya. Ninaomba tena kupitia Bunge lako, Wakurugenzi wa Halmashauri maana Mabaraza ya Ardhi ya Kata yanasimamiwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI na Wakurugenzi wa Halmashauri wanasimamia kwa niaba yake, Waendelee kusimamia mabaraza haya ili wananchi waendelee kupata haki zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, ni kweli kati ya Mabaraza ya Wilaya zote 139 ni Mabaraza 94 tu ndiyo yenye Wenyeviti wa Baraza la Wilaya. Tayari ofisi yangu imeendelea kufanya mawasiliano ya kuomba vibali vya ajiri kwa ajili ya kupata ajira ya kuajiri Wenyeviti wengine 45, lakini kwenye maeneo yote ikiwemo Wilaya ya Chunya kwenye maeneo aliyotaja Mheshimiwa Mbunge ikiwemo Maeneo ya Bintimanyanga na maeneo ya Shoga tunaendelea kutoa maelezo kwa Msajaili wa Baraza la Ardhi la Wilaya kutumia Wenyeviti wa Mabaraza ya Ardhi ya Wilaya ya jirani kwenda kwenye mabaraza haya kwenda kusikilza

mashauri mpaka pale Serikali itakapokamilisha Wenyeviti kwenye Mabaraza ya Wilaya zote, ninakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Maji, Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 35

**Kuvunjwa kwa Mradi wa Maji wa *KAVIWASU* – Karatu**

**MHE. CECILIA D. PARESSO** aliuliza:-

Je, kwa nini Serikali ilivunja Mradi wa Maji wa *KAVIWASU* katika Mji wa Karatu bila kuwashirikisha wananchi?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Maji Namba 5 ya mwaka 2019 ya Usambazaji wa Maji na Usafi wa Mazingira kupitia kifungu Na. 13(1)(b) vyombo vya watumia maji vinaruhusiwa kutoa huduma za maji kwa wananchi katika maeneo mbalimbali nchini ambapo chombo cha watumia maji cha *KAVIWASU* kilikuwa kinatoa huduma kwenye baadhi ya maeneo ya Mji wa Karatu.

Mheshimiwa Spika, katika kuboresha huduma ya maji kwenye Mji wa Karatu, Serikali iliunganisha vyombo viwili vya kutoa huduma ya maji vya *KARUWASU* na *KAVIWASU* kuwa chombo kimoja ambacho mpaka sasa kimeendelea kutoa huduma ya maji kwa ufanisi katika eneo lote la Mji wa Karatu. Uundaji wa chombo hicho ulishirikisha wananchi ambapo Wizara ilifanya majadiliano ya kina na Mamlaka za Serikali, Wawakilishi wa Wananchi wa Karatu na wadau wa maji na kufikia maamuzi ya kuviunganisha vyombo hivyo viwili ili kiwepo chombo kimoja

madhubuti kitakachosimamia utoaji wa huduma endelevu na kuondoa mkanganyiko wa bei za huduma.

**SPIKA:** Mheshimiwa Cecilia Paresso, swali la nyongeza.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, mchakato wa uvunjwaji wa Bodi hii haukishirisha wananchi na hapa mmekiri mlienda kwenye Mamlaka ya Serikali, kwa wawakilishi wa wananchi lakini hamkufika kwa wananchi. Je, ni lini mtafika kwa wananchi na kuwapa sababu za kwa nini mlivunja mradi huu? *(Makofi)*

Swali la pili, mmeeleza kwamba baada ya chombo hiki kuundwa kuna ufanisi wa maji, naomba niwaambie Wizara hakuna ufanisi wowote matokeo yake tumerudi kwenye adha kubwa ya ukosefu wa maji katika Mji wa Karatu. Ni lini na kwa haraka mtarekebisha tatizo hili ili wananchi waweze kupata maji kwa uhakika? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Cecilia Paresso, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, naomba nirudie tena Mheshimiwa Waziri yeye mweyewe, Jumaa Hamidu Aweso na Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo walishirikiana na Waheshimiwa Madiwani waliweza kushirikisha wananchi. Kama wananchi hawakupata taarifa wote basi kuendelea kutoa elimu ni moja ya jukumu la Wizara, kwa hiyo tutaendelea kutoa elimu kwa sababu dhamira ya Wizara ni njema kabisa, lengo la kuunganisha hivi vyombo ni kupunguza mzigo wa gharama za bei kwa wananchi na kabla ya kuviunganisha mwananchi aliweza kulipia *unit* ya maji shilingi 2,000 na baada ya kuviunganisha tunamshukuru sana Mheshimiwa Waziri alihakikisha bei zimeshuka na sasa hivi ni shilingi 1,300.

Mheshimiwa Spika, kuonesha ufanisi mkubwa wa mradi wa huduma ya maji, tayari Wizara, Karatu tumeiangalia kwa jicho la kipekee kabisa na tayari kazi zinaendelea, tutahakikisha huduma ya maji Karatu wataendelea kuboreshewa lengo ni kupata maji safi na salama bombani yakiwa ya kutosha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mheshimiwa Mwanakhamis Kassim Said, Mbunge wa Magomeni, sasa aulize swali lake.

Na. 36

**Ushirikiano wa *TFF* na *ZFF***

**MHE. MWANAKHAMIS KASSIM SAID** aliuliza:-

Je, *TFF* inashirikianaje na *ZFF* kupandisha hadhi Ligi ya Zanzibar na kuendeleza vipaji vya wachezaji wa Zanzibar?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mheshimiwa Hamis Mwinjuma, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, nakushukuru, kwa niaba ya Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mwanakhamis Kassim Said, Mbunge wa Jimbo la Magomeni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania *(TFF)* chini ya Bodi ya Ligi Kuu Tanzania *(TPLB)* imekuwa ikishirikiana na *ZFF* katika mipango mbalimbali kwa lengo la kuendeleza Soka la Tanzania. Kwa sasa Bodi ya Ligi ipo katika mchakato wa kuandaa mafunzo ya uendeshaji wa Bodi ya Ligi ya Zanzibar ambayo kimsingi yatalenga namna ya uendeshaji wa Bodi ya Ligi katika masuala ya menejimenti, ligi na masuala ya uwekezaji, udhamini na masoko.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa kuibua vipaji, *TFF* imekua ikishirikiana na *ZFF* katika uteuzi wa wachezaji katika timu za Taifa

za Vijana, ambapo vijana kutoka Zanzibar wamekuwa wakiitwa katika vikosi vya timu ya Taifa ya vijana na hatimaye kucheza katika timu ya Taifa ya wakubwa *(Taifa Stars),* ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwanakhamis Kassim Said, swali la nyongeza.

**MHE. MWANAKHAMIS KASSIM SAID:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii na mimi kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuirejesha Ligi ya Muungano?

Swali langu la pili, je, ushirikiano wa *ZFF* na *TFF* unasaidia Soka la Zanzibar la Wanawake? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Ninapenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mwanakhamis Kassim Said, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza Serikali inayo dhamira ya dhati ya kuhakikisha Ligi ya Muungano inaanzishwa upya na tunafahamu umuhimu wake kwenye kuimarisha ushirikiano hasa kwenye upande wa michezo. Kwa hivyo, kwa nyakati tofauti *TFF* na *ZFF* wamekuwa wakikaa kuangalia namna bora ya kuianzisha tena Ligi ya Muungano, japokuwa wanapata changamoto kwenye kupata udhamini wa kulifanya hili lakini nikuhakikishie dhamira ipo na tutahakikisha Ligi ya Muungano inaanza tena.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili kuhusu Ligi ya Wanawake, *TFF* na ZFF zimekuwa zikiendesha *program* mbalimbali za kiutawala na makocha wanawake kwa Soka la Zanzibar na unaweza kuona miongoni mwa mafanikio ambayo yameshapatikana ni kwa timu za wanawake za Zanzibar kufanya vizuri kwenye mashindano ya *CECAFA*. Nakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Dkt. Alfred James Kimea, Mbunge wa Korogwe Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 37

**Ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji Korogwe**

**MHE. DKT. ALFRED J. KIMEA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga miundombinu ya umwagiliaji katika mabonde ya mpunga ya Kwamgumi na Kwamsisi - Korogwe?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa Niaba ya Waziri wa Kilimo, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Alfred James Kimea, Mbunge wa Korogwe Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Korogwe ina zaidi ya skimu 64 zilizoendelezwa na ambazo hazijaendelezwa ikiwemo Skimu ya Kwamgumi inayokadiriwa kuwa na ukubwa wa hekta 210 na Kwamsisi yenye ukubwa unaokadiriwa kufika hekta 1,500.

Mheshimiwa Spika, katika skimu ya Kwamgumi Serikali imefanya uwekezaji wa awali kwa kufanya ujenzi wa mfereji mkuu wenye urefu wa kilomita tatu. Aidha, Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imefanya ukaguzi na tathmini ya awali kwa ajili ya kufanya ukarabati na uendelezaji wa miundombinu ya umwagiliaji katika skimu hii, ikiwemo usakafiaji wa mifereji ya kupitisha maji kwa ajili ya umwagiliaji. Hivyo basi, upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa Skimu ya Kwamgumi utaingizwa katika mpango na bajeti ya Tume ya Taifa ya Umwagiliaji katika mwaka wa fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2023/2024 Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji ina mpango wa kujenga miundombinu katika Skimu ya Kwamsisi. Aidha, mchakato wa manunuzi kwa ajili ya kumpata Mkandarasi wa kufanya ujenzi katika skimu hii umeanza.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Alfred Kimea swali la nyongeza.

**MHE. DKT. ALFRED J. KIMEA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii kuuliza swali la nyongeza. Pia napenda kuipongeza Serikali kwa majibu yake mazuri na yenye kutia matumaini kwa wananchi wa Kata ya Kwamsisi pamoja na Kwamngumi kwa kuwa hiki kilikuwa kilio chetu sisi sote.

Mheshimiwa Spika, swali langu la nyongeza, ninahitaji *commitment* ya Serikali kwamba ni kweli mwaka huu tutaenda kujengewa Skimu hii ya Kwamsisi na mwakani tutaenda kujengewan Skimu ya Kwamngumi maana imekuwa ahadi ya siku nyingi. Kwa hiyo, naomba *commitment* ya Serikali kwamba jambo hili linaenda kutokea mwaka huu na mwaka ujao.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kama ambavyo nimejibu katika jibu la msingi, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Korogwe Mjini, ahadi ya Serikali tulivyoahidi hapa itatekelezeka kwa asilimia mia moja. Hiki ninachokizungumza, nina uhakika nacho, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi, Mbunge wa Mlalo, sasa aulize swali lake.

Na. 38

**Serikali kupanua Soko la Kahawa**

**MHE. RASHID A. SHANGAZI** aliuliza:-

Je, kuna mpango gani wa kuongeza mnyororo wa thamani wa zao la Kahawa ikiwa ni miongoni mwa mikakati ya kukuza soko la Kahawa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi, Mbunge wa Jimbo la Mlalo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Tasnia ya Kahawa inatekeleza mkakati wa miaka mitano wa Maendeleo ya Tasnia ya Kahawa (2021 - 2025). Moja ya malengo ya mkakati huo ni kuongeza thamani ya kahawa kutoka 7% za sasa mpaka 15% ya kahawa yote inayozalishwa nchini.

Mheshimiwa Spika, katika kupunguza utegemezi wa soko la nje, Serikali imeweka mazingira mazuri ya kuvutia uwekezaji kwenye viwanda vya kuongeza thamani ya kahawa kwa ngazi ya tatu na ngazi ya nne *(tertiary processing)*.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2023/2024, Bodi ya Kahawa kwa kushirikiana na Sekta Binafsi iliweka lengo la kuzalisha miche bora ya kahawa milioni 20. Hadi kufikia Juni, 2023 miche 17,866,980 ya kahawa sawa na 89% ya lengo ilizalishwa. Miche hiyo imeanza kusambazwa kwa ajili ya wakulima katika maeneo yanayopata mvua za vuli.

**SPIKA:** Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi, swali la nyongeza.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina swali moja la nyongeza. Kwa kuwa kahawa yenyewe ni bidhaa ambayo ni malighafi, swali langu ni kwamba: Ni upi mkakati wa Serikali kuvutia sekta binafsi katika kuongeza thamani kwa maana ya kuzalisha bidhaa ambazo zitachukua kahawa kama malighafi kwa mfano *perfume,* dawa na bidhaa nyinginezo ndani ya nchi yetu? Ni upi mkakati wa Serikali kuvutia uwekezaji wa aina hiyo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Namshukuru sana Mheshimiwa Mbunge kwa swali la msingi ambalo lina tija katika kuongeza thamani katika zao la kahawa. Miongoni mwa mikakati yetu ambayo tulikuwa tumeiweka ni pamoja na kuvutia wawekezaji wengi kuja nchini.

Mheshimiwa Spika, moja ya sababu ambayo tumeiweka hapo, mwekezaji yeyote atakayekuja nchini kuwekeza kwenye viwanda vyetu hususani vya kahawa, maana yake tumepunguza baadhi ya kodi ambazo zilikuwa ni kodi kero kwa wawekezaji ikiwemo kuzuia baadhi ya bidhaa ambazo zinatoka nje, zinazoweza kuua soko la ndani, pamoja na kuwapa vivutio vya muda wa kufanya kazi hizo pamoja na mazingira ya kibiashara kuyaongeza katika soko letu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimwondoe shaka Mheshimiwa Mbunge kwamba moja ya mkakati wa Serikali yetu ni kuvutia wawekezaji na kila mwekezaji atafanya biashara zake hapa katika hali ya usalama zaidi, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Mheshimiwa Juliana Didas Masaburi, Mbunge wa Viti Maalum, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Saashisha Mafuwe.

Na. 39

**Chuo cha Maendeleo ya Jamii - Musoma**

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE K.n.y. MHE. JULIANA D. MASABURI** aliuliza:-

Je, lini Serikali itakipandisha hadhi Chuo cha Maendeleo ya Jamii Musoma ili kiweze kutoa shahada?

**SPIKA:** Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Mheshimiwa Mwanaidi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante na kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum,

napenda kujibu swali la Mheshimiwa Juliana Didas Masaburi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ili chuo kiweze kufikia hatua ya kutoa elimu kwa ngazi ya shahada, kinatakiwa kiwe na ithibati kamili na kiwe na vigezo stahiki ikiwemo miundombinu ya kutosha kutoa kozi husika, rasilimaliwatu ya kutosha na yenye sifa stahiki na Bodi ya Uendeshaji.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hatua zinazoendelea ili kuboresha mazingira ya chuo kwa ujumla wake, Wizara itaendelea kushirikiana na wadau wa kisekta kufanya tathmini ya kina kuhusu lini kozi hiyo ianze hasa kwa kuzingatia mahitaji halisi ya soko la ajira kwa wahitimu wa shahada, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, swali la nyongeza.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Spika, ahsante, na kwa niaba ya Mheshimiwa Juliana Didas Masaburi, nashukuru sana kwa majibu ya Serikali. Pamoja na hayo majibu ya Serikali, katika chuo hiki, wanafunzi wanapata taabu sana maeneo ya kuishi ili kupata taaluma pale. Ni upi mpango wa Serikali kuhakikisha inajenga mabweni kwenye eneo hili na chuo hiki ili wanafunzi wapate sehemu ya kukaa?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Katika Kanda ya Kaskazini, mikoa yote hakuna Chuo cha Maendeleo ya Jamii; je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Chuo cha Maendeleo ya Jamii katika Jimbo la Hai ambapo tayari tumeshapanga eneo la kujenga lipo tayari?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Spika, ahsante, napenda kujibu maswali ya nyongeza mawili kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tunatambua kuwa umuhimu wa miundombinu ya utoshelevu katika kujenga mabweni ya wanafunzi katika vyuo, Serikali itaendelea kutenga rasilimali fedha ili kuweza kuendelea kujenga mabweni hayo katika kila sehemu

ya vyuo ili wanafunzi wapate kuwa na maendeleo mazuri na kuwa karibu na kuishi maeneo ya shule.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili, ushauri wake tumeupokea na tunawapongeza Wanajimbo la Hai kwa kuwa na kiwanja cha kujenga Chuo cha Maendeleo ya Jamii. Wameona umuhimu wa vyuo hivi. Wizara itaendelea kutenga fedha kadiri bajeti itakavyoruhusu, katika mwaka wa fedha 2025, kuona vipi Chuo hiki tunakijenga ili wananchi waweze kuwa na chuo katika Mkoa wao, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Michael Costantino Mwakamo, Mbunge wa Kibaha Vijijini sasa aulize swali lake.

Na. 40

**Hitaji la Sheria ya Wazee**

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO** aliuliza:-

Je, lini Serikali itawasilisha Bungeni Muswada wa Sheria ya Wazee?

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba tupunguze kidogo sauti wakati tunazungumza mambo ya muhimu kabisa ya majimbo yetu. Tupunguze sauti kidogo ili tuweze kusikilizana.

Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM,** alijibu:-

Mheshmiwa Spika, ahsante, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinisia, Wanawake na Makundi Maalum, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Michael Costantino, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, napenda kulithibitishia Bunge lako tukufu kuwa Serikali inatambua na kuthamini mchango mkubwa wa wazee nchini. Sera ya Wazee ya mwaka 2003 iko katika hatua za

mwisho za mapitio ili kujumuisha masuala mapya yanayojitokeza tangu kupitishwa kwa Sera hiyo iliyopo.

Mheshimiwa Spika, kukamilika kwa mapitio ya Sera ya Wazee kutatoa fursa ya kutungwa Sheria ya Wazee na Serikali kuwakilisha Muswada huo wa Sheria ya Wazee Bungeni kwa hatua za sheria hiyo iliyotungwa, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwakamo, swali la nyongeza.

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu ya Serikali, lakini naomba niulize maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza: Kwa kuwa Muswada huu una muda mrefu takribani miaka 20 sasa na lilikuwa ni tegemeo la wazee wengi kupokea sheria hii: Je, Serikali inaweza ikatueleza vikwazo vilivyosababisha kuichelewesha sheria hii kutungwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Kwa kuwa wazee hawa wamelitumikia Taifa hili kwa muda mrefu: Je, Serikali ina mipango gani ya haraka ya kuwahudumia wazee hawa ili waweze kupata huduma zinazostahili kwenye ofisi za Serikali wakati wakiwa wanasubiri sheria hiyo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUMU:** Mheshimiwa Spika, ahsante, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ili Muswada ukamilike na ufikishwe Bungeni kuna taratibu na sheria na miongozo ambayo iliyowekwa na sasa inafanyiwa kazi. Mara baada ya kumalizika Muswada huo, utawasilishwa Bungeni kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili, Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inajali sana wazee; na katika Sheria mpya ambayo imetungwa tumeweka kipengele cha ulinzi na usalama kwa wazee. Kwa hiyo, kupitia Bunge lako tukufu naelekeza kwamba taasisi zote za Serikali na binafsi ziweze kuweka utaratibu maalum wa kuwasaidia wazee katika huduma

za jamii pale wanapofika sehemu hizo, kwani Serikali inawapenda wazee na wazee ni tunu ya Taifa letu, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Tumaini Bryceson Magessa, Mbunge wa Busanda sasa aulize swali lake.

Na. 41

**Kuboresha Vituo vya Polisi Busanda**

**MHE. TUMAINI B. MAGESSA** aliuliza:-

Je, upi mpango wa kuboresha Vituo vya Polisi Busanda hususani Kituo cha Katoro na Chigunda?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mhandisi Masauni, majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Tumaini Bryceson Magessa, Mbunge wa Busanda kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama maandalizi ya kuboresha vituo vya Katoro na Chigunda, tathmini kwa ajili ya ukarabati na uboreshaji wa mazingira ya vituo hivyo imeshafanyika na kubaini kuwa kiasi cha shilingi 37,265,000 zinahitajika. Fedha hizo tunatarajia kuzitenga kwenye Bajeti ya Serikali ya mwaka 2024/2025 ili kugharamia ukarabati wake.

**SPIKA:** Mheshimiwa Tumaini Magessa, swali la nyongeza.

**MHE. TUMAINI B. MAGESSA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali kwamba kuna fedha imetengwa. Nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, uboreshaji wa vituo hivi ulihitaji vile vile uongezaji wa idadi wa askari. Nini kauli ya Serikali juu ya uongezaji wa askari kwenye vituo hivi?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Uboreshaji wa vituo hivi vile vile ulihitaji kujenga nyumba za askari kwenye maeneo ya vituo hivi. Nini kauli ya Serikali kwenye ujenzi wa nyumba hizo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Bryceson Magessa, Mbunge wa Busanda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na suala la upungufu wa askari, hivi karibuni tunaendelea na mchakato wa kuajiri askari wapya. Wako askari ambao wanakamilisha mafunzo yao hivi karibuni na wengine tumetangaza hivi karibuni askari wapya. Kwa hiyo, miongoni mwa askari hao watakapomaliza mafunzo yao tutawapeleka ili kukabiliana na upungufu wa askari kwenye maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, halikadhalika tunatambua pia changamoto ya makazi ya askari katika maeneo hayo. Namwomba Mheshimiwa Mbunge awe na subira tukikamilisha ukarabati katika bajeti ijayo tutaangalia vile vile uwezekano wa kutatua changamoto au kupunguza changamoto ya makazi ya askari katika eneo hilo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Nishati Mheshimiwa Emmanuel Peter Cherehani, Mbunge wa Ushetu sasa aulize swali lake.

Na. 42

**Umeme wa uhakika-Kahama**

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI** aliuliza:-

Je, nini mkakati wa Serikali wa kupeleka umeme wa uhakika katika Halmashauri za Ushetu, Msalala na Kahama?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Judith Kapinga, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba Waziri wa Nishati, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Emmanuel Peter Cherehani, Mbunge wa Ushetu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ili kuboresha hali ya upatikanaji wa umeme kwenye Halmashauri za Ushetu, Msalala na Kahama, Shirika la Umeme Tanzania *(TANESCO)* lina mpango wa muda mfupi wa kujenga kituo kidogo cha umeme *(Switching Station)* kwenye eneo la Nyamirangano lililopo kwenye Halmashauri ya Ushetu. Kupitia kituo hicho kidogo, *TANESCO* itaongeza njia nyingine za umeme kutokea kwenye kituo hicho kwenda Ushetu, Msalala na Kahama ambazo zitasaidia kuboresha hali ya upatikanaji wa umeme. Mradi huu unategemewa kukamilika 2024 na unagharimu jumla ya shilingi bilioni 1.2, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Emmanuel Cherehani, swali la nyongeza.

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza naishukuru Serikali kwa majibu mazuri. Hali ya makali ya mgao wa umeme katika Wilaya ya Kahama pamoja na Halmashauri yake ni makali mno, hali ni ngumu, wafanyabiashara wanashinda wamekaa, umeme umekatika siku nzima. Sasa Mheshimiwa Waziri yupo tayari kufanya ziara katika Wilaya hii ya Kahama pamoja na Halmashauri zake ajionee hali ilivyo kwa wananchi hawa?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili. Je, Serikali ina mkakati gani sasa wa kuipa Mkoa wa ki-*TANESCO* Wilaya hii ya Kahama ambayo inakua kwa kasi kwa nchi hizi za maziwa makuu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Nishati napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Emmanuel Cherehani.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na mgao wa umeme, kwa sababu sasa hivi tumetengamaa na tumepunguza kidogo ule upungufu ambao ulikuwepo, niwaelekeze *TANESCO* na kituo chetu cha pamoja cha gridi *(Grid Control Center)* wahakikishe maeneo yote yanaendelea kupata umeme kulingana na jinsi ambavyo tunaboresha upatikanaji huo wa umeme.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na ziara, nitafika Ushetu Mheshimiwa Mbunge. Suala la pili kuhusiana na kuweka kituo cha kimkoa Ushetu, Mheshimiwa Mbunge tutaendelea kuangalia tathmini kama Wilaya ya Kahama inafaa kuwekwa kama Mkoa wa ki-*TANESCO* kwa ngazi ya mkoa, na kama itafaa, basi tutafanya hivyo, lakini kama haifai, tutaendelea kuboresha huduma ili wananchi wa Ushetu waendelee kupata huduma bora na stahili za masuala ya umeme. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Profesa Ndakidemi, swali la nyongeza.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa. Hospitali mpya ya Wilaya ya Mabogini imeshaanza kutoa huduma, je, Serikali ina mpango gani kupeleka umeme katika Hospitali yetu hii mpya?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Hospitali ya Mabogini tayari tumeshaifanyia tathmini na tupo katika mchakato wa kupata fedha ili ifikapo Januari, 2024 tuweze kuhakikisha Hospitali hii ambayo tayari inafanya kazi iweze kupatiwa umeme wa uhakika, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Venant Daud Protas, Mbunge wa Igalula, sasa aulize swali lake.

Na. 43

**Uvamizi wa tembo kwenye makazi na mashambani – Igalula**

**MHE. VENANT D. PROTAS** aliuliza:-

Je, lini Serikali itapeleka Askari na kulipa fidia kwa Wananchi waliovamiwa na Tembo kwenye makazi na mashamba yao Jimbo la Igalula?

**SPIKA:** Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Dunstan Kitandula, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Venant Daud Protas, Mbunge wa Jimbo la Igalula, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania *(TAWA)* imeweka askari sita wakiwemo askari wa uhifadhi wawili na askari wa vijiji *(VGS)* wanne katika kituo cha kudhibiti wanyamapori wakali na waharibifu cha Ndala kilichopo katika Wilaya ya Nzega mkoani Tabora. Aidha, askari hao wamepewa vitendea kazi ikiwemo pikipiki mbili na silaha ambavyo vinawawezesha kudhibiti wanyamapori hao popote wanapoonekana ikiwemo Jimbo la Igalula.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikilipa kifuta jasho na kifuta machozi kwa wananchi wanaopata madhara kutokana na Wanyama pori ambapo kwa upande wa Wilaya ya Uyui ambayo inajumuisha Jimbo la Igalula Wizara imepokea maombi ya wananchi 17 waliopata madhara ya wanyama pori wakali na waharibifu, maombi hayo kwa sasa yanaendelea kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Spika, kupitia Bunge lako tukufu niendelee kutoa rai kwa wakurugenzi wa Halmashauri wa wilaya hususan zenye changamoto za wanyama pori wakali na waharibifu kuharakisha kuwasilisha maombi yanayotokana na madhara ya Wanyama pori hao Wizarani ndani ya siku saba ili kuiwezesha

Serikali kufanya malipo ya kifuta jasho na kifuta machozi kwa wakati.

**SPIKA:** Mheshimiwa Venant Daud Protas, swali la nyongeza.

**MHE. VENANT D. PROTAS:** Mheshimiwa Spika, ahsante, pamoja na majibu ya Serikali naomba niulize maswali mawili ya nyongeza. Kumekuwa na wimbi kubwa la tembo kuvamia makazi ya watu na mashamba, lakini kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kuna askari wanatokea Ngara. Tumekuwa tukitoa taarifa ya uvamizi wa tembo huwa inachukuwa zaidi ya siku mbili mpaka nne kwenda kutatua tatizo hilo.

Mheshimiwa Spika, je, Serikali mtanipa lini askari watakao kaa katika Jimbo la Igalula siyo hao wa Ngara na siwajui na sijawahi kuwaona?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, tumekuwa na uvamizi na uharibifu wa mali za wananchi na mwaka jana tulikwenda kufanya tathmini wananchi zaidi ya hao 17 walivamiwa na uharibifu mkubwa. Lini mtawalipa fidia wananchi waliopata athari hizo? Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Venant Daud Protas, Mbunge wa Jimbo la Igalula kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli nchi yetu imekuwa na wimbi kubwa la matukio ya wanyama wakali na waharibifu kushambulia maeneo ya wananchi wetu. Serikali imekuwa ikijitahidi kuhakikisha kwamba pale tunapopata taarifa tunawatuma askari wetu kwa haraka kwenda kusaidia kukabiliana na changamoto hizi.

Mheshimiwa Spika, sasa tathmini iliyokuwa imefanyika ilionekana kabisa askari hawa tuliokuwa nao kwenye eneo lile wana uwezo wa kushughulikia jambo hili, lakini kwa sababu ya *concern* ya Mheshimiwa Mbunge baada ya kikao hiki cha leo nitakaa nae tuweze kuona ni jinsi gani tunaweza kushirikiana na

halmashauri kutoa mafunzo kwa maafisa wanyama pori wa vijiji ili waweze kushirikiana na wale wa Serikali kuondokana na changamoto iliyopo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuwalipa hawa wananchi ambao wamepata madhara haya kama nilivyosema kwenye jibu la msingi tuko kwenye hatua za mwisho za kufanya tathmini ili tuweze kuwalipa. Tathmini hii ikikamilika nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge wale watakaostahili kulipwa watapata malipo yao kwa wakati.

**SPIKA:** Mheshimiwa Oliver Daniel Semuguruka Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 44

**Kukitangaza Kivutio cha Maporomoko ya Maji Rusumo**

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaona umuhimu wa kukitangaza vya kutosha Kivutio cha Maporomoko ya Maji Rusumo ili kuchangia pato la Taifa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Oliver Daniel Semuguruka, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara inaendelea kushirikiana na Halmashauri za Wilaya kubaini vivutio mbalimbali vya utalii nchini kwa lengo la kuongeza wigo wa mazao ya utalii, katika kutekeleza hilo mwaka 2021 wataalam wa Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Ngara walibaini vivutio vya utalii na fursa mbalimbali za uwekezaji na shughuli za utalii katika Mkoa wa Kagera.

Mheshimishiwa Spika, miongoni mwa vivutio vilivyobainishwa ni Maporomoko ya Maji ya Mto Rusumo ambayo yanatoa fursa ya uendelezaji wa shughuli za utalii. Hata hivyo, tathmini ya awali iliyofanywa na watalaam wa Wizara imebaini kwamba kiasi kikubwa cha maji ya maporomoko hayo kimechepushwa kwa ajili ya uzalishaji wa umeme na hivyo kupunguza mvuto wa utalii wa maporomoko pekee.

Mheshimishiwa Spika, kwa mujibu wa ushauri wa watalaam, mara baada ya kukamilika kwa mradi wa uzalishaji wa umeme na kukabidhiwa Serikalini, tathmini mpya itafanyika ili kuunganisha utalii wa maporomoko ya maji na utalii wa uzalishaji wa umeme. Endapo tathmini hiyo itaonesha uwezekano wa eneo hilo kutumika kama kivutio cha utalii wa maporomoko ya maji na utalii wa uzalishaji umeme, Serikali itajielekeza kwenye kufanya maboresho ya miundombinu katika maporomoko hayo na kuyatangaza ndani na nje ya nchi kwa lengo la kuvutia watalii kutembelea katika kivutio hicho.

Mheshimiwa Spika, kupitia Bunge lako tukufu niendelee kuwahamasisha Watanzania wenzangu kuwa na utamaduni wa kutembelea vivutio mbalimbali vya utalii. Aidha, nitoe wito kwa Mheshimiwa Mbunge, uongozi wa Mkoa na wadau wengine kwa ujumla kuhamasisha uwekezaji wa huduma ikiwemo huduma za malazi na miundombinu mbalimbali katika vivutio vya utalii vilivyopo katika Mkoa wa Kagera.

**SPIKA:** Mheshimiwa Oliver Semguruka, swali la nyongeza.

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana ninalo swali moja la nyongeza. Kwanza, niishukuru sana Serikali kwa majibu mazuri ya kutia moyo. Kwa kuwa umekiri kuwepo kwa maporomoko hayo ambayo ni kivutio lakini yamepotea baada ya uchepushaji kwenye mradi wa umeme Rusumo. Je, huoni sasa ipo haja kupitia Wizara yako na Wizara ya Nishati mshirikiane kurejesha maporomoko hayo yawe kama awali ili yaendelee kuwa kivutio katika Wilaya yetu ya Ngara?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru naomba kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge Semguruka kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Ngara kwa kushirikiana na kampuni ya umeme ambayo itapewa jukumu la kuendesha mradi ule wa umeme pale Rusumo tayari wanamkakati wa kupanda miti katika eneo lote lile la ukanda wa mradi ule, ni imani yetu kwamba baada ya kufanyika upandaji wa miti ule hali ya upatikanaji wa maji katika eneo lile itaimarika na hivyo uwezekano mkubwa wa kivutio hiki kuendelea kutumika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hassan Zidadu Kungu, swali la nyongeza.

**MHE. HASSAN Z. KUNGU:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Je, ni upi mkakati wa Serikali wa kutoa ajira kwa mkataba wa muda mfupi kwa askari wa *VGS* ilikuweza kupunguza tatizo kubwa ama uhaba wa askari wa wanyama pori nchini? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, nakupa uhuru ikiwa unayo majibu unaweza kujibu kama huna kwa sasa linaweza kuja kama swali la msingi.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hassan kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inao mkakati wa kuhakikisha kwamba pale ambapo mafunzo ya askari wa vijiji yamefanyika na kumekuwa na uhitaji wa askari hawa kupatiwa ajira, tunashirikiana na halmashauri kuona jinsi ambavyo kupitia miradi mbalimbali tulioyonayo akari hawa badala ya kupewa ajira wanaanzishiwa miradi itakayowaingizia kipato ili wakati wakifanya shughuli hii ya uhifadhi lakini vilevile waweze kujiongezea kipato.

Mheshimiwa Spika, tumeanza zoezi hilo kwa mradi wa *REGROW* ambao unajielekeza kwenye kufungua fursa za utalii katika mikoa ya Kusini tunaamini mafunzo tutakayoyapata kutokana na mradi huu yatatuonesha ni jinsi gani tunaweza kuendeleza katika maeneo mengine.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ndaisaba George Ruhoro, swali la nyongeza.

**MHE. NDAISABA G. RUHORO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, kwa kuwa kivutio chetu pekee cha maporomoko ya Rusumo sasa kimepunguza mvuto baada ya uwekezaji wa mradi wa umeme pale Rusumo, Serikali haioni kuna haja sasa ya kuisaidia Ngara kuendeleza vivutio vingine ili Ngara isiondoke kwenye ramani ya kupata watalii, ahsante SANA.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ndaisaba kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Kivutio cha Rusumo siyo kivutio pekee kilichopo katika ukanda huu tunazo mbuga za wanyama zilizoko katika ukanda huu. Vilevile, kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi tunaangalia kutumia uwepo wa mradi wa umeme kuufanya kama sehemu ya kivutio. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba katika kuendeleza utalii katika ukanda huu tutaunganisha vivutio vingine vyote vilivyopo ili Sekta ya Utalii iweze kunufaisha ukanda huu na nchi yetu kwa ujumla.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali kutoka kwenu na majibu kutoka upande wa Serikali. Wabunge ambao bado wamesimama kule nyuma tafadhali watafute viti waketi. Tafuta kiti kilichokaribu nawe maana unanifanya nikusubiri umalize kutembea, ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge nitaleta tangazo nililonalo, hapa mbele ninalo tangazo moja linahusu wageni na kabla sijaleta tangazo hilo niwaombe radhi kwa Wabunge ambao walikuwa wametamani sana kuuliza maswali ya nyongeza kwa sababu ya changamoto tuliyoipata siku ya kwanza maswali yetu kwa sasa ni mengi. Kwa hiyo, watauliza wale wenye maswali ya msingi, ni

pale tu muda mdogo utakapopatikana watapewa watu wachache sana.

Kwa hiyo, niwaombe wale ambao hamjapeleka maswali yenu ya msingi myapeleke ili yapangiwe muda kwa sababu maswali yanakuwa ni mengi kwa siku na lazima tumalize kwa wakati. Waheshimiwa Wabunge naleta tangazo la wageni.

Tunao wageni waliokaa Jukwaa la Spika na tutaanza na hao; kwanza, ni wageni wangu ambao ni viongozi wa Chama Cha Mapinduzi Taifa, yupo Ndugu Paul Christian Makonda, Katibu wa *NEC,* Itikadi na Uenezi, karibu sana Bungeni kiongozi wetu. Pia ameongozana na Ndugu Shaibu Akwilombe ambaye ni Katibu Msaidizi Mkuu, Idara ya Itikadi na Uenezi, karibu sana. *(Makofi)*

Pia ameongozana na Ndugu Peter Josephat Niboye, Katibu Msaidizi Idara ya Itikadi na Uenezi, karibu sana, na ameongozana na maafisa wengine wa Chama Cha Mapinduzi Ndugu Peter Daffi, karibuni sana. *(Makofi)*

Yupo pia Wakili Kisaka Eneza Mnzava, karibu sana, na yupo pia Ndugu Barnaba Kalembo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia katika Jukwaa la Spika wapo dada zangu, yupo Adelina Mpaka, huyu ni dada yangu mkubwa kabisa, karibu sana; yupo anayefuata lakini si kwa ukubwa Odima Mpaka, karibu sana; pia yupopia dada mwingine mdogo Rhoida Mpaka, karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni wengine pia walioko Jukwaa la Spika na hawa ni viongozi wa dini kutoka *Maranatha Christian Centre (MCC)* Kanda na Mashariki ya Pwani, nafikiri ndiyo inavyoitwa.

Yupo Askofu John Lobulu Nengala ambaye ni Askofu wa Kanda ya Mashariki Pwani na huyu pia ndiye kiongozi wa msafara, karibu sana Bungeni. *(Makofi)*

Ameongozana na Askofu Kwamti Mganga Mlumba, karibu sana; yupo pia Mchungaji Joachim Michael Makundi, ahsante sana. *(Makofi)*

Yupo Mchungaji Sadiki Samwel Kinanga, karibu sana; yupo Mchungaji Festus Timoth Sambwe, karibu sana na yupo Ndugu Ernest Noah Loisolo, karibu sana. *(Makofi)*

Wapo pia wageni wawili wa Mheshimiwa Profesa Adolf Mkenda ambaye ni Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia ambao ni Profesa Carolyne I. Nombo ambaye ni Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo pia Profesa James E. Mdoe ambaye ni Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, karibu sana. *(Makofi)*

Karibuni sana ikiwa kuna wageni wengine wamekaa hapo pengine sina majina yao lakini tunawakaribisha sana. *(Makofi)*

Wapo wageni mbalimbali wa Waheshimiwa Wabunge; kwanza ni wageni wawili wa Mheshimiwa Dkt. Steven Kiruswa ambaye ni Naibu Waziri wa Madini ambao ni wapiga kura wake kutoka Jimboni kwake Longido, Mkoa wa Arusha, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 41 Mheshimiwa Abeid Ramadhani Ighondo ambao ni Wanakwaya wa Nivue na viongozi wa Chama, Kata na wapiga kura wawili kutoka Singida Kaskazini, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 11 wa Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka ambao ni viongozi wa Chama Cha Mapinduzi na viongozi wa mila kutoka Kitwai, Wilaya ya Simanjiro, Mkoa wa Manyara, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 10 wa Mheshimiwa Deus Sangu ambao ni Madiwani kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga, Mkoa wa Rukwa, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni saba wa Mheshimiwa Ritta Kabati ambao ni rafiki zake kutoka Marekani, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 40 wa Mheshimiwa Priscus Tarimo ambao ni Walimu Wakuu wa Shule za Msingi kutoka Moshi Mjini, Mkoa wa

Kilimanjaro wakiongozwa na Mwalimu Lawrence Kissima, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Tunao wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo, ni wanafunzi 57 na walimu nane *kutoka St. Mary's Dodoma*, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Tunao wageni 60 na walimu nane kutoka Shule ya Msingi Chemchemi kutoka Dodoma, karibuni sana Bungeni. Wageni wetu mnakaribishwa sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya tangazo hilo tuaendelea na ratiba yetu. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. PAMELA PALLANGYO – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA KAMATI

**Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali kuhusu Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa hesabu zilizokaguliwa na Serikali Kuu, Mashirika ya Umma na Kaguzi za Ufanisi kwa Mwaka wa Fedha uliuoishia tarehe 30 Juni, 2022**

**Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa kuhusu Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa hesabu zilizokaguliwa za Mamlaka za Seriakli za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha ulioishi tarehe 30 Juni, 2022**

**Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezajiwa wa Mitaji ya Umma kuhusu uwekezaji wa mitaji ya umma kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tutaanza uwasilishaji sasa wa Taarifa hizi za Kamati na tutaanza na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali *(PAC),* kwa niaba yake anakuja kusoma Makamu Mwenyekiti wa Kamati hii Mheshimiwa Japhet Hasunga.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI (PAC):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti naomba taarifa yetu yote iingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard)*.

Mheshimiwa Spika, hii ni Taarifa ya Kamati kuhusu Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali kwa Hesabu zilizokaguliwa za Serikali Kuu na Mashirika ya Umma kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2022.

Mheshimiwa Spika, utangulizi, kwa mujibu wa Kanuni ya 136(16) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari 2023 naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali kuhusu Hesabu za Serikali kwa Hesabu zilizokaguliwa za Serikali Kuu na Mashirika ya Umma kwa Mwaka wa Fedha Ulioishia Tarehe 30 Juni, 2022 na kuliomba Bunge liipokee na kuijadili.

Mheshimiwa Spika, aidha naomba kukupongeza sana kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani *(IPU)*. Ushindi huo ni wa heshima kubwa kwa Bunge letu Tukufu na nchi yetu kwa ujumla. Tunakuombea kila la kheri katika kutimiza majukumu yako katika *IPU*.

Mheshimiwa Spika, majukumu ya msingi ya Kamati ya Kudumu ya Hesabu za Serikali yamefanunuliwa katika kifungu cha 13 Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari mwaka 2023. Kwa mujibu wa kifungu hicho Kamati ina majukumu yafuatayo: -

(a) Kushughulikia maeneo yenye matumizi mabaya ya fedha za umma katika Wizara za Serikali na mashirika ya umma yaliyoainishwa katika Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali;

Mheshimiwa Spika, naomba kuliweka vizuri hili kwamba tunayoyazungumzia katika taarifa hii ni yale maeneo yenye matumizi mabaya. Kwa hiyo, mambo mazuri yaliyofanywa na Serikali hatuyabainishi kwenye ripoti hii, tunabainisha maeneo yenye mapungufu. Yapo mazuri tumeyanoti, tumeyaona lakini tunaenda kwenye yale yenye mapungufu.

(b) Kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo yaliyokwishatolewa na Kamati ili kuondoa matatizo yaliyobainishwa kwa mujibu wa kanuni hii na;

(c) Kutoa mapendekezo na ushauri kwa wizara za Serikali na mashirika ya umma kuhusu matumizi mazuri ya fedha za Umma ili kupunguza matumizi mabaya ya fedha za Umma.

Mheshimiwa Spika, kuhusu muundo wa taarifa; kwa madhumuni ya kurahisisha ufuatiliaji wa taarifa hii naomba kubainisha sehemu kuu nne. Sehemu ya kwanza inatoa maelezo ya jumla. Sehemu ya pili inahusu uchambuzi wa Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu hesabu za Serikali Kuu na mashirika ya umma. Sehemu ya tatu inahusu maoni na mapendekezo ya Kamati na sehemu ya nne ni hitimisho na hoja.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya uchambuzi wa taaarifa ya CAG kwa mafungu mahususi ya Serikali Kuu na mashirika ya umma umegawanya hoja katika makundi nane kama ifuatavyo:-

i. Dosari katika usimamizi wa ukusanyaji wa mapato;

ii. Dosari katika usimamizi wa mikataba;

iii. Mapitio ya hesabu za taasisi za huduma za afya;

iv. Kaguzi maalum;

v. Taarifa ya ukaguzi wa fedha za UVIKO 19 kutoka *IMF*;

vi. Mapitio ya hesabu za Mifuko ya Hifadhi ya Jamii;

vii. Mapungufu ya kiutendaji yanayochangia upotevu wa fedha za umma na;

viii. Hoja za ukaguzi zinazotokana na uzingatiaji wa sheria, miongozo na taratibu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha hoja za kwenye kila kundi kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika kuhusu dosari katika usimamizi na ukusanyaji wa mapato ya Serikali. Katika hoja hii *CAG* alibainisha uwepo wa taasisi za Serikali ambazo hazikufikia malengo ya makusanyo ya mapato kama ifuatavyo: -

(a) Mamlaka ya Mapato Tanzania haikukusanya mapato ya kiasi cha shilingi bilioni 887.3 kutokana na sababu mbalimbali kama vile usimamizi usioridhisha wa mafuta yanayosafirishwa kwenda nje ya nchi kupitia hapa nchini na usimamizi wenye dosari kwenye makusanyo ya mizigo *(consolidators)*.

(b) Kampuni ya *TANOIL* ilipata hasara ya shilingi bilioni 7.8 kutokana na mapungufu ya kiutendaji kama vile kuuza mafuta kwa bei ya chini kinyume na bei elekezi za *EWURA* na kutozingatia miongozo na taratibu za kampuni.

(c) Tume ya Madini haikukusanya mapato ya shilingi bilioni 30.7 ambapo sehemu kubwa ya deni hilo inadaiwa na kampuni ya *TANCO* ambapo deni la *TANCO* peke yake ni shilingi bilioni 23.7.

(d) Wizara ya Maliasili na Utalii haikukusanya mapato ya Dola za Marekani 599,000 kutoka kwa kampuni ya *MS Game Hunters* ambayo ilikiuka kwa makusudi masharti ya zabuni. *(Makofi)*

(e) Wakala wa Majengo Tanzania alikua na limbikizo la madeni la shilingi bilioni 82.2. Katika madeni hayo kodi za nyumba zinazodaiwa ilikuwa ni shilingi bilioni 40.5 na madeni ya mauzo ya nyumba ilikuwa ni shilingi bilioni 14.2.

Mheshimiwa Spika, eneo la pili ni hoja za ukaguzi zinazotokana na dosari katika usimamizi wa mikataba na athari zake katika matumizi ya fedha za Umma.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo uchambuzi wa Kamati umebainisha uwepo wa upotevu mkubwa wa fedha za Serikali ni mapungufu au dosari katika uingiaji na usimamizi wa mikataba. Uchambuzi wa Kamati umefafanua mafungu hayo yenye changamoto kama ifuatavyo: -

(a) Kampuni ya *IPTL* kutotekeleza sharti la kinga ya kisheria hivyo kuifanya Serikali na *TANESCO* kupewa madai ya shilingi bilioni 148 kutokana na *IPTL* kutotekeleza wajibu wake huo. *(Makofi)*

(b) Mapungufu katika usimamizi wa mradi wa usambazaji maji Same - Mwanga - Korogwe. Miongoni mwa dosari za mradi huo ni kuchelewa kukamilika kwa wakati, ongezeko kubwa la gharama za mradi, dhamana za mkopo kwisha kabla ya muda na kuvunjwa kwa mkataba kila mara.

(c) Hoja nyingine kuhusu mikataba inahusu ujenzi wa reli ya kisasa *SGR*. Katika eneo hili *CAG* alibainisha changamoto kama vile ongezeko la muda wa kukamilika kwa mradi kwa zaidi ya siku 1,414 na pia dosari mbalimbali zilizobainishwa katika ununuzi wa vichwa na mabehewa ya treni.

(d) TANESCO ilinunua na kutumia jumla ya mita mia nane sabini nan ne na kumi na tisa zenye thamani ya shilingi bilioni 115. Hata hivyo, mita hizo hazikuthibitishwa na Wakala wa Vipimo, kitu ambacho kinaweza kusababisha hasara kwa wateja au kwa shirika lenyewe.

(e) Hoja nyingine inahusu riba ya shilingi bilioni 113.8 ambayo *TANESCO* inadaiwa na kampuni ya *Pan African Energy* kwa kuchelewa kulipa madeni yake. *(Makofi)*

(f) *TANROADS* walitozwa riba ya shilingi bilioni 36.4 kwa kuchelewa kuwalipa wahandisi na washauri wa miradi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu mapitio ya kaguzi za hesabu katika taasisi za huduma za afya. Kamati ilipitia taarifa za fedha za taasisi za Umma zinazohusiana na utoaji wa huduma za afya. Matokeo ya uchambuzi wa Kamati kwa taasisi hizo ni kama ifuatavyo: -

(a) Mfuko wa Taifa ya Bima ya Afya ulikuwa unaidai Serikali shilingi bilioni 228 ambazo zinapunguza uwezo wa mfuko kutekeleza majukumu yake.

(b) Bohari Kuu ya Dawa *MSD* ilikuwa na madeni ambayo inaidai Serikali kiasi cha shilingi bilioni 275.5. Vilevile, katika *MSD* kulikuwa na manunuzi ya dawa kutoka nchini Misri kwenye kampuni ya *Al-Handasia* na *EIPICO* kulikoisababishia Serikali hasara.

(c) Vilevile, kulikuwa na changamoto za kisheria za uundwaji na uendeshaji wa Hospitali ya Muhimbili - Mloganzila.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uchambuzi wa taarifa ya kaguzi maalum. Katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 Kamati imefanikiwa kupitia na kuchambua jumla ya taarifa za kaguzi maalum tano. Naomba kulifahamisha Bunge lako Tukufu matokeo ya kaguzi hizo maalum kwa muhtasari kama ifuatavyo: -

(a) Ukaguzi maalum kuhusu uendeshaji na usimamizi wa mikataba ya maridhiano ya kukiri makosa yaani *plea bargaining*. Ukaguzi ulibaini masuala yafuatayo: -

i. Baadhi ya washtakiwa kushindwa kukamilisha malipo ya bakaa ya fidia kulingana na mikataba ya maridhiano ya kukiri kosa au makosa na hukumu ya mahakama kiasi cha shilingi bilioni 170.6.

ii. Kiasi cha jumla ya shilingi milioni 828,531,288 kati ya shilingi bilioni 53,761,056,294…

**SPIKA:** Mwenyekiti ngoja, hebu hiyo takwimu, fedha isome upya.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI (PAC):** Mheshimiwa Spika, fedha?

**SPIKA:** Hapa kwenye (b) hebu soma tena.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI (PAC):** Mheshimiwa Spika, kiasi cha jumla ya shilingi milioni 328,531,288 kati ya shilingi bilioni 53,761,056,294 zilizowekwa kimakosa na washtakiwa watatu ambao utaratibu wa kumaliza kesi zao haukuwa na mkataba wa maridhiano ya kukiri kosa au makosa. *(Makofi)*

iii. Kutowasilishwa kwa majalada 15 ya kesi katika ukaguzi yenye fidia ya shilingi milioni 80,652,888.

(b) Taarifa ya ukaguzi maalumu kuhusu shughuli za utaifishaji, makabidhiano na ugawaji wa mali zilizotaifishwa yaani *forfeiture*.

Mheshimiwa Spika, ukaguzi ulibaini masuala yafuatayo: -

i. Kutokuwepo kwa mwongozo juu ya madhumuni ya Serikali baada ya kutaifisha mali;

ii. Kukosekana kwa mwongozo wa umiliki wa mali zilizotaifishwa ambazo hazina takwa au utaratibu wa kisheria wa kusajiliwa katika rejista ya hati miliki;

iii. Sheria kutokutambua haki ya waathirika wa mali zilizotaifishwa;

iv. Mali zilitaifishwa lakini hakuna uthibitisho wa makabidhiano kati ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka na Wizara ya Fedha na Mipango;

v. Utaifishaji wa madini ya almasi *karat* 71,654.56 yenye thamani ya Dola za Marekani milioni 29,509,821.84 bila mmiliki wa madini kuhusishwa.

(c) Taarifa ya ukaguzi maalum wa matumizi ya fedha za mfuko wa tozo na tuzo wa Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Spika, ukaguzi maalum ulibaini yafuatayo: -

i. Taasisi 31 zilipokea huduma ya ulinzi zikiwa na mikataba iliyokwisha muda wake bila kuhuishwa na kutolipa kiasi cha shilingi bilioni 2.2.

ii. Taasisi 21 kutolipa huduma za ulinzi za Jeshi la Polisi zenye thamani ya shilingi bilioni 1.6.

iii. Kamandi tano peke yake kupelekewa fedha badala ya nchi nzima.

(d) Uchambuzi wa taarifa ya ukaguzi maalum wa mfuko wa kufa na kuzikana wa Jeshi la Polisi; ukaguzi ulibaini masuala yafuatayo:-

i. Ukiukwaji wa mwongozo wa mfuko na viongozi kujinufaisha binafsi.

ii. Malipo ya watia sahihi wa mfuko yasiyothibitisha uhalali wake ya shilingi milioni 754,654,944.

iii. Ubadhirifu wa fedha za mfuko wa kufa na kuzikana kupitia akaunti za wanufaika wa shilingi milioni 28,200,000.

iv. Udanganyifu katika ufufuaji wa akaunti namba 22901603799 Mkoa wa Kusini Unguja na kufanyikka ubadhirifu wa shilingi milioni 988,450,000. *(Makofi)*

v. Ubadhirifu wa fedha kupitia akaunti ya Mkoa wa Kusini Unguja wa shilingi milioni 511,500,000. *(Makofi)*

*vi.* Ubadhirifu wa fedha wa shilingi milioni 306 Makao Makuu Polisi Zanzibar. *(Makofi)*

vii. Kutumika kwa fedha za mfuko wa kufa na kuzikana kinyume na taratibu wa shilingi milioni 39,946,000 Mkoa wa Kusini Pemba.

viii. Kutoandaliwa kwa taarifa za fedha na kutowasilishwa katika mkutano wa mfuko.

ix. Kutokaguliwa kwa mfuko wa kufa na kuzikana.

(e) Taarifa ya ukaguzi maalum wa kampuni ya uendeshaji wa kiwanja cha ndege cha Kilimanjaro *(KADCO)*.

Mheshimiwa Spika, ukaguzi ulibaini masuala yafuatayo: -

i. Serikali kupewa hisa 379,339 chini ya kiwango cha thamani ya mali ilizochangia.

ii. Kuendelea kuendesha na kusimamia Uwanja wa Ndege wa *KIA* chini ya *KADCO* kinyume na Azimio la Bunge na maelekezo ya Baraza la Mawaziri. *(Makofi)*

iii. *KADCO* imepata hasara ya shilingi milioni 794,012,858 na Dola za Marekani 388,380.32.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uchambuzi wa fedha za mkopo wa UVIKO 19 zilizotolewa na Shirika la Fedha la Kimataifa – IMF; hoja zilizobainika katika ukaguzi ni kama ifuatavyo: -

i. Wazabuni kutowasilisha kwa wakati vifaa vya tiba vyenye thamani ya shilingi bilioni 17.92.

ii. Wazabuni kutowasilisha magari yenye thamani ya shilingi bilioni 18.85.

iii. Vifaa tiba vyenye thamani ya shilingi bilioni 14.81 kutoanza kutumika.

iv. Migongano ya maslahi katika ununuzi wa vifaa vya ujenzi kwa shilingi milioni 517.58.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mapitio ya kaguzi katika mifuko ya hifadhi za jamii. Uchambuzi wa Kamati katika taarifa za Mifuko ya Hifadhi ya Jamii *NSSF* na *PSSSF* ulibaini hoja kadhaa za ukaguzi kama ifuatavyo: -

i. Uwepo wa mkopo wa muda mrefu ambao *NSSF* haijakusanya wa shilingi bilioni 1,174.

ii. Michango ya wanachama ambayo haijakusanywa na *NSSF* ya shilingi bilioni 408.

iii. Hoja zinazohusiana na kodi ya iliyokuwa *PPF*, *LAPF* na *PSSF* za shilingi bilioni 714.

iv. Madeni ambayo Serikali inadaiwa na *PSSSF* kiasi cha shilingi trillion 2.452. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mapungufu ya kiutendaji ambayo yanachangia upotevu wa fedha za umma.

(a) Uwepo wa mikopo iliyoiva yenye thamani ya shilingi bilioni 21 kwenye Mfuko wa Pembejeo za Kilimo *(AGITF)* ambayo haijakusanywa mpaka leo.

(b) Uwepo wa bakaa ya fedha ya kiasi cha shilingi bilioni 26.6 katika akaunti ya mirathi bila kufanyiwa usuluhishi wa kibenki *(bank reconciliation)*.

(c) Matumizi ya takriban shilingi bilioni 5.6 kwa mwaka kuhudumia wafungwa 3,110 waliomaliza kutumikia vifungo vyao.

(d) Kampuni ya mbolea *TFC* kutotekeleza majukumu yake ya msingi kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 pamoja na kupewa ruzuku ya shilingi bilioni 10.2.

(e) Ubadhirifu wa shilingi milioni 261.3 uliofanyika katika Jeshi la Zimamoto na Uokoaji ambapo mhusika amefukuzwa kazi lakini hajafikishwa mahakamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu hoja za ukaguzi za ujumla zinazohusu uzingatiaji wa sheria, taratibu na kanuni *(compliance audit issues)*.

(a) Kutozingatia ipasavyo kwa Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma katika mchakato wa ajira katika Benki Kuu ya Tanzania.

(b) Baadhi ya taasisi za Serikali kutozingatia mwongozo wa Wizara ya Fedha katika utunzaji wa mali za Serikali kwenye mfumo wa kielektroniki.

Mheshimiwa Spika, kuhusu maoni na mapendekezo ya Kamati. Mapendekezo ya Kamati yametolewa kwa kuzingatia ukubwa wa athari ya hoja inayohusika, matokeo yenye kuambatana na hoja husika, uwezekano wa hoja kujirudia na hatua zilizotakiwa kuchukuliwa kushughulikia hoja husika.

Mheshimiwa Spika, Mapendekezo ya Kamati yanasomwa sambamba katika randama ya kwanza iliyoambatanishwa na taarifa hii. Kuhusu *nakisi* ya ukusanyaji wa mapato kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania - *TRA* kiasi cha shilingi bilioni 887.3. Bunge linaazimia kwamba: -

(a) TRA ihakikishe ndani ya Mwaka wa Fedha 2023/2024 inakamilisha usimikaji na utekelezaji wa mifumo yote muhimu ya usimamizi na udhibiti wa kodi ili kuhakikisha mapato stahiki ya Serikali yanakusanywa kwa ukamilifu.

(b) TRA ihakikishe kesi zote za mapingamizi ya kodi kama zilivyoletwa na walipakodi zinashughulikiwa kwa mujibu wa Sheria na kanuni zilizopo ili kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya Serikali.

(c) TRA ihakikishe inaweka mifumo thabiti ya usimamizi wa kodi katika michezo ya kubahatisha na mafuta ambayo yanapitia hapa nchini Kwenda nchi nyingine.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza azimio hili hatua kali zichukuliwe kwa wanaokiuka Sheria za Umma na Umma ujulishwe ipasavyo.

(d) TRA itengeneze mfumo maalum wa kusimamia makusanyo ya mizigo yaani *consolidators* ili kuhakikisha mapato ya Serikali yanakusanywa kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Spika, Hasara ya shilingi bilioni 7.84 katika *TANOIL;* Bunge linaazimia kwamba, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali afanye Ukaguzi wa Kiuchunguzi *(Forensic Audit)* katika Kampuni ya *TANOIL* ili kubainisha kwa kina sababu na mazingira ya hasara za *TANOIL*. Katika kutekeleza jukumu hilo *CAG* azingatie maeneo yafuatayo:-

(a) Kupitia kwa kina utaratibu uliotumika kuanzisha Kampuni ya *TANOIL* na malengo yake;

(b) Kupitia na kuchambua utaratibu na njia *(business model)* za kibiashara zinazotumika na *TANOIL* kufanya biashara ya mafuta na endapo zina tija na ufanisi;

(c) Kuchunguza uhusika wa iliyokuwa Menejimenti na uongozi wa *TANOIL* katika kusababisha hasara kwa kampuni hasa kwa maamuzi waliyokuwa wanafanya kinyume na taratibu na miongozo iliyopo; na

(d) Kuchunguza masuala mengine yeyote yanayohusiana na *TANOIL* ambayo yanahusiana na fedha za umma.

Mheshimiwa Spika, Mapato yasiyokusanywa, dola za Marekani 599,000 katika Wizara ya Maliasili na Utalii; Bunge linaazimia kwamba:-

(a) Serikali ikamilishe uandaaji wa Kanuni zitakazoweka sharti la adhabu kwa wazabuni waliokiuka masharti ya uwekezaji katika zabuni za vitalu vya uwindaji wa kitalii; na

(b) Kampuni husika iliyokiuka masharti ya zabuni *"M/s Game Hunters Tanzania Limited"* izuiwe kufanya shughuli zozote katika sekta ya uwindaji wa kitalii hapa nchini kwa kukiuka masharti ya zabuni kwa makusudi hali ambayo imeikosesha Serikali mapato.

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya *IPTL* kutotekeleza Masharti ya Mkataba, hivyo Serikali na *TANESCO* kutopata nafuu ya kifedha kiasi cha shilingi bilioni 148.4; Bunge linaazimia kwamba:-

(a) Serikali itekeleze kwa ukamilifu masharti yaliyoambatishwa kwenye Kinga ya Kisheria *(Indemnity)* iliyotolewa na *IPTL* dhidi ya madai yoyote ambayo yangetokea kwa Serikali baada ya kutolewa kwa fedha katika Akaunti ya Tegeta *Escrow*; na

(b) Serikali isifanye malipo mengine yoyote kwa mashauri yatakayofunguliwa dhidi ya wamiliki wa *IPTL* ili kutopoteza fedha za umma.

Mheshimiwa Spika, Mapungufu Katika Utekelezaji wa Mradi wa Maji wa Same hadi Korogwe; Bunge linaazimia kwamba, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali afanye Ukaguzi Maalumu katika Mradi wa Maji Same, Mwanga hadi Korogwe kwa kuzingatia maeneo yaliyobainishwa kama inavyoonyeshwa katika ripoti kubwa.

Mheshimiwa Spika, Manunuzi ya Mita za Umeme bila Kukaguliwa na Wakala wa Vipimo; Bunge linaazimia kwamba, Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi Serikalini *(PPRA)* ifanye ukaguzi maalumu wa ununuzi wa mita za umeme uliofanywa na *TANESCO* na kisha kutoa taarifa yake kwenye Bunge letu hili Tukufu.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Madini kutokukusanya madeni ya kiasi cha shilingi bilioni 30.757; Bunge linaazimia kwamba, Tume ya Madini ihakikishe madeni husika yanakusanywa ndani ya mwaka wa fedha 2023/2024. Aidha, kwa vipengele vya Sheria ya Madini, Sura 123 ambavyo vinakwaza makusanyo ya mapato ya Serikali vifanyiwe marekebisho kabla ya kukamilika kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Spika, Bohari Kuu ya Madawa *(MSD)* na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya *(NHIF),* Bunge linaazimia kwamba:-

(a) Serikali ianze kupunguza deni linalodaiwa na *MSD* kiasi cha takribani shilingi bilioni 275 na shilingi bilioni 228 za Mfuko wa Bima ya Afya ndani ya mwaka wa fedha 2023/2024; na

(b) Serikali ikamilishe uchunguzi wa ununuzi wa vifaa tiba na madawa uliofanywa katika kwa kampuni ya *M/s. AL HANDASIA ya* Nchini Misri na kuchukua hatua stahiki kwa wahusika kwa kuzingatia matokeo ya uchunguzi.

Mheshimiwa Spika, Ukaguzi Maalum kuhusu Uendeshaji na Usimamizi wa Mikataba ya Maridhiano ya Kukiri Makosa; Bunge linaazimia kwamba, Serikali ifanye uchunguzi wa kina na mahsusi katika suala hili kwa kuzingatia masharti ya Katiba na Sheria ili wahusika wachukuliwe hatua ipasavyo kwa dosari zilizojitokeza katika mchakato huu.

Mheshimiwa Spika Matumizi ya Fedha za Mkopo wa UVIKO Zilizotolewa na Shirika la Fedha la Kimataifa *(IMF);* Bunge linaazimia kwamba:-

(a) Serikali itekeleze mapendekezo yote ya ukaguzi maalum wa fedha za UVIKO kama yalivyotolewa na *CAG* na kuwasilisha Bungeni Taarifa ya Utekelezaji wa mapendekezo hayo katika kipindi cha robo mwaka; na

(b) Katika miradi iliyotekelezwa kwa fedha za mikopo, Serikali ihakikishe inatenga fedha za kutosha kwa ajili ya ufuatiliaji na tathmini pamoja na kuimarisha usimamizi.

Mheshimiwa Spika, Kutozingatiwa Ipasavyo kwa Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma Wakati wa Mchakato wa Ajira katika Benki Kuu ya Tanzania *(BOT);* Bunge linaazimia kwamba, Bodi ya *BOT* iwachukulie hatua za kinidhamu Watumishi wote waliohusika kwenye mchakato wa ajira hizo kwa ukiukaji wa Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma ili jambo hilo lisijitokeze tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mapungufu katika mchakato wa ununuzi wa vishkwambi 300; Bunge linaazimia kwamba, Serikali ihakikishe inakuwa na mpango na mkakati endelevu wa maandalizi ya kina ya utekelezaji wa shughuli zote ambazo utekelezaji wake

unajulikana kabla, kama vile Sensa ya Watu na Makazi na Uchaguzi Mkuu. Aidha, kuwe na Mfuko Maalum wa kugharamia shughuli zinazotekelezwa kwa kalenda maalumu kama Sensa na Uchaguzi Mkuu ili kuepuka hoja za ukaguzi zinazotokana na utekelezaji wa shughuli hizo kwa dharura.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Pembejeo za Kilimo *(AGITF)* na Kampuni ya Mbolea Tanzania *(TFC);* Bunge linaazimia kwamba:-

(a) Mfuko wa Pembejeo za Kilimo uhakikishe unakusanya madeni husika ndani ya mwaka wa fedha 2023/2024. Aidha, mifumo ya udhibiti iimarishwe ili kuepuka ongezeko la mikopo chechefu; na

(b) *TFC* iandae Mpango wa Biashara wenye tija ili kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kwa kuwafikia wakulima nchi nzima ili thamani ya fedha ya Serikali iliyotumika na Kampuni ionekane bayana.

Mheshimiwa Spika, Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ya *PSSSF* na *NSSF*; Bunge linaazimia kwamba Serikali iwasilishe Bungeni Mpango wa muda mrefu wa kulipa madeni ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uwepo wa kiasi kikubwa cha fedha katika Akaunti ya Mirathi katika Fungu 40 la Mahakama; Bunge linaazimia kwamba, Afisa Masuuli wa Fungu 40, Mahakama ya Tanzania akamilishe usimikaji na utekelezaji wa Mfumo wa Kidijitali wa Utunzaji wa Kumbukumbu *(e-Trace)* ikiwa ni pamoja na kumbukumbu za Akaunti ya Mirathi. Aidha, usuluhishi wa kibenki wa akaunti husika ufanyike kwa wakati ili kuepusha upotevu wa fedha zilizopo kwenye akaunti hiyo.

Mheshimiwa Spika, Ukaguzi wa Kiufundi wa ujenzi wa Reli ya Kisasa *(SGR);* Bunge linaazimia kwamba:-

(a) Serikali ihakikishe inapata ufadhili wa kifedha wenye unafuu wa uhakika na kwa wakati na wakati wa utekelezaji wa *SGR* kwa vipande vinavyoendelea na ujenzi na kwa vipande vilivyobaki ili mradi ukamilike kwa wakati na kuchangia ukuaji wa uchumi;

(b) Serikali ihakikishe kuwa juhudi zinachukuliwa za kulinda taswira chanya ya miradi yote mikubwa ya Kimkakati iliyotekelezwa hapa Nchini ikiwemo Mradi wa *SGR* ili itekelezwe na kukamilika kwa wakati; na

(c) *TRC* iendelee kusimamia shughuli zote za ujenzi wa Reli ya Kisasa kwa kuzingatia kikamilifu sheria za nchi.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Tuzo na Tozo wa Jeshi la Polisi na Mfuko wa Kufa na Kuzikana wa Jeshi la Polisi; Bunge linaazimia kwamba:-

(a) Kanuni za Mfuko wa Tuzo na Tozo wa Jeshi la Polisi ziandaliwe na kutumika ipasavyo zikiainisha bayana vyanzo vya mapato ya Mfuko, Taratibu za Matumizi ya Mfuko na uwajibikaji katika Fedha za Mfuko;

(b) Hatua za Kisheria na Kinidhamu zichukuliwe kwa watuhumiwa wote 27 waliohusika na ubadhirifu wa fedha za Mfuko wa Kufa na Kuzikana wa Jeshi la Polisi; na

(c) Jeshi la Polisi lihakikishe Kanuni za Kusimamia Mfuko wa Kufa na Kuzikana zinaandaliwa na kuanza kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Ukaguzi Maalumu wa Kampuni ya Uendeshaji wa Uwanja wa Ndege Kilimanjaro *(KADCO);* Bunge linaazimia kwamba, Serikali itekeleze mapendekezo yote ya *CAG* yanayohusu ukaguzi maalum uliofanyika *KADCO* kwa hoja zinazohusu utendaji na fedha zikusanywe.

Mheshimiwa Spika, Hitimisho; Shukurani; napenda kutumia fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa uongozi wako. Uongozi wako umeiwezesha Kamati yangu kutekeleza majukumu yake bila vikwazo kwa kutoa maelekezo na miongozo thabiti kwa Kamati.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali kwa kutekeleza majukumu ya Kamati hii kwa ufanisi na weledi mkubwa. Naomba majina yao yote yaingizwe kwenye Taarifa Rasmi za Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Bi. Nenelwa Mwihambi, *ndc* kwa uongozi wake thabiti wa Sekretarieti ya Bunge ambayo imeratibu shughuli za Kamati kwa ufanisi mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho japo siyo kwa umuhimu, Kamati inatambua na kuthamini ushirikiano mkubwa ilioupata kutoka Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi pamoja na Wizara ya Fedha. Tunawashukuru sana kwa ushirikiano waliouonyesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza na naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI (PAC) KUHUSU RIPOTI ZA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI KWA HESABU ZILIZOKAGULIWA ZA SERIKALI KUU NA MASHIRIK YA UMMA KWA MWAKA WA FEDHA ULIOISHIA TAREHE 30 JUNI, 2022 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

*Imetolewa chini ya Kanuni ya 136(16) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari, 2023*

**SEHEMU YA KWANZA**

## 1.0 MAELEZO YA JUMLA

### 1.1 Utangulizi

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) kuhusu Hesabu za Serikali kwa Hesabu zilizokaguliwa za Serikali Kuu na Mashirika ya Umma kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2022 na kuliomba Bunge liipokee na kuijadili. Madhumuni ya Taarifa hii ni kulijulisha Bunge lako Tukufu, iwapo matumizi ya Fedha za Umma yamefanyika kwa namna iliyokusudiwa na Bunge na kwamba matumizi hayo yamezingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za Fedha za Umma.

**Mheshimiwa Spika,** katika kutimiza madhumuni hayo, Taarifa hii inagusa Hesabu za Serikali Kuu na Hesabu za Mashirika ya Umma

kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2022 kama zilivyokaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Jambo kuu katika Taarifa hii linahusu matumizi ya fedha za umma hususani dosari za matumizi ya fedha za umma zinazohitaji kufanyiwa kazi.

**Mheshimiwa Spika,** vilevile naomba kukupongeza sana kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU). Ushindi huo ni wa heshima kubwa kwa Bunge letu Tukufu na Nchi yetu kwa ujumla. Tunakuombea kila lakheri katika kutimiza majukumu yako katika IPU.

### 1.2 Muundo wa Taarifa

**Mheshimiwa Spika**, kwa madhumuni ya kurahisisha ufuatiliaji wa taarifa hii, naomba kubainisha sehemu kuu tatu ambazo ni za msingi pamoja na hitimisho lenye shukurani na utoaji wa hoja. Sehemu ya kwanza inatoa maelezo ya jumla ikiwemo muundo wa Taarifa, majukumu ya Kamati, msingi wa kazi za Kamati na muhtasari wa matokeo ya Uchambuzi wa Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Lengo la Sehemu hii ni kubainisha muktadha wa Taarifa ili kuwezesha ufuatiliaji utakaosaidia kufanya uamuzi.

**Mheshimiwa Spika**, sehemu ya pili inahusu uchambuzi wa Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Hesabu za Serikali Kuu na  Mashirika ya Umma.Katika Sehemu hii, Taarifa inafafanua mambo ya msingi kuhusu uchambuzi na kubainisha matokeo ya uchambuzi huo. Lengo la sehemu hii ni kuonesha dosari zilizobainika katika matumizi ya Fedha za Umma na kuweka msingi wa mtazamo wa Kamati kuhusu Matumizi ya Fedha za Umma kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022. Sehemu hii inajenga msingi wa Sehemu ya Tatu inayohusu Maoni na Mapendekezo.

### 1.3 Majukumu ya Kamati

**Mheshimwa Spika**, maudhui ya Taarifa hii yanahusu Matumizi ya Fedha za Umma kwenye Serikali Kuu na Mashirika ya Umma Nchini. Mambo hayo yanasimamiwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali kama ilivyobainishwa katika Kifungu

cha 13 cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023. Kwa mujibu wa Kifungu hicho Kamati ina majukumu yafuatayo: -

a) Kushughulikia maeneo yenye matumizi mabaya ya fedha za umma katika Wizara za Serikali na Mashirika ya Umma yaliyoainishwa katika Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG);

b) Kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo yaliyokwishatolewa na Kamati ili kuondoa matatizo yaliyobainika kwa mujibu wa kanuni hii; na

c) Kutoa mapendekezo na ushauri kwa Wizara za Serikali na Mashirika ya Umma kuhusu matumizi mazuri ya fedha za umma ili kupunguza matumizi mabaya ya fedha za umma.

**Mheshimiwa Spika,** Msingi wa majukumu hayo unatokana na Taarifa ya Hesabu zilizokaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kama ilivyobainishwa katika Kifungu cha 15 cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023.

### 1.4 Njia Zilizotumika Katika Utekelezaji wa Kazi za Kamati

**Mheshimiwa Spika**, Kanuni za Bunge Toleo la Februari, 2023 zimeweka masharti kwamba Taarifa yoyote ya Kamati inayoingia Bungeni, inatakiwa kubainisha njia zilizotumiwa na Kamati kufanya kazi inayotolewa Taarifa. Kwa msingi huo naomba kubainisha njia na mbinu zilizotumika na kuwezesha kukamilika kwa taarifa hii. Naomba kuzitaja njia hizo kama ifuatavyo: -

a) Mapitio ya jumla ya Ripoti za CAG ili kubaini maeneo ya kuwekea mkazo na kukidhi masharti ya Ripoti hiyo ulikuwa msingi wa kazi za Kamati zilizopangwa kwenye Ratiba;

b) Kupokea Vidokezo (*"briefs")* vya Ripoti za CAG kwa hoja za ukaguzi za mafungu yaliyopangwa kujadiliwa na Kamati kabla ya Kukutana na Afisa Masuuli anayehusika. Mbinu hii iliiwezesha Kamati kuzielewa

hoja na wigo wa mahojiano na Afisa Masuuli kwa lengo la kupata undani wa tatizo la matumizi mabaya ya fedha za umma;

c) Mahojiano na maafisa masuuli kuhusu hoja za ukaguzi ili kupata undani wa matatizo ya matumizi ya fedha za umma na kubaini chimbuko la tatizo, wigo wa dosari na uwezekano wa kuepuka matumizi mabaya ya fedha za umma;

d) Uchambuzi wa kina wa Taarifa za Wakaguzi wa hesabu za Fungu linalohusika kwa pamoja na majibu ya Menejimenti za Taasisi, wizara au Shirika lililokaguliwa. Lengo ni kuelewa kwa kina muktadha wa hoja na matatizo ya matumizi mabaya ya fedha za Umma; na

e) Tafiti mbalimbali kuhusu masuala ya usimamizi wa fedha za umma. Lengo la njia hii ni kuona na kuutumia uzoefu wa jumla unaopatikana kwa tafiti hizo ili kutathmini maeneo yenye matumizi mabaya ya fedha za umma kama yalivyoainishwa na CAG.

**Mheshimiwa Spika,** njia na mbinu hizo ziliiwezesha Kamati kufanya uchambuzi wa kina kwa nia ya kulishauri Bunge kuhusu hatua za kuchukua. Mbinu hizo ziliendana na matumizi na marejeo ya miongozo ifuatayo: -

a) Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977 inayoonesha dhamana ambayo Serikali imepewa na wajibu wa Bunge kuisimamia na kuishauri Serikali ikiwemo eneo la matumizi ya fedha za umma;

b) Sheria ya Ukaguzi wa Umma, 2008 inayofafanua masharti muhimu kwa ajili ya kuwezesha ukaguzi, uandaaji wa Ripoti za CAG, uwasilishaji wake na hatimaye kujadiliwa na Kamati;

c) Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, Sura 348 inayoweka miongozo ya matumizi ya fedha za umma na kusaidia kuamua iwapo kuna matumizi mabaya ya fedha za umma;

d) Sheria ya Bajeti, Sura ya 439, inayohusika na usimamizi wa matumizi ya Fedha za Umma kwa kuweka taratibu za utekelezaji wa bajeti na usimamizi wake;

e) Sheria ya Msajili wa Hazina Sura 370 inayogusa usimamizi wa matumizi ya Fedha za Umma katika mashirika ya umma;

f) Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura 410, inayoweka taratibu za kufuatwa wakati wa ununuzi wa bidhaa, huduma na kuingia mikataba kwa gharama ambazo zinahusisha matumizi ya fedha za umma;

g) Sheria ya Usajili wa Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu, Sura 286, inayosimamia weledi wa wahasibu na wakaguzi ili kuwezesha kumbukumbu za kutumainiwa za fedha na usimamizi bora wa matumizi ya Fedha za Umma;

h) Sheria ya Kinga Madaraka na Haki za Bunge, Sura 296 inayoliwezesha Bunge, Wabunge na Kamati za Bunge kupata stahili kutokana na madaraka yake na kupata ushahidi bila kukwama wakati wa kufuatilia matumizi ya fedha za umma; na

i) Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 zinazobainisha utaratibu wa Ripoti za CAG kuhusu matumizi ya fedha za umma kuwasilishwa Bungeni, kushughulikiwa na Kamati na hatimaye Kamati kutoa Taarifa hii.

### 1.5 Muhtasari wa Matokeo ya Utekelezaji wa Shughuli za Kamati

**Mheshimiwa Spika**, kwa kipindi cha mwezi Agosti 2023 hadi Novemba 2023, shughuli za Kamati zilijielekeza katika kushughulikia maeneo yenye matatizo sugu ya matumizi mabaya ya fedha za umma katika wizara na mashirika ya umma kama yalivyobainishwa katika Taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa mwaka wa fedha unaoshia tarehe 30 Juni, 2022. Aidha, shughuli hizo zilikusudia kufuatilia utekelezaji wa maoni na mapendekezo yaliyotolewa na Kamati ya Bunge ya

Hesabu za Serikali (PAC) kwa nyakati tofauti kwa kipindi chote cha mwaka 2022.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, kwa mwaka wa fedha ulioishia Juni 30, 2022, kwa upande wa Serikali Kuu, CAG alikagua na kutoa Hati za ukaguzi kwa Wizara na Idara za Serikali **65**, Balozi **43**, Sekretarieti za Mikoa **26**, Wakala **30** na Mifuko Maalumu **16.** Aidha, katika kundi hilo la Serikali Kuu, Kaguzi za Vyama vya Siasa **19**, Hospitali za Rufaa na Maalumu **34** na Taasisi nyinginezo **129** zilifanyika na kukamilika. Zaidi ya hayo, ukaguzi ulijumuisha Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Hesabu Jumuifu za Taifa *(consolidated accounts)* na ukaguzi wa awali wa mafao ya wastaafu kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2022.


**Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/22, katika mafungu ya Serikali Kuu, CAG alitoa jumla ya Hati **336** kwa Taasisi ambazo ziliwasilisha taarifa za fedha kwa ajili ya ukaguzi. Kati ya hizo, Hati **323** zilikuwa zinaridhisha, Hati **10** zilikua Hati zenye shaka, Hati **2** zilikuwa mbaya, na CAG alishindwa kutoa maoni kwa Taasisi **1**.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Mashirika ya Umma, jumla ya kaguzi **206** zilifanyika, ambapo katika kaguzi hizo Hati zilitolewa kwa Mashirika **203** ambapo kati ya hizo, Hati **193** zilikuwa Hati zinazoridhisha, **5** ni Hati zenye shaka na Mashirika **2** CAG hakuweza kutoa maoni *(disclaimer of opinion)*. Hapakutolewa hati mbaya katika Mashirika ya Umma.

**Mheshimiwa Spika,** katika ngazi ya Kamati, Kamati ilifanikiwa kuchambua na kujadili taarifa ya hesabu zilizokaguliwa za mafungu 18 ya Serikali Kuu, Mashirika ya Umma 39, Taasisi zinazojitegemea 10 na Mifuko Maalumu 13.

**Mheshimiwa Spika,** mchanganuo wa Taasisi zilizofika mbele ya Kamati kwa mahojiano umebainishwa katika Chati Na. 1.1 hapa chini: -

**Chati Na. 1.1: mchanganuo katika asilimia wa mafungu yaliyohojiwa na Kamati Agosti – Oktoba, 2023**




**Chati.Na. 1.1: Mchanganuo wa mafungu yaliyofika mbele ya Kamati kati ya Agosti – Novemba, 2023.**

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa kina wa hoja zilizofanyiwa kazi na Kamati kwa kila fungu unapatikana katika sehemu ya pili ya taarifa hii.

## 1.6 Ufuatiliaji wa Mapendekezo Yaliyotolewa na Kamati

**Mheshimiwa Spika,** kama ilivyoelekezwa katika Kifungu cha 13(b) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari, 2023 Kamati imekuwa ikifuatilia utekelezaji wa maoni,ushauri, mapendekezo na maazimio ya Kamati na Bunge kwa nyakati tofauti tofauti.

**Mheshimiwa Spika,** jambo hili hufanyika kwa CAG kufanya uhakiki wa maoni na mapendekezo yanayokuwa yametolewa na Kamati kwa fungu husika. Aidha, kila fungu linapofika mbele ya Kamati, CAG huipitisha Kamati kwenye taarifa ya utekelezaji wa maoni na mapendekezo ya Kamati kwa fungu husika kabla ya kuanza kupitia na kuchambua taarifa ya hesabu za fungu hilo.

## 1.7 Vigezo vya Uchambuzi

**Mheshimiwa Spika**, uaandaji wa vigezo vya kuzingatiwa ni jambo muhimu katika uhakiki na tathmini yoyote. Suala la matumizi mabaya ya fedha za umma linaweza kubainika kutokana na vigezo vya matumizi ya fedha za umma. Aidha, uamuzi wa

kuwahoji Maafisa Masuuli kutokana na Ripoti za CAG ni jambo lililohitaji kuwekewa vigezo. Kwa sababu hiyo, baada ya kupokea Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Kamati ilitengeneza vigezo muhimu vya kuzingatia katika kutimiza majukumu yake ya Kikanuni. Vigezo hivyo vilitoa mwongozo wa uchaguzi wa mafungu ambayo yalipewa kipaumbele katika uchambuzi na mahojiano na Maafisa Masuuli.

**Mheshimiwa Spika**, vigezo vilivyozingatiwa wakati wa kuchagua vipaumbele katika utekelezaji wa shughuli za Kamati vilikuwa kama ifuatavyo: -

a) Uzito wa hoja ya ukaguzi kama ilivyoibuliwa na CAG;

b) Maslahi ya Umma kuhusu hoja za fungu linalohusika;

c) Hali ya hati ya ukaguzi iliyotolewa kwa fungu linalohusika;

d) Kujirudia mara kwa mara kwa hoja husika katika Wizara, Idara, Wakala, Balozi au Mradi wa Maendeleo uliokaguliwa;

e) Kiwango cha fedha kinachohusika katika hoja za ukaguzi wa fungu linalohusika;

f) Kuleta uendelevu wa ufuatiliaji wa ushauri na maelekezo yaliyotolewa na Kamati kwa fungu husika kwa siku za nyuma;

g) Kutoa kipaumbele kwa Sekta na Mashirika Mkakati (Strategic sectors and parastatals) kwa kuzingatia utekelezaji wa malengo ya sasa ya Serikali;

h) Kaguzi maalum (Special audit) zilizofanyika hivi karibuni; na

i) Uzingatiaji wa kaguzi za ufanisi kwa mwaka husika.

**Mheshimiwa Spika,** vigezo hivyo viliisaidia Kamati kuendelea na mchakato wa kufuatilia matumizi ya fedha za umma kwa kuzingatia Ripoti za CAG. Nikiri kuwa bila vigezo hivyo ingekuwa vigumu kugusa aina mbalimbali za matumizi mabaya ya fedha za umma.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 MATOKEO YA UCHAMBUZI

**Mheshimiwa Spika,** kufuatia vigezo na mambo ya msingi niliyoyataja hapo awali, uchambuzi wa Taarifa ya CAG kwa mafungu mahususi ya Serikali Kuu na Mashirika ya Umma ulibainisha mambo yafuatayo kuhusu matumizi na usimamizi wa fedha za umma: -

### 2.1 Dosari Katika Usimamizi wa Ukusanyaji wa Mapato ya Serikali

#### 2.1.1 Nakisi ya Ukusanyaji wa Mapato Kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) Kiasi cha Sh. 887,301,296,148

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipitia na kuchambua taarifa ya hesabu zilizokaguliwa za Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni 2022. Lengo kubwa la uchambuzi wa taarifa hiyo ilikuwa ni kufanya tathmini ya hali halisi ya ukusanyaji wa mapato chini ya Mamlaka hiyo ukilinganisha na lengo lililokusudiwa. Hali kadhalika, Kamati ilijielekeza kupitia na kuchambua matumizi ya fedha yanayofanywa na TRA katika shughuli za ukusanyaji wa mapato ya Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kawaida Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) huandaa taarifa za hesabu katika mifumo miwili (2) tofauti, ambapo hesabu za makusanyo (revenue statement) huandaliwa katika Mfumo wa Kimataifa wa Uandaaji wa Taarifa za Hesabu (IFRS). Kwa upande wa hesabu za matumizi (expenditure statements), TRA huandaa hesabu zake kwa kutumia Mfumo wa Kihasibu wa Kimataifa wa Uandaaji Taarifa za Hesabu za Serikali (IPSAS)[1].

[1] International Public Sector Accounting Standards (IPSAS)

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa taarifa ya bajeti na makusanyo halisi ya TRA kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2022 imebainisha kwamba, TRA ilipangiwa kukusanya **Sh. 22,191,166,964,000**. Hata hivyo, makusanyo halisi yalikuwa **Sh.21,303,865,667,853** sawa ikiwa ni pungufu ya Sh. **887,301,296,148** sawa na asilimia 4. Kamati inatambua jitihada za TRA katika kukusanya kodi na mafanikio ambayo yamekuwa yakionekana kwa siku za karibuni.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na mafanikio hayo, Kamati ilijielekeza kuchambua taarifa ya CAG kuhusu ukaguzi wa TRA na kubainisha mapungufu kadhaa ambayo yamechangia kutofikiwa kwa malengo ya ukusanyaji wa mapato. Dosari hizo na kiasi cha fedha ambacho hakijakusanywa ni kama ifuatavyo: -

a) Kuchelewa kusajili mapingamizi ya Kodi (tax objection) yenye thamani ya **Sh.40,238,900,889**. Katika mapitio ya rejista za kodi katika Mikoa ya Kikodi 137, Kamati ilibaini uwepo wa mapingamizi ya kodi yenye thamani ya **Sh. 40,238,900,889** ambayo yamechukua muda wa miezi 6 hadi 94 kusajiliwa na Kitengo cha Ufundi tangu yalipowasilishwa;

b) Dosari katika utoaji wa taarifa sahihi za kodi itokanayo na michezo ya kubahatisha kiasi cha **Sh.1,406,970,429**. Katika uchambuzi wa taarifa ya CAG ilibainika kwamba wachezesha bahati nasibu 15 katika Mkoa wa Kikodi wa Ilala waliwasilisha taarifa za chini za kodi kwa kiasi cha **Sh. 2,567,061,857**. Aidha, wachezesha bahati nasibu 5 waliwasilisha taarifa za kodi za juu kwa kiasi cha **Sh. 1,160,091,428**, hivyo kufanya taarifa za kodi ya kiasi cha **Sh. 1,406,970,429** kuwasilishwa chini ya kiwango ilivyotakiwa (Net understatement). Hii ni kinyume na Kifungu cha 32 (2) cha Sheria ya Michezo ya Kubahatisha Sura, 41 [R.E. 2019];

c) Changamoto katika Mfumo wa Kielektroniki wa ufuatiliaji mizigo katika bidhaa zinazosafirishwa nje ya Nchi kwa kupitia hapa Nchini (ECTS). Hoja hii imechangia upotevu wa mapato ya Serikali hasa

katika nyakati ambazo mfumo huo hushindwa kufanya kazi maeneo ya mipakani hivyo kutoa mwanya wa udanganyifu;

d) Ushuru wa mafuta wenye thamani ya **Sh. 2,010,337,382** kwa lita za mafuta **2,271,511.45** ambayo yalitakiwa kusafirishwa nje ya Nchi lakini yakabaki na kutumika hapa Nchini haukukusanywa hivyo kuikosesha Serikali mapato stahiki;

e) Kutozingatiwa kwa Sheria ya Kodi kwa wafanyabishara waliosajiliwa kama wakusanya mizigo (consolidators).CAG alibaini kuwa wakusanya mizigo hao hukusanya mizigo ya wafanyabiashara na kuisafirisha katika kasha moja na kisha kulipa kodi. Hata hivyo, uchunguzi umebaini kuwa wasafirisha mizigo hao huonesha katika taarifa zao fedha kamisheni waliyolipwa na wafanyabishara wadogo badala ya kodi iliyolipwa kwa kuzingatia risiti ya kielektroniki. Hii ni kinyume na Tangazo la Serikali Na. 337 la Mwaka 2018 linalowataka kutoa taarifa sahihi za mizigo na kulipa kodi stahiki wao wenyewe;

f) Mwisho CAG alibaini ukadiriaji usio sahihi wa kodi ya zuio kiasi cha **Sh. 704,566,741** hivyo kuikosesha Serikali mapato stahiki.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilifanya mahojiano ya kina na Wakaguzi kwa pamoja na Bodi na Menejimenti ya TRA ili kuchambua misingi ya kutokusanywa kwa kodi ipasavyo na mikakati ya kuondokana na changamoto za kutofikiwa kwa ufanisi wa ukusanyaji wa mapato ya Serikali.Mathalani katika mapungufu ya ukusanyaji wa kodi ya VAT, ukaguzi ulibaini dosari katika mifumo ya TRA. Hii inathibitishwa na maelezo[2] ya Mkaguzi wa Hesabu za TRA Ndugu Donad Mayyo aliyotoa mbele ya Kamati na kunukuliwa kama ifuatavyo:-

[2] Rejea Ukurasa wa 34 wa Majadaliano ya Kamati, Taarifa Rasmi za Bunge Kikao cha Saba Tarehe 15 Agosti, 2023

**Nukuu:-**

***" Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi wakati tunafile hizo returns za VAT , mfumo unavuta taarifa za mauzo za mlipa kodi kutoka kwenye EFDs database pia inavuta manunuzi liyofanya mlipa kodi. Kwa hiyo eneo hili tuonaona meendelea kuboreshwa, lakini changamoto iliyopo ni mzigo una kiasi gani? Ndiyo mfumo hauwezi kuvuta kiasi cha mzigo, lakini thamani ya mzigo unavutwa na kodi ambayo melipwa. Kwa hiyo kwenye mfumo mpya sisi tulikuwa tunashauri, quantity ya item ambayo mlipa kodi ameimport pia ziwe tracked huku kwa maana ya wakati zinauzwa locally. Hapo ndiyo bado mamlaka haijaboresha sehemu hii…"***

**Mwisho wa Nukuu.**

**Mheshimiwa Spika,**kama maelezo ya wakaguzi hapo juu yalivyonukuliwa, bado kuna changamoto kubwa ya mifumo ya usimamizi wa kodi katika TRA inayotakiwa kufanyiwa kazi ili kuongeza ufanisi wa ukusanyaji wa mapato ya Serikali. Suala la mapungufu katika mifumo ya ukusanyaji kodi liliendelea kuwekewa msisitizo na Naibu Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Ndugu Benja Majura katika maelezo yake kwa Kamati kama yalivyonukuliwa hapa chini:-

**Nukuu:-**

***"…. Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nafikiri muendelee kuweka msisitizo kwamba hiyo mifumo ya ukusanyaji kodi iimarishwe kiasi kwamba kusiwe kuna dukuduku lolote kwa mlipa kodi na wao wenyewe wanapokusanya kodi.."***

**Mwisho wa Nukuu.**

**Mheshimiwa Spika,** katika kujibu hoja za Kamati kuhusiana na masuala ya changamoto za mifumo ya ukusanyaji wa mapato katika TRA, Bodi na Menejementi ya TRA walikuwa na maelezo ya

ufafanuzi. Kwa kuanza naomba kunukuu maelezo[3] ya Mwenyekiti wa Bodi ya TRA Ndugu Uledi Mussa mbele ya Kamati kama ifuatavyo:-

**Nukuu:-**

***"….Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu wa Korea Kusini ndiyo wanatusaidia katika hatua hii ya modernazition , tunataka tufikie wakati ambapo mlipa kodi asiwajibike kabisa kwenda kwenye Ofisi ya TRA. Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni suala ambalo haliepukiki kabisa, kwa sababu hatuwezi kufanya shughuli zetu za kukusanya mapato ya Serikali kwa kutumia mifumo ambayo imepitwa na wakati. Hilo tunalifanyia kazi na Serikali imeshatupa pesa kwaajili ya kutekeleza hilo. Hata Mheshimiwa Rais ametupa support kubwa sana kwenye hilo eneo, kwa sababu hata mwenyewe anataka TRA iwe ni miongoni mwa taasisi bora kabisa kwa upande wa ukusanyaji mapato.."***

**Mwisho wa Nukuu.**

**Mheshimiwa Spika,** vilevile Kamishina Mkuu wa TRA Ndugu Alphayo Kidata aliifahamisha Kamati hatua zinazochukuliwa katika kutatua changamoto ya mifumo. Naomba kunukuu maelezo yake mahsusi katika eneo hili kama ifuatavyo:-

**Nukuu:-**

***"…kwa sababu tu ya muda ningeyafafanua kwa kirefu sana kuona hiyo computarization ilipofikia sasa hivi, enhancement ya TANCIS na enhancement ya IDRAS , mifumo yote hii ina component zote ambazo Mheshimiwa Mwambe amezizungumzia ambazo zinazingatiwa effectively. Bahati nzuri Mheshimiwa Rais alitoa maelekezo kwamba anataka hii mifumo iwe imekamilika na mkataba wetu na hao Wakorea***

[3] Rejea Ukurasa wa 72 wa Majadiliano ya Kamati, Taarifa Rasmi za Bunge, Kikao cha Saba Tarehe 15 Agosti, 2023

***ulikuwa wa miezi 46. Tumekubaliana nao wame-confirm by writing kwamba watafanya kazi usiku na mchana na kuongeza manpower ili waweze kuachieve the same goal within 36 months, tunafanya kazi ili ndoto zilizozungumzwa na wajumbe zitimie…'***

**Mwisho wa Nukuu.**

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo, Kamati ilisisitiza umuhimu wa kukamilika kwa mifumo ya ukusanyaji wa mapato na kwa marekebisho ya mifumo hiyo kukamilika kwa wakati. Hoja ya Kamati ilisisitizwa kwa maelezo ya Mhe. Joseph G. Kakunda, Mb na Mjumbe wa Kamati ya PAC ambaye alisisitiza suala hili kwa maelezo[4] yafuatayo:-

**Nukuu:-**

***"…Ukirejea mission ya TRA kwamba ni kuwezesha urahisi wa kulipa kodi na kuhimiza ulipaji wa kodi wa hiari. Agizo la Kamati kuhusu mifumo ni la mwaka 2018, specifically iliagiza Bodi ya TRA kukamilisha mfumo mpya wa makusanyo ya ndani ( IDRAS[5]) lakini kwenye majibu na ukaguzi uliofuatia mpaka leo, mfumo huu haujakamilika. Sasa specifically we need to know muda mrefu ni miaka mingapi, miaka 50, 100 au mingapi?... nilifikiri zingekuwa zimekamilika leo…"***

**Mwisho wa Nukuu.**

### 2.1.2 Hasara ya Kiasi cha Sh.7,840,000,000 Katika Kampuni ya TANOIL

**Mheshimiwa Spika,** Kampuni ya TANOIL ni Kampuni Tanzu ya Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) ambayo imepewa jukumu la kufanya biashara ya uagizaji na usambazaji wa nishati ya mafuta. Uchambuzi wa Taarifa ya ukaguzi ya TANOIL imebainisha mapungufu katika usimamizi wa mapato ya

[4] Rejea Ukurasa wa 87 wa Majadiliano ya Kamati, Taarifa Rasmi za Bunge, Kikao cha Saba, Tarehe 15 Agosti, 2023

[5] Intergrated Domestic Revenue Accounting System (IDRAS)

Serikali. Kwa msingi huo, matarajio ya Serikali kwa kuanzishwa kwa kampuni hii bado hayajafikiwa ipasavyo.

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2021/2022, Kampuni ya TANOIL ilipata hasara ya **Sh. 7,840,000,000** ukilinganisha na hasara ya **Sh. milioni 166. 26** kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Uchambuzi wa kina Kamati umebaini hoja zifuatazo katika TANOIL ambazo zimechangia upotevu fedha za umma;

a) Menejimenti ya TANOIL haikuwa ikifanya usuluhisho wa kila mwezi wa mafuta yaliyonunuliwa na kuuzwa kwa kipindi husika. Mathalani kwa ukaguzi wa Juni 30, 2022 CAG alibaini kutofanyika usulushishi wa mafuta ya thamani ya **Sh. bilioni 1.8**;

b) Kuchelewa kunakili mapato yatokanayo na uuzaji wa mafuta. Katika hili CAG alibaini uwepo wa shehena 2 za mafuta yenye thamani ya **Sh. 16,182,909,231** ambayo ilipokelewa mwezi juni 2022 lakini haikuandikwa kwenye kwenye vitabu vya uhasibu vya TANOIL hadi mwaka wa fedha unakamilika;

c) CAG alibaini dosari kubwa katika bei za uuzaji mafuta zinazotumiwa na TANOIL ukilinganisha na kiwango bei kikomo zinazotolewa na EWURA.Mathalani, TANOIL waliuza mafuta kwa kampuni za ndani kwa bei ya chini hali iliyosababisha kupata hasara tarajali ya kifedha ya **Sh. 53,703,851,248**, na

d) Vilevile CAG alifanya mapitio ya nyaraka za malipo zilizotolewa kwa wateja na kubaini kuwa wateja walipewa ankara za malipo zenye bei ya chini ukilinganisha na bei iliyokubaliwa na kuidhinishwa na Menejimenti ya TANOIL.Matokeo ya hatua hiyo ni kuchaji bei ya chini wateja (undercharging of revenue) kwa kiasi cha **Sh. 30,942,362,750**.

**Mheshimiwa Spika,** mapungufu yaliyobainishwa hapo juu yamechangia kwa kiasi kikubwa hasara na upotevu wa mapato stahiki ya Serikali. Kamati ilifanya mahojiano na Bodi na

Menejimenti ya TANOIL na hatua wanazochukua kukabiliana na suala hilo. Mathalani mchango[6] wa Mhe. Issa J. Mtemvu, Mb na Mjumbe wa Kamati ya PAC kuhusu dosari zilizojitokeza ni kama unavyonukuliwa hapa chini:-

**Nukuu:-**

***"…..Moja ni kwamba, Mkaguzi anatambua kabisa bei zinaongozwa na EWURA, lakini walifika sehemu wakapunguza bei (undepriced) kwa zaidi ya sh 70/= wakati maelekezo yanasema, wanaweza kupunguza isizidi asilimia 30 ya bei elekezi, kwenye range na kupelekea hasara ya zaidi ya shilingi bilioni 53…"***

**Mwisho wa Nukuu.**

**Mheshimiwa Spika,** katika kujibu hoja ya Mhe. Issa J. Mtemvu kuhusu upotevu wa mapato ya Serikali kutokana na kutoza bei chini ya kiwango kilichokubaliwa, Ndugu James Sanawa – Ag. TGM (TANOIL) alikiri kutokea kwa suala hilo kwa maelezo yake kama ifuatavyo:-

**Nukuu:-**
***"…Mwenyekiti, nashukuru. Ni kweli kwamba zilitokea discounts ambazo ni juu ya kiwango au mwongozo uliotolewa…"***

**Mwisho wa Nukuu.**

**Mheshimiwa Spika,** ni kwa msingi huo TANOIL imeendelea kupata hasara kwa sababu ya kufanya maamuzi bila ya kuzingatia miongozo na taratibu zilizopo. Hata Kamati ilipoomba maelezo ya endapo TANOIL ilipata kibali cha kutoza bei chini ya kiwango cha EWURA hawakuwa na kibali hicho.Naomba kunukuu maelezo ya Mhe. Japhet N. Hasunga, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya PAC kama ifutavyo:-

[6] Rejea Ukurasa wa 82 wa Majadiliano ya Kamati , Taarifa Rasmi za Bunge, Kikao cha Nane tarehe 16 Agosti, 2023

**Nukuu:-**

***"… Sisi tunataka kibali mlipata wapi cha kucharge below standards za EWURA au prices za EWURA na below standards mlizokuwa mmekubaliana kwenye Menejimenti kwamba sisi bei zetu zitakuwa ni hizi?..." Tumesoma hapo kwenye report ikaonekana kwamba ninyi kuna watu wameact wameenda kucharge tofauti kabisa yaani below hata zile za Menejimenti, ndiyo tunataka utupe kibali…"***

**Mwisho wa Nukuu.**

**Mheshimiwa Spika,** katika kujibu hoja ya Mhe. Japhet N. Hasunga, Mb na Makamu Mwenyekiti wa PAC kuhusu uwepo wa kibali husika, maelezo ya Ndugu Gabriel Mwero , Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa TANOIL alikiri kutokuwepo kwa kibali husika. Maelezo yake ni kama yanavyonakiliwa hapa chini:-

**Nukuu:-**

***"… Mwenyekiti,naomba basi nijibu. Ni kweli hicho kibali hakikuwepo…"***

**Mwisho wa Nukuu.**

### 2.1.3 Tume ya Madini Kutokusanya Madeni Yanayofikia Sh. 30,757,555,988

**Mheshimiwa Spika,** katika kupitia na kuchambua taarifa ya hesabu zilizokaguliwa za Tume ya Madini, Kamati imebaini ongezeko la mapato ambayo hayajakusanywa na Tume ya Madini katika mwaka wa fedha 2021/2022. Hadi ukaguzi wa hesabu zinazoishia tarehe 30 Juni, 2022 unakamilika, Tume ya Madini ilikuwa haijakusanya madeni ya kiasi cha **Sh. 30,757,555,988**.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa kina wa Kamati katika hesabu za Tume ya Madini ulibainisha kwamba, sehemu kubwa ya madeni ambayo hayajakusanywa yanatokana na Tume ya Madini kudai kiasi **Sh.23,741,548,000** sawa na asilimia 77 ya deni

lote ambazo zinadaiwa kutoka kampuni ya TANCOAL kwa kipindi cha zaidi ya mwaka mmoja wa fedha.Deni hili la TANCOAL linathibitishwa katika maelezo ya Mkaguzi wa Hesabu za Tume ya Madini mbele ya Kamati kama ifuatavyo:-

**Nukuu:-**

***"…Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha kati ya makusanyo hayo kuanzia tarehe 01 Julai, 2022 mpaka tarehe 30 Juni, 2023 TANCOAL hawajalipa chochote katika deni lao, hivyo ninaishauri Tume iongeze juhudi katika kukusanya madeni hayo ili kuzuia hasara kwa Serikali…"***

**Mwisho wa Nukuu.**

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa Ofisi za Maafisa Madini Wakazi 29 na Ofisi ya Makao Makuu ya Tume ya Madini, katika Ofisi za Madini za Mikoa 17 mapato yasiyokusanywa yameongezeka kwa kiwango kinacholeta shaka kwa wakaguzi. Mathalani kwa Kituo cha Ofisi ya Madini Mkoa wa Shinyanga mapato yasiyokusanywa yaliongezeka kwa 17% (kutoka **Sh. 54,820,142** hadi **Sh. 63,918,241**), vilevile kwa Kituo cha Tabora mapato yasiyokusanywa yaliongezeka kwa 355% (kutoka **Sh. 170,009,014** hadi **Sh. 774,073,152**).

**Mheshimiwa Spika,** hoja ya mapato yasiyokusanywa kwa Tume ya Madini iliendelea kubainika pia kutokana na Tume kutokusanya mrabaha unaotokana na shughuli za ukaguzi wa madini ya ujenzi wenye thamani ya **Sh.890,007,615.48**. Mapato hayo hayakukusanywa katika Ofisi za Mikoa za Madini za Mikoa ya Shinyanga, Musoma na Kahama. Kutokukusanywa kwa mapato haya ni kinyume na masharti ya Kifungu cha 87 (1) cha Sheria ya Madini ya Mwaka 2010.

**Mheshimiwa Spika,** Menejimenti ya Tume ya Madini iliitwa na kufika mbele ya Kamati siku ya tarehe 16 Agosti, 2023, ambapo pamoja na masuala mengine walitakiwa kutoa maelezo ya sababu za kutokukusanya mapato ya mrabaha stahiki wa Serikali. Majibu yao kwa hoja hii yalikuwa kama ifuatavyo, naomba kuyanukuu hapa chini: -

**Nukuu:**
***"……. Tume imewasiliana na Wizara ya Madini na taasisi wadau ili kuwezesha ukusanyaji wa mapato, ikiwemo maboresho ya sheria ya madini (Cap 123)….. "***

**Mwisho wa Nukuu.**

**Mheshimiwa Spika,** kwa maelezo ya Menejimenti ya Tume ya Madini ni kwamba mrabaha husika haukusanywi ipasavyo kutokana na changamoto za utekelezaji wa baadhi ya masharti ya Sheria ya Madini, Sura 123. Hata hivyo, Kamati haikuona msingi wa majibu hayo kwa sababu, Sheria ya Madini, Sura 123 ni ya muda mrefu tangu mwaka 2010, hivyo endapo Tume ya Madini ambacho ndio chombo cha msingi cha kusimamia utekelezaji wa Sheria hiyo kwenye eneo la ukusanyaji wa mapato, kingekuwa kimeona changamoto zinazokwamisha ukusanyaji wa mapato ya Serikali wangewasilisha mapema mapendekezo ya kuondoa changamoto hizo za kisheria.

### 2.1.4 Mapato Yasiyokusanywa Kutokana na Mzabuni Kukiuka Masharti ya Mnada wa Vitalu vya Uwindaji Dola za Marekani 599,000

**Mheshimiwa Spika,** mnamo tarehe 09 Oktoba 2023, Kamati ilipitia na kuchambua taarifa ya hesabu zilizokaguliwa za Fungu 69 Wizara ya Maliasili na Utalii. Katika uchambuzi wake, Kamati ilibaini uwepo wa fedha kiasi cha **Dola za Marekani 599,000** ambazo Wizara ilishindwa kukusanya kutokana na mzabuni aliyeshinda zabuni ya vitalu 7 vya uwindaji wa kitalii kukiuka masharti ya mnada kwa makusudi hivyo kuikosesha Serikali mapato stahiki. Suala hili lilikiuka masharti yaliyowekwa katika Sehemu ya VI ya Sheria ya Usimamizi wa Wanyamapori Sura, 283 ya Mwaka 2009.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa taarifa ya ukaguzi, katika mwaka 2021/2022, Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori aliendesha mnada wa kielektroniki kwa kutangaza vitalu vya uwindaji katika tovuti ya Wizara kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 8(1) ya Kanuni za Uhifadhi Wanyamapori za Mwaka 2015. Uchambuzi wa taarifa ya ukaguzi umeendelea kubainisha

kwamba, kati ya tarehe 20 na 26 Septemba, 2023, Kampuni ya "*M/s Game Hunters Tanzania Ltd*" ilishiriki katika mnada wa kielektroniki wa vitalu vya uwindaji na kushinda vitalu (7).Hata hivyo, Kampuni hiyo ilikataa kulipa fedha ilizotakiwa kulipa kwa mujibu wa masharti ya mnada na hivyo kuingilia mchakato mzima wa mnada wa vitalu na kuikosesha Serikali mapato stahiki.

**Mheshimiwa Spika**, hoja ya ukaguzi ya CAG katika eneo hili inabainisha kwamba mzabuni husika alishindwa kulipa fedha stahiki za Serikali kwa makusudi. Naomba kunukuu sehemu ya hoja ya ukaguzi kama iliyoandikwa na CAG:-

**Nukuu:-**
***"..In our review it's noted that M/s Game Hunters Tanzania Ltd participated in the E – auction won seven ( 7) hunting blocks. However we noted that in vain and in deliberately reason the winning company refused to pay the allocation fees as a result interfered the proceedings of the auction with the intention to spoil the good aim of allocating the hunting blocks to investors…"***

**Mwisho wa Nukuu.**

**Mheshimiwa Spika,** mchanganuo wa vitalu ambavyo kampuni ya M/s Game Hunters Tanzania Ltd ilishinda na kiasi cha fedha kilichotakiwa kulipwa umefafanuliwa katika jedwali Na. 2.1 hapa chini:-

**Jedwali Na. 2.1: Vitalu vilivyotakiwa kulipiwa na Kampuni ya M/S Game Hunters Tanzania Ltd.**

| Na. | Jina la Kitalu | Mahali kilipo | Ukubwa(Sq. km) | Kiasi cha Fedha ( USD) |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Piti GR W | Katavi - Rukwa | 1,072 | 90,000 |
| 2. | Ugalla – Msima GR E | Malagarasi – Muyovosi | 2,099 | 81,000 |
| 3. | Ugalla – Msima GR W | Malagarasi - | 2,104 | 81,000 |

| Na. | Jina la Kitalu | Mahali kilipo | Ukubwa(Sq. km) | Kiasi cha Fedha ( USD) |
|---|---|---|---|---|
| | | Muyovosi | | |
| 4. | Mlele GCE - N | Katavi - Rukwa | 1,252 | 81,000 |
| 5. | Lwafi – Nkamba GR | Rukwa | 2,228 | 100,000 |
| 6. | Inyonga GR E | Katavi - Rukwa | 6,569.93 | 81,000 |
| 7. | Inyonga GR C | Katavi - Rukwa | 3,446.34 | 85,000 |
| **JUMLA** | | | | **599,000** |

**Chanzo:** ***Taarifa ya Ukaguzi ya Wizara ya Maliasili na Utalii, 2021/2022.***

**Mheshimiwa Spika,** Kamati iliomba kupata maelezo ya Wizara ni hatua gani walichukua kwa mzabuni huyo aliyekiuka masharti ya mnada hali iliyoikosesha Serikali mapato. Wizara ilitoa maelezo kuwa hapakuwa na Kanuni zinazoweka utaratibu wa kuchukua hatua kwa mzabuni anayekiuka masharti ya mnada wa ununuzi wa vitalu kwa wakati huo. Aidha, Wizara ilifafanua kwamba ipo katika hatua za mwisho kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha kutengeneza Kanuni za Mnada wa Kielektroniki ambazo pamoja na mambo mengine zitaweka utaratibu wa adhabu kwa wanaokiuka masharti ya mnada wa vitalu.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati haikuridhika na majibu yaliyotolewa kwa kuzingatia ukweli kwamba, mnada huu ulikuwa ni wa awamu ya tano tangu kuanza kufanyika, hivyo Wizara ilikuwa na uzoefu wa kutosha wa kuendesha minada husika ya vitalu vya uwindaji wa kitalii. Kwa msingi huo walitakiwa kuwa na kila njia ya kudhibiti shughuli za minada ya vitalu na kuiepusha Serikali na hasara iliyojitokeza.

### 2.1.5 Madeni Ambayo Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) Haujakusanya Kiasi cha Sh. 82,237,804,606

**Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2022 Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) ulikuwa na madeni ambayo hayajakusanywa (Receivables) ya jumla ya **Sh. 82,237,804,606**. Kati ya madeni ambayo hayajakusanywa , madeni ya kodi ya nyumba ni **Sh. 40,507,924,419** (49%) na madeni ya mauzo ya nyumba ni **Sh. 14,203,142,225** (17%).

**Mheshimiwa Spika,** hoja ya uwepo wa madeni unatokana pamoja na mambo mengine kwa TBA kutowachukulia hatua watumishi wa umma ambao waliuziwa nyumba 219 za Serikali zilizopo eneo la Bunju Dar es Salaam na nyumba 9 Arusha, kushindwa kuwachukulia hatua wapangaji 25 ambao wanadaiwa kodi **Sh.82,597,800** Mkoa wa Mbeya.Aidha TBA haikukusanya kodi kwa kipindi cha kuanzia miezi 10 hadi 103 kwa taasisi za umma kiasi cha **Sh. 4,767,496,800**.Vilevile TBA inadai **Sh.926,102,398.30** toka kwa Taasisi mbalimbali kutokana na kutekeleza kazi za usimamizi wa miradi.

**Mheshimiwa Spika,** athari ya kutokusanya mapato haya muhimu ya Serikali ni pamoja na kutochangia ipasavyo fedha katika mfuko mkuu wa Serikali. Vilevile kutokukusanywa kwa mapato hayo kunaathiri shughuli za usimamizi wa miradi ya TBA. Mathalani kwa mwaka huu tunaoutolea taarifa, TBA hawakujenga nyumba 632 zilizopangwa katika mradi wa Bunju na kutokamilika kwa wakati kwa miradi inayotekelezwa kwa kutumia makusanyo ya ndani.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipata fursa ya kupata maelezo ya Afisa Masuuli TBA siku ya tarehe 25 Oktoba, 2023 ili kujadiliana kuhusu hoja ya mapato ambayo hayajakusanywa, TBA waliifahamisha Kamati wameanza kutumia Mawakala wa Mahakama kukusanya madeni ya kodi za nyumba. Vilevile mawasiliano yamefanyika kwa Taasisi za Serikali kupitia kwa Makatibu Wakuu wa Wizara kuwasilisha madeni ya Taasisi ili yaingizwe kwenye mpango wa bajeti.

### 2.2 Hoja za Ukaguzi Zinazotokana na Dosari katika Usimamizi wa Mikataba na Athari zake Katika Matumizi ya Fedha za Umma

**Mheshimiwa Spika,** eneo lingine ambalo uchambuzi wa Kamati umebainisha uwepo wa upotevu mkubwa wa fedha za Serikali ni mapungufu au dosari katika uingiaji na usimamizi wa Mikataba. Uchambuzi wa Kamati umefafanua mafungu mahsusi yenye changamoto hiyo kama ifuatavyo: -

### 2.2.1 Kampuni ya IPTL Kutotimiza Wajibu wa Kimkataba Hivyo Serikali Kuwa Hatarini Kupatiwa Madai ya Sh. bilioni 148.4 Yanayotokana na IPTL

**Mheshimiwa Spika,** mnamo tarehe 26 Mei, 1995, Kampuni ya IPTL na TANESCO waliingia mkataba wa mauziano ya umeme (PPA)[7].pamoja na masharti mengine, katika mkataba huo, ilikubaliwa kwamba IPTL wangezalisha umeme kwa kiasi cha megawati 100.

**Mheshimiwa Spika,** wakati wa utekelezaji wa mkataba husika, kulijitokeza kutokukubalina kiwango cha tozo ya ununuzi wa umeme (Tarrif dispute) kati ya TANESCO na IPTL. Kutokana na mgogoro huo, tarehe 05 Julai, 2006, Serikali, IPTL na Benki Kuu ya Tanzania (BOT) waliamua kufungua Akaunti ya Escrow ili kutunza fedha zilizotokana na mgogogoro wa tozo za umeme. Benki Kuu ya Tanzania ilikuwa Wakala wa Akaunti husika (Escrow Agent).

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa makubaliano ya Akaunti ya Escrow, Serikali ililipa fedha za tozo ya umeme katika Akaunti hiyo na kuweka dhamana kwa niaba ya TANESCO. Aidha, TANESCO iliacha kulipia tozo ya malipo ya umeme kwa mujibu wa mkataba wa uzalishaji (PPA) kwenda kwa IPTL na badala yake ikaanza kuweka malipo husika kwenye Akaunti ya Escrow.

**Mheshimiwa Spika,** ilipofika mwezi Oktoba 2013, TANESCO na IPTL walifikia makubaliano kuhusu mgogoro wa tozo za ununuzi wa umeme. Kwa msingi huo, tarehe 21 Oktoba, 2013, aliyekuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini kwa niaba ya Serikali aliingia makubaliano na Kampuni ya IPTL ya kutoa fedha kwenye Akaunti ya Escrow. Makubaliano hayo yalifahamika kama "Agreement for Delivery of Funds to IPTL". Aidha, taarifa ya CAG inabainisha kwamba, kati ya tarehe 28 Novemba na 06 Disemba, 2013 fedha za Akaunti ya Escrow zilihamishwa kwenda kwa Kampuni ya PAP ambaye kwa muda huo alitambulishwa kama mmliki wa IPTL.

**Mheshimiwa Spika,** kufuatia uhamisho huo wa fedha, Benki ya Standard Chartered Hongkong (SCBHK) iliibua madai kwamba,

[7] Power Purchase Agreement

Kampuni ya PAP imetoa **Dola za Marekani Milioni 75** zilizokuwa kwenye Akaunti ya Escrow kuilipa Kampuni ya VIP Engenieering ambayo ilikuwa na hisa 30% katika IPTL badala ya kulipa wajibu wa TANESCO kwa SCBHK ambalo ni deni lililochukuliwa hapo awali kwa kuzingatia masharti ya mkataba wa uzalishaji na uuzaji wa umeme (PPA).

**Mheshimiwa Spika,** hoja ya SCBHK katika eneo hili inatokona na maelezo kwamba, Kampuni ya IPTL Tanzania ilikuwa na mkopo Benki ya Standard Chartered Hong Kong ambao kwa upande wao wanadai kuwa kampuni ya Pan African Power Solutions Tanzania walitumia baadhi ya fedha kutoka kwenye akaunti ya escrow kulipa hisa za kampuni ya VIP katika Kampuni ya Independent Power Tanzania, badala ya kutimiza wajibu wa malipo wa Shirika la Umeme Tanzania chini ya PAP na kulipa mkopo.

**Mheshimiwa Spika,** kwa sababu hiyo, mwaka 2016 Kituo cha Kimataifa cha Kutatua Migogoro ya Uwekezaji (ICSID)[8] kiliamua kuwa TANESCO lazima iilipe Benki ya Standard Chartered Hong Kong **Dola za Marekani milioni 148.4** pamoja na riba. Kufuatia uamuzi huo, mnamo mwaka 2018 Serikali iliwasilisha kesi ya madai katika Mahakama Kuu ya Tanzania dhidi ya kampuni ya IPTL ili kutekeleza hati ya fidia iliyotiwa saini tarehe 27 Oktoba 2013 ambayo inalinda hatua ya Serikali kutoa fedha kwenye akaunti ya Escrow kutokana na madai ya wahusika wa nje.

**Mheshimiwa Spika,** uamuzi wa tarehe 1 Machi 2021 ulikuwa kwa upande wa Serikali na kampuni ya IPTL ilikubali kuilipa Serikali **Dola za Marekani Milioni 148.4** mnamo tarehe 01 Machi 2021, hata hivyo hadi wakati wa ukaguzi, mwezi Disemba 2022, IPTL hawakuwa wamelipa kiasi kinachodaiwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ina hofu kuwa endapo Serikali italipa madai ya Benki ya Standard Chartered Hong Kong kufuatia uamuzi wa Kituo cha Kimataifa cha Kutatua Migogoro bila kupata kiasi hicho kutoka kwa kampuni ya IPTL, itakuwa imefanya malipo mara mbili kwa kuwa malipo ya umeme tayari yalifanywa kwenye akaunti ya escrow, na kampuni ya IPTL ilitoa

[8] International Centre for Settlement of Investment Disputes

ahadi kupitia hati ya kulinda madai(Indemnity)[9] ambayo iliiondolea Serikali madai yoyote ya Benki ya Standard Chartered Hong Kong.

**Mheshimiwa Spika,** katika kufafanua uzito wa hoja hii naomba kunukuu maoni ya CAG katika taarifa yake kwa Kamati kama ifuatavyo: -

> **Nukuu:**
> ***"…nina mashaka kuwa kuchelewa kwa kampuni ya IPTL kulipa deni lake kunasababisha Serikali kuchelewa kupata fedha za kuilipa Benki ya Standard Chartered Hong Kong. Hali hii inapelekea kuongezeka kwa mkopo kwa sababu ya riba inayoongezeka hivyo kuchafua sifa ya Nchi yetu katika jukwaa la kimataifa…."***
> **Mwisho wa Nukuu.**

**Mheshimiwa Spika,** kwa msingi wa nukuu ya CAG hapo juu, ni dhahiri kuwa kampuni ya IPTL imekiuka masharti ya utekelezaji wa mkataba. Aidha, Serikali na TANESCO bado hawajafuatilia kikamilifu utekelezaji wa masharti ya kipengele cha mkataba kinachotaka kumbana IPTL kutekeleza wajibu wake.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inatambua kuwa mikataba mingi ambayo TANESCO iliingia na kuisababisha Serikali hasara ni ya kihistoria. Hata hivyo, kunatakiwa jitihada kumaliza migogoro ya kesi hizo. Mathalani, maelezo ya aliyekuwa Mkurugenzi Mkuu wa TANESCO Ndugu Maharage Chande kwa Kamati kuhusu uvunjifu na hasara inayotokana na mikataba hiyo ni kama ifuatavyo:-

> **Nukuu.**
> ***"…Mheshimiwa Mwenyekiti, niwahakikishie sisi na Bodi yetu tuko makini kwenye mikataba na hakuna mkataba mpya ambao tumevunja bila ya kufuata sheria.. hii tunayopambana nayo ni mikataba ya kihistoria. Kama tunavyofahamu, DOWANS imeprogress, RICHMOND, DOWANS, SYMBION na inaendelea na IPTL nayo***

[9] Security against or exemption from legal liability for one's actions

***inaendelea…..Mkataba wa IPTL kama mnavyofahamu kuna Kamati ya Serikali (GNT) iko katika mazungumzo ya kunegotiate settlement ya kesi, matokeo ya kesi iliyotokea. Kwa hiyo tupo bado kwenye Kamati hizo kupambana kupunguza gharama ambazo tunaweza kuziingia…"***

**Mheshimiwa Spika,** ukifuatilia kwa makini historia ya suala hili la IPTL na majibu ya TANESCO hapo juu ni dhahiri kwamba endapo Serikali haitachukua hatua za haraka katika suala hili kuna uwezekano mkubwa wa Serikali kutopata nafuu ya kifedha kutokana na IPTL kuvunja masharti ya makubaliano ya utolewaji wa fedha katika iliyokuwa Akaunti ya Escrow. Hivyo Serikali inaweza kulazimika kulipa madai mbalimbali ambayo yanaendelea kuibuliwa kutoka kwa taasisi, kampuni au watu binafsi waliokuwa wanaidai Kampuni ya IPTL hapo awali.

### 2.2.2 Mapungufu Katika Usimamizi wa Mradi wa Usambazaji Maji Same - Mwanga - Korogwe

**Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2021/22 Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali alikagua Hesabu za Wizara ya Maji zilizojumuisha taarifa za Mradi wa Usambazaji Maji wa Same-Mwanga-Korogwe. Mradi huu unatekelezwa na Serikali ya Jamhuri ya Tanzania kupitia Wizara ya Maji kwa ushirikiano na Benki ya Kiarabu ya Maendeleo ya Uchumi wa Afrika (BADEA), Shirikisho la Nchi Wanachama Wauzaji wa Mafuta ya Petroli (*Organization of the Petroleum Exporting Countries* - OPEC),Mfuko wa Kimataifa wa Maendeleo wa OPEC (OFID), Mfuko wa Maendeleo wa Kuwait (*Kuwait Fund for Arab Economic Development*- KFD), na Mfuko wa Maendeleo wa Saudi (SFD) ikiwa ni mkopo wa masharti nafuu kama inavyooneshwa katika jedwali 2.2 hapa chini:

**Jedwali Na. 2.2: Mchanganuo wa Ufadhili wa Mradi wa Usambazaji Maji Same - Mwanga - Korogwe**

| Mkataba Na. | Mdau | Mchango (USD) | Kiasi kilicholipwa (USD) | Bakaa (USD) |
|---|---|---|---|---|
| I | BADEA | 8,602,194.05 | 5,554,566.30 | 2,746,411.39 |
| | OFID | 12,001,714.96 | 7,758,353.12 | 3,831,772.05 |
| | GOT | 20,752,793.14 | 13,391,726.27 | 6,625,717.49 |
| | **Jumla** | **41,356,702.15** | **26,704,645.69** | **13,203,900.93** |
| II | Kuwait | 27,311,696.75 | 12,008,554.18 | 13,652,536.81 |
| | GOT | 8,767,162.89 | 3,854,793.48 | 4,382,518.42 |
| | **Jumla** | **36,078,859.64** | **15,863,347.66** | **18,035,055.23** |
| IV | BADEA | 4,300,389.32 | 3,569323.13 | 632,468.68 |
| | OFID | 9,369,913.84 | 7,777,028.48 | 1,378,055.95 |
| | SFD | 17,624,546.38 | 14,628,373.50 | 2,592,084.77 |
| | GOT | 3,954,948.20 | 3,282,607.01 | 581,663.82 |
| | **Jumla** | **35,249,797.74** | **29,257,332.12** | **5,184,273.22** |
| **Jumla kuu** | | **112,685,359.53** | **71,825,325.47** | **36,423,229.38** |

**Chanzo:** ***Taarifa ya Wizara ya Maji kuhusu Mradi wa Same,Mwanga, Korogwe, 2023.***

**Mheshimiwa Spika,** Mradi huu ulipangwa kutekelezwa katika awamu mbili (*phase I & II*); ambapo awamu ya kwanza inahusisha: Ujenzi wa chanzo *(intake)*; Ujenzi wa kituo cha kupokea na kupooza umeme (*electrical power sub-station*); Ujenzi wa chujio *(water treatment plant)*; Ujenzi wa matenki 16 yenye ujazo tofauti kati ya lita milioni 3 na lita millioni 9 katika miji ya Same na Mwanga; Ujenzi wa miundombinu ya kusambaza maji katika miji ya Same na Mwanga; Kujenga miundombinu ya maji katika Vijiji 2 vya Ruvu Mferejini na Ruvu Jiungeni katika Wilaya ya Same na Vijiji 7 vya Handeni, Lang'ata Bora, Lang'ata Kagongo, Nyabinda, Kiti cha Mungu, Njia Panda na Kirya katika Wilaya ya Mwanga.

**Mheshimiwa Spika,** katika awamu ya pili mradi huu unahusisha ujenzi wa miundombinu ya kusambaza maji katika Vijiji 29 ambapo Vijiji 14 vipo Wilaya ya Same; Vijiji 10 Wilaya ya Mwanga na Vijiji 5 katika Wilaya ya Korogwe.

**Mheshimiwa spika,** Katika awamu ya kwanza Wizara ya Maji iliingia mikataba mitatu yaani tarehe 20 Novemba 2014 na

Mkandarasi M.A. Kharafi & Sons, tarehe 13 Oktoba 2016 na mkandarasi Badr East Africa Enterprises Ltd na tarehe 6 Agosti 2018 na mkandarasi Badr East Africa Enterprises Ltd; yote kwa ujumla ikiwa na thamani ya **Dola za Marekani milioni 112.69** kwa ajili ya kutekeleza ujenzi wa mradi huo. Mkataba huu ulikuwa ukisimamiwa na Mhandisi Mshauri M/S ECG Engineering Consultants Groups S.A kwa kushirikiana na Howard Humphreys (Tanzania) Limited kupitia mkataba uliosainiwa tarehe 31 Julai 2013 kwa gharama ya **Dola za Marekani 432,320** na **shilingi 126,149,375** bila VAT.

**Mheshimiwa Spika,** Mkataba wa kwanza uliingiwa kati ya Wizara ya Maji na Kharafi & Sons **USD 41,356,702.15** tarehe 20 Novemba 2014 Wizara ya Maji ilisaini mkataba na Kharafi & Sons kwa kiasi cha **Dola za Marekani USD 41,356,702.15**; na ulitarajiwa kukamilika tarehe 16 Julai 2017 kwa kutekeleza kazi zifuatazo: Ujenzi wa Chanzo; Ujenzi wa Chujio; Ujenzi wa Tenki la kuhifadhi maji Kisangara; Ujenzi wa bomba la kusafirisha maji ghafi kwenda kwenye chujio na Ujenzi wa bomba la kusafirisha maji yaliyotibiwa kwenye tenki la kisangara.

**Mheshimiwa Spika,** Mkataba huu ni "Time Based" hivyo umekuwa ukifanyiwa marekebisho (addendum) mara muda wa awali unapoisha na marekebisho ya mwisho (Addendum No.8) yalisainiwa tarehe 31 Julai 2023 yakifanya jumla ya gharama za mkataba huu kuwa **Dola za Marekani 2,085,019.20** na **Sh. 1,816,301,229.87** bila VAT kwa mkataba wa awali na nyongeza zake zote 8. Hadi kufikia tarehe 30 Septemba 2023 Kiasi kilicholipwa kwa Mhandisi Mshauri M/S ECG Engineering Consultants Groups S.A ni **USD 1,691,702.27** na **Sh. 1,169,540,051.28** kwa Howard Humphreys (Tanzania) Limited.

**Mheshimiwa Spika,** Mkataba Na. I ulisitishwa tarehe 29 Desemba 2020 kwa sababu za mkandarasi (mjenzi) kukiuka masharti ya mkataba kwa kushindwa kuhuisha dhamana ya utekelezaji kazi wa mradi (Performance Guarantee). Mkandarasi alikuwa ametekeleza kazi kwa asilimia 64 na akiwa amelipwa jumla ya **Dola za Marekani 26,704,645.75**. Hata hivyo baada ya majadiliano ya muda mrefu mkandarasi alirejeshwa tena tarehe 13 Machi 2023 ikiwa ni miaka miwili na miezi 2 baada ya kusitishwa kwa mkataba wa awali. Hali hii imesababisha

kuongezeka kwa gharama za mkataba kutoka **Dola za Marekani 41,356,702.15** hadi **Dola za Marekani 54,428,952.22** ikiwa ni ongezeko la **Dola za Marekani 13,072,250.07.**

**Mheshimiwa Spika,** Mkataba Na. II wa mradi huu ulikusudia kujenga miundombinu ya maji katika Vijiji 2 vya Ruvu Mferejini na Ruvu Jiungeni katika Wilaya ya Same na Vijiji 7 vya Handeni, Lang'ata Bora, Lang'ata Kagongo, Nyabinda, Kiti cha Mungu, Njiapanda na Kirya katika Wilaya ya Mwanga. Hata hivyo Mkataba Na.II haukutangazwa na hivyo kazi hazikutekelezwa.

**Mheshimiwa Spika,** Mkataba Na. III uliingiwa kati ya Wizara ya Maji na Badr East Africa Enterprises Ltd **USD 36,078,859.64**. Mkataba huu ulisainiwa tarehe 6 Agosti 2018 kati ya Wizara ya Maji na Mkandarasi M/S Badr East Africa Enterprises Ltd kwa thamani ya **Dola za Marekani 36,078,859.64**. Mkandarasi alianza utekelezaji tarehe 5 Septemba 2018 na mkataba ulitarajiwa kukamilika tarehe 4 Machi 2021.Mkataba huu ulikuwa kwa ajili ya kazi zifuatazo: Ujenzi wa kituo cha kusukuma maji Kisangara; Ujenzi wa tanki la Vudoi (Mwanga); Ujenzi wa mtandao wa maji katika mji wa Mwanga; Ujenzi wa bomba la kusafirisha maji kutoka Kisangara hadi tenki la Kiverenge; Ujenzi wa bomba kuu kutoka tenki la Kiverenge hadi kwenye tenki la Vudoi (Mwanga).

**Mheshimiwa Spika,** hata hivyo mkataba huu ulisitishwa tarehe 30 Desemba 2020. Kazi zilizofanyika zilikuwa zimefikia thamani ya **Dola za Marekani 18,056,478.93** na kiasi kilichokuwa kimelipwa ni **Dola za Marekani 15,863,347.66.**

**Mheshimiwa Spika,** Mkataba Na. IV uliingiwa kati ya Wizara ya Maji na Badr East Africa Enterprises Ltd USD 35,249,092.76. Mkataba huu ulisainiwa tarehe 13 Oktoba 2016 kati ya Wizara ya Maji na M/S Badr East Africa Enterprises Ltd wenye thamani ya **Dola za Marekani 35,249,092.76**. Mkataba huu ulianza tarehe 1 Juni 2017 na ulitarajiwa kuisha 30 Desemba 2020. Mkataba huu ulikuwa kwa ajili ya kutekeleza kazi zifuatazo: Ujenzi wa tenki la maji Kiverenge; Ujenzi wa Matenki 3 ya Same I, II & III; Ujenzi wa bomba kuu kutoka tenki la Kiverenge hadi kwenye matenki ya Same I, II &III; Ujenzi wa tanki la Vudoi (Mwanga) na Ujenzi wa mtandao wa maji katika mji wa Same.

**Mheshimiwa Spika,** kama ilivyokuwa kwa mikataba ya awali, mkataba huu ulisitishwa tarehe 30 Desemba 2020 wakati mkandarasi M/S Badri E.A Enterise Ltd akiwa ametekeleza kazi kwa asilimia 87 zenye thamani ya **Dola za Marekani 30,065,975.55**; na kiasi cha **Dola za Marekani 29,258,384.00** kikiwa kimelipwa kwa mkandarasi.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa taarifa ya ukaguzi, sababu za kusitishwa kwa mikataba yote miwili ya M/S Badri East African Enterprises Limited ni uwepo wa vitendo vya udanganyifu katika nyaraka za mkandarasi ambapo aliwasilisha **"*Advance payment guarantee*" na "*Retention Money Guarantee*" za kughushi.**

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na kusitishwa kwa mikataba hiyo ya awali, Wizara imekuwa ikiingia mikataba mingine midogo kutekeleza mradi huo. Mathalani, ukaguzi ulibaini mwaka 2021 Wizara ya Maji iliikabidhi Mamlaka ya Usambazaji maji na usafi wa Mazingira ya jiji la Dar es Salaam (DAWASA) kujenga miundombinu ya kusambaza maji (*distribution networks*) katika miji ya Same na Mwanga. Kazi hizi zilikuwa zimefikia asilimia **46.7** kwa mji wa Mwanga na asilimia **86.7** kwa mji wa Same kabla ya kuvunja mkataba.

**Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia DAWASA iliingia mkataba na kampuni ya Advent Construction Ltd tarehe 27 Oktoba 2021 kwa kiasi cha **Shilingi 6,267,771,550.23** kwa ajili ya kukamilisha ulazaji wa bomba kuu kutoka Kiverenge hadi Same na ufungaji wa mfumo wa umeme na viungio katika matenki. Mkataba huo ulianza tarehe 21 Aprili 2022 na ulitarajiwa kukamilika 21 Desemba 2022. Hata hivyo, Wizara ilimpa mkandarasi muda wa nyongeza mpaka tarehe 18 Aprili 2024. Kazi imefikia asilimia 51 na kiasi cha **Sh. 1,256,344,682.50** kimelipwa hadi kufikia tarehe 30 Septemba 2023.

**Mheshimiwa Spika,** tarehe 11 Februari 2022 Wizara ya Maji iliingia mkataba na Helpdesk Engineering Ltd kwa ajili ya kazi ya kulaza mabomba hayo katika kilomita 34.5 na kukamilisha ujenzi wa tenki la Vudoi (Mwanga) na ufungaji wa viungio katika tenki hilo kwa mkataba wa **Dola za Marekani 5,905,797.25**. Mkataba huu ulianza tarehe 27 Mei 2022 na ulitarajiwa kukamilika tarehe 27 Oktoba 2022 hata hivyo muda uliongezeka mpaka 31 Desemba

2023. Mkandarasi alishalipwa **Dola za Marekani 1,615,299.67** na hali ya utekelezaji ni asimilia 38.1 hadi kufikia tarehe 30 Septemba 2023.

**Mheshimiwa Spika,** tarehe 24 Oktoba 2022 Wizara iliingia mkataba na Mkandarasi M/s Central Electricals Ltd wa kununua na kufunga transfoma (zenye uwezo wa 12MVA) katika kituo cha kusukuma maji cha Kisangara kwa **Dola za Marekani 2,322,663.17**. Mkataba huu ulianza tarehe 8 Novemba 2022 na ulitegemewa kukamilika 7 Aprili 2023 lakini muda umeongezeka hadi tarehe 6 Aprili 2024. Kiasi cha **Dola za Marekani 348,399.48** kimelipwa kama malipo ya awali na Barua ya Muamala ya **Dola za Marekani 1,509,731.06** ya tarehe 20 Septemba 2023. Kazi imefikia asilimia 3.1 hadi kufikia tarehe 30 Septemba 2023.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya kuwasilisha mtiririko huo wa taarifa za utekelezaji wa mradi, naomba kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba, kwa ujumla hali ya utekelezaji wa mikataba yote ni 79% hadi kufikia tarehe 30 Septemba 2023 kwa mikataba yote.

**Mheshimiwa Spika,** taarifa ya ukaguzi imebainisha mapungufu mengine mahsusi katika utekelezaji wa mkataba huo kama ifuatavyo:-

a) Kuisha muda wa dhamana ya mkopo kabla ya fedha zote za mkopo kutolewa. Katika hoja hii ukaguzi ulibaini kuwa makubaliano ya mkopo yalimalizika tarehe 30 Disemba, 2020 wakati watoaji wa mkopo wakiwa wametoa mkopo wenye thamani ya **Dola za Marekani 71,825,325.47** sawa na **Sh. bilioni 165.63** ambayo ni 64% ya makubaliano ya mkopo hivyo kuacha kiasi cha **Dola za Marekani milioni 40.86** sawa na **Sh.bilioni 94.22** ambazo hazijatolewa. Hoja ya kutokuwepo makubaliano ya kuongeza muda wa mkataba wa mkopo (loan financing agreement) unathibitishwa na maelezo ya CAG kama yalivyonukuliwa hapa chini:-

**Nukuu:**

***"….We are yet to receive documents for extension grants from Saudi Fund Development (SFD) and Kuwait Fund for Arab Economic Development (KFD)…"***

**Mwisho wa Nukuu.**

b) Wizara ya Maji kusaini mkataba na kampuni ya M/s Helpdesk Engineering Ltd kabla ya kuandaa hesabu za mwisho za mradi (final accounts) baada ya kuvunjwa kwa mkataba wa awali wa mkandarasi[10]. Athari ya kutoandaa hesabu za mwisho za mradi ni kuwa gharama za mkandarasi mpya zinakosa uhalali na usahihi. Hoja hii inathibitishwa na maelezo ya CAG kama yanavyonukuliwa hapa chini:-

**Nukuu:-**

***" ….Until the final account report is submitted, assessment to justify the relevance of the costs of the uncompleted works by the terminated contractor (M/s BADR) to substantiate the basis for determining the contract price of the incoming contractor M/s Helpdesk can be underatken…."***

**Mwisho wa Nukuu.**

c) Ongezeko la gharama za mkataba kwa 64% bila ya kuwa na sababu za msingi. Katika hoja hii ukaguzi ulibaini kuwa gharama za awali za mkataba katika awamu ya IV zilikuwa **Dola za Marekani 2,295,328.00** sawa na **Sh. 5,293,026,368**. Kwa mujibu wa taarifa ya ukaguzi, tarehe 11 Februari, 2022 Wizara ya Maji ilisaini mkataba Na. ME-011/2020- 2021/CONTRACT/W/03 na Kampuni ya M/s Helpdesk Engineering kwaajili ya kujenga bomba lenye urefu wa kilometa 34.5 kwa

[10]Rejea Mkataba Na. ME- 011/2018/2019/W/CONTRACT/01 with M/s BADR EAST AFRICA ENTERPRISES LTD uliovunjwa kupitia barua yenye Kumb. Na. ECGHH/SMK/KF607/2021 ya tarehe 9 Machi 2021

gharama ya **Dola za Marekani 3,610,256.25**. Hata hivyo, kabla ya kuanza utekelezaji wa mradi Wizara ikatengeneza mabadiliko ya mkataba ambayo ilibadili mawanda ya kazi na kuongeza gharama za mradi kwa **Dola za Marekani 2,295,328** hivyo kuongeza gharama za mradi hadi kufikia **Dola za Marekani 5,905,587.25**. CAG hakupata uthibitisho iwapo kulikuwa na ushahidi wa vibali vya kuruhusu maamuzi hayo. Vilevile CAG alishangazwa na uharaka wa Wizara kusaini nyongeza ya kazi kabla ya kuanza utekelezaji wa mradi katika mkataba wa awali;

d) DAWASA walilipa gharama za mkandarasi M/s Kharafi & Son kwa mkataba uliovunjwa **Sh. 360,237,233.29** bila ya kuwa na mkataba; na

e) DAWASA walimlipa mshauri mwelekezi kiasi cha **Sh. 360,764,500** bila ya kuwa na mkataba.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia hoja ambazo ukaguzi huu umebaini, ni dhahiri kwamba utekelezaji wa mradi wa maji wa Same, Mwanga, Korogwe umekuwa na changamoto kubwa. Kuna mapungufu makubwa ya usimamizi wa mradi huu hali ambayo imesababisha gharama za mradi kuongezeka, kuvunjwa kwa mikataba kila mara, changamoto za ufadhili wa mradi na pia kutokamilika kwa wakati kwa mradi. Aidha mradi huu ni wa muda mrefu hivyo busara ya Kamati iliona ni bora ukaangaliwa kwa kina kabla ya kuhitimisha hoja yake.Hivyo majibu ya Wizara ya maji yalipokelewa na yametumika kuandaa maeneo ambayo yanatakiwa kufanyiwa kazi zaidi na CAG. Kutokana na dosari hizo, Kamati imeandaa pendekezo mahsusi la kufanyika ukaguzi wa kina wa mradi huu ambalo lipo katika sehemu ya tatu ya taarifa hii.

### 2.2.3 Uchambuzi wa Taarifa ya Ukaguzi wa Kiufundi Kwenye Utekelezaji wa Mradi wa Ujenzi Reli ya Kisasa (SGR)

**Mheshimiwa Spika,** Ukaguzi huu wa Kiufundi (Technical Audit) ulizingatia vipande 5 vya mradi. Vipande hivyo ni kipande cha 1 na 2 (Dar es Salaam hadi Morogoro; na Morogoro hadi

Makutupora), ukaguzi ulilenga kufuatilia mapendekezo ya ukaguzi wa awali, kazi ambazo hazijakamilika, uwekaji wa mfumo wa umeme, ununuzi wa mabehewa na vichwa vya kuvuta mabehewa na ufungaji wa ishara na mawasiliano.

**Mheshimiwa Spika,** kwa vipande vya 3, 4, na 5,ukaguzi ulijikita kwenye hatua zote za mradi ikihusisha kupanga mradi, usanifu wa awali, mchakato wa ununuzi wa mkandarasi, utekelezaji wa mkataba na kufuatilia kuzingatiwa kwa masuala ya rasilimali watu, mazingira, usalama kazini, na mambo ya kijamii.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya uchambuzi wa taarifa ya Ukaguzi huo wa Kiufundi, naomba kulitaarifu Bunge lako matokeo ya ukaguzi kwa kuzingatia taarifa husika kama ifuatavyo:-

**2.2.3.1 Kutokuwepo Vielelezo vya Vigezo vya Viwango vya Umeme Vilivyotolewa kwa Mkandarasi Kwaajili ya Kuweka Bei**

**Mheshimiwa Spika,** taarifa ya ukaguzi inabainisha kwamba, Sura ya 2 ya Mwongozo wa Upangaji na Majadiliano ya Miradi ya Kuongeza Mikopo, Utoaji wa Dhamana na kupokea Ruzuku, iliyoandaliwa na Wizara ya Fedha na Mipango mwezi Novemba 2020 inazitaka Wakala za utekelezaji wa mradi huu kuhakikisha kuwa upembuzi yakinifu na mapendekezo ya mradi kuwa na taarifa zote muhimu ili kuwezesha uamuzi sahihi na kuonesha picha halisi ya uwezekano wa utekelezaji wa mradi.

**Mheshimiwa Spika,** kipindi cha majadiliano ya mkataba kati ya Muunganiko wa Kampuni ya Yapi Merkezi na Mota-Engil na TRC (kwa kipindi hicho ilikuwa inaitwa RAHCO) yaliyofanyika Januari, 2017, ilihusisha tathmini ya masuluhisho ya kitaalamu au kiufundi na gharama za usanifu na uwekaji wa Mfumo wa Nyaya za Umeme wa Juu (Overhead Catenary System (OCS)) na vituo vya kupoozea umeme kwa ajili ya uendeshaji wa Reli ya Kisasa ya Umeme.

**Mheshimiwa Spika,** hata hivyo, hapakuwa na sifa za kiufundi zilizotolewa kwa mkandarasi ili kuruhusu kunukuliwa kwa bei kulingana na sifa za kiufundi zilizowekwa, kama vile idadi ya vichwa na mabehewa katika kila sehemu za mifumo ya umeme wa treni wa juu (Overhead Catenary System), matumizi yake na

nguvu hazikujulikana.CAG anabainisha kwamba, ukosefu wa sifa za kiufundi zilizotolewa kuhusiana na miundombinu ya umeme kulimpa nafasi mkandarasi yeye mwenyewe kuamua alete mfumo wenye sifa ipi.

**2.2.3.2 Ongezeko la Gharama za Mradi kwa Kipande cha 3 na 4 kwa wastani wa Dola za Marekani Milioni 1.3 na Milioni 1.6 Mtawalia**

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa taarifa ya CAG mapitio ya nyaraka za mikataba zilizotolewa kwa vipande vya 1, 2 na 5 yalibaini uwepo wa ongezeko la gharama za ujenzi wa SGR kwa kilomita (km). Taarifa ya ukaguzi inafafanua kwamba kwa vipande 1,2, na 5, kwa kutumia njia ya ushindani gharama za ujenzi kwa kilomita 1 ilikuwa Dola za **Marekani milioni 4.1**, **milioni 4.6 na milioni 3.9** mtawalia, wakati kwa kipande cha 3 na 4 mchakato wa zabuni ulifanyika kwa njia ya mzabuni mmoja (Single source), gharama ya ujenzi wa SGR kwa kilomita moja ilikuwa **Dola za Marekani millioni 5.2** na **Dola milioni 5.5** mtawalia.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na tofauti hiyo, taarifa ya CAG inabainisha kwamba hapakuwa na faida ya kiuchumi (Economic benefits) kwa Shirika la Reli (TRC) kwa kutoa zabuni kupitia njia ya chanzo kimoja (Single Source) kwa M/S Yapi Merkezi. Hii ni kwa sababu gharama za awali ujenzi wa miradi mingine zilikuwa chini ikilinganishwa na mkataba aliopewa mkandarasi wa kipande cha 3 na 4. Pamoja na hilo, ukaguzi ulibaini kuwa mawanda ya kazi kwa kipande cha 3 na 4 ya mradi yalikuwa madogo na yalikuwa na miundombinu michache kuliko ile ya kipande cha 1, 2, na 5.

**2.2.3.3 Masharti ya Mkopo Kutoka Benki Kwenda kwa Serikali Kuwa na Vigezo Ambavyo Vilipunguza Ushindani kwa Wazabuni**

**Mheshimiwa Spika,** katika eneo hili taarifa ya CAG inafafanua kwamba Kifungu cha 64 (1) cha Sheria ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2011 na Kanuni ya 149 (1) ya Kanuni ya Ununuzi wa Umma GN. 446 ya mwaka 2013 inataka njia za ushindani wa zabuni zipewe kipaumbele ili kupata bei za ushindani kutoka kwa wazabuni mbalimbali, hivyo kuruhusu serikali kupata thamani ya fedha.

**Mheshimiwa Spika,** mapitio ya njia za ununuzi zilizotumika katika ununuzi wa mkandarasi wa kipande cha 3 na 4 reli ya kisasa (SGR) yalibainisha kuwa Benki ya Standard Chartered ambako Serikali ilitarajia kupata mkopo iliweka sharti kwamba ingekubali jukumu la kuwa Mratibu wa Kimataifa, na Wakala Kiongozi aliye na Mamlaka kupanga ufadhili na mkopo kwa Wizara ya Fedha na Mipango (MoFP) tu kwa masharti kwamba kampuni ya Yapi Markezi iteuliwe kama mkandarasi.Taarifa ya CAG inafafanua kwamba, Wizara ya Fedha na Mipango (MoFP) ilikubali mkopo huo na masharti yake kutoka Benki ya Standard Chartered kupitia barua yenye kumbukumbu namba PST/GEN/2021/01/55.

**2.2.3.4 Ongezeko la Muda wa Kukamilika kwa Mradi Kwa Zaidi ya Siku 1,414**

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa mkataba namba PA/003/HQ/2016-17/W/01 wa Ujenzi wa Mradi wa Reli ya kisasa (Standard Gauge Lot 1) kati ya Reli Assets Holding Company Limited inayojulikana kwa sasa kama Shirika la Reli Tanzania (TRC) na YAPI-MOTA ENGIL JV, mradi huo ulitakiwa kukamilika tarehe 1 Novemba 2019. Hata hivyo, taarifa ya CAG inabainisha kuwa, mradi huo uliongezwa muda wa kukamilika mara saba, na kuongeza siku 1414 hadi muda wa kukamilika, sawa na miaka 3 na miezi 9.

**Mheshimiwa Spika,**kuchelewa huku kumetokana na kucheleweshwa kwa uamuzi wa uhamishaji wa miundombinu ya bandari na makabidhiano ya eneo la ujenzi (access to site), na kuchangia kuchelewa kwa mradi kwa siku 959. Aidha, kuchelewa kwa maamuzi kuhusu kiunganishi cha bandari cha kilomita 4, na reli ya zamani (MGR), na kuchelewa makabidhiano ya eneo la kazi (access to site). Ucheleweshaji huo pia ulisababishwa na kuchelewa kuanzishwa kwa njia za juu na mapitio na marekebisho ya mwajiri ya njia ya eneo la 6.1, 9.1, na 11.1, ikijumuisha kuchelewa zaidi kutompa mkandarasi eneo kamili la kazi na uhamishaji wa miundo mbinu. Muda wa umalizaji kazi uliongezwa hadi kufikia tarehe 15 Septemba 2023.

**2.2.3.5 Dosari Mbalimbali Zilizobainishwa Katika Ununuzi wa Vichwa na Mabehewa ya Treni**

**Mheshimiwa Spika,** katika mchakato wa ununuzi wa mabehewa mbalimbali ya treni, Taarifa ya Ukaguzi wa Kiufundi imebainisha mapungufu kadhaa kama ifuatavyo:-

i. TRC ilikataa zabuni mara mbili kwa ajili ya manunuzi ya Rolling stocks (vichwa vya treni ya umeme na makochi/mabehewa ya abiria) ambapo mzabuni aliye na bei ya **Dola za Marekani 263,460,514** alikataliwa na kufanya manunuzi yasiyo na ushindani kwa **Dola za Marekani 478,507,468** kulikosababisha ongezeko la gharama ya **Dola za Marekani 215,046,954** (sawa na ongezeko la asilimia 82) lisilo la lazima;

ii. Katika mkataba wa manunuzi ya locomotives na makochi/mabehewa ya abiria yaliyotumika, TRC ilitekeleza mkataba bila dhamana ya utendaji kazi, hali iliyosababisha hasara ya **Euro 5,320,400** sawa na **Sh. bilioni 13.7**. Hii ilitokana na mkandarasi kushindwa kutekeleza mkataba na TRC kushindwa kutoza gharama zitokanazo na uvunjifu wa masharti ya mkataba (liquidated la Ongezeko la Thamani (VAT). Mkandarasi alidai sababu hizo zinakiuka kanuni na masharti ya mkataba kulingana na kifungu cha 67 cha masharti ya jumla ya mkataba., matumizi hayo hayaakisi manufaa yaliyokusudiwa ya mradi kwa wananchi;

iii. Shirika la Reli Tanzania (TRC) lilimuomba Balozi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Nchini Uturuki kufanya uchunguzi wa kina kwa mzabuni M/s Eurowagon juu ya ununuzi wa vichwa viwili na mabehewa 30 ya abiria yaliyotumika ili kuthibitisha hali ya kisheria na uwepo wa kampuni, uwezo wa kitaalamu na kiufundi, uwezo wa rasilimali na uthibitishaji wa wateja wanaohudumiwa au waliowahi kufanya kazi na kampuni hiyo. Balozi alibaini kuwa, kampuni haitekelezi mradi wowote

unaoendana na huo kwa sasa.Aidha, uwezo wa kifedha wa kampuni ulibainika kutotosha kutekeleza mradi wa uingizaji wa mabehewa yaliyotumika Nchini isipokuwa walipata ufadhili kutoka kwa vyanzo vingine. Licha ya mapungufu hayo yaliyoaninshwa na Balozi, bado TRC iliidhinisha zabuni hiyo kutolewa kwa M/s Eurowagon;

iv. Kampuni ya M/s Eurowagon haikuwasilisha dhamana ya utendajikazi (Performance Security) licha ya kukumbushwa mara kadhaa na Shirika la Reli Tanzania (TRC). Shirika la Reli Tanzania (TRC) iliendelea kutekeleza mkataba huu pasipo kupatiwa dhamana ya utendajikazi jambo ambalo lilipelekea kusitishwa kwa mkataba pasipo kukata dhamana kama fidia kwa kutotimiza wajibu wa kazi. Zaidi ya hayo, Kifungu kidogo cha 8.7 cha mkataba kati ya Shirika la Reli Tanzania (TRC) na M/S Eurowagon kinaitaka kutoza 0.15% ya thamani ya mkataba kwa siku kama fidia ya bidhaa ambazo hazijawasilishwa, hadi kiwango cha juu cha 10% ya thamani ya mkataba; na

v. Shirika la Reli Tanzania (TRC) haikutoza **Euro 2,660,200** kwa ucheleweshaji wa kuwasilisha bidhaa hivyo kuleta hasara ya mapato yenye thamani ya **Euro 2,660,200** ambayo ingekatwa kama fidia ya dhamana ya utendajikazi na kupelekea Jumla ya hasara ya **Euro 5,320,400**.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya kupokea hoja za Ukaguzi wa Kiufundi kuhusu Ujenzi wa Reli ya Kisasa, Kamati ilikutana siku ya tarehe 26 Oktoba, 2023 ili kujadiliana na Bodi na Menejimenti ya TRC. Katika mahojiano na uongozi wa TRC, maelezo ya ufafanuzi katika hoja kadhaa zilitolewa kama ifuatavyo:-

**a) Hoja inayohusu kukosekana vigezo vya umeme wakati wa kubadilisha mfumo wa injini za Treni kutoka za kutumia dizeli kwenda kwenye umeme**

**Mheshimiwa Spika,** ufafanuzi wa hoja hii kutoka kwa TRC

ulibainisha kwamba, mabadiliko ya kutoka kwenye injini za zinazotumia mafuta ya dizeli kwenda kwenye umeme yalitokana na mapendekezo ya Kamati ya Wataalamu wa Serikali. Aidha, TRC ilitoa maelezo kuwa uamuzi huo ulikuwa na manufaa ya kuongeza ufanisi wa Reli ya Kisasa inayojengwa.Mathalani mwendokasi wa treni ulikuwa unaongezwa kutoka kilimoita 120 kwa saa. Hadi kilomita 160. Pamoja na maelezo hayo, TRC waliifahamisha Kamati kuwa hapakuwa na gharama za ziada kwa uamuzi wa kubadilisha kutoka mfumo wa matumizi ya dizeli kwenda kwenye umeme. Naomba kunukuu sehemu ya maelezo ya Ndugu.Masanja K. Kadogosa akifafanua kuhusu hoja hii kama ifuatavyo:-

> **Nukuu:-**
> ***"…Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kitu ambacho ni kizuri sana katika decision ile gharama zilezile actually even belowndiyo gharama ambazo zimetujengea much more superior train reli yetu kuliko hata ya diesel. Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana nyingine ni kwamba***
> ***bajeti ambayo Bunge lako liliidhinisha hatuku-break kwa sababu tunataka twende kwenye ya umeme. Bado gharama zilikuwa within the budget which was below engineering estimate. Kwa hiyo, hicho nafikiri ndiyo the positive side ya kuweza kuieleza Kamati yakokwamba rationale za Serikali ambazo tulifikia maamuzi lakini bado hazikufanya turudi Bungeni kuomba extra budget ili tuweze kutekeleza.Kwa mfano, kwa Kenya average yao ni 6.2 million/- kwa kilomita moja sisi kwetu mpaka sasa hivi tumefika Mwanza kwa sababu tunazungumzia lot ya kwanza mpaka ya tano average yetu mpaka sasa hivi iko around 3.9 milion/- kwa kilomita moja. Kwa hiyo, unaweza ukaona tofauti ilivyo kubwa…"***
>
> **Mwisho wa Nukuu.**

**b) Hoja kuhusu kutumia mzabuni mmoja wa ujenzi wa kipande cha 3 na cha 4**

**Mheshimiwa Spika,** katika hoja hii, TRC walikiri mbele ya Kamati kuwa walitumia njia ya ununuzi ya mzabuni mmoja (Single source). Njia hiyo waliitumia kwa sababu kuu mbili,kwanza njia hiyo ilikuwa inaruhusiwa kwa mujibu wa Kifungu cha 4 (1) (b) cha Sheria ya Ununuzi wa Umma ya Mwaka 2011 na Kanuni ya 161 (c) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2003. Pili mkandarasi aliyependekezwa alikuwa anaendelea na kazi, hivyo kusingekuwa na gharama kubwa za kujiandaa kwa kazi (Mobilization cost). Vilevile Kamati ilifahamishwa kuwa TRC ilifanya majadiliano na mkandarasi ili kupata thamani ya fedha kwa kuzingatia uzoefu kutoka miradi mingine inayoendelea na makadirio ya kihandisi (Engineering Estimate) ili kuhakikisha gharama halisi ya mradi inapatikana.

**Mheshimiwa Spika,** TRC waliifahamisha Kamati kuwa Bodi ya Zabuni mara ya kwanza ilikataa pendekezo la kutumia mzabuni mmoja. Kwa sababu hiyo, Menejimenti ya TRC ilikata rufaa PPRA ambao nao hawakuafiki pendekezo la kutumia mzabuni mmoja. Hata hivyo, TRC waliendelea kufafanua mbele ya Kamati kwamba, baada ya majadiliano na mashauriano ndani ya Serikali, Bodi ya Zabuni ya TRC iliridhia na hivyo kutoa fursa kwa mkataba wa zabuni husika kusainiwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati pia ilitaka kujua endapo kulikuwa na ulazima wa Serikali kuchukua mkopo kwa ajili ya ujenzi wa kipande cha 3 na cha 4 cha SGR. TRC walitoa maelezo kwamba, Serikali iliona umuhimu wa kupata fedha kukamilisha mradi kwani bila kutumia njia ya mkopo ni vigumu kupata fedha katika Taasisi nyingine za fedha kugharamia mradi wa SGR. Naomba kunukuu sehemu ya maelezo ya Ndugu Masanja K. Kadogosa, Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli kuhusu hoja hii aliyotoa mbele ya Kamati kama ifuatavyo;-

> **Nukuu:-**
> ***"…Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu ninachoweza kukwambia ni kwamba hatuna alternative yoyote ya kufanya SGR, I have been here kwa***

> ***muda, nje ya kutumia ECA[11]. Tumeenda kwenye financial institutions zingine zote, tumekosa pesa..."***

**Mwisho wa Nukuu.**

**c) Hoja kuhusu utofauti wa gharama za ujenzi kwa vipande tofauti ambapo kwa wastani kipande cha 3 & 4 kinajengwa kwa gharama kubwa zaidi**

**Mheshimiwa Spika,** hoja hii pia iliibuliwa na CAG ambapo maelezo ya TRC yalifafanua kwamba ni dhana isiyo sahihi kuchukua wastani wa gharama za ujenzi wa kipande kimoja na kulinganisha na kipande kingine. Aidha, TRC walifafanua kwamba tarehe za ujenzi zilikuwa tofauti hivyo gharama haziwezi kuwa sawa.Mathalani walitoa mfano kuwa katika kipande cha 1 na cha 2 walichoronga kupita chini ya mlima kwa kilomita 3 na pia walichoronga kukwepa mkondo wa mto mkondoa kwa kilomita 120. Kwa hatua hii maana yake kipande cha 2 kina madaraja mengi kuliko kipande cha 1 kwa kuwa ardhi haifanani hivyo hata gharama za ujenzi haziwezi kuwa sawa.

**Mheshimiwa Spika,** katika hoja hii kulitolewa maelezo pia kuhusu utofauti wa jiolojia ya ardhi unachangia utofauti wa gharama za ujenzi. Mathalani katika ujenzi wa kipande cha 3, katika eneo la Makutupora, reli inapita zaidi ya kilomita 50 katika eneo la Bonde la Ufa hivyo gharama zake ni tofauti na ujenzi kwenye eneo la ardhi ya tambarale.Kwenye eneo la Bonde la Ufa gharama zitakuwa juu kuliko eneo tambarale.

**Mheshimiwa Spika,** hoja nyingine ya ufafanuzi katika eneo hili ilihusu gharama za usafirishaji wa vifaa vya ujenzi kutofautiana kutokana na umbali wa mradi. Mfano gharama za usafiri kwa mradi kwa maeneo yaliyokuwa jirani na Dar es Salaam ilikuwa nafuu ukilinganisha na gharama za utekelezaji mradi katika eneo la Makutupora na Tabora.Kwa msingi huo dhana ya kufanya ulinganifu kwa kutumia wastani wa gharama za vipande vya ujenzi haikuwa sawa bila ya kuzingatia vigezo kadhaa vilivyofafanuliwa.

[11] ECA ( Export Credit Agency)

## d) Kuhusu hoja za Mabehewa

**Mheshimiwa Spika,** kuhusu gharama za mabehewa ya treni na vichwa vya kuvuta mabehewa, TRC walitoa ufafanuzi katika hoja kadhaa kama ifuatavyo; kwanza waliifahamisha Kamati kuwa zabuni iliyohojiwa na CAG ya mwaka 2017 na baadaye manunuzi yakafanyika mwaka 2021 hazikuwa na uhusiano wowote. Kwa msingi huo "specifications" zilizokuwa kwenye zabuni ya mwaka 2017 ni tofauti kabisa na "specifications" za zabuni ya ununuzi iliyofanyika mwaka 2021 hivyo gharama zisingekuwa sawa.

**Mheshimiwa Spika,** TRC waliendelea kufafanua utofauti wa gharama pia ulisababishwa na hoja kuwa, kwa zabuni ya awali ya mwaka 2017 katika vichwa 17 vilivyokuwa vimeagizwa, vichwa 3 tu ndiyo vilikuwa na uwezo wa kuvuta mabehewa ya abiria na vinaenda kwa kasi ya kilomita 160 kwa saa na vingine vyote vinaenda kilomita 120 kwa saa. Hata hivyo kwa zabuni mpya ya ununuzi ya mwaka 2021, ni kwamba vichwa vyote vinaenda kwa kilomita 160 kwa saa.

**Mheshimiwa Spika,** kuna hoja nyingine iliyohusu vichwa vya treni vilivyotumika kununuliwa kutoka kampuni ya Eurowagon.TRC walifafanua kuwa suala hili lina historia yake ambapo katika hatua ya awali walitangaza zabuni ya kwanza hawakupata mtu, hivyo wakaifuta. Wakatangaza zabuni ya pili wakapata mzabuni kutoka Afrika Kusini ila pia wakaifuta kwa mzabuni kutokizi vigezo. Wakatangaza zabuni ya 3 wakapata mzabuni kutoka China ila pia wakaifuta kwasababu ya kukosa vigezo.Baada ya hapo TRC kwa maandishi wakaishauri Serikali kwamba kwa walipofikia sasa ni bora kuangalia uwezekano mbadala wa kupata vichwa vya treni kwa sababu ujenzi unategemewa kukamilika mwaka 2019 na wakati huo ilikuwa Mwezi Novemba 2018.

**Mheshimiwa Spika,** TRC waliifahamisha Kamati kuwa kulikuwa na hatari ya ujenzi wa kipande cha reli cha 1 na cha 2 kukamilika bila ya kuwa na treni yeyote ya majaribio.Hii ingekuwa na athari kubwa kwa sababu kitaalamu kuna muda wa kufanya majaribio ya uimara wa reli *(liability pull in, keeps in)*. Hicho ndio kipindi ambacho uimara wa reli unaangaliwa kwa kupitisha treni yenye uzito mkubwa ili kupima uimara wa madaraja na makaravati.

**Mheshimiwa Spika,** hivyo TRC waliishauri Serikali lazima kuwepo na treni ya majaribio.Katika hatua hii kulikuwa na njia 3 za kupata treni hizo, moja ilikuwa ni kununua treni mpya *(off shelf),* njia ya pili ilikuwa ni kukodisha treni na njia ya tatu ilikuwa ni kununua vichwa vya treni vilivyokwisha tumika.TRC walitanga zabuni ya ununuzi wa vichwa vya treni vipya hawakupata mzabuni yeyote katika hatua hiyo.Hivyo wakabakiwa na njia mbili pekee za kukodisha vichwa vya treni au kununua vichwa vya treni vilivyokwisha tumika. Baada ya uchambuzi wa kina, walibaini gharama za kukodisha vichwa vya treni ni wastani wa asilimia 77 ya kukodisha vichwa vya treni hivyo, TRC kama wataalamu wakaishauri Serikali, kwamba ni vema wakanunua vichwa vilivyotumika ila vikafanyiwa matengenezo kidogo hali ambayo inavifanya kuwa na uwezo wa hadi asilimia 85 ya vichwa vipya. Hivyo walitumia masharti ya Sheria ya Ununuzi wa Umma kupitia kwa Waziri wa Fedha ambaye aliunda Timu ya Wataalamu iliyomshauri kuhusu ununuzi huo.

**Mheshimiwa Spika,** kulikuwa na hoja pia kuhusu TRC kutozingatia ushauri wa Balozi wa Tanzania Nchini Uturuki kuhusu Kampuni ya Eurowagon. Ufafanuzi katika eneo hili ulibainisha kwamba, TRC walichukua hatua za kujikinga endapo kampuni hiyo ingekiuka masharti. Walihakikisha kwamba katika mkataba wanaweka sharti la kuhamisha umiliki wa mabehewa ya abiria wakati wa utengenezaji kwenda kwenye umiliki wa TRC.

**Mheshimiwa Spika,** TRC wamefafanua kuwa walivunja mkataba na kampuni ya M/s Eurowagon kwasababu mkandarasi alishindwa kuleta dhamana ya kutekeleza mradi (Perfomance Guarantee) na TRC walimtafuta mkandarasi mwingine kwaajili ya kumalizia kazi ya ukarabati wa vichwa vya umeme na mabehewa kwa ajili ya Reli ya SGR. Hadi sasa mkandarasi husika anaendelea na utekelezaji wa kazi hiyo.

**e) Hoja kuhusu ongezeko la muda wa utekelezaji wa mradi kwa siku 1441**

**Mheshimiwa Spika,** maelezo ya TRC yalifafanua kwamba, ongezeko la muda wa mradi kwa kipande cha kwanza yalitokana pamoja na mambo mengine mvua kubwa zilizonyesha juu ya kiwango kati ya Septemba 2019 hadi Juni

2020, hivyo kuathiri shughuli za ujenzi. Aidha kulikuwepo na hoja ya mlolongo mrefu wa utwaaji wa ardhi na kuwalipa wahusika fidia katika eneo la mradi hivyo kuchelewesha shughuli za mradi.

**Mheshimiwa Spika,** hoja nyingine ya ufafanuzi katika eneo hili ilihusu uingiliano wa miradi mingine iliyokuwa ikitekelezwa katika eneo la mradi. Miradi hiyo ni ya ujenzi ya BRT, upanuzi wa bandari na mradi wa DMDP. Vilevile kulikuwa na mgogoro baina ya wabi awa utekelezaji wa mradi kwa maana ya wakandarasa kampuni ya Yapi Merkezi na Mota Engil ambao ulikuja kumalizwa baadaye ila uliathiri kasi ya utekelezaji wa mradi.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya uchambuzi wa kina wa hoja za CAG na maelezo ya TRC, kuna mambo kadhaa ambayo Kamati iliyabaini. Kwanza tofauti ya gharama za ujenzi kwa vipande tofauti lazima itakuwepo kwa kuwa ujenzi wa kipande cha 1 na cha 2, ulifanyika miaka 6 iliyopita (2016/2017), wakati ujenzi wa kipande cha 3 na 4 umefanyika mwaka 2021/2022. Hivyo lazima kutakuwa na ongezeko la gharama za vipuri na gharama za ujenzi kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ina maoni kwamba , mradi wa SGR ni miongoni mwa miradi ya kielelezo na kimkakati ambayo Serikali inatekeleza kwa gharama kubwa.Ni vigumu kutekeleza mradi mkubwa kama huu kwa fedha za ndani. Hivyo, pamoja na changamoto zilizobainishwa na CAG na majibu ya TRC ni muhimu sana kwa mradi huu kuangaliwa kwa upekee. Aidha, kwa upekee huo jitihada muhimu zichukuliwe ili mradi ukamilike kwa wakati na kwa kuzingatia maslahi mapana ya Nchi yetu.

**2.2.4 Manunuzi ya Mita za Umeme bila ya Kukaguliwa na Wakala wa Vipimo**

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2021/2022, Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) lilinunua na kutumia jumla ya mita 874,019 zenye thamani ya **Sh. bilioni 115**. Hata hivyo, mita hizo hazikuthibitishwa na Wakala wa Vipimo kitu ambacho kinaweza kusababisha hasara kwa mteja au Shirika.

**Mheshimiwa Spika,** hatua hii ya TANESCO ni kinyume na Kanuni ya 22(1) ya Kanuni za Uzani na Vipimo za mwaka 2019

zinazoelekeza kuwa hakuna mita itakayoruhusiwa kutumiwa na mkandarasi au mnunuzi kwa madhumuni ya kupima umeme au gesi inayotolewa au kutumika kwake isipokuwa imethibitishwa na Wakala wa Vipimo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inatambua uharaka unaokuwepo kutokana na hitaji kubwa la wananchi kuhitaji huduma ya kuunganishiwa umeme hivyo kuilizamisha TANESCO muda mwingine kukiuka Sheria husika ili kuunganishia wananchi umeme.Hata hivyo, bado TANESCO wana fursa ya kukaa na Wakala wa Vipimo ili kuandaa utaratibu maalumu utakaotumiwa kuhakiki ubora wa mita hizo bila kuchelewesha huduma kwa wananchi.Aidha, TANESCO wanaweza kuongeza kipengele cha upimaji wa mita (Consider establishing tender requirement through incorporating meter test, calibration and verification evidence by WMA as a criterion of accepting meters) kama kigezo cha zabuni kwa mita za umeme ili kupunguza takwa la upimaji wa mita hizo baada ya ununuzi.

**Mheshimiwa Spika,** athari inayotokana na mita za umeme kutokaguliwa ni pamoja na uwezekano wa kuruhusu mita za umeme zisizokuwa na ubora kuingia sokoni na hivyo kuipotezea Serikali mapato hasa endapo mita hizo zisizokuwa na ubora kuwa na mianya ya kuruhusu wizi wa umeme.

### 2.2.5 Riba ya Sh. bilioni 113.8 Inayodaiwa na Kampuni ya Pan Africa Energy kwa TANESCO

**Mheshimiwa Spika,** katika uchambuzi wa taarifa ya hesabu zilizokaguliwa za TANESCO kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2022, katika eneo la usimamizi wa matumizi, Kamati ilibaini kuchelewa kwa TANESCO kuilipa Kampuni ya Pan Africa Energy fedha kutokana na matumizi ya gesi. Kuchelewa huko kumesababisha TANESCO kudaiwa riba kutokana na kutolipa ankara za madai zenye thamani ya **Shilingi bilioni 113.8**.

**Mheshimiwa Spika,** TANESCO na Pan Africa Energy, wana mkataba wa mauziano ya gesi (Gas Sales Agreement) ambapo katika mkataba huo, masharti yake ni kwamba Pan Africa Energy akitoa ankara ya madai, TANESCO anatakiwa alipe ndani ya kipindi walichokubaliana mapema iwezekanavyo na

endapo watachelewa kulipa basi TANESCO watachajiwa riba ya 4% kwa mwaka juu ya LIBOR[12].LIBOR ni "London Interbank Offered Rate" ambayo kwa sasa hivi ni 5.1%. Hivyo, hiyo 5.1% ikijumlishwa na ile 4% inayotozwa na Pan Africa Energy jumla inakuwa 9.1% ambayo TANESCO anatakiwa kulipwa katika Dola za Marekani.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa taarifa ya ukaguzi, TANESCO waliripoti kiasi wanachodaiwa kilikuwa ni **Dola za marekani milioni 107.08** ambayo ni sawa na **Sh. bilioni 246.7**. katika hizo kulikuwa na ankara 115 ambazo zilikuwa na riba iliyotozwa kutokana na kuchelewa kulipa malipo kwa mujibu wa mkataba. Riba katika ankara hizo zilikuwa na thamani ya **Sh. bilioni 113.8**.

**Mheshimiwa Spika,** ucheleweshaji huu wa malipo unasababisha upotevu wa fedha za Serikali takribani **Sh. bilioni 11** kila mwaka kama malipo ya riba. Kamati iliitaka Bodi ya TANESCO kutoa maelezo kuhusiana na hoja hii. Hata hivyo, TANESCO kupitia kwa Msajili wa Hazina waliifahamisha Kamati kuwa jambo hili bado lipo kwenye mazungumzo na halijakamilika hivyo Kamati ikaona ni muhimu Bunge likafanya uamuzi katika hoja hii.

### 2.2.6 Mapungufu Katika Mchakato wa Ununuzi wa Vishkwambi 300,000 Katika Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

**Mheshimiwa Spika,** mnamo mwezi Machi 2022, kwa kupitia kikao cha kamati ya kitaifa ya Sensa kilichofanyika tarehe 06 Machi 2022, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ilipewa jukumu la ununuzi wa vishikwambi 300,000 ambavyo vingetumika kwenye sensa ya watu na makazi iliyofanyika tarehe 23 Agosti 2022. Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ilianza taratibu za ununuzi kupitia zabuni namba ME-024/2021-22/HQ/G/34 ambapo wazabuni 14 walialikwa kuwasilisha maombi ya zabuni zao zilizogawanyika katika loti sita za vishikwambi 50,000 kwa kila loti.

**Mheshimiwa Spika,** Wizara iliingia mkataba na wazabuni watatu kwa ajili ya kuwasilisha vishikwambi 300,000 vyenye thamani ya jumla ya **Sh. 123,778,844,369.6** (mikataba ya awali yenye thamani ya **Sh. 104,786,192,840** na mkataba wa nyongeza wenye thamani

[12] LIBOR ni London Interbank Offered Rate

ya **Sh. 18,992,651,529.6** bila ya kodi ya ongezeko la thamani). Aidha, muda wa kuwasilisha vishikwambi ulikuwa ni siku 40 kuanzia tarehe ya kusainiwa mkataba.

**Mheshimiwa Spika,** ununuzi huu ulipaswa kufanyika kwa muda wa miezi miwili, yaani kutoka mwezi Machi 2022 na kuwasili Mwezi Mei 2022 kwa ajili ya kufanya maandalizi ya sensa kama vile kufanya mafunzo kwa maafisa wa sensa. Hili lilipelekea wizara kufanya mabadiliko ya njia ya ununuzi kutoka Ushindani wa Kimataifa na kutumia ununuzi wa dharura wa kununua moja kwa moja kutoka viwandani au wazabuni walioidhinishwa na kiwanda. Kamati ilibaini kuwa, kati ya wazabuni 14 walioalikwa kuwasilisha nyaraka za zabuni, 10 ndio waliowasilisha nyaraka za zabuni na kati ya hao wazabuni watatu walishinda zabuni hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa kina wa ununuzi huu, ulibaini hoja kadhaa ambazo ni muhimu Bunge lako Tukufu likafahamishwa kama ifuatavyo:-

a) Manunuzi kufanyika kwa njia ya kugawa loti badala ya ununuzi wa pamoja ambao ungewezesha kupunguza gharama za ununuzi husika;

b) Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kupokea dhamana ya zabuni bila kujiridhisha uhalali wa dhamana hizo kwa watoa dhamana;

c) Idara tumizi kutoshirikishwa kikamilifu kuwa sehemu ya Kamati ya Tathmini ya Zabuni kinyume na Kifungu Na. 39(e) ya Sheria ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2013;

d) Kufanya tathmini ya uwezo wa mzabuni (post qualification) na majadiliano na mzabuni (negotiations) kwa wakati mmoja. Ilipaswa kuanza kwanza tathmini maana tathmini ya uwezo wa mzabuni inaweza kupelekea mzabuni kutokuwa na sifa;

e) Dosari zilizobainika kwenye mkataba kati ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Mzabuni Shenzhen

Technology Company Limited wenye thamani ya **Sh. 46,859,442,840** uliosainiwa tarehe 5 Agosti 2022. Bodi ya Zabuni haikuridhia mzabuni huyu kupewa mkataba na hii ikapelekea Wizara kuomba ushauri kutoka Mamlaka ya Ununuzi wa Umma (PPRA) na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Ofisi hizi zilishauri Afisa Masuuli kuwa na tahadhari endapo mzabuni atapewa zabuni;

f) Ilibainika kuwa mzabuni Shenzhen Technology Company alisaini mkataba wa **Sh. 46,859,442,840** na kuutekeleza bila kuwa na dhamana ya mkataba (performance security). Vile vile, wazabuni wengine wawili waliopewa zabuni na kusaini mikataba yenye jumla ya **Sh.57,926,750,000** waliwasilisha dhamana ya mkataba (performance security) za **Sh. 5,792,675,000** kwa kuchelewa kwa siku kuanzia 45 na 52 baada ya kuanza kutekeleza mikataba. Hii ni kinyume na kanuni 29(1) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma;

g) Kuchelewa kuwasilisha vishikwambi 150,000. Mzabuni Shenzhen Technology Company alichelewa kuwasilisha vishikwambi kwa siku takribani siku 24. Wizara ya Elimu haikukata 'liquidated damages' kinyume na makubaliano ya mkataba; na

h) Dosari mbalimbali kwenye vishikwambi vilivyokabidhiwa Ofisi ya Taifa ya Takwimu. Ilibainika kuwa kati ya vishikwambi 208,480 vilivyokabidhiwa Ofisi ya Taifa ya Takwimu, 178,482 vilirudishwa Wizara ya Elimu kupitia ofisi za wathibiti ubora 22,965 vilirejeshwa Wizara ya Elimu makao makuu, 6,620 vilipelekwa Wizara ya Elimu Zanzibar, 1,242 havijarejeshwa na 171 vimepotea.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilikutana na Afisa Masuuli wa Wizara ya Elimu ili kupata maelezo yake kuhusiana na hoja hii ya vishkwambi. Afisa Masuuli alitoa maelezo kwamba, manunuzi haya yalifanywa kwa njia ya dharula ili kuwahi mchakato wa sensa ya watu na makazi iliyopangwa kufanyika mwezi Agosti, 2023.

**Mheshimiwa Spika,** katika hatua nyingine ya uwajibikaji Afisa Masuuli aliifahamisha Kamati kuwa alichukua hatua za kuvunja Bodi ya Zabuni ya Wizara kutokana dosari zilizojitokeza. Vilevile Afisa Masuuli alilifikisha suala hili kwenye vyombo vya Dola kwa uchunguzi kupitia barua yenye Kumb. Na. EDC.10/WEST/02/132 ya tarehe 18 Agosti, 2023.

**Mheshimiwa Spika,** hata hivyo Kamati ilikuwa na maoni kwamba, shughuli za Sensa zilipangwa na kujulikana mapema, hivyo taratibu za manunuzi zilitakiwa pia kufanyika mapema ili kuepuka dosari ambazo zilitokana na ununuzi kwa njia ya dharula.

### 2.2.7 Tozo ya Riba Kiasi cha Sh. 36,860,022,478.59 Kwa TANROADS kwa Kuchelewa Kuwalipa Wahandisi na Washauri wa Miradi

**Mheshimiwa Spika,** hoja ya ukaguzi inayohusu tozo inayotokana na riba kwa Wakala wa Barababara Nchini (TANROADS) kuchelewa kuwalipa wakandarasi na washauri wa miradi imeendelea kuwa changamoto kubwa. Katika eneo hili, Kamati kwa nyakati tofauti imekuwa ikitoa ushauri wa namna bora ya kuboresha malipo kwa wahandisi na washauri wa miradi ili kuepuka riba kubwa inayotozwa kwa kuchelewa kulipa malipo husika.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka 2021/22, TANROADS imetozwa riba ya kiasi cha **Sh.36,860,022,478.59** kutokana na dosari niliyoibainisha hapo awali.Riba hizi sio tu zinasababisha upotevu wa fedha za umma lakini pia zinachangia kuongeza gharama za miradi kwa kiasi kikubwa.

**Mheshimiwa Spika,** katika kujibu hoja hii, TANROADS waliifahamisha Kamati kuwa kuanzia Julai 2021 iliamuliwa kwamba kila IPC au ankara iwasilishwe Wizara ya Ujenzi ndani ya siku saba badala ya kusubiri mwisho wa mwezi ili kuomba kutolewa fedha kwa haraka.

**Mheshimiwa Spika,** hata hivyo, Kamati imethibitisha kuwa suala la utoaji wa fedha kwa wakati halijapatiwa suluhu ya kudumu, hivyo kuendelea kuisababishia Serikali hasara kwa kulipa riba kubwa kwenye miradi. Fedha hizo za riba zingeweza kutumika katika

maeneo mengine yenye uhitaji wa rasilimali fedha na kuleta matokeo chanya kwa maendeleo ya Taifa.

### 2.3 Mapitio ya Kaguzi za Hesabu Katika Taasisi za Huduma za Afya

**Mheshimiwa Spika,** kupitia uchambuzi wa Taarifa ya CAG kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2022, Kamati ilipitia taarifa za fedha za Taasisi za Umma zinazohusiana na utoaji wa huduma za afya. Matokeo ya uchambuzi wa Kamati kwa Taasisi hizo ni kama ifuatavyo: -

#### 2.3.1 Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF)

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa taarifa ya hesabu zilizokaguliwa za Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya ulibaini hoja zifuatazo ambazo ningependa kuzileta mbele ya Bunge lako Tukufu;

a) **Madeni Ambayo NHIF Inadai Kiasi cha Sh. bilioni 228**

Ukaguzi ulibaini kuwa hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2022 NHIF ilikuwa inadai kiasi cha **Sh. bilioni 228** ambazo zilikuwa hazijalipwa. Kwa mujibu wa CAG katika deni hilo, Taasisi za Serikali zilikuwa zinadaiwa kiasi cha **Sh. bilioni 210**.Hadi ukaguzi unakamilika hapakuwa na malipo yeyote yaliyofanyika ili kulipa deni husika.

Mchanganuo wa deni la Serikali unahusisha deni la Wizara ya Mambo ya Ndani **Sh. bilioni 45.4**, Taasisi ya Mifupa Moi **Sh. bilioni 18.2**, NIDA **Sh. bilioni 17.3** na Hospitali ya Benjamini Mkapa **Sh. bilioni 129.3**.

b) **Kiasi kikubwa cha fedha ya mikopo ya watumishi wa NHIF Sh. bilioni 41.42 bila ya kuwa na mfuko wa kuzungusha fedha**

Ukaguzi, ulibaini kuwa hadi tarehe 30 Juni 2022, Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya ulikuwa na mikopo ya watumishi ambayo haijalipwa inayofikia jumla ya **Sh. bilioni 41.42**, ambapo kiasi cha **Sh. bilioni 11.18**

kilikuwa ni mikopo mipya iliyotolewa wakati wa mwaka 2021/22 bila kuzingatia mahitaji ya Aya 1.4 ya Sera ya Mikopo ya Wafanyakazi wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya ambayo inahitaji mikopo kutolewa chini ya mfumo wa Mfuko wa Kukopa na Kulipa. Aidha, ukaguzi ulibaini kupungua kwa ukwasi wa fedha wa Mfuko huo. Vilevile Mfuko uliongeza kikomo cha mikopo ya wafanyakazi na kuendesha Mfuko bila ya kuwa katika utaratibu wa mzunguko wa marejesho "Revolving Fund".

c) **Ongezeko la Gharama za Matibabu Kuliko Michango ya Wanachama**
Katika miaka mitano iliyopita, gharama za matibabu zimekuwa zikiongezeka ukilinganisha na michango ya wanachama. Katika mwaka 2021/2022, Mfuko ulikuwa na nakisi ya **Sh. bilioni 132.6** ukilinganisha na nakisi ya **Sh. bilioni 59** kwa mwaka 2021.Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa kwa mapato ya michango ya wanachama imekuwa ikiongezeka kwa wastani wa 12.9% wakati malipo ya gharama za matibabu yamekuwa yakiongezeka kwa wastani wa 24.6%. Kwa msingi huo, Mfuko unatumia fedha kutoka kwenye vyanzo vingine kama uwekezaji kulipia gharama za matibabu.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipata fursa ya kujadiliana na Bodi na Menejimenti ya NHIF siku ya tarehe 23 Oktoba, 2023 kujadili taarifa husika ya ukaguzi. Kwa hoja ya madeni ya Serikali, NHIF imeifahamisha Kamati kuwa Wizara ya Fedha imetoa ahadi ya kulipa fedha hizo katika mwaka wa fedha 2023/2024.

**Mheshimiwa Spika,** hata hivyo hadi tunawasilisha taarifa hii leo hapa Bungeni, bado Kamati haikupata taarifa ya maandishi ya utaratibu wa kuanza kulipa madeni hayo na pia hapakuwa na mkataba kati ya NHIF na Hospitali ya Benjamini Mkapa kuhusu mkopo uliotolewa hapo awali.

**Mheshimiwa Spika,** kwa hoja ya madeni ya watumishi wa NHIF waliopewa mikopo, Bodi ya NHIF iliifahamisha Kamati kuwa utaratibu huo wa mikopo umesitishwa tangu mwezi Julai, 2023.

Hata hivyo, hoja ya Kamati inabaki kwamba fedha zote zilizokopwa ni muhimu zikarejeshwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali na taratibu za kuwa ma mfuko wa marejesho kwa mzunguko ukaanzishwa na kusimamiwa ipasavyo.

### 2.3.2 Bohari Kuu ya Dawa (MSD)

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipata fursa ya kupitia na kuchambua taarifa ya hesabu zilizokaguliwa za Bohari Kuu ya Madawa (MSD) kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2022. Masuala ya muhimu yaliyojitokeza katika hesabu za MSD ni kama ifuatavyo:-

**a) Madeni Ambayo MSD Inaidai Serikali Kiasi cha Sh. 275,599,227,000**

MSD walipata hati inayoridhisha yenye masuala ya msisitizo[13]. Hoja ya msisitizo katika MSD ilihusu deni[14] ambalo Wizara ya Afya ilikuwa inadaiwa na MSD kiasi cha **Sh. 275,599,227,000**. Hali hii inaathiri uwezo wa MSD katika kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Hadi sasa deni hilo halijalipwa na hivyo kuathiri utekelezaji wa majukumu ya MSD;

**b) Ukiukwaji wa Sheria Katika Ununuzi wa Vifaa Tiba Kutoka Kampuni ya Misri-AL HANDASIYA NA EIPICO**

Katika mwaka wa ukaguzi 2021/22 timu ya ukaguzi ilipitia mafaili mawili ya manunuzi na nyaraka zake za mikataba na kubaini kuwa:-

Tarehe 12 Oktoba 2021, Bohari ya Dawa (MSD) iliingia Mkataba, Na. IE-009/2021-2022/G/50, na AL HANDASIA kwa ajili ya kutoa bidhaa mbalimbali za matibabu vya aina 75. Kufuatia mkataba huu tarehe 11 Oktoba 2021, uongozi wa MSD ulifanya malipo ya awali kwa msambazaji, M/s. AL HANDASIA, jumla ya **Sh. 3,462,315,764**. Malipo haya yalifanywa kupitia vocha ya malipo Na. BPHQ-00005988, na yalikuwa ni kwa mujibu wa ankara namba 28858/10/2021.281, ya tarehe 11/10/2021, kwa madhumuni ya

[13] Unqualified Opinion with Emphasisi of Matter

[14] Rejea Ukurasa 1 kwa Hesabu Zilizokaguliwa za MSD. AR/PA/MSD/2021/22

kufanikisha uwasilishaji wa vifaa mbalimbali vya matibabu vya aina 75. Tarehe ya mwisho ya uwasilishaji iliyokubaliwa kwa pande zote iliwekwa tarehe 30 Oktoba 2021.

Ilipofika tarehe 8 Novemba 2021, MSD iliingia Mkataba Na. IE-009/2021/2022/HQ/50/02 na Kampuni ya Misri ya Kimataifa ya Viwanda vya Dawa (EIPICO) kwa ajili ya kutoa aina mbalimbali za bidhaa za matibabu. Bei iliyokubaliwa ilikuwa **Sh. 10,891,279,309** kwa makubaliano ya miezi 12.

Ukaguzi zaidi uliofanywa kwenye mikataba hiyo miwili ulibaini dosari zifuatazo:-

i. Kiasi cha malipo ya awali **Sh.3,462,315,764** yaliyofanywa kwa AL-HANDASIYA na kulipwa moja kwa moja kwenye Akaunti ya AL-HANDASIYA yenye jina la ACME TRADE INTER yenye AC Namba 0045609416002 katika Benki ya Egypt GULF, yalifanyika bila kupata dhamana kutoka kwa Benki na pia bila kuwasilisha Dhamana ya Utendaji kazi na mtoa huduma. Hii ni kinyume na Kifungu cha 58 (2) cha Sheria ya Manunuzi ya Umma, (CAP 410 R.E. 2022) kinachomtaka mzabuni aliyefanikiwa kuwasilisha dhamana ya utendakazi kwa kuzingatia masharti yaliyoainishwa katika kanuni;

ii. Kwa mujibu wa Kanuni ya 244 (1) ya Kanuni za manunuzi, 2013 MSD ilitakiwa kupokea jumla ya vifaa tiba 75 baada ya kulipa malipo ya awali ya **Sh. 3,462,315,764**.Hata hivyo ukaguzi ulibaini kuwa malipo ya awali ya **Sh. 3,462,315,764** kwa AL-HANDASIA yalijumuisha aina 49 tu za bidhaa za matibabu;

iii. Ukaguzi ulibaini kuwa uongozi wa MSD ulifanya jitihada za kuwasiliana na msambazaji AL-HANDASIA kupitia Ubalozi wa Tanzania nchini Misri kupitia barua yenye Nambari ya Marejeleo CBA.99/169/01/99 ya tarehe 26 Oktoba 2021.

Hata hivyo, hadi kufikia tarehe ya ukaguzi tarehe 30 Novemba 2022, walikuwa hawajapata jibu lolote kutoka kwa Ubalozi kuhusu AL-HANDASIA. Aidha, ukaguzi ulibaini kuwa malipo ya awali ya **Sh. 3,462,315,764** yaliyofanywa kwa AL-HANDASIA yalibakia kutojulikana (unaccounted for)

iv. Baada ya juhudi za MSD kuitafuta AL-HANDASIA kushindikana na kampuni hiyo kutoweka na malipo ya awali ya **Sh.3,462,315,764** yaliyotolewa na MSD, pamoja na kushindwa kupeleka vifaa vya matibabu vilivyokubaliwa kwa mujibu wa makubaliano ya kimkataba, MSD iliamua kutafuta msambazaji mwingine, ambaye ni EIPICO, kwa mpango usio rasmi wa kufidia fedha ambazo AL-HANDASIA ilitoweka nazo. Kutokana na hali hiyo, MSD iliingia Mkataba Namba IE-009/2021-2022/G/50/2 na EIPICO kwa ajili ya usambazaji wa aina mbalimbali za dawa (pamoja na bidhaa za AL-HANDASIA) wa **Sh.10,891,279,309** chini ya makubaliano ya muda wa miezi 12;

v. Baada ya kukagua hati za mkataba kwa wasambazaji wawili wa AL-HANDASIYA na EIPICO kwa kandarasi Na.IE-009/2021-2022/G/50/1 na No.IE-009/2021-2022/G/50/2, mtawalia, ilibainika kuwa hapakuwa na kifungu chochote cha mkataba kinachoelezea uhusiano wowote kati ya wasambazaji wawili. Zaidi ya hayo, hakukuwa na makubaliano kati ya AL-HANDASIYA na EIPICO katika kushughulikia maelekezo ya MSD iwapo msambazaji mmoja atashindwa kusambaza bidhaa, na hivyo kila mzabunii alitakiwa kutimiza wajibu wake peke yake, kwa mujibu wa sheria na masharti yaliyotajwa katika mikataba yao;

vi. Mapitio ya barua isiyo na namba ya kumbukumbu kutoka EIPICO ya tarehe 24 Novemba 2021 ilieleza wasiwasi wa AL-HANDASIYA kushindwa kutimiza agizo lake la vifaa tiba 49 kwa MSD zenye thamani ya **Sh. 3,462,315,764**. Barua hiyo inaeleza kuwa kushindwa kwa AL-HANDASIYA kulitokana na ukosefu wa baadhi ya nyaraka muhimu. Hata hivyo, hali hii ya kukosa 'baadhi ya nyaraka muhimu' na AL-HANDASIYA kama ilivyoelezwa na EIPICO haikufafanuliwa na AL-HANDASIYA au MSD katika kifungu chochote cha mkataba cha mikataba yao;

vii. Mwisho, baada ya uchambuzi zaidi uliofanywa na timu ya ukaguzi, ilibainika kuwa EIPICO iliweza kusambaza dawa za aina 12 pekee zenye thamani ya **Sh. 3,462,315,764** kutoka kwenye mkataba wao wenye thamani ya **Sh. 10,891,279,309**.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya uchambuzi wa kina wa masuala yaliyojitokeza katika mikataba hiyo miwili, Kamati ilifanya mahojiano na Bodi na Menejimenti ya MSD. Uongozi wa MSD uliifahamisha Kamati kuwa ilifanya kikao na TMDA mnamo tarehe 17 Mei, 2022 kujadili namna bora ya kuhakiki ubora na usalama wa bidhaa zilizopokelewa kutoka Misri. Baada ya Kikao hicho wliomba kibali[15] Wizara ya Afya kutumia bidhaa za afya kutoka nchini Misri.

**Mheshimiwa Spika,** kuhusu hatua za kisheria na kinidhamu kwa watumishi wa MSD waliohusika na hoja hii, Menejimenti ya MSD iliifahamisha Kamati kuwa uongozi wa juu wa MSD uliokuwepo wakati wa uingiaji mikataba hii uliondolewa na Mamlaka husika.Aidha kwa watumishi watendaji walihamishwa katika maeneo mengine ili kupisha uchunguzi. Kuhusu hatua za kijinai kwa waliohusika na suala hili, uongozi wa MSD uliifahamisha

[15] Rejea Barua ya MSD kwenda Wizara ya Afya ya tarehe 3 Juni, 2022 yenye Kumb. Na. CA.130/169/01B/14

Kamati kuwa shauri hili la ununuzi wa bidhaa lipo katika Mamlaka za Kiuchunguzi (TAKUKURU).

**Mheshimiwa Spika,** hoja ya Kamati katika suala hili ni kuwa, uchunguzi wa TAKUKURU umechukuwa muda mrefu kukamilika ili hatua za kijinai ziweze kuchukuliwa kwa wahusika. Hivyo uchunguzi unapochukua muda mrefu unakwamisha upatikanaji wa haki katika kuimarisha nidhamu ya matumizi ya fedha za umma.

### 2.3.3 Changamoto Zilizopo Katika Uanzishwaji na Uendeshaji Kisheria wa Hospitali ya Muhimbili Tawi la Mlognzila (MNH-Mloganzila)

**Mheshimiwa Spika,** katika uchambuzi wa taarifa za ukaguzi wa Taasisi za huduma za afya, Kamati ilipitia na kuchambua taarifa ya hesabu zilizokaguliwa za Hopsitali ya Taifa Muhimbili na Hospitali ya Muhimbili Mloganzila. Katika uchambuzi huo, Kamati ilibaini hoja kubwa ya ukaguzi inayohusu kutokuwepo misingi ya kisheria ya uanzishwaji na uendeshaji wa MNH Mloganzila (Absence of legal establishement of MNH Mloganzila).

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa taarifa ya ukaguzi, Hospitali ya MNH-Mloganzila hapo awali ilifahamika kama Kituo cha Kitaaluma cha Chuo Kikuu cha Muhimbili, MUHAS (MAMC)[16]. Malengo makuu ya Kituo yalikuwa kuwa Hospitali ya Kufundisha, Kituo kikuu cha Matibabu, Elimu na Utafiti utoaji wa huduma inayomlenga mgonjwa na elimu bora ya kliniki na utafiti. Ilikusudiwa kuwa hospitali ya juu ya kufundishia na kutoa huduma anuwai ambazo hutolewa na hazipatikani sana ndani ya Taasisi moja.

**Mheshimiwa Spika,** kituo cha Tiba cha MUHAS (MAMC) kilifanya kazi katika kipindi cha miaka miwili 2017 hadi 2018 chini ya MUHAS na kilizinduliwa rasmi na serikali na kuwekwa chini ya Bodi na Menejimenti ya Hospitali ya Taifa ya Muhimbili na kupewa jina la MNH-Mloganzila baada ya hapo tarehe 3 Oktoba 2018.Katika ukaguzi CAG alibaini kuwa MNH Mloganzila ilikuwa na watumishi 619 na Watumishi 685 kwa mwaka 2021-22 na 2020-21 mtawalia.

[16] Muhas Academic Medical Centre (MAMC)

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na kuwa MNH-Mloganzila ipo chini ya Bodi ya Wadhamini na menejimenti ya MNH, taarifa ya ukaguzi imebainisha kwamba masuala ya hospitali hayakuwekwa na kuripotiwa chini ya taarifa za fedha za MNH, yalifanywa tu chini ya MNH kutokana na utata na kukosekana kwa notisi ya wazi ya kisheria ya jinsi ya kufanya hivyo. Ni kwa msingi huo, hesabu zilizoandaliwa na Hospitali ya Mloganzila zenye thamani ya mali ya takribani **Sh. bilioni 140** hazitoi taswira sahihi na badala yake zilitakiwa kuandaliwa hesabu jumuifu za MNH.

**Mheshimiwa Spika,** hoja ya MNH – Mloganzila kutokuwa na idhini ya uanzishwaji kisheria inathibitishwa na maelezo[17] ya Ndugu Priscus Ngowi, Mkaguzi Mkuu wa Nje mbele ya Kamati kama yanavyonukuliwa hapa chini:-

> **Nukuu:-**
> ***"….Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ambayo tuliipata ni kwamba legal mandate, establishment ya Taasisi ya Mloganzila ilikuwa haijakamilika. Hatujui kwamba baada ya hilo tamko kutoka, Hospitali ya Mloganzila inabaki chini ya Wizara ya Elimu ya juu ambapo MUHAS inaripoti huko au Wizara ya Afya? Kwa hiyo hatukupata any correspondence kutoka Wizara zote mbili kwamba hii sasa inasimamaje. Muhimbili pale anaendesha atalipwa management fee au Mloganzila inakuwa kama idara ndani ya Muhimbili. Kwa hiyo, hiyo ndiyo changamoto ambayo tumekutana nayo…"***
> **Mwisho wa Nukuu.**

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuendelea kunukuu maelezo ya Ndugu Priscus Ngowi, Mkaguzi Mkuu wa Nje kutoka Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi akiendelea kuifahamisha Kamati kuhusu changamoto za uanzishwaji na uendeshaji wa MNH- Mloganzila. Maelezo hayo ni kama ifuatavyo:-

[17] Rejea Ukurasa wa 48 wa Mahojiao ya Kamati , Taarifa Rasmi za Bunge, Kikao cha Tisa cha Tarehe 17 Agosti, 2023

**Nukuu:-**

***"…Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwenye uendeshaji wa Taasisi ni kwamba Muhimbili kuna DG na Mloganzila kuna Deputy, kwa hiyo kila Mkurugenzi aliyeko Muhimbili kuna Mkurugenzi wa chini yake yupo Mloganzila ndiyo wanavyo-run. Mheshimiwa wenyekiti, changamoto nyingine ni kwamba ni Taasisi moja lakini zina taratibu zake, kwa hiyo hata wanavyoomba hizi funds za NHIF wanaomba kupitia Muhimbili. Kwa hiyo changamoto ambazo mnaziona, yaani mimi nafanya kazi, nadai malipo yangu, lakini inabidi nitumie mtu mwingine. Kwa hiyo hela inalipwa kwake, halafu Muhimbili ndiyo anampa Mloganzila… Mheshimiwa Mwenyekiti, hata issue za manunuzi wanakuwa wanatumia jina moja kwa hiyo inakuwa ni changamoto kuweza kujua ya Mloganzila ni ipi na ya Muhimbili ni ipi. Sasa current hapa hatufahamu sasa kwamba je, Mloganzila inasimama yenyewe au Mloganzila inaunganishwa na mwingine? Bado hata sisi Wakaguzi hatuelewi inakuwaje.***

**Mwisho wa Nukuu.**

**Mheshimiwa Spika,** hoja ya pili kuhusu MNH Mloganzila ilihusu kutokuwepo kwa mfumo huru wa Taarifa za Hospitali (HIS[18]).Ukaguzi umebaini kuwa MUHAS iliingia mkataba namba PA/007/2013-2014/G/89 na Kampuni ya Samsung na T Corporation wa tarehe 16 Desemba, 2014 kwa gharama za **Dola za Marekani 24,600,000** ukiwa ni Ugavi na ufungaji wa vifaa tiba, pamoja na uwekaji wa Taarifa za Hospitali.

**Mheshimiwa Spika,** CAG alifanya mapitio ya mfumo uliofungwa na Samsung C & T Corporation ambapo pamoja na mambo mengine alibaini kwamba, mfumo wa taarifa za hospitali uliotolewa na kusakinishwa haukulingana na maelezo ya kiufundi yaliyokubaliwa katika mkataba.Kutokana na changamoto hizo, hospitali ilitumia mfumo wa JEEVA tangu mwaka 2018 kutoka

[18] Hospital Information System

MNH-Upanga kama Mfumo wa Taarifa za Usimamizi wa Hospitali (HMIS) ambao unashughulikia huduma za hospitali. JEEVA imeunganishwa kutoka kwa moduli tofauti ikiwa ni usajili wa wagonjwa, usimamizi wa rasilimali watu, malipo, fedha, PMU, maabara, duka la dawa na kadhalika.

**Mheshimiwa Spika,** tathmini ya CAG katika mfumo wa "JEEVA" ilibaini kuwa hospitali ya Mloganzila imewekwa kama kitengo cha biashara ambacho hakina uhuru wa kiutendaji. Hivyo MNH – mloganzila inalazimika kufuata taratibu za uendeshaji na miongozo ya fedha ya kiwango sawa cha MNH-Upanga kwa kuwa ni kitengo cha biashara ndani ya MNH Upanga.Athari za jambo hili ni pamoja na maagizo ya ununuzi wa ndani (LPO) hayawezi kuripotiwa mfululizo kutokana na muingiliano wa mfumo na MNH, nambari za LPO zinaweza kwenda bila mpangilio kutoka kwa mtumiaji yeyote kutoka MNH Mloganzila au MNH Upanga baada ya kutolewa.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na dosari hizo, ukaguzi umebaini kuwa MNH Mloganzila haina makusanyo ya akaunti ya GepG yaliyounganishwa na "JEEVA", makusanyo yote yanafanyika kupitia akaunti kuu za makusanyo za MNH-Upanga na baadaye kugawiwa MNH Mloganzila. MNH Mloganzila ikiwa kama kitengo cha biashara katika mfumo wa "JEEVA" inaweka ukomo sawa wa huduma za mfumo zinazofanya kazi kikamilifu.

### 2.4 Uchambuzi wa Taarifa za Kaguzi Maalumu

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2021/2022, Kamati imefanikiwa kupitia na kuchambua jumla ya Taarifa za Kaguzi Maalumu tano. Kaguzi hizo zinahusu Fungu 35 Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ( Kaguzi 2) , Fungu 28 Jeshi la Polisi ( Kaguzi 2) na Ukaguzi Maalumu wa Kampuni ya Uendelezaji wa Uwanja wa Ndege wa Kilimanjaro ( KADCO). Naomba kulifahamisha Bunge lako Tukufu matokeo ya Kaguzi hizo Maalumu kama ifuatavyo:-

**2.5 Uchambuzi wa Taarifa ya Ukaguzi Maalumu Kuhusu Uendeshaji na Usimamizi wa Mikataba ya Maridhiano ya Kukiri Makosa (Plea Bargain)**

**Mheshimiwa Spika,** mnamo tarehe 1 Machi 2022 Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali aliamua kufanya Ukaguzi Maalumu kuhusiana na Uendeshaji na Usimamizi wa Mikataba ya Maridhiano ya Kukiri Makosa katika Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kupitia Kifungu cha 29 (1) cha Sheria ya Ukaguzi wa Fedha za Umma Sura ya 418 Marejeo ya 2021 kinachompa Mamlaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kufanya ukaguzi wowote atakoona unastahili.

**Mheshimiwa Spika,** ukaguzi huu maalumu ulikuwa na lengo la kujiridhisha na sheria na taratibu zilizotumiwa na Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kama zilizingatiwa wakati wa kuingia mikataba ya maridhiano ya kukiri makosa, utekelezaji wa mikataba yake, utimilifu wa makusanyo yaliyopokelewa Benki, uhalali wa malipo yaliyofanyika na usahihi wa salio lililokuwepo katika akaunti ya Mkurugenzi wa Mashtaka iliyopo Benki Kuu kufikia Mwezi Machi, 2022.

**Mheshimiwa Spika,** mawanda ya ukaguzi huu maalumu ulijikita katika kipindi cha miaka mitatu (3) kuanzia terehe 1 Julai, 2019 mpaka 31 Machi, 2022 na uliongozwa na hadidu sita (6) za rejea kama ifuatavyo;- Kubaini na kutambua idadi ya kesi zilizoendeshwa kwa utaratibu wa kuingia Mkataba wa Maridhiano ya kukiri Makosa, Kiasi cha fidia kilichoahidiwa na kulipwa na Washitakiwa, na bakaa ambayo bado haijalipwa hadi kufikia tarehe 30 Machi 2022 na kuthibitisha endapo makosa yaliyo kwenye mashauri yaliyoendeshwa kwa Mikataba ya Maridhiano ya Kukiri Makosa yalistahili kupata ahueni husika.

**Mheshimiwa Spika,** hadidu nyingine za rejea zilizozingatiwa katika ukaguzi huu ni pamoja na kuthibitisha endapo mchakato wa kuingia makubaliano ya kukiri makosa ulikuwa wa haki na uwazi, Kupitia Mikataba ya Maridhiano ya Kukiri Makosa kujiridhisha na uthabiti wa vifungu na utekelezaji wake, Kuhakiki malipo yaliyofanyika toka kwenye Akaunti ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) (Maridhiano ya Kukiri Makosa) 9921169817 ili kuthibitisha uhalali na ukamilifu wake sambamba na kuthibitisha

ufasaha wa Bakaa iliyokuwepo tarehe 31 Machi 2022.Ukaguzi uliangalia mikataba ile tu ambayo kesi zake zilikuwa zimemalizika Mahakamani.

**Mheshimiwa Spika,** jambo la kwanza na muhimu katika ukaguzi ilikuwa ni kiasi cha fedha kilichoahidiwa kukusanywa (pledges) na kiasi halisi kilichokusanywa kutokana na mikataba ya kukiri makosa. Naomba kunukuu maelezo ya Ndugu Hiram J. Kisamo Mkaguzi kutoka Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi aliyotoa mbele ya Kamati siku ya tarehe 21 Agosti, 2023 kuhusu fedha zilizokusanywa na kuahidiwa. Maelezo hayo ni kama ifuatavyo:-

> **Nukuu:-**
> ***"…. Mheshimiwa Mwenyekiti, utakumbuka palikuwa na sintofahamu hapa kwamba shilingi ngapi zimekusanywa na shilingi ngapi zipo kwenye akaunti ya plea argain. Kwa hiyo, ukaguzi wetu ulijiridhisha kwamba hadi tarehe 30 Machi, 2022 ahadi ambazo zilikuwa zimekuwa pledged kwa ujumla wake zilikuwa shilingi bilioni 219.12 ambapo kati ya hizo, fidia cash ambayo ilikuwa imelipwa kuhusiana na plea bargain ilikuwa around shilingi bilioni 48,515,161,976. Hivyo, hadi kufikia tarehe 30 Machi, 2022 ndiyo ilikuwa mwanzo wa ukaguzi wetu, tulijiridhisha kwamba pledge zote ambazo zilikuwa zimewekwa kwenye mchakato wa maridhiano wa kukiri kosa, zilikuwa zinakaribia shilingi bilioni 219…"***
> **Mwisho wa Nukuu.**

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia maelezo hapo juu ya wakaguzi, fedha zilizotakiwa kukusanywa katika mikataba ya kukiri kosa zilikuwa **Sh. bilioni 219** na kiasi halisi kilichokusanywa kilikuwa **Sh. 48,515,161,976**. Hivyo kiasi cha **Sh. 170,614,243,393** kilikuwa hakijalipwa hadi ukaguzi huu unakamilika.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo, naomba kulifahamisha Bunge lako Tukufu hoja nyingine mahsusi za ukaguzi zilizotokana na ukaguzi huu maalumu. Ukaguzi huu maalumu

ulibaini masuala yafuatayo ambayo yanahusiana na matumizi na usimamizi wa fedha za umma:-

a) Baadhi ya washitakiwa kushindwa kukamilisha malipo ya bakaa ya fidia kulingana na mikataba ya maridhiano ya kukiri kosa/makosa na hukumu ya mahakama kiasi cha **Sh.170,614,243,393**;

b) Ukaguzi ulibaini kuwa kiasi cha jumla ya **Sh. 328,531,288** kati ya **Sh. 53,761,056,294** ziliwekwa kimakosa na washitakiwa watatu (3) ambao utaratibu wa kumaliza kesi zao haukuwa wa Mkataba wa Maridhiano ya Kukiri Kosa/Makosa (Plea Bargain) bali ulitumika utaratibu wa kawaida wa kukiri hatia;

c) Kutowasilishwa kwa majalada 15 ya kesi katika ukaguzi yenye fidia ya jumla **Sh.80,652,888**. Katika hoja hii ukaguzi ulibaini kuwa majalada kumi na tano (15) hayakuwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi hivyo kusababisha kupungua kwa mawanda ya ukaguzi na kushindwa kufikia malengo ya ukaguzi na hitimisho.

d) Fedha zitokanazo na utaifishaji kuwekwa kimakosa kwenye akaunti ya DPP ya maridhiano ya kukiri makosa **Sh. 6,103,646,447.86**. Katika hoja hii ukaguzi ulibaini kuwa kiasi cha **Sh. 6,103,646,447.86** kilichotokana na zoezi la utaifishaji kiliwekwa kimakosa katika akaunti ya DPP ya maridhiano ya kukiri makosa badala ya akaunti za utaifishaji zilizokuwa zimefunguliwa kwa dhumuni hilo. Kutoweka fedha hizo katika akaunti ya Utaifishaji kunaleta athari ya kukwamisha ufikiaji wa dhumuni la Serikali la kuanzisha akaunti maalum ya fedha za kigeni zilizotaifishwa ili kupunguza hasara na gharama za kubadilisha fedha za kigeni kwenda katika shilingi;

e) Malipo ya Tozo za mahakama Jumla **Sh.2,113,278,701.58** kulipwa kimakosa kwenye

akaunti ya DPP (Maridhiano ya kukiri makosa). Katika hoja CAG alibaini kuwa kiasi cha **Sh.2,113,278,701.58** tozo za mahakama kililipwa kimakosa kwenye akaunti ya DPP (Maridhiano ya kukiri makosa) kwenye akaunti namba 9921169817 hali iliyopelekea jumla ya mahakama 22 kutojumuisha mapato hayo katika vitabu vya hesabu na hivyo taarifa za mapato za mahakama kutokuwa sahihi;

f) Kutokuwepo kwa utaratibu wa kutunza kumbukumbu katika vikao vya majadiliano ya kukiri makosa baina ya washtakiwa na OTM. Katika hoja hii ukaguzi ulibaini kuwa OTM ilikuwa haitunzi kumbukumbu sahihi za makubaliano ya kukiri makosa. Hii iliathiri kutokuwepo kwa kumbukumbu sahihi za majadiliano kwa ajili ya rejea za baadae na hivyo kuchangia kutokuwepo kwa uwazi katika mchakato wa majadiliano;

g) Mapungufu katika utunzaji wa nyaraka na majalada ya mashauri. Katika hoja hii CAG alibaini kuwa na mapungufu katika utunzaji wa nyaraka muhimu katika majalada ya mashauri yaliyomalizika kwa makubaliano ya kukiri makosa. Athari ya kukosekanika kwa nyaraka muhimu kwenye majalada kunapunguza uwazi katika mchakato mzima wa kufikia mkataba wa maridhiano ya kukiri makosa;

h) Malalamiko ya kukosekana kwa hiyari ya washitakiwa kuanzisha mchakato wa maridhiano ya kukiri makosa. Katika hoja hii CAG alibaini kuwepo kwa malalamiko kwenye jamii kuhusiana na uvunjaji wa haki kwa ulazimishwaji wa washtakiwa kuingia katika maridhiano ya kukiri makosa;

i) Ukaguzi ulibaini mapungufu katika uendeshaji wa kesi Namba ECO.77/2018 kati ya Jamhuri dhidi ya washitakiwa Deodatus P. Mwanyika, Alex Lugendo Na Asa Mwaipopo. Katika hoja hii ukaguzi ulibaini kuwepo mienendo miwili ya mahakama (Court

proceedings) na mikataba miwili tofauti inayoonesha makubaliano ya washtakiwa kukiri makosa. Nyaraka za kwanza zinaonyesha kuwa washtakiwa walikiri kosa la kukwepa kodi na nyaraka ya pili inaonyesha kuwa washtakiwa walikiri kosa la kusababishia Mamlaka ya Serikali hasara. Kutokana na hili CAG alibaini kuwa nyaraka za makubaliano ya kukiri, hati ya mashtaka na kumbukumbu za mahakama zilikuwa na dosari;

j) Madhaifu na ukiukwaji haki katika kesi ya uhujumu uchumi namba ECO 8/2020 dhidi ya Lucas Pius Malya. Katika hoja hii ulibaini kuwa OTM, TRA na Kikosi kazi cha ukusanyaji wa Kodi kutozingatia taratibu na msingi ya haki katika kutekeleza majukumu yao ya msingi. Ukiukwaji huo ulijumuisha kumuweka mtuhumiwa gerezani kwa makosa ya kikodi pasipo kufuata utaratibu, na kulazimishwa kufanya malipo ya **Sh. 55,000,000** pasipo kuwepo kwa mkataba wa makubaliano ya kukiri kosa hali iliyomuumiza ndugu Lucas Pius Mallya binafsi, kibiashara na kutia doa utendaji wa vyombo husika vya Serikali;

k) Kukosekana kwa dhamana na zuio la hati ya kusafiria ya raia wa kigeni ambao hawakumaliza kulipa fidia **Sh.880,950,000**. Katika hoja hii CAG alibaini kuwa Mikataba ya washtakiwa wa kigeni ilikosa dhamana na zuio la hati zao za kusafiria kulikosababisha Jamhuri na waathirika binafsi kupata hasara ya fidia iliyotakiwa kulipwa baada ya washtakiwa kurudi katika nchi zao ama kutojulikana walipo;

l) Mikataba ya kukiri makosa kuwa na kiasi pungufu ya kile kilichopendekezwa awali na washitakiwa kwenye barua zao za dhamira **Sh.689, 362,985.07**. Katika hoja hii ukaguzi ulibaini uwepo wa Mikataba ya Maridhiano ya kukiri makosa iliyokuwa na kiasi pungufu na kilichopendekezwa na washtakiwa katika barua zao walizowasilisha kwa Mkurugenzi wa

Mashtaka. Jambo hili liliashiria uwepo wa mianya ya rushwa juu ya mikataba ya maridhiano ya kukiri makosa;na

m) Kutotekelezwa hukumu/amri za mahakama kuhusu marejeo ya tathmini ya kodi iliyopaswa kulipwa **Sh.61,805,200,298** kutokana na kesi za ukwepaji kodi.Katika hoja hii ukaguzi ulibaini kuchelewa kutekelezwa kwa amri za mahakama kwa zaidi ya miaka miwili kutokana na TRA kutorejea hukumu hizo na kufanya tathmini ya kodi kama ilivyoelekezwa na Mahakama.

**Mheshimiwa Spika,** kuna hoja nyingine ambayo Kamati ilitaka kupata maelezo ambayo inahusu madai ya uwepo wa fedha za mikataba ya kukiri makosa zilizowekwa nje ya nchi. Kutokana na hoja hii, Kamati ilipata maelezo ya wakaguzi ambayo yalibainisha hapakuwa na fedha zilizowekwa nje ya nchi badala yake kulikuwa na dosari za kiuandishi katika mojawapo ya fedha iliyowekwa kwenye akaunti ya DPP.Fedha hizo zilikuwa kiasi cha **Sh. 1,600,000,000** zilizowekwa na Profesa Anna Tibaijuka. Profesa Anna Tibaijuka aliweka fedha hizo kutokana na maelezo kwamba fedha hizo zilihusiana na mtuhumiwa mmojawapo wa kukiri makosa.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kununukuu maelezo ya Ndugu Hiram J. Kisamo Mkaguzi wa Hesabu kutoka Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi aliyoyatoa mbele ya Kamati siku ya tarehe 21 Agosti, 2023 kuhusu hoja hii kama ifuatavyo:-

**Nukuu:-**

***"…Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika ukaguzi wa hii fedha ya Mama Tibaijuka kuna vitu tulivibaini katikati. Hii field huwa inaandikwa address ya kule ambako fedha zinakwenda kwenye ile account. Kwa hiyo, katika ile address kulikuwa kuna maneno hela ametoa kwenye account yake ya CRDB imeandikwa address yake kwa ufasaha kwenda account ya DPP. Jina la account ya DPP lilikuwa limeandikwa kwa ufasaha kabisa na account number except kwenye upande wa address ilikuwa***

***imeandikwa Zhengzhou-China. Lakini kwa ukaguzi tuliofanya tumeongea na watu wa DPP tukaongea na Mama mwenyewe,tukaongea na wafanyakazi wa CRDB waliofanya hii transfer wote wakadhihirisha kwamba hiyo Zhengzhou-China ilikuwa ni makosa ya kiuandishi. Mheshimiwa Mwenyekiti, pale ilitakiwa iandikwe Dar es salaam-Tanzania kwa sababu account ya DPP ameandikwa pale juu na address yake then ilitakiwa isomeke Dar es salaam – Tanzania. Benki walithibitisha na wakataundikia kwa barua ku-confirm kwamba yalifanyika makosa ya kiuandishi. Badala ya kuandika Dar es salaam wakaandika Zhengzhou-China. Kwa hiyo, maelekezo tuliyokuwa tumepata kwenye swift hii kwamba kuna fedha ziko nje ya Nchi kupitia hii kiashiria hiki cha hii document kutoka kwa Prof. Tibaijuka tulijiridhisha kwamba kweli hakukuwa na hizo fedha nje ya Nchi…"***

**Mwisho wa Nukuu.**

**Mheshimiwa Spika,** kwa maelezo hayo ni dhahiri kwamba fedha za akaunti ya kukiri makosa hazikupelekwa nje ya Nchi kama Ukaguzi huu Maluumu wa CAG ulipokuwa unakamilika.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na uzito wa hoja zilizoibuliwa na Ukaguzi huu Maalumu, Kamati ilifanya mahojiano na Afisa Masuuli wa Fungu – 35 Ofisi ya Taifa ya Mashtaka hapa Bungeni siku ya tarehe 21 Agosti, 2023 kujadili matokeo ya ukaguzi huo. Kwa mujibu wa Sheria ya Fedha za Umma Sura 348, Afisa Masuuli wa Fungu 35 ni Naibu Mkurugenzi wa Mashtaka. Hata hivyo, Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) na Mwanasheria Mkuu wa Serikali walihudhuria kikao husika ili kutoa maelezo ya ufafanuzi pale walipotakiwa kufanya hivyo.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kunukuu maelezo ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) Ndugu Silvester Mwakitalu kuhusu ushiriki wake kwenye kikao husika cha Kamati kama ifuatavyo:-

**Nukuu:-**

***"…Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muundo wa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, Afisa Masuuli ni Naibu Mkurugenzi wa Mashtaka. Yeye kimsingi anashughulika na masuala ya fedha na nidhamu ya watumishi. Masuala ya kisheria (kesi) haya ni ya Mkurugenzi wa Mashtaka. Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa nature ya mjadala wa leo wakati mwingine kuna mambo yatamhusu Mkurugenzi wa Mashtaka mwenyewe. Kwa hiyo, tukaona ni vyema tuwepo tuweze kusaidia kutoa ufafanuzi badala ya kumwachia Afisa Masuuli ambaye kimsingi yeye anashughulika sana na masuala ya fedha na nidhamu ya watumishi…"***

**Mwisho wa Nukuu.**

**Mheshimiwa Spika,** vilevile naomba kunukuu maelezo ya Mhe.Jaji Dkt. Eliezer M. Feleshi, Mb – Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuhusu ushiriki wake kwenye kikao cha kujadili hoja za ukaguzi maalumu kama ifuatavyo:-

***"…uwepo wangu leo umechagizwa na jambo lililonifikia ofisini. Hivyo, nikalazimika kuambatana na Mkurugenzi wa Mashtaka ili pamoja na mambo mengine kama Mshauri wa Serikali na Bunge kwa mambo yale yanayotoka Serikalini kuja huku, ikiwapendeza basi mtafanya jambo la kiutaratibu walau kuomba…"***

**Mwisho wa Nukuu.**

**Mheshimiwa Spika,** kama maelezo ya hapo juu ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ilikuwa ni muhimu kwa viongozi hao wawili kuhudhuria katika kikao cha kujadili matokeo ya ukaguzi maalumu.Katika maelezo yake DPP alikiri mbele ya Kamati kuwa kulikuwa na changamoto za kisheria katika utekelezaji wa mikataba ya kukiri kosa. Naomba kunukuu sehemu ya maelezo yake kama ifuatavyo:-

**Nukuu:-**

***"…Mheshimiwa Mwenyekiti, mapungufu mengi ambayo yamebainika kwenye ripoti ya ukaguzi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, mengi tumeshayafanyia kazi, kwa sababu tulipata fursa ya kukaa na Wakaguzi mapema, lakini tulipata fursa ya kupitia taarifa hii kabla haijafika kwako. Kwa hiyo, mengi tumeshayafanyia kazi na sasa zipo vizuri. Yanayohitaji kurekebisha sheria mengine tumeshapeleka kwa Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria ili aweze kuanzisha mchakato wa kurekebisha sheria…"***

**Mwisho wa Nukuu.**

**Mheshimiwa Spika,**kupitia mahojiano ya Kamati na Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG), kulijitokeza pia hoja ya hatua za kinidhamu zilizochukuliwa kwa baadhi ya Watumishi wa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka na Mahakama kutokana na dosari zilizobainishwa na CAG. Kwa ujumla majibu ya Serikali yalifafanua kuwa hatua za kinidhamu bado hazijakamilika kwa kuwa kuna uchunguzi bado unaendelea. Naomba kunukuu sehemu ya maelezo ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG), Mhe. Jaji Dkt. Eliezer M. Feleshi kuhusu hatua za kinidhamu kwa baadhi ya watumishi waliohusika na mapungufu ya mikataba ya kukiri kosa kama ifuatavyo:-

***"…Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kilicho-pose taarifa ya CAG, nafikiri ni recommendation, mambo yanayotajwa kama ya kweli hayo, ndiyo maana tumesema kwamba haya yote, yaliyo mengi kama ni specific maana yake yanafanyiwa uchunguzi mahususi. Kwa ujumla wa yote, mengine ndiyo yale niliyoeleza hapo nyuma kwamba, kuhusiana na hayo mambo ya Plea Bargain, mambo yote yenye utata zaidi ambayo DPP hana majibu, Serikali kwa sasa haina majibu, labda CAG itokee naye hana majibu. Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana Mheshimiwa Rais baada ya kuona labda CAG ameibua nini, wengine wameenda kwake,***

***wengine wameenda kwa Waziri Mkuu na Mamlaka nyingine,akataka uchunguzi ufanyike. Ndiyo maana lile pendekezo la nne, ukweli limependekeza kwamba kwa mambo ambayo yataendelea kuwa na utata, yafanyiwe uchunguzi mahususi. Uchunguzi mahususi maana yake unaweza ukawa kati ya sheria zetu tulizonazo, lakini Mheshimiwa Rais anaweza akaanzisha commission of enquiry chini ya ile sheria mahususi. Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Mwambe, niseme tu kwamba, kwa sababu haki za watumishi zimelindwa na Katiba, chochote ambacho kimeibuliwa kwenye taarifa ya Mkaguzi, maana yake kinahitaji substantiation, na endapo mtakuja kuthibitika, maana yake mkondo wa Sheria yetu utatumika…."***

**Mwisho wa Nukuu.**

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na maelezo hayo ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ni dhahiri kwamba mapendekezo ya CAG yanayohusu hatua za kinidhamu kwa baadhi ya watumishi wa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka na Mahakama hazijachukuliwa hadi kukamilika kwa uchunguzi.

### 2.4.2 Uchambuzi wa Taarifa ya Ukaguzi Maalumu Kuhusu Shughuli za Utaifishaji, Makabidhiano na Ugawaji wa Mali Zilizotaifishwa (Forfeiture)

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia wajibu wake wa Kikatiba na Kisheria, CAG alifanya ukaguzi maalumu kuhusu shughuli za utaifishaji, makabidhiano na ugawaji wa mali zilizotaifishwa. Ukaguzi huu pia unaangukia katika Fungu – 35, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ambapo Naibu Mkurugenzi wa Mashtaka ndiye Afisa Masuuli.

**Mheshimiwa Spika,** katika kupitia na kuchambua matokeo ya ukaguzi huu maalumu, Kamati ilijielekeza katika hoja ambazo zina uhusiano wa moja kwa moja na matumizi ya fedha za umma. Ambapo katika kujielekeza huko, uchambuzi uliangalia pia baadhi ya maamuzi yaliyofanyika na ambayo endapo

hayatafanyiwa kazi yanaweza kuisababishia Serikali hasara kwa siku zijazo.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kulifahamisha Bunge lako Tukufu matokeo ya ukaguzi huo maalumu kama ifuatavyo:-

**2.4.2.1 Kutowepo kwa mwongozo juu ya madhumuni ya Serikali baada ya kutaifisha madini, magogo na mali zinginezo kwa muda mrefu bila kuchukua hatua yeyote**

**Mheshimiwa Spika,** katika eneo hili ukaguzi uligundua kuendelea kuhifadhi mali zilizotaifishwa kwa muda mrefu bila kuwepo malengo mahususi jambo linalohatarisha usalama na thamani ya mali husika zilizotaifishwa. Ukaguzi ulipendekeza Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango kukamilsha uandaaji wa Mwongozo na kanuni zitakazo simamia shughuli za utaifishaji hadi hatua ya makabidhiano ili kuhakikisha usalama wa mali husika, thamani na kuongeza tija katika utaifishaji na mapambano dhidi ya uhalifu.

**2.4.2.2 Kukosekana kwa mwongozo wa umiliki wa mali zinazotaifishwa ambazo hazina takwa au utaratibu wa kisheria wa kusajiliwa katika regista ya Hati Miliki**

**Mheshimiwa Spika,** katika hadidu hii hoja kubwa iliyoibuliwa na ukaguzi ni kwamba, mali nyingi zilizotaifishwa hukaa muda mrefu bila kuchukuliwa hatua sahihi za kuzitumia ili kuleta tija katika utaifishaji na kuchochea jitihada za kuzuia uhalifu. Kuhusu jambo hili CAG alipendekeza kuwa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kushirikiana na vyombo vingine vya Serikali kuharakisha kuandaa mwongozo wa kisheria wa nini kifanyike kuhusiana na mali zilizotaifishwa.

**2.4.2.3 Sheria kutotambua haki ya mwathirika wa mali zilizotaifishwa**

**Mheshimiwa Spika,** ukaguzi ulibaini kuwa waathirika wa uhalifu (victims of offence) hawarejeshewi mali zao baada ya kufanyiwa uhalifu jambo ambalo linapelekea vyombo vya kusimamia haki kuonekena havitendi haki kwa baadhi ya waathirika wa uhalifu. Katika hili CAG alipendekeza kufanyika kwa marekebisho katika

Sheria ya Mazalia ya Uhalifu na Sheria ya Uhujumu Uchumi pamoja na sheria nyingine ili kuweka uwazi haki na pia fursa ya kutathmini jinsi gani mwathirika wa uhalifu anaweza kufidiwa au kurejeshewa mali yake baada ya uhalifu.

**2.4.2.4 Mali zilizotaifishwa lakini hakuna uthibitisho wa makabidhiano kati ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka na Wizara ya Fedha na Mipango**

**Mheshimiwa Spika,** katika eneo hili ukaguzi ulibaini uwepo wa mali zilizoainishwa ambazo zilitaifishwa na hakukuwa na uthibitisho wa makabidhiano kati ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka na Wizara ya Fedha na Mipango. Ukosefu wa taarifa kamili za makabidhiano ya mali zilizotaifishwa kunapelekea uwezekano wa upotevu wa mali husika, kuharibika au kutoa fursa ya kutumika kwa matumizi nje ya Serikali, hivyo kukwamisha kufikia tija katika lengo la kisheria la utaifishaji mali. Pia kutowepo kwa hati au taarifa za makabidhiano kunapelekea kutojua mali zilipo na Taasisi gani inawajibika kwa wakati husika.

**Mheshimiwa Spika,** utaratibu wa hifadhi ya mali zilizotaifishwa ni kuwa, baada ya kukamilika kwa taratibu za mahakama, mali zote zilizotaifishwa zikabidhiwe haraka kwa Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango kwa hati maalumu za makabidhiano na Kuboresha uandaaji na utunzaji wa taarifa za mali zilizotaifishwa na makabidhiano yake ili kuimarisha usimamizi na ufuatiliaji wake.

**2.4.2.5 Mali zilizotaifishwa na kukabidhiwa kwa Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango kabla ya amri/hukumu ya Mahakama**

**Mheshimiwa Spika,** hoja ya ukaguzi katika eneo hili ilikuwa kwamba kutekeleza makabidhiano ya mali zilizotaifishwa kabla ya amri ya Mahakama kunakinzana na matakwa ya sheria inayosimamia mchakato wa utaifishaji wa mali na kunaweza kusababisha changamoto katika kutoa haki.

**2.4.2.6 Utaifishaji wa madini ya almasi karati 71,654.56 yenye thamani ya Dola za Marekani 29,509,821.84 bila mmiliki wa madini kuhusishwa**

**Mheshimiwa Spika,** katika hii hoja taarifa ya ukaguzi maalumu inabainisha kuwa katika mapitio ya mkataba wa maridhiano ya kukiri kosa katika kesi ya uhujumu uchumi namba 54/2017 Mahakama ya Uhujumu Uchumi Dar- es salaam baina ya "Serikali na Archard Alphonce Kalugendo na Edward Joseph Rweyemamu" washtakiwa walifunguliwa shtaka la kuisababishia Serikali hasara ya **Dola za Marekani 1,118,291.43** (sawa na **Sh.2,486,397,982.54**).

**Mheshimiwa Spika,** ukaguzi ulibaini kuwepo utaifishwaji wa karati 71,654.56 za Almasi zenye thamani ya **Dola za Marekani 29,509,821.84** kama mazalia ya uhalifu kwa makubaliano baina ya Serikali na washtakiwa ambao ni watumishi wa Serikali pasipo kutaarifiwa au kuwepo mmiliki wa madini hayo au mwakilishi wake.Hivyo, uamuzi huu unaweza kuisababishia Serikali hasara kwa siku zijazo kutokana na sheria za utaifishaji kutofuatwa.

**2.4.2.7 Fedha zilizotaifishwa kuwekwa kimakosa katika akaunti ya makubaliano ya kukiri makosa kiasi cha Sh 6,093,646,447.86**

**Mheshimiwa Spika,** katika Ukaguzi huu Maalumu kulibainika hoja ya kuhifadhi fedha zilizotaifishwa katika akaunti ya makubaliano ya kukiri makosa badala ya akaunti maalumu za utaifishaji mali inapoteza mtiririko wa utambuzi na ufuatiliaji wa fedha zilizotaifishwa jambo ambalo linaweza kupelekea fedha hizo kutumika kinyume na malengo yaliyokusudiwa.

**2.4.2.8 Fedha taslimu zilizotaifishwa kukabidhiwa Hazina bila kupitia akaunti za utaifishaji mali zinazokadiriwa kufikia sh 1,300,501,994.17**

**Mheshimiwa Spika,** hoja ya ukaguzi katika eneo hili ni kwamba utaratibu wa kukabidhi fedha taslim Hazina bila kupitia akaunti rasmi za utaifishaji unaleta shaka juu ya uthibiti, usimamizi na usalama wa fedha unaoweza kupelekea upotevu au matumizi yasiyo sahihi ya fedha husika.

**Mheshimiwa Spika,** utaratibu sahihi ni kwa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kuhakikisha kuwa fedha zote zilizotaifishwa zinahifadhiwa katika akaunti sahihi za utaifishaji mali na kuandaa mwongozo na kutoa elimu kwa watendaji wote wanaohusika na shughuli za utaifishaji mali juu ya uasalama na uthibiti wa fedha zilizotaifishwa ili utekelezaji wake usivunje sheria au kutoa fursa ya upotevu.

**2.4.2.9 Kutowepo kwa daftari la utunzaji fedha zinazotokana na utaifishaji mali, kutotoa stakabadhi ya fedha zilizotaifishwa na kutowepo rejesta ya mapokezi ya fedha zilizotaifishwa**

**Mheshimiwa Spika,** hoja ya ukaguzi katika eneo hili ni kwamba kukosekana kwa daftari na rejesta ya fedha zilizotaifishwa na kutotoa stakabadhi inaonesha kuwa mfumo wa udhibiti wa ndani wa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka haukuwa madhubuti hivyo inakuwa vigumu kutambua na kutoa taarifa ya jinsi fedha zilivyopokelewa katika akaunti hizo na kukwamisha ufuatiliaji wa makusanyo ya fedha jambo linaloweza kupelekea upotevu wa fedha za umma.

**Mheshimiwa Spika,** utaratibu unaofaa ni kwa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha kuweka utaratibu sahihi wa usimamizi wa akaunti zote za utaifishaji ili kuhakikisha kuwa zinakuwa na daftari sahihi la utunzaji fedha na kufanya usuluhishi wa benki kila mwezi na kuhakikisha kuwa Idara ya Fedha inakuwa na rejesta ya fedha zote zilizotaifishwa na usuluhishi wa miamala yote ufanyike. Nilishauri pia kuimarisha mfumo wa uthibiti wa ndani katika kurekodi, kukusanya, kutunza na kutoa taarifa za fedha zinazotokana na utaifishaji ili kutoa taarifa sahihi kwa wakati.

**2.4.2.10 Ukusanyaji wa fedha zilizozuiliwa na kutaifishwa kutoka benki za biashara kwa awamu na kushindwa kuhamishwa kiasi chote kilichotaifishwa kwenda katika akaunti za utaifishaji za Ofisi ya Taifa ya Mashtaka**

**Mheshimiwa Spika,** hoja ya ukaguzi katika eneo hili ni kwamba jumla ya kiasi cha **Sh.14,646,730,922.76** kilitaifishwa na kurejeshwa kwenye akaunti za utaifishaji za Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kutoka benki mbili za biashara "DCB na NMB" kwa awamu tatu mpaka sita bila ya kuwepo kwa mkataba au ushahidi wa makubaliano

juu ya urejeshaji wake na riba itakayozaliwa baada ya kuchelewa kurejesha. Hata hivyo, ni benki ya NMB pekee ndiyo iliyoweza kurejesha kiasi chote na riba ya **Sh. 685,961,812.38** wakati benki ya DCB ilirejesha kwa awamu sita bila ya riba yoyote.

**Mheshimiwa Spika,** kwa msingi huo Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ilitakiwa kuimarisha mikakati ya urejeshaji wa fedha zote zinazotaifishwa toka kwenye akaunti za benki za biashara mara baada ya amri ya mahakama kutolewa na kuhakikisha fedha zote zilizotaifishwa zinakusanywa na kuingizwa katika akaunti za Utaifishaji ili kuepuka upotevu wa fedha za Serikali.

**Mheshimiwa Spika,**baada ya kubainisha mapungufu yaliyojitokeza katika zoezi zima la utaifishaji wa mali, Kamati ilifanya mahojiano na Afisa Masuuli wa Fungu 35 ili pamoja na mambo mengine kuifahamisha Kamati hatua zilizochukuliwa kwa chagamoto zilizobainishwa. Ni muhimu kukumbuka kwamba, zoezi hili la utafishaji mali likiendeshwa bila utaratibu litakuja kuwa na athari mbaya kwa Serikali kwa siku zijazo hasa kama Serikali itapelekwa mahakamani na kushindwa katika kesi. Naomba kunukuu maelezo ya Mheshimiwa Japheti N. Hasunga, Mb – Makamu Mwenyekiti wa PAC wakati akisisitiza suala la utaifishaji mali bila ya kuwa na miongozo sahihi kama ifuatavyo:-

> **Nukuu:-**
> ***"…Waheshimiwa Wajumbe, ukienda eneo lile lingine mimi nilikuwa naona hivi kulikuwa na issues ambazo zipo, kwa mfano maswali ya kwa nini hakukuwa na mwongozo wa utaifishaji, utunzaji, ugawaji na usafirishaji wa mali zilizotaifishwa. Hilo ni swali tunaweza kuliuliza. Pia kwa nini hakukuwepo na daftari la mali zilizotaifishwa? kukosekana kwa usalama wa mali zilizotaifishwa kutokuwepo kwa uthaminishaji wa mali zilizotaifishwa, kutokuwa na ukamilifu au kutokuwa na mfumo wa umiliki au usajili wa mali zilizotaifishwa na kadhalika na kutokuwepo kwa mfano, zile pikipiki 40 ambazo mmesema mpaka sasa hivi hazijulikani zilipo…"***

**Mwisho wa Nukuu.**

**Mheshimiwa Spika,** Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) Ndugu Silvester Mwakitalu, aliifahamisha Kamati kuwa ni kweli palikuwa na changamoto ya miongozo ya kusimamia zoezi la utaifishaji mali.Naomba tena kunukuu sehemu ya maelezo yake kwa Kamati kama ifuatavyo:-

> **Nukuu”-**
> ***“…Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu wa kutaifisha mali upo kwa mujibu wa sheria. Ipo Sheria ya Mazalia ya Uhalifu na ipo Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, Sura ya 20. Sheria hizi kimsingi zimepewa vifungu vya kuruhusu. Nakiri kwamba, katika sheria hizi hakukuwa na ufafanuzi wa kutosha namna sasa ya kutekeleza. Kwa hiyo, wakati mwingine ni practice tu zilitumika. Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuwa tumeona changamoto hizo, sasa tumeanza kutengeneza miongozo na miongozo mingi tayari imekamilika. Ipo michache ambayo nilipeleka kwa wadau ili waweze kuiona na kui-validate na baadaye tutaanza kuitumia…”***
>
> **Mwisho wa Nukuu.**

**Mheshimiwa Spika,** hoja ya msingi ya Kamati katika eneo hili ni kwamba, utaifishaji wa mali bila kuwa na miongozo thabiti unaiweka Serikali katika hatari ya kuja kudaiwa fedha siku za usoni endapo itapelekwa Mahakamani na kushindwa kesi. Aidha, kutokuwepo kwa miongo kunasababisha mali hizo ambazo zinaweza kuwa za umma kupotea, kuibiwa au kuharibika.

### 2.4.3 Uchambuzi wa Taarifa ya Ukaguzi Maalumu wa Matumizi ya Fedha za Mfuko wa Tozo na Tuzo wa Jeshi la Polisi

**Mheshimiwa Spika,** Jeshi la Polisi lilianzisha Mfuko wa Tuzo na Tozo mwaka 2010 kwa lengo la kukusanya fedha kutoka vyanzo vya ndani na nje ya Jeshi hilo. Mnamo tarehe 21 Juni 2010, Katibu Mkuu Wizara ya Fedha kupitia barua yenye Kumb. Na. TYC/H/50/9 ya tarehe 21 Juni 2010 alitoa kibali kwa Jeshi la Polisi kuanzisha mfuko huo na kwamba fedha zitakazo kusanywa kutoka taasisi mbalimbali zitakazopatiwa huduma ya ulinzi zitawekwa katika

akaunti Na. 9921152001 ya Mfuko huo iliyopo Benki Kuu ya Tanzania (iliyofunguliwa baada ya kibali hicho kutolewa).

**Mheshimiwa Spika,** Kifungu Na. 66(1) na (2) cha Sheria ya Jeshi la Polisi na Huduma Saidizi, Sura ya 332 kimeainisha vyanzo vya mapato vya Mfuko huo kuwa ni faini kwa kosa lolote la kinidhamu, tuzo zote, fidia na faini za kisheria zinalipwa kwa mtoa habari/mtafutaji mali zisizodaiwa (endapo mtoa habari/mtafutaji mali huyo ni afisa wa polisi). Pia, faini zinazotozwa na mahakama kutokana na shambulio dhidi ya afisa polisi.

**Mheshimiwa Spika,** Kifungu Na. 66(3) cha Sheria hiyo kimeainisha kuwa Inspekta Jenerali wa Polisi ndiye mwenye mamlaka ya matumizi ya fedha kutoka katika Mfuko huo, ambapo Agizo Na. 2(b) VI la Maagizo ya Jumla ya Jeshi la Polisi (PGO) Na. 135 linaruhusu Jeshi hilo kutoa huduma ya ulinzi kwa taasisi mbalimbali za Serikali, mabenki, migodi na makampuni binafsi kwa malipo kulingana na idadi ya askari watakaohusika. Pia, Agizo Na. 2(c) la Maagizo hayo limeainisha mamlaka hayo kama ifuatavyo:-

a) Kutoa msaada kwa mwenza/familia ya Askari aliyefariki aliyekuwa na ngazi ya chini hadi Mrakibu, na kwa askari aliyeondolewa jeshini kwa tatizo la kiafya;

b) Kutoa tuzo/zawadi kwa askari walioshambuliwa kwa silaha au kuumizwa katika matukio au kwa manufaa ya Jeshi la Polisi;

c) Kuwalipa askari wa ngazi za chini hadi Mrakibu tuzo kwa ajili ya kutunuku vitendo au utumishi katika kutekeleza majukumu; na

d) Matumizi kwa manufaa na maendeleo ya burudani na michezo iliyoidhinishwa na shughuli nyingine zilizoandaliwa na Jeshi.

**Mheshimiwa Spika,** ukaguzi maalumu katika mfuko wa Tuzo na Tozo wa Jeshi la Polisi umebainisha dosari kadhaa katika matumizi ya fedha za umma katika maeneo yafuatayo:-

a) Taasisi 31 zilipokea huduma ya ulinzi zikiwa na mikataba iliyokwisha muda wake bila kuhuishwa na kutolipa kiasi cha **Sh. 2,257,733,304**. Katika kipindi cha kati ya mwaka mmoja hadi mitano ambacho Jeshi halikuwa na mikataba na taasisi hizo, liliendelea kutoa huduma za ulinzi na kutoza kiasi cha jumla ya **Sh. 5,432,172,340**. Hata hivyo, kiasi cha **Sh. 3,174,439,036** kililipwa na kiasi cha **Sh. 2,257,733,304** hakikuwa kimelipwa hadi wakati wa ukaguzi Oktoba 2022;

b) Taasisi 21 Kutolipia Huduma ya Ulinzi ya Jeshi la Polisi **Sh. 1,623,718,172**. Jumla ya hati za madai 1,820 zenye thamani ya **Sh. 24,112,248,110** zilitolewa na Jeshi la Polisi Tanzania kwa taasisi 21 kati ya 28 zilizopatiwa huduma ya ulinzi na Jeshi hilo. Hata hivyo, kiasi cha **Sh.22,488,529,938** kililipwa na **Sh. 1,623,718,172** hakikulipwa kwa Jeshi licha ya taasisi hizo kupatiwa huduma ya ulinzi;

c) Uhakiki wa utaratibu unaotumika kutoa Hati za madai (invoices) ulibaini dosari ikiwa ni pamoja na Kutounganishwa kwa Mfumo wa Mapato ya Ulinzi na Mfumo wa Malipo ya Serikali (Government e-Payment Gateway (GePG)) kinyume na Kifungu cha 7(1) cha Sheria ya Fedha za Umma, Sura ya 348. Pia, kumepelekea kukosekana kwa udhibiti wa mapato yanayokusanywa kupitia mfumo wa Mapato ya Ulinzi; Aidha, taarifa za Mfumo wa Mapato ya Ulinzi katika sehemu ya "IGP Payment report module" zilitofautiana na taarifa zilizoonekana kwenye hati za madai zilizotolewa kutoka kwenye mfumo huo, hivyo kuwepo hitilafu ya taarifa za mfumo husika;Kompyuta Na. DESKTOP-6VLGSFB iliyosimikwa Mfumo wa Mapato ya Ulinzi haikuwa na nywila hivyo kutoa fursa kwa mtumiaji asiyehusika na kuhatarisha usalama wa taarifa;

d) CAG kupitia barua yenye Kumb. Na. CTA.35/364/O1D/94 ya tarehe 13 Januari 2022 alimuomba Gavana Benki Kuu kuthibitisha miamala

iliyofanyika katika Akaunti Na. 9921152001 ya Mfuko wa Tuzo na Tozo kuanzia Julai 2018 hadi Novemba 2021. Kufuatia maombi hayo, mnamo tarehe 19 Januari 2022 Ndg. A. M. Hollevas na Ndg. M. E. Mmari, kutoka Idara ya Huduma za Kibenki Benki Kuu (BoT) kupitia barua yenye Kumb. Na. EA.4/263/01/293 walibainisha kuwa mwezi Machi 2019 baada ya kupokea maelekezo ya Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango, Benki hiyo ilihamisha kiasi cha **Sh. 2,622,247,480** kutoka Akaunti Na. 9921152001 ya Tuzo na Tozo Kwenda Akaunti Na. 9921169777 ya 'CPS Miscellenous Deposit Expebditure Account' kwa shughuli za Jeshi la Polisi. Pia, aliwasilisha barua za tarehe 12 Machi 2019 na 19 Januari 2022 zilizosainiwa na Ndg. Victus P. Tesha na W. A. Ngao mtawalia, kwa niaba ya Katibu Mkuu Hazina zilizomuelekeza Meneja Idara ya Utendaji, Benki Kuu kuhamisha kiasi kilichoombwa cha **Sh. 2,622,247,480**. Licha ya kuomba kuhamishiwa kwenye Akaunti ya matumizi ya Jeshi la Polisi Mwaka 2019 fedha hizo zilikuwa bado hazijatumika hadi wakati wa ukaguzi huo Oktoba 2022; na

e) Ukaguzi ulibaini kuwa katika kipindi chote cha miaka mitatu kuanzia 2018/19 hadi 2020/21 jumla ya komandi tano za Makao Makuu Dar es Salaam, Makao Makuu Dodoma, Kamanda wa Mkoa Geita, Simiyu na Dodoma pekee kati ya 62 za Jeshi la Polisi ndizo zilipata mgao wa kiasi cha **Sh. 14,925,668,791.36**. Mgao huo ulifanyika kwa kibali cha IJP na hakukuwa na mwongozo wowote wa Jeshi la Polisi unaoweka misingi katika matumizi na mgao wa fedha hizo, hali iliyopelekea komandi/vikosi vingine 57 kutopokea kiasi chochote kutoka Mfuko wa Tuzo na Tozo katika kipindi cha miaka mitatu, licha ya kushiriki katika uzalishaji wa fedha hizo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilifanya mahojiano na Afisa Masuuli wa Fungu 28 – Jeshi la Polisi akiwa ameambatana na uongozi wa Juu wa Jeshi la Polisi siku ya tarehe 24 Agosti, 2023 kupata ufafanuzi

wa dosari zilizobainishwa hapo juu. Mathalani kwa hoja ya Mfuko wa Tuzo na Tozo wa Jeshi la Polisi kutokuwa na Kanuni za Uendeshaji, hoja hii inathibitishwa na maelezo ya Kamishina wa Fedha na Lojistiksi wa Jeshi la Polisi Ndugu Liberatus Sabas kama yanavyonukuliwa hapa chini:-

> **Nukuu:-**
> ***"…Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kulikuwa na hili suala la mfuko kuendeshwa bila ya kuwa na kanuni. Suala hili tumelifanyia kazi, rasimu ya kanuni imeshaandaliwa na tunavyozungumza sasa hivi ipo kwa Katibu Mkuu Hazina, ambaye kimsingi naye baada ya kuipitia akiridhika basi itapitishwa rasmi kutumika kama kanuni za kuendeshea mfuko wa tuzo na tozo. Kwa hiyo, kwa sasa hivi ipo kwa Katibu Mkuu Hazina…"***

**Mwisho wa Nukuu.**

**Mheshimiwa Spika,** maelezo hayo hapo juu yanathibitisha kuwa Mfuko wa Tozo na Tuzo wa Jeshi la Polisi kwa muda wote uliendeshwa bila Kanuni hivyo kuchangia mapungufu ya usimamizi thabiti wa fedha za umma.

**Mheshimiwa Spika,** kwa hoja ya fedha za Mfuko wa Tuzo na Tozo wa Jeshi la Polisi kutumika kwa kiasi kikubwa kwenye komandi tano pekee badala ya Nchi nzima, hoja hii pia ilithibitishwa na maelezo ya Afisa Masuuli Fungu 28, Ndugu Kaspar Kaspar Mmuya mbele ya Kamati tarehe 24 Agosti, 2023, kama yanavyonukuliwa hapa chini:-

> ***"…Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati anaendelea kutoa maelezo ya swali la msingi, kwanza ninaomba kukiri kuwa, kwa taarifa iliyomo ya CAG ipo sahihi kuwa ni command tano ndiyo zilipokea fedha hizi shilingi bilioni 14 plus. Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo tatizo ndiyo maana kwa nafasi ya Katibu Mkuu alitoa maelekezo ya kufuata Kanuni ambayo itaandaliwa rasmi***

> ***ambayo itapelekea fedha hizi zipelekwe kwenye mikoa kulingana na mahitaji…"***

**Mwisho wa Nukuu.**

### 2.4.4 Uchambuzi wa Taarifa ya Ukaguzi Maalumu wa Mfuko wa Kufa na Kuzikana wa Jeshi la Polisi

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipata fursa pia ya kupitia na kuchambua taarifa ya ukaguzi Maalumu kuhusu Mfuko wa Kufa na Kuzikana wa Jeshi la Polisi. Kwa ajili ya kutoa usuli (maelezo ya awali) kuhusu Mfuko huu kwa Bunge lako Tukufu, naomba kulifahamisha Bunge kuwa , Inspekta Jenerali wa Polisi kupitia Kifungu Na. 7(2) cha Sheria ya Jeshi la Polisi na Huduma Saidizi, Sura ya 332 alianzisha Mfuko wa Kufa na Kuzikana kwa mamlaka aliyonayo.

**Mheshimiwa Spika,** Kifungu Na. 66(1) na (2) cha Sheria hiyo, vilevile kimeainisha chanzo cha mapato ya Mfuko huo kuwa ni michango ya Askari ya kiasi cha **Sh. 5,000** kila mwezi inayokatwa kutoka kwenye mishahara yao na kukusanywa kupitia Akaunti Na. 2016600444 iliyopo katika Benki ya NMB.

**Mheshimiwa Spika,** kama ilivyokuwa kwa ukaguzi wa Mfuko wa Tuzo na Tozo wa Jeshi la Polisi, ukaguzi huu ulifanyika kufuatia ombi la Katibu Mkuu Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kupitia barua yenye Kumb. Na. CJA.95/199/01/52 na Na. CJA.95/199/01/53 za tarehe 18 Novemba 2021, na kwa kuzingatia Kifungu Na. 27 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma, Sura 418 kinachompa mamlaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kufanya Ukaguzi wa Kiuchunguzi baada ya kupokea taarifa zinazoonesha dalili za ubadhirifu, ambapo ukaguzi huu ulikamilika tarehe 31 Oktoba 2022.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo ya utangulizi naomba kulifahamisha Bunge lako Tukufu matokeo ya ukaguzi huo maalumu kama ifuatavyo:-

### 2.4.4.1 Ukiukwaji wa Mwongozo wa Mfuko na Viongozi Kujinufaisha Binafsi

Taarifa ya ukaguzi maalumu imebainisha kwamba, waliokuwa Meneja wa Mfuko huo ASP. Yusta Andrew Mwasanyamba (Julai 2018 hadi Januari 2020) na Insp. Abdallah Kambini (Februari 2020 hadi Novemba 2021) hawakuitisha vikao vya Sekretarieti wala vya wanachama wa Mfuko kinyume na Kipengele 18.1 cha Mwongozo wa Mfuko. Hata hivyo, katika kipindi cha uongozi wao Sekretarieti ya Mfuko huo haikuwa imeundwa, pia, Hesabu za Mfuko huo hazikuwahi kuandaliwa. Kadhalika, IJP. Simon Sirro, aliyekuwa Mlezi wa Mfuko kuanzia 2017 hadi 2022 alishindwa kumuelekeza Mwenyekiti kuitisha Mkutano Mkuu wa Mfuko katika kipindi chote cha miaka 5, kinyume na Kipengele Na.18.1 cha Mwongozo wa Mfuko wa Kufa na Kuzikana, 2009. Pia, Mwenyekiti CP Benedict Wakulyamba alishindwa kutimiza majukumu yake. CP Benedict Wakulyamba, aliyekuwa Kamishna wa Utawala na Mwenyekiti wa Mfuko na IJP Mstaafu Simon Sirro, aliyekuwa Mlezi wa Mfuko walieleza kuwa aliyekuwa Meneja wa Mfuko Insp. Abdalla Kambini aliyetoroka, alihusika na upotevu wa fedha na nyaraka za Mfuko wa Kufa na Kuzikana. Timu ya Ukaguzi ilihakiki akaunti binafsi ya Ndg. Abdallah Kambini Na. 20108003207 iliyopo Benki ya NMB (iliyokuwa ikipokea mishahara) na kubaini kupokelewa kwa kiasi cha **Sh. 5,000,000** (miamala mitano ya **Sh. 1,000,000**) kutoka Akaunti Na. 20106600444 ya Mfuko wa Kufa na Kuzikana kati ya tarehe 27 Agosti 2018 na 20 Septemba 2019.

### 2.4.4.2 Malipo kwa Watia Saini wa Mfuko Yasiyothibitika Uhalali Wake Sh. 754,654,944

Kupitia ukaguzi ilibainika wakati wa uhakiki kuwa miamala hiyo ya kiasi cha **Sh. 754,654,944** kilicholipwa kwa watia saini hao hakikuwa na nyaraka za malipo hayo kwa wanufaika wala nyaraka za matumizi ya fedha hizo. Kufuatia kukosekana kwa nyaraka, Timu ya Ukaguzi kupitia barua yenye Kumb. Na.CTA.35/364/01D/107 ya tarehe 28/02/2022 ilimuomba Inspekta Jenerali wa Polisi kuwezesha upatikanaji wa watia saini hao wanne ili waweze kueleza matumizi ya kiasi hicho cha fedha walichoidhinisha hundi na kulipwa kwao katika nyakati tofauti.

### 2.4.4.3 Ubadhirifu wa Fedha za Mfuko wa Kufa na Kuzikana Kupitia Akaunti za Wanufaika Sh. 28,200,000

Uhakiki wa taarifa ya kibenki ya akaunti Na. 22606600144 ya Mfuko wa Kufa na Kuzikana ya Mkoa wa Kipolisi wa Kinondoni kwa kipindi kinachoanzia Julai 2018 hadi Novemba 2021 ulibaini kiasi cha **Sh. 28,200,000** kililipwa kwa wanufaika sita kupitia akaunti zao binafsi, hivyo Jeshi la Polisi lilitakiwa kuchukua hatua stahiki dhidi ya Ndg. Erasto Mtweve na kurejesha kiasi cha **Sh. 28,200,000** kutoka kwa wanufaika Ndg. Msanga Juma Rajabu, Joseph Mikongoti, Motomoto Erasto Kilasa, Nyamya Lameck Norbert, Msengi Boniface Martin na Joseph Beda kwa kushiriki katika ubadhirifu wa kiasi hicho.

### 2.4.4.4. Udanganyifu katika Ufufuaji wa Akaunti Na. 22901603799 Mkoa wa Kusini Unguja na kufanyika ubadhirifu wa Sh. 988,450,000

Ukaguzi ulibaini kuwa Hamza Khamis Haji, aliyekuwa Mkaguzi Msaidizi, E.2350 SGT Abdalla Said Abdalla na F.2061 CPL Makame Ismail Mohamed kwa pamoja walishirikiana kufanya udanganyifu katika kuhuisha Akaunti Na. 22901603799 kwa lengo la kuwezesha ubadhirifu huo na kusababisha hasara ya kiasi cha **Sh. 988,450,000** kwa Mfuko wa Kufa na Kuzikana wa Jeshi la Polisi;

### 2.4.4.5 Ubadhirifu wa Fedha Kupitia Akaunti ya Mkoa Kusini Unguja Sh.511,500,000

Ukaguzi ulibaini kiasi cha **Sh. 511,500,000** (**Sh.127,500,000** + **Sh.384,000,000**) kati ya kiasi cha **Sh.576,500,000** kilicholipwa hakikuwafikia walengwa (askari/warithi wa askari aliyefariki) baada ya walipwaji PF. 21751 A/Insp. Hamza Haji na H.6450 PC Suleiman Khamis Mohamed kushindwa kuthibitisha matumizi ya fedha hizo.

### 2.4.4.6 Ubadhirifu wa Fedha Taslimu Sh. 306,000,000 Makao Makuu ya Polisi Zanzibar (PHQ)

Ukaguzi ulibaini, Watia saini na walipaji WP. 9980 SGT Amina Abdalla Ameir, E. 7416 D/SGT Khamis Abdalla Shaka, na PF 18538 Inspekta Ally Hassan Zyuma wanawajibika katika ufujaji wa kiasi

cha **Sh. 306,000,000** kisichothibitika matumizi yake. Hata hivyo, kuhusishwa kwa viongozi waandamizi kuwa walitambua ubadhirifu wa fedha hizo na wao kushiriki, licha ya kutokuwepo ushahidi wa nyaraka, kunathibitisha kuwa sababu za kutokuchukuliwa kwa hatua za kiusimamizi kwa fedha za Mfuko na viongozi hao wakati kiasi kikubwa cha fedha kikifanyiwa ubadhirifu na sehemu ndogo ya kiasi cha **Sh. 94,500,000** kilicholipwa kwa wanufaika kama ilivyopaswa.

**2.4.4.7 Kutumika kwa Fedha za Mfuko wa Kufa na Kuzikana Kinyume na Taratibu Sh. 39,946,000 Mkoa wa Kusini Pemba**

Ukaguzi ulibaini kuwa hakukuwa na maelezo ama ufafanuzi juu ya matumizi ya kiasi cha **Sh. 24,946,000** (Sh.91,284,500 - Sh.51,338,500 - Sh.15,000,000). Kadhalika matumizi ya **Sh. 15,000,000** kwa ajili ya ununuzi wa mafuta ya dizeli hayakubaliki kufanyika kwa fedha za Mfuko wa Kufa na Kuzikana na pia hayakuthibitika kufanyika kwa kuwa hakukuwa na nyaraka za ununuzi wala matumizi ya mafuta hayo. Hivyo, matumizi ya kiasi cha **Sh. 39,946,000** ya fedha za Mfuko hayakubaliki kwa kuwa hayana vielelezo stahili.

**2.4.4.8 Kutoandaliwa kwa Taarifa za Fedha na Kutowasilishwa Katika Mkutano Mkuu wa Mfuko**

Kwa mujibu wa taarifa ya ukaguzi, CP Benedict Wakulyamba, aliyekuwa Mwenyekiti wa Mfuko na Sekretarieti yake hawakutimiza majukumu yaliyoainishwa katika Mwongozo wa Mfuko ikiwemo kupitia taarifa za mapato na matumizi ya Mfuko katika ngazi ya taifa na mikoa na kuwasilisha taarifa hizo kwenye mkutano mkuu wa Mfuko, kuhakikisha Mfuko unaandaa vitabu vya hesabu, na kutunza kumbukumbu muhimu za Mfuko. Kwa ujumla katika vipindi tofauti aliyekuwa Meneja wa Mfuko ASP. Yusta Andrew Mwasanyamba na Insp. Abdalla Bakari Kambini hawakutimiza majukumu yao ikiwemo kushindwa kuhakikisha kuwa Mfuko unaandaa taarifa za fedha, kufunga hesabu za kila mwaka, kuitisha vikao vya Mfuko na mkutano mkuu hali iliyopelekea udhaifu katika usimamizi na kukosekana uwajibikaji katika matumizi ya fedha za Mfuko.

### 2.4.4.9 Kutokaguliwa kwa Mfuko wa Kufa na Kuzikana

Timu ya Ukaguzi ilibaini kuwa Mfuko wa Kufa na Kuzikana haukuwahi kukaguliwa tangu mwaka 2018/19 hadi 2020/21 baada ya kuombwa kuwasilisha taarifa zilizokaguliwa kupitia barua yenye Kumb. Na. CTA.35/364/01D/90 ya tarehe 11 Januari 2022. ASP. Yusta Andrew Mwasanyamba, aliyekuwa Meneja wa Mfuko wa Kufa na Kuzikana kuanzia Julai 2018 hadi Februali 2020 hakuweza kueleza sababu zilizopelekea kutokaguliwa kwa Mfuko.

### 2.4.4.10 Watia Saini Kuwalipa Watu Wasiokuwa Wanachama na Wasiotambulika Jeshini Sh. 179,672,000.

Ukaguzi ulibaini malipo kwa wanufaika wasiotambulika na Jeshi la Polisi ni kama inavyoonekana kwenye Jedwali Na. 2.3 hapa chini:-

**Jedwali Na. 2.3: Malipo kwa Wanufaika wasiotambulika na Jeshi la Polisi**

| Mkoa | Watia Saini husika | Idadi ya miamala | Kiasi |
|---|---|---|---|
| Ilala | Deus John Shija, PF. 17903 INSP. Jane John Mganga, CPL John Kaposwe | 131 | 88,040,000 |
| Kanda Maalumu | Godson Anael Kimambo, G.7322 SGT Said Omary Shekue | 88 | 74,000,000 |
| Kinondoni | Erasto Mtweve, Mahuna Salehe Koshuma, Maridadi Halima Hemed | 37 | 17,632,000 |
| Jumla | 90,202,344,830 | 6.9 | 179,672,000 |

**Chanzo:** ***Taarifa ya Ukaguzi Maalumu wa Mfuko wa Kufa na Kuzikana wa Jeshi la Polisi, Agosti, 2023.***

Kama inavyoonekana hapo juu, wahusika hao 3 walijihusisha na malipo kwa watu wasiokuwa Polisi. Taarifa ya Afisa Masuuli imebainisha kuwa Jane John Mganga, CPL John Kaposwe Erasto Mtweve, Mahuna Salehe Koshuma na Maridadi Halima Hemed walifukuzwa kazi na kesi yao inaendelea katika Mahakama ya Kisutu. Hata hivyo, SGT Deus John Shija alistaafu kazi tarehe 01 /07 /2021 na hadi sasa hajachukuliwa hatua za kisheria.

### 2.4.4.11 Kutorejeshwa Kiasi cha Sh. 759,192,010 za Fedha za Mfuko wa Kufa na Kuzikana Baada ya Kuazimwa na Matumizi ya Kiasi cha Sh. 855,838,668 Kutothibitika

Taarifa ya ukaguzi imebainisha kuwa, ACP Leonard Bonaventura Ngassa, Mkuu wa Fedha wa Jeshi la Polisi alibainisha kuwa Jeshi hilo lilirejesha kiasi cha **Sh. 232,256,508** kati ya kiasi cha **Sh. 991,448,518** kilichoazimwa na Jeshi kutoka Mfuko wa Kufa na Kuzikana. Uhakiki wa vielelezo vilivyowasilishwa ulibaini kuwa kiasi cha **Sh. 759,192,010** hakikuwa kimerejeshwa kama ilivyobainishwa. Hata hivyo, ilibainika kuwa matumizi ya kiasi cha **Sh. 855,838,668** ya fedha zilizoazimwa hayakuthibitika usahihi na uhalali wake kwa kuwa hakukuwa na vielelezo stahili vilivyowasilishwa.

### 2.4.5 Uchambuzi wa Taarifa ya Ukaguzi Maalumu wa Kampuni ya Uendeshaji wa Kiwanja cha Ndege Kilimanjaro (KADCO)

**Mheshimiwa Spika,**ukaguzi huu umefanyika kufuatia Maazimio ya Bunge la 12 Mkutano wa Tisa Kikao cha Pili cha Tarehe 2 Novemba 2022 yaliyotokana na mjadala wa Taarifa ya Kamati ya Hesabu za Serikali (PAC) iliyochambua Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2021, ambapo Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) alizingatia masuala yaliyojitokeza Bungeni yaliyopaswa kuhakikiwa wakati wa ukaguzi.

**Mheshimiwa Spika,** wakati wa mjadala huo, Bunge liliihoji Serikali, pamoja na mambo mengine, kuhusu Uwanja wa Ndege wa Kilimanjaro (KIA) kutokabidhiwa kwa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (TAA) pamoja na uwepo wa maelekezo ya Baraza la Mawaziri kupitia Kikao chake Na. 15 cha mwaka 2009 baada ya ununuzi wa Hisa za Wanahisa Wenza kukamilika. Aidha, Bunge

lilihoji uhalali wa Mkataba wa Uendeshaji (Concession Agreement) kati ya KADCO na Serikali kuendelea baada ya Serikali kununua Hisa za Wanahisa Wenza mwaka 2009, ambapo ufafanuzi ulitolewa kuwa mkataba huo uliendelea kuwa hai licha ya Serikali kununua Hisa zote.

**Mheshimiwa Spika,** kufuatia mjadala huo, Bunge liliazimia kwamba Serikali ifanye tathmini ili kuhamishia shughuli za KADCO kwenye Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (TAA) kama ilivyo kwa viwanja vingine. Vilevile Bunge liliazimia kwamba CAG afanye Ukaguzi wa Kina wa KADCO (Comprehensive Audit).Mnamo tarehe 18 Oktoba, 2023 Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali aliwasilisha Taarifa husika kwa Katibu wa Bunge kwa barua yenye Kumb. Na. CTA.35/364/01H/63.

**Mheshimiwa Spika,** ukaguzi huu maalumu ulihakiki Hisa zilizotolewa kwa Serikali kulingana na mchango wa mali zake kwa Kampuni ya KADCO, ununuzi wa Hisa za Wanahisa Wenza (76%) kuanzia 2009 hadi 2010, ukaguzi ulihakiki mapato na matumizi baada ya Kampuni hiyo kumilikiwa na Serikali kwa asilimia 100 na pia ukaguzi uliangalia utekelezaji wa maelekezo ya Baraza la Mawaziri na Azimio la Bunge.

**Mheshimiwa Spika,** kabla ya kueleza masuala yaliyobainika wakati wa ukaguzi naomba kwanza kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwa ufupi kuhusiana na Kampuni ya KADCO. Kampuni hiyo ilianzishwa tarehe 11 Machi 1998 kufuatia Mkataba wa Makubaliano (MoU) wa tarehe 21 Oktoba 1996 kati ya Serikali ya Tanzania na "Airport Alliance" ambayo ni muunganiko wa Makampuni ya Mott MacDonald LTD, British Airways PLC na Mamlaka ya Anga ya Uingereza (UK Civil Aviation Authority).

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa taarifa ya CAG, Kampuni hiyo ilikuwa na Wanahisa wanne ambao ni Mott MacDonald International Limited (Hisa 41.4%), Inter-Consult Ltd (Hisa 4.6%), Serikali ya Tanzania (Hisa 24%) na South African Infrastructure Fund (Hisa 30%).Serikali na KADCO ziliingia Mkataba wa Uendeshaji (Concession Agreement), Mkataba wa Wanahisa (Shareholders Agreement), na Mkataba wa Upangishaji wa Ardhi na Majengo ya KIA (Lease Agreement). Mikataba hiyo iliingiwa kufuatia uamuzi wa Serikali kupitia Waraka wa Baraza la Mawaziri

Na. 48/1998 wa mwaka 1998 kuwa uendelezaji na uendeshaji wa KIA ufanywe na Kampuni binafsi.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo ya utangulizi, naomba kufafanua masuala mahsusi yaliyobainika kwenye Ukaguzi Maalumu wa KADCO kama ifuatavyo:-

### 2.4.5.1 Mapato Yaliyokusanywa na Matumizi ya KADCO Kati ya Mwaka 2010 Hadi 2022

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya uhakiki wa hesabu za KADCO imebainisha kiasi cha fedha klichokusanywa na kutumiwa na KADCO kati ya mwaka 2010 hadi 2021. Katika kipindi hicho, mapato ya KADCO yalikuwa **Sh.230,781,685,001** na matumizi yalikuwa **Sh. 213,076,786,270**.

### 2.4.5.2 Serikali Kupewa Hisa 379,339 Chini ya kiwango na Thamani ya Mali ilizochangia

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya ukaguzi imebaini kuwa mnamo Novemba 1998 wanahisa Mott MacDonald International Limited na Iter-Consult Limited walipewa hisa 649,085 na 72,130 mtawalia kwa bei ya Sh. 1,352 kwa kila hisa. Vilevile, mnamo Mwezi Agosti 1999, Serikali ya Tanzania ilipatiwa jumla ya Hisa 378,251 (sawa na 24%) za KADCO kwa bei ya Sh. 2,711 kwa kila Hisa baada ya kuchangia mali zake zilizopo katika Taarifa ya Uthamini wa Mali na Hesabu za mwaka unaoishia tarehe 31 Disemba 1999 kuwa na thamani ya jumla ya Sh. 1,020,205,394.

**Mheshimiwa Spika,** mali hizo ni pamoja na Magari 15, Samani za Ofisini 1,050, Mtambo wa kudhibiti moto (firetender) 1, ‘ground handling equipment’ 2, vifaa kwa ajili ya karakana ya uhandisi 15, ‘observation accessories’ 48, na mashine mbalimbali 43. Kulingana na thamani ya mali zake, Serikali ingepata jumla ya Hisa 754,590 endapo bei ya Sh. 1,352 kwa kila hisa ambayo ilitumika kwa Wanahisa wengine (Mott MacDonald International Limited na Iter-Consult Limited) pia ingetumika kwa Serikali. Kwa msingi huo, idadi ya Hisa zilizotolewa kwa Serikali zilikuwa pungufu kwa Hisa 376,339 (754,590-378,251).

**Mheshimiwa Spika,** Vilevile CAG alibaini hoja muhimu katika eneo hili kwamba, uthamini wa mali ulifanywa na Kampuni ya H&R Consult Ltd ya Dar es Salaam ikishirikiana na WT Partnership (bila ushirikishwaji wa Serikali). Wathamini hao waliteuliwa na KADCO. Hivyo, kwa kuwa wathamini hao walichaguliwa na KADCO kuna uwezekano wa kuwa walilinda maslahi ya KADCO na siyo ya Serikali.

**2.4.5.3 Kuendelea Kuendesha na Kusimamia KIA Chini ya KADCO Kinyume na Azimio la Bunge na Maelekezo ya Baraza la Mawaziri**

Mheshimiwa Spika, Baraza la Mawaziri kupitia Mkutano wake Na. 5/2009 wa tarehe 14 Mei 2009 lilielekeza kwamba, baada ya ununuzi wa Hisa za Wanahisa wengine, shughuli za uendeshaji wa KIA ziwe chini ya TAA katika kipindi ambacho Serikali inatafuta Mwekezaji mahiri wa kuendeleza na kuendesha KIA. Vilevile, Bunge la 12 kupitia Mkutano wake wa Tisa katika Kikao cha Pili cha tarehe 2 Novemba 2022 liliazimia kuwa shughuli zote za KIA ziwe chini ya TAA.

**Mheshimiwa Spika,** hadi wakati wa ukaguzi huu Mwezi Septemba 2023, shughuli za uendeshaji wa KIA zimeendelea kusimamiwa na KADCO kinyume na maagizo ya Baraza la Mawaziri na maazimio ya Bunge.

**Mheshimiwa Spika,** Ndg. Gabriel J. Migire, aliyekuwa Katibu Mkuu Uchukuzi kupitia barua yake ya 02 Juni, 2022 yenye Kumb. Na. 26/318/01/103 aliomba ushauri wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuhusu jitihada za Serikali kuandaa Sheria ya TAA ambayo pamoja na mambo mengine, itaweka utaratibu wa kisheria wa uendeshaji wa Viwanja vyote vya Ndege vya Serikali Nchini ikiwemo KIA.

**Mheshimiwa Spika,** akitoa ushauri wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ndugu Hassan Nkya kwa niaba ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali alifafanuwa kwamba Sheria iliyopo ( The Executive Agencies Act, CAP 245 establishing TAA of 1990)inatoa mamlaka kwa TAA kuendesha na kuendeleza viwanja vya ndege ya umma.Naomba kunukuu sehemu ya maelezo ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kama ifuatavyo:-

**Nukuu:-**

***" …The Executive Agencies Act, CAP 245 establishing TAA of 1999, empowers TAA to manage, operate and develop publicly owned airports. He farther opined that proposed legislation should not focus on establishing a new institution for managing , operating , and developing airport, but continuing the TAA under the legislation…"***

**Mwisho wa Nukuu.**

**Mheshimiwa Spika,** kwa msingi wa nukuu hapo juu, maelezo ya aliyekuwa Katibu Mkuu, Uchukuzi yanapingana na ushauri wa kisheria wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika hoja hii. Ushauri wa kisheria uliotolewa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ulibainisha kwamba TAA ina mamlaka kisheria[19] ya kusimamia shughuli za Viwanja vya Ndege Nchini hivyo kurejeshwa kwa usimamizi wa shughuli za KIA kwa Mamlaka hiyo kunaendana na matakwa ya kisheria na hakuzuii hatua ya Serikali ya uandaaji wa Sheria ya TAA.

### 2.4.5.4 KADCO Imepata hasara ya Sh. 794,012,858 na Dola za Marekani 388,380.32

**Mheshimiwa Spika**, hoja nyingine iliyobainika katika Ukaguzi Maalumu ilihusu uhakiki wa mapato. Katika uhakiki huo ilibainika kuwa jumla ya kiasi cha Sh. 502,807,857.52 na Dola za Marekani 388,380.32 hakikusanywa kutokana na sababu mbalimbali.Fedha hizo zinajumuisha makundi yafuatayo; kodi za pango za nyumba na maeneo ya biashara (Sh. 218,771,559.90 na USD 388,380.32), kutokusanywa ada za malipo ya huduma za Jengo la Watu Mashuhuri (Sh. 131,600,000) na kutokusanywa kwa fedha za kuchelewa kulipa malipo yatokanayo na ada za maegesho ya magari (Sh. 152,436,297.62).

[19] Rejea Order 3 of Schedule 3.2 of the Executive Agencies ( Tanzania Airports Authority) (Establishment Order) Vide GN. No. 404 of 1999

**Mheshimiwa Spika,** katika eneo hili CAG alibaini pia KADCO imepata hasara ya kiasi cha Sh. 291,2015,000 kutokana na kufanya malipo zaidi ya kiasi kilichostahili kwa watoa huduma. Hasara iliyotokana na malipo kwa watoa huduma hao ni kama ifuatavyo:-

a) M/s Transkim Networking Ltd **(Sh. 249,465,000)**;

b) M/s Arusha Region Express Services Cooperative Society **(Sh. 16,000,000)**; na

c) M/s Lulu Cleaning Services **( Sh. 25,740,000)**.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mara ya kwanza Kamati ilipanga kukutana na Uongozi wa KADCO, TR na Wizara ya Uchukuzi ili kujadili Taarifa ya Ukaguzi huu Maalumu siku ya tarehe 24 Oktoba, 2023. Hata hivyo baada ya kupitia na kuchambua uzito wa hoja za ukaguzi na utekelezaji wake, Kamati iliamua kusogeza mbele kikao cha kujadili taarifa hiyo siku ya ijumaa tarehe 27 Agosti, 2023.Lengo la kusogeza mbele kikao husika ilikuwa kutoa fursa kwa Katibu Mkuu Wizara ya Uchukuzi ambaye ni Afisa Masuuli wa Wizara kufika mbele ya Kamati kwa mahojiano ya kina.

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na udhuru wa Afisa Masuuli aliowasilisha kwa Katibu wa Bunge, Kamati ilikutana na Afisa Masuuli Uchukuzi siku ya tarehe 30 Oktoba , 2023. Afisa Masuuli alikuwa ameambatana na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Maafisa wa Ofisi ya Msajili wa Hazina na Menejimenti ya KADCO.

**Mheshimiwa Spika,** Afisa Masuuli Uchukuzi alitoa maelezo kwamba uhamishaji wa shughuli za KADCO kwenda TAA umekuwa na changamoto za kisheria. Aliifahamisha Kamati kuwa baada ya Serikali kununua hisa asilimia 100, kulikuwa bado na mikataba ya ukodishaji wa uendeshaji wa uwanja ambayo ilikuwa inasubiri kukamilika.

**Mheshimiwa Spika,** Mwanasheria Mkuu wa Serikali aliifahamisha Kamati kuwa Serikali inaendelea na mchakato wa kukamilisha uhamishaji wa shughuli za KADCO kwenda TAA. Kuna masuala waliona ni muhimu yashughulikiwe kwanza ikiwa ni pamoja na

kukamilisha uhamishaji wa hisa zote za KADCO kwenda Serikalini. Aidha kulikuwa na hoja ya kuangalia masuala ya watumishi waliokuwa KADCO ambayo ilikuwa ni Kampuni binafsi iliyosajiliwa chini ya Sheria ya Makampuni kwenda Serikalini.

**Mheshimiwa Spika,** kamati ina maoni kuwa hoja hii kutokamilika miaka 14 baada ya kutolewa kwa maelekezo ya Baraza la Mawaziri na takribani mwaka 1 baada ya Azimio la Bunge, ni dhahiri hoja hii haijafanyiwa kazi ipasavyo.Mathalani Kamati haikuona msingi wa kuchelewa kutekeleza agizo hilo kwa sababu ya hoja ya kuangalia masuala ya watumishi. Kwa mfano Serikali haikuchukua muda mrefu kuunganisha Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ( LAPF, GEPF na PSPF), hivyo hoja hiyo haikukubaliwa na Kamati.Vilvile hoja ya kumalizika kwa 'concession agreement' tangu tarehe 16 Julai, 2023 haikupata majibu ya kutosha toka kwa Afisa Masuuli na kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

### 2.5 Uchambuzi wa Taarifa ya Matumizi ya Fedha za Mkopo wa Uviko 19 Zilizotolewa na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF)

**Mheshimiwa Spika,** Tanzania ni kati ya Nchi zilizoathiriwa na janga la UVIKO -19 na kusababisha madhara hasi kwenye ukuaji wa uchumi na kijamii. Kutokana na matokeo hayo, Serikali iliandaa Mpango kukabiliana na athari hizo unaoangazia sekta za afya, elimu, maji, utalii, ustawi wa jamii, nishati na uwezeshaji wa kiuchumi kwa pande zote mbili za Tanzania Bara na Zanzibar. Gharama iliyokadiriwa kwaajili ya kutekeleza mpango huo ilikuwa **Sh. trilioni 3.62**.

**Mheshimiwa Spika,** mnamo tarehe 7 Septemba 2021, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilisaini mkopo wa masharti nafuu wa dola za Marekani 567.3 milioni (sawa na **Sh. bilioni 1,310.65**) kutoka kwa Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) ili kutekeleza Mpango wa kukabiliana na athari za Kijamii na Kiuchumi zitokanazo na UVIKO-19 (TCRP). Jumla ya **Dola za Marekani 567.3 milioni** (sawa na **Sh. bilioni 1,291.74**) zilipokelewa na Wizara ya Fedha mnamo Septemba na Desemba 2021. Utofauti unaonekana kwenye shilingi ni athari ya mabadilishano ya fedha (exchange rate) kati ya Shilingi na dola. Fedha hizi ziligawanywa kama inavyoonekana kwenye Jedwali Na. 2.4 hapa chini:-

**Jedwali Na. 2. 4: Mchanganuo wa Mgawanyo wa Fedha za Uviko**

| Sekta | Kiasi | Asilimia | Taasisi |
|---|---|---|---|
| Afya | 448,790,341,197 | 34.7 | MoH & PO - RALG |
| Elimu | 372,370,603,626 | 28.8 | MoST & PO- RALG |
| Maji | 139,354,573,798 | 10.79 | MoW |
| Maliasili na Utalii | 90,202,344,830 | 6.9 | MoNRT |
| Hifadhi ya Jamii | 5,542,514,000 | 0.4 | TASAF |
| Uwezeshaji Vijana, Wanawake na Wenye ulemavu | 5,000,000,000 | 0.39 | PO -RALG |
| Usimamizi na Ufuatiliaji | 297,800,000 | 0.02 | MoFP |
| Zanzibar | 230,184,478,249 | 17.8 | RGoZ |
| Jumla | 1,273,845,988,662 | 100 | |

**Chanzo:** ***Taarifa ya CAG kuhusu ukaguzi wa matumizi ya fedha za Uviko, Agosti, 2023.***

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa uhakiki uliofanyika na CAG hadi kufikia tarehe 25 Agosti, 2023, Wizara ya Fedha ilikuwa imetoa kiasi cha **Sh. trilioni 1.273** (98.61%) kwenda kwenye utekelezaji wa miradi katika sekta zilizopewa kipaumbele. Kwa msingi huo, kulikuwa na salio la **Sh. bilioni 17.896** (1.39%). Fedha zilizobaki kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali ni **Sh. bilioni 17.472** kwa ajili ya TAMISEMI zilizotengwa kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba na **Sh. milioni 424.12** kwa ajili ya Wizara ya Elimu kwa lengo la ujenzi wa miundombinu ya elimu.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilikutana kwa mara ya kwanza na Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG) siku ya tarehe 10 Agosti, 2023 kwa

ajili ya kupitia na kuchambua matokeo ya ukaguzi huu Maalumu. Mlipaji Mkuu wa Serikali alikuwa ameambatana na Maafisa Masuuli kutoka katika sekta mbalimbali zilizotengewa fedha na kutekeleza miradi.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya majadiliano, Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG) aliomba kwamba, Serikali ipatiwe muda wa ziada kuwasilisha baaadhi ya majibu na vielelezo ambavyo kwa tarehe husika vilikuwa haivijawasilishwa na kuhakikiwa na CAG hivyo kutotoa taarifa sahihi za hali halisi ya utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi hadi kufikia siku ya kikao cha Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia ombi la Mlipaji Mkuu wa Serikali, Kamati iliona ni busara kutoa muda zaidi kwa Serikali kuwasilisha majibu ya mapendekezo ya ukaguzi kwa CAG kwa uhakiki. Uamuzi wa Kamati ulizingatia ukweli kwamba fedha husika za mkopo zilitumika kutekeleza miradi katika sekta mbalimbali ikiwamo afya, elimu, uwezeshaji wananchi kiuchumi na mamlaka za Serikali za Mitaa.CAG alikamilisha uhakiki wa majibu ya hoja za ukaguzi na kuwasilisha taarifa ya uhakiki wa hoja kwa Kamati tarehe 29 Septemba, 2023.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kulifahamisha Bunge lako Tukufu hoja zilizobainika katika Ukaguzi huo Maalumu na ambazo hadi tarehe 29 Septemba, 2023 zilikuwa hazijajibiwa ipasavyo. Hoja hizo ni kama ifuatavyo: -

### 2.5.1 Wazabuni Kutowasilisha kwa Wakati Vifaa Tiba Vyenye Thamani ya Sh. bilioni 17.92

**Mheshimiwa Spika,** Ukaguzi ulibaini kuwa wazabuni walishindwa kuwasilisha kwa wakati vifaa tiba vyenye thamani ya jumla ya **Sh. bilioni 17.92** vilivyokuwa vimelipiwa na Hospitali 21 licha ya kumalizika kwa kipindi cha mkataba wa usambazaji wa vifaa tiba katika hospitali hizo.

**Mheshimiwa Spika,** hadi wakati wa ukaguzi huo mwezi Novemba, 2022 Menejimenti ya Hospitali hizo hazikuwa zimechukua hatua stahiki kulingana na Kanuni ya 242 (2) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2013.

### 2.5.2 Wazabuni Kutowasilisha Magari Yenye Thamani ya Sh. bilioni 18.85

**Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Afya ilifanya malipo ya **Sh. 8,098,433,520** kwa mzabuni Toyota Tanzania Limited kwa ajili ya ununuzi wa magari 28 kati ya magari hayo magari 20 yalikuwa magari ya wagonjwa na magari 8 yalikuwa magari ya kukusanyia damu. Hadi wakati wa ukaguzi huu mzabuni huyo alikuwa hajawasilisha magari hayo.

**Mheshimiwa Spika,** katika hoja hii CAG alibaini kuwa Wizara ya Afya ilifanya malipo ya **Sh. 10,751,084,251** kwa mzabuni UNICEF kwa ajili ya ununuzi wa magari 125 na pikipiki 10 hadi wakati wa ukaguzi huu mzabuni UNICEF alikuwa hajawasilisha magari hayo.

### 2.5.3 Vifaa Tiba Vyenye Thamani ya Sh. bilioni 14.81 Kutoanza Kutumika

**Mheshimiwa Spika,** Hospitali Tisa (9) za Rufaa za Mkoa (RRH) na Hospitali Nne (4) za Rufaa za Kikanda zilinunua vifaa mbalimbali vya matibabu vyenye thamani ya **Sh. bilioni 14.81** ; lakini vifaa hivyo havikutumiwa hadi wakati wa ukaguzi huu mnamo mwezi Novemba 2022 kutokana na kutokamilika kwa majengo ya radiolojia, EMD na ICU.

**Mheshimiwa Spika,** majibu ya Serikali katika hoja hii yalifafanua kwamba, Vifaa vya matibabu vimewekwa na vimeanza kutoa huduma katika hospitali za mikoa ya Tanga, Tabora, Mawenzi, Geita, Simiyu, Chato, Mtwara, Bugando Medical Centre na Benjamin Mkapa. Aidha, matumizi ya idara za dharura zenye thamani ya **Sh.1,735,656,595.00** katika hospitali za mikoa ya Katavi, Ligula na Singida zinatarajiwa kuanza hivi karibuni baada ya kukamilika kwa ujenzi, ambapo Wizara imepokea jumla ya **Sh. 3,662,194,566.18** tarehe 26 Julai, 2023 kutoka Wizara ya Fedha.

**Mheshimiwa Spika,** hata hivyo, hoja ya ukaguzi inabaki kuwa baadhi ya vifaa tiba havijaanza kutumika hivyo kutokuwepo na thamani ya fedha ya umma kwa manunuzi yaliyofanyika.

### 2.5.4 Majengo ya Hospitali Yenye Thamani ya Sh. milioni 291.18 Kutoanza Kutumika

**Mheshimiwa Spika,** taarifa ya ukaguzi ilibaini kwamba, majengo manne (4) ya hospitali yaliyokamilika yenye thamani ya **Sh. milioni 291.18** yalikuwa hayatumiki hadi kufikia Novemba 2022, licha ya kukamilika, kutokana na sababu mbalimbali, ikiwa ni pamoja na ukosefu wa vifaa vya TEHAMA kwa ajili ya vyumba vya matibabu na vifaa tiba vya Idara ya Dharura (EMD).

**Mheshimiwa Spika,** mchanganuo wa majengo hayo ambayo yalikuwa hayajaanza kufanya kazi na thamani yake umefafanuliwa katika Jedwali Na.2.5 hapa chini.

**Jedwali Na. 2. 5: Orodha ya Majengo yaliyokamilika ila Hayajaanza Kutoa Huduma**

| Hospitali | Majengo | Tahamani |
|---|---|---|
| Tanga RRH | EMD | 100,000,000 |
| Tabora RRH | Telemedicine Room | 100,000,000 |
| Katavi RRH | Staff House | 60,441,500 |
| Simiyu RRH | Telemedicine Room | 30,736,000 |
| **Jumla** | | **291,700,500** |

**Chanzo:** ***Taarifa ya CAG Kuhusu Ukaguzi wa Fedha za Uviko, Septemba, 2023.***

**Mheshimiwa Spika**, majibu ya Wizara ya Afya katika hoja hii ni kwamba, EMD katika Hospitali ya Mkoa wa Tanga na nyumba ya wafanyakazi katika Hospitali ya Mkoa wa Katavi zimeanza kutoa huduma zilizokusudiwa.Kwa kuwa vifaa vya ICT vimetolewa na vimewekwa katika Hospitali za Rufaa za Mikoa, Wizara imewasiliana na Taasisi ya Sayansi na Teknolojia (DIT) kutathmini utayari wa Hospitali hizo ikiwemo Tabora na Simiyu kuanza kutoa huduma za "telemedicine" (Rejea barua yenye Kumb. No. GA.138/143/02/21 tarehe 07/09/2023).

**Mheshimiwa Spika,** hata hivyo, hoja ya msingi ya Kamati inabaki kwamba, uwepo wa baadhi ya majengo yaliyojengwa kwa fedha za umma na kutotumika kwa kipindi kirefu tangu

kukamilika kwake ni matumizi yasiyokuwa na tija ya fedha za umma.

### 2.5.5 Uhamishaji wa Fedha za Ujenzi Kutokana na Upungufu wa Ardhi katika Shule za Dar es Salaam Shilingi Milioni 920

**Mheshimiwa Spika,** katika fedha zilizoelekezwa kwenye eneo la elimu, hoja ya kwanza ya ukaguzi ilihusu uhamishaji wa fedha za ujenzi kutokana na upungufu wa ardhi katika shule za Mkoa wa Dar es Salaam kiasi cha **Sh. milioni 920**. Mathalani ukaguzi ulibaini katika Halmashauri ya Manispaa ya Temeke, fedha zilizotengwa awali kwa madhumuni ya ujenzi zilihamishiwa shule nyingine kutokana na kikwazo cha ufinyu wa nafasi kwa ujenzi wa madarasa. Mpango wa awali ulihusisha ujenzi wa madarasa 44, lakini baadaye, madarasa 39 yalihamishiwa sehemu nyingine hivyo kusababisha jumla ya uhamishaji wa **Shilingi milioni 720.**

**Mheshimiwa Spika,** katika Halmshauri ya Manispaa ya Kinondoni, fedha zilihamishiwa shule tofauti ndani ya eneo la Manispaa, kutokana na vikwazo vya upatikanaji wa ardhi kwa ujenzi wa madarasa. Kwa mfano, katika mpango wa awali wa mradi, madarasa 146 yalikuwa yamekusudiwa, lakini kati ya hayo, madarasa 10 yalishindwa kujengwa hivyo fedha kuhamishiwa kwenye shule nyingine, ikifikia jumla ya **Shilingi milioni 200**.

**Mheshimiwa Spika,** hoja ya Kamati katika eneo hili inajengwa kwenye msingi kwamba pamoja na uhamishaji wa fedha kuwa ni kwenda katika shule ndani ya manispaa husika, kuna mashaka juu ya usawa wa mahitaji ya madarasa kwa wanafunzi kati ya shule zilizopangwa upya na zile zilizokusudiwa awali.Kwa mfano, uhamishaji wa fedha kwenda Shule ya Sekondari Michael Tarimo na Baraza kwa ujenzi wa madarasa 10, licha ya shule tayari kujenga madarasa 15 kwa kutumia rasilimali zake, ulisababisha jumla ya madarasa 25 kuwepo, wakati shule ilikuwa na wanafunzi 150 pekee, wanaotumia madarasa matatu pekee, na kusababisha madarasa zaidi ya 20 kutotumiwa.

### 2.5.6 Migongano ya Maslahi Katika Ununuzi wa Vifaa vya Ujenzi kwa Shilingi Milioni 517.58

**Mheshimiwa Spika,** ukaguzi maalumu ulibaini kwamba Halmashauri tano (5) zilinunua vifaa vyenye thamani ya **Shilingi milioni 517.58** kutoka kwa watu binafsi ambao walikuwa ni wafanyakazi au wanafamilia wa wafanyakazi wa Halmashauri, kinyume cha Kanuni ya 7 (4) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma za Mwaka 2013. Orodha ya Halmashauri zilizofanya manunuzi yenye mgongano wa Maslahi imefafanuliwa katika Jedwali Na.2.6 hapa chini:-

**Jedwali Na. 2.6: Orodha ya Halmashauri zilizofanya manunuzi yenye asili ya mgongano wa kimaslahi**

| Na. | Halmashauri | Thamani |
|---|---|---|
| 1. | Geita DC | 361,576,867 |
| 2. | Uyui DC | 72,899,750 |
| 3. | Mapanda DC | 54,821,543 |
| 4. | Kasulu DC | 22,414,500 |
| 5. | Songea MC | 5,867,260 |
| **Jumla** | | **517,599,920** |

**Chanzo:** ***Taarifa ya Ukaguzi Maalumu wa Fedha za Uviko, Septemba, 2023.***

**Mheshimiwa Spika,** kama jedwali hapo juu linavyobainisha, Halmashauri tano zilikiuka Sheria ya Ununuzi wa Umma na Kanuni zake. Aidha CAG alipendekeza hatua za kisheria zichukuliwe kwa wahusika. Majibu ya Serikali yameeleza kuwa tarehe 02 Agosti, 2023 Makatibu Tawala wa Mikoa ya Halmshauri husika waliandikiwa barua kuchukua hatua stahiki dhidi ya watumishi wote waliohusika katika ukiukwaji huo wa taratibu za manunuzi.

**Mheshimiwa Spika,** CAG katika uhakiki aliofanya mwezi Septemba, 2023, ameifahamisha Kamati kuwa, Halmashauri husika zimechukua hatua ambapo watumishi waliofanya kosa hilo waliandikiwa barua za onyo. Hata hivyo, Kamati ina maoni kuwa barua za onyo hazitoshi kama adhabu kwa watumishi

wanaohusika na ubadhirifu wa fedha za umma. Hivyo, hatua kali zaidi za kiuwajibikaji zinatakiwa kuchukuliwa kwa wahusika.

### 2.5.7 Malori 10 yenye thamani ya Sh.bilioni 2.20 yaliyowasilishwa yakiwa na uwezo wa nguvu ya injini (Horse Power) tofauti na makubaliano ya mkataba

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Sekta ya Maji, hoja ya kwanza ya ukaguzi ilihusu kuwasilishwa malori 10 yenye thamani ya **Sh. bilioni 2.20** yakiwa na uwezo wa nguvu ya injini (Horse Power) tofauti na makubaliano ya mkataba.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa wa sehemu ya 5 (engine) ya maelezo ya kiufundi ya malori kwa mkataba namba ME-011/2021-2022/contract/G/09 Lot 1 kwa ajili ya kusambaza vifaa vya ujenzi wa mabwawa ikiwa ni malori 10 yenye thamani ya **Sh.2.20 bilioni** ambayo yalitaka malori husika kuwa na injini ya dizeli yenye sifa zifuatazo; ***"4 strokes, six cylinders, and water-cooled, turbo charged, intercooled, and developing 300-360 HP"***. Hata hivyo, kinyume chake, malori 10 yaliyowasilishwa yalikuwa na uwezo wa HP 335 badala ya HP 340 kama ilivyotolewa na muuzaji wakati wa zabuni.

**Mheshimiwa Spika,** katika hoja hii, Wizara ya Maji ilijibu kwamba malori yaliyoletwa yana uwezo wa HP 340. Hata hivyo, hadi tunawasilisha taarifa hii hapa Bungeni, CAG kwa niaba ya Bunge hajafanya uhakiki kuthibitisha nguvu ya injini za malori hayo kuwa na HP 340 kama ambavyo Wizara ya Maji imewasilisha majibu. Kwa msingi huo, Kamati bado ina mashaka iwapo malori husika yalikidhi vigezo na kwa kuwa hoja haijafungwa ni vema Bunge lako Tukufu likaifahamu na kuchukua hatua stahiki.

### 2.5.8 Kutokufanyika kwa upembuzi yakinifu kwa miradi ya maji yenye thamani ya Sh. bilioni 1.16

**Mheshimiwa Spika,** Kifungu cha 1.4.2 cha Mwongozo wa Usanifu wa Maji cha mwaka 2009 kinaitaka Taasisi inayotekeleza mradi, wakati wa hatua ya upangaji wa mradi, pamoja na mambo mengine kufanya upembuzi yakinifu, ili kuwa na taarifa zinazojitosheleza kubaini na kutambua kama kuna faida na

athari zinazoweza kutokea kwa kutekeleza mradi katika jamii na athari katika mazingira kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika,** ukaguzi maalumu ulibaini kuwa, Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira mjini Moshi ilitekeleza Mradi wa Usambazaji Maji katika Kata ya Kimochi wenye thamani ya **Sh.milioni 500** (ambayo ilikuwa ni kwa ajili ya upanuzi wa mtandao wa maji uliokuwepo ambao ulijengwa miaka ya 1970) bila kufanya upembuzi yakinifu. Vilevile, ukaguzi ulibaini kuwa hakuna upembuzi yakinifu uliofanyika kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa maji wa Njoro II wenye thamani ya **Sh.667 milioni** ambao ulitekelezwa na RUWASA Mkoani Kilimanjaro.

**Mheshimiwa Spika,** kutofanyika upembuzi yakinifu huongeza hatari ya kukosa fursa za kutambua na kupunguza hatari zinazoweza kutokea kwa mradi na jamii na kutokuwa na uhakika katika miradi ya ujenzi. Wizara ya Maji inatakiwa kutoa majibu ya hoja hii.

### 2.5.9 Uwasilishaji wa hati fungani ya utendaji kazi ambayo haikukidhi matakwa ya kimkataba ya mradi wenye thamani ya Sh. milioni 415

**Mheshimiwa Spika,** Kifungu cha 9.1 cha matakwa maalum ya mkataba Na.AE/029/2021-22/G-49 kati ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Arusha Mjini na Mzabuni, kwa ajili ya usambazaji wa mabomba kwa lengo la uboreshaji wa Mifumo ya usambazaji wa maji katika Mifumo ya Usambazaji Maji ilioko Pembezoni na mijini ikijumuisha maeneo ya Jiji la Arusha, ikiwa na thamani ya **Sh.415 milioni** ulihitaji dhamana ya benki au dhamana ya utendaji kazi kuwa 10% ya Bei ya Mkataba.

**Mheshimiwa Spika,** ukaguzi ulibaini kuwa, hati fungani iliyowasilishwa na mzabuni ikiwa ni dhamana ya utendaji kazi ilikuwa na jumla ya **Sh. milioni 20.76**. Kiasi hiki kilikuwa ni sawa na 5% tu ya jumla ya mkataba. Athari ya kuwasilisha dhamana ya utendaji kazi ambayo sio sahihi ni pamoja na kuinyima Serikali fursa ya kupata nafuu ya kifedha iwapo mzabuni atashindwa kutekeleza wajibu wake. Vilevile suala hili linadhihirisha mapungufu katika usimamizi wa miradi.

### 2.5.10 Kuchelewa kuanza na kukamilika kwa ujenzi wa maeneo ya biashara kwa wafanyabiashara wadogo licha ya kupokelewa Kwa fedha na Halmashauri husika

**Mheshimiwa Spika,** katika eneo la uwezeshwaji wa kiuchumi na kijamii, ukaguzi ulibaini kuwa Halmashauri kadhaa zilipokea fedha kwa lengo la kusaidia wafanyabiashara wadogo waliokumbwa na athari kubwa za janga la UVIKO -19. Hata hivyo, ujenzi huo ulikuwa ukiendelea mpaka sasa (25 Agosti 2023) huku maeneo mengine ujenzi ukiwa haujaanza kabisa, licha ya kutengwa kwa fedha.

**Mheshimiwa Spika,** Halmashauri ya Jiji la Mbeya ilipewa kiasi cha **Shilingi milioni 541,** hata hivyo, mradi ulioko eneo la Uwanja wa Ndege wa Zamani bado unaendelea, huku ukiwa na kasoro kama vile Mfereji wa maji ya mvua (canal) umekamilika kwa asilimia 50, Vibati vya chuma vya mifereji havijasakinishwa kwenye Banda Kuu, ambalo lilikuwa limetengwa kwa ajili ya wafanyabiashara wadogo, Ofisi ya Wafanyabiashara wadogo na choo chake kiko hatua ya mwisho, lakini baadhi ya sehemu bado hazijakamilika, ikiwa ni pamoja na madirisha, sakafu na ufungaji wa umeme, na upakaji rangi.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Halmashauri ya Jiji la Tanga, Licha ya kupokea kiasi cha **Shilingi milioni 540**, ujenzi bado haujaanza. Kizuizi kikubwa kikiwa ni eneo lililotengwa kwa mradi (Bondeni City) kuwa katika mgogoro na mmiliki wake. Kwa upande wa Jiji la Arusha, ilipokea kiasi cha **Shilingi milioni 500** kwa ajili ya mradi. Hata hivyo, hadi kufikia wakati wa ukaguzi (25 Agosti 2023), eneo ambalo mradi ungejengwa halikuwa limethibitishwa bado kutokana na kutokuweo kwa hati miliki. Fedha zilizotengwa kwa sasa zimehifadhiwa kwenye akaunti ya amana yenye jina la "Machinga" ikiwa na kiasi chote cha **Sh. milioni 500**.

**Mheshimiwa Spika,** hoja ya msingi ya Kamati katika eneo hili la uwezeshaji wananchi kiuchumi ni kwamba, kutokukamilika kwa wakati kwa miradi hii kunaonyesha changamoto kubwa katika kupanga na kutekeleza miradi ya maendeleo, hali inayopelekea dhima ya miradi husika katika kuwawezesha kiuchumi wafanyabiashara wadogo walioathirika na janga la UVIKO

kushindwa kutimia. Hii ni sambamba na Serikali na wananchi kutopata thamani halisi ya kifedha ya mkopo uliochukuliwa.

### 2.6 Mapitio ya Kaguzi Katika Mifuko ya Hifadhi ya Jamii

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipata fursa ya kupitia na kuchambua taarifa ya Hesabu za Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Mifuko hiyo ni Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) na Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma (PSSSF).

**Mheshimiwa Spika,** umuhimu wa kufanya uchambuzi mahsusi wa hesabu za Mifuko ya Hifadhi ya Jamii unatokana na ukweli kwamba, Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ina thamani kubwa ya fedha za umma zilizowekezwa katika eneo hilo. Mathalani hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2022, thamani ya Mfuko wa NSSF na PSSSF ukiondoa madeni zilifikia **Sh.6,079,579,648,000**[20]. Huu ni uwekezaji mkubwa ambao lazima Bunge lipate fursa ya kufuatilia fedha za umma zilizowekezwa katika Mifuko hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kulifahamisha Bunge lako Tukufu matokeo ya uchambuzi wa taarifa za ukaguzi wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kama ifuatavyo:-

#### 2.6.1 Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF)

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati katika taarifa za Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), ulibainisha hoja kadhaa za ukaguzi kama ifuatavyo:-

##### 2.6.1.1 Uwepo wa Mikopo ya Muda Mrefu Ambayo Haijakusanywa

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2022 NSSF ilikuwa inadai Taasisi mbalimbali za Serikali kiasi cha **Sh. bilioni 1,174**,kiasi hicho kinachohusisha deni la msingi na riba.Deni hili ni malimbikizo ya tangu mwaka 2008 hadi 2022 (mwaka 1 hadi miaka 15).

[20] Rejea Uchambuzi wa Kamati kwenye Hesabu Zilizokaguliwa za NSSF na PSSSF zinazoishia 30 Juni, 2022

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi zaidi wa Kamati umebainisha kwamba, hadi kufikia tarehe 12 Oktoba, 2023 deni la Serikali ambalo limehakikiwa na Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali linafikia **Sh. 493,597,125,507.20** kati ya kiasi cha deni la **Sh. 557,324,040,155.54** kilichowasilishwa Serikalini kwa uhakiki. Deni hilo linajumusiha 85% ya dhamana ambayo Serikali ilitoa kwa Kampuni ya General Tyre East Africa (GTEA) sawa na **Sh. 19,799,475,000.00** na kiasi kingine cha **Sh. 106,546,631,137.63** inayohusu ujenzi wa daraja la Nyerere.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilifahamishwa kuwa kupitia barua ya Katibu Mkuu Hazina ya tarehe 27 Septemba, 2023 yenye Kumb. Na. CJA.374/547/01B alitakiwa kuandaa kikao cha ngazi ya juu ambacho kilitakiwa kufanyika tarehe 06 Oktoba, 2023 ili kujadiliana namna bora ya malipo ya deni husika.

**Mheshimiwa Spika,** hadi tunapowasilisha taarifa ya Kamati leo hii ndani ya Bunge lako Tukufu, bado utaratibu wa kulipa deni husika haujatolewa na hivyo deni linabaki palepale hivyo kuendelea kuathiri mizania ya hesabu za NSSF.

**2.6.1.2 Michango ya Wanachama Ambayo Haijakusanywa Sh. bilioni 408**

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati katika taarifa ya hesabu zilizokaguliwa za NSSF ulibaini ongezeko la michango isiyokusanywa ambayo inaathiri hali ya ukwasi ya Mfuko katika kutimiza majukumu yake. Hadi kukamilika kwa mwaka wa fedha 2020/2021 jumla ya kiasi cha **Sh. bilioni 408** kilikuwa ni michango ambayo inadaiwa kutoka kwa waajiri na wanachama.

**Mheshimiwa Spika,** Mfuko uliunda Timu Maalumu za kufuatilia ulipaji wa michango husika. Hatua za ukusanyaji zilihusisha uingiaji wa makubaliano maalumu ya malipo ili kupunguza madeni husika. Kwa jitihada hizo, kiasi cha **Sh. 194,224,567,487.29** kilifanikiwa kukusanywa kati ya kipindi cha Oktoba 2022 na Juni, 2023.Hata hivyo, bado kuna kiasi kikubwa cha michango ambayo bado haijakusanywa.

**Mheshimiwa Spika,** hoja ya Kamati ni kwamba kutokukusanywa michango husika kunaathiri utekelezaji wa shughuli za

Mfuko.Vilevile kwa Mfuko kutokukusanya michango kunaathiri haki za hifadhi ya jamii ya wanachama kwa siku zijazo.

### 2.6.1.3 Dosari Katika Uwekezaji Kwenye Kampuni ya Sisalana Company Limited

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kifungu cha 3.3 cha Sera ya Uwekezaji ya NSSF kinaelekeza Mfuko kuhakikisha maslahi mapana ya wananachama yanalindwa kwa kuhakikisha kwamba uwekezaji unaofanywa na Mfuko unafanyika katika maeneo ambayo yanaleta faida na tija kubwa. Mnamo mwaka 2021 Mfuko uliamua kuchukua mali za iliyokuwa Kampuni ya "*Sisalana Tanzania Ltd*" iliyokuwa inamilikiwa na "*Kampuni ya Katani Limited*". Utwaaji huo ulitokana na dhamana iliyokuwa imewekwa na Kampuni ya Katani baada ya kuchukua mkopo NSSF na kushindwa kulipa.

**Mheshimiwa Spika,** hivyo NSSF kuichukua kampuni hiyo kulilenga kurejesha kiasi cha **Sh. 60,179,077,514.17** ambacho kilikuwa kinadaiwa hadi kufikia tarehe 31 Disemba, 2020. Kiasi hicho kinajumuisha Sh. **44,444,733,966.17** ambalo ni deni la msingi na limbikizo la riba kiasi cha **Sh. 15,734,343,548**.

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2022, NSSF walikuwa wamewekeza kwenye kampuni hiyo jumla ya **Sh. bilioni 2.5.** Pamoja na uwekezaji huo, CAG alibainisha changamoto kadhaa zinazotakiwa kufanyiwa kazi ili uwekezaji husika uwe na tija. Masuala hayo ni pamoja na haya yafuatayo:-

a) Kutokamilika kwa mchakato wa upembuzi yakinifu ambapo taarifa ya awali ya upembuzi yakinifu iliwasilishwa na mshauri mtaalamu 18 Septemba, 2022;

b) Kutokamilika kwa mchakato wa kisheria wa kuhamisha mali za iliyokuwa Kampuni ya Katani kuja NSSF; na

c) Kuamua muundo wa uendeshaji wa Kampuni mpya baada ya kukamilika mchakato wa uhamishaji wa mali.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na hoja tajwa hapo juu, Kamati katika mahojiano na Bodi na Menejimenti ya NSSF, waliifahamisha Kamati kuwa watahakikisha kwanza wanapata suluhu ya changamoto hizo kabla ya kuendelea kuwekeza fedha za umma katika mradi huo.Kuhusu makusanyo ya michango, Kamati ina maoni kuwa jitihada zinahitajika zaidi ili kuongeza kasi ya ukusanyaji wa michango. Kwa upande wa madeni ya Serikali, Kamati imeamua kwa mara nyingine kuileta hoja hii mbele ya Bunge kwaajili ya kupata azimio la Bunge.

**2.6.2 Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Serikali (PSSSF)**

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa taarifa ya hesabu zilizokaguliwa za Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma (PSSSF) ulibaini hoja zifuatazo:-

**2.6.2.1 Hoja Zinazohusiana na Kodi za Iliyokuwa PPF, LAPF na PSSSF**

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2021/2022 PSSSF ilikadiriwa na TRA madai ya kodi ya mapato (Corporate Income Tax) inayotokana na iliyokuwa Mifuko ya PPF , LAPF na PSSSF yenyewe ya kiasi cha **Sh. 714,927,007,506**.Kwa mujibu wa taarifa ya CAG ukaguzi wa kodi kwa iliyokuwa PPF kati ya mwaka 2016 hadi 2018 ulikadiriwa kiasi cha **Sh. 150,783,006,790**, ukaguzi wa kodi kwa iliyokuwa LAPF kati ya mwaka 2016 hadi 2018 ulibainisha kiasi cha **Sh. 143,091,168,050** na kwa PSSSF yenyewe kati ya mwaka 2019 hadi 2021 ilikadiriwa kodi ya **Sh.421,052,832,666**.

**Mheshimiwa Spika,** hoja ya Kamati katika eneo hili ni makadirio hayo makubwa ya kodi ya kiasi cha **Sh. 714,927,007,506**. Hii inatokona na msingi kwamba, kwa kuzingatia tathmini ya mwisho iliyofanywa kwenye mfuko ilibaini kuwa hali ya kifedha ya mfuko (funding level) ilikuwa 22.3% wakati hali inayopendekezwa ni 40%. Hivyo madai hayo ya kodi ikitokea yakalipwa yataathiri sana uwezo wa mfuko kutekeleza majkumu yake.

**Mheshimiwa Spika,** mnamo tarehe 24 Oktoba, 2023, Bodi wa Wadhamini ya PSSSF iliifahamisha Kamati kuwa wamewasilisha

rufaa yao kwa TRA na pia kwa Bodi ya Rufaa ya Kodi (TRAB) ili kushughulikia makadirio hayo ya kodi.

#### 2.6.2.2 Madeni Ambayo Serikali Inadaiwa na PSSSF Kiasi cha Sh. trilioni 2.452

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inatambua jitihada zilizochukuliwa na Serikali mapema tarehe 15 Disemba, 2021 kwa kutoa hati fungani isiyokuwa taslim yenye thamani ya Sh. trilioni 2. 177 ili kupunguza deni ambalo PSSSF ilikuwa inadai la jumla ya Sh. trilioni 4,629. Hivyo hadi sasa deni ambalo limebaki ni kiasi cha Sh. trilioni 2.452.

**Mheshimiwa Spika,** hadi sasa Serikali haijatoa taarifa rasmi ya mpango wa kuanza kulipa deni lililobaki. Kutolipwa kwa deni hilo pia kunaathiri uwezo wa PSSSF kutimiza majukumu yake kwa ufanisi.

### 2.7 Mapungufu ya Kiutendaji Ambayo Yanachangia Upotevu wa Fedha za Umma

**Mheshimiwa Spika,** katika eneo hili, Kamati ilijielekeza katika kupitia, kuchambua na kujadili hoja kadhaa za ukaguzi zinazohusu mapungufu ya kiutendaji (operational audit issues) katika taasisi za umma. Aidha, katika kujibu hoja za eneo hili, Kamati imefafanua ni kwa namna gani mapungufu hayo ya kiutendaji yanavyochangia kwa namna moja au nyingine matumizi mabaya ya fedha za umma.Hoja za kiutendaji na athari zake katika usimamizi wa matumizi ya fedha za umma ni kama ifuatavyo: -

#### 2.7.1 Uwepo wa Mikopo Iliyoiva Yenye Thamani ya Sh. 21,375,045,194.81 Kwenye Mfuko wa Pembejeo za Kilimo (AGITF) Ambayo Haijakusanywa

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka tunaotolea taarifa, Kamati imebaini uwepo wa mikopo yenye thamani ya **Sh. 21,375,045,194.81** kwenye Mfuko wa Pembejeo (AGITF) ambayo haijakusanywa na hivyo kuashiria upotevu wa fedha za umma. Kiasi hicho cha **Sh. 21,375,045,194.81** ni 81% ya kiasi chote cha **Sh.**

**26,422,092,100.55** ambacho ndio thamani ya mikopo ya Mfuko (Loan portfolio).

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa uwepo wa mifumo isiyokuwa thabiti ya udhibiti wa ndani kwa kiasi kikubwa ndiyo imesababisha Mfuko wa Pembejeo kushindwa kusimamia ipasavyo mikopo mbalimbali iliyotolewa ya zana na pembejeo za Kilimo.Sambamba na hilo Mfuko haukuwa na rasilimali watu ya kutosha kuweka usimamizi wa fedha za umma unaofaa.

**Mheshimiwa Spika,** maelezo ya Kamati yanathibitishwa na maelezo ya Bodi na Menejimenti ya Mfuko wa Pembejeo. Mathalani katika Taarifa ya Hesabu zilizokaguliwa za Mfuko na kusainiwa na Bodi ya Mfuko wa Pembejeo iliyoandikwa katika aya 1.8 ya Taarifa ya Hesabu[21] katika ukurasa wa 14, kuhusiana na ongezeko la mikopo chechefu, Bodi inakiri kwa kutoa maelezo yafuatayo ambayo naomba kuyanukuu:-

> **Nukuu:**
> ***"….. There is an increased rate of NPL of the outstanding loans which accounted to 83% of the total loan portfolio. Internal and external factors led to non perfoming loans; internal factors include inadequate loan analysis, inadequate loan monitoring, understaffing, inadequate loan system automation, insuffficitent fund to cater with increased demand of loans from farmers and luck of fund regualations. The external factors include diversion of loan purpose, inherent risks in agriculture business, price fluactuations and unreliable market for agricultural produces… "***
> **Mwisho wa Nukuu.**

**Mheshimiwa Spika,** kwa msingi wa maelezo hayo ya Bodi ya Mfuko wa Pembejeo kama yalivyonukuliwa, ni dhahiri kwamba mapungufu mengi yaliyosababisha uwepo wa mikopo chechefu

[21] Rejea AR/CG/AGITF/2021/22 katika ukurasa wa 14

(NPL) yanatokana na mapungufu ya ndani ya kiutendaji kama vile kutofanyika upembuzi na uchambuzi wa kutosha kabla ya kutoa mikopo, kutokuwa na mifumo thabiti ya kielekitroniki ya kusimamia mikopo na kutokuwepo ufuatiliaji wa kutosha wa mikopo iliyotolewa katika Sekta ya Kilimo.

### 2.7.2 Uwepo wa Bakaa ya Fedha Kiasi cha Sh. 26,656,717,909.04 Katika Akaunti ya Mirathi Bila ya Kufanyiwa Usuluhisho wa Kibenki (Reconciliation)

**Mheshimiwa Spika,** katika kupitia na kuchambua taarifa ya hesabu zilizokaguliwa za Fungu – 40 Mahakama, ilibainika uwepo wa kiasi cha fedha **Sh. 26,656,717,909.04** ambazo ni fedha za mirathi kwa watu mbalimbali lakini orodha ya wanufaika haikuwa imefanyiwa usuluhisho. Ukaguzi ulibaini kwamba, Rejista za Mirathi zinatunzwa kwenye mfumo wa makablasha (manual probate register), bado hazijawekwa kwenye mfumo wa kidigitali (electronic register).

**Mheshimiwa Spika,** dosari hii inaongeza uwezekano wa kupotea kwa nyaraka za mirathi na pia kutokuwa na taarifa sahihi na ugumu wa kufanya usuluhishi. Mathalani Kwa mwaka wa fedha 2021/22 bakaa ya fedha ya mirathi katika Akaunti ya Amana ilikuwa **Shs. 49,617,060,437**.

**Mheshimiwa Spika,** kiasi hiki kikubwa cha fedha kisipowekewa utaratibu mzuri wa kuhifadhiwa kinaweza kutumiwa vibaya na baadhi ya watumishi wasiokuwa waaminifu kwa manufaa yao binafsi badala ya wanufaika wa mirathi kwa mujibu wa Sheria. Uwezekano wa hoja hii ulithibitishwa na maelezo ya Mtendaji Mkuu wa Mahakama Profesa Olesante Ole Gabrieli mbele ya Kamati ambaye alikiri uwepo wa kesi za baadhi ya watumishi wa Mahakama kupelekwa mahakamani kwa kutumia vibaya fedha za Akaunti ya Mirathi na pia kesi za baadhi ya watu kutaka kutumia fedha za Akaunti ya Mirathi kwa udanganyifu.Maelezo yake yamenukuliwa kama ifuatavyo:-

**Nukuu:-**

***"…Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka niwaeleze jambo fulani kuhusu mirathi na tuweze kufahamu***

***kwa ujumla wake. Suala la mirathi lina mtego wake. Kwa sababu usipokuwa pia mwangalifu unapigwa vibaya sana. Wapo wajanja wengi hawana huruma hata na ile fedha ya mirathi. Tunavyoongea hapa mimi nimeshashtakiwa mbali kwamba nakataa kulipa hela ya mirathi. Nitasema kwa sababu namuona ndugu yangu Mtemvu na ni watu wa maeneo yake. Watu ambao wamepewa fidia TANESCO, walishafidiwa wakaja waka-raise tena issue kwamba tunadai na wapo ambao wamekufa katika ile mirathi. Nikasema hapana, milioni 976 ya Serikali mimi nitaitoaje. Nitajibu nini kwa CAG. Kwa hiyo, nimepigwa, nimeshtakiwa mpaka Mahakamani nimefunguliwa kesi…"***

**Mwisho wa Nukuu.**

### 2.7.3 Matumizi ya Takribani Sh. 5,675,750,000 kwa Mwaka Kuhudumia Wafungwa 3,110 Waliomaliza Kutumikia Vifungo Vyao

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Taarifa ya Ukaguzi ya Fungu 29 - Idara ya Huduma za Magereza kwa mwaka 2021/2022 ulibainisha kwamba, Idara ya Huduma za Magereza ilikuwa na wahamiaji haramu 1,264 ambao wanatumikia vifungo vyao. Katika idadi hiyo, 1,264 walikuwa wanatumikia vifungo vyao, 45 walikuwa wameshikiliwa rumande na 3,110 walikuwa bado wamekamilisha vifungo vyao ila hawajarudishwa kwenye Nchi zao.

**Mheshimiwa Spika,** hoja ya CAG na Kamati katika eneo hili, ni gharama kubwa ambazo zinatumiwa na Serikali kuhudumia wahamiaji haramu ambao wamemaliza kutumikia vifungo vyao. Kwa wastani, Idara ya Huduma za Magereza inatumia bajeti ya takribani **Sh. 5,675,750,000** kwa mwaka kwa chakula cha wahamiaji haramu waliokamilisha vifungo vyao.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kunukuu hoja hii ya ukaguzi kama ilivyoandikwa na CAG kama ifuatavyo:-

**Nukuu:-**

***"… We are of the view that Prisons use a lot funds to maintain those immigrants as the food itself for one prisoner is budgeted to cost TZS 5,000 for one day, hence having 3,110 immigrants at the Prisons cost TZS 5,675,750,000 in a year (3,110 x 5,000TZS x 365) which creates debts to Government as funds to maintain them were not budgeted during the year and migrants are not allowed to work compared to other prisoners who could generate revenue to the Prisons through various activities such as farming, civil works etc…"***

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na hoja hiyo ya ukaguzi, Kamati ilikutana na Afisa Masuuli, Wizara ya Mambo ya Ndani siku ya Alhamisi tarehe 19 Oktoba, 2023 Dodoma ili kupata maelezo yake ah atua anazochukuwa kujibu hoja hii ya ukaguzi.

**Mheshimiwa Spika,** Afisa Masuuli aliifahamisha Kamati jitihada kadhaa zilizochukuliwa kupunguza idadi ya wahamiaji haramu waliomaliza kutumikia vifungo vyao. Afisa Masuuli alifafanua kuwa vibali vya kuruhusu kutoka wahamiaji haramu 2,710 waliomaliza vifungo vyao vimetolewa.Hivyo CAG katika ukaguzi wake ujao atahakiki endapo wahamiaji haramu hao wamerejeshwa katika Nchi zao za asili.

### 2.7.4 Kampuni ya Mbolea Tanzania (TFC) Kutotekeleza Majukumu Yake ya Msingi kwa Mwaka 2021/2022 Pamoja na Kupewa Ruzuku ya Serikali Sh. 10,210,710,614

**Mheshimiwa Spika,** eneo lingine ambalo Kamati imebainisha kuwa na changamoto ya matumizi yenye tija ya fedha za umma ni katika Kampuni ya Mbolea Tanzania (TFC). Kwa mujibu wa taarifa ya ukaguzi ya TFC kwa mwaka 2021/2022, Kampuni ya TFC haikufanya biashara yake ya msingi kwa mwaka mzima na hivyo kutengeneza mapato ya kibiashara yenye thamani ya sifuri. Hii ni pamoja na TFC kupokea ruzuku ya Serikali yenye thamani ya **Sh. 10,210,710,614** kwa mwaka husika wa fedha.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa barua ya mapungufu ya ukaguzi ya TFC (Management letter), CAG amenukuliwa akifafanua hoja ya TFC kutotekeleza majukumu yake kama ifuatavyo, naomba kunukuu: -

> **Nukuu:**
> ***"……. Non execution of mandated functions, review of operational and financial performance noted Company reported zero revenue during the financial year 2021/22 despite being subsidized by Government TZS 10,210,710,614, This is because the company did not trade during the period. Further, we have noted that TFC is not effectively performing the 28 objectives of its establishment…"***
>
> **Mwisho wa Nukuu.**

**Mheshimiwa Spika,** kama nukuu hapo juu inavyofafanua, kwa TFC kushindwa kutekeleza majukumu yake pamoja na mambo mengine, CAG alibaini kulisababishwa na TFC kutokuwa na Mpango Mkakati (Strategic Plan) na Mpango wa Biashara (Business Plan) ambao umepitishwa na Bodi kwa mwaka 2019/2020 hadi 2023/2024 na badala yake menejimenti ya TFC ilidai kuwa ipo katika utaratibu wa kumpata Mtaalamu Mshauri ili afanye mapitio ya Mpango Mkakati uliopo ifikapo mwezi Disemba, 2023.

**Mheshimiwa Spika,** hoja ya msingi ya Kamati katika hesabu zilizokaguliwa za TFC inabaki kuwa, ni kwa kiasi gani matumizi ya **Sh. 10,210,710,614** yalikuwa na tija kwa Kampuni ambayo ilitengeneza mapato yenye thamani ya **sifuri** (zero revenue) kwa mwaka mzima wa fedha.

### 2.7.5 Dosari za Kiutendaji Katika Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA) Mikoa ya Tanga, Pwani na Tabora Hivyo Kuisababishia Serikali Hasara

**Mheshimiwa Spika,** mapitio na uchambuzi wa hesabu zilizokaguliwa za Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA) katika

Mkoa wa Tanga, Tabora na Pwani ulibainisha mapungufu makubwa kama ifuatavyo: -

a) Mikataba yote ya kukodisha mitambo iliyoingiwa katika Mkoa wa Tanga haikuwa na barua za maombi kutoka kwa watu waliokodisha mitambo hiyo;

b) Mikataba 27 ya ukodishaji mitambo Tanga ilikuwa na namba moja ya mkataba na haikusajiliwa kwenye daftari la mikataba;

c) Mikataba 27 ya ukodishaji vifaa haikuwa na tarehe ya kuanza wala kukamilika kwa mkataba;

d) Hapakuwa na nyaraka kubainisha ruhusa ya utolewaji wa mitambo (Release order) na hata makabidhiano ya mtambo baada ya kazi; na

e) Kutokukusanywa mapato ya **Sh. 919,600,000** za ukodishaji wa mitambo ya kusaga mawe katika Mikoa ya Tanga na Pwani.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilikutana na Afisa Masuuli TEMESA siku ya tarehe 07 Agosti, 2023 ili kujadili hatua zilizochukuliwa kutokana na viashiria vya matumizi mabaya ya fedha za umma kama yalivyoainishwa hapo juu. Majibu ya Afisa Masuuli yalifafanua kwamba kuna hatua kadhaa za kiuwajibikaji na kiutendaji zimechukuliwa kama navyonukuu hapa chini: -

**Nukuu: -**

***"…. Wakala umefanya uchunguzi maalum katika mikoa ya Pwani na Tanga na kujiridhisha kulikuwa na usimamizi usioridhisha wa ukodishaji mitambo hivyo Wakala umeandaa mwongozo wa usimamizi wa ukodishaji mitambo ulianza kutumika mwezi Julai 2022. Aidha, Wakala umechukua hatua za kinidhamu kwa aliyekuwa Meneja wa Mkoa Tanga…"***

**Mwisho wa Nukuu.**

**Mheshimiwa Spika,** kama nukuu hapo juu inavyofafanua, hatua kadhaa zimechukuliwa na Afisa Masuuli TEMESA hasa za kiutendaji katika kuimarisha mifumo ya udhibiti wa ndani na hatua za kinidhamu kwa aliyekuwa Meneja wa TEMESA Tanga. Hata hivyo hatua za kisheria kwa ubadhirifu wa fedha za umma hazijachukuliwa kwa watendaji wa TEMESA katika Mikoa ya Tanga, Pwani na Tabora ambao walihusika na matumizi mabaya ya fedha za umma.

### 2.7.6 Ubadhirifu wa Sh. 261,352,688.34 Uliofanyika Katika Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Ambapo Mhusika Amefukuzwa Kazi ila Hajafikishwa Mahakamani

**Mheshimiwa Spika,** eneo lingine ambalo Kamati ilibaini upotevu wa fedha za umma ni katika Fungu 14, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji.katika hoja hii ukaguzi wa hesabu za Fungu 14 ulibaini uwepo wa ubadhirifu wa fedha kiasi cha **Sh. 261,352,688.34** kwa fedha zilizotolewa katika Benki ya CRDB kwenye akaunti **" *Fire and Rescue Account*"**. Hata hivyo, wakaguzi walipoomba nyaraka za matumizi hayo hazikuwasilishwa kwaajili ya ukaguzi na uhakiki.

**Mheshimiwa Spika,** ubadhirifu wa fedha kutoka kwenye akaunti hiyo ya zimamoto umefafanuliwa na maelezo ya Mkaguzi Mkuu wa Nje[22] wa Fungu 14, Ndugu Hamza S. Songa aliyotoa mbele ya Kamati tarehe 09 Agosti, 2023[23] kama ifuatavyo:-

> **Nukuu:-**
> ***"Mwenyekiti, hizi zilikuwa ni fedha zilikuwa zinatoka moja kwa moja kwenye akaunti ya CRDB, kuingia kwenye akaunti ya zimamoto. Sasa chanzo cha ile fedha hakikujilikana na hata tukiuliza menejimenti nayo ilikuwa haijui.. kulikuwa na changamoto kwa sababu walikuwa hawafanyi reconciliation. Sasa kulikuwa na cashier ambaye anaonekana alikuwa***

[22] Chief External Auditor (CEA)

[23] Rejea Ukurasa wa 8 wa Taarifa Rasmi za Bunge, Majadiliano ya Kamati ya tarehe 09 Agosti, 2023

***anatengeneza kama signature ambazo wahusika walikuwa wanasema siyo za kwetu…"***

**Mwisho wa Nukuu.**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilimtaka Afisa Masuuli Fungu 14 kutoa maelezo ya hatua zilizochukuliwa kwa askari "cashier" aliyehusika na upotevu wa fedha hizo. Afisa Masuuli aliifahamisha Kamati kuwa suala hili lipo chini ya uchunguzi wa TAKUKURU tangu mwaka 2020. Hata hivyo, katika hatua za ndani wao kama Jeshi wamechukua hatua ya kumfukuza kazi askari aliyehusika. Naomba kunukuu maelezo ya Mheshimiwa Japheti Hasunga, Mb kuhusu hoja hii kama yalivyonukuliwa[24] kama ifuatavyo:-

**Nukuu:-**
***"….Accounting Officer angetuambia yeye kwenye upande wake amechukua hatua gani apart from report ya TAKUKURU , kuna vitu vingine ambavyo ni administrative procedure au masuala ya kisheria ambayo unaweza kuwachukulia watumishi hatua za kinidhamu na nini mmechukua hatua gani kwa hao walikuwa wanahusika…"***

**Mwisho wa Nukuu.**

**Mheshimiwa Spika,** katika kutoa ufafanuzi wa hatua zilizochukuliwa, Kamishina Jenerali wa Zimamoto Ndugu John Masunga alitoa maelezo yafuatayo:-

**Nukuu:-**

***"….Mheshimiwa Mwenyekiti , hili linanihusu mimi kwa sababu huyu askari ni wa rank interfile siyo Afisa., kwa hiyo kwa askari wa rank interfile kwa mamlaka niliyonayo nina uwezo wa kumfukuza kazi. Naomba niijulishe Kamati yako Tukufu kwamba, baada ya tukio hili mimi nilichukua***

[24] Rejea Ukurasa wa 56 wa Majadiliano ya Kamati Katika Taarifa Rasmi za Bunge ya Tarehe 09 Agosti, 2023.

***hatua zangu na nilishamfukuza kazi tayari, ili aendelee na shtaka lake linaloendelea…"***

**Mwisho wa Nukuu.**

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na hatua zilizochukuliwa za kumfukuza kazi askari husika, Kamati bado ilikuwa na hoja kwamba, uchunguzi wa TAKUKURU umechukua muda mrefu kukamilika wakati ushahidi wa ubadhirifu upo wazi.Aidha, Kamati ina maoni kwamba hatua ya kumfukuza kazi askari huyo ni hatua moja lakini uwajibikaji kamili ni pale hatua za kisheria ikiwa ni pamoja na kufikishwa mahakamani zitakapokamilika.Vilevile Kamati ina hofu kwamba suala hili lilihusisha zaidi ya mtu mmoja ikiwa ni pamoja na watumishi wa benki, lakini hadi sasa hatua zimechukuliwa kwa mtu mmoja pekee.

**2.7.7 Uwepo wa Deni la Sh. bilioni 1.8 Ambalo TTCL Inadai Lakini Haiwatambui Wadaiwa**

**Mheshimiwa Spika,** hoja nyingine kwenye masuala ya kiutendaji ambayo Kamati imebaini kuchangia upotevu wa mapato ya Serikali ni katika Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL). Katika uchambuzi, kamati ilibaini kwamba hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 kulikuwa na madeni ya muda mrefu ambayo TTCL inadai toka kwa wateja mbalimbali yenye thamani ya **Sh. bilioni 1.8** ambayo wateja husika hawakuwa wanafahamika.

**Mheshimwa Spika,** taarifa ya ukaguzi imebainisha kwamba, TTCL ilifanya jitihada kwa kufanya usuluhishi na pia kwa kuwasiliana na wateja mbalimbali ili kupata taarifa sahihi kuhusu madeni hayo.

**Mheshimiwa Spika,**Kamati ilifanya mahojiano na uongozi wa TTCL siku ya tarehe 13 Oktoba, 2023 Dodoma ili kupata maelezo ya hatua zinazochukuliwa ili kuimarisha mifumo ya udhibiti wa mapato. TTCL waliifahamisha Kamati kuwa changamoto kubwa kwao imekuwa ni kutokuwepo taarifa za muda mrefu ndani ya shirika zinazohusu masuala ya fedha. Aidha, walibainisha uwepo wa changamoto ya rasilimali watu na mifumo na kwamba wanaendelea kuboresha maeneo hayo.

**Mheshimiwa Spika,** hoja ya Kamati katika eneo hili inabaki kuwa ya msingi. Hii inatokana na ukweli kwamba, tangu mwaka jana 2022, Kamati iliitaka TTCL kuchukua hatua za kusafisha vitabu vya hesabu ili vitoe taswira halisi ya Shirika. Hata hivyo, jambo hilo halijakamilika kwa zaidi ya mwaka mmoja sasa. Hivyo ni dhahiri kwamba, mianya ya upotevu wa mapato ya Serikali bado ipo kwa kutokuwa na vitabu vya hesabu vyenye taarifa sahihi.

### 2.8 Uchambuzi wa Hoja za Ukaguzi za Ujumla Zinazohusu Uzingatiaji wa Sheria, Taratibu na Kanuni (Compliance Audit Issues)

**Mheshimiwa Spika,** eneo la mwisho la uchambuzi wa Kamati katika Taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ulijikita katika masuala ya ujumla yanayohusu uzingatiaji wa Sheria, Taratibu na Kanuni. Katika eneo hili, Kamati ilibaini hoja za ukaguzi katika maeneo yafuatayo:-

#### 2.8.1 Kutozingatiwa Ipasavyo Kwa Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma Wakati wa Mchakato wa Ajira Katika Benki Kuu ya Tanzania (BOT)

**Mheshimiwa Spika,** taarifa ya CAG katika ukaguzi wa Benki Kuu ya Tanzania (BOT) kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2022 imeabinisha kwamba, katika mchakato wa ajira 87 ndani ya Benki Kuu ya Tanzania, Menejimenti ya Benki iliongeza kigezo cha umri wa juu kwa kuwataka watu wote wanaotegemea kuomba ajira katika Benki lazima wawe na umri usiozidi miaka 30.

**Mheshimiwa Spika,** kigezo hicho cha umri kiliongezwa kati kati ya mchakato wa kuandaa orodha fupi ya watahiniwa. (shortlisting) na hakikuwa kimejumuishwa katika tangazo la awali la ajira husika. Suala hili linaenda kinyume na Kifungu D.39 cha Kanuni za Kudumu za Utumishi za Mwaka 2009. Kifungu husika kinabainisha wazi kwamba, umri wa juu wa kuajiriwa kwenye utumishi wa umma ni miaka 45.

**Mheshimiwa Spika,** hoja ya pili ya ukaguzi katika mchakato wa ajira husika ilihusu kutojumuishwa kwa watahiniwa 269 waliokuwa wamekidhi vigezo vya kuitwa kwenye usaili katika nafasi 9 za ajira. Taarifa ya ukaguzi imebainisha kwamba orodha ya watahiniwa

iliyokuwa imeidhinishwa kwa usaili ilikuwa 1,439 lakini idadi ya watahiniwa walioitwa kwa usaili ilikuwa 1,170. CAG hakupata nyaraka yeyote ya uthibitisho ya kurasimisha uamuzi huo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilikutana na Afisa Masuuli, BOT siku ya tarehe 19 Oktoba , 2023 ili kupata maelezo ya sababu za ukiukwaji wa Vifungu vya Kanuni za Kudumu za utumishi wa Umma za Mwaka 2009. Maelezo ya Afisa Masuuli na Menejimenti kwa ujumla yalikuwa yanasisitiza kuwa lengo lao lilikuwa kuangalia uwezekano wa kupata watumishi wenye umri mdogo ambao watafanya kazi na Benki kwa muda mrefu.

**Mheshimiwa Spika,** maelezo haya hayakuiridhisha Kamati ipasavyo.Kamati ina maoni kuwa mapungufu yaliyojitokeza katika mchakato wa ajira yanapunguza uadilifu wa mchakato husika. (integrity of the process). Aidha, maamuzi yaliyofanyika katikati ya mchakato kwa kiasi fulani yaliathiri utendaji wa haki kwa Watanzania waliotegemea kuomba ajira husika katika mfumo wa ushindani.

**Mheshimiwa Spika,**katika kuhitimisha hoja hii, naomba kunukuu maelezo ya CAG kama ifuatavyo:-

**Nukuu:-**

***"… Those anomalies are mainly caused by inadequate documentation of recruitment process which could enhance effective analysis and selection process and there after enhance fairness in recruitment process…"***

**Mwisho wa Nukuu.**

**Mheshimiwa Spika,** ni kwa msingi huo hoja ya kamati inabaki kutaka mchakato husika ufanyiwe mapitio kama ambavyo pendekezo mahsusi la Kamati linavyosomeka katika sehemu ya tatu ya taarifa hii.

## 2.8.2 Mapungufu ya Kiutendaji Katika Bodi ya Bima ya Amana (DIB)

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kifungu cha 32 cha Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya Mwaka 2006 kinatoa masharti ya kuanzishwa Bodi ya Bima ya Amana (DIB). Aidha, kifungu husika kinatoa maelekezo ya taratibu zote za msingi katika uendeshaji,usimamizi wa fedha na mali za DIB.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa taarifa ya ukaguzi ya CAG, alibaini kwamba DIB imekuwa ikijiendesha kwa kutegemea zaidi usaidizi wa Benki Kuu ya Tanzania ( BOT) wakati kwa mujibu wa Sheria DIB ni Taaisisi inayotakiwa kujitegemea. Mathalani Mkurugenzi wa DIB amekuwa akiwajibika kiutawala na kimajukumu moja kwa moja kwa Naibu Gavana wa Benki Kuu anayesimamia udhibiti wa ndani na utawala wa BOT badala ya kuwajibika kwa Bodi ya DIB. Aidha, DIB imekuwa ikitumia miongozo ya fedha , miongozo ya kiutumishi na taratibu nyingine za BOT. Hali hii inaathiri uhuru wa kiutendaji wa DIB.

**Mheshimiwa Spika,** dosari nyingine iliyobainika katika DIB ni kukosekana Kanuni za Unedeshaji wa DIB. Kwa msingi huo, kutokuwepo kwa Kanuni za Undeshaji wa DIB kunakwamisha utekelezaji wa vifungu vya 36 hadi 63 vya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya Mwaka 2006.Vifungu hivyo pamoja na mambo mengine vinaweka utaratibu wa kumpata Kiongozi wa DIB,Menejimenti na muundo wa DIB.

**Mheshimiwa Spika,** hoja ya mwisho katika DIB ilihusu mgongano wa kimaslahi katika usimamizi wa taasisi hiyo uliopo kwa muundo wake wa sasa. Kwa mujibu wa Kifungu 37 (3) cha Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya Mwaka 2006, Gavana wa Benki Kuu ndiye pia Mwenyekiti wa Bodi ya DIB. Suala hili linabainisha uwepo wa mgongano wa kimaslahi kwa sababu kwa mujibu wa Sheria BOT ni chombo cha udhibiti wa Taaisi za Fedha ikiwa ni pamoja na DIB. Naomba kunukuu hoja ya CAG katika eneo hili kama ifuatavyo:-

**Nukuu:-**

***"… We are of the view that Governer being chair of both DIB and BoT create operational conflict of interest and limit checks and balance as the same person responsible for regulating the bank is also responsible for liquidating the insolvent banks or financial institutions…"***

**Mwisho wa Nukuu.**

**Mheshimiwa Spika**, kwa msingi huo, CAG anasisitiza umuhimu wa kutenganisha majukumu ya Gavana wa oTn a shughuli za DIB ili DIB iwe huru kiuendeshaji kwa kuzingatia madhumuni ya uanzishwaji wake.

### 2.8.3 Baadhi ya Taasisi za Serikali Kutozingatia Mwongozo wa Wizara ya Fedha Katika Utunzaji wa Mali za Serikali kwenye Mfumo wa Kielektroniki

**Mheshimiwa Spika,** eneo lingine linalohusu uzingatiaji wa Sheria ambalo Kamati imelibaini linahusu baadhi ya Taasisi za Serikali kutozingatia kikamilifu maelekezo ya Wizara ya Fedha ya kufunga hesabu kwa kuhakikisha thamani ya mali za Taasisi inatumika thamani iliyowekwa kwenye mfumo wa kielekroniki wa utunzaji kumbukumbu wa mali za Serikali (GAMIS)[25].

**Mheshimiwa Spika,** Taasisi nyingi zilizofika mbele ya Kamati zilibainika kutozingatia maelekezo ya ukufunga hesabu kwa kuzingatia tahamani iliyopo kwenye mfumo wa GAMIS. Kwa msingi huo, hesabu za Taasisi hizo hazitoi taswira sahihi yenye uhalisia wa Taasisi.

**Mheshimiwa Spika,** hoja nyingine kuhusu utunzaji wa mali za Serikali ilibainika kwenye mlolongo mrefu wa kisheria uliopo wa kuondoa mali chakavu. Kutokana na hoja hii, Taasisi nyingi za Serikali zina mlundikano wa mali ambazo hazina thamani na hivyo kuharibika. Aidha uwepo wa mali hizo unasababisha upotevu wa mali za Serikali na kutengeneza hoja za ukaguzi kwa Taasisi.

[25] Government Assest Management Iformation System

### 2.8.4 Baraza la Taifa Usalama Barabarani Kutokufunga Hesabu na Hesabu Husika Kutokaguliwa

**Mheshimiwa Spika,** hoja ya mwisho ya Kamati inahusu Baraza la Taifa la Usalama Barabarani. Baraza Baraza hili linaundwa na Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti, na wajumbe wasiopungua 10 wanaoteuliwa na Waziri kuingia kwenye baraza hili. Kwa uratatibu ulivyo Naibu Waziri wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi huwa ndiye Mwenyekiti wa Baraza, na pia Naibu Waziri wa Wizara ya Uchukuzi ndio Makamu Mwenyekiti na Katibu wa Baraza ni Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani Nchini Tanzania.

**Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2022 Baraza la Taifa la Usalama Barabarani halikupata hati ya ukaguzi kwa vile Baraza halikuwasilisha taarifa za fedha ndani ya muda unaotakiwa kwa mujibu wa kifungu cha 30 cha Sheria ya Fedha za Umma ya mwaka 2001 (iliyorejewa 2020), aidha Baraza halikuwahi kuandaa taarifa za fedha toka lilipoanzishwa mwaka 1986.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilifanya mahojiano na Mwenyekiti wa Baraza hili siku ya tarehe 26 Oktoba , 2023 ili kutoa maelezo ya sababu za hesabu za Baraza kutokaguliwa. Mwenyekiti wa Baraza ambaye ni Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mhe. Jumanne Sagini, Mb aliifahamisha Kamati kuwa ni kweli kumekuwa na changamoto za kiundeshaji za Baraza. Hata hivyo hatua zimeanza kuchukuliwa kwa kuhakikisha Baraza linakuwa na watumishi wenye sifa za kiuhasibu ili kuhakikisha hesabu zinafungwa na kukaguliwa kwa wakati. Kwa msingi huo aliithibitishia Kamati kuwa hesabu za mwaka 2022/2023 zimefungwa na CAG ameanza kuzikagua.

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 MAONI NA MAPENDEKEZO

### 3.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia uchambuzi wa Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu ukaguzi wa hesabu za serikali kuu na mashirika ya umma kwa mwaka wa

fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2022, Kamati ina maoni na mapendekezo kama ifuatavyo: -

### 3.2 Maoni

**Mheshimiwa Spika**, maoni ya Kamati yamezingatia jukumu la Bunge kuwa chombo mahsusi cha usimamizi wa matumizi ya fedha za umma. Kwa mantiki hiyo, Kamati ina maoni ya ujumla yafuatayo: -

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ina maoni ya jumla kuwa kuna changamoto kwa Taasisi za Serikali zilizopewa jukumu la ukusanyaji wa mapato ya Serikali hivyo baadhi ya Taasisi hizo kusababisha mrundikano wa makusanyo ambayo hayajakusanywa.Vilevile Kamati ina maoni kwamba, usimamizi wenye dosari wa mikataba ni eneo ambalo linachangia upotevu mkubwa wa mapato ya Serikali, hivyo linatakiwa kuangaliwa kwa uangalifu mkubwa.

**Mheshimiwa Spika,** vilevile Kamati ina maoni kwamba baadhi ya Taasisi za Umma zimekuwa hazizingatii Sheria, Kanuni , Taratibu na Miongozo muhimu inayohusu usimamizi wa fedha za umma hali inayochangia matumizi yenye dosari katika matumizi ya fedha za umma.Ni maoni ya Kamati kuwa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii inakabiliwa na changamoto za madeni hasa ya Serikali hivyo kuathiri ukwasi wa Mifuko husika.

### 3.3 Mapendekezo

**Mheshimiwa Spika,** mapendekezo ya Kamati yametolewa kwa kuzingatia ukubwa wa athari ya hoja inayohusika, matokeo yenye kuambatana na hoja husika, uwezekano wa hoja kujirudia na hatua zinazotakiwa kuchukuliwa kushughulikia hoja husika. Mapendekezo ya Kamati yanasomwa sambamba katika **Randama ya 1** iliyoambatishwa na taarifa hii.

#### 3.3.1 Kuhusu Nakisi ya Ukusanyaji wa Mapato Kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) Kiasi cha Sh. Sh.887,301,296,148

**KWA KUWA,** Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) imebainisha nakisi ya kiasi cha **Sh.**

**Sh.887,301,296,148** cha mapato ambayo hayakukusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kwa mwaka wa fedha 2021/2022 kutokana na mapungufu mbalimbali ikiwa ni pamoja na usimamizi usiokuwa thabiti wa mafuta yanayosafirishwa kwenda nje ya Nchi na kisha kutumika hapa Nchini na kuchelewa kusajili mapingamizi ya kodi;

**NA KWA KUWA,** kutokusanywa kwa mapato hayo kunasababisha upotevu wa mapato ya Serikali na pia kunapunguza uwezo wa Serikali kuwa na rasilimali za kutosha kutimiza majukumu yake;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba:-

a) TRA ihakikishe ndani ya mwaka wa fedha 2023/2024 inakamilisha usimikaji na utekelezaji wa mifumo yote muhimu ya usimamizi na udhibiti wa kodi ili kuhakikisha mapato stahiki ya Serikali yanakusanywa kwa ukamilifu;

b) TRA ihakikishe kesi zote za mapingamizi ya kodi kama zinavyo letwa na walipa kodi zinashughulikiwa kwa mujibu wa Sheria na Kanuni zilizopo ili kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya Serikali;

c) TRA ihakikishe inaweka mifumo thabiti ya usimamizi wa kodi katika michezo ya kubahatisha na mafuta ambayo yanapitia hapa nchini kwenda nje ya Nchi. Katika kutekeleza azimio hili hatua kali za kisheria zichukuliwe kwa wanaokiuka Sheria na umma ujulishwe ipasavyo; na

d) TRA itengeneze mfumo maalumu wa kusimamia wakusanya mizigo (consolidators) ili kuhakikisha mapato ya Serikali yanakusanywa kwa mujibu wa Sheria.Aidha, Kodi yote ambayo ilikuwa haijakusanywa ikusanywe kwa mujibu wa Sheria na Taratibu zilizopo.

### 3.3.2 Hasara ya Tsh. 7,840,000,000 katika TANOIL

**KWA KUWA,** Taarifa ya CAG imebainisha hasara ya kiasi cha **Sh. Sh.7,840,000,000** katika kampuni ya TANOIL;

**NA KWA KUWA,** Hasara hizo zinachangia upotevu wa mapato ya Serikali na hivyo kutofikiwa lengo la kuanzishwa kwa Kampuni husika;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba:-

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali afanye Ukaguzi wa Kiuchunguzi (Forensic Audit) katika Kampuni ya TANOIL ili kubainisha kwa kina sababu na mazingira ya hasara za TANOIL. Katika kutekeleza jukumu hilo CAG azingatie masuala yafuatayo:-

a) Kupitia kwa kina utaratibu uliotumika kuanzisha Kampuni ya TANOIL na malengo yake;

b) Kupitia na kuchambua utaratibu na njia (Business model) za kibiashara zinazotumiwa na TANOIL kufanya biashara ya mafuta na endapo zina tija na ufanisi;

c) Kuchunguza uhusika wa iliyokuwa Menejimenti na uongozi wa TANOIL katika kusababisha hasara kwa kampuni hasa kwa maamuzi waliyokuwa wanafanya kinyume na taratibu na miongozo; na

d) Kuchunguza masuala mengine yeyote yanayohusiana na TANOIL ambayo yanahusiana na fedha za umma.

### 3.3.3 Mapato yasiyokukusanywa Dola za Marekani 599,000 Katika Wizara ya Maliasili na Utalii

**KWA KUWA,** Taarifa ya CAG imebainisha uwepo wa kiasi cha **Dola za Marekani 599,000** ambacho hakikusanywa katika Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mzabuni kukiuka masharti ya zabuni kwa makusudi;

**NA KWA KUWA,** Kutokusanywa kwa mapato hayo ni upotevu wa mapato ya Serikali;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba:-

a) Serikali ikamilishe uaandaaji wa Kanuni zitakasoweka sharti la adhabu kwa wazabuni wanaoikiuka masharti ya uwekezaji katika zabuni za vitalu vya uwindaji wa kitalii; na

b) Kampuni husika iliyokiuka masharti ya zabuni *"M/s Game Hunters Tanzania Ltd"* izuiwe kufanya shughuli zozote katika sekta ya uwindaji wa kitalii hapa nchini kwa kukiuka masharti ya zabuni kwa makusudi hali ambayo iliikosesha Serikali mapato.

### 3.3.4 Kampuni ya IPTL Kutotimiza Wajibu wa Kimkataba Hivyo Serikali Kuwa Hatarini Kupatiwa Madai ya Sh. bilioni 148.4 Yanayotokana na IPTL

**KWA KUWA,** Taarifa ya CAG imefafanua kwamba Kampuni ya IPTL imeshindwa kutekeleza wajibu wake wa kimkataba kwa kinga ya kisheria iliyoitoa dhidi ya madai ya Serikali;

**NA KWA KUWA,** Kutotekelezwa kwa kinga hiyo ya kisheria kunasababisha Serikali kuendelea kudaiwa madai mbalimbali yanayotokana na IPTL ikiwamo madai ya **Sh. bilioni 148. 4**;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba:-

a) Serikali itekeleze kwa ukamilifu masharti yaliyoambatishwa kwenye Kinga ya Kisheria (Indemnity) iliyotolewa na IPTL dhidi ya madai yoyote ambayo yangetokea kwa Serikali baada ya kutolewa kwa fedha katika Akaunti ya Tegeta Escrow; na

b) Serikali isifanye malipo mengine yoyote kwa mashauri yanayofunguliwa dhidi ya wamiliki wa IPTL ili kutopoteza fedha za umma kwa sababu ina Kinga ya Kisheria kwa suala hilo.

### 3.3.5 Mapungufu Katika Utekelezaji wa Mradi wa Maji wa Mwanga, Same hadi Korogwe

**KWA KUWA,** CAG amebainisha dosari kadhaa katika utekelezaji wa mradi wa maji wa Same, Mwanga hadi Korogwe;

**NA KWA KUWA,** Dosari za kiutekelezaji zimesababisha ongezeko kubwa la gharama za mradi, kutokamilika mradi kwa wakati na kutofikiwa malengo ya mradi kwa wakati;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba;

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali afanye Ukaguzi Maalumu katika Mradi wa Maji Same, Mwanga hadi Korogwe kwa kuzingatia maeneo yafuatayo: -

a) Kuchunguza taarifa za mkataba wa mkopo kati ya Serikali na wadau wa maendeleo ili kupata taarifa sahihi za mwenendo wa mkopo na kiasi ambacho kimeshatolewa na kila mdau wa maendeleo pamoja na gharama za mkopo hadi sasa;

b) Kuchunguza na kupata taarifa sahihi za akaunti maalumu inayohusika na upokeaji fedha za mkopo wa mradi wa Same-Mwanga-Korogwe na kulinganisha na malipo yote yaliyofanywa tangu kuanza kwa mradi

c) Kupitia andiko la mradi na marejeo yake ili kubaini kama uibuaji wa mradi ulizingatia mahitaji halisi ya wananchi;

d) Kuchunguza na kubainisha kasoro zilizoko kwenye hatua za uandaaji wa zabuni, mchakato wa zabuni, tathimini ya zabuni na tuzo ya mikataba ya ujenzi wa Mradi wa Same-Mwanga-Korogwe (Vipande Namba I, II, III na IV);

e) Kuchunguza na kubainisha kasoro za usimamizi wa utekezaji wa mikataba ya ujenzi wa mradi wa Same-

Mwanga-Korogwe zilizosababisha kuchelewa kukamilika kwa ujenzi wa mradi;

f) Kubainisha hasara zilizotokana na ujenzi wa mradi wa Same-Mwanga-Korogwe pamoja na wahusika waliosababisha hasara hizo; na

g) Kuchunguza na kubainisha kama ununuzi wa wakandarasi wa ujenzi na usimamizi wa mradi wa Same-Mwanga-Korogwe ulifanyika kwa mujibu wa Sheria ya Ununuzi wa Umma.

**3.3.6 Manunuzi ya Mita za Umeme bila Kukaguliwa na Wakala wa Vipimo**

**KWA KUWA,** Uchambuzi wa Kamati katika taarifa za CAG umebainisha mapungufu katika mchakato wa manunuzi ya mita za umeme bila ya kufanyiwa uhakiki na Wakala wa Vipimo;

**NA KWA KUWA,** kutohakikiwa huko kunasababisha uwezekano wa mita za umeme zisizokuwa na ubora kuingia sokoni na hivyo kuikosesha TANESCO mapato;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba:-

Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi Serikalini (PPRA) ifanye ukaguzi maalumu wa ununuzi wa mita za umeme uliofanywa na TANESCO na kisha kutoa taarifa yake kwa Bunge.

**3.3.7 Tume ya Madini Kutokukusanya Madeni ya Kiasi cha Sh.30,757,555,988**.

**KWA KUWA,** Uchambuzi wa Kamati katika taarifa za CAG umebainisha kutokusanywa kwa mapato kiasi cha **Sh. 30,757,55,988** kutokana na changamoto mbalimbali;

**NA KWA KUWA,** Kutokusanywa kwa mapato husika kunaikosesha Serikali mapato stahiki kwaajili ya shughuli za maendeleo;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba; Tume ya Madini ihakikishe madeni husika yanakusanywa ndani ya mwaka wa

fedha 2023/2024. Aidha, kwa vipengele vya Sheria ya Madini Sura 123 ambavyo vinakwaza makusanyo ya mapato ya Serikali vifanyiwe marekebisho kabla ya kukamilika mwaka wa fedha 2023/2024.

### 3.3.8 Bohari Kuu ya Madawa (MSD) na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF)

**KWA KUWA,** Taarifa ya CAG imebainisha uwepo wa deni ambalo MSD na NHIF inadai Serikali kwa muda mrefu kiasi cha **Sh.bilioni 275** na **Sh. bilioni 228** mtawalia . Vilevile Taarifa hiyo imefafanua kuhusu dosari katika mikataba 2 ya ununuzi wa dawa na vifaa tiba kutoka Nchini Misri;

**NA KWA KUWA,** MSD na NHIF zinakabiliwa na changamoto ya kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kwa sababu ya mzigo wa deni ambalo Serikali inadaiwa. Aidha, kwa vyombo vya dola kutokamilisha uchunguzi wa mikataba ya ununuzi wa dawa na vifaa tiba kutoka nchini Misri kunakwamisha hatua za kisheria kuchukuliwa kwa wahusika wa manunuzi hayo.;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba:-

a) Serikali ianze kupunguza deni inalodaiwa na MSD kiasi cha takribani **Sh. bilioni 275** na **Sh. bilioni 228** za NHIF ndani ya mwaka wa fedha 2023/2024; na

b) Serikali ikamilishe uchunguzi wa ununuzi wa vifaa tiba na madawa uliofanywa kutoka kwa kampuni ya M/s. AL HANDASIA ya nchini Misri na kuchukua hatua stahiki kwa wahusika kwa kuzingatia matokeo ya uchunguzi; na

### 3.3.9 Taarifa ya Ukaguzi Maalumu Kuhusu Uendeshaji na Usimamizi wa Mikataba ya Maridhiano ya Kukiri Makosa (Plea Bargain)

**KWA KUWA,** Taarifa ya CAG kuhusu Ukaguzi Maalumu wa Mikataba ya Kukiri Makosa imebainisha changamoto kadhaa hususan mapungufu katika utaratibu wa kuendesha na kusimamia mikataba hiyo;

**NA KWAKUWA,** Mapungufu yaliyobainika pamoja na mambo mengine yalihusu usimamizi usioridhisha wa fedha za umma;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba; Serikali ifanye uchunguzi wa kina na mahsusi katika suala hili kwa kuzingatia masharti ya Katiba na Sheria ili wahusika wachukuliwe hatua ipasavyo kwa dosari zilizojitokeza katika mchakato huu.

### 3.3.10 Taarifa ya Matumizi ya Fedha za Mkopo wa Uviko Zilizotolewa na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF)

**KWA KUWA,** Taarifa ya CAG kuhusu Ukaguzi Maalumu wa matumizi ya Fedha za Mkopo wa Uviko 19 imebainisha changamoto kadhaa katika matumizi ya fedha hizo kwa watekelezaji wa kisekta ikiwa ni pamoja na baadhi ya miradi kutoanza kufanya kazi kwa wakati ;

**NA KWA KUWA,** Mapungufu yaliyobainika yana athari kwenye matumizi ya fedha za umma hasa kwa miradi kuchelewa kukamilika au kutotekelezwa ipasavyo kwa masharti yaliyoingiwa;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba:-

a) Serikali itekeleze mapendekezo yote ya ukaguzi maalumu wa fedha za uviko kama yalivyotolewa na CAG na kuwasilisha Bungeni Taarifa ya Utekelezaji wa mapendekezo hayo katika kipindi cha kila robo mwaka; na

b) Katika miradi inayotekelezwa kwa fedha za mikopo, Serikali ihakikishe inatenga fedha za kutosha kwa ajili ya ufuatiliaji na tathmini pamoja na kuimarisha usimamizi.

### 3.3.11 Kutozingatiwa Ipasavyo Kwa Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma Wakati wa Mchakato wa Ajira Katika Benki Kuu ya Tanzania (BOT)

**KWA KUWA,** Uchambuzi wa Kamati katika taarifa ya CAG umebaini mapungufu katika mchakato wa ajira uliofanyika katika Benki Kuu ya Tanzania (BOT);

**NA KWA KUWA,** Mapungufu hayo yanaathiri uadilifu wa mchakato kwasababu kulikuwa na uwezekano wa kuwanyima haki baadhi ya watanzania walioomba nafasi husika;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba;

Bodi ya BOT iwachukulie hatua za kinidhamu Watumishi wote waliohusika kwenye mchakato wa ajira hizo kwa ukiukwaji wa Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma ili jambo hilo lisijitokeze tena ili kutenda haki kwa watanzania wote.

### 3.3.12 Mapungufu katika mchakato wa ununuzi wa vishkwambi 300,000

**KWA KUWA,** Uchambuzi wa Kamati katika taarifa ya CAG umeainisha mapungufu kadhaa katika zabuni ya ununuzi wa vishkwambi 300,000 vilivyonunuliwa na Wizara ya Elimu kwaajili ya matumizi ya Sensa;

**NA KWA KUWA,** Mapungufu hayo yalisababisha changamoto kadhaa katika ununuzi na baadaye ugawaji wa vishkwambi hivyo kwa wahusika;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba;

Serikali ihakikishe inakuwa na mpango na mkakati endelevu wa maandalizi ya kina ya utekelezaji wa shughuli zote ambazo utekelezaji wake unajulikana mapema, kama vile Sensa ya Watu na Makazi na Uchaguzi Mkuu. Aidha kuwe na Mfuko Maalumu wa kugharamia shughuli zinazotekelezwa kwa kalenda maalumu kama Sensa na Uchaguzi Mkuu ili kuepuka hoja za ukaguzi zinazotokana na utekelezaji wa shughuli hizo kwa dharula.

### 3.3.13 Mfuko wa Pembejeo za Kilimo (AGITF) na Kampuni ya Mbolea Tanzania ( TFC)

**KWA KUWA,** Taarifa za ukaguzi katika hesabu za Mfuko wa Pembejeo za Kilimo (AGITF) umebaini uwepo wa mikopo chechefu ya kiasi cha Sh. **21,375,045,194.81.** Vilevile CAG amebainisha changamoto katika Kampuni ya Mbolea (TFC) hali

ambayo iliifanya Kampuni hiyo kutopata mapato ya kibishara kama inavyotakiwa;

**NA KWA KUWA,** Mapungufu hayo yanasababisha uwezekano wa fedha za umma kutokusanywa kutokana na mikopo chechefu katika Mfuko wa Pembejeo.Aidha, kwa TFC kutotekeleza majukumu yake hauakisi matumizi sahihi ya ruzuku ya Serikali inayopelekwa kwa Kampuni hiyo;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba;

a) Mfuko wa Pembejeo za Kilimo uhakikishe unakusanya madeni husika ndani ya mwaka wa fedha 2023/2024. Aidha, mifumo ya udhibiti iimarishwe ili kuepuka ongezeko la mikopo chechefu;

b) TFC iandae Mpango wa Biashara wenye tija ili kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kwa kuwafikia wakulima Nchi nzima ili thamani ya fedha ya Serikali inayotumika na Kampuni ionekane bayana.

### 3.3.14 Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ya PSSSF na NSSF

**KWA KUWA,** Kamati imebainisha changamoto kadhaa katika hesabu za Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Changamoto hizo ni pamoja na uwepo wa madeni ambayo Serikali inadaiwa na Mifuko ya PSSSF na NSSF;

**NA KWA KUWA,** Madeni husika yanapunguza uwezo wa Mifuko kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba; Serikali iwasilishe Bungeni Mpango wa muda mrefu wa kulipa madeni ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii.

### 3.3.15 Uwepo wa Kiasi Kikubwa cha Fedha Katika Akaunti ya Mirathi Katika Fungu 40 Mahakama

**KWA KUWA,** Kupitia taarifa ya ukaguzi wa Fungu 40, Mahakama,Kamati imebainisha uwepo wa kiasi kikubwa cha fedha katika Akaunti ya Mirathi ambayo haikuwa imefanyiwa usuluhishi;

**NA KWA KUWA,** Uwepo wa fedha hizo katika Akaunti ya Mirathi bila usuluhishi inaweza kuchangia upotevu wa fedha za mirathi ambazo hazijalipwa;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba;

Afisa Masuuli wa Fungu 40, Mahakama ya Tanzania akamilishe usimikaji na utekelezaji wa Mfumo wa Kidijitali wa Utunzaji wa kumbukumbu *(E -Trace)* ikiwa ni pamoja na kumbukumbu za Akaunti ya Mirathi. Aidha, usuluhishi wa kibenki wa Akaunti husika ufanyike kwa wakati ili kuepusha upotevu wa fedha zilizopo kwenye Akaunti hiyo.

### 3.3.16 Ukaguzi wa Kiufundi wa ujenzi wa Reli ya Kisasa (SGR)

**KWA KUWA,** Kupitia taarifa ya ukaguzi wa Kiufundi wa ujenzi wa Reli ya Kisasa,Kamati imebainisha changamoto kadhaa katika utekelezaji wa mradi kwa masuala kama changamoto za ununuzi, kuchelewa kukamilika kwa mradi na ugharamiaji wa mradi kwa ujumla wake;

**NA KWA KUWA,** Kuchelewa kukamilika kwa mradi huu kunasababisha kuchelewa kupata thamani halisi ya fedha kwa uwekezaji huo muhimu na mkubwa wa kimkakati wa Serikali.

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba;

a) Serikali ihakikishe inapata ufadhili wa kifedha wenye unafuu wa uhakika na kwa wakati wa mradi wa SGR kwa vipande vinavyoendelea na ujenzi na kwa vipande vilivyobaki ili mradi ukamilike kwa wakati na kuchangia ukuaji wa uchumi.

b) Serikali ihakikishe kuwa juhudi zinachukuliwa za kulinda taswira chanya ya miradi yote mikubwa ya Kimkakati inayotekelezwa hapa Nchini ikiwemo Mradi huu wa SGR ili itekelezwe na kukamilika kwa wakati na;

c) TRC iendelee kusimamia shughuli zote za ujenzi wa Reli ya Kisasa kwa kuzingatia kikamilifu Sheria za Nchi.

### 3.3.17 Mfuko wa Tuzo na Tozo wa Jeshi la Polisi na Mfuko wa Kufa na Kuzikana wa Jeshi la Polisi

**KWA KUWA,** Kupitia taarifa ya Ukaguzi Maalumu katika Mfuko wa Tuzo na Tozo wa Jeshi la Polisi umebainisha dosari kadhaa ikiwa ni pamoja na fedha za Mfuko kutumika kwa matumizi yasiyokusudiwa na Kamandi chache tu kupokea fedha za Mfuko badala ya kupelekwa nchi nzima. Vilevile , Taarifa ya Ukaguzi Maalumu wa Mfuko wa Kufa na Kuzikana imebainisha ubadhirifu mkubwa katika Mfuko huo;

**NA KWA KUWA,** Dosari zote zilizobainika kwenye Kaguzi hizo Maalumu zinahusu matumizi mabaya ya fedha za Umma.

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba;

a) Kanuni za Mfuko wa Tuzo na Tozo wa Jeshi la Polisi ziandaliwe na kutumika ipasavyo zikiainisha bayana vyanzo vya mapato ya Mfuko, Taratibu za Matumizi ya Mfuko na Uwajibikaji katika Fedha za Mfuko;

b) Hatua za Kisheria na Kinidhamu zichukuliwe kwa watuhumiwa wote 27 waliohusika na ubadhirifu wa fedha za Mfuko wa Kufa na Kuzikana wa Jeshi la Polisi; na

c) Jeshi la Polisi lihakikishe Kanuni za kusimamia Mfuko wa Kufa na Kuzikana zinaandaliwa na kuanza kufanya kazi.

### 3.3.18 Ukaguzi Maalumu wa Kampuni ya Uendeshaji Uwanja wa Ndege Kilimanjaro (KADCO)

**KWA KUWA,** CAG alikamilisha Ukaguzi Maalumu wa KADCO na kuwasilisha kwa Katibu wa Bunge Taarifa yake Mwezi Oktoba 2023. Taarifa hiyo imebainisha dosari ikiwa ni pamoja na mapungufu katika uuzaji wa hisa za KADCO, dosari katika usimamizi wa fedha na mikataba na kutotekelezwa kwa Maamuzi ya Baraza la Mawaziri na Azimio la Bunge linalohusu kurudisha shughuli za KADCO kwenda TAA;

**NA KWA KUWA;** Mapungufu yote yaliyobainika yanahusu matumizi na usimamizi wa fedha za umma;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba; Serikali itekeleze mapendekezo yote ya CAG yanayohusu ukaguzi maalumu uliofanyika KADCO kwa hoja zinazohusu utendaji na fedha kama ilivyokuwa.

## SEHEMU YA NNE

### 4.0 HITIMISHO
### 4.1 Shukurani

**Mheshimiwa Spika,** Napenda kutumia fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa uongozi wako. Uongozi wako umeiwezesha Kamati yangu kutekeleza majukumu yake bila vikwazo kwa kutoa maelekezo na miongozo thabiti kwa Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** Nawashukuru wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali kwa kutekeleza majukumu ya Kamati hii kwa ufanisi na weledi mkubwa.

**Mheshimiwa Spika,** Naomba kuwatambua Waheshimiwa Wajumbe hao kama ifuatavyo: -

1) Mhe. Naghenjwa Livingstone Kaboyoka, Mb – **Mwenyekiti**
2) Mhe.Japheti Ngailonga Hasunga, Mb - **M/ Mwenyekiti**
3) Mhe. Eng. Isack Aloyce Kamwele, Mb
4) Mhe. Joseph George Kakunda, Mb
5) Mhe. Geoffrey Idelphonce Mwambe, Mb

6) Mhe. Simon Songe Lusengekile, Mb
7) Mhe. Anton Albert Mwantona, Mb
8) Mhe. Kiswaga Boniventura Destery, Mb
9) Mhe. Juma Othman Hija, Mb
10) Mhe. Idarus Faina Ravia, Mb
11) Mhe.Jacqueline Ngonyani Msongozi Mb
12) Mhe.Janeth Maurice Masaburi, Mb
13) Mhe.Esther Nicholas Matiko, Mb
14) Mhe. Anatropia Lwehikila Theonest, Mb
15) Mhe.Condester Michael Sichalwe, Mb
16) Mhe.Nancy Hassan Nyalusi, Mb
17) Mhe. Daudi Protas Venant, Mb
18) Mhe.Issa Jumanne Mtemvu, Mb
19) Mhe. Bakar Hamad Bakar, Mb
20) Mhe. Emmanuel Lekishon Shangai, Mb

**Mheshimiwa Spika,** napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Bi. Nenelwa Mwihambi, *ndc* kwa uongozi wake thabiti wa Sekretarieti ya Bunge ambayo imeratibu shughuli za Kamati kwa ufanisi mkubwa.

**Mheshimiwa Spika,** mwisho japo sio kwa umuhimu, Kamati inatambua na kuthamini ushirikiano mkubwa ilioupata kutoka Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi (NAOT) na kwa namna ya kipekee kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Ndugu Charles Kichere. Aidha naishukuru Wizara ya Fedha kupitia Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG), Mhasibu Mkuu wa Serikali (AcGen), Msajili wa Hazina (TR) na Idara ya Usimamizi wa Mali za Serikali (DGAM) na Maafisa wao wote kwa ushirikiano waliotoa katika kuratibu majibu ya hoja za ukaguzi na mahojiano ya Kamati na Maafisa Masuuli.

**4.2 Hoja**

**Mheshimiwa Spika,** nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Naomba kutoa Hoja.

Naghenjwa Livingstone Kaboyoka, Mb
**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU**
**YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI (PAC)**
02 Novemba, 2023

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Ahsanteni sana. Makamu Mwenyekiti ahsante sana kwa wasilisho hili la muhimu kabisa, tunakushuru.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Kamati nyingine. Niamwita sasa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa yaani *LAAC*, Mheshimiwa Halima James Mdee.

**MHE. HALIMA J. MDEE – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, hotuba yetu ina *page* 121. Nitakachosoma hapa ni *summary* kwa hiyo naomba *Hansard* ichukue yote kama ilivyo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati kuhusu Hesabu za Serikali kwa Hesabu zilizokaguliwa za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2022 na kuliomba Bunge lako lipokee na kuijadili.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifanikiwa kuchambua na kujadili Taarifa za Hesabu zilizokaguliwa na kufanya mahojiano na Wakurugenzi wa Halmashauri 74 ambazo ni sawa na Asilimia 40.2 ya Halmashauri zote 184.

Mheshimiwa Spika, Matokeo ya Uchambuzi; katika mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2022, *CAG* alikagua jumla ya Halmashauri 184 na kutoa Hati kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, idadi ya Hati zinazoridhisha zilikuwa ni 170 sawa na 92.39%, Hati zenye shaka 13 sawa na 7.06% na, idadi ya Hati mbaya ilikuwa ni moja.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa jumla wa Kamati umebaini kuwa, Idadi ya Halmashauri zilizopata Hati zinazoridhisha zimepungua kutoka Halmashauri 176 zilizotolewa mwaka wa fedha 2020/2021, hadi Halmashauri 170. Kwa Hati ya shaka, idadi ya Halmashauri imeongezeka kutoka Halmashauri nane mwaka 2020/2021 hadi Halmashauri 13 kwa mwaka 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, tafsiri ya hati hizi ni kwamba halmashauri zilizidi kufanya vibaya kwenye eneo la matumizi ya fedha za umma.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini maeneo muhimu yenye changamoto ya uwajibikaji na matumizi mabaya ya fedha za umma kama ifuatavyo: -

(a) Mifumo dhaifu ya ukususanyaji wa mapato ya ndani Pamoja na kushindwa kukusanya madai *(Receivables);* Mapungufu yaliyoibuliwa na Kamati katika eneo hili ni kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, moja, Ukosefu wa ubunifu wa vyanzo vipya vya mapato ya ndani; Kamati imezitaka Halmashauri zote zilizohojiwa kuachana na fikra za kutegemea Ruzuku toka Serikali Kuu kwa kiasi kikubwa na badala yake wataalam waliopewa madaraka watafakari na kuibua vyanzo vipya vya mapato ya ndani kulingana na fursa zinazopatikana katika maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa taarifa ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI iliyowasilishwa mbele ya Kamati, katika mwaka wa fedha unaojadiliwa 2021/2022, Halmashauri 184 zilipokea ruzuku kutoka Serikali Kuu zenye jumla ya shilingi trilioni 5.99. Huku mapato ya ndani yanayokusanywa na Halmashauri 184 yakiwa shilingi bilioni 891 tu. Utegemezi huu hatuwezi kuendelea nao.

Mheshimiwa Spika, mbili, Upotevu wa mapato wa shilingi bilioni 11.07 yaliyokusanywa kupitia mashine za kukusanyia mapato *(POS)* ambayo hayakuwasilishwa benki; jumla ya Halmashauri 98 sawa na asilimia 53.2 hazikuwasilisha Benki fedha zilizokusanywa kupitia mashine za *POS*. Kamati ilibaini kwamba wahusika wengi hawachukuliwi hatua kutokana na TAKUKURU kuchukua muda mrefu kutoa maamuzi ya kiuchunguzi; na Wakurugenzi wamekuwa wakitumia TAKUKURU kama kichaka cha kutochukua hatua dhidi ya wakusanya mapato ambao wamekusanya pesa na kuzitumia kwa matumizi mengine badala ya kuziwasilisha benki.

Mheshimiwa Spika, tatu, Halmashauri kushindwa kukusanya shilingi bilioni 37.34 kutoka katika vyanzo muhimu vya mapato;

uchambuzi wa Kamati kutoka kwenye Taarifa ya CAG umebaini maeneo saba muhimu ambayo Halmashauri 146 zimeshindwa kukusanya mapato ikiwa ni pamoja na:-

(a) Leseni za biashara shilingi bilioni 13.9;

(b) Mauzo ya viwanja shilingi Bilioni 12.2;

(c) Kodi ya Pango Bilioni 5.6;

(d) Ushuru wa taka shilingi bilioni 3.01;

(e) Leseni ya vileo bilioni 1.7;

(f) Fukwe na maeneo ya wazi ni shilingi Milioni 299; na

(g) Ushuru wa huduma shilingi Milioni 439.

Mheshimiwa Spika …

**SPIKA:** Ngoja, fukwe na maeneo ya wazi, kiasi gani?

**MHE. HALIMA J. MDEE – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, ushuru wa fukwe shilingi milioni 299 na ushuru wa huduma za uwindaji shilingi 439, ununuzi wa viwanja shilingi bilioni 12.2. Sawa Mheshimiwa?

**SPIKA:** Sawa, endelea.

**MHE. HALIMA J. MDEE – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, mapato yasiyokusanywa yameongezeka kutoka shilingi bilioni 14.29 mwaka 2020/2021 hadi kufikia shilingi bilioni 37.33 mwaka 2021/2022. Ongezeko hili ni sawa na asilimia 61.7. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hali hii inatokana na uzembe wa Wakurugenzi wa Halmashauri katika usimamizi wa ukusanyaji wa mapato ya Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, nne, Ushuru wa Huduma usiokusanywa shilingi bilioni 36.22; utozaji wa ushuru wa huduma wa kiwango kisichozidi 0.3 umefafanuliwa katika Vifungu vya 6(1)(u) na 7(1)(y) vya Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura namba 290 kama kilivyorekebishwa na Kifungu cha 44 na 45 cha Sheria ya Mwaka 2020. Halmashauri 40 zimeshindwa kukusanya ushuru kutokana na kukosa taarifa sahihi za mauzo ghafi ya wafanyabiashara wenye leseni halali waliopo katika maeneo yao. Mfano wa Halmashauri ambazo hazikukusanya ushuru wa huduma kutokana na kukosa taarifa sahihi ya mauzo ni Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam shilingi bilioni 25.96; Halmashauri ya Jiji la Arusha shilingi bilioni 4.55; na Halmashauri ya Mji wa Iringa shilingi milioni 508.

Mheshimiwa Spika, tano, Halmashauri kufanya malipo bila viambatanisho shilingi bilioni 11.78; katika hali isiyotarajiwa, baadhi ya halmashauri katika halmashauri 71 wamelipa jumla ya shilingi bilioni 10.08 kwa wazabuni bila kudai risiti za kielektroniki. Vilevile Wakurugenzi wa halmashauri 40 walilipa shilingi bilioni 1.70 bila viambatisho timilifu.

Mheshimiwa Spika, hoja hiyo imeongezeka kwa asilimia 67.15 ambapo, katika Mwaka wa Fedha 2020/2021, yalifanyika matumizi yasiyo na viambatisho ya shilingi bilioni 3.87 ikilinganishwa na shilingi bilioni 11.78 za mwaka 2021/2022. *(Makofi)*

(b) Ukiukaji wa Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura 410 na mapungufu katika usimamizi wa mikataba shilingi bilioni 106.

Mheshimiwa Spika, Ununuzi wa Umma ni shughuli ya kiuchumi inayohusisha sehemu kubwa ya Pato la Taifa *(GDP)*. Takribani asilimia 70 ya Bajeti ya Serikali na Taasisi zake hutumika kwenye manunuzi wa umma.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi uliofanywa na Kamati umebaini uwepo wa dosari nyingi za matumizi ya fedha za umma katika eneo la ununuzi ambapo, tatizo hili limesababishwa na Wakurugenzi na Maafisa Manunuzi kukiuka Sheria zilizotungwa na Bunge lako Tukufu kwa makusudi. Mambo yaliyojadiliwa ni kama ifuatavyo: -

(i) Ununuzi ulifanyika bila kuidhinishwa na Bodi ya wazabuni shilingi bilioni 5.7 zikihusisha halmashauri 23 sawa na asilimia 12.5 ya halmashauri zote 184. Mfano, Ileje shilingi milioni 348; Makambako Mji shilingi milioni 222; na Halmashauri ya Wilaya ya Tarime milioni 176.

(ii) Ununuzi uliofanywa nje ya mpango wa ununuzi wa Halmashauri, bilioni 14.02.

Mheshimiwa Spika, kinyume na Kanuni ya 69(3) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2013 pamoja na marekebisho yake ya mwaka 2016, Halmashauri 19 zilikiuka matakwa ya Kanuni tajwa hapo juu ambazo ni sawa na asilimia 10.3 ya Halmashauri zote.

Mheshimiwa Spika, tatu, baadhi ya Halmashauri Kufanya malipo kabla ya kupokelewa kwa bidhaa nunuliwa kwa thamani ya bilioni 3.29 ambapo wamebainika Wakurugenzi wa Halmashauri 26 ambazo ni sawa na asilimia 14.1 ya *Halmashauri zote walifanya utumbo huu.* **[Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

Mheshimiwa Spika, Nne, mikataba ambayo haikuhakikiwa na Mwanasheria bilioni 6.68. Wakurugenzi 20 waliingia mikataba bila ya mikataba hiyo kuhakikiwa na Mwanasheria. Mfano wa Halmashauri zilizoingia ni kama ifuatavyo:-

Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam bilioni 2.93, Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema milioni 549 na Halmashauri ya Wilaya ya Kyerwa milioni 320.

Mheshimiwa Spika, Tano, ununuzi uliofanyika bila ushindanishi wa bei bilioni 7.45. Asilimia 24.5 ya Halmashauri zote 184 zimekosa haki ya kupata bei shindani. Mfano wa Halmashauri zilizofanya ununuzi ni kama zifuatazo:- Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe milioni 800, Halmashauri ya Wilaya ya Bunda kwa Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere hapa ni milioni 576, Halmashauri ya Wilaya ya Ileje milioni 283, Halmashauri ya Mji wa Tunduma milioni 257 na Halmashauri ya Wilaya ya Uvinza milioni 173.

Mheshimiwa Spika, tunasema tutataja mpaka watu wanyooke. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, ununuzi kufanyika nje ya Mfumo wa Manunuzi wa Kielektroniki *(TANePS)*. Katika ukaguzi wa hesabu zilizoishia mwezi Juni, Halmashauri kadhaa zimefanya ununuzi nje ya mfumo wa *TANePS* kinyume na Sheria ya Ununuzi wa Umma. Mfano ni Halmashauri ya Wilaya ya Maswa bilioni 6.99, Halmashauri ya Wilaya ya Temeke bilioni Mbili na Halmashauri ya Mji wa Tarime milioni 1.3. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Halmashauri kufanya ununuzi nje ya mfumo kunapelekea uwepo wa urasimu na mazingira ya rushwa, upendeleo na ukiukwaji wa sheria.

Mheshimiwa Spika, Saba, mapungufu katika mchakato wa zabuni, taratibu za ununuzi na usimamizi wa mikataba. Ukaguzi ulibaini mapungufu katika miradi yenye thamani ya Shilingi milioni tatu na elfu moja inayotekelezwa na Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe ambapo, Halmashauri ilisaini mkataba na Mkandarasi ambaye hakukidhi vigezo. Hali kadhalika Halmashauri ya Jiji la Arusha ilitoa zabuni ya bilioni 3.9 kwa ajili ya ujenzi wa jengo la *OPD* katika Hospitali ya Jiji la Arusha kwa M/S B. H. Ladwa Ltd ambae hakushinda zabuni hiyo.

Mheshimiwa Spika, changamoto kama hizi ipo pia katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu, Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi, Halmashauri ya Wilaya ya Maswa, Halmashauri ya Mji Mbinga, kama zilivyofafanuliwa katika taarifa kubwa.

(c) kutolipwa kwa malimbikizo ya mishahara na madai ya wafanyakazi bilioni 119.94.

Mheshimiwa Spika, madeni ambayo hayajalipwa kwa muda mrefu ni pamoja na malimbikizo ya mishahara bilioni 42.25, posho za likizo bilioni 12.12, gharama za uhamisho bilioni 22.9, posho ya kujikimu bilioni 4.8, posho ya samani bilioni 4.4, posho ya makazi bilioni mbili, posho ya matibabu bilioni mbili, mafunzo bilioni 1.2 na malimbikizo mengine bilioni 27.9.

(d) Kutopeleka makato ya Watumishi kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na Taasisi nyingine Bilioni 260.07.

Mheshimiwa Spika, hoja hii inazihusu halmashauri 37 ambazo hazikuchangia michango ya kisheria na kuzalisha deni la bilioni 260 ambapo michango ya lazima ni bilioni 1.36 na adhabu ya kutopeleka michango ni bilioni 258. Mifano ni Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga ililazimika kutakiwa kulipa adhabu ya bilioni 3.137. Vilevile, Halmashauri ya Wilaya ya Bunda imetakiwa kulipa faini ya Shilingi milioni 114 kutokana na kutowasilisha michango kwa muda mrefu.

(e) Ucheleweshwaji wa Malipo kwa Wazabuni na Wakandarasi.

Mheshimiwa Spika, hili ni tatizo kubwa karibia Halmashauri zote, ni tatizo pia kwa upande wa Serikali Kuu. Imekuwa ni desturi kwa Halmashauri nyingi kuua biashara za wazabuni wazawa kwa kutowalipa madeni yao kwa wakati. Halmashauri zinazoongoza kudaiwa na Wazabuni ama Wakandarasi ni Halmashauri ya Wilaya ya Iringa bilioni 2.86, Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino bilioni 2.84, Halmashauri ya Mji Tarime bilioni 1.734 na Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni bilioni 1.732.

(f) Kutorejeshwa kwa fedha zilizotolewa kama mkopo kwenye vikundi shilingi bilioni 88.42 na uwepo wa vikundi hewa.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa hoja hii, Halmashauri 180 sawa na asilimia 97.8 ya Halmashauri zote, zimeshindwa kukusanya marejesho ya mikopo kwa muda mrefu. Deni hilo limeongezeka kutoka bilioni 47.01 iliyoripotiwa katika mwaka wa fedha ulioishia Juni, 2021 hadi bilioni 88.42. Ongezeko hili ni sawa na asilimia 47.

Mheshimiwa Spika, aidha, Halmashauri zimeongezeka kutoka 155 hadi 180. Hiki ni kiashiria cha uwepo wa tatizo sugu kwenye Halmashauri zetu, Mikoa yetu na TAMISEMI wenyewe. Mfano, Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni bilioni 7.86, Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam bilioni 5.56, Halmashauri ya Temeke bilioni 2.89, Halmashauri ya Jiji la Arusha bilioni 2.71, Jiji la

Tanga bilioni 1.31 na Mbarali bilioni 1.16. Tumesema tutataja mpaka mnyooke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Fedha kutopeleka Fedha za Miradi.

Mheshimiwa Spika, Kamati imekutana na changamoto ya kusimama kwa miradi mingi ya maendeleo inayotekelezwa katika Halmashauri kutokana na Wizara ya Fedha kutopeleka fedha. Mfano wa Halmashauri zilizopokea ruzuku ya maendeleo pungufu ya bajeti kutoka Serikali Kuu ni kama ifuatavyo:-

Halmashauri ya Wilaya ya Ileje pungufu kwa asilimia 63, Halmashauri ya Wilaya ya Hanang' pungufu kwa asilimia 58, Jiji la Dar es Salaam pungufu kwa asilimia 53 na Halmashauri ya Wilaya ya Tarime pungufu kwa asilimia 39. Kutopeleka fedha za maendeleo katika Halmashauri kunakwamisha ukamilishaji uliopangwa wa miradi ya maendeleo. *(Makofi)*

Halmashauri kutochangia mapato yake ya ndani katika Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Mwongozo wa Ofisi ya Rais TAMISEMI umezielekeza Halmashauri kutenga asilimia 40 au asilimia 60 kutokana na vigezo ambavyo imevitoa ya mapato yake ya ndani kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Hata hivyo, Halmashauri nyingi badala ya kupeleka fedha kwenye miradi ya maendeleo zimekuwa zikitumia fedha hizo kwenye matumizi ya kawaida. Mfano wa Halmashauri hizo ni Halmashauri ya Wilaya ya Bunda haikupeleka asilimia 84, Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino haikupeleka asilimia 78, Halmashauri ya Uvinza haikupeleka asilimia 54, na Halmashauri ya Rorya haikupeleka asilimia 49.8.

Mheshimiwa Spika, kwa Halmashauri 74 tulizokutana nazo, jumla ya bilioni 13.4 hazikupelekwa katika miradi ya maendeleo kutoka katika vyanzo vya ndani.

Mheshimiwa Spika, kuna hoja ya kutokamilika kwa miradi ya maendeleo kwa wakati eneo hili linahusu shilingi bilioni 112.24, ikiongozwa na: Jiji la Tanga imetumia bilioni 9.62 lakini miradi haijakamilika, Muleba ilipokea bilioni 2.06 kutekeleza miradi 17

haijakamilika. Igunga ina miradi 27 iliyopaswa kutekelezwa kati ya 2015/2016 mpaka 2020/2021 yenye thamani ya shilingi bilioni 1.07 na wenyewe hawajatekeleza. Mengi ya miradi hiyo ni maboma ya zahanati yaliyojengwa kwa nguvu za wananchi kuanzia mwaka 2000, 2015 mingine hadi 2021, hii ni aibu!

Pangea *Mineral Limited* kugoma kutoa fedha kwa ajili ya mradi wa Hospitali ya Manispaa ya Kahama.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Madini iliandika barua yenye Kumbukumbu Namba AB. 112/250/01C/16 ya Tarehe 21 Machi, 2022 kwa Halmashauri ya Manispaa ya Kahama ikiwataka Pangea *Mineral Limited* walipe shilingi bilioni 3.985 kwa ajili ya kusaidia ujenzi wa jengo la wagonjwa wa nje na wodi ya wazazi ikiwa ni fedha kwa ajili ya mpango wa kufunga mgodi wa Buzwagi. Hata hivyo, Pangea imekataa kutekeleza hoja hiyo na maelekezo hayo na imeilipa Kahama shilingi milioni 805.6 peke yake na kugoma kutoa zingine.

Mheshimiwa Spika, tunaitaka Serikali ichukue hatua za maksudi ili kuhakikisha deni hilo linalipwa kwa Halmashauri ya Kahama ili miradi iliyopangwa itekelezwe. *(Makofi)*

Utendaji usioridhisha wa baadhi ya Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, wakati wa mahojiano na Wakurugenzi wa Halmashauri za Wilaya ya Nkasi, Kibaha na Kigoma, tulibaini kuwepo utendaji usioridhisha wa Halmashauri hizo pamoja na uwepo wa viashiria vya ubadhirifu wa fedha za umma, kama ilivyofafanuliwa katika taarifa kubwa. Kamati tutaliomba Bunge ili kuiomba Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kufanya ukaguzi maalum katika Halmashauri hizo kuanzia kipindi cha 2019/2020 hadi 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, kuna changamoto Bohari Kuu ya Dawa kutopeleka dawa yenye thamani ya shilingi bilioni 8.16. Mfano wa Halmashauri ambazo hazikupokea dawa ni Halmashauri ya Temeke bilioni 3.4, Jiji la Dar es Salaam bilioni 2.9 na Sengerema bilioni 1.04 lakini tatizo hili ni la nchi nzima. Kamati hairidhishwi na utendaji wa *MSD* katika eneo hili kwa kuwa katika taarifa iliyopita deni lilikuwa ni bilioni 1.17 imeongezeka toka 1.17 mpaka 8.16. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna upungufu mkubwa sana katika shughuli za ufuatiliaji katika Sekretarieti ya Mikoa. Tumeandika kwa ufasaha kabisa kwenye taarifa yetu ndefu, kwa sababu ya muda tunaomba mfuatilie lakini kwa ufupi ni kwamba Kamati hairidhishwi na namna Makatibu Tawala wanavyosimamia Halmashauri zao, kutokana na Halmashauri hizo kuwa na utendaji usioridhisha na hakuna hatua zozote zinazochukuliwa na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa juu ya watumishi wanaobainika kwenda kinyume na taratibu za utumishi.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mapendekezo ya Kamati. Kuhusu Mifumo dhaifu ya ukusanyaji wa mapato pamoja na kushindwa kukusanya mapato, Bunge liazimie kwamba:

a) Serikali iandae mikataba ya utendaji kazi na ukusanyaji wa mapato ya ndani itakayokuwa vigezo *(key performance indicators)* kwa Wakurugenzi wote. Aidha katika kila robo mwaka, kila Katibu Tawala Mkoa afanye tathmini iwapo Wakurugenzi hao wamefikia malengo ya ukusanyaji wa mapato na kuwasilisha taarifa hizo Ofisi ya Rais – TAMISEMI;

b) Serikali kupitia TAMISEMI ihakikishe fedha zote zilizokusanywa kupitia mashine za *(POS)* shilingi bilioni 11.07 zinawasilishwa Benki kabla ya mwezi Aprili, 2024;

c) Serikali ihakikishe kiasi cha shilingi bilioni 37.34 kutoka katoka vyanzo muhimu vya mapato ya ndani ambavyo havijakusanywa vinakusanywa;

d) Kila Mkurugenzi wa Halmashauri kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mapato Tanzania, wahakikishe kunakuwa na taarifa sahihi kuhusu mauzo ghafi ya wafanyabiashara waliosajiliwa ili kukusanya ushuru wa huduma kwa mujibu wa Sheria;

Mheshimiwa Spika, kuhusu matumizi yasiyofaa ya fedha za umma. Bunge liazimie kwamba:

a) Serikali iwachukulie hatua za kinidhamu watumishi wote waliofanya malipo ya fedha taslimu kwa kiasi kilichohojiwa cha bilioni 1.51;

b) Serikali ichukue hatua za kinidhamu na kisheria kwa watu wote waliofanya matumizi ya shilingi bilioni 11.78 bila ya nyaraka;

c) Serikali ichukue hatua kwa watumishi wa Halmashauri waliotumia shilingi bilioni 7.7 kutoka katika akaunti ya amana;
d) Serikali ielekeze Makatibu Tawala Mikoa kufuatilia na kuhakikisha watumishi wa Halmashauri waliofanya matumizi yasiyo na tija ya shilingi milioni 898.85 wanachukuliwa hatua za kinidhamu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Ukiukwaji wa Sheria ya Ununuzi wa Umma. Bunge liazimie:

a) Mamlaka ya Usimamizi wa Ununuzi wa Umma ifanye ukaguzi wa kina katika maeneo yote yaliyobainishwa katika ripoti ya Mkaguzi Mkuu ambayo yameonesha ukiukwaji wa sheria ikiwemo matumizi ya *force account* na kuchukua hatua ipasavyo.

b) Serikali ihakikishe inalipa madeni ya Wakandarasi na Wazabuni yenye jumla ya shilingi bilioni 7.8;

c) Serikali ihakikishe waliosababisha hasara kwa kufanya ununuzi wa vifaa vya ujenzi zaidi ya mahitaji kama ilivyoainishwa katika ripoti ya CAG wanachukuliwa hatua;

d) Serikali ihakikishe bidhaa zilizolipiwa kabla ya kupokelewa za bilioni 3.9 zinapokelewa na kuhakikiwa kwa mujibu wa mikataba.

Mheshimiwa Spika, kushindwa kulipa madeni *(Payables)*. Bunge liazimie kwamba;

a) Serikali Kuu na Halmashauri zilipe malimbikizo ya Mishahara na Madai ya Wafanyakazi ya bilioni 119.94;

b) Serikali ifanye uchambuzi wa madeni ya wastaafu wote nchini waliohudumu katika Mamlaka za Serikali za Mitaa na kuwalipa madeni yao haraka iwezekanavyo;

c) Wakurugenzi wote wa Halmashauri wahakikishe wanasilisha makato ya Watumishi kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na Mfuko wa Bima ya Afya kwa mujibu wa Sheria na kuhakikisha deni la shilingi bilioni 260.07 linalotokana na kutowasilishwa kwa michango linalipwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Uendeshaji usiofaa wa Mfuko wa Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu. Bunge linaazimia kwamba:

a) Kwanza Halmashauri zichangie asilimia 10 kama inavyotakiwa;

b) Wakurugenzi wahakikishe kiasi cha shilingi bilioni 88.42 kilichokopeshwa katika vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kinakusanywa kabla ya mwezi Juni, 2024;

Mheshimiwa Spika, kuhusu mapungufu katika utekelezaji wa miradi ya Maendeleo. Bunge liazimie kwamba:

a) Wizara ya Fedha ipeleke katika Halmashauri fedha za utekelezaji wa miradi ya maendeleo kama ilivyoidhinishwa na Bunge pamoja na kukamilisha utoaji wa fedha za miradi yote ambayo haijakamilika;

b) Serikali isimamie na kuhakikisha deni la Pangea *Mineral Limited* la shilingi bilioni 3.179 linalipwa kwa Halmashauri ya Wilaya ya Kahama;

c) Ofisi ya Rais TAMISEMI kwa kushirikiana na Makatibu Tawala Mkoa wahakikishe fedha zote za miradi ya maendeleo zilizobadilishiwa matumizi bila ya kupata

kibali cha Wizara ya Fedha zinarejeshwa ili ziweze kutumika katika kutekeleza miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utendaji usiyoridhisha na baadhi ya Halmashauri, Bunge linaazimia kwamba; moja, Kuiomba Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, kufanya Ukaguzi Maalumu katika Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi, maelezo yote kuhusiana na halmashauri na hadidu za rejea zipo kwenye taarifa kubwa, zichukuliwe na *Hansard* kama sehemu ya taarifa hii; Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kuomba kufanya Ukaguzi Maalumu kwa Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha, maelezo yote ya Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha yachukuliwe kama yalivyo kwenye Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, mwisho, kuomba Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kufanya Ukaguzi Maalumu katika Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma. Vilevile kwa sababu ya muda maelezo yote, yachukuliwe kama yalivyo kwenye Taarifa Kuu ya Kamati ili Mkaguzi Mkuu aweze kwenda kufanya Ukaguzi Maalumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu utendaji katika Sekta ya Afya, Bunge linaazimia Bohari Kuu ya Madawa *(MSD)* ipeleke dawa na vifaa tiba vyenye thamani ya shilingi milioni 8.16 ambavyo vimeshalipiwa kwa kuzingatia maombi ya halmashauri. Vilevile *(MSD)* ipeleke dawa kwa wakati na vifaa tiba kila inapokuwa vimelipiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, Serikali ifanye tathimini ya kina juu ya uwezo wa watumishi wanaopewa jukumu la kujaza fomu za Bima ya Afya na kuwachukulia hatua stahiki watumishi wote wataobainika kusababisha hasara ya shilingi bilioni 1.77; na Halmashauri zote nchini kutopokea dawa kutoka *(MSD)* ambazo muda wake wa matumizi ni chini ya miezi sita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu upungufu wa ufuatiliaji katika Sekretarieti za Mikoa, Bunge liazimie kwamba: -

(a) Serikali ihakikishe inaziwezesha ipasavyo Sekretarieti za Mikoa kwa kuzipatia watalamu wa kutosha na vitendea kazi kwa ajili ya ufuatiliaji kwenye halmashauri zote ndani ya mikoa yao.

(b) Kila Katibu Tawala Mkoa *(RAS)* awe na utaratibu wa kukutana na Wakurugenzi wote mara kwa mara ili kufanya tathmini ya utendaji wa halmashauri, utekelezaji wa hoja na mapendekezo ya *CAG* pamoja na utekelezaji wa mapendekezo ya *LAAC* na kuwasilisha Taarifa Ofisi ya Rais, TAMISEMI. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu utekelezaji wa mapendekezo yote yaliyotolewa katika Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu ya za Serikali, kuhusu Hesabu za Serikali za Mitaa, Bunge linaazimia Serikali itekeleze kikamilifu mapendekezo yote yaliyotolewa na *CAG* katika hesabu hizi za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha ulioishia Juni, 2022.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nitumie nafasi hii kuhitimisha kwa kukupongeza sana wewe, Mwalimu wangu kuwa Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani *(IPU)*. Hakika unatosha. Umahiri wako katika kutekeleza majukumu yako imeonekana duniani. Vilevile napenda kukushukuru wewe binafsi kwa uongozi wako thabiti ambao umeiwezesha Kamati yangu kutekeleza majumu yake kikamilifu bila ya vikwazo kwa kutoa maelekezo na miongozo muhimu katika Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawashukuru Wajumbe wangu wa Kamati, wapendwa sana, kwa kuwa wavumilivu na kutekeleza majukumu ya Kamati hii kwa ufanisi na weledi mkubwa. Majina yao natamani kuyataja, ila naomba yaingie kwenye *Hansard* kwa ajili ya muda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Bi. Nenelwa Mwihambi, *ndc*. kwa ushauri wake kwa Kamati pamoja na wasaidizi wake wote kwa kuratibu shughuli za Kamati na kufanikisha kusomwa kwa taarifa hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho, japo siyo kwa umuhimu, Kamati inatambua na kuthamini ushirikiano mkubwa tunaopata kutoka kwa Ofisi ya *CAG,* na kwa namna ya kipekee Mdhibiti mwenyewe na Mkaguzi Mkuu *(CAG)* Ndugu Charles Kichere. Aidha, napenda kuishukuru Ofisi ya Rais, TAMISEMI pamoja na Wizara ya Fedha kwa ushirikiano mkubwa mliotupa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawashukuru Wabunge wote kwa kunisikiliza.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**TAARIFA YA KAMATI KUHUSU RIPOTI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI KWA HESABU ZILIZOKAGULIWA ZA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA KWA MWAKA WA FEDHA ULIOISHIA TAREHE 30 JUNI, 2022 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

***(Inatolewa chini ya Kanuni ya 136 (16) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023)***

**SEHEMU YA KWANZA**

**1.0 MAELEZO YA JUMLA**

**1.1. Utangulizi**

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati kuhusu Hesabu za Serikali kwa Hesabu zilizokaguliwa za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2022 na kuliomba Bunge liipokee na kuijadili. Madhumuni ya Taarifa hii ni kulijulisha Bunge lako tukufu, iwapo fedha za umma zimetumika kwa mujibu wa Sheria na taratibu zilizowekwa kwa ajili ya ustawi wa wananchi.

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa hii inafafanua Hesabu za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa fedha unaoishia Tarehe 30 Juni, 2022 zilizokaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Uchambuzi umejikita katika kuangalia mifumo ya uwajibikaji na kuhakikisha viongozi waliopewa dhamana wanatumia rasilimali za nchi kwa mujibu wa Sheria na taratibu zilizowekwa pamoja na kuhakikisha dosari katika matumizi ya fedha za umma zinafanyiwa kazi na kuondolewa.

**1.2. Muundo wa Taarifa**

**Mheshimiwa Spika**, kwa muktadha wa ufuatiliaji wa taarifa hii, Kanuni ya 142 ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari, 2023 imeweka sharti la muundo wa Taarifa ya Kamati inayowasilishwa Bungeni. Kwa mantiki hiyo, naomba

kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuhusu sehemu kuu tatu zikihitimishwa na sehemu ya nne yenye shukrani na utoaji wa hoja. Sehemu ya kwanza ni maelezo ya jumla ikijumuisha muundo wa Taarifa, majukumu ya Kamati, msingi wa kazi za Kamati, muhtasari wa matokeo ya Uchambuzi wa Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na ufuatiliaji wa mapendekezo yaliyotolewa na Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, sehemu ya pili inahusu uchambuzi wa Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Hesabu za Mamlaka za Serikali za Mitaa. Katika sehemu hii, Taarifa inabainisha mambo muhimu kuhusu uchambuzi pamoja na matokeo ya uchambuzi huo, lengo ikiwa ni kuonesha maeneo yenye matumizi mabaya ya fedha za umma kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022. Aidha, sehemu hii inajenga msingi wa sehemu ya Tatu inayohusu Maoni na Mapendekezo.

**1.3. Majukumu ya Kamati**

**Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa majukumu ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa ni kwa mujibu ya Kifungu cha 14 cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari, 2023. Kwa mujibu wa Kifungu hicho, majukumu ya Kamati ni yafuatayo: -

a) Kushughulikia maeneo yenye matumizi mabaya ya fedha za Serikali za Mitaa yaliyoainishwa katika Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali;

b) Kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo yaliyokwishatolewa na Kamati ili kuondoa matatizo hayo; na

c) Kutoa mapendekezo na ushauri kwa Serikali za Mitaa kuhusu matumizi mazuri ya fedha ili kuhakikisha kwamba, tatizo la matumizi mabaya ya fedha za Umma linapungua.

**Mheshimiwa Spika**, Msingi wa majukumu hayo unatokana na Taarifa ya Hesabu zilizokaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kama ilivyobainishwa katika Kifungu cha 15 cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023.

### 1.4. Njia Zilizotumika Katika Utekelezaji wa Kazi za Kamati

**Mheshimiwa Spika**, Pamoja na mambo mengine yaliyoainishwa katika Kanuni ya 142 (a) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari, 2023, Taarifa inatakiwa kubainisha njia au mbinu zilizotumika na Kamati katika kutekeleza majukumu yake. Kwa msingi huo, naomba kuzitaja njia na mbinu zilizotumika katika kutekeleza majukumu ya Kamati na kukamilisha Taarifa hii kama ifuatavyo: -

a) Mapitio ya jumla ya Ripoti Kuu ya Mwaka ya CAG kuhusu Hesabu za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Lengo lilikuwa ni kubaini maeneo yenye matatizo katika mapato na matumizi ya fedha za umma katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha husika;

b) Kupokea Taarifa fupi za CAG (*Briefs*) ambazo zinaonesha utekelezaji wa Mapendekezo ya Kamati, Hoja za ukaguzi na Mapendekezo ya CAG kuhusu Hesabu za Halmashauri husika. Taarifa hizi huwaweka Wajumbe katika nafasi nzuri ya kuzielewa hoja kwa undani wake na kubaini maeneo yenye matumizi mabaya ya fedha za umma;

c) Mahojiano na Wakurugenzi kuhusu hoja zilizobainishwa katika Ripoti ya CAG ili kubaini chimbuko la dosari pamoja na athari iliyotokana na matatizo ya matumizi mabaya ya fedha za umma; na

d) Uchambuzi wa kina wa Taarifa za wakaguzi, majibu ya Wakurugenzi wa Halmashauri iliyokaguliwa pamoja na mashauriano na Wadau wengine kuhusu hoja za Ukaguzi zilizojitokeza. Lengo ni kuelewa kwa kina msingi wa hoja na namna ya kupunguza matatizo ya matumizi mabaya ya fedha za Umma.

**Mheshimiwa Spika**, njia na mbinu hizo ziliiwezesha Kamati kufanya uchambuzi wa kina wa Taarifa ya Hesabu za Halmashauri zilizokaguliwa na CAG kwa lengo la kulishauri Bunge juu ya hatua za kuchukua. Ili kuhakikisha kunakuwa na usimamizi mzuri wa matumizi ya fedha za umma, Kamati ilifanya rejea ya Sheria, Kanuni na Miongozo mbalimbali kama ifuatavyo: -

a) Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977;
b) Sheria ya Ukaguzi wa Umma (Sura ya 418) na kanuni zake za Mwaka 2009;
c) Sheria ya Fedha za Halmashauri (Sura ya 290) na Mwongozo wa Matumizi ya fedha katika Serikali za Mitaa (*the Local Government Financial Memoranda*);
d) Sheria ya Ununuzi wa Umma (Sura ya 410) na kanuni zake, (kama zilivyo boreshwa mwaka 2016);
e) Sheria ya Bajeti (Sura ya 439) na kanuni zake, 2015;
f) Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki ya Bunge, Sura 296;
g) Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023; na
h) Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma, 2009.

**1.5. Muhtasari wa Matokeo ya Utekelezaji wa majukumu ya Kamati**

**Mheshimiwa Spika**, Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 imeelezea Mamlaka, Majukumu na Wajibu wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali katika kuhakikisha kunakuwa na uwajibikaji na uadilifu katika usimamizi wa rasilimali za Umma. Kwa muktadha huo, kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2022, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali alifanya ukaguzi na kutoa ripoti katika jumla ya Mamlaka 184 za Serikali za Mitaa.

**Mheshimiwa Spika**, tarehe 06 Aprili, 2023, Serikali iliweka mezani Ripoti mbalimbali za CAG. Miongoni mwa Ripoti hizo ilikuwa ni Ripoti Kuu ya Mwaka ya Ukaguzi wa Hesabu za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Kwa mujibu wa Kanuni ya 43 (1) & (8) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, Ripoti hiyo hujadiliwa na kuwasilishwa Bungeni na Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC).

**Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza wajibu wa Bunge wa kikatiba wa kufuatilia nidhamu ya mapato na matumizi katika Halmashauri na kwa kuzingatia Kifungu cha 14 cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari, 2023, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa ilifanikiwa kuchambua na kujadili Taarifa za Hesabu zilizokaguliwa na kufanya mahojiano na Wakurugenzi wa jumla ya **Halmashauri 74** ambazo ni sawa na **Asilimia 40.2** ya Halmashauri zote 184.

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi wa kina wa hoja zilizofanyiwa kazi na Kamati umefafanuliwa katika sehemu ya pili ya taarifa hii.

### 1.6. Ufuatiliaji wa Maazimio ya Bunge na Mapendekezo yaliyotolewa na Kamati

**Mheshimiwa Spika**, Mwezi Juni 2023, Kamati ilipata fursa ya kipekee ya kufuatilia utekelezaji wa Maazimio Kumi na Mbili (yenye vipengele Kumi na Tatu) ya Bunge yaliyotokana na Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa ukaguzi wa Hesabu za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Katika kutekeleza jukumu hilo, Kamati haikuridhishwa na namna Serikali imetekeleza Maazimio yaliyotolewa na Bunge kwa kutotekeleza Maazimio yote kikamilifu.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na mambo mengine, Kifungu cha 14 (b) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari, 2023 kimeipa LAAC jukumu la kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo yaliyokwishatolewa na Kamati ili kuondoa matatizo ya matumizi mabaya ya fedha za umma.

**Mheshimiwa Spika**, jukumu hili hutekelezwa kwa CAG kufanya uhakiki wa maoni na mapendekezo yaliyotolewa na Kamati kwa Halmashauri husika. Aidha, Kamati hupata nafasi ya kupitia taarifa ya utekelezaji wa maoni na mapendekezo yaliyotolewa kila inapokutana na Halmashauri husika kupitia '*briefs*' za CAG.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 UCHAMBUZI WA RIPOTI KUU YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI YA UKAGUZI WA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

### 2.1 Maelezo ya jumla

**Mheshimiwa Spika**, Madaraka na majukumu ya Bunge katika kusimamia matumizi ya fedha za umma yapo kwa mujibu wa Katiba, Sheria na Kanuni mbalimbali za Nchi. Katika kuhakikisha utekelezaji wa madaraka na majukumu hayo na kuliwezesha Bunge kufuatilia matumizi ya rasilimali za umma pamoja na kukamilisha mnyororo wa uwajibikaji, Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 imempa

CAG Mamlaka ya kuwasilisha ripoti yake Bungeni ili iweze kufanyiwa kazi na kupata Maazimio ya Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, katika kuhakikisha mapendekezo yanayotolewa na CAG yanashughulikiwa kikamilifu ili kuondoa matatizo yaliyobainika na kujiridhisha juu ya ufanisi wa mamlaka hizo katika kukusanya na kutumia fedha za umma, Kamati ilichambua Ripoti Kuu ya Mwaka ya CAG kuhusu Hesabu za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Baada ya uchambuzi huo na kwa kutumia Kanuni ya 109 ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari, 2023 ukaelekeza Taarifa hii ipangwe kwenye Orodha ya Shughuli za leo.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kulijulisha Bunge lako tukufu kuhusu uchambuzi wa Ripoti ya CAG ambao ndio msingi wa mapendekezo ya Kamati yanayowasilishwa kwa njia ya Hoja kama ilivyoelekezwa na Kanuni ya 61 ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari, 2023.

### 2.2 Vigezo vya Uchambuzi

**Mheshimiwa Spika**, ili kufikia malengo ya Bunge katika kusimamia eneo la matumizi ya fedha za umma katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa, uchambuzi wa Ripoti ya CAG ulifanyika kwa kuzingatia vigezo muhimu vilivyowekwa na Kamati ili kubaini maeneo yenye matumizi mabaya ya fedha za umma. Vigezo hivyo vilitumika katika kutoa mwelekeo na mwongozo wa Halmashauri ambazo zilipewa kipaumbele katika uchambuzi wa Taarifa za Hesabu zilizokaguliwa (*individual financial statements*) pamoja na kufanya mahojiano na Wakurugenzi wa Halmashauri.

**Mheshimiwa Spika**, vigezo vilivyozingatiwa wakati wa uchambuzi wa Ripoti ya CAG pamoja na kuchagua vipaumbele katika utekelezaji wa shughuli za Kamati vilikuwa kama ifuatavyo: -

a) Uzito wa hoja ya ukaguzi kama ilivyoibuliwa na CAG;
b) Maslahi ya Umma kuhusu hoja za Halmashauri husika;
c) Hali ya hati ya ukaguzi iliyotolewa kwa Halmashauri husika;
d) Kujirudia mara kwa mara kwa hoja husika katika Halmashauri au Mradi wa Maendeleo uliokaguliwa;
e) Kiwango cha fedha kinachohusika katika hoja za ukaguzi wa Halmashauri husika; na

f) Kuleta uendelevu wa ufuatiliaji wa ushauri na maelekezo yaliyotolewa na Kamati kwa Halmashauri husika kwa siku za nyuma.

**Mheshimiwa Spika**, uwepo wa vigezo hivyo umerahisisha mchakato wa Kamati wa kufuatilia matumizi ya fedha za umma katika Halmashauri. Kukosekana kwa vigezo hivyo kusingeiwezesha Kamati kufikia malengo yake ya kubainisha maeneo ya matumizi mabaya ya fedha za umma.

**2.3 Matokeo ya Uchambuzi**

**Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2022, CAG alikagua jumla ya Halmashauri 184. Kati ya Hizo, Halmashauri 170 sawa na 92.39% zilipata Hati zinazoridhisha za ukaguzi, Halmashauri 13 sawa na 7.06% zilipata Hati zenye Shaka za ukaguzi, Halmashauri 1 sawa na 0.54% ilipata Hati Mbaya ya ukaguzi. Orodha ya Hati hizo ni **kiambatisho namba 1** cha Taarifa hii.

Uchambuzi wa jumla wa Kamati umebaini kuwa, Idadi ya Halmashauri zilizopata Hati zinazoridhisha zimepungua kutoka Halmashauri 176 zilizotolewa katika mwaka wa fedha 2020/2021 hadi kufikia Halmashauri 170. Kwa upande wa Hati zenye shaka, idadi ya Halmashauri imeongezeka kutoka Halmashauri 8 kwa mwaka 2020/2021 hadi Halmashauri 13 kwa mwaka 2021/2022.

**Mheshimiwa Spika**, kwa muktadha ya uwasilishaji wa taarifa hii, uchambuzi wa Hesabu za Halmashauri kwa Mwaka wa Fedha ulioishia Tarehe 30 Juni, 2022, Kamati ilibaini maeneo Kumi muhimu yenye changamoto za matumizi mabaya ya fedha za umma ikiwa ni pamoja na kutokuwepo kwa mifumo thabiti ya udhibiti wa ndani, udhaifu wa mifumo ya uwajibikaji, ukiukwaji wa Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa Sura 290, ukiukwaji wa Sheria ya Ununuzi wa Umma Sura 410, ukiukwaji wa Kanuni za utoaji na usimamizi wa mikopo kwa vikundi vya wanawake, vijana, na watu wenye ulemavu ya mwaka 2019 pamoja na marekebisho yake ya mwaka 2021 pamoja na ukiukwaji wa Kanuni, na Miongozo mbalimbali inayotolewa na Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya utangulizi huo wa sehemu hii ya pili, mambo yafuatayo kuhusu matumizi na usimamizi wa fedha za umma katika Halmashauri yalibainika: -

**2.4 Mifumo dhaifu ya ukusanyaji wa Mapato ya ndani pamoja na kushindwa kukusanya Madai (Receivables)**

**Mheshimiwa Spika**, licha ya kwamba, mtazamo wa ujumla ni kuangalia namna Halmashauri zinavyotumia fedha za Umma, Kamati imejikita pia katika kuchambua ufanisi katika ukusanyaji wa mapato ya ndani kwa kuwa, matumizi hayawezi kufanyika kama yalivyopangwa ikiwa hakuna fedha zilizokusanywa.

Ili kujiridhisha iwapo Halmashauri zinatekeleza wajibu wake kikamilifu katika eneo hili, Kamati imefanya uchambuzi katika maeneo makuu mawili ya mtiririko wa mapato pamoja na Mifumo ya ukusanyaji wa mapato ili kujihakikishia iwapo shughuli zilizopangwa kufanyika katika Bajeti za Halmashauri zote nchini zinaweza kukamilika ikilinganishwa na mapato ya Halmashauri hizo. Mapungufu yaliyoibuliwa na Kamati katika eneo hili ni kama ifuatavyo: -

**2.4.1 Ukosefu wa Ubunifu wa vyanzo vipya vya Mapato ya Ndani**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imekuwa ikizitaka Halmashauri zote zinazofika kuhojiwa kuachana na fikra za kutegemea Ruzuku toka Serikali Kuu kwa kiasi kikubwa na badala yake wataalamu waliopewa madaraka watafakari na kuibua vyanzo vipya vya mapato ya ndani kulingana na fursa zinazopatikana katika maeneo yao ili kuipunguzia mzigo Serikali. Suala hili limetokana na ukweli kwamba, Halmashauri nyingi nchini zimeshindwa kufikia malengo ya ukusanyaji wa mapato ya kila mwaka.

Aidha, baadhi ya Halmashauri zina uwezo wa kukusanya zaidi mapato ya ndani lakini hazifanyi hivyo kutokana na Wizara ya Fedha kushusha ukomo wa bajeti (*ceiling*) kwa Halmashauri zote nchini ambapo, suala hilo linafanyika kwa mujibu wa Sera, Miongozo na Taratibu za bajeti zilizowekwa na IMF Kimataifa zinazoelekeza ongezeko la bajeti kwenda kidogo kidogo. Hali hii inatengeneza uzembe wa ukusanyaji wa mapato na kutoa mianya ya upotevu wa mapato hayo. Ni maoni ya Kamati kuwa, Serikali ifanye tathimini ya uwezo wa kila Halmashauri wa

kukusanya mapato ili iweze kuweka ukomo (ceiling) wa ukusanyaji kulingana na uwezo wa Halmashauri husika.

Mfano wa Halmashauri ambazo zimekusanya zaidi ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ni kama inavyooneka katika Jedwali namba 1

**Jedwali Na. 1**: Halmashauri zilizokusanya mapato ya ndani zaidi ya bajeti

| **S/N** | **Jina la Halmashauri** | **Makadirio yaliyopitishwa** (Sh.) | **Makusanyo halisi (Sh.)** | **Ziada (Sh.)** | **Asilimia** |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | H/Mbozi | 3,189,570,028 | 4,120,553,434 | 930,983,406 | 29 |
| 2. | H/W Ileje | 1,402,601,000 | 1,787,698,108 | 385,097,108 | 27 |
| 3. | H/W Bukoba | 1,863,000,000 | 2,206,317,104 | 343,317,104 | 18 |
| 4. | H/W Kyerwa | 2,653,439,360 | 3,057,241,900 | 403,802,540 | 15 |
| 5. | H/W Mbinga | 4,691,336,000 | 5,334,702,413 | 643,166,413 | 14 |
| 6. | H/W Geita | 4,639,333,853 | 5,213,864,682 | 574,530,828.76 | 12 |

Licha ya Kwamba, ukusanyaji wa mapato ya vyanzo vya ndani katika Halmashauri umeongezeka na kufikia **Shilingi Bilioni 891.84** katika mwaka wa fedha 2021/2022 ikilinganishwa na **Shilingi Bilioni 760.95** katika mwaka wa fedha 2020/2021, Kamati haijaridhishwa na mtiririko huo wa mapato kwa kuwa bado utegemezi wa ruzuku kutoka Serikali ni mkubwa sana.

Kwa mujibu wa taarifa ya OR – TAMISEMI iliyowasilishwa mbele ya Kamati, katika mwaka wa fedha unaojadiliwa 2021/2022, Halmashauri 184 zilipokea ruzuku kutoka Serikali kuu zenye jumla ya **Shilingi Trilioni 5.99**. Kati ya hizo **Trilioni 4.11** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **Shilingi Trilioni 1.88** zilikuwa ni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, hali hii lazima ibadilike kwa kuwa, Kamati inaamini kwamba, iwapo Wataalamu waliopewa Mamlaka wataamua kutumia taaluma zao ipasavyo na kuwa wabunifu, kutakuwa na mabadiliko makubwa katika utendaji wa Halmashauri. Hali itakayowezesha mapato ya Halmashauri kuongezeka.

**Jedwali Na. 2:** Mwenendo wa Mapato ya Ndani kwa kipindi cha miaka mitatu (2019/2020 – 2021/2022)

| Mwaka wa Fedha | Bajeti iliyoidhinishwa (Sh.) | Makusanyo halisi (Sh.) | Makusanyo Pungufu/Ziada (Sh.) | % (Tofauti/Bajeti) |
|---|---|---|---|---|
| 2019/20 | 759,907,423,938 | 709,573,567,541 | (50,333,856,397) | (7) |
| 2020/21 | 822,375,950,562 | 769,422,329,061 | (52,953,621,501) | (6) |
| 2021/22 | 873,898,493,691 | 891,836,133,308 | 17,937,639,617 | 2 |

*Chanzo:* ***Uk: 18 wa Ripoti Kuu ya Ukaguzi wa Serikali za Mitaa Mwaka 2021-22***

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi wa Taarifa za Halmashauri kuhusu mwenendo wa ukusanyaji wa mapato ya ndani kwa baadhi ya Halmashauri zilizofika mbele ya Kamati ambazo zilikusanya pungufu ya bajeti iliyoidhinishwa ni kama inavyoonekana katika Jedwali namba 3.

**Jedwali Na. 3**: Halmashauri zilizokusanya mapato ya ndani pungufu ya bajeti kwa mwaka wa fedha 2021/2022

| S/N | Jina la Halmashauri | Makadirio yaliyopitishwa (Sh.) | Makusanyo halisi (Sh.) | Upungufu (Sh.) | Asilimia |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | H/W Kilindi | 2,434,000,000 | 1,744,272,330 | 689,727,670 | 28 |
| 2. | H/Mji Handeni | 1,718,393,733 | 964,106,813 | 754,286,920 | 44 |
| 3. | H/W Kishapu | 4,538,685,148 | 3,062,855,274 | 1,475,829,874 | 33 |
| 4. | H/W Gairo | 1,420,310,000 | 1,097,425,192 | 322,884,808 | 23 |
| 5. | H/W Korogwe | 2,118,730,000 | 1,397,085,810 | 721,644,190 | 34 |
| 6. | H/W Bunda | 1,776,485,000 | 1,235,914,898 | 540,570,102 | 30 |
| 7. | H/W Itigi | 1,903,990,833 | 1,443,714,014 | 460,276,819 | 24 |

**Mheshimiwa Spika**, kutofikiwa kwa makusanyo ya mapato ya ndani katika Halmashauri hizo kunatokana na watendaji kukosa ubunifu katika kuhakikisha wanakusanya mapato ya ndani ya kutosha kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za Halmashauri pamoja na miradi ya maendeleo.

**2.4.2 Upotevu wa mapato ya Shilingi Bilioni 11.07 yaliyokusanywa kupitia Mashine za kukusanya mapato (POS) ambayo hayakuwasilishwa Benki**

**Mheshimiwa Spika**, imekuwa ni desturi ya Halmashauri nyingi nchini kutumia fedha mbichi ambapo, jumla ya Halmashauri 98 ambazo ni sawa na **Asilimia 53.2** hazikuwasilisha Benki fedha zilizokusanywa kupitia mashine za POS. Hii inatokana na uzembe wa Wakurugenzi wa Halmashauri kushindwa kufanya ufuatiliaji wa mara kwa mara kwa waliopewa jukumu la kukusanya mapato na kusababisha ubadhirifu wa fedha za umma.

Kutowasilishwa kwa fedha hizo ni ukiukwaji wa Kifungu cha 42 (2) cha Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura 290 ikiwa ni pamoja na kwenda kinyume na Aya ya 3.4 (v) ya Mwongozo wa Usimamizi wa Mapato ya Halmashauri wa Mwaka 2019, ambapo, Halmashauri zinapaswa kuchukua hatua stahiki za udhibiti, ikijumuisha uwekaji wa mapato yanayokusanywa benki kwa haraka ili kuimarisha mfumo wa ukusanyaji wa mapato.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini uwepo wa Halmashauri nyingi kwa upande mmoja kushindwa kutekeleza shughuli zake kikamilifu kutokana na kukosekana kwa fedha na upande mwingine kukusanya fedha bila ya kuziwasilisha benki kama Sheria inavyohitaji. Licha ya kuwa tatizo hili limepungua kutoka **Shilingi Bilioni 17** zilizoripotiwa katika ripoti ya CAG inayoishia tarehe 30 Juni, 2021, jambo hili haliwezi kuendelea kuvumiliwa kwa kuwa kunatia shaka juu ya usalama wa fedha hizo na kunasababisha upotevu wa fedha za Umma. Mfano wa Halmashauri ambazo hazikuwasilisha benki fedha zilizokusanywa kwa POS ni kama zinavyoonekana katika Jedwali Na. 4.

**Jedwali Na. 4**: Halmashauri zilizokusanya mapato kupitia POS bila ya kuziwasilisha Benki

| Na | Jina la Halmashauri | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | H/Jiji Dar es Salaam | 1,047,974,053 |
| 2. | H/W Uvinza | 569,733,796 |
| 3. | H/W Ushetu | 399,898,950 |

| | | |
|---|---|---|
| 4. | H/M Kinondoni | 335,077,075 |
| 5. | H/W Bunda | 264,315,158 |
| 6. | H/W Kilindi | 250,049,535 |
| 7. | H/M Iringa | 217,739,927 |
| 8. | H/W Musoma | 194,692,833 |
| 9. | H/W Itigi | 176,512,104 |
| 10. | H/W Mbozi | 135,719,340 |

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imewaelekeza Wakurugenzi wote kuzingatia taratibu za fedha na kuacha matumizi ya fedha mbichi kwa kuongeza udhibiti katika ukusanyaji wa mapato ya ndani na kuchukua hatua stahiki kwa watakaohusika na ukiukwaji wa sheria na taratibu hizo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati pia haijaridhishwa na hali iliyopo hivi sasa ambapo Wakurugenzi wengi wa Halmashauri wamekuwa wakieleza kuwa, wengi waliohusika kesi zao zipo TAKUKURU. Hata hivyo hakuna hatua zinazochukuliwa kutokana na TAKUKURU kuchukua muda mrefu kutoa maamuzi ya kiuchunguzi. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, Wakurugenzi wamekuwa wakitumia TAKUKURU kama kichaka cha kutochukua hatua dhidi ya wakusanya mapato ambao wamekusanya pesa na kuzitumia katika matumizi mengineyo badala ya kuziwasilisha benki.

**2.4.3 Mawakala wa Ukusanyaji wa Mapato kutowasilisha kiasi cha Shilingi Bilioni 4.94**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inapata mashaka na namna Mawakala wa ukusanyaji wa mapato katika Halmashauri wanapatikana na wanasimamiwa na Wakurugenzi kutokana na fedha nyingi kupotea katika mikono ya mawakala hao bila ya kuchukuliwa hatua kwa muda mrefu. Aidha, Kamati imebaini Wakurugenzi kushindwa kufanya upembuzi yakinifu juu ya hali halisi ya vyanzo vya mapato kabla ya kuingia mikataba na wakusanya mapato. Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura ya 290 katika Kifungu cha 26 (a) na (b) kinamtaka mtu anayestahili kuteuliwa na Halmashauri, kukusanya na kupokea kiasi stahiki kutoka kwa kila mlipakodi katika eneo ambalo amepangiwa na

kuhakikisha kiasi chote kilichokusanywa kinalipwa kwa Halmashauri inayohusika.
Kutozingatiwa kwa Kifungu hicho kunasababisha Halmashauri kutofikia malengo ya ukusanyaji wa mapato ya ndani na fedha hizo kuwanufaisha watu wachache. Katika Halmashauri zilizofika mbele ya Kamati, mawakala walioingia mkataba na Halmashauri ya Wilaya ya Muheza pamoja na Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam hawakuwasilisha kiasi cha **Shilingi 177,862,460** na **Shilingi 470,754,116** mtawalia kinyume na masharti ya mkataba.

**Mheshimiwa Spika**, ili kurudisha nidhamu katika ukusanyaji wa mapato ya ndani, Kamati imezielekeza Halmashauri zote kuhakikisha kunakuwa na ufuatiliaji na utekelezaji wa mikataba yote ya mawakala wa kukusanya mapato.

**2.4.4 Halmashauri kushindwa kukusanya Shilingi Bilioni 37.34 kutoka katika Vyanzo muhimu vya Mapato**

**Mheshimiwa Spika**, mifumo imara ya udhibiti wa ndani ni pamoja na ufanisi katika makisio na makusanyo ya mapato ya ndani. Kila Mkurugenzi anatakiwa kuwa na taarifa sahihi za walipa kodi wanaopatikana katika eneo lake la usimamizi. Hata hivyo, katika hali isiyo ya kawaida, kuna baadhi ya Halmashauri ambazo hazina takwimu sahihi za walipa kodi waliopo katika kila chanzo cha mapato kinachotakiwa kukusanywa katika Halmashauri zao. Hii inatokana na Wakurugenzi kutohuisha kanzidata ya walipa kodi na kuzikosesha Halmashauri zao mapato na kuiongezea mzigo Serikali.

Uchambuzi wa Kamati kutokana na Taarifa ya CAG umebaini maeneo Saba muhimu ambayo Halmashauri 146 zimeshindwa kukusanya mapato ikiwa ni pamoja na Leseni za biashara **Shilingi 13,940,477,444**, Mauzo ya viwanja **Shilingi 12,292,508,723**, Kodi za pango **Shilingi 5,642,483,546**, Ushuru wa Taka Shilingi **3,016,026,871**, Leseni za vileo Shilingi **1,712,215,056**, Fukwe/Maeneo ya wazi **Shilingi 292,613,800** na Ushuru wa huduma za uwindaji Shilingi **439,606,284**.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imekuwa ikifuatilia uthabiti wa mifumo ya ukusanyaji wa mapato kwa miaka mitatu mfululizo. Ufuatiliaji huo umebaini kuongezeka kwa udhaifu katika eneo la ukusanyaji

wa mapato ya ndani kutokana na kuongezeka kwa mapato yasiyokusanywa kutoka **Shilingi 14,296,172,065** mwaka wa fedha 2020/2021 hadi kufikia **Shilingi 37,335,931,724** kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Ongezeko hili ni sawa na **Asilimia 61.7**. Pamoja na jitihada zinazofanywa za kutafuta fedha za utekelezaji wa miradi ya maendeleo, baadhi ya Halmashauri hazioni umuhimu wa jitihada hizo za Serikali kwa kuacha kukusanya fedha katika vyanzo ambavyo tayari vinafahamika.

Hadi kuwasilishwa kwa taarifa hii, Halmashauri ambazo hazikukusanya kiasi kikubwa cha fedha zinaonekana katika Jedwali Na 5.

**Jedwali Na. 5**: Halmashauri ambazo hazikukusanya mapato kutoka vyanzo mbalimbali

| Na | Jina la Halmashauri | Chanzo cha Mapato | Kiasi |
|---|---|---|---|
| 1. | H/W Mbinga | madai ya kibiashara (Receivables) | 2,541,335,901 |
| 2. | H/M Kinondoni | madai ya kibiashara (Receivables) | 2,297,602,105 |
| 3. | H/Jiji Arusha | Kodi ya pango | 1,594,180,885 |
| 4. | H/W Muheza | Mapato ya vizimba | 246,240,000 |
| 5. | H/W Meru | Leseni za Biashara | 245,497,983 |
| 6. | H/W Geita | Leseni za biashara pamoja na ushuru wa nyumba za wageni | 235,734,644 |
| 7. | H/W Manyoni | Mauzo ya viwanja | 212,199,778 |
| 8. | H/W Rungwe | Ada za leseni na pango | 163,172,200 |
| 9. | H/W Muleba | Leseni za Biashara na vileo | 113,878,000 |

**Mheshimiwa Spika**, Hali hii inatokana na uzembe wa Wakurugenzi wa Halmashauri katika usimamizi wa ukusanyaji wa mapato ya Halmashauri.

### 2.4.5 Ushuru wa Huduma usiokusanywa Shilingi Bilioni 36.22

**Mheshimiwa Spika**, utozaji wa ushuru wa huduma wa kiwango kisichozidi Asilimia 0.3 umefafanuliwa katika Vifungu vya 6(1) (u) na 7(1) (y) vya Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura ya 290 kama iliyorekebishwa na Kifungu cha 44 na 45 cha Sheria ya Fedha, 2020. Ushuru wa huduma ni chanzo cha mapato katika Halmashauri zetu. Hata hivyo, Kamati haijaridhishwa na hali iliyopo katika Halmashauri 40 ambazo zimeshindwa kukusanya ushuru huo kutokana na kukosa taarifa sahihi za mauzo ghafi ya wafanyabiashara wenye leseni halali waliopo katika maeneo yao.

Mfano wa Halmashauri chache ambazo zimeshindwa kukusanya ushuru wa huduma katika mwaka wa fedha 2021/2022 ni kama zinavyoonekana katika Jedwali Namba 6 la Taarifa hii.

**Jedwali Na 6**: Halmashauri ambazo hazikukusanya ushuru wa huduma kutokana na kutokuwa na kukosa taarifa sahihi za mauzo ghafi

| Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| 1. | H/Jiji Dar es Salaam | 25,961,761,567 |
| 2. | H/Jiji Arusha | 4,550,087,824 |
| 3. | H/M Iringa | 508,857,386 |
| 4. | H/W Mbinga | 162,321,204 |

**Mheshimiwa Spika**, Juhudi za makusudi zinatakiwa ili kuokoa fedha zilizopotea kwa kutokusanywa ambazo zingetumika kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo kwa kuwa, kushindwa kukusanya ushuru wa huduma kunaathiri utekelezaji wa shughuli zilizokusudiwa katika mwaka husika. Kupitia OR – TAMISEMI, Kamati imezielekeza Halmashauri zote nchini kuhakikisha zinakuwa na taarifa sahihi za mauzo ghafi ya wafanyabiashara kutoka TRA pamoja na taarifa za walipa kodi ya huduma na kuhakikisha fedha hizo zinakusanywa.

### 2.4.6 Mashine za kukusanyia mapato (POS) kuzimwa kwa muda mrefu

**Mheshimiwa Spika**, usimamizi usio imara wa mifumo ya ukusanyaji wa mapato umesababisha kukosekana kwa mapato ya Halmashauri kutokana na Mashine za kukusanyia mapato (POS) kuzimwa kwa muda mrefu kama inavyoonekana katika Jendwali Namba 7.

**Jedwali Na 7:** Halmashauri ambazo Mashine za POS zimezimwa kwa muda mrefu

| Na. | Jina la Halmashauri | Idadi ya Siku |
|---|---|---|
| 1. | H/W Chamwino | Siku 4 hadi siku 1,905 |
| 2. | H/ W Uvinza | Siku 1133 |
| 3. | H/ W Ushetu | Siku 70 hadi 397 |
| 4. | H/W Sengerema | Siku 185 |

**Mheshimiwa Spika**, ni maoni ya Kamati kwamba, uzimaji wa mashine hizi za POS ni hujuma za makusudi zinazofanywa na baadhi ya watu waliopewa dhamana ya kukusanya mapato ili kuzikosesha Halmashauri hizo mapato. Changamoto hii imekuwa ikijirudia katika kila Ripoti ya CAG na tafsiri yake ni kutochukuliwa kwa hatua stahiki na madhubuti dhidi ya wahusika.

### 2.4.7 Udhaifu katika ukusanyaji wa mapato ya maduka na vibanda

**Mheshimiwa Spika**, imebainika kuwa, Mikataba ya upangishaji wa vibanda na fremu za biashara katika maeneo ya masoko na stendi iliyoingiwa kati ya Halmashauri nyingi na wafanyabiashara katika maeneo ya Halmashauri hizo, hailindi maslahi ya Halmashauri kutokana na mikataba hiyo aidha kuisha muda wake na kutohuishwa au kuwa na masharti ambayo inazinyima Halmashauri nguvu ya kukusanya mapato kama inavyotakiwa.

Kamati imechambua utendaji wa Halmashauri katika eneo la uwekezaji wa vibanda na maduka na kubaini uwepo wa mapungufu ya mikataba kama vile kutokuwa na mikataba iliyohuishwa, mikataba kutokuwa na masharti ya muda,

Halmashauri kutokuwa na idadi kamili ya vibanda na maduka yaliyopangishwa, kukosekana kwa taarifa sahihi za wapangaji wa maeneo hayo, kutofahamika kwa gharama sahihi za ujenzi na taratibu za uendeshaji wa vibanda na maduka hayo na kutokuwa na takwimu sahihi za makadirio ya mapato yanayotakiwa kukusanywa na Halmashauri.

**Mheshimiwa Spika**, hali hii inasababisha Halmashauri kushindwa kufikia malengo ya makusanyo ya mapato na kutofikiwa kwa lengo lilikosudiwa la utoaji wa huduma kwa jamii pamoja na kusababisha migogoro kati ya Halmashauri na wafanyabiashara hao. Kwa muktadha huo, Kamati imezielekeza Halmashauri zenye changamoto hiyo zihakikishe mikataba inayoingiwa na wafanyabiashara inalinda maslahi ya pande zote, Halmashauri zitengeneze Sheria Ndogo ambazo zitasimamia ukusanyaji wa mapato katika maeneo yao na kuhakikisha kuwa wapangishwaji hao wana mikataba halali iliyohuishwa yenye masharti yote muhimu katika utekelezaji wa mikataba hiyo.

Kamati imebaini kuwa, Maafisa manunuzi na wanasheria wa Halmashauri waliopewa dhamana ya kuzisaidia Halmashauri hizo katika uingiaji wa mikataba kutotekeleza wajibu wao kikamilifu. Aidha, Kamati inasisitiza kitengo cha Sheria katika Halmashauri zote kishirikishwe kikamilifu katika hatua zote kuanzia hatua za awali za uandaaji mpaka utekelezaji wa mikataba hiyo.

### 2.5 Matumizi yasiyofaa ya Fedha za umma

**Mheshimiwa Spika**, jukumu kubwa la Kamati hii pamoja na mambo mengine ni kushughulikia maeneo yenye matumizi mabaya ya fedha za Serikali za Mitaa. Katika eneo hili, Kamati ilichambua kwa kina taarifa zilizowasilishwa na CAG ili kuhakikisha matatizo ya matumizi mabaya ya fedha za umma yanaondolewa kwa kutoa mapendekezo stahiki.

Kazi iliyofanywa na Kamati ni kuhakikisha rasilimali za Umma zinasimamiwa vema na kutumika kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na taratibu ili kuwanufaisha wananchi wote. Sheria mbalimbali zimewekwa ili kuhakikisha kunakuwa na uwazi na uwajibikaji katika kusimamia matumizi ya fedha za umma pamoja na kuhakikisha malipo yote yanafanyika kwa uhalali, wakati na

utimilifu. Licha ya kuwepo kwa Sheria na Kanuni mbalimbali, bado kumekuwa na baadhi ya Wakurugenzi ambao waliamua kuanzisha taratibu zao za matumizi ya fedha za umma ambazo zinakinzana na Sheria ya Nchi. Changamoto zilizobainika ni kama ifuatavyo:-

**2.5.1 Kufanya Malipo kwa Fedha Taslimu Shilingi Bilioni 1.51**

**Mheshimiwa Spika**, kwa kiasi kikubwa nchi yetu imehamishia shughuli zake katika mifumo ya kielektroniki ili kupunguza urasimu na kuongeza ufanisi katika utendaji. Sababu moja wapo ya matumizi mabaya ya fedha za umma ni kufanya malipo ya fedha taslimu kwa wazabuni.

Ili kuzuia tatizo hilo, Aya ya 6.8.3 ya Mwongozo wa Uhasibu wa Halmashauri wa Mwaka 2021 inazitaka Halmashauri kufanya malipo yote kwa njia ya kielekitroniki katika akaunti ya benki ya mlipwaji, na kwa hali yoyote ile Mamlaka isilipe kwa hundi au fedha taslimu. Pamoja na katazo hilo, bado kuna Wakurugenzi wa Halmashauri 14 ambao hawakuona umuhimu wa kutumia mifumo ya kielektroniki katika kufanya malipo. Mfano wa Halmashauri hizo ni kama zilivyo katika Jedwali Na. 8.

**Jedwali Na.8**: Halmashauri ambazo zilifanya malipo kwa fedha taslimu

| Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---:|
| 1. | H/Jiji Arusha | 309,160,000 |
| 2. | H/M Iringa | 264,433,520 |
| 3. | H/W Urambo | 55,216,500 |

**Mheshimiwa Spika**, Iwapo tatizo hilo litaendelea katika Halmashauri bila ya wahusika kuchuliwa hatua stahiki, hakutakuwa na sababu ya Serikali kutumia nguvu kubwa kuwekeza katika mifumo ya kielektroniki.

**2.5.2 Halmashauri kufanya malipo bila ya viambatisho Shilingi Bilioni 11.78**

**Mheshimiwa Spika**, Serikali imekuwa ikitumia nguvu kubwa katika kutoa elimu kwa umma juu ya kutoa na kupokea risiti za kielektroniki ili mapato stahiki ya Serikali yaweze kupatikana na

kuwezesha utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo. Muitikio wa kudai risiti umekuwa ni mkubwa katika jamii, hata hivyo, katika hali isiyotarajiwa, baadhi ya wataalamu katika Halmashauri 71 wamelipa jumla ya **Shilingi Bilioni 10.08** kwa wazabuni mbalimbali bila kudai risiti za kielektroniki. Vile vile Wakurugenzi wa Halmashauri 40 walilipa **Shilingi Bilioni 1.70** bila viambatisho timilifu.

**Mheshimiwa Spika**, Sheria na Kanuni zilizowekwa zimeweka utaratibu mzuri ambao ukifuatwa hakutakuwa na hoja za ukaguzi kwa kiasi kikubwa. Hata hivyo, Wataalamu na Wakurugenzi waliopewa dhamana ya kusimamia matumizi ya fedha za umma wamekuwa wakiiikosesha Serikali mapato kwa kukiuka Kifungu cha 36 (1) cha Sheria ya Utozaji wa Kodi, Sura ya 438 ambacho kinamtaka mtu ambaye anasambaza bidhaa, anatoa huduma au anayepokea malipo kuhusiana na usambazaji wa bidhaa au huduma aliyotoa, kutoa risiti au ankara kwa kutumia mashine za kielektroniki. Kifungu hiki kimewekwa ili kuzuia mianya ya ukwepaji wa kodi kwa wazabuni inayosababisha ukusanyaji mdogo wa mapato ya Serikali.

Aidha Agizo la 34(1) na 104(2) la Randama ya Fedha ya Serikali za Mitaa ya Mwaka 2009 linamtaka Mwekahazina kuweka mfumo mzuri wa uhasibu na utunzaji wa nyaraka zote muhimu, kwa muda usiopungua miaka mitano. Pamoja na agizo hilo katika randama, hoja hiyo imeongezeka kwa **Asilimia 67.15** ambapo, katika mwaka wa fedha 2020/2021, yalifanyika matumizi yasiyo na viambatisho ya **Shilingi Bilioni 3.87** ikilinganishwa na **Shilingi Bilioni 11.78** za mwaka wa fedha 2021/2022 kinyume na matarajio ya Kamati ya kutaka kupungua kwa hoja hii. Mfano wa Halmashauri hizo ni Jedwali namba 9 la taarifa hii.

**Jedwali Na. 9:** Halmashauri ambazo zilifanya malipo bila ya viambatisho

| Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---:|
| 1. | H/W Ileje | 248,760,648 |
| 2. | H/W Bahi | 238,341,535 |
| 3. | H/W Iramba | 140,731,303 |
| 4. | H/W Meru | 127,536,474 |
| 5. | H/W Uvinza | 106,718,435 |
| 6. | H/W Mbozi | 101,814,620 |

**Mheshimiwa Spika**, kutokuwepo kwa viambatisho timilifu kunatia mashaka ya uhalali wa kufanyika kwa malipo hayo na kukosekana kwa thamani ya fedha.

**2.5.3 Matumizi ya Fedha za Akaunti ya Amana kinyume na malengo yaliyokusudiwa Shilingi Bilioni 7.7**

**Mheshimiwa Spika**, Halmashauri zimepewa dhamana ya kutunza fedha kutoka kwa waweka amana mbalimbali kwa shughuli maalumu ambapo shughuli hizo huainishwa wakati wa uwekaji wa fedha hizo katika Akaunti ya Amana zinazosimamiwa na Halmashauri. Utaratibu wa utoaji wa fedha hizo katika Akaunti unahitaji uthibitisho wa matumizi sawa na lengo kuu la amana hizo.

Kwa ujumla Wakurugenzi wote wa Halmshauri wanafahamu misingi ya uwekaji na utolewaji wa fedha hizo. Hata hivyo, wasimamizi hao wameamua kuvunja taratibu kwa kutumia fedha hizo kinyume na malengo yaliyokusudiwa hali inayovunja uaminifu kwa waweka amana pamoja na kuiweka Serikali katika madeni makubwa ambayo yanaepukika.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imekuwa ikiripoti suala hili katika Taarifa zinazowasilishwa Bungeni. Kujirudia rudia kwa hoja hii inatoa tafsiri kwamba, baadhi ya wakurugenzi wa Halmashauri wameamua kuacha kufuata Sheria, kanuni na Taratibu za nchi na kuleta athari kwa wananchi wote kwa kuwa, kutumia fedha kinyume na lengo kunakwamisha utekelezaji wa shughuli zilizopangwa. Ripoti ya CAG ya hesabu za Halmashauri inayoishia mwezi Juni, 2022 imeripoti kiasi cha **Shilingi 3,153,314,281** kilichotumiwa na Halmashauri 31 kwa matumizi yasiyopangwa.

Vile vile, Halmashauri 27 zilifanya malipo kutoka katika akaunti ya amana **Shilingi 3,268,872,285** bila ya uthibitisho wa amana hizo kupokelewa. Kwa tafsiri ya haraka, Wakurugenzi wa Halmashauri hizo waliamua kukwamisha utekelezaji wa shughuli zilizopangwa kufanyika kwa kutumia fedha hizo kwa matumizi ambayo hayakuwepo licha ya ukweli kwamba, hapakutakiwa kufanyika kwa malipo hayo.

**Jedwali Na 10**: Halmashauri zilizotumia fedha kutoka Akaunti ya Amana kinyume na taratibu

| Na | Jina la Halmashauri | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | H/W Tarime | 186,474,143 |
| 2. | H/W Iramba | 129,743,686 |
| 3. | H/W Bariadi | 94,471,475 |
| 4. | H/W Bahi | 53,623,715 |
| 5. | H/W Kondoa | 25,720,673 |

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imekuwa ikisisitiza juu ya uzingatiaji wa taratibu za uendeshaji wa Akauti ya Amana ili kuwe na matumizi sahihi ya fedha zinazohifadhiwa katika akaunti hiyo.

**2.5.4 Halmashauri kufanya matumizi yasiyo na tija ya Shilingi Milioni 898.85**

**Mheshimiwa Spika**, lengo la Kamati kama jicho la Bunge ni kuhakikisha kunakuwa na ustawi wa wananchi katika Halmashauri kwa kufanya matumizi yenye faida kiuchumi kwa wananchi. Kinyume na lengo hilo, Halmashauri 9 zilifanya matumizi ambayo hayakuwa na manufaa kwa wananchi.

Tathmini ya Kamati juu ya tija ya matumizi ya fedha za umma imebaini kuongezeka kwa tatizo hilo kwa kiasi cha **Shilingi Milioni 234.85** ambapo katika mwaka wa fedha 2020/2021 Halmashauri zilifanya matumizi yasiyo na tija ya **Shilingi 664** ikiwa ni ongezeko la **Asilimia 26.1**. Katika mwaka wa fedha 2021/2022, Halmashauri zilizofika mbele ya kamati zilizofanya matumizi yasiyo na tija zimetajwa katika Jedwali namba 11.

**Jedwali Na 11:** Halmashauri zilizofanya matumizi ambayo hayana tija

| Na | Jina la Halmashauri | Kiasi | Sababu |
|---|---|---|---|
| 1. | H/Jiji Arusha | 322,295,500 | Kutokuwa na taarifa ya kuthibitisha matumizi yaliyofanyika katika ukarabati wa barabara na kukosekana kwa |

| Na | Jina la Halmashauri | Kiasi | Sababu |
|---|---|---|---|
| | | | uthibitisho wa kufanyika kwa kazi hiyo |
| 2. | H/M Temeke | 111,815,294 | Ulipaji wa faini uliosababishwa na kuchelewa kulipa mkopo wa CRDB |
| 3. | H/W Hanang’ | 34,420,000 | kufanya upembuzi yakinifu kwa ajili uanzishwaji wa vyuo vya kati (*tertiary training institute*) katika eneo ambalo si mali ya Halmashauri na kutokuwa na nyaraka zozote zinazothibitisha kufanyika kwa upembuzi yakinifu |
| 4. | H/Mji Bunda | 26,709,540 | Ufyatuaji wa tofali kwa ajili ya ujenzi wa majengo ya Hospitali ya Wilaya ambazo hazikuwa na ubora hivyo kusababisha msingi ulioanza kujengwa kwa kutumia tofali hizo kulivunjwa |
| 5. | H/W Bariadi | 7,265,000 | Fedha kutumika kwa ajili ya maandalizi ya shamba darasa la miwa ambalo CAG hakukuta mazao yoyote katika eneo hilo |

**Mheshimiwa Spika**, matumizi yasiyo na tija ni hasara kwa Halmashauri hizo kwa kuwa fedha hizo zingeweza kutumika katika shughuli nyingine ambazo zina manufaa kwa maendeleo ya wananchi.

**2.6 Ukiukwaji wa Sheria ya Ununuzi wa Umma Sura 410 na Mapungufu katika usimamizi wa Mikataba Shilingi 106,799,578,781**

**Mheshimiwa Spika**, Ununuzi wa Umma ni shughuli muhimu ya kiuchumi inayohusisha sehemu kubwa ya Pato la Taifa (GDP). Takribani **Asilimia 70** ya Bajeti ya Serikali na Taasisi zake hutumika kwenye ununuzi wa umma.

uchambuzi uliofanywa na Kamati umebaini uwepo wa dosari nyingi za matumizi ya fedha za umma katika eneo la ununuzi ambapo, Serikali imepoteza na inaendelea kupoteza kiasi kikubwa cha fedha. Tatizo hili limesababishwa na Wakurugenzi na Maafisa Manunuzi waliopewa jukumu la kusimamia rasilimali za Taifa na kuhakikisha rasilimali hizo zinakusanywa na kutumiwa kwa namna ambayo ina manufaa makubwa zaidi kwa wananchi wote kwa ujumla kwa kuzingatia Katiba, Sheria, Kanuni na Miongozo mbalimbali ya Nchi kukiuka Sheria zilizotungwa na Bunge lako Tukufu.

Azma ya Kamati ni kuhakikisha matatizo ya matumizi mabaya ya fedha za umma katika eneo la ununuzi yanaondolewa. Katika kutekeleza azma hiyo, Kifungu cha 48(3) cha Sheria ya Ununuzi wa Umma Na. 7 ya Mwaka 2011 kinamtaka CAG katika ripoti yake atoe maoni kama Taasisi husika zimefata taratibu za Ununuzi kama zilivyoainishwa katika Sheria husika na Kanuni zake ili kujiridhisha iwapo kuna uzingatiaji wa matakwa ya Sheria hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, katika eneo la uzingatiaji wa Sheria ya Ununuzi wa Umma pamoja na Kanuni zake, Kamati imechambua kwa kina Ripoti ya CAG kwa Hesabu za Mamlaka za Serikali za Mitaa zinazoishia tarehe 30 Juni, 2022 kama ifuatavyo:-

**2.6.1 Ununuzi uliofanyika bila kuidhinishwa na Bodi za Zabuni Shilingi Bilioni 5.7**

**Mheshimiwa Spika**, Kanuni ya 55 (2), 163 (4) na 185 (1) za Kanuni za Ununuzi wa umma za Mwaka, 2013 zinazuia Halmashauri kutoa zabuni isipokuwa kama zabuni hiyo imeidhinishwa na bodi husika ya zabuni. Ukiukwaji wa Kanuni hizo, unaondoa mamlaka ya Bodi ya zabuni kutekeleza majukumu yake ya uangalizi na hivyo kuhatarisha ubora wa bidhaa zitakazonunuliwa.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imefanya uchambuzi na kubaini uwepo wa **Halmashauri 23** zilizohusika katika hoja hii ambazo ni sawa na **Asilimia 12.5** ya Halmashauri zote 184 zilizopo Nchini. Katika mahojiano ambayo Kamati imefanya na baadhi ya Wakurugenzi waliofika mbele ya Kamati, Halmashauri zilizofanya ununuzi bila ya kuidhinishwa na Bodi ya zabuni ni kama inavyoonekana katika Jedwali namba 12.

**Jedwali Na. 12**: Halmashauri zilizofanya ununuzi bila ya kuidhinishwa na Bodi ya Zabuni

| Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| 1. | H/W Ileje | 348,161,496 |
| 2. | H/ Mji Makambako | 222,383,031 |
| 3. | H/W Tarime | 176,674,700 |
| 4. | H/W Mbozi | 85,900,460 |
| 5. | H/W Bunda | 26,527,704.033 |

**Mheshimiwa Spika**, ili kupata thamani ya fedha katika ununuzi wa umma, Halmashauri zote zinatakiwa kuzitumia Bodi za zabuni kwa ukamilifu wake. Aidha, Bodi hizo zinatakiwa kufanya kazi yake kwa ufanisi na weledi wa hali ya juu.

**2.6.2 Ununuzi uliofanyika nje ya Mpango wa ununuzi wa Halmashauri Shilingi Bilioni 14.02**

**Mheshimiwa Spika**, kufanya Ununuzi nje ya mpango wa ununuzi wa mwaka kunaweza kuisababisha Halmashauri kushindwa kufikia malengo yake ya mwaka kutokana na kufanyika kwa matumizi yasiyopangwa. Aidha, jambo hilo ni kinyume na Kanuni ya 69(3) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2013 na marekebisho yake ya mwaka 2016 ambayo inaitaka taasisi nunuzi kufanya makisio ya mahitaji yake ya bidhaa, huduma, na ujenzi kwa usahihi kadiri iwezekanavyo kwa kuzingatia huduma au shughuli ambazo zipo katika mpango kazi na kujumuishwa katika makadirio ya kila mwaka.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati katika eneo hili umebaini uwepo wa Halmashauri 19 zilizokiuka matakwa ya Kanuni tajwa hapo juu ambazo ni sawa na **Asilimia 10.3** ya Halmashauri zote.

### 2.6.3 Baadhi ya Halmashauri Kufanya malipo kabla ya kupokelewa kwa bidhaa nunuliwa Shilingi Bilioni 3.29

**Mheshimiwa Spika,** taratibu za malipo kwa bidhaa nunuliwa zimewekwa kisheria ili kuziepusha Halmashauri kuingia katika hasara ya kupokea bidhaa ambazo hazikutakiwa au hazikidhi viwango. Taratibu hizo zimefafanuliwa kwa kina katika Kanuni ya 242 (1) na 248 ya Kanuni za Ununuzi wa Umma, 2013.

**Mheshimiwa Spika**, baadhi ya Wakurugenzi katika Halmashauri zetu wamekuwa wakikiuka Sheria, Kanuni na Taratibu zilizowekwa kwa makusudi na kuiingiza Serikali katika hasara. Wakurugenzi wa Halmashauri 26 ambazo ni sawa na **Asilimia 14.1** ya Halmashauri zote waliziweka Halmashauri zao katika hatari ya kupata hasara kwa kukiuka matakwa ya Kanuni. Mfano wa Halmashauri hizo ni jedwali namba 13.

**Jedwali Na. 13**: Halmashauri zilizofanya malipo kabla ya kupokea bidhaa nunuliwa

| Na | Jina la Halmashauri | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | H/W Korogwe | 93,782,000 |
| 2. | H/W Kilindi | 67,663,500 |

**Mheshimiwa Spika**, Kufanya malipo kwa wazabuni kabla ya kupokelewa kwa bidhaa nunuliwa ni matumizi yasiyofaa ya fedha za umma iwapo wazabuni hao watashindwa kabisa kuwasilisha bidhaa hizo au watawasilisha bidhaa ambazo hazikidhi viwango vya ubora unaohitajika au wakiwasilisha bidhaa ambazo hazikutakiwa.

### 2.6.4 Mikataba ambayo Haikuhakikiwa na Mwanasheria Shilingi Bilioni 6.68

**Mheshimiwa Spika**, Serikali imekuwa ikipoteza fedha kutokana na kushindwa kesi katika mashauri mbalimbali. Aidha, kesi nyingi zimekuwa zikisababishwa na uzembe wa baadhi ya wataalamu wetu kushindwa kutekeleza majukumu yao kikamilifu. Pamoja na mambo mengine, ofisi ya Mwanasheria ipo katika kuhakikisha Serikali inaingia katika mikataba ambayo haitaleta madhara kwa Taifa na haitasababisha upotevu wa rasilimali za Umma.

Hata hivyo, Kamati imefahamishwa kuhusu uwepo wa Wakurugenzi wa Halmashauri 20 kuingia katika mikataba yenye thamani ya zaidi ya **Shilingi Bilioni 6** bila ya mikataba hiyo kuhakikiwa na Mwanasheria.

**Mheshimiwa Spika**, waliopewa dhamana ya kusaini mikataba kabla ya kuhakikiwa na kujumuisha maoni ya Mwanasheria wanaziweka Halmashauri husika katika hatari za kisheria. Halmashauri zilizokiuka matakwa ya Kanuni ya 59 na 60 ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka 2013 (na marekebisho yake ya mwaka 2016) ni kama ifuatavyo.

**Jedwali Na. 14**: Halmashauri zilizoingia mikataba bila ya kupitiwa na Mwanasheria

| Na. | Jina la Halmashauri | Thamani ya Mkataba (Sh.) |
|---|---|---|
| 1. | H/Jiji Dar es Salaam | 2,930,234,090 |
| 2. | H/W Sengerema | 549,440,000 |
| 3. | H/W Kyerwa | 320,265,950 |
| 4. | H/W Bariadi | 207,733,500 |
| 5. | H/Jiji Arusha | 80,420,000 |

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inazielekeza Halmashauri zote kutumia wanasheria wenye utaalamu na uadilifu ili kuzisaidia Halmashauri hizo kabla ya kuingia mikataba na kuiondolea mzigo Serikali wa gharama za uendeshaji wa kesi nyingi zinazotokana na uzembe wakati wa uingiaji wa mikataba mbalimbali.

### 2.6.5 Ununuzi uliofanyika bila Ushindanishi wa bei Shilingi Bilioni 7.45

**Mheshimiwa Spika**, Asilimia 24.5 ya Halmashauri zote 184 zimekosa haki ya kupata bei shindani zaidi na thamani ya fedha katika ununuzi uliofanywa na Halmashauri hizo kutokana na Wakurugenzi wao kukataa kukidhi matakwa ya Kanuni ya 164(1) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2013 ambayo inazitaka taasisi nunuzi kupata nukuu ya bei kutoka kwa wazabuni wasiopungua watatu. Mfano wa Halmashauri zilizokiuka kanuni hizo zimetajwa katika jedwali namba 15.

**Jedwali Na. 15**: Halmashauri zilizofanya ununuzi bila ya ushindanishi wa bei

| S/N | Jina la Halmashauri | Kiasi (sh) |
|---|---|---|
| 1. | H/W Karagwe | 800,000,000 |
| 2. | H/W Bunda | 576,039,073 |
| 3. | H/W Ileje | 283,356,469 |
| 4. | H/Mji Tunduma | 257,829,333 |
| 5. | H/W Uvinza | 173,320,675 |
| 6. | H/Mji Bunda | 140,900,000 |
| 7. | H/W Mbozi | 24,500,000 |

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imechambua kwa kina taarifa zote zilizowasilishwa mbele ya Kamati na kusikitishwa na baadhi ya Wakurugenzi na Maafisa Manunuzi kutengeneza taratibu zao na kufanya kazi kwa mazoea kinyume na Sheria iliyotungwa na Bunge kwa kutotumia njia ya ushindanishi wa bei kama ilivyofafanuliwa katika Sheria na kusababisha hasara pamoja na kukosekana kwa thamani ya fedha. Hayo ni matumizi mabaya ya fedha za umma.

**2.6.6 Malipo ya awali kwa mkandarasi yenye mapungufu Shilingi Bilioni 4.13**

**Mheshimiwa Spika**, Kifungu cha 54.2 cha Masharti ya jumla ya mkataba (GCC) kimeelezea namna malipo ya awali kwa wakandarasi yanavyopaswa kufanyika. Pamoja na ufafanuzi uliotolewa, bado kuna Halmashauri ambazo zimekwenda kinyume na taratibu na kuashiria upotevu wa fedha za Umma. Halmashauri ambazo zimefanya malipo ya awali yenye mapungufu kwa wakandarasi ni **kiambatisho Namba 2** cha Taarifa hii.

**2.6.7 Ununuzi kufanyika nje ya Mfumo wa TANePS**

**Mheshimiwa Spika**, katika ukaguzi wa hesabu zilizoishia mwezi Juni, 2022, Halmashauri kadhaa zimefanya ununuzi nje ya mfumo wa TANePS kinyume na Sheria ya Ununuzi wa Umma. Katika Halmashauri chache zilizofika mbele ya Kamati, Halmashauri zifuatazo zilifanya ununuzi nje ya mfumo wa TANePS.

**Jedwali Na. 16**: Halmashauri zilizofanya ununuzi nje wa Mfumo wa TANePS

| S/N | Jina la Halmashauri | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | H/W Maswa | 6,992,078,511 |
| 2. | H/M Temeke | 2,001,515,101 |
| 3. | H/Mji Tarime | 1,348,161,411 |
| 4. | H/W Musoma | 897,214,610 |
| 5. | H/W Bariadi | 407,018,048 |

**Mheshimiwa Spika**, Halmashauri kufanya ununuzi nje ya mfumo kunapelekea uwepo wa urasimu na mazingira ya rushwa, upendeleo na ukiukwaji wa sheria.

**2.6.8 Mapungufu katika Mchakato wa Zabuni, taratibu za Ununuzi na usimamizi wa Mikataba**

**Mheshimiwa Spika**, ukaguzi wa CAG katika eneo la ununuzi uliangalia pia mchakato wa zabuni, taratibu za ununuzi pamoja na utoaji wa mikataba ya miradi. Kwa muktadha huo, Ukaguzi ulibaini mapungufu katika mikataba ya miradi yenye thamani ya **Shilingi 3,000,001,000** inayotekelezwa na H/W Karagwe ambapo, Halmashauri ilisaini mkataba na mkandarasi Sure Civil and Building akiungana na Lucas Construction Company Ltd (JV). Katika mkataba huo, mapungufu kadhaa yalibainika ikiwa ni pamoja na zabuni kupewa mkandarasi asiyekidhi vigezo vilivyowekwa na Bodi ya usajili ya Wakandarasi, Mkataba kusainiwa na Kampuni ya ukandarasi ambayo haikuwepo wakati wa mchakato wa ununuzi wala kupitishiwa na Bodi ya zabuni na njia ya ushindani wa bei kutumika kinyume na taratibu za ununuzi wa umma.

**Mheshimiwa Spika**, Halmashauri ya Jiji la Arusha ilitoa zabuni ya **Shilingi 3,915,527,364** kwa ajili ya ujenzi wa jengo la OPD katika Hospitali ya Jiji la Arusha kwa mzabuni asiyekidhi vigezo. Uchambuzi umebaini mapungufu katika utoaji wa zabuni hiyo kwa kuwa, tathmini ya zabuni hiyo ilifanyika mara sita na kutolewa maoni tofauti tofauti ambapo, mara tano zilifanywa na kamati moja ya tathmini na mara moja ilifanywa na kamati ya tathmini nyingine iliyoteuliwa bila ya uwepo wa sababu za msingi za kufanya hivyo. Aidha, Menejimenti ya Halmashauri ya Jiji la Arusha kupitia Ajenda ya Na. 4 BZ 4/2022/22 ya kikao cha Bodi ya zabuni

cha Tarehe 30 Novemba, 2021, kilimzawadia zabuni M/s B.H.Ladwa Ltd ambaye hakushinda zabuni hiyo (*unsuccessful bidder*).

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifanya uchambuzi wa taratibu zilizofanywa na Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu katika mapokezi ya bidhaa yaliyofanywa kinyume na taratibu za zabuni. Halmashauri ilimpa mzabuni Sango Investment and General Supplies Ltd **Shilingi 40,572,000** kwa ajili ya ununuzi wa vishikwambi 30 aina ya "Model A 10.1 size Samsung; RAM 3GB, internal storage 64GB network supported by both WIFI and WAN". Hata hivyo Halmashauri ilikubali kupokea vishikwambi vya aina ya "Model 10.4 size Samsung, RAM 2GB, internal storage 32 GB, supported by both Brand band and WIFI". Vishikwambi vilivyowasilishwa vina uwezo wa chini ikilinganishwa na vilivyoagizwa. Hali hii inatia mashaka ya weledi wa watumishi waliokubali kupokea vishikwambi hivyo hali ya kuwa wanafahamu kuwa ni tofauti na vile vilivyoagizwa.

**Mheshimiwa Spika**, Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali ilifanya malipo ya **Shilingi 181,483,925** kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya upasuaji vya wodi za wanaume, wanawake, chumba cha kuhifadhia maiti katika Hospitali ya Wilaya ya Mbarali ambapo, Halmashauri haikushindanisha zabuni, bidhaa hizo hazikuingizwa katika daftari la kupokelea vifaa na hapakuwa na hati ya kupokelea na kutoa vifaa stoo.

Pamoja na hayo, Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali ililipa **Shilingi 61,104,082** kwa mzabuni M/s Mbeya Cement Co. Ltd kwa ununuzi wa **mifuko 4,272** ya saruji badala ya **mifuko 3,282** iliyohitajika kwa majengo manne husika kulingana na makadirio ya gharama za ujenzi (BOQ). Mifuko ya ziada ya saruji iliyonunuliwa ilikuwa ni zaidi ya **mifuko 616** yenye thamani ya **Shilingi 8,800,000**. Katika ujenzi wa majengo hayo, Halmashauri ililipa Kampuni ya Ando Roofing Product Ltd na ALAF Ltd kiasi cha **Shilingi 102,956,004** kwa ununuzi wa bati ambacho ni zaidi ya **Shilingi 58,094,004** ikilinganishwa na kiasi cha **Shilingi 44,862,000** kilichopo katika hati ya gharama za ujenzi kwa majengo yote manne. Pamoja na matatizo yote hayo, Mkurugenzi alishindwa kuwasilisha nyaraka za manunuzi ya **Shilingi 171,260,182** kwa ajili ya uhakiki.

**Mheshimiwa Spika**, kwa tafsiri ya haraka, Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali imetumia vibaya fedha za umma kwa kuisababishia hasara Serikali ya jumla ya **Shilingi 66,894,004** kwa kununua mifuko ya saruji na bati za ziada na kushindwa kuthibitisha matumizi ya vifaa hivyo.

**Mheshimiwa Spika**, mapungufu katika mchakato wa zabuni yamesababisha kuondolewa kwa wazabuni wenye bei ya chini bila ya sababu za msingi na kusababisha kuongezeka kwa gharama katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi. Katika mchakato wa ununuzi wa mashine ya uchimbaji (excavator), Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi iliwaita wazabuni wawili M/S Achelis Tanganyika ambaye alikuwa na bei ya **Shilingi 321,750,000** na M/S Mantrac Tanzania Ltd ambaye alikuwa na bei ya **Shilingi 526,870,000** kwa ajili ya kufanya majadiliano kwa madhumuni ya kupunguza bei.

Baada ya majadiliano baina ya Halmashauri na wazabuni hao, M/S Achelis Tanganyika Ltd alipunguza bei hadi kufikia **Shilingi 313,000,000** na M/S Mantrac Tanzania Ltd alipunguza bei hadi kufikia **Shilingi 500,910,000**. Timu ya tathmini pamoja na Kamati ya Fedha walipitisha zabuni hiyo kwa kumpatia M/S Mantrac Tanzania Ltd kwa bei ya mkataba wa **Shilingi 500,910,000** na kumuacha M/S Achelis Tanganyika mwenye bei ndogo ya **Shilingi 313,000,000** kwa sababu kwamba, M/S Achelis Tanganyika hakuwa na ofisi katika Mkoa wa Mbeya na mtambo wake ni mdogo na haupatikani katika soko la ndani.

**Mheshimiwa Spika**, kutokuwa na watu wenye ujuzi wa kufanya tathimini (evaluation) na majadiliano (negotiation) katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi, kumeisababishia Halmashauri kuwa na ongezeko la gharama za mradi kwa kiasi cha **Shilingi 187,910,000** fedha ambayo ingetumika katika utekelezaji wa miradi mingine.

**Mheshimiwa Spika**, Halmashauri ya Mji Mbinga ilibainika kuwa na mapungufu katika ufanyaji wa tathmini ya fundi ujenzi kwa ajili ya ujenzi wa maabara na kichomea taka katika kituo cha Afya cha Myangayanga. Mapungufu yaliyobainika ni pamoja na mzabuni mmoja kuondolewa katika mchakato wa kufanyiwa tathimini pamoja na kutofautiana kwa bei za wazabuni katika mchakato

wa tathimini ambapo, Mzabuni John Mbilinyi aliwasilisha zabuni ya **Shilingi 1,500,000** wakati muhutasari wa kikao cha ufunguzi wa zabuni inasoma **Shilingi 1,150,000**. Vile vile, mzabuni Daud Amon aliwasilisha zabuni ya **Shilingi 1,200,000** wakati muhutasari wa kikao cha ufunguzi wa zabuni inasomeka **Shilingi 1,500,000**. Kwa muktadha huo, Mkataba wa zabuni alipatiwa John Mbilinyi mwenye bei kubwa.

**Mheshimiwa Spika**, tathimini ya haraka ya Kamati kutokana na mchakato huo imebaini kuwa, mabadiliko ya bei katika mihutasari ya kikao cha ufunguzi wa zabuni yalifanywa kwa dhamira ya kumpatia zabuni hiyo mtu ambaye wanamtaka licha ya bei yake kuwa kubwa ikilinganishwa na mzabuni mwingine. Suala hili ni kinyume na Sheria, Kanuni na taratibu.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilikutana na Halmashauri ya wilaya ya Maswa na kubaini uvunjwaji wa mkataba (MOU) baina yake na Ng'hami Industries Company Limited ambaye ni mmiliki na mwendeshaji wa Duka la Dawa la Maswa lililopo katika Hospitali ya Wilaya Maswa. Lengo la kusaini makubaliano hayo kwa pande zote mbili ni kwa ajili ya uendeshaji wa biashara ya madawa ambapo Kampuni ya Ng'hami itakuwa ndiyo muendeshaji mkuu na msimamizi wa mradi huo na itatakiwa kutoa gawio kwa Halmashauri.

Kipengele C cha makubaliano hayo kinaeleza kuwa, Kampuni ya Ng'hami itawajibika kuzalisha mapato na kutoa gawio kwa Halmashauri ya Wilaya ya Maswa mara mbili kwa mwaka. Gawio hilo litatokana na Asilimia 50 ya mapato yatakayopatikana. Ukaguzi uliofanywa na CAG umefafanua kuwa, katika mwaka uliokaguliwa, hakuna gawio lolote lililotolewa kwa Halmashauri kinyume na Kipengele C cha makubaliano hayo. Aidha, hapakuwa na nyaraka zozote zinazoonesha kukusanywa kwa mapato kutoka katika mradi huo.

**Mheshimiwa Spika**, Halmashauri kushindwa kukusanya mapato yake kutoka katika kampuni ya Ng'hami kunakwamisha utekelezaji wa shughuli za Halmashauri zilizopangwa katika bajeti ya mwaka husika.

### 2.6.9 Matumizi yasiyo sahihi ya nguvu kazi (*force account)*

**Mheshimiwa Spika**, Masharti ya Kifungu cha 64(5) cha Sheria ya Ununuzi wa Umma ya Mwaka 2011 na Kanuni ya 167 (1) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma, 2013 kama ilivyorekebishwa inaainisha masharti yanayoweza kuhalalisha matumizi ya *force account*.

Aidha, Kipengele cha 11.1 cha Mwongozo wa nguvu kazi '*force account*' kwa taasisi nunuzi nchini uliotolewa na Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma, kinaitaka idara inayofanya matumizi au idara ya ufundi kuainisha kazi za ujenzi au matengenezo yanayohitajika kutekelezwa.

Sheria inaitaka taasisi nunuzi kutekeleza mradi kwa utaratibu wa kutumia rasilimali za ndani (*force account*) iwapo kuna watumishi wa umma wenye sifa za kusimamia ujenzi husika na thamani ya ujenzi iliyokadiriwa haivuki ukomo wa thamani kwa kazi za ujenzi itakayoainishwa katika kanuni.

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na Sheria ya ununuzi (kwa mwaka wa fedha 2021/2022) kutokuwa na masharti ya ukomo wa thamani ya miradi, kutokuwepo kwa uandaaji wa taarifa ya ukaguzi wa kazi zilizofanyika, kutokuwa na udhibiti wa ubora wa kazi iliyotekelezwa, kutokuwa na viwango vya weledi na uzoefu wa watekelezaji wa miradi ya ujenzi kwa utaratibu wa *force account* kulisababisha matumizi mabaya ya *force account* na kukosekana kwa ubora wa miradi iliyotekelezwa kwa *force account* ikiwa ni pamoja na baadhi ya Halmashauri kufanya ununuzi wa vifaa vya ujenzi zaidi ya mahitaji halisi vya **Shilingi Milioni 435.02**.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imeielekeza OR – TAMISEMI kufanya uchambuzi wa kina wa miradi yote iliyotekelezwa kwa kutumia *force account* ili kufahamu iwapo kuna thamani ya fedha ya miradi hiyo na kiasi cha ukiukwaji wa Sheria na Kanuni za ununuzi wa Umma.

### 2.7 Kushindwa kulipa Madeni (Payables) ya Halmashauri

**Mheshimiwa Spika**, Halmashauri kama zilivyo Taasisi nyingine zimekuwa zikidaiwa madeni mbalimbali ikiwa ni pamoja na madeni ya watumishi, wazabuni, kodi ya zuio, makato ya mikopo, michango ya mifuko ya hifadhi ya Jamii pamoja na madeni ya

taasisi mbalimbali. Pamoja na mambo mengine, kutolipwa kwa madeni hayo kwa wakati kunaziweka Halmashauri katika hatari ya kufunguliwa mashitaka, kuchelewesha ukamilishaji wa miradi ya maendeleo, kuongezeka kwa gharama za miradi kutokana na riba na kuwanyima watumishi haki zao za msingi.

Kamati imefanya uchambuzi wa kina wa Ripoti ya CAG ya hesabu zilizokaguliwa za Mamlaka za Serikali za Mitaa zinazoishia tarehe 30 Juni, 2022 na kubaini ongezeko la madeni katika Halmashauri mbalimbali. Mambo yaliyojadiliwa kwa kina na Kamati ni kama ifuatavyo:-

**2.7.1 Kutolipwa kwa malimbikizo ya Mishahara na Madai ya Wafanyakazi Shilingi Bilioni 119.94**

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na vigezo vingine, ufanisi wa watumishi katika Halmashauri unatokana na kulipwa kwa madai yao kwa ukamilifu na kwa wakati. Hamasa na morali ya watumishi katika kutekeleza majukumu yao inapungua kadiri ambavyo Serikali inashindwa kukidhi mahitaji yao. Madeni ambayo hayajalipwa kwa muda mrefu ni pamoja na Malimbikizo ya mishahara **Shilingi 42,257,173,197**, Posho za likizo **Shilingi 12,122,259,653**, Gharama za uhamisho **Shilingi 22,961,738,620**, Posho ya kujikimu **Shilingi 4,871,678,948**, Posho ya Samani **Shilingi 4,444,427,298**, Posho ya Makazi **Shilingi 2,008,781,240**, Posho ya Matibabu **Shilingi 2,089,341,915**, Mafunzo **Shilingi 1,276,597,652** na Malimbikizo mengine **Shilingi 27,912,232,383**.

**Mheshimiwa Spika**, malimbikizo ya mishahara yamegawanyika katika maeneo makuu mawili ambayo ni madeni yanayotakiwa kulipwa na Serikali Kuu na madeni ambayo yanatakiwa kulipwa na Halmashauri kutokana na mapato ya ndani. Licha ya juhudi zilizofanywa na Serikali katika kupunguza deni la watumishi kutoka **Shilingi Bilioni 160** iliyoripotiwa katika mwaka wa fedha 2020/2021 hadi kufikia **Shilingi Bilioni 119.94** bado kuna mzigo mkubwa wa madeni hayo.

Wakati Kamati inafanya uchambuzi wa Halmashauri zilizofika mbele ya Kamati ilibainika kuwepo kwa madeni makubwa ambayo Serikali haikulipa kwa watumishi wa Halmashauri kama inavyoonekana katika Jedwali Namba 17.

**Jedwali Na. 17**: Halmashauri ambazo zinadai malimbikizo ya mshahara kutoka Serikali Kuu

| S/N | Jina la Halmashauri | Kiasi (sh) |
|---|---|---|
| 1. | H/W Rungwe | 2,549,451,950.81 |
| 2. | H/W Bahi | 2,109,925,941 |
| 3. | H/W Busega | 1,091,254,903 |
| 4. | H/W Geita | 1,053,980,488 |
| 5. | H/W Muheza | 1,052,567,417 |
| 6. | H/W Ludewa | 1,045,992,171 |
| 7. | H/W Korogwe | 864,535,789 |
| 8. | H/W Iramba | 577,592,240 |

**Mheshimiwa Spika**, Serikali na Halmashauri kutolipa malimbikizo ya mishahara na madai ya wafanyakazi kwa wakati kunawakatisha tamaa watumishi na matokeo yake inaleta athari kwa Serikali kutofikia malengo yake ya kutoa huduma bora kwa umma.

**2.7.2 Makato ya Posho za Wah. Madiwani kutopelekwa Benki ya CRDB PLC Shilingi Milioni 327.98**

**Mheshimiwa Spika**, ili kuboresha maslahi ya wawakilishi wa wananchi katika ngazi ya kata, Benki ya CRDB ilitoa mikopo kwa Wah. Madiwani kwa kusaini hati ya makubaliano na Halmashauri husika kwamba, Halmashauri hizo zitakuwa zinawakata madiwani katika posho zao za kila mwezi na kuwasilisha fedha hizo Benki kwa ajili ya ulipaji wa madeni hayo.

Katika hali ya kushangaza, Halmashauri tatu zimekuwa zikiwakata madiwani fedha za marejesho ya mkopo na kuzitumia fedha hizo kwa matumizi mengineyo badala ya kuziwasilisha fedha hizo benki ya CRDB kama ilivyoainishwa katika mkataba ambao benki imeingia na Halmashauri hizo. Hali hiyo inaziweka Halmashauri hizo katika hatari ya kufunguliwa kesi ya madai.

Katika utekelezaji wa majukumu yake, Kamati ilikutana na Halmashauri ya Wiaya ya Maswa ambayo haikuwasilisha marejesho yake CRDB ya kiasi cha **Shilingi 148,198,689.85** kilichokatwa kutoka katika posho za wah. Madiwani kinyume na makubaliano ya kimkataba. Aidha, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Busega alikiuka makubaliano kwa kutorejesha CRDB

kiasi cha **Shilingi 131,223,821.91** kilichokatwa katika posho za Wah. Madiwani na badala yake kutumia fedha hizo kwa matumizi mengineyo.

**2.7.3 Kutopeleka makato ya Watumishi kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na Taasisi nyingine husika Shilingi Bilioni 260.07**

**Mheshimiwa Spika**, utaratibu wa kuchangia katika mifuko ya Hifadhi ya Jamii uliwekwa ili kumsaidia mtumishi wa umma kuweza kukidhi mahitaji yake ya msingi pindi atakapo staafu. Utaratibu huo upo kwa mujibu wa Kifungu cha 18 (1) cha Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii ya Watumishi wa Umma, 2018 ambacho kinamtaka mwajiri kuchangia katika Mifuko hiyo Asilimia Ishirini ya mshahara wa mfanyakazi.

Pamoja na matakwa hayo ya kisheria, bado kuna baadhi ya Wakurugenzi ambao hawapeleki kabisa michango hiyo na wengine kupeleka kwa kuchelewa hali inayozalisha deni kwa Halmashauri husika linalotokana na adhabu ya kulipa faini kama ilivyoelekezwa katika Kifungu cha 19 (1) na (2) cha Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii ya Watumishi wa Umma ya Mwaka 2018.

**Mheshimiwa Spika**, athari ya michango ya watumishi kutopelekwa katika mifuko ya hifadhi ya Jamii inashuka moja kwa moja kwa watumishi ambao hushindwa kupata mafao yao kwa wakati pindi wanapostaafu. Mfano, Katika Halmashauri ya Jiji la Tanga, watumishi waliostaafu walishindwa kulipwa mafao yao kutoka PSSSF kutokana na Mkurugenzi kushindwa kupeleka michango yao yenye jumla ya **Shilingi 8,606,998**. Ili waweze kupata mafao yao, watumishi hao waliamua kuilipa pesa hiyo PSSSF kwa niaba ya Halmashauri kwa utaratibu kwamba, Halmashauri itawarejeshea fedha zao. Hadi Kamati inajadili Taarifa ya Hesabu za Halmashauri, kiasi cha **Shilingi 7,899,063** kilikuwa hakijalipwa kwa wastaafu hao. Kitendo hiki kinarudisha nyuma ustawi wa wastaafu hao.

Ukiukwaji wa Kifungu cha 19 (1) na (2) cha Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii ya Watumishi wa Umma ya Mwaka 2018 umeisababishia Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga kutakiwa kulipa adhabu ya **Shilingi 3,137,762,978** inayotokana na kuchelewa kuwasilisha michango ya watumishi kwenye mfuko wa PSSSF.

**Mheshimiwa Spika**, Halmashauri ya Wilaya ya Bunda imekuwa ikiwakata watumishi wake 8 wanaolipwa kutoka katika mapato ya ndani kati ya mwaka 2006 hadi 2022. Aidha, Mkurugenzi ameshindwa kuwasilisha PSSSF kiasi cha **Shilingi 56,254,839** kwa kipindi cha **miezi 27 hadi 133** na kusababisha kutakiwa kulipa faini ya **Shilingi 114,475,055**. Vile vile, Halmashauri haikupeleka makato ya Waheshimiwa Madiwani katika Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) ya kiasi cha **Shilingi 10,305,000**.

**Mheshimiwa Spika**, Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu iliingia gharama ambazo hazina manufaa kutokana na Mkurugenzi kutopeleka michango ya watumishi wake kwa wakati baada ya kuwakata katika mishahara yao. Hadi mwezi Agosti, 2023, Mkurugenzi alishindwa kupeleka PSSSF michango ya watumishi ya **Shilingi 41,856,602** kwa muda uliotakiwa na kupelekea Halmashauri kutakiwa kulipa **Shilingi 149,793,808,361** kama adhabu ya kutowasilisha michango hiyo kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika**, wastaafu wengi wamekuwa wakikumbwa na usumbufu mkubwa wakati wa kufuatilia mafao yao kutokana na michango yao kutowasilishwa katika mifuko husika. Jambo hili halileti taswira nzuri kwa watumishi ambao walitumia sehemu kubwa ya maisha yao katika kuitumikia Serikali.

**2.7.4 Ucheleweshwaji wa Malipo kwa Wazabuni na Wakandarasi**

**Mheshimiwa Spika**, kwa muda mrefu, Serikali imekuwa ikitozwa riba kutokana na kuchelewesha malipo kwa kazi zilizokwisha fanyika au kwa huduma ambayo imekwishatolewa. Kiasi kikubwa cha fedha hizo kinacholipwa kama riba kingeweza kutumika katika kutekeleza miradi ya maendeleo kwa maslahi mapana ya Taifa.

Nia njema ya Serikali ya kuwezesha ukuaji wa makampuni ya ndani inakuwa haiakisi kile kinachofanyika katika Halmashauri zetu nchini ambapo, baadhi ya Wakurugenzi hawaoni umuhimu wa kuwalipa wazabuni na wakandarasi baada ya kupokea huduma. Inafahamika kwamba, ununuzi wowote unaofanyika unatokana na bajeti iliyoidhinishwa na Bunge. Hata hivyo, Wakurugenzi kwa bahati mbaya au kwa kukusudia wameshindwa kuweka kipaumbele katika ulipaji wa madeni yao na kusababisha athari

katika utoaji wa huduma, pamoja na kuchelewa kwa muda wa utekelezaji wa miradi.

**Mheshimiwa Spika**, imekuwa ni desturi kwa Halmashauri nyingi nchini kuua biashara za wazabuni wazawa kwa kutowalipa madeni yao kwa wakati licha ya kwamba Halmashauri hizo zinakuwa zimekwishapokea huduma kutoka kwa wazabuni hao. Kwa Halmashauri zilizofika mbele ya Kamati, zimebainika kuwa na madeni mengi na ya muda mrefu ambapo, Wakurugenzi hawakuonesha nia ya kulipa madeni hayo kutokana na kutokuwa na mpango wa kuingiza madeni hayo katika bajeti zinazofuata. Hali hii inaondoa uwezo wa wafanyabiashara wa ndani kushiriki katika kukuza biashara zao pamoja na uchumi wa taifa kwa kuwa wengi wao wanategemea kulipwa fedha hizo ili waweze kufanya marejesho ya mikopo iliyochukuliwa katika benki za kibiashara.

**Jedwali Na. 18**: Halmashauri zinazoongoza kudaiwa na Wazabuni/Wakandarasi

| S/N | Jina la Halmashauri | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | H/M Iringa | 2,867,302,995 |
| 2. | H/W Chamwino | 2,847,179,787 |
| 3. | H/Mji Tarime | 1,734,453,472 |
| 4. | H/M Kinondoni | 1,732,121,841 |
| 5. | H/W Karagwe | 1,594,640,649 |
| 6. | H/W Hanang' | 968,598,826 |
| 7. | H/W Kwimba | 952,139,921 |
| 8. | H/W Maswa | 858,886,687 |
| 9. | H/Mji Kondoa | 851,653,384 |

**Mheshimiwa Spika**, Kamati haijaridhishwa na namna Halmashauri zinavyoshindwa kuthamini biashara za wazawa na hii ni mifano michache ya Halmashauri tulizokutana nazo ambazo zinadaiwa na wazabuni kwa kuwa, karibu Halmashauri zote nchini zinadaiwa na wazabuni na hazioneshi jitihada ya kulipa madeni hayo. Hali hii inasababisha wafanyabiashara kukosa imani na Serikali yao ikiwa ni pamoja na kuua mitaji yao.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imezielekeza Halmashauri zote kuweka katika bajeti zao madeni ya wazabuni ili madeni hayo yaweze

kulipwa kwa wakati. Hali kadhalika, Kamati iliweka makubaliano na Wakurugenzi waliofika mbele ya Kamati na kuwekeana mpango wa ulipaji na muda wa utekelezaji wa madeni ya wazabuni. Aidha, Kamati inatumia nafasi hii kuzitaka Halmashauri zote nchini kulipa madeni yote ya wazabuni.

**2.8 Uendeshaji usiofaa wa Mfuko wa Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu**

**Mheshimiwa Spika**, Serikali kupitia azimio la Bunge la mwaka 1993 ilianzisha mikopo ya uwezeshaji kwa Vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu inayotokana na Asilimia 10 ya mapato ya ndani ya Halmashauri lengo likiwa ni kuwezesha Makundi ya Wanawake na Vijana kuanzisha na kuendeleza shughuli za ujasiliamali, kujiongezea kipato, kukuza uchumi na kupunguza umaskini kwa kuwapa mikopo yenye masharti nafuu.

Changamoto mbalimbali zilizosababisha kushindwa kufikia kwa lengo la kutolewa kwa mikopo hiyo, zilipelekea Mwaka 2018 Bunge kufanya marekebisho ya Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa Sura 290 kwa kuongeza kifungu cha 37A ambacho kimeweka masharti ya utengaji na utoaji wa Mikopo kwa vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu. Ili kuhakikisha kunakuwa na utekelezaji mzuri wa Sheria hiyo, Mwaka 2019, OR-TAMISEMI iliandaa Kanuni za Usimamizi na Utoaji wa Mikopo kwa Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu zilizofanyiwa marekebisho mwaka 2021.

**Mheshimiwa Spika**, Kanuni za Usimamizi na Utoaji wa Mikopo kwa Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu zimefafanua kwa kina wajibu wa kutenga fedha na kutoa mikopo, sifa na utaratibu wa kupata mkopo, taratibu za uombaji wa mkopo, taratibu za kutoa mkopo, matumizi ya fedha za mkopo, mafunzo kwa vikundi, hatua za kuchukua pindi kikundi kikishindwa kurejesha mkopo, majukumu ya Afisa Maendeleo ya Jamii, majukumu ya Kamati ya huduma za mikopo, majukumu ya timu ya Menejimenti ya Halmashauri, majukumu ya Kamati ya kudumu ya fedha, uongozi na mipango, majukumu ya ofisi za wakuu wa Mikoa na majukumu ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI.

Licha ya kuwepo kwa ufafanuzi huo, Kamati imesikitishwa na kitendo cha Wakurugenzi wengi kukiuka taratibu zilizowekwa kisheria. Uchambuzi wa Kamati katika eneo hili ni kama ifuatavyo:-

**2.8.1 Kushindwa kuchangia Bilioni 5.06 kwenye Mfuko wa Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu**

**Mheshimiwa Spika**, kufanikiwa kwa lengo la utoaji wa mikopo ya Asilimia 10 kutaiwezesha jamii kujikwamua kiuchumi. Hata hivyo, baadhi ya Halmashauri zimekuwa zikikwamisha azma ya Serikali kwa kutopeleka kikamilifu fedha hizo licha ya kwamba, Kifungu cha 37(A) cha Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura ya 290 (iliyorekebishwa mwaka 2019) kinazitaka Halmashauri kuchangia Asilimia 10 ya mapato yake ya ndani kwenye Mfuko wa Wanawake, Vijana na Watu wenye ulemavu kwa madhumuni ya kufadhili vikundi vilivyosajiliwa vya wanawake, vijana, na watu wenye ulemavu.

CAG ameripoti jumla ya Halmashauri 53 ambazo ni sawa na **Asilimia 28.8** ya Halmashauri zote zilizoshindwa kukamilisha michango yake katika mfuko wa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Uchambuzi wa Kamati kwa Halmashauri zilizofika mbele ya Kamati umeona ukubwa wa changamoto hiyo kwa Halmashauri nyingi kutokamilisha michango yake katika mfuko huo ambapo, Jumla ya **Shilingi 1,766,710,647** hazikupelekwa katika mfuko huo. Mfano wa Halmashauri ambazo hazikukamilisha michango yake zimetajwa katika jedwali namba. 19.

**Jedwali Na. 19**: Halmashauri ambazo hazikukamilisha michango katika Mfuko wa Wanawake, Vijana na watu wenye ulemavu

| **Na.** | **Jina la Halmashauri** | **Kiasi (Sh.)** |
|---|---|---|
| 1. | H/W Hanang’ | 164,492,228 |
| 2. | H/W Mufindi | 126,218,663 |
| 3. | H/W Geita | 93,151,682.53 |
| 4. | H/W Sengerema | 87,173,586 |
| 5. | H/W Manyoni | 72,621,194 |
| 6. | H/W Igunga | 65,620,434 |

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na changamoto ya kutopeleka fedha katika mfuko wa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu, kuna Halmashauri chache ambazo zilizingatia Kanuni hiyo na kupeleka kiasi chote cha fedha katika mfuko huo. Kamati inawapongezwa Wakurugenzi ambao, katika mwaka wa fedha 2021/2022 walizingatia matakwa ya Kanuni hiyo kwa kupeleka fedha zote kama inavyohitajika. Halmashauri zilizopeleka fedha zote za Asilimia 10 kutoka katika mapato ya ndani ni pamoja na H/W Itigi, H/W Mbogwe, H/Mji Mafinga, H/M Kahama, H/M Kinondoni, H/W Bukombe, H/Jiji Tanga, H/M Moshi, H/Mji Tunduma na H/W Muheza.

**2.8.2 Kutorejeshwa kwa fedha zilizotolewa kama Mkopo kwenye Vikundi Shilingi Bilioni 88.42**

**Mheshimiwa Spika**, uwajibikaji katika eneo la usimamizi wa mikopo inayotolewa katika vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu ni jukumu la kila mdau anayehusika katika zoezi hilo. Kutokuwepo kwa usimamizi mzuri wa mikopo hiyo kunaziweka Halmashauri katika hatari ya kupoteza fedha hizo na kutofikia malengo ya kuwainua wananchi kiuchumi. Aidha, Afisa maendeleo ya jamii wa Halmashauri husika anatakiwa kufuatilia marejesho ya mikopo hiyo.

Ili kuhakikisha kuna ufanisi katika urejeshaji wa mikopo, Kanuni imeelekeza sehemu ya fedha ya marejesho kutumikia kwa ajili ya usimamizi wa mikopo. Pamoja na uwepo wa fursa hiyo, Maafisa maendeo ya jamii wameshindwa kutekeleza majukumu yao kikamilifu kwa kutofuatilia urejeshaji wa fedha zilizokopeshwa kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa ya CAG imebainisha uwepo wa **Halmashauri 180** ambazo ni sawa na **Asilimia 97.8** kushindwa kusimamia na kuhakikisha fedha ya Serikali iliyokopeshwa inarejeshwa kwa mujibu wa mikataba iliyoingiwa kati ya Halmashauri na vikundi hivyo ili iweze kuwanufaisha watu wengine wenye uhitaji. Kamati imesikitishwa na hali hiyo kwa kuwa, wakati wa mahojiano na Wakurugenzi waliofika mbele ya Kamati, hapakutolewa sababu za msingi za kushindwa kukusanya fedha hizo licha ya muda wa marejesho ya mikopo hiyo kumalizika.

Kanuni ya usimamizi na utoaji wa mikopo kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu imefafanua hatua zinazotakiwa kuchukuliwa kwa kikundi kitakachoshindwa kurejesha mkopo kwa mujibu wa mkataba. Hata hivyo, hakuna hatua zozote zinazochukuliwa na Wakurugenzi kwa vikundi hivyo na kuacha kiasi kikubwa cha fedha katika mikono ya watu wachache. Katika uchambuzi wa Kamati, zipo baadhi ya Halmashauri ambazo hazijakusanya mikopo yake kufikia hadi kiasi cha **Shilingi Bilioni Moja**.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na Kamati kushauri mara kwa mara juu ya ukusanyaji wa mikopo, deni hilo limeongezeka kutoka **Shilingi Bilioni 47.01** iliyoripotiwa katika mwaka wa fedha ulioishia Juni, 2021 hadi **Shilingi Bilioni 88.42**. Ongezeko hili ni sawa na **Asilimia 47**. Tafsiri ya ongezeko hili ni uzembe wa Wakurugenzi pamoja na Maafisa Maendeleo ya jamii kuamua kukopesha fedha za umma bila ya kuzingatia Kanuni na miongozo ya utoaji wa mikopo hiyo.

**Jedwali Na. 20**: Halmashauri ambazo hazikukusanya fedha zilizokopeshwa kwa Vikundi vya Wanawake, Vijana na watu wenye ulemavu

| Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| 1. | H/M Kinondoni | 7,862,496,312 |
| 2. | H/Jiji Dar es Salaam | 5,562,659,779.92 |
| 3. | H/M Temeke | 2,894,366,125 |
| 4. | H/Jiji Arusha | 2,716,923,000 |
| 5. | H/Jiji Tanga | 1,317,500,900 |
| 6. | H/W Mbarali | 1,160,090,116 |
| 7. | H/W Mbinga | 669,922,371 |
| 8. | H/Mji Kasulu | 659,570,543 |
| 9. | H/W Igunga | 550,613,078 |
| 10. | H/W Urambo | 489,603,728 |
| 11. | H/Wilaya Musoma | 293,755,597 |

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilizielekeza Halmashauri zote ilizokutana nazo kuhakikisha fedha zote zinakusanywa na kuwekeana mpango thabiti wenye muda wa utekelezaji wa ukusanyaji wa fedha hizo. Aidha, kupitia taarifa hii inayosomwa katika Bunge

lako Tukufu tunazielekeza Halmashauri zote kuhakikisha kiasi chote kilichohojiwa na CAG kinakusanywa hadi kufikia mwezi Juni, 2024.

**2.8.3 Utoaji wa mikopo bila kuzingatia uwiano Shilingi Bilioni 20.79**

**Mheshimiwa Spika**, dhamira ya Serikali ya kupanga uwiano wa ugawaji wa mikopo ni kuhakikisha makundi yote muhimu yanapata haki sawa. Kifungu cha 37A (1-2) cha Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura ya 290 (iliyorekebishwa mwaka 2019) kinataka fedha zilizotengwa kutolewa kama mikopo kwa vikundi vilivyosajiliwa vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kwa uwiano wa 40% kwa wanawake, 40% kwa vijana na 20% kwa watu wenye ulemavu.

Kwa mujibu wa Taarifa ya CAG, Halmashauri 45 zilitoa mikopo bila ya kuzingatia uwiano na kuvinyima vikundi vingine fursa ya kupata mkopo. Hali hii isipodhibitiwa italeta malalamiko miongoni mwa wananchi na kuona makundi mengine kuwa yametengwa.

**2.8.4 Vikundi vilivyositisha shughuli za Biashara kushindwa kurejesha Shilingi Bilioni 2.25**

**Mheshimiwa Spika**, ni wajibu wa Halmashauri kutoa mafunzo kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu juu ya masuala ya uongozi, usimamizi wa fedha, uendeshaji wa miradi na utoaji wa taarifa hususan zinazohusu mkopo husika ili kuongeza tija ya matumizi ya mikopo itakayotolewa. Kanuni za utoaji na usimamizi wa mikopo inavitaka vikundi vyote kutumia fedha zinazopatikana kutekeleza miradi iliyoidhinishwa wakati wa kupata mkopo. Aidha, Kanuni inamtaka Afisa Maendeleo ya Jamii wa Halmashauri, kufuatilia uendeshaji na uwepo wa vikundi, urejeshaji wa mikopo iliyotolewa na ufuatiliaji wa mikopo iliyotolewa ili kuhakikisha kuwa inatumika kama ilivyokusudiwa.

Kamati imebaini uzembe wa baadhi ya Maafisa Maendeleo ya Jamii kutotekeleza takwa la kikanuni la kufuatilia na kuhakikisha fedha zote zilizokopeshwa zinarejeshwa ndani ya muda kwakuwa kutorejeshwa kwa fedha hizo ni upotevu wa fedha za umma. Katika Halmashauri zilizofika mbele ya Kamati, tatizo hilo lilibainika katika H/W Busega ambayo imeshindwa kukusanya kiasi cha **Shilingi 32,920,000** kilichotolewa kama mkopo katika vikundi vya vijana kutokana na vikundi hivyo kusitisha shughuli zake.

**2.8.5 Uwepo wa Vikundi Hewa vilivyopewa mikopo ya Shilingi Milioni 895.94**

**Mheshimiwa Spika**, utaratibu unahitaji kikundi kinachotarajia kuomba mkopo kuwa na nyaraka muhimu kama Katiba ya kikundi, barua ya utambulisho kutoka kwa Mtendaji wa Mtaa/Kijiji, Namba ya NIDA ya kila mwanakikundi na taarifa ya kina ya kikundi na shughuli wanazozifanya. Taarifa hizo zinaiwezesha Halmashauri kufahamu kwa undani aina ya watu ambao wanapatiwa mikopo hiyo.

Katika kufanya uhakiki wa vikundi vilivyopewa mikopo, CAG alishindwa kukutana na vikundi vilivyopewa mikopo ya **Shilingi Milioni 895.94**. Katika hali isiyotarajiwa, hata Maafisa Maendeleo ya Jamii wa Kata husika hawana taarifa za vikundi hivyo hali inayodhihirisha upotevu wa fedha za umma.

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa majadiliano na Halmashauri mbalimbali, CAG aliifahamisha Kamati kuwa, baadhi ya Halmashauri zilishindwa kuthibitisha uwepo wa baadhi ya vikundi. Mfano wa Halmashauri hizo ni H/M Kahama ambayo ilishindwa kukusanya mkopo wa **Shilingi 133,752,600** kwa vikundi ambavyo havijulikani vilipo.

Kwa upande wa H/Jiji Dar es Salaam, CAG alipohitaji kufanya uhakiki wa vikundi vilivyopewa mikopo, hakufanikiwa kukutana na vikundi 34 vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu vilivyopewa mikopo ya jumla ya **Shilingi 698,700,000** kutokana na kutokuwepo kwa vikundi hivyo.

**2.8.6 Fedha za Mikopo ya Vikundi kugawanywa miongoni mwa wanavikundi Shilingi Milioni 774.66**

**Mheshimiwa Spika**, ili kuwe na uhakika na urejeshwaji wa fedha zilizokopwa, Afisa Maendeleo ya Jamii anatakiwa Kusimamia uendeshaji na uhai wa vikundi. Aidha, mikopo iliyotolewa inatakiwa kutekeleza miradi iliyoidhinishwa na Kamati ya Fedha, Mipango na Usimamizi. Katika kufuatilia matumizi ya fedha zilizotolewa kwa vikundi, Kamati imebaini udhaifu katika usimamizi wa mikopo inayotolewa katika vikundi mbalimbali kwa wana kikundi kugawana fedha za mkopo na hatimaye kushindwa kurejesha mkopo huo.

Katika H/Jiji Arusha, **Shilingi 84,000,000** zilizotolewa kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu ziligawanywa miongoni mwa wana vikundi badala ya kutekeleza shughuli iliyokusudiwa.

**Mheshimiwa Spika**, ni dhahiri kuwa, kutowajibika kwa Wakurugenzi, Kamati ya Mikopo na Maafisa Maendeleo ya Jamii, kumesababisha hasara kubwa kwa taifa kama ambavyo tumeainisha hapo juu.

### 2.9 Mapungufu katika utekelezaji wa miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, Ibara ya 145 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imetamka uwepo wa Halmashauri. Aidha madhumuni ya kuwepo kwa Serikali za Mitaa ambayo ni pamoja na kutekeleza miradi ya maendeleo yametajwa katika Ibara ya 146 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Katika kuhakikisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo unafanyika kwa ufanisi na kuleta tija kwa wananchi, Kamati imeangalia maeneo mbalimbali yenye mapungufu katika miradi inayotekelezwa katika Halmashauri Nchini ikiwa ni pamoja na miradi iliyotelekezwa. Kutotumika kwa miradi ambayo imetumia fedha za umma kunaondoa thamani ya fedha ya miradi hiyo kama ambavyo Halmashauri ya Jiji la Tanga ilivyotumia **Shilingi Milioni 90** kujenga Masoko ya Mchukuuni na Tongoni ambayo mpaka sasa soko la Tongoni halitumiki licha ya kukamilika kwake mwaka 2020.

**Mheshimiwa Spika**, Mapungufu mengine yaliyobainika katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo ni kama ifuatavyo:-

#### 2.9.1 Wizara ya Fedha kutopeleka Fedha za Miradi

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na ukusanyaji finyu wa mapato ya Halmashauri, miradi mingi ya maendeleo inategemea ruzuku kutoka Serikali Kuu. Kamati imekutana na changamoto ya kusimama kwa miradi mingi ya maendeleo inayotekelezwa katika Halmashauri kutokana na Wizara ya Fedha kutopeleka fedha kwa wakati kwa ajili ya ununuzi wa vifaa na malipo ya wakandarasi. Kuchelewa kupeleka fedha hizo kwa kiasi kikubwa kumesababisha kuongezeka kwa gharama za miradi kutokana na

kupanda bei kwa bidhaa pamoja na riba kwa wakandarasi hali inayopelekea miradi hiyo kukosa tija iliyokusudiwa. Jedwali la 21 la taarifa hii linaonesha mifano ya Halmashauri zilizopokea ruzuku ya maendeleo pungufu ya bajeti.

**Jedwali Na. 21**: Halmashauri zilizopokea ruzuku ya maendeleo pungufu ya bajeti kutoka Serikali Kuu

| Jina la Halmashauri | Bajeti ya Maendeleo | Kiasi Kilichopokelewa | Pungufu | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| H/W Ileje | 6,929,636,350 | 2,596,663,801 | 4,332,972,549 | 63 |
| H/W Hanang' | 11,603,408,500 | 4,852,538,327 | 6,750,870,173 | 58 |
| H/Jiji Dar es Salaam | 25,440,770,900 | 11,911,797,740 | 13,528,973,160 | 53 |
| H/W Tarime | 17,727,292,209 | 10,866,886,373 | 6,860,405,836 | 39 |
| H/M Iringa | 9,265,196,965 | 6,172,434,719 | 3,092,762,246 | 33 |
| H/W Muleba | 19,013,674,866 | 12,713,980,617 | 6,299,694,249 | 33 |
| H/Mji Bunda | 8,325,104,651 | 5,886,095,004 | 2,439,009,646 | 29 |
| H/W Mbogwe | 15,718,750,850 | 11,290,665,093 | 4,428,085,757 | 28 |
| H/W Misungwi | 17,917,346,534 | 12,996,636,867 | 4,920,709,667 | 28 |
| H/W Ushetu | 7,860,633,000 | 5,664,785,483 | 2,195,847,517 | 28 |

**Mheshimiwa Spika**, dhamira ya kuwepo kwa Serikali za Mitaa ni kupeleka maendeleo kwa wananchi, Serikali kutopeleka fedha za maendeleo katika baadhi ya Halmashauri kunakwamisha ukamilishaji wa miradi iliyopangwa kutekelezwa katika mwaka husika. Kamati inaendelea kuisisitiza Serikali kuhakikisha inawajibika ipasavyo katika utekelezaji wa bajeti za maendeleo kwa kuhakikisha kiasi kilichotengwa kinapelekwa kwa ukamilifu wake.

### 2.9.2 Halmashauri kutochangia mapato yake ya Ndani katika Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Rais - TAMISEMI ilitoa barua yenye kumbukumbu Na.CBD.421/422/01/43 ya tarehe 3 Januari, 2018

ambapo Halmashauri ziligawanywa katika makundi mawili "A" na "B na kuzielekeza kutenga Asilimia 40 na Asilimia 60 ya mapato ya vyanzo vyake vya ndani, mtawalia kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Lengo la kuzitaka Halmashauri kuchangia katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo ni kuhakikisha Halmashauri zote zinawajibika katika kuharakisha maendeleo ya wananchi katika maeneo yao.

Kamati imepokea taarifa ya miradi mingi iliyosimama kutokana na fedha za mapato ya ndani kutopelekwa katika utekelezaji wa miradi hiyo kwa mujibu wa Sheria na taratibu na badala yake fedha hizo zimekuwa zikitumika katika matumizi ya kawaida ya Halmashauri. Taarifa ya Halmashauri ambazo hazikuchangia kikamilifu katika miradi ya Maendeleo zimeelezwa katika Jedwali namba 22.

**Jedwali Na. 22:** Halmashauri ambazo hazikukamilisha michango ya fedha za miradi ya Maendeleo kutoka katika mapato ya ndani

| Jina la Halmashauri | Asilimia 40 iliyotakiwa kuchangiwa | Michango iliyopelekwa katika miradi | Pungufu | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| H/W Bunda | 373,495,840 | 60,000,000 | 313,495,840 | 84 |
| H/W Chamwino | 729,349,321 | 164,000,000 | 566,497,402 | 78 |
| H/W Uvinza | 827,192,000 | 383,340,000 | 443,852,000 | 54 |
| H/W Rorya | 431,529,378 | 216,730,000 | 214,799,378 | 49.8 |
| H/W Itigi | 538,126,065 | 278,840,192 | 259,285,873 | 48 |
| H/W Korogwe | 442,546,800 | 237,200,294 | 205,346,506 | 46 |
| H/W Kilindi | 697,708,932 | 416,398,818 | 281,310,114 | 40.3 |
| H/W Sengerema | 759,440,179 | 457,672,144 | 301,768,035 | 40 |
| H/Mji Bunda | 521,396,344 | 359,520,149 | 161,876,195 | 31 |

**Mheshimiwa Spika**, tumezielekeza Halmashauri zote ambazo zimekiuka Mwongozo wa OR – TAMISEMI wa kuchangia mapato ya ndani katika miradi ya maendeleo na badala yake kuzitumia katika matumizi ya kawaida kuhakikisha fedha husika zinapelekwa

katika miradi ya maendeleo. Kwa Halmashauri 74 tulizokutana nazo, ambazo jumla ya **Shilingi 13,401,513,174** hazikupelekwa katika miradi ya maendeleo kutoka katika mapato ya ndani, tumewekeana mpango wa utekelezaji na zile ambazo hatujakutana nazo tunatumia fursa hii kuziagiza Halmashauri zote zilizotajwa katika Ripoti ya CAG kukamilisha utekelezaji wa mapendekezo ya CAG.

**2.9.3 kutokamilika kwa miradi ya maendeleo kwa wakati Shilingi Bilioni 112.24**

**Mheshimiwa Spika**, dhamira ya kutekeleza miradi ya maendeleo ni pamoja na kufikisha huduma zitakazowanufaisha wananchi katika maeneo yao. Kuchelewa kukamilika kwa miradi hiyo kunasababisha kuchelewa kupatikana kwa manufaa yaliyokusudiwa licha ya kuwepo kwa kiasi kikubwa cha fedha ambacho kimeshatumika katika miradi hiyo.

Uchambuzi wa Kamati ulibaini miradi iliyotumia jumla ya **Shilingi 9,626,490,048** inayotekelezwa na H/Jiji Tanga ambayo ipo katika hatua mbalimbali, kutelekezwa kwa muda mrefu. Kuchelewa kukamilika kwa miradi hiyo kunawakosesha wananchi fursa ya kunufaika na miradi hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, H/W Muleba ilipokea **Shilingi 2,066,717,792** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi 17 ambayo hadi kukamilika kwa ukaguzi wa mwaka 2021/2022, miradi hiyo ilikuwa haijakamilika. Aidha, uchambuzi wa Kamati umebaini kutokuwepo kwa tathmini ya gharama ya kukamilisha miradi hiyo hali itakayosababisha miradi hiyo kutelekezwa kwa muda mrefu na kukosekana kwa thamani ya fedha.

Tatizo la kutelekeza miradi kwa kiasi kikubwa limeonekana katika H/W Igunga kwa kuwepo kwa miradi 27 iliyopaswa kutekelezwa kwa gharama ya **Shilingi 1,075,200,000** kati ya mwaka wa fedha 2015/16 hadi 2020/21. Mengi ya miradi hiyo ni maboma ya zahanati yaliyojengwa kwa nguvu za wananchi kuanzia mwaka 2000 hadi 2015 ambayo yametelekezwa bila ya kukamilishwa. Hadi Kamati ilipofanya majadiliano na Mkurugenzi wa H/W Igunga, **Shilingi 325,741,250** zilishatumika. Hata hivyo, hakuna tathmini iliyofanyika ili kufahamu gharama halisi zinazotakiwa kwa

ajili ya kukamilisha miradi hiyo kutokana na kutotekelezwa kwa muda mrefu.

**2.9.4 Fedha za Miradi ya Maendeleo zilizobadilishiwa matumizi Billioni 1.60**

**Mheshimiwa Spika**, utumiaji wa fedha kinyume na bajeti kunaathiri utekelezaji wa shughuli za maendeleo zilizopangwa na ni kinyume na Kifungu cha 47 (1) (a) cha Sheria ya Bajeti Sura 439. Taarifa ya CAG imebainisha uwepo wa Asilimia 7.6 ya Halmashauri ambazo zimebadilisha matumizi ya fedha za miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, mfano wa hoja hii ni H/W Bariadi ambayo ilibadilisha matumizi ya **Shilingi 110,224,078** iliyopangwa kutumika kwa ajili ya ujenzi wa nyumba ya Mkurugenzi wa Halmashauri bila ya kupata kibali kutoka Wizara ya Fedha. Vile vile, H/W Rorya ilitumia kwa ajili ya matumizi mengineyo **Shilingi 59,802,030** zilizopangwa kutumika kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Ukaguzi uliofanyika katika H/W Ileje ulibainisha kuwa, Halmashauri ilipokea kiasi cha **Shilingi 800,000,000** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa wodi ya wananawake na wanaume, chumba cha upasuaji na chumba cha kuhifadhia maiti. Katika fedha hizo, Halmashauri ilitumia **Shilingi 214,939,843** kwa ajili ya ujenzi wa uzio, njia za kutembelea (walkways) na jengo la wagonjwa wa nje kinyume na kusudi la matumizi ya fedha hizo.

**Mheshimiwa Spika**, H/W Maswa imehusika pia katika tatizo la kubadilisha matumizi ya fedha za miradi ya maendeleo ambapo, Halmashauri ilipanga kujenga kiwanda cha chaki chenye thamani ya **Shilingi 21,387,183,700**. Kiwanda hiko kilipangwa kujengwa katika eneo la Kiwanda cha Ng'hami. Katika kipindi cha miaka minne mfululizo 2018/19 hadi 2021/22, Halmashauri ilitenga **Shilingi 8,200,000,000** kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo. Aidha, katika kipindi hicho, kiasi cha **Shilingi 8,099,982,784.04** sawa na Asilimia 99 ya fedha zote kilipokelewa na kubakisha kiasi cha **Shilingi 132,000,000.70**. Mapitio ya ripoti ya utekelezaji ilibaini kwamba, **Shilingi 5,870,956,244.04** zilitumika kutekeleza shughuli iliyopangwa katika bajeti. Aidha, **Shilingi 2,097,026,539.30** zilitumika kwa shughuli ambazo hazikupangwa katika bajeti ya mradi huo

kinyume na Agizo 23(1) la Memoranda ya Fedha za Halmashauri ya Mwaka 2009.

**Mheshimiwa Spika**, uamuzi wa H/W ya Maswa kutumia fedha za mradi kwa shughuli ambazo hazikuwa katika bajeti kunathiri mtiririko wa fedha za mradi huo.

**Mheshimiwa Spika**, Utumiaji wa fedha kinyume na malengo ni ukiukwaji wa Sheria lakini pia kunachelewesha ukamilishaji wa miradi iliyoanzishwa hali inayopelekea miradi hiyo kuchelewa kutumika hivyo kukosa thamani ya fedha.

### 2.9.5 Kutotekelezwa kwa Mipango ya Miradi ya Wajibu kwa Jamii (CSR)

**Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha Jamii inanufaika na uwekezaji unaofanywa katika maeneo yao hasa katika eneo la uchimbaji wa madini, Kifungu cha 105 (1), (2) na (4) cha Sheria ya Madini, Sura ya 123 inawataka wenye leseni za madini kuandaa mpango wa miradi ya kurudisha kwa jamii (CSR) na kuuwasilisha kwa Halmashauri katika eneo linalohusika. Vile vile, wajibu wa Halmashauri kusimamia utekelezaji wa mpango uliowasilishwa umeelezwa katika kifungu cha 105(4) cha Sheria ya Madini, Sura ya 123.

Kamati imekutana na Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga na kubaini kutotekelezwa kwa miradi ya CSR kutoka katika Makampuni 8 za uchimbaji wa madini kinyume na Kifungu cha Sheria kilichofafanuliwa hapo juu. Hadi Halmashauri ilipokutana na Kamati ni Mradi wa umaliziaji wa Zahanati iliyopo katika Kijiji cha Paradiso wenye thamani ya **Shilingi Milioni 15** ndio uliotekelezwa na kuacha kutekeleza miradi iliyobaki yenye thamani ya **Shilingi Milioni 98**.

**Mheshimiwa Spika**, dhamira ya Serikali ya kutekeleza mpango wa wajibu kwa jamii inashindwa kukamilika kutokana na Makampuni ya Madini kukiuka makubalino kama ambavyo mgodi wa kuchimba dhahabu wa Geita (GGML) kukataa kutoa fedha za CSR za jumla ya **Shilingi 3,911,650,602** kinyume na makubaliano iliyoingia na Halmashauri ya Wilaya ya Geita.

**Mheshimiwa Spika**, tathmini ya jumla ya Kamati kuhusu utekelezaji wa mpango wa wajibu kwa jamii (CSR) kwa Halmashauri zote zenye miradi ya aina hiyo imebaini kuwa, makubaliano (MOU) kati ya Halmashauri na wawekezaji hayalindi maslahi ya Halmashauri ambapo MOU zinatoa nafasi kwa Halmashauri kushiriki kwenye uandaaji wa mpango wa wajibu kwa jamii (CSR) na kunyima nguvu kwenye utekelezaji wa miradi hiyo kwani kwa sehemu kubwa Halmashauri haishiriki wakati wa utekelezaji wa mradi bali wanakabidhiwa itakapokamilika.

**Mheshimiwa Spika**, Udhaifu wa Halmashauri katika kuingia makubaliano (MOU) inanyima fursa na kutolinda masilahi ya wananchi kiujumla.

**2.9.6 Utekelezaji wa Miradi ambayo haina Tija kwa Serikali**

**Mheshimiwa Spika**, Serikali imejenga vituo vya afya takriban 352 Nchi nzima, Kituo cha Afya cha Tlawi kilichopo katika Halmashauri ya Mji wa Mbulu ni miongoni mwa vituo hivyo vilivyojengwa na Serikali. Kamati imechambua kwa kina kuhusu mradi huu ambapo imebainika kuwa, kituo hiko hakikujengwa katika eneo linalomilikiwa na H/Mji Mbulu na badala yake kilijengwa katika eneo la Kanisa Katoliki Tlawi kwa gharama za **Shilingi 500,000,000.** Serikali ilipeleka vifaa tiba vyenye thamani ya **Shilingi 352,844,470** na katika mwaka wa fedha 2021/2022, Serikali pia ilichangia **Shilingi 127,415,000** kwa ajili ya dawa na vifaa tiba.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na Serikali kuwekeza katika ujenzi wa majengo, vifaa tiba, ruzuku za MSD na wafanyakazi 10, H/Mji Mbulu haina mamlaka na rasilimali zote zilizowekwa. Aidha, mapato na matumizi ya Kituo hiko cha Afya hayatambuliki na hayakaguliwi na kuifanya Halmashauri kushindwa kukisimamia kituo hiko. Kamati inashindwa kufahamu sababu ya Serikali kufanya uwekezaji katika eneo ambalo halina mamlaka nayo na hakuna faida inayopatikana.

**2.9.7 Pangea Mineral Limited kugoma kutoa fedha kwa ajili ya mradi wa Hospitali ya Manispaa ya Kahama**

**Mheshimiwa Spika,** Tume ya Madini iliandika barua yenye Kumb: AB. 112/250/01C/16 ya tarehe 21 Machi, 2022 kwa Halmashauri ya

Manispaa ya kahama ikieleza kuwa, Pangea Mineral Limited ilitakiwa kutoa **Shilingi Bilioni 3.985** kwa ajili ya kusaidia ujenzi wa jengo la wagonjwa wa nje na wodi ya wazazi ikiwa ni fedha kwa ajili ya mpango wa kufunga mgodi wa Buzwagi. Hata hivyo, Pangea imekataa kutoa kiasi kilichoelekezwa hapo juu kwa barua yenye kumb: Na.PML/BGM/0049/2022 ya tarehe 2 Mei, 2022. Hadi Kamati ilipokutana na Mkurugenzi wa Kahama MC, **Shilingi 805,600,970** pekee ndizo zilizotolewa na Pangea na kubakiwa na deni la **Shilingi 3,179,399,030**.

**Mheshimiwa Spika**, Serikali ichukue juhudi za makusudi ili kuhakikisha deni hilo linalipwa kwa H/M Kahama ili mradi ulioainishwa uweze kutekelezwa kikamilifu.

## 2.10 Utendaji usioridhisha wa baadhi ya Halmashauri

**Mheshimiwa Spika**, usimamizi mzuri wa matumizi ya fedha za Umma kwa kiasi kikubwa unategemewa na ufanisi katika utendaji wa Wakurugenzi wa Halmashauri. Ufanisi huo ni pamoja na kuhakikisha kunakuwa na ongezeko la mapato ya ndani, uzingatiaji wa Sheria, Kanuni, taratibu na miongozo, matumizi sahihi ya fedha za umma na utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo.

Wakati wa mahojiano na Wakurugenzi wa Halmashauri mbalimbali, Kamati ilibaini baadhi yao kuwa na utendaji usioridhisha na kusababisha Serikali kushindwa kufikia malengo yake ya kutoa huduma bora kwa wananchi wake. Baadhi ya Halmashauri zilizokutwa na mapungufu makubwa ni pamoja na H/W Nkasi, H/W Kibaha na H/W Kigoma.

### 2.10.1 Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi

**Mheshimiwa Spika**, H/W Nkasi ilifika katika Kikao tarehe 18 Oktoba, 2023 kwa ajili ya uchambuzi wa Taarifa ya Hesabu zilizokaguliwa kwa mwaka wa fedha 2021/22. Uchambuzi uliofanywa na Kamati ulibaini kuwa, Mkurugenzi alishindwa kutekeleza mapendekezo yaliyotolewa na CAG kwa hesabu zinazoishia Mwezi Juni, 2022, ambapo, Hoja 12 pekee kati ya hoja 33 zilizotolewa na CAG ndizo zilizotekelezwa. Aidha, kwa hoja zilizotolewa kwa miaka iliyopita kuanzia 2017/18 hadi 2020/21, Halmashauri ilitekeleza kikamilifu hoja 11 pekee kati ya hoja 23

zilizotolewa na CAG. Kushindwa kutekeleza hoja na mapendekezo ya CAG kwa muda mrefu kunasababisha matatizo yaliyoibuliwa na CAG kujirudia kila mwaka.

Katika hesabu zinazoishia mwezi Juni, 2022, Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi ilipata **Hati yenye Shaka**. Sababu za kutolewa kwa hati hiyo ni pamoja na:-

a) Mapato ya ruzuku ya Serikali kuripotiwa zaidi kwa **Shilingi 133,440,565** kwa mwaka wa fedha unaoishia Juni, 2022 ambapo Halmashauri ilikuwa na mapato ya ruzuku ya Serikali ya **Shilingi 32,101,738,657** ambapo katika vitabu iliripotiwa **Shilingi 32,235,179,222**;

b) Kupunguzwa kwa fedha taslimu zilizotumika kununua mali za kudumu **Shilingi 162,935,000** ambapo, mapitio ya taarifa ya mtiririko wa fedha ilionesha Halmashauri kutumia **Shilingi 7,648,550,098** kununua mali za kudumu. Hata hivyo baada ya mapitio, CAG alibaini Halmashauri kutumia **Shilingi 7,811,485,098** kwa ajili ya ununuzi wa mali za kudumu ikiwa ni zaidi ya kiasi kilichoripotiwa katika vitabu;

c) Fedha za ruzuku ya miradi ya maendeleo zilizovuka mwaka kuripotiwa pungufu kwenye mizania ya Hesabu **Shilingi 162,772,356** kwa kuwa, uhalisia wa fedha za miradi ya maendeleo ni **Shilingi 704,689,630** tofauti na kiasi kilichoripotiwa katika vitabu cha **Shilingi 541,917,282**;

d) Kuzidishwa kwa madai na madeni yanayohusiana na mfuko wa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kwa kuripoti bakaa ya fedha zilizobaki kwenye mfuko huo kwa ziada ya **Shilingi 11,151,947** kutokana na deni liliowekwa katika "Note 32" kuwa **Shilingi 3,259,042** tofauti na madeni yaliyoripotiwa katika "Note 47" ya **Shilingi 14,410,989**. Aidha, kutokana na uamuzi wa kutounganisha taarifa za fedha za mfuko wa WYDF, Halmashauri ilitakiwa kuondoa kwenye hesabu jumuifu madai ya **Shilingi 144,269,000** yanayohusiana na mikopo isiyorejeshwa kwa mwaka wa fedha ulioishia Juni, 2021. Hata hivyo, kiasi hicho hakikuondolewa katika hesabu jumuifu za Halmashauri hivyo kusababisha madai kuwa zaidi kwa mwaka wa fedha ulioishia Juni, 2022;

e) Kiasi ambacho hakikuchangiwa katika mfuko wa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kwa mujibu wa Kanuni kutotambuliwa kama deni katika vitabu vya Halmashauri kiasi cha **Shilingi 118,684,731** kinyume na Kanuni na Maelekezo yaliyotolewa na OR – TAMISEMI;

f) Tofauti ya kiasi kilichooneshwa kwenye mtiririko wa fedha (*operating activities*) na kiasi kilichooneshwa kwenye usuluhishi wa mtiririko (*reconciliation*) wa fedha **Shilingi 43,980,146**; na

g) Kutofautiana kwa kiasi linganifu kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2021 bila ya kutolewa kwa taarifa juu ya sababu za marekebisho na maeneo yaliyoathiriwa.

**Mheshimiwa Spika**, H/W Nkasi imekosa ubunifu wa vyanzo vipya vya mapato na kukosa udhibiti wa vyanzo vilivyopo kwa kushindwa kufikia malengo ya ukusanyaji wa mapato ya ndani kwa miaka mitatu mfululizo. Katika kipindi cha Miaka mitatu 2019/20 hadi 2021/22, Halmashauri ilikusanya mapato ya ndani pungufu kwa Asilimia 24, Asilimia 22 na Asilimia 11 mtawalia.

H/W Nkasi kwa kutofuata taratibu haikuwasilisha RUWASA fedha ya matazamio **Shilingi 171,456,413** ambayo ilitakiwa kuhamishwa kutoka katika Akaunti ya Amana. Aidha, kumekuwa na ukiukwaji wa Sheria na Kanuni za Ununuzi wa Umma katika maeneo mengi ambapo, Halmashauri ilifanya ununuzi wa **Shilingi 153,332,283** bila ya idhini ya Bodi ya zabuni, kufanya ununuzi wa **Shilingi 126,507,937** bila ya taratibu za ushindanishi wa bei, kufanya ununuzi wa **Shilingi 144,915,320** bila ya uwepo wa mikataba, manunuzi ya bidhaa bila ya kupata idhini ya Mkurugenzi **Shilingi 255,177,689** na kufanya manunuzi ya **Shilingi 7,706,634,454** nje wa mpango wa ununuzi wa Halmashauri.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2021/22, H/W Nkasi ilipokea **Shilingi 12,358,658,980** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kutoka Serikali Kuu na wadau mbalimbali wa maendeleo. Fedha hizo ni sawa na **Asilimia 124** ikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa na Bunge ya **Shilingi 9,996,701,980**. Licha ya Halmashauri kupokea ziada ya **Shilingi 2,361,388,409**, bado kuna miradi ya maendeleo ambayo utekelezaji wake haujakamilika.

Vile vile, Mwongozo unaitaka H/W Nkasi kutenga Asilimia 40 ya mapato yake ya ndani kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Katika mwaka wa fedha unaoishia mwezi Juni, 2022, Halmashauri ilitakiwa kupeleka fedha za utekelezaji wa miradi ya maendeleo **Shilingi 797,789,105**. Hata hivyo, Halmashauri ilipeleka **Shilingi 380,101,534** tu ambayo ni sawa na **Asilimia 48** ya fedha zote zilizotakiwa kupelekwa na kuacha kupeleka **Shilingi 417,687,571** sawa na **Asilimia 52**.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati haijaridhishwa na utendaji wa H/W Nkasi kutokana na uwepo wa dosari nyingi katika vitabu vya Halmashauri hali inayotia mashaka ya uwezo na weledi wa watendaji waliopewa dhamana ya kusimamia na kutumia fedha za umma kwa niaba ya wananchi wa eneo hilo.

### 2.10.2 Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha

**Mheshimiwa Spika**, tarehe 11 Oktoba, 2023, Kamati ilifanya majadiliano na Mkurugenzi wa H/W Kibaha kuhusu hesabu zilizokaguliwa kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2022. Katika uchambuzi wa taarifa hiyo, Mkurugenzi wa H/W Kibaha alizikataa taarifa zilizowasilishwa na CAG katika maeneo mbalimbali hasa kuhusu kiwango cha fedha kilichopelekwa katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo kutoka katika mapato yake ya ndani.

**Mheshimiwa Spika**, ili kuthibitisha ufafanuzi uliotolewa na Mkaguzi wa Mkoa wa Pwani kutoka Ofisi ya Taifa ya ukaguzi **Ndg. Mary T. Dibobo** kuhusu kiasi cha fedha kilichopelekwa na H/W Kibaha katika miradi ya maendeleo kutoka katika mapato ya ndani.

**Nukuu:-**

***"Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, ninaomba nitoe maelezo hapo kwamba sisi figure ambayo tunaitoa kama mapato lindwa tunaichukua kwenye taarifa ya mwisho ya CAG ambayo ni ya mwaka 2021/2022 kilichokuwepo kwenye financial statement. Kwa hiyo, tuna-relay pale, contradiction hapa nimeona ni kwenye haya mapato lindwa kwa sababu wao wamesema mapato lindwa ni shilingi milioni 700. Sisi tumesema ni***

***shilingi milioni 300. Hii milioni 300 yetu base yetu ni kitabu cha financial statement cha mwisho cha mwaka 2021/2022"***

**Mwisho wa Nukuu.**

CAG aliieleza Kamati kuwa, katika mwaka wa fedha 2021/22, Halmashauri ilipaswa kupeleka katika miradi ya maendeleo kiasi cha **Shilingi 1,714,909,856** sawa na 40% ya mapato yake ya ndani. Hata hivyo hadi Taarifa inawasilishwa mbele ya Kamati, H/W Kibaha ilipeleka kiasi cha **Shilingi 412,672,179** tu na kushindwa kupeleka **Shilingi 1,302,237,677** sawa na **Asilimia 75.93**. Hata hivyo Mkurugenzi alidai kupeleka kiwango kikubwa zaidi ya kilichowasilishwa na CAG bila ya kuwa na uthibitisho. Vile vile, Mkurugenzi alishindwa kutoa takwimu sahihi kuhusu hoja zilizoibuliwa na wajumbe.

**Mheshimiwa Spika**, ili kuthibitisha ukinzani uliotokea katika eneo la fedha za miradi ya maendeleo kutoka katika mapato ya ndani ya Halmashauri, naomba kunukuu majibu yaliyotolewa na Mkurugenzi wa H/W Kibaha Ndg. **BUTAMO NDALAHWA** kuhusu hoja hiyo.

**Nukuu:-**

***"Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kukihakikishia kikao chako kwamba, tumepeleka fedha kwenye miradi ya maendeleo, jumla ya shilingi bilioni 2.1 ukijumlisha na ile bilioni 412 ambayo CAG ameandika…"***

**Mwisho wa Nukuu.**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitanzika na kushindwa kuendelea na majadiliano kutokana na kutokubaliana kati ya mkaguzi na mkaguliwa ambapo Mkaguzi mwingine kutoka Ofisi ya Taifa ya ukaguzi Ndg. **LUCAS N. PADARI** alieeleza Kamati kuwa,

**Nukuu**:-

"***Mheshimiwa Mwenyekiti, napata kigugumizi kwa sababu ya hesabu walizotupatia na CAG atatoa opinion.***

***Kama atatoa unqualified opinion, ina maana hizi taarifa ambazo wanazotoa alitakiwa apate qualification. Ndiyo maana yake, kwa hiyo wanataka ku dispute opinion ya CAG, kitu ambacho naona kwamba kitakuwa ni kigumu sana*."**

**Mwisho wa Nukuu.**

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na tatizo hilo, mapungufu kadhaa yalibainika katika utendaji wa H/W Kibaha ikiwa ni pamoja na uwepo wa tofauti kubwa kati ya makisio ya mapato ya ndani na uhalisia wa makusanyo, kutopeleka fedha katika mfuko wa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kwa kiasi cha **Shilingi 172,669,937** pamoja na kutoa fedha hizo bila ya kuzingatia uwiano uliowekwa.

Mapungufu mengine yaliyobainika katika H/W Kibaha ni kutokamilika kwa wakati kwa miradi ya maendeleo inayotekelezwa kwa fedha za ruzuku na fedha za mapato ya ndani. Vile vile, Halmashauri imekuwa ikikiuka Sheria ya Ununuzi wa Umma na Kanuni zake kwa kufanya ununuzi ulioidhinishwa na wajumbe wawili tu wa Bodi ya zabuni wa **Shilingi 63,406,000** kinyume na Sheria, ununuzi wa samani za ofisi za **Shilingi 392,734,592.37** kwa kutumia zabuni ya chanzo kimoja badala ya kutumia ushindanishi wa bei.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati haikuridhishwa na mwenendo wa ulipwaji wa madeni ya watumishi kutokana na uwepo wa madeni yasiyolipika kwa muda mrefu ya **Shilingi 978,314,070**, madeni kwa ajili ya kusafirisha watumishi wastaafu na waliofariki pamoja na mizigo yao **Shilingi 108,432,521**. Vile vile, Mkurugenzi ameruhusu watumishi wake kupokea mishahara chini ya kiwango kilichowekwa cha kutopungua moja ya tatu ya mshahara wa mwezi kabla ya makato (*basic salaries*).

**Mheshimiwa Spika**, Ukaguzi uliofanya wa Nyongeza Na. 2 (Addendum No.2) kati ya H/W Kibaha na SUMA JKT kuhusu mradi wa kuboresha jengo la ofisi la Halmashauri awamu ya kwanza kupitia Mkataba No.LGA/010/2016-2017/W/BLD/01 wa **Shilingi 2,745,425,524** katika kipindi cha kuanzia 10/07/2017 hadi

10/07/2019 uliibua mapungufu kadhaa ikiwa ni pamoja na muda wa kumalizika kwa mkataba kutoainishwa katika mkataba, Nyongeza Na 2 kutolewa nje ya muda wa mkataba ambapo, mkataba ulimalizika tarehe 25/1/2022 bila ya uwepo wa muda wa nyongeza wakati nyongeza ilisainiwa tarehe 08/06/2022.

Mapungufu mengine yaliyobainika katika mradi huo ni mkataba huo wa nyongeza kutopata idhini ya Bodi ya zabuni, mkataba kutopitiwa na Mwanasheria wa Halmashauri, kutokuwepo kwa makadirio ya gharama za mkandarasi kwa kazi au bidhaa nunuliwa, na kutokamilika kwa mradi huo hadi kufikia tarehe 22/09/2022.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya uchambuzi wa kina wa utendaji wa Halmashauri hii. Kamati inaona kuna haja ya Serikali kuongeza usimamizi katika Halmashauri hii ikiwa ni pamoja na kuchunguza iwapo kuna matumizi sahihi ya fedha za umma.

### 2.10.3 Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma

**Mheshimiwa Spika**, tarehe 26 Oktoba, 2023, Kamati ilikutana na H/W Kigoma kwa ajili ya kujadili na kuchambua taarifa ya Hesabu zilizokaguliwa za Halmashauri hiyo kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Katika kufanya majadiliano na Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Kamati ilibaini utendaji usioridhisha wa Halmashauri hiyo ikiwa ni pamoja na kutotekelezwa kikamilifu na kwa muda mrefu kwa hoja na mapendekezo ya CAG pamoja na maagizo ya LAAC.

**Mheshimiwa Spika**, mtiririko wa mapato wa Halmashauri hii si wa kuridhisha kutokana na kukosekana kwa ubunifu wa kuibua vyanzo vipya vya mapato na kushindwa kuongeza usimamizi wa mapato ya ndani ambapo katika kipindi cha miaka mitatu mfululizo, makadirio ya bajeti ya makusanyo ya ndani hayajafika **Shilingi Bilioni Moja**.

Kwa upande wa uchangiaji wa fedha za utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika kipindi cha miaka mitatu mfululizo, H/W Kigoma ilishindwa kupeleka jumla ya kiasi cha **Shilingi 357,588,380** ambapo katika mwaka wa fedha 2021/2022 **Shilingi 129,935,244** hazikupelekwa katika miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, H/W Kigoma haikuwasilisha kwa CAG taarifa inayoonesha kiasi cha madeni ya watumishi kilicholipwa hadi sasa kati ya **Shilingi 2,388,222,000**.

Katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo, H/W Kigoma ilitekeleza miradi yenye jumla ya **Shilingi 3,260,000,000** bila kupata hati miliki za ardhi. Vile vile, Kamati imebaini uwepo wa miradi ya maendeleo ambayo haijakamilika ya **Shilingi 1,750,000,000**. Aidha, Halmashauri ilitelekeza miradi yenye thamani ya **Shilingi 125,540,000** ambayo mikataba yake iliisha muda kabla ya kazi kukamilika.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na changamoto zilizoainishwa hapo juu, H/W Kigoma ilifanya malipo ya **Shilingi 76,109,385** kwa wazabuni mbalimbali bila ya kupokea risiti za kielektroniki (EFD) hali iliyokosesha mapato ya Serikali pamoja na kupokea bidhaa nunuliwa za **Shilingi 38,346,800** bila ya kufanya ukaguzi.

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa majadiliano na Mkurugenzi na watendaji wa H/W Kigoma, Kamati haijaridhishwa na ufanisi wa watendaji hao kwa kutotoa taarifa sahihi kwa Kamati pamoja na kuwepo kwa mapungufu mengi ambayo, endapo watumishi hao wangewajibika ipasavyo, mapungufu hayo yasingekuwepo. Kamati imeilekeza OR – TAMISEMI kufanya usimamizi wa Karibu wa Halmashauri hii.

### 2.11 Changamoto za kiutendaji katika Sekta ya Afya

**Mheshimiwa Spika**, CAG amefanya ukaguzi katika Sekta ya Afya ili kutathmini mwenendo wa utoaji wa huduma za afya katika Halmashauri. Kamati inafahamu juhudi zinazochukuliwa na Serikali katika kuimarisha huduma za Afya Nchini. Hata hivyo, Serikali haifikii malengo yaliyokusudiwa kutokana na mapungufu mbalimbali ikiwa ni pamoja na upungufu wa miundombinu na uhaba wa dawa na vifaa tiba. Changamoto zilizojadiliwa na Kamati ni pamoja na:-

### 2.11.1 Bohari Kuu ya Dawa (MSD) kutopeleka Dawa na Vifaa Tiba Shilingi Bilioni 8.16

**Mheshimiwa Spika**, Serikali kupitia Wizara ya Fedha imekuwa ikipeleka fedha MSD kwa ajili ya ununuzi wa dawa na vifaa tiba katika Hospitali na vituo vya Afya. Hata hivyo, Kamati imebaini kutopelekwa kwa dawa na vifaa tiba kama zinavyoagizwa na Halmashauri. Kutosambazwa kwa dawa na vifaa tiba vilivyoagizwa kunaathiri uwezo wa vituo vya afya katika utoaji wa huduma bora kwa jamii. Mfano wa Halmashauri ambazo hazijapokea dawa na vifaa tiba kutoka MSD imetajwa katika jedwali namba 23.

**Jedwali Na. 23**: Halmashauri ambazo hazikupokea dawa na vifaatiba kutoka MSD

| S/N | Jina la Halmashauri | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | H/M Temeke | 3,416,418,284 |
| 2. | H/Jiji Dar es Salaam | 2,952,045,395 |
| 3. | H/W Sengerema | 1,045,610,476 |
| 4. | H/W Maswa | 658,652,000.54 |
| 5. | H/W Mbinga | 577,711,402 |

**Mheshimiwa Spika**, Kamati haijaridhishwa na hali ya upatikanaji wa dawa na vifaa tiba katika Hospitali, zahanati na vituo vya afya mbalimbali nchini hali inayosababishwa na MSD kutowajibika ipasavyo na kuhatarisha maisha ya wananchi.

### 2.11.2 Ujenzi wa Hospitali, Vituo vya Afya na Zahanati kutokamilika kwa wakati vyenye thamani ya Shilingi Bilioni 85.59

**Mheshimiwa Spika**, ili kusogeza upatikanaji wa huduma ya afya kwa wananchi, Serikali iliamua kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali za Wilaya, Vituo vya afya pamoja na zahanati katika maeneo mbalimbali. Mpango huo umeshindwa kuleta manufaa yaliyokusudiwa kutokana na changamoto kadhaa zinazosababisha kutokamilika kwa vituo vya afya. Changamoto kubwa zilizobainika ni Wizara ya Fedha kutopeleka fedha za miradi, kutofanyika kwa upembuzi yakinifu ili kubaini muda halisi

wa utekelezaji wa mradi, ukosefu wa wataalamu pamoja na kuchelewa kupokea vifaa kutoka kwa wazabuni.

Mfano wa changamoto ya kutokamilika kwa vituo vya Afya ni H/Mji Kondoa ambayo ilipokea **Shilingi Milioni 100** kutoka Serikali Kuu kwa ajili ya ujenzi wa Zahanati za Choka na Mulua pamoja na **Shilingi Milioni 100** kutoka katika mapato ya ndani kwa ajili ya ujenzi wa Zahanati za Ausia na Chandimo. Uhakiki wa utekelezaji wa miradi hiyo uliofanywa na CAG umebaini kutokamilika kwa Zahanati hizo licha ya fedha hizo kutumika kwa kiasi kikubwa.

**Mheshimiwa Spika**, H/W Ileje ilipokea **Shilingi 4,145,000,000** kutoka Serikali kuu kwa ajili ya uboreshaji wa miundombinu ya Hospitali ya Wilaya Itumba. Katika sehemu ya mradi huo, **Shilingi 500,000,000** ilitakiwa kutumika kwa ajili ya ujenzi wa wodi tatu za wanawake, wanaume na watoto. Hata hivyo, miradi hiyo haijakamilika licha ya fedha zote kutumika na kuisha.

H/W Muheza ilitumia **Shilingi 500,000,000** kwa ajili ya ujenzi wa majengo matatu ya wodi ya wanaume, wodi ya wanawake na wodi ya watoto katika Hospitali ya Wilaya Muheza. Hata hivyo, hadi kuwasilishwa kwa taarifa ya CAG mbele ya Kamati, majengo hayo yalikuwa hayajakamilika wakati fedha za mradi zilishatumika zote. Vile vile, Halmashauri ilitumia **Shilingi 40,146,202** kwa ajili kukamilisha jengo la watoto bila ya kupata kibali.

### 2.11.3 Madai kutoka Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) Shilingi Bilioni 1.77

**Mheshimiwa Spika**, Halmashauri zinatakiwa kuwasilisha NHIF madai ya gharama za matibabu yaliyotolewa kwa wagonjwa wanaostahiki kupata huduma za afya kwa kutumia bima. Kwa kipindi kirefu kumekuwa na tatizo la NHIF kukataa kufanya marejesho ya fedha hizo kutokana fomu za bima ya afya kujazwa kimakosa kwa kutozingatia vifungu vya utambuzi wa magonjwa, kutoonyesha vipimo vya utambuzi na kutokuwepo kwa idhini halali kwa kutaja baadhi.

**Mheshimiwa Spika**, licha ya kuwa ukubwa wa hoja hii umepungua kutoka **Shilingi Bilioni 2.34** mwaka wa fedha 2020/2021 hadi **Shilingi Bilioni 1.77**, tatizo hili limekuwa linajirudia

mara kwa mara ikizingatiwa waliopewa jukumu la ujazaji wa fomu hizo ni watu wenye utaalamu na ni waajiriwa wa Serikali. Kamati haioni sababu ya makosa hayo kuendelea kutokea kwakuwa kunavikosesha vituo vya afya fedha ambayo ingetumika kununua dawa na vifaa tiba ili kuboresha afya za wanachi.

Mfano wa tatizo la kutorejeshewa fedha kutoka NHIF limetokea katika H/W Kwimba ambapo kiasi cha **Shilingi 42,551,680** kilichopaswa kurejeshwa na NHIF ambacho ni gharama ya huduma iliyotolewa kwa wanufaika wa mfuko huo, hakikurejeshwa kutokana na madai hayo kukataliwa na NHIF.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaendelea kuwasisitiza Wakurugenzi kuchukua hatua stahiki kwa watumishi wote wanaobainika kusababisha hasara hiyo.

### 2.11.4 Kutoteketezwa kwa dawa zilizokwisha muda wake Shilingi Milioni 976.58

**Mheshimiwa Spika**, sote tunafahamu madhara yatokanayo na matumizi ya dawa zilizokwisha muda wake kwa wananchi. Halmashauri zimeshindwa kuwa na mifumo thabiti ya upokeaji na utoaji wa dawa ambayo itahakikisha dawa iliyopokelewa kwanza ndio itakayotoka ili kuondoa tatizo la dawa kukaa kwa muda mrefu bila matumizi. Vile vile, Bunge lilishazielekeza Halmashauri zote nchini kutopokea dawa kutoka kwa MSD ambazo muda wa matumizi unakaribia kuisha kwakuwa uteketezaji wa dawa hizo ni gharama na hasara kwa Halmashauri.

Halmashauri zinatakiwa kufuata utaratibu uliowekwa na Serikali wa uteketezaji wa dawa haraka iwezekanavyo ili kuepusha madhara kwa umma pindi dawa hizo zitakapofika katika mikono ya watu wasio na maadili. Hata hivyo, kuna baadhi ya Halmashauri ambazo zimeamua kutaka kuhatarisha afya za wananchi kwa kuhifadhi kwa muda mrefu dawa zilizokwisha muda wa matumizi yake.

**Mheshimiwa Spika**, H/W Kwimba haikufuata taratibu za kuteketeza dawa zilizokwisha muda wake wa matumizi zenye thamani ya **Shilingi 77,567,630** ambazo zipo kwa muda mrefu tangu mwaka 1989 hadi 2022. Aidha, H/Mji Mafinga inatunza

dawa zilizokwisha muda wake wa matumizi kwa zaidi ya miaka mitano zenye thamani ya **Shilingi 94,718,208**.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imezielekeza Halmashauri hizo kuhakikisha zinafuatilia na kupata kibali cha kuteketeza dawa hizo kutoka Wizara ya Fedha kitengo cha Usimamizi wa Mali za Serikali ili zoezi hilo liweze kufanyika haraka iwezekanavyo.

### 2.11.5 Fedha Kwa Ajili ya Ununuzi wa Dawa na Vifaa Tiba Zilizobadilishwa Matumizi Shilingi Milioni 455.72

**Mheshimiwa Spika**, Mwaka 2017 Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ilielekeza kuwa, Asilimia 50 ya mapato ya ada zilizokusanywa kama gharama za uchangiaji wa matibabu zitengwe kwa ajili ya ununuzi wa dawa na vifaa tiba katika vituo husika. Pamoja na maelekezo hayo, baadhi ya Halmashauri zilibadilisha matumizi ya fedha hizo kwa kulipa posho na matumizi mengine ya kawaida badala ya ununuzi wa dawa na vifaa tiba. Kutonunuliwa kwa dawa na vifaa tiba kama ilivyopangwa kunakwamisha juhudi za Serikali za kuboresha afya za wananchi wake.

Ukaguzi uliofanywa katika Halmashauri ya Mji Mbinga ulibaini matumizi ya **Shilingi 21,713,308** fedha ambazo, zilipaswa kutumika kwa ajili ya ununuzi wa dawa na vifaa tiba na badala yake fedha hizo zilibadilishiwa matumizi.

### 2.11.6 Kutokufungwa kwa Mfumo wa ukusanyaji wa mapato wa Kielektroniki (GoT-HOMIS) katika Vituo vya Afya

**Mheshimiwa Spika**, Serikali iliidhinisha matumizi ya Mfumo wa ukusanyaji wa mapato wa kielektroniki (GoT-HOMIS) kwa ajili ya kusimamia mapato na matumizi ya vituo vya afya. Lengo likiwa ni kuhakikisha kunakuwa na usimamizi wa pamoja wa mali na taarifa za vituo vya afya nchini.

Uchambuzi wa Kamati kuhusu matumizi ya mfumo huo umegundua baadhi ya Halmashauri kutofunga mfumo huo katika vituo vya Afya hali inayosababisha upotevu wa mapato ambayo yangetumika kwa ajili ya shughuli za uendeshaji wa vituo hivyo pamoja na ununuzi wa dawa na vifaa tiba. Baadhi ya

Halmashauri ambazo bado hazijakamilisha ufungaji wa mfumo huo katika vituo vyake vyote vya afya ni kama inavyoonekana katika jedwali namba 24.

**Jedwali Na. 24**: Halmashauri ambazo hazijafunga GOT-HOMIS

| Na | Jina la Halmashauri | Idadi Ya Vituo |
|---|---|---|
| 1. | H/W Chamwino | 62 |
| 2. | H/W Nkasi | 48 |
| 3. | H/W Mbinga | 35 |
| 4. | H/W Uvinza | 31 |
| 5. | H/W Babati | 25 |
| 6. | H/W Buhigwe | 21 |

### 2.12 Changamoto za Kiutendaji katika Sekta ya Elimu

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na kukagua iwapo Hesabu za Halmashauri zimezingatia Sheria, Kanuni na taratibu za uandaaji wa hesabu, CAG pia amekugua ufanisi na ubora wa elimu ya awali, msingi, sekondari, watu wazima na elimu isiyo rasmi inayotolewa nchini. Katika ukaguzi wake, CAG ameangalia iwapo kuna rasilimali za kutosha kama walimu wenye uwezo, miundombinu mbalimbali kama madarasa na vifaa vya kufundishia.

Kamati imefanya uchambuzi wa kina wa taarifa hiyo. Aidha, mapungufu kadhaa katika Sekta ya elimu yamebainika katika Halmashauri zilizofika mbele ya Kamati. Mapungufu hayo ni kama ukosefu wa miundombinu muhimu, upungufu wa walimu na vitendea kazi pamoja na kutopelekwa kwa ukamilifu ruzuku ya elimu bure (*capitation grant*). Ufafanuzi kuhusu hoja hizo ni kama ifuatavyo:-

#### 2.12.1 Upungufu wa Walimu katika Shule za Msingi na Sekondari

**Mheshimiwa Spika**, tathimini ya taarifa ya CAG kuhusu uwiano wa mwalimu kwa mwanafunzi uliiwezesha Kamati kufahamu ukubwa wa tatizo lililopo katika Sekta ya elimu nchini. Kwa mujibu wa mpango wa III wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2021/22 hadi

2025/26, uwiano katika shule za msingi unatakiwa kuwa ni mwalimu mmoja kwa wanafunzi 50 **(1:50)**. Aidha kwa shule za Sekondari, uwiano unatakiwa kuwa ni wa mwalimu mmoja kwa wanafunzi 20 **(1:20)**. Kulingana na sampuli iliyochukuliwa na CAG katika baadhi ya shule nchini, changamoto ya upungufu wa walimu umebainika katika Halmashauri ya Wilaya ya Meru ambapo kuna upungufu wa **walimu 145** wa somo la sayansi.

Tatizo la upungufu wa walimu lipo katika Mamlaka zote za Serikali za Mitaa. Mfano katika H/W Bahi, walimu wa shule za msingi wanaohitajika ni **2241** na walimu waliopo ni walimu **768** hivyo kufanya upungufu wa **walimu 1473**. Aidha, katika Halmashauri hiyo hiyo, idadi ya walimu wa Sekondari waliopo ni 340 ikilinganishwa na mahitaji ya walimu 380, hivyo kufanya pungufu ya walimu 40.

**Mheshimiwa Spika**, OR – TAMISEMI ililieza Kamati kuwa, ongezeko la uandikishaji wa wanafunzi wa elimu ya msingi na sekondari, limesababisha pia ongezeko la mahitaji ya walimu katika ngazi hizo za elimu. Hadi kufikia tarehe 30 Septemba, 2023 kulikuwa na jumla ya walimu wa Serikali **273,021** sawa na **Asilimia 52.81** ya mahitaji ya walimu **536,821** na kufanya upungufu wa walimu katika shule za msingi na sekondari kuwa **263,800**.

**Mheshimiwa Spika**, Serikali ichukue jitihada za makusudi katika kuboresha ubora wa elimu nchini kwa kuhakikisha kunakuwa na walimu wa kutosha.

### 2.12.2 Wanafunzi kukatisha masomo kabla ya kuhitimu

**Mheshimiwa Spika**, maendeleo ya nchi yoyote duniani kwa kiasi fulani yanahitaji watu wenye elimu bora itakayowawezesha kuzitumia vizuri rasilimali za nchi kwa mujibu wa Sheria, kanuni na miongozo mbalimbali ya nchi husika hivyo, ni jukumu la Serikali kutafuta namna bora ya kuwafanya wananchi wake kupata elimu bora kwa wakati sahihi.

Taarifa ya CAG imechambua mwenendo wa wanafunzi katika shule za msingi na sekondari na kubaini changamoto ya wanafunzi kukatisha masomo kabla ya kuhitimu darasa la Saba na kidato cha Nne. Katika sampuli ya Ukaguzi katika Halmashauri

11 iliyofanywa na CAG ilibainika kuwa, kati ya 2015 na 2021, wanafunzi **19,945** (25%) kati ya **78,786** waliosajiliwa mwaka 2015 hawakuhitimu darasa la saba.

Vile vile, ukaguzi katika Halmashauri 19 ulibaini kuwa, wanafunzi **22,039** sawa na **Asilimia 28** kati ya **82,236** waliojiunga na kidato cha kwanza mwaka 2018 hawakufanikiwa kufanya mtihani na kupata cheti cha kuhitimu kidato cha IV.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati Katika Halmashauri ya Wilaya ya Gairo ulionesha changamoto ya wanafunzi wa sekondari kukatisha masomo kabla ya kuhitimu. Katika kipindi cha mwaka 2018 – 2021 jumla ya **wanafunzi 3330** walisajiliwa katika shule mbalimbali ambapo waliohitimu ni **wanafunzi 2798** na kuwa na **wanafunzi 532** waliokatisha masomo.

Changamoto hiyo pia ilibainika katika H/W Kyerwa ambapo, katika mwaka 2021, wanafunzi wa shule ya msingi ambao walikatisha masoko kwa mwaka 2021 ni **1,887** na wanafunzi wa shule za sekondari waliokatisha masomo kwa mwaka 2021 ni **247**.

**Mheshimiwa Spika**, matarajio ya nchi ni kuwa na watu wenye elimu yenye manufaa kwa taifa. Kuongezeka kwa idadi ya wanafunzi wanaokatisha masomo yao kunarudisha nyuma juhudi zinazofanywa na Serikali za kuimarisha miundombinu ya shule mbalimbali ili nchi iwe na kizazi chenye elimu bora. Kamati inaisisitiza Serikali kuwa na mbinu mbadala za kuhakikisha watoto wote waliosajiliwa katika shule mbalimbali wanahitimu masomo yao.

### 2.12.3 Upungufu wa Miundombinu katika Shule za Awali, Msingi na Sekondari

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inatambua juhudi za Serikali katika kuimarisha miundombinu katika shule za awali, msingi na sekondari. Pamoja na ujenzi wa madarasa na miundombinu mingine muhimu kama ununuzi wa madawati na vitabu, kuboresha uwiano wa vyoo na kuboresha mazingira ya kazi kwa walimu katika ngazi zote katika Halmashauri nchini, bado kuna upungufu wa miundombinu hiyo katika baadhi ya Halmashauri nchini.

Katika hesabu zinazoishia mwezi Juni, 2022, CAG alifanya ukaguzi katika Mamlaka 45 za Serikali za Mitaa katika eneo la miundombinu ya madarasa ili kutathmini iwapo kuna uwiano sahihi wa idadi ya wananfunzi ikilinganishwa na idadi ya vyumba vya madarasa. Katika ukaguzi huo, mahitaji ya vyumba vya madarasa katika shule za msingi yalikuwa ni **57,866**, madarasa yaliyopo hadi kipindi cha ukaguzi yalikuwa ni **30,550** hivyo kuwa na pungufu ya vyumba vya madarasa **27,316**.

Vile vile, Katika elimu ya Sekondari, mahitaji yalikuwa ni vyumba vya madarasa **7,132**, wakati idadi halisi ya madarasa hadi kipindi cha ukaguzi ilikuwa ni **6,349** na kuwa na pungufu ya vyumba vya madarasa **783.** Takwimu hizi ni kwa ajili ya Halmashauri 45 tu kati ya Halmashauri zote 184.

**Mheshimiwa Spika**, ili kufahamu ukubwa wa tatizo la miundombinu katika shule za awali, msingi na sekondari, Kamati ilikutana na OR – TAMISEMI ili kujadili kwa kina kuhusu hoja iliyoibuliwa na CAG. Taarifa ya OR – TAMISEMI ilieleza kuwa, hadi kufikia mwezi Septemba, 2023, idadi ya wanafunzi wa elimu ya awali ilikuwa ni wanafunzi 1,562,285 ambapo, mahitaji ya miundombinu ya kutosheleza idadi hii ni vyumba vya madarasa 51,825 (**uwiano 1:30**). Hata hivyo, vyumba vya madarasa vilivyopo ni 5,049 sawa na **Asilimia 9.7** na kufanya upungufu wa vyumba vya madarasa 46,776 sawa na **Asilimia 90.3**.

Kwa upande wa elimu msingi, idadi ya wanafunzi wa darasa la I hadi la VII ilikuwa ni 10,824,374 na uwiano unaotakiwa wa idadi ya wanafunzi kwa madarasa ni **1:45**. Kwa mujibu wa Taarifa ya OR – TAMISEMI, mahitaji ya vyumba vya madarasa kwa shule za msingi ni vyumba vya madarasa takriban **274,880** wakati vyumba vya madarasa vilivyopo ni **144,810** sawa ya **Asilimia 52.7** ya mahitaji. Kwa muktadha huo, upungufu wa vyumba vya madarasa kwa shule za msingi ni madarasa **130,070**.

Taarifa ya OR – TAMISEMI ilifafanua kuhusu changamoto ya upungufu katika shule za sekondari ambapo, hadi kufikia mwezi Septemba, 2023, idadi ya wanafunzi wa kidato cha I hadi IV ni 2,619,207 ambapo, mahitaji ya vyumba vya madarasa ni **76,102**

na vyumba vilivyopo ni **75,380** sawa na **Asilimia 99** na kuwa na upungufu wa vyumba vya madarasa **722**.

**Mheshimiwa Spika**, H/W Iramba ina upungufu mkubwa wa nyumba za walimu wa shule za msingi na sekondari ambapo, mahitaji ya nyumba za walimu wa shule za msingi ni **1,500** wakati nyumba zilizopo ni **306** hivyo kufanya kuwa na upungufu wa nyumba **1,200** sawa na **Asilimia 80**. Kwa upande wa nyumba za walimu wa sekondari, mahitaji ni nyumba **322** na nyumba zilizopo ni **281**.

### 2.13 Utekelezaji wa Bajeti ya Ruzuku ya Matumizi ya kawaida (OC)

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imefanya mapitio ya utekelezaji wa bajeti katika Halmashauri ili kujiridhisha iwapo bajeti zilizoidhinishwa na Bunge zinakidhi matakwa ya kifungu cha 46 (1) cha Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, [Sura ya 290 Iliyorekebishwa 2019].

Mapitio hayo yalifanyika ili kutathimini iwapo kuna udhibiti wa ndani na usimamizi wa bajeti za Halmashauri. Vile vile, Kamati ilitaka kufahamu endapo fedha zinazotolewa katika mfuko mkuu zinalingana na bajeti zilizoidhinishwa na Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, Katika eneo la utekelezaji wa bajeti, uchambuzi wa taarifa za hesabu zilizokaguliwa kwa mwaka wa fedha 2021/22 zimeonesha tofauti katika mapokezi ya fedha za ruzuku ya matumizi ya kawaida ambapo, baadhi ya Halmashauri zimepokea kiwango zaidi ya Bajeti na baadhi zimepokea kiwango chini ya bajeti.

Matarajio ya Kamati ni kuona Mamlaka za Serikali za Mitaa zinakusanya mapato ya kutosha ya kuziwezesha kutekeleza shughuli zake za kawaida na kupunguza utegemezi wa ruzuku ya Serikali katika eneo hilo ili kazi kubwa ya Serikali iwe ni katika kutekeleza na kukamilisha miradi ya maendeleo katika maeneo yao. Hata hivyo, Ruzuku ya Serikali kwa matumizi ya kawaida ya Halmashauri iliongezeka kwa **Shilingi 46,151,796,462** kutoka **Shilingi 4,760,974,162,598** mwaka 2020/2021 hadi **Shilingi 4,807,125,959,060** mwaka wa fedha 2021/2022. Mfano wa Halmashauri zilizopokea

fedha zaidi au pungufu ya bajeti ni kama inavyoonekana katika Jedwali namba 25.

**Jedwali Na. 25**: Halmashauri zilizopokea fedha za ruzuku ya matumizi ya kawaida zaidi/pungufu ya bajeti iliyoidhinishwa

| Jina la Halmashauri | Bajeti ya matumizi ya kawaida | Kiasi kilichopo kelewa kutoka Serikali Kuu | Ziada | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| H/W Ileje | 7,691,432,123 | 21,690,850,758 | 3,999,418,635 | 23 |
| H/W Hanang' | 27,516,208,000 | 33,326,811,838 | 5,810,603,838 | 21 |
| H/Jiji Dar es Salaam | 103,966,197,650 | 123,097,503,935 | 19,131,306,285 | 19 |
| H/W Kyerwa | 17,667,613,000 | 20,183,037,819 | 2,515,424,819 | 14 |
| H/W Kilindi | 18,912,316,162 | 14,544,261,565 | (4,368,054,597) | (23) |
| H/W Mbarali | 35,369,420,835 | 28,152,146,048 | (7,217,274,787) | (20) |
| H/Mji Kondoa | 12,150,155,488 | 9,975,831,137 | (2,174,324,351) | (18) |
| H/W Itigi | 11,161,831,550 | 9,152,986,146 | (2,008,845,404) | (18) |
| H/W Korogwe | 31,028,301,290 | 25,797,342,656 | (5,230,958,634) | (17) |

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifanya kikao na Wizara ya fedha ili kupata ufafanuzi wa kina kuhusu taratibu za utoaji wa fedha kwa Halmashauri pamoja na sababu za kutoa fedha zaidi au pungufu ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge. Hata hivyo, kwa bahati mbaya Wizara ya Fedha haikutoa majibu ya kina kuhusu hoja hiyo hali inayoshiria uwepo wa bajeti mbili kwa maana ile inayopitishwa na bajeti na ile inayotekelezwa na Wizara ya Fedha. Kamati inaitaka Wizara ya Fedha kutathmini taratibu za utoaji wa fedha za ruzuku kwa Halmashauri bila ya kukiuka Sheria zilizopo.

### 2.14 Mapungufu katika shughuli za ufuatiliaji katika Sekretarieti za Mikoa

**Mheshimiwa Spika**, Sheria ya Tawala za Mikoa Na. 19 ya Mwaka 1997, inatoa jukumu la kuratibu na kusimamia utendaji wa Halmashauri kwa Sekretarieti za Mikoa chini ya usimamizi wa Katibu Tawala wa Mkoa.

Katika kuhakikisha kuwa Sekretarieti za Mikoa zinatekeleza kwa ufanisi zaidi majukumu yake, mwezi Januari, 2022 Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,

aliidhinisha muundo mpya wa Sekretarieti za Mikoa ambapo pamoja na mambo mengine, muundo huo umeanzisha Seksheni ya Usimamizi, Ufuatiliaji na Ukaguzi *(Management, Monitoring & Inspection – MMI)*. Seksheni hii inaongozwa na Katibu Tawala Msaidizi wa Mkoa ambaye chini yake anapaswa kuwa na wataalam sita (6) wenye taaluma za fedha, ukaguzi na utawala.

Majukumu ya Seksheni hii kuhusiana na usimamizi wa Halmashauri ndani ya Mkoa husika ni pamoja na:

a) Kufanya ukaguzi kwa lengo la kuhakiki na kushauri kuhusu uzingatiaji wa Sera, Sheria, Kanuni na thamani ya fedha katika utendaji wa Halmashauri;

b) Kuwezesha kuandaliwa kwa mipango ya kukuza mapato ya ndani ya Halmashauri na kufuatilia utekelezaji wake;

c) Kushauri na kuwezesha matumizi sahihi na usimamizi wa fedha za umma katika Halmashauri; na

d) Kufanya ufuatiliaji kuhusu utekelezaji wa mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, Ili maboresho haya ya muundo wa Sekretarieti za Mikoa yaweze kuleta tija iliyokusudiwa, ni muhimu Serikali ikahakikisha Sekretarieti za Mikoa zinawezeshwa ipasavyo kutekeleza majukumu yake ikiwa ni pamoja na kuzipatia Wataalam wa kutosha, magari na bajeti ya kutosha kwa ajili ya ufuatiliaji kwenye Halmashauri zote ndani ya Mkoa.

**Mheshimiwa Spika**, Katika kuhakikisha kunakuwa na usimamizi thabiti wa Halmashauri, Makatibu Tawala Mikoa wanatakiwa kutekeleza majukumu yao kikamilifu kwa kuhakikisha utendaji wa Wakurugenzi unazingatia matakwa ya Sheria, Kanuni na miongozi ya nchi, Hoja na Mapendekezo yanayotolewa na CAG zinatekelezwa kikamilifu, miradi ya maendeleo katika mikoa yao inatekelezwa kwa mujibu wa bajeti iliyotengwa na kuhakikisha kunakuwa na usimamizi wa ukusanyaji wa mapato.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na mambo mengine, Kamati haijaridhishwa na namna baadhi ya Makatibu tawala

wanavyozisimamia Halmashauri zao kutokana na Halmashauri hizo kuwa na utendaji usioridhisha na hakuna hatua zozote za haraka zinazochukuliwa na Ofisi hiyo ya Mkuu wa Mkoa juu ya watumishi wanaobainika kuenenda kinyume na Sheria na taratibu za utumishi.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inawapongeza Makatibu Tawala wa Mikoa ya Kagera na Mwanza kwa utendaji wao mzuri na kuwa na usimamizi bora wa Halmashauri zilizopo katika Mikoa yao. Kutokana na usimamizi wao, Halmashauri wanazozisimamia zimekuwa zikifanya vizuri hususani katika utekelezaji wa hoja na mapendekezo yanayotolewa na CAG.

Aidha, RAS wa Mkoa wa Kagera aliifahamisha Kamati kuwa, amekuwa na utaratibu wa kukutana na Wakurugenzi wote wa Halmashauri zake katika kila robo mwaka kwa ajili ya kutathimini utekelezaji wa hoja na mapendekezo ya CAG pamoja na uendeshaji wa Halmashauri hizo. Ni matarajio ya Kamati kuwa, Makatibu Tawala wa mikoa yote wataiga mfano huo mzuri ili kuimarisha utendaji wa Halmashauri zilizopo katika mikoa yao.

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 MAONI NA MAPENDEKEZO

### 3.1 Melezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika**, baada ya uchambuzi wa Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu ukaguzi wa hesabu za Halmashauri kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2022, Kamati ina maoni na mapendekezo kama ifuatavyo: -

### 3.2 Maoni

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia kuwa jukumu la bunge ni kuishauri na kuisimamia Serikali katika eneo la matumizi ya fedha za Umma. Kamati ina maoni ya Jumla yafuatayo:-

**Mheshimiwa Spika**, Halmashauri nyingi nchini hazina mtiririko mzuri wa mapato ya ndani kutokana na kushindwa kufikia malengo yake ya ukusanyaji wa mapato ya ndani. Kamati ina maoni ya jumla kuwa, Halmashauri zote nchini ziongeza ufanisi katika ukusanyaji wa mapato ya ndani na kudhibiti mianya yote ya

upotevu wa mapato ili Halmashauri ziwe na uwezo wa kutekeleza shughuli zake za msingi na kupunguza utegemezi wa ruzuku ya Serikali. Aidha, Kamati inawashauri Wakurugenzi wote kutafakari kwa mapana juu ya vyanzo vipya vya mapato na fursa zinazoweza kupatikana katika maeneo yao ya usimamizi.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati pia ina maoni kwamba, OR – TAMISEMI pamoja na Makatibu Tawala Mikoa waongeze usimamizi katika Halmashauri zote na kuhakikisha kunakuwa na uzingatiaji wa Sheria na Kanuni za utengaji wa fedha za utekelezaji wa miradi ya maendeleo kutoka katika mapato ya ndani ya Halmashauri ili miradi inayotakiwa kutekelezwa katika maeneo yao ikamilike kwa wakati na kuleta tija kwa wananchi.

**Mheshimiwa Spika**, kumekuwa na ukiukwaji wa Sheria mbalimbali kama Sheria ya ununuzi wa Umma, Sheria ya fedha za Serikali za Mitaa na Kanuni na miongozo mbalimbali. Ukiukwaji wa Sheria hizo unasababisha matumizi mabaya ya fedha za umma na kuiingiza Serikali katika hasara. Kamati ina maoni kwamba, Serikali isimamie uzingatiaji wa Sheria za nchi na kuchukua hatua stahiki kwa watumishi wote waliobainika kukiuka Sheria hizo ili kuongeza uwajibikaji katika matumizi ya rasilimali za umma.

### 3.3 Mapendekezo

**Mheshimiwa Spika**, utoaji wa mapendekezo ya Kamati ni kwa mujibu wa athari ya hoja pamoja na hatua zinazopaswa kuchukuliwa ili kuondoa hoja hizo. Mapendekezo ya Kamati ni kama ifuatavyo:-

#### 3.3.1 Mifumo dhaifu ya ukusanyaji wa Mapato pamoja na kushindwa kukusanya Madai (Receivables)

**KWA KUWA**, Halmashauri nyingi zimekuwa na mifumo dhaifu ya ukusanyaji wa mapato yatokanayo na vyanzo vya ndani pamoja na kukosa uthabiti katika ukusanyaji wa madai kutoka kwa wadaiwa mbalimbali (Receivables);

**NA KWA KUWA**, mifumo dhaifu inatoa mianya ya uvujaji na upotevu wa fedha za umma na kuzifanya Halmashauri kutofikia malengo yake ya kibajeti hivyo kuongeza utegemezi wa ruzuku ya Serikali;

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba:

a) Serikali iandae mikataba ya utendaji kazi na ukusanyaji wa mapato ya ndani itakayokuwa na vigezo (key performance indicators) kwa Wakurugenzi wote. Aidha katika kila robo mwaka, kila Katibu Tawala Mkoa afanye tathimini iwapo Wakurugenzi hao wamefikia malengo ya ukusanyaji wa mapato na kuwasilisha taarifa hiyo OR – TAMISEMI kwa hatua stahiki;

b) Serikali (OR – TAMISEMI na Makatibu Tawala Mikoa) ihakikishe fedha zote zilizokusanywa kupitia Mashine za kukusanya mapato (POS) **Shilingi Bilioni 11.07** zinawasilishwa Benki kabla ya mwezi Aprili, 2024 na watendaji wote waliohusiwa wachukuliwe hatua za kisheria;

c) Kila Halmashauri ifanye upya tathimini ya kina juu ya uwezo wa mawakala wa ukusanyaji wa mapato na kuhakikisha mikataba yote kati ya Halmashauri na Mawakala hao inapitiwa na Mwanasheria wa Halmashauri na hatua za kisheria kwa Mawakala watakaokiuka matakwa ya kimkataba zichukuliwe;

d) Serikali ihakikishe kiasi cha Shilingi **Bilioni 37.34** kutoka katika vyanzo muhimu vya mapato ya ndani ya Halmashauri kinakusanya;

e) Kila Mkurugenzi wa Halmashauri kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mapato Tanzania, wahakikishe wanakuwa na taarifa sahihi kuhusu mauzo ghafi ya wafanyabiashara wote waliosajiliwa katika maeneo yao na kukusanya ushuru wa huduma kwa mujibu wa Sheria;

### 3.3.2 Matumizi yasiyofaa ya Fedha za umma

**KWA KUWA**, Taarifa ya CAG imebainisha uwepo wa matumizi mabaya ya fedha za umma katika Halmashauri ambapo rasilimali za Umma zimekuwa zikitumika kinyume na Sheria, kanuni, Miongozo na Taratibu;

**NA KWA KUWA**, matumizi yasioyofaa ya fedha za umma yamekuwa yakisababisha hasara mbalimbali kwa Halmashauri;

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba:
a) Serikali iwachukulie hatua za kinidhamu watumishi wote waliofanya malipo kwa fedha taslimu kwa kiasi kilichohojiwa cha **Shilingi Bilioni 1.51** kinyume na Aya ya 6.8.3 ya Mwongozo wa Uhasibu wa Halmashauri wa Mwaka 2021;

b) Serikali ichukue hatua za kinidhamu na kisheria kwa watu wote waliofanya matumizi ya **Shilingi Bilioni 11.78** bila ya nyaraka halali za matumizi hayo;

c) Serikali ichukue hatua kwa watumishi wa Halmashauri waliotumia kiasi cha **Shilingi Bilioni 7.7** kutoka katika akaunti ya amana kwa matumizi yasiyopangwa na kuhakikisha fedha hizo zinarejeshwa;

d) Serikali kupitia OR – TAMISEMI iwaelekeze Makatibu Tawala Mikoa kufuatilia na kuhakikisha watumishi wa Halmashauri zao waliofanya matumizi yasiyo na tija ya **Shilingi Milioni 898.85** wanachukuliwa hatua za kinidhamu.

**3.3.3 Ukiukwaji wa Sheria ya Ununuzi wa Umma Sura 410 na Mapungufu katika usimamizi wa Mikataba**

**KWA KUWA**, Halmashauri nyingi zimebainika kutozingatia Sheria ya Ununuzi wa umma Sura 410 na kanuni zake pamoja na uwepo wa dosari katika usimamizi wa mikataba;

**NA KWA KUWA**, ukiukwaji wa Sheria hiyo kwa kipindi kirefu umekuwa ukiingiza Serikali katika hasara na fedha nyingi za umma zimekuwa zikipotea katika eneo hili hadi kufikia **Shilingi 106,799,578,781**;

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba:
a) Mamlaka ya Usimamizi wa Ununuzi wa Umma (PPRA) ifanye ukaguzi wa kina katika maeneo yote yaliyobainishwa katika ripoti ya CAG ambayo yameonesha kuwepo kwa ukiukwaji wa Sheria ya Ununuzi wa Umma ikiwa ni pamoja na matumizi ya *force account* na kuchukua hatua stahiki kwa watumishi waliohusika na dosari hizo kwa mujibu wa Sheria;

b) Serikali kupitia OR - TAMISEMI ihakikishe wanasheria wanapitia mikataba yote iliyohojiwa na CAG ya **Shilingi Bilioni 6.68** ambayo haikuhakikiwa na Mwanasheria na kuainisha dosari zilizomo katika mikataba hiyo na hatua stahiki zichukuliwe kwa waliohusika. Vile vile, Kwa Mkurugenzi atakayeingia mkataba mpya bila ya kuhakikiwa na mwanasheria, hatua za kisheria zichukuliwe dhidi yake;

c) Serikali ihakikishe inalipa madeni ya wakandarasi na wazabuni yenye jumla ya **Shilingi Bilioni 7.8** kwa mujibu wa mikataba ya kazi waliyoingia;

d) Serikali ihakikishe waliosababisha hasara kwa kufanya ununuzi wa vifaa vya ujenzi zaidi ya mahitaji kama ilivyoainishwa katika Ripoti Kuu ya CAG wanachukuliwa hatua za Kisheria na kuhakikisha hasara hiyo inafidiwa;

e) Serikali ihakikishe bidhaa zilizolipiwa kabla ya kupokelewa za **Shilingi Bilioni 3.29** zinapokelewa na kuhakikiwa kwa mujibu wa mikataba; na

f) Serikali ichukue hatua stahiki kwa Wakurugenzi waliofanya ununuzi wa **Shilingi Bilioni 7.45** bila ya kutumia njia ya ushindanishi wa bei na kusababisha dosari kadhaa katika ununuzi uliofanyika.

### 3.3.4 Kushindwa kulipa Madeni (Payables) ya Halmashauri

**KWA KUWA**, imekuwa ni desturi ya Serikali na Halmashauri kutolipa madeni mbalimbali ya watumishi na wazabuni kwa wakati,

**NA KWA KUWA**, kutolipwa kwa madeni hayo kunawakosesha watumishi haki zao za msingi na kuwaondolea morali ya kazi, kunaua mitaji ya wazabuni na kunaziweka Halmashauri katika hatari ya kufunguliwa mashtaka,

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba:
a) Serikali Kuu na Halmashauri zilipe malimbikizo ya Mishahara na Madai ya Wafanyakazi ya **Shilingi Bilioni 119.94**;

b) Serikali ifanye uchambuzi wa madeni ya Wastaafu wote nchini waliohudumu katika Mamlaka za Serikali za Mitaa na kuwalipa madeni yao haraka iwezekanavyo;

c) Halmashauri zote ambazo zilikata marejesho ya mikopo ya wah. Madiwani na kutowasilisha fedha hizo Benki au Taasisi yoyote ya fedha ziwasilishe fedha hizo kulingana na mikataba waliyoingia;

d) Wakurugenzi wote wa Halmashauri wahakikishe wanawasilisha makato ya Watumishi kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na Mfuko wa Bima ya Afya kwa mujibu wa Sheria na kuhakikisha deni la **Shilingi Bilioni 260.07** linalotokana na kutowasilishwa kwa michango hiyo linalipwa; na

e) Serikali Kuu na Halmashauri zilipe madeni ya wazabuni kwa kuzingatia umri wa madeni hayo. Madeni yaliyoripotiwa katika Taarifa za Hesabu za Halmashauri zote nchini yalipwe kwa mujibu wa mikataba.

**3.3.5 Uendeshaji usiofaa wa Mfuko wa Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu**

**KWA KUWA**, kumekuwepo kwa kutozingatiwa kwa kanuni za usimamizi na utoaji wa mikopo kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu;

**NA KWA KUWA**, ukiukwaji wa Kanuni hiyo umesababisha lengo la utoaji wa mikopo hiyo kwa jamii lisifikiwe;

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba:
a) Kila Halmashauri ichangie Asilimia 10 ya mapato yake ya ndani kwenye Mfuko wa Wanawake, Vijana na Watu wenye ulemavu na kuhakikisha kiasi kilichohojiwa cha **Shilingi Bilioni 5.06** kinapelekwa katika mfuko huo;

b) Wakurugenzi wahakikishe kiasi cha **Shilingi Bilioni 88.42** kilichokopeshwa katika vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kinakusanywa kabla ya mwezi Juni, 2024;

c) Pindi utaratibu wa utoaji wa mikopo hiyo utakapoanza tena, Serikali ihakikishe mikopo hiyo inatolewa kwa kuzingatia uwiano uliowekwa kisheri wa 4:4:2; na

d) Serikali ihakikishe Halmashauri ambazo zilitoa mikopo kwa Vikundi vilivyositisha shughuli za Biashara na kushindwa kurejesha **Shilingi Bilioni 2.25** pamoja na Halmashauri zilizotoa mikopo kwa vikundi ambavyo havikupatikana kwa ajili ya uhakiki (Vikundi hewa) vyenye **Shilingi Milioni 895.94** zinafanya ufuatiliaji wa kina na kuhakikisha fedha hizo zinakusanywa.

### 3.3.6 Mapungufu katika utekelezaji wa miradi ya Maendeleo

**KWA KUWA**, utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika Halmashauri kunaimarisha lengo la Serikali kutoa huduma bora kwa jamii;

**NA KWA KUWA**, kutokamilika kwa miradi ya maendeleo kunakwamisha wajibu wa Serikali ya kuihudumia jamii na kunaondoa thamani ya fedha zilizotumika katika miradi mbalimbali;

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba:
a) Wizara ya Fedha ipeleke katika Halmashauri fedha za utekelezaji wa miradi ya maendeleo kama ilivyoidhinishwa na Bunge pamoja na kukamilisha utoaji wa fedha za miradi yote ambayo haijakamilika;

b) Halmashauri zote ambazo hazijakamilisha utoaji wa fedha za utekelezaji wa miradi ya maendeleo kutoka katika mapato yake ya ndani zipeleke fedha hizo kwa ajili ya kukamilisha utekelezaji wa miradi iliyosimama;

c) Halmashauri zifanye tathimini ya miradi yote ya maendeleo ambayo haijakamilika na imetekelezwa kwa muda mrefu ili kujua thamani halisi ya kiasi cha fedha kinachotakiwa kukamilisha miradi hiyo ikiwa ni pamoja na miradi iliyoanza kujengwa kwa nguvu za wananchi na kuingiza katika bajeti kwa ajili ya ukamilishaji;

d) OR – TAMISEMI kwa kushirikiana na Makatibu Tawala Mkoa wahakikishe fedha zote za miradi ya maendeleo zilizobadilishiwa matumizi bila ya kupata kibali cha Wizara ya Fedha zinarejeshwa ili ziweze kutumika katika kutekeleza miradi iliyopangiwa;

e) Serikali kupitia OR – TAMISEMI ihakikishe utata juu ya uendeshaji wa Kituo cha Afya cha Tlawi katika Halmashauri ya Mji wa Mbulu unaondolewa na kila upande unapata haki yake;

f) Serikali isimamie na kuhakikisha deni la Pangea Mineral Limited **Shilingi 3,179,399,030** linalipwa kwa Halmashauri ya Manispaa ya kahama; na

g) Serikali iangalie upya uamuzi uliofanywa wa kupunguza kiwango cha Halmashauri cha kuchangia katika miradi ya maendeleo kutoka Asilimia 40 kwenda Asilimia 20 ya makusanyo ya mapato ya ndani kwani uamuzi huu unasababisha uzembe na kutowajibika kwa Wakurugenzi na kupunguza kasi ya maendeleo.

### 3.3.7 Kutotekelezwa kwa Mipango ya Miradi ya kurudisha kwa jamii (CSR)

**KWA KUWA**, Halmashauri hususani kwenye vitengo vya Sheria vimekuwa dhaifu katika kutengeneza makubaliano (MOU) ya utekelezaji wa mipango ya wajibu kwa jamii (CSR)

**NA KWA KUWA**, kutengeneza makubaliano (MOU) dhaifu kunapelekea Halmashauri husika kushindwa kushiriki katika utekelezaji wa miradi inayotekelezwa kutokana na Mpango wa wajibu kwa jamii (CSR), jambo linalopelekea miradi hiyo kutokuwa na uwazi katika utekelezaji na kushindwa kulinda maslahi ya Halmashauri;

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba, Serikali isimamie mipango yote ya wajibu kwa jamii inayotekelezwa kwenye Halmashauri kwa kuhakikisha kwamba, MOU zinazotengenezwa zinaipa Halmashauri nafasi ya kushiriki na kuwa na maamuzi katika hatua zote za utekelezaji wa miradi ya CSR ili kulinda Maslahi mapana ya wananchi.

### 3.3.8 Utendaji usioridhisha wa baadhi ya Halmashauri

**KWA KUWA**, kumekuwa na changamoto ya kukosekana kwa ufanisi katika usimamizi wa rasilimali za umma kwa baadhi ya Wakurugenzi;

**NA KWA KUWA**, changamoto hiyo imechangia kwa kiasi kikubwa mapato ya ndani kushindwa kukusanywa, kuwepo kwa matumizi mabaya ya fedha za umma na kutotekelezwa kwa miradi ya maendeleo;

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba:

a) Kuiomba Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kufanya Ukaguzi Maalumu kwa Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi kuanzia mwaka wa fedha 2019/2020 hadi 2021/22 kwa kuzingatia maeneo yafuatayo;

   i. Kufanya ukaguzi na kujiridhisha kuhusu taratibu za ukusanyaji wa mapato ya ndani ya Halmashauri kwa ujumla, ikijumuisha mapitio ya mikataba ya ukusanyaji mapato, Utaratibu wa uwasilishaji wa fedha za makusanyo ya mapato pamoja na matumizi ya mifumo ya ukusanyaji mapato,

   ii. Kukagua mapato ya fedha za miradi ya maendeleo zilizopokelewa kutoka katika vyanzo mbalimbali vikijumuisha Hazina, Wahisani mbalimbali, mikopo, michango ya Halmashauri katika miradi ya Maendeleo kutoka kwenye vyanzo halisi vya mapato ya ndani, pamoja na michango ya wananchi,

   iii. Kufanya ukaguzi wa kina kuhusu mapato na matumizi ya mfuko wa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu,

   iv. Kufanya ukaguzi wa kina ili kubaini kama kulikuwa na ukiukwaji wa Sheria ya Manunuzi ya Mwaka 2011 na Kanuni zake za Mwaka 2013 katika upatikanaji wa Wakandarasi wa Ujenzi, Washauri elekezi na wauzaji wa vifaa vya ujenzi kwa miradi iliyotekelezwa katika Halmashauri,

v. Kupitia na kujiridhisha kama Miradi ya maendeleo iliyotekelezwa inakidhi viwango na kwa mujibu wa Memoranda ya Makubaliano, mikataba na pia kama ilizingatia thamani ya fedha,

vi. Kukagua na kujiridhisha juu ya madeni ambayo Halmashauri inadaiwa na taasisi mbalimbali, na

vii. Kufanya ukaguzi wa eneo lolote lile ambalo Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ataona linafaa kufanyiwa ukaguzi wa Kina.

b) Kuiomba Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kufanya Ukaguzi Maalumu kwa Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha kuanzia mwaka wa fedha 2019/2020 hadi 2021/22 kwa kuzingatia maeneo yafuatayo;

i. Kufanya ukaguzi wa kina wa fedha za miradi ya maendeleo kwa fedha za Serikali kuu na fedha za mapato ya ndani ikiwa ni pamoja na utekelezaji wa miradi hiyo pamoja na kuhakiki iwapo Sheria ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2011 na Kanuni zake za mwaka 2013 ilizingatiwa katika kuwapata wakandarasi/mafundi/washauri elekezi;

ii. Kufanya ukaguzi wa kina kwenye mauzo ya viwanja (*sale of plots*) vya Halmashauri ikiwemo viwanja vipya kwenye eneo la kimkakati la kwala (Kwala Industrial Area) na Kuhakiki fedha za mauzo ya viwanja kama zimekusanywa zote na kuingizwa kwenye mfumo wa mapato na kwenye akaunti ya benki ya Halmashauri,

iii. Kuhakiki kama mfumo wa mapato wa Halmashauri unafanya kazi sawasawa na pia kuhakiki kama vyanzo vyote vya mapato vinavyotumia PoS vina PoS kwa ajili ya kukusanyia mapato,

iv. Kuhakiki matumizi ya mapato yaliyotokana na kiwanja cha SinoTan kilichopo katika Plot Na I Block B Kwala chenye thamani ya Sh. 2,500,000,000 Ambazo fedha hizi zinasemekana kutumika kulipia fidia ya Sh. 1,552,976,324 ya

eneo lililonunuliwa na Halmashauri kwa ajili ya ujenzi wa soko la kisasa Mlandizi,

v. Kufanya uhakiki wa kina wa uhalali na usahihi wa madeni (payables) yanayotokana na wazabuni na madeni ya watumishi waliyopo kazini, waliostaafu, waliofariki na wengine waliohama,

vi. Kufanya ukaguzi wa kina wa Mfuko wa Wanawake, Vijana na Watu wenye ulemavu ili kujiridhisha kama Sheria, Kanuni na taratibu za fedha zimezingatiwa na mikopo ilitolewa kwa vikundi halali na marejesho yanafanyika,

vii. Kufanya ukaguzi wa kina wa ujenzi wa jengo la Ofisi lililopo katika Plot Na 178 Block B Kisabi kujengwa katika eneo ambalo halikufanyiwa tathimini ya athari za kimazingira (*Environmemtal impact assessment*) na athari zitakazopatikana kutokana na kutofanyika kwa tathimini hiyo, na

viii. Kukagua maeneo mengine yenye viashiria vya ubadhirifu ambayo Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ataona yanafaa kufanyiwa ukaguzi wa kina ikiwemo kiwanda cha uzalishaji tofali.

c) Kuiomba Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kufanya Ukaguzi Maalumu kwa Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma kuanzia mwaka wa fedha 2019/2020 hadi 2021/22 kwa kuzingatia maeneo yafuatayo;

i. Kufanya ukaguzi wa kina wa taratibu za ukusanyaji wa mapato ya ndani ya Halmashauri kwa miaka mitatu kuanzia mwaka wa fedha 2019/20 hadi 2021/22 ikijumuisha mapitio ya mikataba ya ukusanyaji mapato, taratibu za uwasilishaji wa fedha za makusanyo ya mapato pamoja na matumizi ya mifumo ya ukusanyaji wa mapato,

ii. Kufanya ukaguzi wa kina wa fedha za miradi ya maendeleo zilizopokelewa kutoka katika vyanzo mbalimbali iwapo zimetumika kama ilivyokusudiwa na kwa mujibu wa Sheria na taratibu za fedha na kwamba kuna thamani ya fedha (value for money) imepatikana,

iii. Kufanya ukaguzi wa kina wa utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa soko la kimataifa la Kagunga,

iv. Kuchunguza na kubaini kama kulikuwa na ukiukwaji wa Sheria ya Ununuzi wa umma ya Mwaka 2011 na Kanuni zake za Mwaka 2013 ikiwemo upatikanaji wa Wakandarasi wa Ujenzi, Washauri Waelekezi na wauzaji wa vifaa vya ujenzi, na

v. Kukagua maeneo mengine yenye viashiria vya ubadhirifu ambayo Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ataona yanafaa kufanyiwa ukaguzi wa kina.

### 3.3.9 Changamoto za kiutendaji katika Sekta ya Afya

**KWA KUWA**, kumekuwa na upungufu wa miundombinu na uhaba wa dawa na vifaa tiba katika Hospitali za Wilaya, Kituo cha Afya na zahanati nchini;

**NA KWA KUWA**, kukosekana kwa miundombinu muhimu katika maeneo hayo ya kutolea huduma za afya kunazorotesha juhudi za Serikali katika kuwapatia wananchi wake huduma bora;

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia Kwamba:

a) Bohari Kuu ya Dawa (MSD) ipeleke dawa na vifaa tiba vyenye thamani ya **Shilingi Bilioni 8.16** ambavyo vimeshalipiwa kwa kuzingatia maombi ya Halmashauri. Vile vile, MSD ipeleke kwa wakati dawa na vifaa tiba kila inapokuwa imelipwa;

b) Serikali kukamilisha ujenzi wa Hospitali, Vituo vya Afya na Zahanati vyenye thamani ya **Shilingi Bilioni 85.59** kama ilivyoainishwa na CAG,

c) Serikali ifanye tathimini ya kina juu ya uwezo wa watumishi wanaopewa jukumu la kujaza fomu za bima ya afya na kuwachukulia hatua stahiki watumishi wote watakaobainika kusababisha hasara ya **Shilingi Bilioni 1.77** iliyotokana na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) kukataa kufanya marejesho ya fedha hizo,

d) Halmashauri zote nchi kutopokea dawa kutoka MSD ambazo muda wake wa matumizi ni chini ya Miezi Sita, na

e) OR – TAMISEMI kuchukua hatua stahiki kwa watu waliohusika na kubadili matumizi ya fedha kwa ajili ya Ununuzi wa Dawa na Vifaa Tiba ya **Shilingi Milioni 455.72**.

### 3.3.10 Changamoto za Kiutendaji katika Sekta ya Elimu

**KWA KUWA**, rasilimali muhimu katika sekta ya elimu ni pungufu ikilinganishwa na mahitaji yaliyopo;

**NA KWA KUWA**, upungufu wa miundombinu muhimu, walimu na vitendea kazi unapunguza ufanisi na ubora wa elimu inayotolewa katika shule za Serikali;

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba:
a) Serikali iajiri na kupeleka walimu katika shule za msingi na sekondari ili kupunguza tatizo la uhaba wa walimu hasa katika maeneo ya vijijini,

b) Serikali izingatie waraka kuhusu utoaji wa Ruzuku ya elimu bila malipo kwa Shule za Serikali uliotolewa tarehe 28 Disemba, 2015,

c) Serikali ifanye tathmini na kufahamu sababu zinazopelekea wanafunzi kukatisha masomo yao kabla ya kuhitimu na kuwachukulia hatua wote waohusika kusababisha tatizo hilo, na

d) Serikali iboreshe na kujenga miundombinu muhimu kama nyumba za walimu, vyumba vya madarasa, matundu ya vyoo na maabara katika shule za msingi na sekondari.

### 3.3.11 Utekelezaji wa Bajeti ya Ruzuku ya Matumizi ya kawaida (OC)

**KWA KUWA**, kumekosekana usimamizi wa bajeti za Halmashauri kwa mapato yanayotokana na ruzuku ya matumizi ya kawaida;

**NA KWA KUWA**, hali hiyo imesababisha Wizara ya Fedha kutoa fedha kwa kutozingatia bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa kutoa fedha pungufu au zaidi;

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba, Wizara ya Fedha izingatie bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa kutoa fedha kwa Halmashauri zote kwa usawa.

**3.3.12 Mapungufu katika shughuli za ufuatiliaji katika Sekretarieti za Mikoa**

**KWA KUWA**, kumekuwa na mapungufu kwa Sekretarieti za Mikoa katika kuzisimamia Halmashauri;

**NA KWA KUWA**, kutokuwepo na uthabiti katika shughuli za usimamizi na ufuatiliaji wa Halmashauri nchini kumesababisha utendaji usioridhisha wa Halmashauri;

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba:

a) Serikali ihakikishe inaziwezesha ipasavyo Sekretarieti za Mikoa kwa kuzipatia Wataalamu wa kutosha na vitendea kazi kwa ajili ya ufuatiliaji kwenye Halmashauri zote ndani ya Mkoa; na

b) Kila Katibu Tawala Mkoa (RAS) awe na utaratibu wa kukutana na Wakurugenzi wote mara kwa mara ili kufanya tathimini ya utendaji wa Halmashauri, utekelezaji wa hoja na mapendekezo ya CAG pamoja na utekelezaji wa mapendekezo ya LAAC na kuwasilisha taarifa OR –TAMISEMI.

**3.3.13 Utekelezaji wa mapendekezo yote yaliyotolewa katika taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Hesabu za Serikali za Mitaa**

**KWA KUWA**, bado kuna changamoto kubwa ya utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa na CAG kwa Halmashauri zote nchini

**NA KWA KUWA,** changamoto hiyo inaashiria uendelevu wa matatizo ya matumizi mabaya ya fedha za umma katika Halmashauri zote

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba, Serikali itekeleze kikamilifu mapendekezo yote yaliyotolewa katika Taarifa za

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Hesabu za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2022.

## SEHEMU YA NNE

## 4.0 HITIMISHO

### 4.1 Hitimisho

**Mheshimiwa Spika**, napenda kutumia fursa hii kukupongeza kwa kuchaguliwa kwa kishindo kuwa Raisi wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU), Umahiri wako katika kutekeleza majukumu yako umeonekana Duniani. Vile vile, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa uongozi wako thabiti ambao umeiwezesha Kamati yangu kutekeleza majukumu yake kikamilifu na bila ya vikwazo kwa kutoa maelekezo na miongozo muhimu kwa Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, nawashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa kwa kuwa wavumilivu na kutekeleza majukumu ya Kamati hii kwa ufanisi na weledi mkubwa.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwatambua Wajumbe hao kama ifuatavyo: -

1) Mhe. Halima James Mdee, Mb. – Mwenyekiti
2) Mhe. Stanslaus Shing'oma Mabula, Mb. – M/Mwenyekiti
3) Mhe. Ally Mpembenwe Twaha, Mb. – Mjumbe
4) Mhe. Conchesta Leonce Rwamlaza, Mb. – Mjumbe
5) Mhe. Ester Amos Bulaya, Mb. – Mjumbe
6) Mhe. Issa Ally Mchungahela, Mb. – Mjumbe
7) Mhe. Jeremiah Mrimi Amsabi, Mb. – Mjumbe
8) Mhe. Jesca J. Msambatavangu, Mb. – Mjumbe
9) Mhe. Munde Tambwe Abdallah, Mb. – Mjumbe
10) Mhe. Lemburis Saputu Mollel, Mb. – Mjumbe
11) Mhe. Suma Ikenda Fyandomo, Mb. – Mjumbe
12) Mhe. Daimu Iddi Mpakate, Mb. – Mjumbe
13) Mhe. Ally Juma Makoa, Mb. – Mjumbe
14) Mhe. Hawa Mchafu Chakoma, Mb. – Mjumbe
15) Mhe. Michael C. Mwakamo, Mb. – Mjumbe
16) ) Mhe. Asha Abdallah Juma, Mb. – Mjumbe

17) Mhe. Amina Iddi Mabrouk, Mb. – Mjumbe
18) Mhe. Idrissa Juma Abdul-Hafar, Mb. – Mjumbe
19) Mhe. Abdul Yusuf Maalim, Mb. – Mjumbe
20) Mhe. Mussa Omar Salim, Mb. – Mjumbe

**Mheshimiwa Spika**, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Bi. Nenelwa Mwihambi, ndc. kwa ushauri wake kwa Kamati pamoja na wasaidizi wake wote kwa kuratibu shughuli za Kamati na kufanikisha kusomwa kwa taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, mwisho japo siyo kwa umuhimu, Kamati inatambua na kuthamini ushirikiano mkubwa ilioupata kutoka Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi (NAOT) na kwa namna ya kipekee kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Ndugu Charles Kichere. Aidha, napenda kuishikuru OR – TAMISEMI pamoja na Wizara ya Fedha kwa ushirikiano walioutoa katika Kamati kwa kutoa ufafanuzi kila ilipohitajika kufanya hivyo.

**4.2 Hoja**

**Mheshimiwa Spika**, Nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza.

**Mheshimiwa** Spika, Naomba kutoa Hoja

Halima James Mdee, Mb.
**MWENYEKITI KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA (LAAC)**
02 Novemba, 2023

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Ahsante Mwenyekiti sana kwa uwasilishaji wa hoja hizi. Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamwita Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji na Mitaji ya Umma, kwanza tunayo matangazo ya wageni. *(Makofi)*

Tunao, Wageni wawili wa Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa ambaye ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, TAMISEMI na hawa ni Ndugu Charles Msonde ambaye ni Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais TAMISEMI

anayeshughulikia elimu. Ameongozana na Mhandisi Rogatus Mativila ambaye ni Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, TAMISEMI anayeshughulikia miundombinu. Karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wakati wa wawasilisho la Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa *(LAAC),* kuna neno moja alilisema hapo nataka kulifuta kwa sababu siyo neno la Kibunge. Alisema, "utumbo" wakati akisoma taarifa yake. Kwenye ile taarifa kubwa, ilikuwa ni ukurasa wa 30. Kwa hiyo, Taarifa Rasmi za Bunge zitaondoa hilo neno "Utumbo" ili tukae vizuri kwa mujibu wa Kanuni zetu. *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma *(PIC),* Mheshimiwa Deus Sangu. *(Makofi)*

**MHE. DEUS C. SANGU – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UWEKEZAJI WA MITAJI YA UMMA (PIC):** Mheshimiwa Spika, Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma *(PIC)* kuhusu Uwekezaji wa Mitaji ya Umma kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uhai na kutuwezesha kufika siku ya leo. Kutokana na ufinyu wa muda, naomba taarifa hii yote kama inavyosomeka katika kitabu cha Kamati, iingie katika kumbukumbu za Taarifa Rasmi ya Bunge *(Hansard)*.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii adhimu kukupongeza kwa dhati kwa ushindi wa kishindo ulioupata kwenye kinyang'anyiro cha kuwania nafasi ya Uraisi wa Umoja wa Mabunge Duniani. Tuna imani na wewe katika kupeperusha bendera ya Tanzania na kutangaza sifa njema ya nchi yetu Tanzania ya uongozi bora.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma *(PIC)* kuhusu Uwekezaji wa Mitaji ya Umma kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, inayowasilishwa Bungeni ili kuwezesha Bunge kujadili mwenendo wa Uwekezaji ya Mitaji ya Umma na kuazimia kuhusu mwenendo huo.

Mheshimiwa Spika, Muundo wa Taarifa hii umezingatia masharti ya Kanuni ya 142 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023. Kutokana na masharti hayo, Taarifa imegawanyika katika sehemu kuu tatu; Utangulizi, Uchambuzi wa Taarifa ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma na Maoni na Mapendekezo ya Kamati katika muundo wa hoja uliyowekwa kwa masharti ya Kanuni ya 61 (3) ya Kanuni za Bunge.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya kwanza inafafanua maelezo ya msingi kuhusu taarifa hii, inabainisha msingi wa ufuatiliaji ya mitaji ya umma kikatiba, Kanuni za Bunge, Sheria ya Msajili wa Hazina Sura ya 370, na Sheria nyingine za nchi. Aidha, sehemu hii inabainisha muundo wa uwekezaji wa mitaji ya umma, wigo wa ufuatiliaji wa mitaji ya umma na njia zinazotumika kufuatilia.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya pili, inahusu uchambuzi wa taarifa za uwekezaji wa mitaji ya umma, inafafanua hali ya mwenendo wa uwekezaji wa mitaji ya umma kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Ufafanuzi huo umejikita kwenye lengo la kubainisha iwapo uwekezaji una ufanisi na kwamba una tija, iwapo uwekezaji unazingatia taratibu na miongozi ya biashara. Katika ufanikishaji wa azma hiyo, taarifa kuhusu thamani ya uwekezaji wa Serikali, gawio, mchango wa asilimia 15 wa mapato ghafi, michango ya asilimia 70 ya ziada na michango mingineyo, na rejesho la riba ya mikopo na ulinganisho ya ufanisi wa mtaji unawekeza kwenye taasisi ambapo Serikali ina hisa chache na kule ambapo ina hisa zaidi.

Mheshimiwa Spika, ufafanuzi wa sehemu hii unaonesha kama ifuatavyo:-

(a) Thamani ya uwekezaji ya mitaji ya umma kwa mwaka 2021/2022 ilifikia shilingi trilioni 73.36. Kiasi hiki ni sawa na ongezeko la asilimia nane ukilinganisha na uwekezaji huo kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ambapo thamani yake ilikuwa ni shilingi trilioni 67.95.

(b) Gawio: Sheria ya Kampuni, Sura ya 180 pamoja na Kifungu 15 (2) (b) cha Sheria ya Msajili wa Hazina Sura ya 370 imeweka masharti yanayowezesha Serikali kupata gawio. Uchambuzi unaonesha kuwa katika kipindi cha mwaka wa fedha

2021/2022 Serikali ilikusanya jumla ya shilingi bilioni 357.52 ikiwa ni gawio kutoka kwenye mashirika yanayofanya biashara. Aidha, kiasi cha gawio kilichokusanywa kilichangiwa na mashirika 25 tu kati ya mashirika 66 yanayopaswa kuchangia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nirudie sehemu hii. Hiki kiasi cha shilingi bilioni 357.52 ilikuwa ni gawio kutoka kwenye mashirika yanayofanya biashara. Aidha, kiasi cha gawio kilichangiwa na mashirika 25 tu kati ya mashirika 66 yanayopaswa kuchangia sawa na asilimia 38 ya mashirika yote yanayopaswa kupeleka gawio kwa Serikali. Hali hii inaonesha kwamba ongezeko hili linachangiwa na taasisi chache tu zinazotumia mtaji wa umma na tasisi nyingi hazitoi gawio. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uchambuzi zaidi umeonesha kwamba, mashirika matatu yaliyoongoza kwa kutoa gawio ni Benki Kuu ya Tanzania iliyotoa shilingi bilioni 200, *Airtel Tanzania* iliyotoa shilingi bilioni 104.2 na *NMB* iliyotoa shilingi bilioni 28. Kwa ujumla Kamati imebaini kuwa asilimia 95 ya jumla ya kutoka kwenye taasisi hizo 25 imepatikana katika taasisi tatu tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kisheria ni wajibu wa kila taasisi unaotumia mtaji wa umma kutoa gawio. Laiti uwajibishwaji ungelitumika na kuhimiza taasisi zote zinazotumia mtaji wa umma na kuendesha biashara katika ulipaji wa gawio Serikali ingeweza kupata kiasi kikubwa cha gawio jambo ambalo lingeongeza uwezo wa Serikali katika uendeshaji wa shughuli zake za Umma. *(Makofi)*

(c) Michango ya asilimia 15. Sheria ya Mamlaka na Majukumu ya Msajili wa Hazina inataka mashirika yanayofanya biashara yatoe asilimia 15 ya mapato ghafi kwa *(gross revenue)* kwa mwaka wa kuchangia katika Mfuko wa Hazina. Taarifa zinaonesha kuwa katika kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022, Msajili wa Hazina alikusanya shilingi 324.02 kutokana na mapato ghafi ya Mashirika na Taasisi za Serikali kwa mujibu wa sheria. Kiasi hicho ni sawa na asilimia 105.5 ya lengo.

Mheshimiwa Spika, wastani wa ufanisi ya makusanyo ya asilimia 15 ya mapato ghafi ni asilimia 80 tu ya lengo la makusanyo. Mwenendo huu kimahesabu unaonesha kuwa na

ufanisi. Hata hivyo, bado kazi ya ziada inahitajika kwani lengo la makusanyo bado liko chini ukilinganisha na wingi wa mashirika ambayo yanaangukia chini ya kifungu hiki. Ni vema Serikali iongeze jitihada katika kuhakikisha mashirika yanayohusika yanatekeleza kikamilifu jukumu hili la kupeleka gawio.

(d) Sheria ya Msajili wa Hazina inazingatia taasisi au mashirika ya umma kuwasilisha asilimia 70 ya ziada baada ya kutoa gharama za uendeshaji na matumizi yanayoruhusiwa. Kwa mwaka wa fedha 2021/2022 jumla ya shilingi bilioni 105.02 zilikusanywa chini ya kipengele hiki. Kiasi kilichokusanywa ni sawa na asilimia 112 la lengo lililokusudiwa. Mwenendo huo unaonesha ufanisi kwa lengo la asilimia 90 lilifikiwa katika kipindi cha miaka mitatu.

Mheshimiwa Spika, vilevile Mwongozo wa Msajili wa Hazina kuhusu Uchangiaji au Ukusanyaji wa Mapato Yasiyo ya Kikodi unaelekeza taasisi ambazo hazichangii chini ya Sheria ya Gawio na Mchango wa Asilimia 15 na Ziada kuchangia Mfuko wa Serikali chini ya kipengele cha michango mengineyo. Uchambuzi wa Kamati ulibaini kukiukwa kwa mwongozo huu ambapo taasisi zinazoangukia katika kipengele hiki baadhi zimekuwa zikipata faida lakini baadhi zimekuwa hazitekelezi kabisa na nyingine zimekuwa zikijipangia kiasi kidogo cha kuchangia. Mfano, Kamati ilikutana na Bodi ya Chai Tanzania ambayo kwa kipindi cha miaka mitatu mfululizo ilichangia shilingi bilioni mbili tu kwa miaka mitatu.

(e) Ulinganisho wa marejesho ya uwekezaji katika mashirika na taasisi za umma na Kampuni ambayo Serikali ina hisa chache. Kwa mwaka wa fedha 2021/2022 marejesho ambayo Serikali ilipata…

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu ngoja. Bodi ya Chai imechangia kiasi gani kwa miaka mitatu?

**MHE. DEUS C. SANGU – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UWEKEZAJI WA MITAJI YA UMMA (PIC):** Mheshimiwa Spika, Bodi ya Chai Tanzania ilichangia shilingi milioni mbili tu kwa miaka mitatu.

(e) Ulinganisho wa marejesho ya Uwekezaji kati ya Mashirika na Taasisi za Umma na Kampuni ambazo Serikali ina Hisa chache.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2021/2022, marejesho ambayo Serikali ilipata kutoka kwa uwekezaji kwenye Kampuni ya ambapo ina hisa chache ni asilimia 8.9 ikilinganishwa na asilimia 2.2 kutoka kwenye Uwekezaji wa Mashirika ya Umma. Tofauti hiyo ni kiashiria cha kutofautiana ufanisi wa mitaji katika uwekezaji kwa maeneo hayo mawili tofauti. Ukizingatia Serikali imewekeza kiasi kikubwa sana kwenye Mashirika ya Umma, lakini Chumo *(return on investment)* yake ni ndogo ukilinganisha na kule ambapo Serikali imeweka hisa chache.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya pili pia inabainisha masuala mbalimbali kuhusu usimamizi na utendaji wa taasisi zinazotumia mtaji wa umma kama ifuatavyo:-

(i) Malimbikizo ya madeni yanayotokana na utoaji wa huduma kwenye taasisi nyingine za Serikali.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya Taasisi zinakabiliwa na madeni makubwa na hazina mipango wala jitihada za kuyalipa au kuyapunguza madeni haya, hususan madeni haya ya taasisi za Serikali jambo linaloathiri utendaji na ufanisi wa taasisi zinazodai. Mfano ni SUMA JKT ambayo inakabiliwa na madeni *(receivables)* inadai Kampuni za Serikali. Nitaanza na Kampuni ya SUMA *Guard* inadai shilingi bilioni 17.70, Kampuni ya Usafi ya SUMA JKT inaidai Serikali shilingi milioni 107.13, Kampuni ya Ujenzi ya SUMA JKT inaidai Taasisi za Serikali shilingi bilioni 14.27, Kampuni ya Huduma za Bandari ya SUMA JKT inadai Taasisi za Serikali shilingi bilioni 5.97.

Mheshimiwa Spika, jumla ya kiasi cha shilingi bilioni 38.06 ni Mapato ya SUMA JKT ambayo imeshindwa kukusanya kutoka kwenye Taasisi za Serikali zilizopata huduma. Hivyo, orodha ya wadaiwa hao ninayo hapa, kwa ruska yako naweza kukukabidhi ili uweze kufanya rejea. Kama kiasi hicho kingelipwa, kingeongeza ukwasi na ufanisi wa Taasisi ya SUMA JKT na hivyo tija ya uwekezaji ingeweza kuongezeka. Ni rai ya Kamati kwa Serikali isimamie kwa ukali kabisa kuhakikisha taasisi zinazodaiwa na SUMA JKT zinalipa madeni hayo haraka iwezekanavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, taasisi nyingine zenye changamoto ni Taasisi ya *DAWASA*, ambayo inavidai vyombo vya Ulinzi na Usalama jumla ya shilingi bilioni 13.93. Hiyo inatokana na huduma ya maji waliyotumia, maana yake wametumia maji bure ya shilingi bilioni 13.93. Vilevile *AICC* inazidai taasisi mbalimbali za Serikali takribani shilingi bilioni 4.45 madeni yanayotokana na kukodi kumbi za Mikutano ya *AICC*. Taasisi hizi zilitumiwa na Kamati kama mfano. Hizi ni taasisi chache miongoni mwa taasisi nyingi zinazokabiliwa na changamoto hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo hili linapunguza mapato ya taasisi zinazodai na kuathiri utendaji wake. Ni vyema Serikali ikaelekeza taasisi zote zinazodaiwa na zinazotumia huduma kutoka kwenye nyingine za Serikali kulipa kwa wakati madeni hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, changamoto ya upungufu wa mtaji kwa baadhi ya Mashirika ya Umma. Taarifa ya Uwekezaji inabainisha kuwa kuna baadi ya Mashirika ya Umma yanakabiliwa na upungufu wa mtaji wa kuendesha, jambo linalosababisha kupungua kwa utendaji na ufanisi. Upungufu huo wa mtaji umekuwa ukisababishwa na taasisi husika kupata hasara mfululizo kwa kipindi kirefu na kuwa na madeni makubwa. Baadhi ya Taasisi zinazokabiliwa kuwa na upungufu wa mtaji ni pamoja na *ATCL*, Shirika la *NDC, TTCL*, Benki ya Maendeleo *(TIB)* na *TRC*. Hizo ni kwa uchache.

Mheshimiwa Spika, Serikali inapaswa kufanya tathmini ya mara kwa mara kwa mashirika yake ili kubainika utendaji wake, ufanisi na tija inayopatikana. Vilevile kubaini hali halisi ya mashirika yake na kuona kama yanasaidia na kuyaokoa Mashirika ambayo kwa namna moja au nyingine yangeweza kusaidiwa mapema, ufanisi ungeimarika na mtaji wa umma ungekuwa salama.

Mheshimiwa Spika, ongezeko la riba inayotokana na ucheleweshaji wa kuwalipa wakandarasi au wazabuni. Utekelezaji wa miradi ya uwekezaji unapaswa kuzingatia mikataba ya utekelezaji ambao hubainisha taratibu zote ikiwemo muda wa malipo na faini kama malipo yatachelewesha au wajibu mwingine wa mkandarasi. Uchambuzi umebaini kuwa baadhi ya taasisi au Mashirika ya Umma ambayo yameshindwa kutekeleza masharti ya mkataba katika kufanya malipo ya wazabuni kwa

wakati, jambo lililosababisha madeni kuendelea kuongezeka baada ya kujumlisha riba ya ucheleweshaji na hivyo kuongeza mzigo mkubwa kwa Serikali.

Mheshimiwa Spika, jambo hili limebainishwa kwenye Ripoti ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali *(CAG)* ya Mwaka 2021/2022 ambapo imedhihiriswa kuwa taasisi 12 zinadaiwa shilingi bilioni 63.77 na hizi ni taasisi chache kati ya taasisi 304 katika Mashirika. Ni taasisi 12 tu zinadaiwa shilingi bilioni 63.77 inayotokana na riba na adhabu za kuchelewa kwa malipo mbalimbali. Aidha, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa baadhi ya taasisi zimekuwa zikisababisha ucheleweshaji wa makusudi hasa kwenye miradi ya ufadhili *(Donor Funded Project)*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utendaji wa mashirika usiozingatia vigezo vilivyowekwa na Msajili wa Hazina. Kwa madhumuni ya ufanisi katika uwekezaji wa mitaji ya umma, Kifungu cha 10(2)(d) cha Sheria ya Msajili wa Hazina, Sura 370, kinamtaka Msajili wa Hazina kuzipa Bodi za Wakurugenzi wa mashirika, malengo ya kifedha na vigezo vya utendaji vinavyopaswa kuiongoza bodi katika uendeshaji wake.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati unabainisha kwamba baadhi ya taasisi au mashirika yamekuwa yakijiendesha bila kuzingatia vigezo walivyopewa. Mfano, baadhi ya taasisi zimekutwa hazina uwiano mzuri wa mapato na matumizi, jambo linaloathiri mtaji wa taasisi. Uwiano wa madeni ya muda mfupi kulinganisha na mapato ya muda mfupi, jambo linaloathiri ulipaji wa madeni haya. Pia, kasi ndogo ya ukusanyaji wa mapato jambo linaloathiri ukwasi wa taasisi.

Mheshimiwa Spika, changamoto ilibainika katika baadhi ya taasisi ikiwepo Bodi ya Chai *(TTB)*, Mfuko wa Pembejeo wa Taifa *(AGTIF)*, Mfuko wa Bima ya Afya wa Taifa *(NHIF)*, Wakala wa Manunuzi wa Serikali *(GPSA)* na hizi ni baadhi ya taasisi chache kati ya zile tulizozipitia.

Mheshimiwa Spika, kuchelewa kukamilika kwa miradi jambo linalosababisha kuongezeka kwa gharama za utekelezaji. Katika wakati wa kuchambua taarifa za mashirika zilizowasilishwa mbele ya Kamati ilibainika kuwa, kuna baadhi ya taasisi na mashirika ya

umma yamekuwa na kasi ndogo katika kutekeleza miradi yake ya uwekezaji. Jambo linalosababisha kuchelewesha kukamilika kwa miradi hiyo na hivyo kulazimika kuongeza muda wa utekelezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, athari ya jambo hili ni kuongezeka kwa gharama ya utekelezaji wa mradi kwani, hulazimika kulipa riba kwa wakandarasi na pia husababisha kuchelewa kuanza kunufaika na kupata chumo *(return on investment)* ya miradi hiyo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Spika, changamoto hii ilibainika katika taasisi ikiwemo *NSSF* kwa kampuni yake Tanzu ya Mkulazi, ambao Mradi wa Kiwanda cha Sukari Mkulazi utekelezaji wake ulitarajia kukamilika Desemba 2022. Mradi huu haujakamilika kwa wakati jambo lililosababisha kufanya mapitio upya, (*review* ya mradi na gharama yake). Ilitoka kwenye Dola za Kimarekani milioni 32.64 na baadaye imeongezeka kwa 146%.

Mheshimiwa Spika, naomba nirudie sehemu hii kwa umuhimu wake. Mradi wa Kiwanda cha Sukari Mkulazi utekelezaji wake ulitarajiwa kukamilika Desemba 2022. Mradi huu haujakamilika kwa wakati jambo lililosababisha kufanyika kwa mapitio upya *(review)*. Gharama za utekelezaji zimebainika kuwa uhitaji wa ongezeko la Dola za Kimarekani milioni 32.64 ambalo ni ongezeko la 146%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, Kuchelewa kukamilika kwa kiwanda kulisababisha miwa iliyokuwa tayari iharibike na kuongeza gharama kwa watunzaji miwa kwa muda wa kuvuna, hivyo kusababisha hasara kwa Serikali ya shilingi bilioni 2.3. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Serikali wa Kupitia Mashirika haya. Kamati imejulishwa kuwa Serikali inafanya mapitio ya taasisi zake kwa lengo la kuona ufanisi wake, kufuta yale yasiyo na tija na kuunganisha baadhi ya mashirika ambayo majukumu yake yanashabihiana.

Mheshimiwa Spika, Kamati inatoa angalizo katika eneo hili. Katika utekelezaji wa jambo hili, kuwa Serikali iweke umakini lengo la kutohamisha mzigo kutoka kwenye taasisi moja na kupeleka

kwenye taasisi nyingine. Haya mambo tumeyaona ambapo Serikali ilikuwa inabadilisha *DAWASCO* kuwa *DAWASA,* kuunganisha *SELF Microfinance* na *UTT Microfinance,* pamoja na kuunganisha Benki ya *TPB* na *TIB Corporate* kuunda *TCB.* Kulikuwa na shida nyingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, athari za mikopo chechefu. Kamati ilibaini kuwa kuna baadhi ya taasisi zinakabiliwa na changamoto ya kuwa na kiasi kikubwa cha tengo chechefu, jambo linaloathiri mizania ya vitabu vya taasisi hizo. Changamoto hii ilibainika kwa Mfuko wa Pembejeo wa Taifa *(AGITF)* na SUMA JKT.

Mheshimiwa Spika, kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 Mfuko wa Pembejeo wa Taifa *(AGITF)* ulikuwa unadaiwa madeni *(receivable)*ya jumla ya shilingi bilioni 26.4 yanayotokana na mikopo ya pembejeo na zana za kilimo zilizotolewa kwa wakulima. Kati ya deni hilo, shilingi bilioni 21.4 ni tengo la madeni chechefu kwa maana ni madeni hayajaweza kulipwa na yamechukua muda mrefu sasa. Kiasi cha mikopo hiyo chechefu ni sawa na 81% ya madeni ya Mfuko kinyume cha takwa la kisheria linalodai tengo la mikopo chechefu kuwa 5% tu.

Mheshimiwa Spika, SUMA JKT inakabiliwa na kiasi kikubwa cha tengo la madeni chechefu katika vitabu vyake ambalo ni takribani shilingi bilioni 50.3 lililotokana na mradi wa kukopesha Matrekta. Msingi wa deni hili ni Serikali iliipatia SUMA JKT mkopo wa Matrekta na zana zake, vyenye thamani ya shilingi bilioni 61. Deni hili limekuwa chechefu baada ya SUMA JKT kushindwa kukusanya marejesho kutoka kwa wakulima takribani shilingi bilioni 38.78. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia baadhi ya zana zimebaki ambazo kutokana na mabadiliko ya teknolojia, changamoto hii inasababisha SUMA JKT kushindwa kulipa deni kwa Serikali. Ni rai kwa Kamati kuwa, Serikali ifanye tathimini kuangalia namna ya kulifuta deni hili kwa SUMA JKT kiuhalisia halilipiki na linaathiri mizania ya vitabu vya Shirika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ipo haja ya Serikali ifanye tathmini ya madeni chechefu, baadhi ya mashirika na kufanya kuyabadilisha kuwa mtaji *(dept to equity convention)* kwani, vitabu vya hesabu

kwa baadhi ya mashirika vimeathiriwa na uwepo wa madeni haya. Jambo hili ni hatari kwa misingi ya kibiashara na utendaji wa shirika kwa ujumla. Mfano, vitabu vya hesabu vya *DAWASA* vinaonesha kwamba, vinaathiriwa na na deni la shilingi bilioni 47 ambalo walirithi kutoka *DAWASCO* ilipokuwa inabadilishwa kuwa *DAWASA*.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa *SELF Microfinance* ina deni la shilingi bilioni 6.03 ambalo ilirithi walipounganishwa na *UTT Microfinance*. Ipo haja ya madeni haya kupitiwa upya na kuona kama kuna uwezekano wa kuyapeleka kutoka kwenye deni na kuwa mtaji *(convention from debt to equity)*. Kwa msingi wa mambo haya, Kamati inatoa mapendekezo iwapo Bunge litaridhia yanaweza yakatatua changamoto zilizopo katika uwekezaji wa mitaji ya umma.

Mheshimiwa Spika, pendekezo la kwanza, mchango katika Mfuko wa Serikali. Bunge linaazimia kwamba: -

(a) Sheria ya Msajili wa Hazina, Sura 370 irekebishwe ili kuweka bayana utaratibu na mfumo wa taasisi zote zinazopata faida ziwajibike kisheria kuchangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali;

(b) Serikali iongeze msisitizo kwa taasisi zinazotumia mtaji wa umma ili zitekeleze wajibu wa kuchangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali na pale ambapo itatokea kutokuzingatiwa kwa wajibu huo, adhabu na hatua nyingine stahiki zitumike kukazia utekelezaji. Kwa sababu kwa sasa ilivyo taasisi inaweza isipeleke gawio na wala hamna hatua yoyote inayochukuliwa. Kwa hiyo, ni kama hiyari pamoja na kwamba kuna sheria.

Mheshimiwa Spika, suala la utegemezi wa Ruzuku kutoka Serikalini. Bunge lliaazimia kwamba: -

(a) Serikali iweke utaratibu wa kufanya tathmini ya mara kwa mara ya taasisi za umma, ili kubaini taasisi zinazohitaji ruzuku na zisizohitaji ruzuku;

(b) Taasisi za umma zinazotumia mtaji wa umma na ambazo zinapatiwa ruzuku ya Serikali zikifikia kiwango cha

kujitegemea zipewe muda mahsusi na kuanza kujitegemea. Maana yake nyingine zina uwezo, zinapokea ruzuku zinaweza zikajitegemea.

Mheshimiwa Spika, pendekezo la tatu, juu ya uzingatiaji wa vigezo vya utendaji vilivyopangwa na Msajili wa Hazina.

(a) Yafanyike marekebisho ya sheria ya Msajili wa Hazina sura 370 ili:-

(i) Kumuongeza nguvu Msajili wa Hazina kwa lengo la kumwezesha kufuatilia na kuziwajibisha bodi zinazoshindwa kuzingatia vigezo na kujielekeza kwenye malengo yaliyowekwa. Kwani, ilivyo sasa hana uwezo wa kuziwajibisha;

(ii) Kuweka utaratibu wa kupata bodi na wajumbe katika bodi hizo kwa njia za ushindani, kwa maana ya kufata vigezo vya ushindani.

(b) Msajili wa Hazina atenge utaratibu wa kufanya mapitio *(periodic review)* ya vigezo vinavyotolewa kwa Bodi ya Wakurugenzi na Menejimenti za Taasisi zinazotumia mtaji wa umma ili kuhakikisha kuwa, vinaendana na hadhi *(status)* ya taasisi husika.

Mheshimiwa Spika, namba nne, ongezeko la riba itokanayo na ucheleweshaji wa kulipa wakandarasi au wazabuni. Bunge linaazimia kwamba: -

(a) Serikali iongeze usimamizi kwa taasisi zake za uwekezaji zinazotekeleza miradi, ili zizingatie masharti ya mikataba baina yao na wakandarasi au watoa huduma kwa lengo la kuepuka riba za ucheleweshaji; na

(b) Uandaliwe utaratibu wa kuziwajibisha bodi za wakurugenzi na menejimenti za taasisi zinazoshindwa kuzingatia masharti ya mikataba na kusababisha hasara katika uwekezaji. Kwani, ilivyo sasa wanasababisha riba hawachukuliwi hatua yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namba tano, athari juu ya Sekta ya Bima *(NIC)*. Bunge linaazimia kwamba Serikali itoe fursa ya taasisi za zinazofanya biashara za kimataifa ikiwemo *NIC* kuweza kufuata *best practice* za soko kwa lengo la kuwawezesha kushiriki kikamilifu na kuweza kushindana kwa lengo la kuwaongezea ufanisi na tija. Kwa, mfano tulikuta Shirika la *NIC* linashindwa kushindana kwa sababu ya kalenda yake inatofautiana na *competitor* wenzake.

Mheshimiwa Spika, Athari za Mikopo Chechefu.

Kwa Kuwa, Taarifa za uwekezaji zimeonesha kuwepo kwa taasisi zinazotumia mtaji wa umma, zenye kiasi kikubwa cha mikopo chechefu *(non-performing loans)* zikiwemo Mfuko wa Pembejeo wa Taifa na SUMA JKT,

Na Kwa Kuwa, Mikopo chechefu kwenye vitabu vya taasisi yoyote inaathiri mizania na kupunguza ukwasi. Jambo linaloathiri uendeshaji na ufanisi wa uwekezaji,

Kwa Hiyo Basi, Bunge linaazimia kwamba, Serikali ihakikishe kuwa: -

(a) Taasisi zote za ukopeshaji ziwe na sera nzuri ya mikopo.

(b) Mikataba kati ya taasisi ya fedha na wakopaji inaandaliwa kwa umakini mkubwa, ili kuboresha na kuondoa mianya inayosababisha mikopo chechefu;

(c) Taasisi zinazotumia mitaji ya umma zinawekewa mifumo Madhubuti ya *TEHAMA* inayotumika kuchakata maombi na kuweka utaratibu mzuri wa kudhibiti na kuimarisha utoaji na ukusanyaji wa mikopo;

(d) Uchambuzi unafanyika ili kubainisha umri wa mikopo chechefu na kuiondoa kwenye vitabu vya taasisi bila kuathiri ulipaji wa mikopo inayolipika; na

(e) Hili ni la muhimu. Hatua stahiki za kinidhamu zichukuliwe dhidi ya waliohusika kusababisha mikopo chechefu kwenye taasisi hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namba saba, tathimini ya utendaji wa Mashirika. Bunge linaazimia kwamba: -

(a) Serikali ifanye tathimini ya taasisi zinazotagemewa kuunganishwa na kubaini hali ya Kifedha *(financial position)* yake kabla ya kuziunganisha;

(b) Madeni chechefu yote yalipwe au kama hayalipiki yafutwe kwenye vitabu vya mashirika au taasisi zinazounganishwa kwa lengo la kuepuka kuhamisha mzigo wa madeni kutoka taasisi ya zamani kupeleka kwenye taasisi mpya;

(c) Kiundwe chombo maalum ambacho kitasimamia mikopo chechefu, ili kutoa nafasi ya Taasisi mpya kuanza na kumbukumbu za vitabu vilivyo safi.

Mheshimiwa Spika, pendekezo la nane, mkakati wa kuhuisha Mashirika yanayojiendesha Kibiashara *(Turnaround Strategy)*. Bunge linaazimia kwamba Serikali kupitia Msajili wa Hazina izisaidie taasisi zinazodhorota kwa kuandaa mpango wa mageuzi *(Turnaround Strategy)* na kuzisimamia kwa karibu ili kuhakikisha zinautekeleza mkakati huo.

Mheshimiwa Spika, pendekezo la tisa, taasisi kubuni na Kuongeza vyanzo mbadala vya mapato. Bunge linaazimia kwamba Serikali ihakikishe kuwa, inazisimamia bodi zote zinazojiendesha kibiashara ili zinafanye tathimini ya na kubuni vyanzo vyote mbadala vya mapato na fursa zaidi ya uwekezaji kwa lengo la kuongeza ukwasi wa taasisi na faida kwa Serikali.

Mheshimiwa Spika, pendekezo la kumi, kutokukamilika kwa miradi ya uwekezaji kwa wakati. Bunge linaazimia kwamba Serikali kupitia Msajili wa Hazina iongeze usimamizi wa karibu kwa taasisi zinazotekeleza miradi, ili zikamilishe miradi ndani ya muda wa mkataba bila gharama ya ziada.

Mheshimiwa Spika, pendekezo la kumi na moja, udhibiti wa upotevu wa maji yaliyotibiwa kwa Mamlaka za Maji, tulipitia.

Kwa Kuwa, mamlaka za maji hutumia mitaji wa umma katika kutibu maji hivyo, zinawajibika kudhibiti upotevu wa maji yaliyotibiwa hadi kufikia au sawa chini ya 25%;

Na Kwa Kuwa, taarifa za uwekezaji za Mamlaka za Maji zinabainisha kuwepo kwa tatizo hilo katika udhibiti wa maji yaliyotibiwa kwa kiasi cha kusababisha hasara ya jumla ya shilingi Bilioni 162.14;

Kwa Hiyo Basi, Bunge linaazimia kwamba, Serikali ihakikishe: -

(a) Mamlaka za Maji zinashirikiana na Serikali za Mitaa kuweka mfumo madhubuti wa utoaji wa taratibu kuhusu kulinda uharibifu wa miundombinu ya maji pale unapotokea; na

(b) Ukaguzi kafanyika mara kwa mara katika miundombinu ya maji na kuboresha maeneo chakavu.

Mheshimiwa Spika, pendekezo namba kumi na mbili, kuimarisha Mfuko wa Taifa Bima ya Afya wa Taifa *(NHIF)*. Bunge liaazimia kwamba: -

(a) Serikali ifanye tathmini ya kina juu ya uhai na uendelevu wa Mfuko;

(b) Mfuko ufanye mapitio na kuboresha utaratibu wa usajili wa makundi ya wanachama wanaojiunga kwa hiyari;

(c) Mfuko uweke mifumo imara ya TEHAMA kwa ajili ya kutambua wateja halali wanaopata huduma, kama vile matumizi ya *biometric;*

(d) Mfuko uweke mfumo thabiti wa kutambua madai halali yanayoletwa kwa Mfuko kutokana na huduma wanazotoa maana yake kumekuwa na madai *fake*.

(e) Tathmini ya vifurushi vinavyoletwa na Mfuko ifanyike na kuboresha kadiri ya mahitaji, kuepuka kuumiza upande wowote kati ya mfuko na wanachama;

Mheshimiwa Spika, namba kumi na tatu, changamoto ya Mtaji kwa baadhi ya taasisi. Bunge linaazimia: -

(a) Serikali ifanye tathimini ya kina juu ya mahitaji ya mtaji kwa baadhi ya mashirika zinazojiendesha kibiashara na kuziruhusu kukopa kwa ajili ya kuongeza mtaji na ufanisi wa uwekezaji;

(b) Serikali iharakishe mchakato wa kuanzisha Mfuko wa Uwekezaji wa Taifa, kwa ajili ya kuyawezesha mashirika ambayo yanafanya vizuri lakini yana changamoto ya mtaji.

Mheshimiwa Spika, pendekezo letu la kumi na nne na la mwisho. Mchakato wa Utungwaji wa Sheria ya Msajili wa Hazina. Bunge linaazimia kwamba Serikali ikamilishe mchakato wa Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Msajili wa Hazina Sura ya 370 na kuiwasilisha Bungeni kwa uamuzi ili kuweka mazingira ya kisheria yanayoongeza ufanisi katika usimamizi wa mitaji ya umma.

Mheshimiwa Spika, hitimisho, napenda kuchukua fursa hii kukushukuru wewe binafsi, kwa uongozi wako na miongozo mbalimbali ambayo umekuwa ukiipa Kamati wakati wa utekelezaji wa majukumu yako mpaka leo tunapowasilisha taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, pia naomba nimshukuru Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wa Bunge kwa weredi waliouonyesha katika kukusaidia wewe katika jukumu la kuliongoza Bunge. Utekelezaji wa majukumu ya Kamati umefanikiwa kwa kiasi kikubwa kutokana na maelekezo, ushauri na miongozo ya kiti chako kwa kipindi chote cha utekelezaji wa Majukumu ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, kipekee napenda kumshukuru na kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuhakikisha kwamba, anakuwa na usimamizi bora katika Taasisi na Mashirika ya Umma na kuwekeza msukumo wa hali ya juu katika uwekezaji wenye tija kwa Taifa hili, kwa sababu tumeona kiwangio cha uwekezaji kwenye mitaji ya umma kimeendelea kukua mwaka hadi mwaka, hadi kufikia hizo trilioni 73.56. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma kwa kutekeleza majukumu ya Kamati hii kwa moyo na uadilifu mkubwa. Naomba kuwatambua Wajumbe hao majina yao na kama yalivyoonekana kwenye Taarifa ya Kamati. Kutokana na changamoto ya muda sitayasoma ila naomba iingie kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Spika, vilevile, napenda kushukuru Ofisi ya Msajili wa Hazina inayoongozwa na Ndugu Nehemia Mchechu, kwa ushirikiano wao wa dhati wanaoutoa katika utekelezaji wa Majukumu ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, pia napenda kuwashukuru watumishi wote wa Ofisi ya Bunge, wakiongozwa na Katibu wa Bunge Ndugu Nenelwa J. Mwihambi, *ndc* kwa ushirikiano wa hali ya juu walioutoa ikiwa ni pamoja na kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kikamilifu na kwa wakati wote mpaka sasa ninapowasilisha Taarifa hii ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, taarifa hii ni matokeo ya uchambuzi wa kina kuhusu Uwekezaji wa Mitaji ya Umma unaofanywa na Taasisi na Mashirika ya Umma, maoni na mapendekezo yanayotokana na uchambuzi uliofanywa na Kamati yanalenga kuishauri Serikali katika eneo la Uwekezaji wa Mitaji ya Umma ili uwekezaji huo uwe wa ufanisi na ulete tija kwa Taifa.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa kutoa hoja kwamba, Bunge likubali kuipokea na kuijadili Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma, kuhusu uchambuzi wa uwekezaji wa Mitaji ya Umma kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, ili hatimaye kupitisha mapendekezo ili yawe Maazimio ya Bunge.

**2 NOVEMBA, 2023**

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UWEKEZAJI WA MITAJI YA UMMA KUHUSU UWEKEZAJI WA MITAJI YA UMMAKWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

## SEHEMU YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

### 1.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (PIC) kuhusu Uwekezaji wa Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, na kuliomba Bunge likubali kuipokea na kuijadili. Taarifa hii inaliarifu Bunge lako kuhusu mwenendo wa Uwekezaji wa Mitaji ya Umma kwa kipindi cha mwaka 2021/2022 ili kuliwezesha Bunge kuujadili mwenendo huo na hatimaye kutoa maazimio yake.

### 1.2 Muundo wa Taarifa

**Mhesimiwa Spika**, Kwa kuwa Taarifa hii inajenga msingi wa majadiliano juu ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma, naomba kubainisha muundo wake ili kurahisisha ufuatiliaji wa Waheshimiwa Wabunge. Kimuundo na kimaudhui, Taarifa hii imegawanyika katika Sehemu Kuu tatu kwa mujibu wa Kanuni ya 142 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 zinazojulikana kwa kifupi kuwa ni Kanuni za Bunge. Sehemu hizo ni:-

(i) Sehemu ya Kwanza inayotoa maelezo ya msingi kuhusu Taarifa hii na kazi za Kamati;

(ii) Sehemu ya Pili inayofafanua shughuli za Kamati za ufuatiliaji wa Mitaji ya Umma ambazo ni chimbuko la maoni na Mapendekezo yanayotolewa; na

(iii) Sehemu ya Tatu na ya mwisho inayohitimisha kwa kubainisha mtazamo wa Kamati juu ya uwekezaji wa mitaji ya umma, ambao ni msingi wa Mapendekezo ya Kamati kuhusu maazimio ya Bunge. Sehemu hii imewekwa kwa mfumo wa hoja unaotakiwa kwa mujibu wa Kanuni ya 61(3) ya Kanuni za Bunge, Toleo la Februari, 2023.

### 1.3 Msingi wa Ufuatiliaji wa Mitaji ya Umma

**Mheshimiwa Spika**, Msingi wa shughuli za Kamati katika Ufuatiliaji wa Mitaji ya Umma, unatokana na Bunge kuwa na madaraka yaliyoelezwa kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, pamoja na sheria zilizotungwa na Bunge kuhusu mambo mbalimbali ya uwekezaji na usimamizi wa mitaji ya umma kama ifuatavyo:-

#### 1.3.1 Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

**Mheshimiwa Spika**, Ufuatiliaji wa Mitaji ya Umma unaofanywa na Bunge lako tukufu, unatokana na misingi ya uendeshaji wa nchi iliyofafanuliwa na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Misingi hiyo ni pamoja na nafasi ya Bunge katika kuisimamia na kuishauri Serikali, hususani kuhusu uwekezaji wa mitaji ya umma. Aidha, Ibara ya 96 ya Katiba imelipa Bunge uwezo wa kuunda Kamati na kufafanua majukumu ya Kamati hizo katika Kanuni za Kudumu za Bunge. Kwa msingi huo, shughuli zote za Kamati ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma zinazoripotiwa katika Taarifa hii, zinaendana na kuzingatia masharti hayo.

#### 1.3.2 Kanuni za Kudumu za Bunge

**Mheshimiwa Spika**, Kanuni za Kudumu za Bunge zinaeleza majukumu ya Kamati za Bunge ikiwa ni pamoja na majukumu ya Kamati hii. Aidha, Kanuni zinafafanua utaratibu wa uendeshaji wa shughuli zote za Kamati za Bunge kama vile shughuli za ufuatiliaji wa mitaji ya umma kwenye taasisi ambazo Serikali ina hisa nyingi na kule ambapo Serikali ina hisa chache. Si hivyo tu, bali pia, Kanuni za Bunge zinaeleza namna ambavyo Taarifa ya Kamati inavyoweza kupangwa kwenye Orodha ya Shughuli za Bunge kama ilivyo leo hii.

**Mheshimiwa Spika**, Tunafahamu kwamba, Kanuni ya 136 (17) ya Kanuni za Bunge imekupa uwezo wa kuagiza Taarifa hii ipangwe kwenye Orodha ya Shughuli za Bunge za leo ili ijadiliwe. Tunakushukuru kwa kutekeleza mamlaka uliyo nayo na sasa Taarifa hii inawasilishwa Bungeni. Naliomba Bunge liipokee na kuijadili ili kutekeleza jukumu la kuishauri na kuisimamia Serikali katika masuala ya uwekezaji wa mitaji ya umma.

### 1.3.3 Sheria ya Msajili wa Hazina (Madaraka na Majukumu), Sura ya 370

**Mheshimiwa Spika**, Sheria ya Msajili wa Hazina (Madaraka na Majukumu), Sura ya 370, imeanzisha Ofisi ya Msajili wa Hazina (OMH) kwa madhumuni ya utwaaji (*acquisition*), umilikaji (*holding*) na usimamizi (*managemen*t) wa mitaji ya umma kwa niaba ya Serikali. Kwa mujibu wa Sheria hii, mitaji ya umma ni pamoja na hisa, hati fungani, dhamana ya hisa ya mikopo, rehani ya ndani au nje ya bodi inayotambulika kisheria, ambayo imetolewa na Serikali au kwa niaba ya Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Sheria hii pia, imefafanua majukumu na madaraka ya Msajili wa Hazina (MH) katika uwekezaji wa mitaji ya umma unaofuatiliwa na Kamati. Kwa msingi huo, ufuatiliaji wa mitaji ya umma unaendana na kutathmini namna utendaji na uendeshaji wa mitaji ya umma ulivyo na ukubalifu (*Compliance*) wa masharti ya Sheria hii kuhusu usimamizi wa mitaji ya umma.

### 1.3.4 Sheria Mbalimbali kuhusu Uwekezaji wa Mitaji ya Umma

**Mheshimiwa Spika,** Zaidi ya Sheria ya Majukumu na Mamlaka ya Msajili wa Hazina, Sura ya 370, zipo pia Sheria mbalimbali zinazoweka masharti kuhusu mitaji ya umma na usimamizi wake. Miongoni mwa Sheria hizo ni Sheria ya Mashirika ya Umma, Sura ya 257, Sheria ya Bajeti, Sura ya 439 na Sheria ya Fedha za Umma, Sura ya 348.

**Mheshimiwa Spika,** Sheria ya Mashirika ya Umma imeweka masharti kuhusu uanzishaji, usimamizi, uongezaji wa ufanisi na mambo mengine yanayohusiana au yanayowezesha madhumuni hayo. Kwa sababu hiyo, Kamati, ilizingatia masharti ya Sheria hii ili kujiridhisha iwapo uwekezaji wa mitaji katika mashirika ya umma unafanyika kwa mujibu wa masharti ya sheria kuhusu usimamizi na ufanisi wa uendeshaji unaotumia mitaji ya umma katika mashirika hayo.

**Mheshimiwa Spika,** Sheria ya Fedha za Umma, imeweka masharti ya udhibiti (cont*rol*), usimamizi (*Management*) na urekebu (*Regulation*) wa makusanyo na matumizi ya fedha za umma katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na masharti ya udhibiti na usimamizi wa kibunge wa fedha na rasilimali za umma. Kwa mujibu wa Sheria hiyo, fedha zinazotumika katika mtaji wa umma,

mali zilizopo katika vitega uchumi vitokanavyo na fedha za umma na mikopo katika uendeshaji wa vitega uchumi ni sehemu ya rasilimali za umma. Kwa msingi huo, chumo (*Returns*) kutokana na fedha za umma linapaswa kuangaliwa kwa kuzingatia masharti ya Sheria hii.

**Mheshimiwa Spika,** Kifungu cha 17 cha Sheria ya Bajeti, Sura ya 439, kinampa Msajili wa Hazina Madaraka na Majukumu ya kusimamia fedha zinazotolewa kwa ajili ya uwekezaji kwenye taasisi au mashirika anayoyasimamia. Kwa mujibu wa Kifungu hicho Msajili wa Hazina analo jukumu na madaraka ya kuhakikisha kwamba mashirika na taasisi anazozisimamia zinalipa magawio na michango stahiki kwa serikali. Vilevile ni wajibu wa Msajili wa Hazina kusimamia mitaji, ruzuku, na fedha zote zinazobakizwa katika mashirika ya umma au taasisi nyingine zinazotumia mitaji ya umma. Kwa msingi huo, Sheria ni miongoni mwa miongozo iliyotumiwa na Kamati katika kutathmini mwenendo wa uwekezaji wa mitaji ya umma.

**1.4 Muundo wa Uwekezaji wa Mitaji ya Umma nchini**

**Mheshimiwa Spika**, Muktadha wa Taarifa ya uwekezaji wa mitaji ya umma Bungeni unatokana na muundo unaotumika nchini wa matumizi na usimamizi wa mitaji ya umma. Serikali kwa maana ya mamlaka ya Utendaji nchini (Executive) ndiyo yenye dhamana ya kutumia mitaji ya umma kwa maslahi ya nchi. Bunge (legislature) lina madaraka ya kusimamia na kuishauri serikali kuhusu shughuli za umma ikiwemo uwekezaji wa mitaji ya umma. Kamati hii inalisaidia Bunge kufuatilia tija na ufanisi wa mitaji ya umma kwa kuripoti Bungeni ili kupata uamuzi wa Bunge.

**1.5 Wigo (Scope) wa ufuatiliaji wa Mitaji ya Umma**

**Mheshimiwa Spika,** Ufuatiliaji wa mitaji ya umma ni jambo lenye mawanda (scope) maalumu. Mawanda hayo yanaonesha mipaka ya kazi na ni ukomo wa matarajio ya matokeo ya kazi ya Kamati. Naomba kuliainishia Bunge hili mipaka hiyo kama ilivyobainishwa katika Kifungu cha 11(1) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge. Kanuni hiyo inaweka ukomo wa kazi za Kamati kwenye mambo makuu mawili. Mambo hayo ni:-

(i) Ufanisi wa miradi ya uwekezaji wa mitaji ya Umma kwa kuzingatia taratibu, Sheria na miongozo mujarabu ya biashara kwenye mashirika ya Umma; na

(ii) Tija inayopatikana kwa kuwekeza mitaji kwenye Kampuni ambazo Serikali ina hisa.

**Mheshimiwa Spika**, Katika wigo huo, Kamati inalenga kubaini iwapo uwekezaji wa mitaji ya umma unawezesha upatikanaji wa chumo (*Returns on Investiment*). Ili kufikia lengo hilo, Kamati ilitaka kujiridhisha na matokeo ya utaratibu uliopo wa usimamizi wa mitaji ya Umma, namna ambavyo Serikali inahodhi hisa na mali katika wakala za Serikali na Kampuni za biashara kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 10 cha Sheria ya Mamlaka na Majukumu ya Msajili wa Hazina pamoja na sheria nyingine za nchi.

**1.6 Njia zilizotumika**

**Mheshimiwa Spika**, Kwa mujibu wa Kanuni ya 142 ya Kanuni za Bunge, Taarifa ya Kamati inayowasilishwa Bungeni inatakiwa kubainisha njia au mbinu zilizotumiwa na Kamati kufanya kazi inayoripotiwa. Naomba kulijulisha Bunge kuwa, Katika ufuatiliaji wa mitaji ya Umma, Kamati ilitumia njia zifuatazo:;-

(i) Kufanya uchambuzi wa masharti ya Sheria inayohusika na uwekezaji uliofanyika ili kubaini uhalali wa wahusika katika uwekezaji huo;

(ii) Kupokea na kuchambua Taarifa za Msajili wa Hazina (TR) kuhusu hali ya jumla ya mitaji ya umma kwenye taasisi na mashirika ya umma au kwenye Kampuni ambazo serikali ina umiliki wa hisa au kuna maslahi ya umma. Nia ni kupata vigezo vya jumla vya uchambuzi wa taarifa za taasisi zilizohusika na uwekezaji;

(iii) Kufanya mahojiano na Bodi na menejimenti za mashirika au taasisi zinazotumia mitaji ya umma ili kuthibitisha usahihi wa hali ya mitaji ya umma katika taasisi au mashirika hayo kabla ya kutoa taarifa Bungeni; na

(iv) Kushuhudia hali ilivyo kwenye baadhi ya miradi ya uwekezaji inayoendeshwa na taasisi na mashirika yanayotumia mitaji ya umma, ili kupata uhalisia.

**1.7 Mambo ya Jumla katika sehemu ya Utangulizi**

**Mheshimiwa Spika**, Nimalizie sehemu ya kwanza kwa kusisitiza mambo makuu manne yaliyoelezwa katika sehemu hiyo ambayo ni:

(i) Kulijulisha Bunge kuhusu Hali na mwenendo wa mitaji ya umma kwa mwaka 2021/2022 ndio lengo la Taarifa hii;

(ii) Taarifa hii inatarajiwa kuwa msingi wa uamuzi wa Bunge kuhusu Hali na Mwenendo wa Uwekezaji wa mitaji ya umma kwa mwaka 2021/2022;

(iii) Katiba, Kanuni za Bunge, Sheria ya Mamlaka na Majukumu ya Msajili wa Hazina na sheria nyingine za nchi ndio msingi wa ufuatiliaji wa mitaji ya Umma;

(iv) Muundo wa Ufuatiliaji wa Mitaji ya Umma unajumuisha Serikali kuwa na mamlaka ya kutumia mitaji katika uwekezaji na Bunge kuwa na madaraka ya kuisimamia na kuishauri Serikali katika shughuli za uwekezaji kwa kuitumia Kamati hii.

**Mheshimiwa Spika**, Naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba, maelezo hayo ni muhimu katika kufuatilia mtiririko kwenye sehemu ya Pili ya Taarifa hii.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 MATOKEO YA UCHAMBUZI WA TAARIFA ZA UWEKEZAJI WA MITAJI YA UMMA

### 2.1 Maelezo ya Jumla kuhusu Uwekezaji wa Mitaji ya Umma

**Mheshimiwa Spika**, Katika uchambuzi wa taarifa za uwekezaji wa mitaji ya umma, dhana ya uwekezaji wa mitaji ya umma ilichukuliwa kuwa ni hatua za Serikali kutumia rasilimali za umma kama vile fedha, ardhi, majengo na dhamana nyingine katika taasisi na mashirika ya umma. Kwa mujibu wa Kifungu cha 2 cha Sheria ya Mamlaka na Majukumu ya Msajili wa Hazina, Sura ya 370, Mtaji wa umma unajumuisha hisa (share), hati fungani (stock debentures), dhamana ya hisa (debenture stock), dhamana ya hisa ya mikopo (loan stock), rehani ndani au nje ya bodi inayotambulika kisheria ambayo imetolewa na Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa ufafanuzi huo, uwekezaji unajumuisha ununuzi wa hisa kwenye kampuni binafsi kwa lengo la kupata gawio, kulinda thamani, kutoa huduma au kulinda maslahi ya umma kwenye kampuni zinazohusika. Kwa maana hiyo, Rasilimali zote zinazotumiwa na serikali kwenye vitega uchumi mbalimbali ndizo zinazotambulika kuwa mitaji ya umma.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Serikali imewekeza katika mashirika na taasisi za umma 247 kama inavyoonekana katika Kiambatisho Na. 01. Uchanganuzi wa uwekezaji huo unaonesha kuwa serikali imewkeza mtaji katika taasisi za aina zifuatazo:

(i) Mashirika ya Umma 35 ambayo yanafanya biashara;
(ii) Taasisi za Elimu ya Juu, Utafiti na Mafunzo stadi 74 ambazo zinatoa Huduma;
(iii) Mamlaka za Maji na Mabonde 43 ambazo zinashughulikia huduma;
(iv) Taasisi 22 za Usimamizi na Udhibiti wa Sekta ambazo zinashughulikia huduma;

(v) Taasisi 14 za Kilimo ambazo zinashughulikia huduma;
(vi) Taasisi za Afya 06 ambazo zinashughulikia huduma;
(vii) Mifuko ya Hifadhi za Jamii (4) ambayo zinashughulikia huduma;
(viii) Taasisi za Uendeshaji wa sekta 7 ambazo zinashughulikia huduma;
(ix) Taasisi 04 za Rufaa za Sheria ambazo zinashughulikia huduma; na
(x) Taasisi 44 nyinginezo ambazo pia zinashughulikia huduma.

**Mheshimiwa Spika,** Serikali pia imewekeza katika taasisi 50 ikiwa na hisa chache kama inavyoonekana katika Kiambatisho Na. 02. Kutokana na uwekezaji wa Serikali katika Taasisi na mashirika yanayotumia mtaji wa umma, mchango katika Mfuko Mkuu wa Serikali ni kama unavyoonekana katika Kiambatisho Na. 3

**2.2 Mwenendo wa Jumla wa Uwekezaji wa Mitaji ya Umma**

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi wa mwenendo wa jumla wa uwekezaji unasaidia kuelewa hali ya jumla ya mitaji ya umma na ufanisi wake. Uchambuzi huo unawezesha ulinganisho wa manufaa, tija na ufanisi kwa sekta mbalimbali za kiuchuni au huduma katika vipindi tofauti. Kutokana na umuhimu huo, Kamati ilitaka kujiridhisha katika mwenendo wa uwekezaji kwa kipindi cha miaka mitatu: 2019/2020 hadi 2021/2022.

**Mheshimiwa Spika**, Mwaka 2019/2020, thamani ya uwekezaji wa mitaji ya umma ilifikia kiasi cha **Shilingi 65,190,000,000,000** na mwaka 2020/2021 kiasi cha **Shilingi 67,950,000,000,000,** lakini mwaka 2021/2022 unaoripotiwa sasa, uwekezaji ulifikia thamani ya **Shilingi 73,360,000,000,000.** Mwenendo huo unaoneshwa katika Jedwali Na. 1

**Jedwali Na. 0:1 Mwenendo wa Uwekezaji Katika Mashirika na Taasisi za Umma**


| Mwaka | Uwekezaji | Rejesho | Asilimia ya Rejesho kwa mtaji |
|---|---|---|---|
| 2019/2020 | 65,190,000,000,000 | 753,950,000,000 | 1.16 |

| Mwaka | Uwekezaji | Rejesho | Asilimia ya Rejesho kwa mtaji |
|---|---|---|---|
| 2020/2021 | 67,950,000,000,000 | 637,660,000,000 | 0.94 |
| 2021/2022 | 73,360,000,000,000 | 850,250,000,000 | 1.16 |


**Chanzo:** Taarifa ya Utendaji ya Msajili wa Hazina kwa mwaka wa fedha 2021/2022, uk. 43

**Mheshimiwa Spika**, Mwenendo huo wa mtaji wa umma na rejesho unaonesha kuwa kutoka mwaka wa fedha 2019/2020 hadi 2021/2022, kiwango cha mtaji wa umma kilikuwa kikiongeza kila mwaka kama inavyoonekana katika Grafu Na. 01. Lakini, Mwenendo wa rejesho ulishuka mwaka 2020/2021 na kupanda tena 2021/2022 kama inavyoonekana katika Grafu Na. 02. Hali hiyo inaonesha kushuka kwa ufanisi wa mtaji wa umma kutoka mwaka 2019/2020 hadi mwaka 2020/2021. Hata hivyo, jambo zuri kwa mwenendo huo ni kuongezeka kwa ufanisi wa mtaji wa umma mwaka 2021/2022 ikilinganishwa na mwaka 2020/2021. Taswira halisi ya mwenendo huo ni kama inavyoonekana katika grafu hapa chini.

**Grafu Na. 0:1 Hali ya Mtaji wa Umma katika Trilioni kwa Kipindi cha Miaka Mitatu Mfululizo**



**Grafu Na. 0:2 Asilimia ya Rejesho kwa Mtaji kwa Kipindi cha Miaka Mitatu Mfululizo**




**Mheshimiwa Spika**, Uwekezaji wa mitaji ya umma unaosimamiwa na Msajili wa Hazina umegawanyika katika makundi mawili (2). Kundi la kwanza ni Uwekezaji kwenye mashirika ambayo Serikali inahisa zaidi ya asilimia 51. Kwa ufafanuzi zaidi kiambatisho Na. 01 kinaonesha Orodha ya Mashirika ambayo, Serikali ina hisa zaidi ya asilimia 51.

**Mheshimiwa Spika**, Kundi la pili ni uwekezaji kwenye taasisi ambazo Serikali ina hisa chache. Kundi hili linajumuisha Kampuni Kumi (10) ambazo zipo nje ya nchi, kwa rejea zaidi Kiambatisho Na. 02 kinaonesha orodha ya Kampuni ambazo Serikali ina hisa chache.

**Mheshimiwa Spika** Mchanganuo wa hali ya uwekezaji kwa kila kundi ni kama unavyofafanuliwa kwenye taarifa hii:-

**2.2.1 Uwekezaji kwenye Mashirika ambayo Serikali inahisa zaidi ya asilimia 51%**

**Mheshimiwa Spika**, hali ya uwekezaji katika mashirika ambayo serikali ina hisa zaidi ya asilimia 51 ni kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 02.

**Jedwali Na. 0:2 Uwiano wa Mtaji na Rejesho kwa Mashirika ambayo Serikali ina Hisa zaidi ya asilimia 51**

| Mwaka | Mtaji | Rejesho (returns) | Asilimia ya Rejesho kwa Mtaji |
|---|---|---|---|
| 2019/2020 | 62,970,000,000,000 | 695,880,000,000 | 0.011 |
| 2020/2021 | 65,430,000,000,000 | 477,930,000,000 | 0.007 |
| 2021/2022 | 70,800,000,000,000 | 645,910,000,000 | 0.009 |

***Chanzo:*** *Taarifa ya Utendaji ya Msajili wa Hazina kwa mwaka wa Fedha 2021/2022, na Taarifa ya Utendaji ya Msajili wa Hazina kwa mwaka wa Fedha 2020/2021*

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi wa hali hiyo unaonesha kuwa, kwa ujumla upatikanaji wa rejesho kwa mtaji unaowekezwa kwenye mashirika ambayo Serikali ina hisa zaidi ya asilimia 51 si wa kuridhisha. Kamati imebaini kuwa katika kipindi cha miaka mitatu 2019/2020 hadi 2021/2022 rejesho la uwekezaji lililopatikana ni wastani wa asilimia 0.01. Hali hii inaonesha ufanisi mdogo wa vitegauchumi katika mashirika hayo, jambo linalohitaji msisitizo zaidi wa kuirekebisha.

**2.2.2 Uwekezaji kwenye Kampuni/Taasisi ambazo Serikali ina hisa Chache**

**Mheshimiwa Spika**, Hali ya Uwekezaji kwenye Kampuni/Taasisi ambazo Serikali ina hisa chache ni kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 03.

**Jedwali Na. 0:3 Uwiano wa Mtaji na Rejesho kwa Mashirika ambapo Serikali ina Hisa chache**


| Mwaka | Mtaji | Rejesho | Asilimia ya Rejesho kwa Mtaji |
|---|---|---|---|
| 2018/2019 | 2,210,000,000,000 | 58,050,000,000 | 2.62 |
| 2019/2020 | 2,510,000,000,000 | 159,730,000,000 | 6.36 |
| 2020/2021 | 2,560,000,000,000 | 204,370,000,000 | 8 |

***Chanzo:*** *Taarifa ya Msajili wa Hazina kwa mwaka wa fedha 2021/2022.*

**Mheshimiwa Spika**, uwekezaji wa Serikali katika Taasisi ambako Serikali ina hisa chache ni sawa na asilimia 3.49 ya uwekezaji wote wa Serikali na mchango wake katika mfuko wa Serikali kwa makusanyo yasiyo ya kikodi ni asilimia 24.03 ya mapato yasiyo ya kikodi yanayotokana na uwekezaji wa Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa ujumla wastani wa rejesho katika mashirika au kampuni ambapo Serikali ina hisa chache ni asimia 5.7. Wastani huo ni mkubwa kuliko wastani wa rejesho katika mashirika ambayo Serikali ina hisa zaidi ya asilimia 51. Aidha, mwenendo wa wastani wa rejesho unaonesha kuwa ufanisi wa vitegauchumi uliongezeka kila mwaka kuanzia mwaka 2019/2020 hadi mwaka 2021/2022 kama inavyoonekana katika grafu.

**Grafu Na. 0:3 Mwenendo wa Wastani wa Rejesho katika Asilimia kwa Kipindi cha Miaka Mitatu Mfululizo**




**Mheshimiwa Spika**, kwa mwenendo huo, rejesho katika taasisi ambazo Serikali ina hisa chache limeongezeka ikilinganishwa na miaka miwili iliyopita. Hali hii inahitaji kuendelezwa kwa kuongeza usimamizi na ufuatiliaji.

### 2.2.3 Hali ya Mitaji katika Kampuni ambazo Serikali ina Hisa Chache

**Mheshimiwa Spika**, Ukweli kuhusu Uwekezaji wa Serikali katika Kampuni ambazo Serikali ina hisa chache unaonesha kwamba, aina

hii ya mitaji ya umma, inatokana na Serikali kuuza asilimia kubwa ya hisa zake ilizokuwa ikimiliki katika kampuni hizo. Lengo la Serikali kufanya hivyo ni kujiondoa kwenye biashara na kuacha sekta binafsi ijiendeshe kwa ufanisi zaidi.

**Mheshimiwa Spika,** Pamoja na lengo hilo, Kifungu cha 10 (1) cha Sheria ya Madini, Sura 123 kinaitaka Serikali kuwa na umiliki wa hisa zisizohamishika (*non-dilutable free carried interest*). Kiasi cha hisa kinatakiwa kuwa hisa zisizopungua asilimia 16 katika kampuni za madini. Serikali imewekeza katika kampuni za madini zipatazo 56, Kati ya kampuni hizo 10 zipo nje ya nchi na 46 zinaendesha shughuli zake ndani ya nchi. Nia ya masharti hayo na uwekezaji huu ni kusimamia maslahi mapana ya nchi ili kuhakikisha yanalindwa na Serikali na kuwawezesha wananchi kunufaika na rasilimali hizo.

**Mheshimiwa Spika**, Kampuni ambapo Serikali ina hisa chache zipo katika makundi 9 ambayo ni:

(i) Kampuni za uzalishaji (manufacturing);
(ii) Kampuni za uchakataji (processing) ;
(iii) Kampuni za usafirishaji (transportation) ;
(iv) Kampuni za uziduaji (extractive) ;
(v) Kampuni za nishati (oil) ;
(vi) Kampuni za mawasiliano (communication);
(vii) Kampuni za huduma za kifedha (financial services) ;
(viii) Kampuni za ujenzi (construction),
(ix) Kampuni za utalii (tourism – leisure); na
(x) Kampuni za huduma nyinginezo (other services)

**Mheshimiwa Spika**, Thamani ya mtaji wa umma katika kampuni hizo hadi tarehe 30 Juni 2022, ilikuwa ni Shilingi trilioni 2.56. Kati ya fedha hizo, kiasi cha Shilingi trilioni 1.8 sawa na asilimia 70.3 kilikuwa kimewekezwa katika kampuni ambazo zinaendesha shughuli zake ndani ya nchi na Shilingi bilioni 763.62 sawa na asilimia 29.7 kilikuwa kimewekezwa katika Kampuni ambazo zipo nje ya nchi.

**2.3 Vigezo Vilivyozingatiwa wakati wa Uchambuzi**

**Mheshimiwa Spika,** Vigezo ni jambo muhimu ili kufikia viwango vya matokeo ya uchambuzi wa Uwekezaji wa mitaji ya Umma. Vigezo ni msingi wa kupata taswira ya hali na mwenendo wa uwekezaji wa mitaji ya umma kwa namna inayowezesha uamuzi wa Bunge katika kuishauri na kuisimamia Serikali. Kifungu cha 11 (1) (a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, kimelelekeza mambo ambayo Kamati itapaswa kujiridhisha wakati wa kufuatilia uwekezaji wa mitaji ya Umma.

**Mheshimiwa Spika,** Kifungu hicho cha Nyongeza ya Nane kimebainsha wajibu wa Kamati kujiridhisha iwapo:

(i) Uwekezaji una ufanisi na tija;
(ii) Uwekezaji umezingatia taratibu; na
(iii) Uwekezaji umezingatia sheria na miongozo mujarabu ya biashara.

**Mheshimiwa Spika**, Ili kubaini ufanisi wa mitaji ya umma na uzingatiaji wa Sheria, Taratibu na miongozo mingine, Kamati ilipochambua uwekezaji unaofanywa kwenye taasisi au shirika la umma, ilitathmini mambo yafuatayo:-

(i) Kiasi cha chumo (returns) kwa njia ya gawio linalopatikana kutokana na uwekezaji wa mitaji ya umma uliofanyika;

(ii) Mwenendo wa Makusanyo ya Michango itokanayo na 15% ya mapato ghafi kutoka Taasisi na mashirika ya umma yanayostahili kuchangia kwa mujibu wa Sheria;

(iii) Kiasi cha Michango kutokana na makusanyo ya ziada na michango mingine;

(iv) Makusanyo ya TTMS; na

(v) Marejesho ya Mikopo na Riba.

**Mheshimiwa Spika,** Mambo hayo ni viashiria vya ufanisi wa uwekezaji wa mitaji ya umma katika taasisi na mashirka ya umma na kwenye kampuni ambapo Serikali ina hisa. Kwa msingi huo, uchambuzi na uchanganuzi wa mitaji ya umma ulifanyika kwa kupima mambo hayo katika taarifa za uwekezaji zilizowasilishwa kwenye Kamati.

### 2.3.1 Gawio

**Mheshimiwa Spika**, Kama inavyoeleweka, matarajio ya mmiliki wa mtaji kwenye kitegauchumi chochote ni pamoja na kupata kiasi cha fedha kutoka katika faida iliyopatikana kutokana na uwekezaji. Kiasi hicho kinachojulikana kama gawio ni miongoni mwa mambo yanayoweza kubainisha ufanisi wa uwekezaji wa mitaji ya umma.

**Mhehimiwa Spika,** Sheria ya Kampuni, Sura ya 180 pamoja na kifungu cha 15(2) (b) cha Sheria ya Msajili wa Hazina, Sura ya 370 imeweka masharti yanayoiwezesha Serikali kupata gawio. Ili kutathimini ufanisi wa uwekezaji wa mitaji ya umma, Kamati ilichambua takwimu za msajili wa Hazina kuhusu gawio lililopokewa na Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi ulionesha kuwa katika kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022, Serikali ilikusanya jumla ya **Shilingi 357,528,737,004.51** ikiwa ni gawio kutoka kwenye mashirika yanayofanya biashara. Uchambuzi zaidi umebainisha kwamba, katika kipindi cha miaka mitatu mfululizo mwenendo wa upokeaji wa gawio umekuwa ukiongezeka kutoka **shilingi 300,240,481,120.53** mwaka 2019/2020, **Shilingi 308,865,867,072.69** mwaka wa 2020/21 na **shilingi Shilingi 357,528,737,004.51** mwaka 2021/2022. Ongezeko la kutoka mwaka 2020/21 na 2021/22 sawa na ongezeko kwa asilimia 15.76

**Mheshimiwa Spika**, Kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Msajili wa Hazina alikadiria kukusanya jumla ya **Shilingi 372,882,603,001.00** kutokana na Gawio. Taarifa za uwekezaji ambazo Kamati ilizichambua zinaonesha kwamba, hadi kufikia mwezi Juni, 2022, Serikali ilikusanya kiasi cha Shilingi **357,528,737,004.51** Mwenendo wa

makadirio na makusanyo ni kama unavyoonekana kwenye jedwali Na. 04 la taarifa, lakini imefafanuliwa kwa kina kwenye Kiambatisho Na. 01 cha taarifa hii.

**Jedwali Na. 0:4 Uwiano wa Makusanyo ya Gawio kwa Makadirio**

| MWAKA | 2019/2020 | 2020/2021 | 2021/2022 |
|---|---|---|---|
| Kiasi kilichotarajiwa na Msajili wa Hazina | **397,000,608,335.30** | **408,882,000,000.00** | **372,882,603,001.00** |
| Kiasi kilichokusanywa | **300,240,481,120.53** | **308,865,867,072.69** | **357,528,737,004.51** |
| Asilimia ya lengo | **75.6** | **75.5** | **95.9** |

***Chanzo****: Zimekusanywa kutoka Taarifa ya Msajili wa Hazina.*

**Mheshimiwa Spika,** Kiasi cha gawio kilichokusanywa kilichangiwa na mashirika 25 kati ya 66 yanayopaswa kuchangia, sawa na asilimia 38 ya Mashirika yaliyotoa gawio kwa Serikali. Hali hii inaonesha kuwa ongezeko hili la gawio linachangiwa na taasisi chache zinazotumia mtaji wa umma huku taasisi nyingi zikiacha kutoa gawio. Kamati inaamini kwamba, laiti uwajibishwaji ungelitumika ili kuzihimiza taasisi zote zinazotumia mtaji wa umma na kujiendesha kibiashara katika ulipaji wa gawio, Serikali ingeliweza kupata kiasi kikubwa zaidi cha gawio jambo ambalo lingeongeza uwezo wa Serikali katika uendeshaji wa shughuli za umma.

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi zaidi umeonesha kwamba, Mashirika matatu yanayoongoza katika utoaji wa gawio kwa mwaka 2021/2022 ni Benki Kuu iliyotoa **shilingi Bilioni 200**, Airtel Tanzania iliyotoa **shilingi bilioni 104.2** na NMB iliyotoa **shilingi Bilioni 28**, kihesabu **asilimia 93** ya jumla ya gawio kutoka taasisi 25, imepatikana kutoka taasisi tatu zilizoongoza. Kwa mtazamo wa Kamati, iwapo kutakuwa na juhudi mahususi za kufuatilia na kusimamia, gawio litaongezeka. Hali hiyo itawezekana ikiwa Serikali

itatathmini changamoto zilizopo na kusimamia utatuzi wake inavyostahili.

**Mheshimiwa Spika**, Miongoni mwa hatua stahiki ni pamoja na Ofisi ya Msajili wa Hazina kuhakikisha kuwa miongozo mujarabu ya uwekezaji inazingatiwa ipasavyo. Kwa kufanya hivyo, Serikali itaweza kupata gawio kubwa kutoka kwenye vitegauchumi mbalimbali. Aidha, kisheria, ni wajibu wa kila shirika au kampuni ya biashara inayotumia mtaji wa umma kutoa gawio. Iwapo wajibu huo utatekelezwa inavyotakiwa, bila shaka, Serikali itapata ongezeko la gawio.

**2.3.2 Mchango wa Asilimia 15 ya Mapato Ghafi**

**Mheshimiwa Spika**, Miongoni mwa mapato katika Mfuko Mkuu wa Serikali (Consolidated Fund) ni michango kutoka mashirika na taasisi zinazostahili kuchangia. Sheria ya Mamlaka na Majukumu ya Msajili wa Hazina inayataka mashirika yasiyofanya biashara, yatoe asilimia 15 ya mapato ghafi (Gross Revenue) kwa mwaka na kuchangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali. Taarifa zilionesha kuwa katika kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022, Msajili wa Hazina alipanga kukusanya kiasi cha **shilingi 298,775,479,691.000** kutokana na mapato ghafi ya mashirika na taasisi za Serikali kwa mujibu wa sheria.

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa za uwekezaji ambazo Kamati ilizichambua zinaonesha kwamba, hadi kufikia mwezi Juni, 2022, Serikali ilikusanya kiasi cha **shilingi 324,025,703,627.12** kutokana na mapatao ghafi ya mashirika na taasisi za Serikali. Kiasi hicho ni sawa na **asilimia 108.5** ya lengo. Aidha, kiasi hicho cha mchango wa mapato ghafi kimeongezeka kwa asilima 69 ikilinganishwa na kiasi cha michango iliyokusanywa kwa mwaka wa fedha 2020/21.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imechambua mwenendo wa upokeaji wa mchango huu kwa kipindi cha miaka mitatu mfululizo kuanzia 2019/20 hadi 2021/22 na kubaini kwamba, kiasi hicho kimekuwa kikipanda na kushuka kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 03.


**Jedwali Na. 0:5 Uwiano wa Makusanyo ya Mchango wa Asilimia 15 ya Mapato Ghafi kwa Makadirio**

| MWAKA | 2019/2020 | 2020/2021 | 2021/2022 |
|---|---|---|---|
| Kiasi kilichotarajiwa na Msajili wa Hazina | **414,928,408,262.55** | **325,419,400,000.00** | **298,775,479,691.00** |
| Kiasi kilichokusanywa | **283,589,921,995.58** | **202,289,555,816.84** | **324,025,703,627.12** |
| Asilimia ya lengo | **68.3** | **62.2** | **108.5** |

***Chanzo****: Zimekusanywa kutoka Taarifa ya Msajili wa Hazina.*

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi wa mwenendo wa mchango wa asilimia 15 za mapato ghafi katika Mfuko Mkuu wa Serikali unaonesha taswira inayoonekana kwenye Grafu Na. 03

**Grafu Na. 0:4 Uwiano wa Makusanyo ya Mchango wa Asilimia 15 ya Mapato Ghafi kwa Makadirio katika Asilimia kwa Miaka Mitatu Mfululizo**




**Mheshimiwa Spika**, Kutokana na mchoro huo, tunaweza kuona kwamba:

(i) Kwa wastani, ufanisi wa Makusanyo ya Mchango wa asilimia 15 ya mapato ghafi ni asilimia 80 ya lengo la makusanyo, kiwango hicho ni kizuri.

(ii) Ufanisi ulishuka mwaka 2020/2021 ikilinganishwa na mwaka 2019/2020. Hata hivyo, kwa mwaka 2021/2022 ufanisi uliongezeka hadi kufikia asilimia 108.5. Hata hivyo, upangaji wa malengo ni jambo linalohitaji kutazamwa kwa kina.

**Mheshimiwa Spika,** mwenendo huu kimahesabu unaonyesha kuwa na ufanisi ingawa bado kazi ya ziada inaitajika kufanyika kwani lengo la makusanyo bado liko chini ukilinganisha na wingi wa mashirika ambayo yanaangukia chini ya kifungu hiki cha kuchangia asilimia 15 kutokana na mapato ghafi. Ni vema Serikali ikaongeza jitihada katika kusimamia mashirika yananyohusika kuhakikisha yanatekeleza kikamilifu jukumu hili la kisheria.

**2.3.3 Asilimia 70 ya Ziada na michango mingineyo**

**Mheshimiwa Spika**, Sheria ya Mamlaka na Majukumu ya Msajili wa Hazina, inazitaka taasisi au mashirika ya umma kuwasilisha asilimia 70 ya ziada baada ya kutoa gharama za uendeshaji na matumizi yanayoruhusiwa. Kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Msajili wa Hazina alipanga kukusanya kiasi cha **shilingi 93,782,962,532.00** kwa mujibu wa masharti hayo ya sheria. Hata hivyo, Taarifa za uwekezaji wa mitaji ya umma zilionesha kuwa, kiasi kilichokusanywa ni shilingi **105,017,840,361.84** sawa na **asilimia 112**.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilitathimini makusanyo ya aina hiyo kwa kipindi cha miaka mitatu mfululizo kama inavyooenekana katika Jedwali Na. 06.

**Jedwali Na. 0:6 Uwiano wa Makusanyo ya Mchango wa Asilimia 70 ya Ziada kwa Makadirio**

| MWAKA | 2019/2020 | 2020/2021 | 2021/2022 |
|---|---|---|---|
| Matarajio ya Msajili wa Hazina | 118,752,832,506.95 | 106,700,000,000.00 | 93,782,962,532.00 |
| Kiasi kilichokusanywa | 156,509,167,422.00 | 96,801,429,354.12 | 105,017,840,361.84 |
| Asilimia ya lengo | 131.8 | 90.7 | 112 |

***Chanzo**: Taarifa za Msajili wa Hazina.*

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwenendo wa sasa wa ukusanyaji unaonyesa kuna ufanisi kwani kwa kipindi chote cha miaka mitatu lengo lilifikiwa kwa asilimia 90 na zaidi. Ni rai ya Kamati kwa Serikali kuongeza usimamizi kwa mashirika ili kuhakikisha yanafanya vizuri zaidi ili kuongeza faida na mchango wa Serikali kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika**, muongozo wa Msajili wa Hazina kuhusu uchangiaji/ukusanyaji wa mapato yasiyo ya kikodi unazielekeza Taasisi ambazo hazichangii chini ya sheria ya Gawio, Mchango wa Asilimia 15 na Ziada kuchangia katika Mfuko wa Serikali chini kipengele cha Michango mingineyo. Uchambuzi wa Kamati ulibaini kukiukwa kwa muongozo huo ambapo taasisi zinazoangukia katika kipengele hiki baadhi zimekuwa zikipata faida lakini baadhi zimekuwa hazitekelezi kabisa na nyingine zimekuwa zikijipangia kiasi kidogo. Mfano Kamati ilikutana na Bodi ya Chai Tanzania ambayo kwa kipindi cha miaka mitatu mfululizo Bodi imechangia shilingi milioni 2 tu.

### 2.3.4 Rejesho la Riba na Mikopo

**Mheshimiwa Spika**, Kwa mujibu wa Sheria ya Mikopo, Misaada na dhamana, Sura 134, Taasisi na Mashirika ya Umma yanaweza kuchukua mikopo kutoka mashirika na taasisi za fedha kwa dhamana ya Serikali. Aidha, kwa mujibu wa Sheria hiyo, Serikali inaweza kuchukua mikopo katika taasisi na mashirika ya fedha na kuzikopesha taasisi na mashirika ya umma ili baadaye zirejeshwe. Ni jukumu la Msajili wa Hazina kufuatilia ulipaji wa mikopo inayostahili kulipwa.


**Mheshimiwa Spika,** Taarifa zilizowasilishwa kwenye Kamati zinaonesha kuwa hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2022, jumla ya shilingi 54,227,849,370.00 zilikuwa zimekusanywa na Ofisi ya Msajili wa Hazina ambazo ni marejesho ya mikopo. Kiasi hicho ni ongezeko la ukusanyaji ikilinganishwa na kipindi kama hicho kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ambapo zilikusanywa jumla ya shiling **19,316,737,868.50.** Mwenendo wa marejesho na mikopo kwa kipindi cha miaka mitatu mfululizo unaonekana katika jedwali Na. 07 na Grafu Na. 01.

**Jedwali Na. 0:7 Mwenendo wa Marejesho ya Riba na Mikopo**

| MWAKA | 2019/2020 | 2020/2021 | 2021/2022 |
|---|---|---|---|
| Kiasi kilichokusanywa katika bilioni | 1.46 | 19.32 | 54.23 |

***Chanzo**: Taarifa ya Utendaji ya Msajili wa Hazina kwa mwaka wa fedha 2020/2021 na Taarifa kwa mwaka 2021/2022*

**Grafu Na. 0:5 Mwenendo wa Kiasi cha Rejesho la Riba na Mikopo Kilichokusanywa katika Bilioni kwa Kipindi cha Miaka Mitatu Mfululizo**




***Chanzo**: Jedwali Na. 07*


**Mheshimiwa Spika**, Mwenendo huo unaonesha ongezeko la marejesho ya mkopo, ongezeko hilo limetokana na kuiva kwa madeni mengine ambayo yalikuwa hayajaiva. Hata hivyo, pamoja na ongezeko hilo Taasisi ya SUMA JKT imeonyesha kuzorota katika urejeshaji wa mkopo wake. Kuzorota kwa SUMA JKT kunasababishwa na fedha ilizokopeshwa zilitumika kutekeleza Mradi wa Matrekta ambayo iliyakopesha kwa wakulima lakini ulipaji wake haukuwa mzuri na kwa sasa hayalipiki kabisa. Tafsiri yake ni kuwa mtaji wa umma unaotumika katika Mradi huu haukuwa na ufanisi.

### 2.3.5 Ulinganisho wa Marejesho ya Uwekezaji kati ya (Wakala za Serikali, Mashirika na Taasisi za Umma) na Kampuni ambapo Serikali ina Hisa chache

**Mheshimiwa Spika**, ili kufahamu tofauti ya mitaji ya umma katika vitegauchumi ambapo Serikali ina umiliki wa hisa chache na kule ambapo Serikali ina hisa nyingi, Kamati ililinganisha rejesho la uwekezaji. Taarifa zilizochambuliwa na Kamati zinaonesha kuwa, kwa mwaka 2021/2022, marejesho ambayo Serikali ilipata kutokana na uwekezaji kwenye Kampuni ambapo ina hisa chache ni asilimia 8.9 ikilinganishwa na asilimia 2.2 kutokana na uwekezaji kwenye mashirika ya umma. Tofauti hiyo ni kiashiria cha kutofautiana ufanisi wa mitaji katika uwekezaji kwenye maeneo hayo mawili tofauti.

**Mheshimiwa Spika**, kwa urahisi wa kutoa taswira ya tofauti kwa miaka mitatu mfululizo, ukokotozi unaonesha tofauti hiyo kama inavyojieleza katika Grafu Na. 06.

**Grafu Na. 0:6 Ulinganisho wa Marejesho ya Uwekezaji kati ya Taasisi ambapo Serikali ina Hisa nyingi na Kwenye Taasisi ambapo Serikali ina Hisa Chache kw Miaka Mitatu Mfululizo**




***Chanzo**: Taarifa ya Utendaji ya Msajili wa Hazina kwa mwaka wa fedha 2021/2022*

**2.4 Usimamizi wa Utendaji Wa Mashirika/Taasisi**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipata fursa ya kupokea, kuchambua na kujadili taarifa za Msajili wa Hazina kuhusu utendaji wa baadhi ya Mashirika/taasisi. Kamati hutekeleza jukumu hii kwa kuzingatia Kifungu 11(1)(b) cha Kanuni za Kudumu za Bunge toleo la Februari, 2023 ambayo inaielekeza Kamati kuchambua na kujadili taarifa zinazohusu uwekezaji katika mashirika ya Umma na kampuni ambazo Serikali ina hisa. Katika kutekeleza hilo Kamati ilibaini mambo mbalimbali ya kiutendaji ambayo ni pamoja na;-

**2.4.1 Utegemezi wa Ruzuku Kutoka Serikalini**

**Mheshimiwa Spika**, Uwekezaji wa Serikali katika mashirika/taasisi unafanyika kwa lengo la kuisaidia kupata mapato zaidi na kuimarisha ustawi wa watu. Matarajio ya Serikali ni taasisi hizi zijiendeshe, zipate faida, zikuze mtaji na hatimaye ziipunguzie mzigo kwa kuacha kutegemea Ruzuku kutoka Serikalini. Taarifa za Uwekezaji zimeonesha Taasisi/mashirika mengi yameendalea na hali

ya kutegemea Ruzuku kutoka Serikalini bila kuwa na dalili ya kujikwamua kutoka kwenye utegemezi wa ruzuku.

**Mheshimiwa Spika,** inafahamika mapato ya Serikali yanapaswa kugawanywa kutekeleza majukumu mengi kwa ajili ya kuimarisha ustawi wa jamii, hivyo kwa taasisi hususani zinazojiendesha kibiashara ni vema zikasimamiwa kiukamilifu kuhakikisha zinaongeza ufanisi kwa lengo la kuongeza mapato yake na mtaji na hatimaye ziweze kujitegemea na kuipunguzia Serikali mzigo.

**2.4.2 Changamoto ya Upungufu wa Mtaji kwa baadhi ya Mashirika ya Umma;**

**Mheshimiwa Spika**, taarifa ya Uwekezaji imebainisha kuwa baadhi ya Mashirika ya Umma yanakabiliwa na upungufu wa mtaji wa kujiendesha jambo linalosababisha kupungua kwa ufanisi wa utendaji wake. Taarifa za mashirika yanayokabiliwa na Upungufu wa mtaji ziaonyesha upungufu huu umekuwa ukisababishwa na kupata hasara mfulululizo kwa kipindi kirefu na kuwa na madeni makubwa.

**Mheshimiwa Spika,** baadhi ya taasisi hizo ni pamoja na Shirika la ndege la Tanzania (ATCL), Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC), Soko la Bidhaa Tanzania (Tanzania Merchantile Exchange- TMX), Shirika la Uzalishaji mali la Jeshi la Polisi (Tanzania Police Forces Corporation Sole), Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL), Benki ya Maendeleo (TIB), Kampuni ya Mabasi yaendayo haraka (UDART) na Tanzania Railway Corparation.

**Mheshimiwa Spika,** Serikali inapaswa kufanya tathimini ya mara kwa mara kwa mashirika yake ili kubaini utendaji wake, ufanisi na tija inayopatikana. Vilevile kubaini hali halisi ya mashirika yake na kuona namna ya kuyasaidia na kuyaokoa mashirika ambayo kwa namna moja ama nyingine kama yangesaidiwa mapema ufanisi wake ungeimarika na mtaji wa umma ungekuwa salama.

**2.4.3 Malimbikizo ya madeni yanayotokana na utoaji wa huduma kwa taasisi nyingine za Serikali;**

**Mheshimiwa Spika**, Katika kupitia taarifa za utendaji kwa taasisi mbalimbali, Kamati ilibaini kuwa baadhi ya Taasisi zinakabiliwa na madeni makubwa na hazina mipango wala jitihada za makusudi za kuyalipa au kuyapunguza madeni hayo. Aidha, baadhi ya Taasisi zimekuwa zikipokea Ruzuku (OC) lakini hazina mpango wa kulipa madeni hasa madeni ya taasisi nyingine za Serikali. Jambo hili linaathiri utendaji na ufanisi wa taasisi zinazo wadai.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa taarifa za SUMA JKT ulibaini kuwa taasisi hii inakabiliwa na madeni (*recivable*) kwenye Kampuni zake Tanzu ikiwemo SUMA *Guard* ambayo inazidai taasisi nyingine za Serikali ilizipatia huduma za Ulinzi kiasi cha **shilingi 17,705,067,267.01,** Kampuni Tanzu ya Usafi ambayo inazidai taasisi nyingine za Serikali jumla ya **shilingi 107,139,660.00,** Kampuni ya Ujenzi inadai **Shilingi 14,274,004,942.70** na Kampuni ya Huduma za Bandari inadai **Shilingi 5,976,517,986.70.**

**Mheshimiwa Spika,** jumla ya kiasi cha Shilingi **38,062,729,856.41** ni mapato ya SUMA JKT ambayo imeshindwa kuyakusanya kutoka kwa taasisi nyingine za Serikali zilizopatiwa huduma kutokulipa. Kama kiasi hichio kingelipwa kingeongeza ukwasi na ufanisi wa SUMA JKT na hivyo tija ya uwekezaji kuongezeka. Ni rai ya Kamati kuwa Serikali isimamie kwa ukali kuhakikisha taasisi zinazohusika zinalipa madeni yake kwa SUMA JKT.

**Mheshimiwa Spika**, taasisi nyingine inayokumbana na changamoto hii ni DAWASA ambayo inavidai vyombo vya ulinzi na usalama jumla ya shilingi **13,928,498,841.64** inayotokana na huduma am aji waliyotumia. Vilevile, AICC inazidai taasisi mbalimbali za Serikali kiasi cha takribani **Shilingi 4,446,682,126.00** madeni yatokanayo na kukodi kumbi za mikutano pale AICC. Aidha, Taasisi zilizotumiwa na Kamati kama mfano ni taasisi chache miongoni mwa taasisi nyingi zinazokabiliwa na changamot hii.

**Mheshimiwa Spika**, Jambo hili linapunguza mapato ya taasisi zinazodai na kuathiri utendaji wake, ni vema Serikali ikazielekeza taasisi zote zinazopata huduma kutoka kwa taasisi nyingine zilipe kwa wakati.

**2.4.4. Ongezeko la Riba itokanayo na ucheleweshaji wa kuwalipa wakandarasi au wazabuni.**

**Mheshimiwa Spika**, taasisi inapotekeleza miradi ya Uwekezaji inapaswa kuzingatia mikataba inayoingia baina yake na Wakandarasi wanaotekeleza mradi. Kwa kawaida mikataba hii hubainisha taratibu zote za utekelezaji ikiwemo muda wa malipo na faini kama malipo yatacheleweshwa au wajibu mwingine wa mkandarasi. Taarifa za Utendaji wa baadhi ya Taasisi za Uwekezaji zimeonesha kuwepo kwa taasisi/mashirika ambayo yameshindwa kutekeleza masharti ya mkataba katika kufanya malipo ya wazabuni kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa ucheleweshaji huu umesababisha madeni hayo kuendelea kuongezeka baada ya kujumlishiwa riba ya ucheleweshaji hivyo huongeza mzigo kwa Serikali. Hii imethibitishwa na Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya mwaka 2021/22 ambayo imedhihirisha kuwa taasisi kumi na mbili (12) zinadaiwa jumla ya **shilingi Bilioni 63.77** iliyotokana na Riba na adhabu za kuchelewa kwa malipo mbalimbali.

Aidha, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa kwa baadhi ya taasisi zimekuwa zikisababisha ucheweshaji wa makusudi hasa kwenye miradi ya ufadhili (*donor funded projects*).

**2.4.5 Utendaji wa mashirika usiozingatia vigezo vilivyowekwa na Msajili wa Hazina**

**Mheshimiwa Spika**, Kwa madhumuni ya ufanisi katika uwekezaji wa mitaji ya umma, Kifungu cha 10(2)(d) cha Sheria ya Msajili wa Hazina (Madaraka na Majukumu), Sura 370, kinamtaka Msajili wa Hazina kuzipa Bodi za Wakurugenzi wa mashirika, malengo ya kifedha na

vigezo vya utendaji viinavyopaswa kuiongoza bodi katika uendeshaji.

Taarifa mbalimbali za uwekezaji zilizowasilishwa kwenye Kamati zinaonesha kuwepo kwa shida ya baadhi ya Taasisi / mashirika ya Umma kujiendesha kwa kutokuzingatia vigezo. Hali hiyo, ni mashaka na wasiwasi kwa ufanisi wa mitaji ya umma inayowekezwa na Serikali. Baadhi ya taasisi zimekutwa hazina uwiano mzuri wa mapato na Matumizi jambo linaloathiri mtaji wa taasisi. Uwiano wa madeni ya muda mfupi kulinganisha na mapato ya muda mfupi jambo linaloathiri ulipaji wa madeni haya. Pia, kasi ndogo ya ukusanyaji wa mapato jambo linaloathiri ukwasi wa taasisi.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati kwa taarifa zilizowasilishwa na Msajili wa Hazina kwa kipindi Kamati cha mwezi Agosti na Oktoba zilibaini changamoto hii kwa Taasisi kadhaa ikiwemo Bodi ya Chai (TTB), Mfuko wa Pembejeo wa Taifa (AGTIF), Mfuko wa Bima ya Afya wa Taifa (NHIF), Wakala wa Manunuzi wa Serikali GPSA, na hizi ni kwa uchache tu.

**2.4.6 Utendaji wa Wakala wa Manunuzi wa Serikali GPSA**
**Mheshimiwa Spika**, taarifa za uwekezaji za Wakala wa Manunuzi wa Serikali (*GPSA*) zimebainisha kuwa GPSA imekuwa na utaratibu wa kuchelewesha utoaji wa huduma zake ambapo baadhi ya taasisi za Serikali na Halmashauri mbalimbali zimekuwa zikiwasilisha maombi yake lakini GPDA huchukua muda mrefu hadi zaidi ya miezi sita kabla ya kufikisha huduma.
Aidha, Uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa gharama inayotozwa na GPSA katika ununuzi wa magari ya Serikali ni kubwa ukilinganisha na bei halisi ya magari inayotozwa na soko. Ufafanuzi wa GPSA kuhusiana na jambo hili ni kuwa GPSA hulazimika kuagiza na kununua magari kwa Wakala wa Toyota Japan badala ya kununua kwa moja kwa moja kwa mzalishaji. Wakala huyu ambae ni Toyota Tanzania hutoza bei kubwa kuliko bei ya Soko.

**Mheshimiwa Spika**, GPSA ilieleza kuwa huu ndio utaratibu wa kibiashara wa Toyota Japan ambapo yeye hafanyi biashara moja

kwa moja na wateja bali hupitia kwa mawakala wake. Aidha GPSA waliripoti kuwa Serikali kupitia wizara ya Fedha wanafanya mazungumzo na Toyota Tanzania kuangalia namna ya kutatua changamoto hii. Ni ushauri wa Kamati kuwa Serikali iharakishe mazungumzo haya na kupata ufumbuzi wa tatizo hili kwani limeendelea kuongeza mzigo kwa Serikali.

**2.4.7 Kuchelewa kukamilika kwa miradi jambo linalosababisha kuongezeka gharama za utekelezaji**

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa kuchambua taarifa za mashirika zilizowasilishwa mbele ya Kamati ilibainika kuwa kuna baadhi ya taasisi na mashirika ya umma yamekuwa na kasi ndogo katika kutekeleza miradi yake ya uwekezaji jambo linalosababisha kuchelewa kukamilika kwa miradi hiyo na hivyo kulazimika kuongeza muda wa utekelzaji. Jambo hili lina athari kwa namna mbili, moja ni kuongezeka kwa gharama za utekelezaji wa mradi kwani hulazimika kulipa riba kwa wakandarasi, Athari ya pili ni kuwa husababisha kuchelewa kuanza kunufaika na kupata chumo litokanalo na uwekezaji huo.

**Mheshimiwa Spika,** changamoto hii ilibainika kwa taasisi kadhaa ikiwemo NSSF kwa kampuni yake Tanzu ya Mkulazi ambapo mradi wa Kiwanda cha Sukari Mkulazi utekelezaji wake ulitarajia kukamilika Disemba 2022. Mradi huu haujakamilika kwa wakati jambo lililosababisha kufanyika kwa mapitio mapya ya gharama za utekelezaji na kubainika kuwa kuna uhitaji wa ongezeko la dola za Marekani **milioni 32.64**, ambalo ni ongezeko la asilimia 146. Aidha, Kuchelewa kukamilika kwa kiwanda kunasababisha miwa iliyokuwa tayari iharibike na kuongezeka kwa gharama za utunzaji miwa iliyopita muda wa kuvuna na hivyo kusababisha hasara ya Shiling **Bilioni 2.3**.

Vilevile, Kamati ilibaini kuwa Wakala wa Maji Vijijini (RUWASA) inajitahidi kubuni miradi mingi lakini miradi hii haikamiliki kwa wakati kutokana na kukumbana na changamoto ya upelekaji wa fedha kutoka Serikalini kwenda RUWASA kutokufanyika kwa wakati. Jambo hili husababisha ucheleweshaji unaosababisha riba, pia linaleta

wasiwasi juu ya ukamilifu wa Azma ya Serikali iliyopo madarakani ya kufanikisha upatikanaji wa maji safi maeneo ya vijijini kwa zaidi ya asilimia 85 kufikia 2025 (kama inavyoelekezwa katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM 2020/2025).

**2.4.8 Mpango wa Serikali wa Kupitia Mashirika**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imejulishwa kuwa msajili wa Hazina anafanya mapitio ya taasisi zote kwa lengo la kuona ufanisi wake, kufuta yale yasiyo na tija na kuunganisha baadhi ya mashirika ambayo majukumu yake yanashabihiana. Kamati inatambua na kupongeza juhudi hizi kwani zinalenga kuleta ufanisi na kuongeza tija ya uwekezaji.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inatoa angalizo katika kipengele cha kuunganisha Mashirika yanayoshabihiana Serikali iweke umakini kwa lengo la kutohamisha mzigo wa taasisi moja kwenda kwa taasisi nyingine kama ilivyofanyika wakati wa kubadilisha DAWASCO kuwa DAWASA, kuunganisha SELF Microfinance na UTT Microfinance pamoja na kuunganisha TPB na TIB Coorporate kuunda TCB.

**2.4.9 Utendaji wa Mfuko wa Bima ya Afya (NHIF)**

**Mheshimiwa Spika,** taarifa ya Msajili wa Hazina inaonyesha Mfuko una hali mbaya kifedha na mtaji wa Mfuko umeendelea kushuka kila mwaka kwani unatafunwa na ongezeko la madeni yanayodaiwa na watoa huduma.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa madeni ya Mfuko kwa kiasi kikubwa yanachangiwa na udhaifu wa Mfumo wa udhibiti wa utoaji wa huduma, mfano kadi moja inaweza kuhudumia mteja zaidi ya mmoja. Mfuko ulitoa taarifa kwa Kamati kuwa kuna uwekezaji umefanyika katika kuimarisha Mfumo wa Utambuzi wa Wanachama na majaribio yamekwishafanyika kwa baadhi ya maeneo ikiwemo Arusha.

**Mheshimiwa Spika**, mwaka wa fedha 2021/22 mfuko umepata nakisi ya **shilingi bilioni 189.65,** ni maoni ya Kamati kuwa Serikali ifuatilie kwa ukaribu utendaji wa Mfumo kuhakikisha unaimarisha mifumo ya

utambuzi wa wagonjwa kwa lengo la kuondoa udanganyifu na kutathimini utendaji wa Mfuko na kuboresha penye mapungufu. Jambo hili litaongeza ukwasi wa mfuko, kuimarisha utendaji wa mfuko na kuleta tija iliyokusudiwa ikizingatiwa kwamba Shirika hili ndilo linatazamiwa kutekeleza jukumu la kusimamia Bima ya Afya kwa wote pindi jambo hili litakapopitishwa.

**2.4.10 Athari za mikopo chechefu**

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa kuchambua taarifa za uwekezaji wa baadhi ya taasisi Kamati ilibaini kuwa kuna baadhi ya taasisi zinakabiliwa na changamoto ya kuwa na kiasi kikubwa cha tengo chechefu jambo linaloathiri mizania ya vitabu vya taasisi. Changamoto hii ilibainika kwa Mfuko wa Pembejeo wa Taifa AGITF na SUMA JKT.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/22 Mfuko wa Pembejeo wa Taifa ulikuwa unadai madeni (receivable) jumla ya **shilingi 26,422,092,100.55** yanayotokana na mikopo ya pembejeo iliyotolewa kwa wakulima ambapo kati ya deni hili **Shilingi 21,375,045,194.81** ni tengo la madeni chechefu kwa maana ni madeni hayajaweza kulipwa na yamechukua muda mrefu sasa, kiasi cha mikopo chechefu kwa AGITF ni sawa na **asilimia 81** ya madeni ya Mfuko kinyume na takwa la kisheria linalohitaji tengo la mikopo chechefu kuwa chini ya **asilima 5**.

**Mheshimiwa Spika,** SUMA JKT pia inakabiliwa na kiasi kikubwa cha tengo la madeni chechefu katika vitabu vyake ambalo ni takribani **Shilingi 50,320,000,000.00** lililotokana na mradi wa kukopesha Matrekta. Msingi wa deni hili ni Serikali iliipatia SUMA JKT mkopo wa Matrekta na zana zake vyenye thamani ya **Shilingi bilioni 61**, Deni hili limekuwa chechefu baada ya SUMA JKT kushindwa kukusanya marejesho kutoka kwa wakulima takribani Shilingi **38,778,866,000.000** lakini pia baadhi ya zana zilizobaki ambazo kutokana na mabadiliko ya teknolojia haziuziki, changamoto hii inasababisha SUMA JKT kushindwa kulipa deni hili la Serikali. Ni rai ya Kamati kuwa Serikali ifanye tathimini na kuangalia namna ya kulifuta deni hili kwa SUMA

JKT kwani kiuhalisia halilipiki na linaathiri mizania ya vitabu vya Shirika.

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa za uwekezaji za baadhi ya mashirika inaonyesha uwepo wa haja kwa Serikali kutathimini madeni chechefu ya baadhi ya Mashirika na kuyabadilisha kuwa mtaji (debt to equity convention) kwani vitabu vya hesabu za baadhi ya mashirika vinaathiriwa na uwepo wa madeni hayo. Jambo hili ni hatari kwa misingi ya kibiashara na utendaji wa shirika kwa ujumla. Mfano vitabu vya hesabu vya DAWASA vinaathiriwa na deni la **shilingi Bilioni 47** ilililoliritihi wakati DAWASCO ilipokuwa inabadilishwa kuwa DAWASA, Mfuko wa SELF Microfinance ina deni la **shilingi bilioni 6.03** ilizozirithi wakati wa kuunganishwa na UTT Microfinance, ipo haja ya madeni haya kubadilishwa kuwa mtaji ili kuweka sawa Mizania ya vitabu vya taasisi hizi.

**2.4.11 Madeni ya Wizara ya Afya na Vituo vya Afya kwa Bohari ya Madawa (MSD)**

**Mheshimiwa Spika**, MSD imekuwa ikihudumia taasisi za Serikali ikiwemo Wizara ya Afya na Vituo vya Afya kwa kuwauzia dawa na vifaa tiba mbalimbali. MSD inakabiliwa na madeni (receivables) ambayo kwa kiasi kikubwa zinapunguza ufanisi wa Bohari. Taarifa ya CAG ya mwaka wa fedha 2021/2022 imebainisha kuwa katika deni la **shilingi bilioni 375.1**ambalo MSD inadai**, shilingi bilioni 255.66** ni deni inalozidai taasisi za Serikali. Endapo Serikali ingelipa deni hili fedha hizo zingeongeza ukwasi wa MSD na kuongeza ufanisi wake wa kutoa huduma, ni vema Serikali ikalizingatia hili kwa lengo la kuimarisha MSD.

**Mheshimiwa Spika**, MSD pia imejenga viwanda vya kuzalisha madawa vya Idofi vilivyopo Makambako - Njombe na imefanya manunuzi ya mashine za kuzalisha dawa aina ya vidonge na syrup lakini uzalishaji haujaanza hivyo tija ya uwekezaji inakosekana. Uwekezaji uliofanyika kwa kiwanda hiki ni mkubwa takribani **Shilingi 6,339,814,023.15** zimetumika kununua mitambo ambayo ilitarajiwa kuzalisha dawa hizo. Fedha iliyowekezwa kwenye ununuzi wa mitambo ni kiasi kikubwa na mpaka sasa haijaleta tija yoyote, ni

vema MSD ikafanya mapitio (review) ya mpango wa ujenzi wa viwanda vile, kisha mpango mkakati kuviendesha ukaandaliwa ili vianze kufanya kazi kwani fedha za Serikali zimekwisha tumika.

**Mheshimiwa Spika**, changamoto nyingine ya MSD ni kuwa ilipata hoja ya ukaguzi ya kuruhusu kupokea dawa ambazo uhai wake (life sparn) umefikia asilimia 80 kwa maana kuwa zinakaribia kuharibika. Ni vema MSD ihakikishe dawa zinazopokelewa hata kama ni za msaada ziwe ndani ya muda unaokubalika kwani taarifa ya GAG ya mwaka 2021/2022 imeonyesha kuwa Maghala ya MSD yalikuwa na bidhaa zilizoisha muda wake zenye thamani ya shilingi bilioni 28.24, dawa bidhaa hizi mwisho wake ni kuteketezwa na fedha za Serikali (mtaji wa umma) ndio zinagharimia zoezi la uteketezaji.

**2.4.12 Athari kwa Sekta ya Bima**

**Mheshimiwa Spika**, Sekta ya Bima ni miongoni mwa maeneo ambayo Mtaji wa umma umewekezwa na unatumika kuisimamia sekta hiyo. Kwa kawaida, katika taasisi, kampuni na mashirika ya bima nchini na duniani kote mwaka wake wa kiuendeshaji ni mwaka wa kawaida wa kalenda (Januari – Disemba). Lakini NIC inalazimika kufuata mwongozo wa Serikali wa kufunga hesabu kwa kuzingatia mwaka wa fedha wa Serikali (Julai – Juni), jambo hili lina athiri tathmini ya mara kwa mara ya sekta ya Bima inayofanywa na NIC ambao pia hulazimika kufunga Hesabu zake kwa kuzingatia mwaka wa fedha wa Serikali, yani Julai kila mwaka – Juni ya mwaka unaofuata.

**Mheshimiwa Spika**, mwongozo huu unasababisha NIC kujiendesha kinyume na Soko la bima nchini na duniani kwa ujumla kwa maana kuwa tathimini zao hufanyika kwa kutumia hesabu ambazo hazijakaguliwa, lakini pia inasababisha taasisi hii kushindwa kukidhi vigezo vya kuingia mkataba wa bima mtawanyo (*re-insurance*) na makampuni mengine kwasababu mikataba yote ya bima mtawanyo huzingatia mwaka wa soko la bima Jan – Dec. NIC inalazimika kuweka mipango yake ya *re-insuarance* kwa vipindi viwili tofauti jambo ambalo ni changamoto kwani ndani ya mwaka

mmoja biashara inaweza kwenda tofauti lakini kama ingeingia ya mwaka mzima athari isingekuwa kubwa.

**Mheshimiwa Spika**, jambo hili linapunguza ufanisi wa Shirika kupunguza ufanisi wa mitaji ya umma uliowekwa NIC. Ni vema taasisi zinazofanya biashara zikapewa uhuru wa kujiendesha na Serikali ikachukua nafasi yake ya kusimamia na kuhakikisha tija inapatikana.

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 MAONI NA MAPENDEKEZO

### 3.1 Maoni

**Mheshimiwa Spika**, Katika sehemu hii ya Mwisho nilihakikishie Bunge lako Tukufu kuwa, Taarifa ni matokeo ya kuzingatia masharti ya Kanuni za Bunge kuhusu majukumu ya Kamati, msingi wa kazi za Kamati pamoja na Masharti kuhusu maudhui na muundo wa Taarifa. Kwa ujumla mambo makuu yanayojitokeza katika Taarifa hii ni:

(i) Baadhi ya Taasisi zinazotumia Mtaji wa Umma hazichangii kabisa na nyingine zinachangia kidogo kuliko inavyostahili katika Mfuko Mkuu wa Serikali;

(ii) Kuna Taasisi za Uwekezaji zinazoendelea kuwa na utegemezi mkubwa wa ruzuku kutoka Serikalini jambo linaloongeza mzigo kwa Seriakali;

(iii) Vigezo vya Utendaji vinavyopangwa na Msajili wa Hazina havizingatiwi na taasisi nyingi zinazotumia mtaji wa Umma;

(iv) Kuna ongezeko la riba kwa taasisi za uwekezaji kutokana na kuchelewesha malipo kwa wakandarasi na watoa huduma wengine;

(v) Masharti ya Ufungaji wa Hesabu yanayolitaka Shirika la Bima la Taifa kufunga Hesabu kwa mwaka wa fedha wa Serikali ili hali taasisi za bima hufunga hesabu kwa kufuata kalenda ya

kawaida ya mwaka jambo linaloisababishia ugumu wa kujipanga kiushindani.

(vi) Baadhi ya taasisi zinazotumia mtaji wa umma katika uwekezaji hukabiliwa na mikopo chechefu, jambo linalozisababishia uwezo mdogo wa kujiendesha na kushindana katika uwekezaji;

(vii) Nia ya kuunganisha mashirika yenye majukumu yanayofanana bila kufanya tathmini ya kina inavyoweza kusababisha taasisi zisizo na changmoto hizo kuathirika;

(viii) Kuwepo kwa Taasisi zinazotumia Mtaji wa Umma ambazo zinajiendesha kwa kuzorota pasipo kuwa na mkakati maalumu wa mageuzi (*Turnaround strategy*);

(ix) Kuwepo kwa Taasisi zenye fursa ya kufanya vizuri zaidi kwa kutumia mtaji wa umma zilizonazo lakini hazitumii ipasavyo fursa zilizonazo kiuwekezaji;

(x) Kutokukamilika kwa miradi ya uwekezaji kwa wakati jambo linaloongeza gharama ya miradi ya uwekezaji na kuchelewesha upatikanaji wa matokeo na tija ya mitaji ya umma;

(xi) Kukosekana kwa Udhibiti madhubuti wa upotevu katika maji yaliyotibiwa, kunasababisha hasara kwa serikali;

(xii) Ufanisi mdogo wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya unaotokana na vifurushi kutokuendana na gharama halisi, Watoa huduma kuwasilisha madai yanayozidi huduma iliyotolewa na ukosefu wa Mifumo mdhubuti ya Udhibiti;

(xiii) Changamoto ya kutokuwa na mitaji ya kutosha kwa baadhi ya Taasisi za uwekezaji kutokana na kutokuwepo kwa mfuko wa uwekezaji; na

(xiv) Dosari zilizopo katika Sheria ya Msajili wa Hazina (Madaraka na Majukumu) Sura ya 370, zinasababisha mianya kwa baadhi ya

Bodi kutokuzingatia vigezo na kuongeza ufanisi wa mitaji ya umma.

**Mheshimiwa Spika**, kwa msingi wa mambo hayo, Kamati inatoa mapendekezo ambayo iwapo Bunge litaridhia yanaweza kuatatua changamoto zilizopo katika uwekezaji wa mitaji ya Umma.

**3.2 Mapendekezo**

**3.2.1 Mchango katika Mfuko wa Serikali**

**KWA KUWA**, Sheria mbalimbali zikiwemo Sheria ya Msajili wa Hazina, Sura 370, Sheria ya Kampuni, Sura ya 180, Sheria ya Fedha za Umma na Sura ya 348 na Sheria ya Bajeti, Sura ya 439 zimeweka masharti yanayozitaka taasisi zinazotumia mtaji wa umma kuchangia katika Mfuko mkuu wa Serikali, Lakini zipo taasisi ambazo hazichangii au zinachangia kidogo kuliko inavyostahili kutokana na kutokuwepo kwa mfumo na utaratibu wa kisheria unaowabana kuhusu kigezo cha uchangiaji.

**NA KWA KUWA**, kukosekana kwa mfumo wa kisheria kuhusu vigezo vya uchangiaji kumechangia baadhi ya taasisi zinazotumia mtaji wa umma kuacha kuchangia au kuchangia kiasi kidogo, jambo linaloathiri lengo la uwekezaji,

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba:

(a) Sheria ya Msajili wa Hazina (Madaraka na Majukumu), Sura ya 370, irekebishwe ili kuweka bayana utaratibu na mfumo wa taasisi zote zinazopata faida ziwajibike kisheria kuchangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali; na

(b) Serikali iongeze msisitizo kwa taasisi zinazotumia mtaji wa umma ili zitekeleze wajibu wa kuchangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali, na pale ambapo itatokea kutokuzingatiwa kwa wajibu huo, adhabu na hatua nyingine stahiki zitumike kukazia utekelezaji.

**3.2.2 Utegemezi wa Ruzuku kutoka Serikalini**

**KWA KUWA**, zipo taasisi zinazotumia mtaji wa umma ambazo zinapata faida ya kutosha, lakini zinaendelea kupata ruzuku ya

Serikali, ili hali ruzuku hiyo ingeliweza kuwekezwa katika vitegauchumi vingine na kuongeza wigo wa fursa za uwekezaji,

**NA KWA KUWA**, Kuendelea kuzipatia ruzuku taasisi hizo zisizoonesha dalili ya kujikwamua kutoka kwenye utegemezi wa ruzuku hata kama zinapata faida ni kubana fursa zilizopo za kutumia mtaji wa umma katika maeneo mengine ya uwekezaji,

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba:

(a) Serikali iweke utaratibu wa kufanya tathimini ya mara kwa mara kwa taasisi za umma ili kubaini taasisi zinazohitaji ruzuku na zisizohitaji ruzuku; na

(b) Taasisi za umma zinazotumia mtaji wa umma na ambazo zinazapatiwa ruzuku ya Serikali, zikifikia kiwango cha kujitegemea zipewe muda mahususi wa kuanza kujitegema ili kuipunguzia Serikali mzigo wa wategemezi wa ruzuku.

### 3.2.3 Uzingatiaji wa Vigezo vya Utendaji Vilivyopangwa na Msajili wa Hazina

**KWA KUWA,** Kifungu cha 10(2)(d) cha Sheria ya Msajili wa Hazina (Madaraka na Majukumu), Sura 370, kinampa Msajili wa Hazina mamlaka ya kuzipatia Bodi za Wakurugenzi wa mashirika, malengo ya kifedha na vigezo vya utendaji lakini hakuna mfumo wa kuziwajibisha bodi zinazoshindwa kuzingatia vigezo na kujielekeza kwenye malengo,

**NA KWA KUWA**, Kutokuzingatiwa kwa vigezo na malengo kutokana na kukosekana kwa mfumo wa uwajibishaji, kunasababisha mashaka na wasiwasi kuhusu ufanisi wa mitaji ya umma,

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba,

(a) Yafanyike Marekebisho ya Sheria ya Msajili wa Hazina (Madaraka na Mamlaka), Sura ya 370, ili:-
    (i) Kuongeza nguvu kwa Msajili wa Hazina kwa lengo la kumwezesha kufuatilia na kuziwajibisha bodi zinazoshindwa

kuzingatia vigezo na kujielekeza kwenye malengo yaliyowekwa.

(ii) Kuweka utaratibu wa kupata bodi na wajumbe wa bodi kwa njia ya ushindani.

(b) Msajili wa Hazina atengeneze utaratibu wa kufanya mapitio *(review)* ya vigezo vinavyotolewa kwa Bodi za Wakurugenzi pamoja na menejimenti za Taasisi zinazotumia mtaji wa umma ili kuhakikisha kuwa, vinaendana na hali (*status*) ya taasisi au shirika.

**3.2.4 Ongezeko la Riba itokanayo na ucheleweshaji wa kulipa wakandarasi au wazabuni**

**KWA KUWA**, Imebainika kuwepo kwa Taasisi za Serikali zinazotumia mtaji wa umma, ambazo zinajitwika mzigo wa riba kutokana na kutokutekeleza masharti ya mikataba baina yao na wakandarasi au wazabuni,

**NA KWA KUWA**, Mzigo wa riba kwa taasisi za serikali zinazotumia mtaji wa umma, unaathiri ukwasi (*liquidity*) na ufanisi katika vitegauchumi vya umma, jambo linaloathiri uwezo wa uendeshaji katika uwekezaji;

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba,

(a) Serikali iongeze usimamizi kwa taasisi zake za uwekezaji zinazotekeleza miradi ili zizingatie masharti ya mikataba baina yao na wakandarasi au watoa huduma kwa lengo la kuepuka riba za ucheleweshaji; na

(b) Uandaliwe utaratibu wa kuziwajibisha bodi za wakurugenzi na menejimenti za taasisi zinazoshindwa kuzingatia masharti ya mikataba na kusababisha hasara katika uwekezaji.

**3.2.5 Athari kwa Sekta ya Bima (NIC)**

**KWA KUWA**, Mashirika au Kampuni za biashara katika tasnia ya Bima zinashindana kimataifa na kwamba, zinatumia utaratibu wa

kujipanga kihesabu kwa kutumia mwaka wa kawaida wa Kalenda ya mwaka, lakini Shirika la Bima la Taifa (NIC), linajipanga kihesabu kwa kutumia mwaka wa fedha wa serikali,

**NA KWA KUWA**, Utaratibu wa NIC kufunga hesabu kwa kuzingatia mwaka wa fedha wa Serikali (Julai – Juni), kutokana na maelekezo ya Serikali, unaathiri tathmini ya mara kwa mara ya sekta ya Bima inayofanyiwa kazi na NIC; na

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba, Serikali itoe fursa kwa Taasisi za umma zinazofanya biashara za kimataifa kuweza kufuata *best practice* za soko kwa lengo la kuwawezesha kushiriki kikamilifu na kuweza kushindana kwa lengo la kuwaongezea ufanisi na tija ya uwekezaji kuweza kupatikana.

**3.2.6 Athari za Mikopo Chechefu**

**KWA KUWA**, Taarifa za uwekezaji zimeonesha kuwepo kwa taasisi zinazotumia mtaji wa umma, zenye kiasi kikubwa cha mikopo chechefu (*non-performing loans* – NPLs), zikiwemo Mfuko wa Pembejeo wa Taifa na SUMA JKT,

**NA KWA KUWA**, Mikopo chechefu (*non-performing loans*), kwenye vitabu vya taasisi yoyote inaathiri mizania na kupunguza ukwasi (liquidity) wa taasisi, jambo linaloathiri uendeshaji na ufanisi wa uwekezaji,

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba, Serikali ihakikishe kuwa:

(a) Taasisi zote za fedha na ukopeshaji ziwe na sera nzuri ya mikopo;

(b) Mikataba kati ya taasisi za fedha na wakopaji inaandaliwa kwa umakini ili kuboresha na kuondoa mianya inayosababisha mikopo chechefu;

(c) Taasisi zinazotumia mitaji ya umma zinaweka Mifumo Madhubuti ya TEHAMA itakayotumika kuchakata maombi na

kuweka utaratibu mzuri wa kudhibiti na kuimarisha utoaji na usimamizi na ukusanyaji wa mikopo;

(d) uchambuzi unafanyika ili kuainisha umri wa mikopo chechefu na kuiondoa kwenye vitabu vya taasisi bila kuathiri ulipaji wa mikopo inayolipika;

(e) Hatua stahiki za kinidhamu zichukuliwe dhidi ya waliohusika au kusababisha mikopo kuwa katika hali ya mikopo chechefu.

**3.2.7 Tathimini ya utendaji wa Mashirika**

**KWA KUWA**, Serikali ina mpango wa kuunganisha baadhi ya Mashirika ya Umma ambayo yenye majukumu yanayoshabihiana na yanayoweza kuunganika, ili kuongeza ufanisi na tija pamoja na kupunguza mzigo wa utegemezi wa Ruzuku kutoka Serikalini,

**NA KWA KUWA,** zoezi hilo linaweza lisiwe na matokeo bora iwapo tathmini ya hali ya fedha kwa mashirika hayo haitafanyika vizuri na kama hakutakuwa na utaratibu mzuri wa kushughulikia mikopo chachefu itakayoachwa na mashirika hayo baada ya kuunganishwa,

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba,

(a) Serikali ifanye tathimini ya taasisi zinazotagemewa kuunganishwa na kubaini hali ya Kifedha (*financial position*) yake kabla ya kuziunganisha;

(b) Madeni chechefu yote yalipwe au yafutwe kwenye vitabu vya mashirika au taasisi zinazounganishwa kwa lengo la kuepuka mzigo wa madeni kuhamishiwa kwa taasisi mpya na kuhamishia tatizo la mizania kwa taasisi mpya.

(c) Kiundwe chombo maalumu ambacho kitasimamia mikopo chechefu ili kutoa nafasi ya Taasisi mpya kuanza na kumbukumbu safi za Hesabu.

### 3.2.8 Mkakati wa Uhuishaji wa Mashirika yanayojiendesha Kibiashara (Turnaround Strategy)

**KWA KUWA**, Taarifa za uwekezaji zinaonesha kuwepo kwa taasisi za serikali zinazojiendesha kibishara na ambazo zinasimimiwa na Msajili wa Hazina, lakini zinazorota katika uwekezaji,

**NA KWA KUWA**,
(a) Kozorota katika uwekezaji kwa taasisi za serikali zinazojiendesha kibishara ni jambo linalosababisha ziendelee kuwa mzigo kwa serikali,

(b) Kuna mfano wa Shirika kama STAMICO ambayo iliwahi kuwa inazorota ikiwa na utegemezi wa Ruzuku kwa 89%, iliposimamiwa na kuandaa Mkakati wa Mageuzi, imeanza kufanya vizuri kiasi cha kuchangia kwenye Mfuko wa Serikali na imeanza pia kupunguza utegemezi hadi kufikia 9% ambayo ni ruzuku ya mishahara tu.

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba, Serikali kupitia Msajili wa Hazina izisaidie taasisi zinazozorota kwa kuandaa mkakati wa mageuzi (Turnaround Strategy) na kuzisimamia kwa karibu ili kuhakikisha zinautekeleza mkakati huo.

### 3.2.9 Taasisi kubuni na Kuongeza Vyanzo Mbadala vya Mapato

**KWA KUWA**, Zipo taasisi au mashirika yanayojiendesha kibiashara ambayo yanayo fursa nzuri ya kuutumia mtaji wa umma na kupata chumo kubwa lakini zimeridhika kuendelea kuwa na utegemezi kwa ruzuku ya Serikali,

**NA KWA KUWA**, kuendelea kwa taasisi au mashirika yenye fursa nzuri kuwa na dosari ya kutegemea ruzuku hata kama taasisi hizo zina fursa ya kufanya vizuri na kuondokana na utegemezi ni kinyume na matarajio ya Bunge na Serikali katika ufanisi wa mitaji ya umma,

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba, Serikali ihakikishe kuwa inazisimamia Bodi zote zinazojiendesha kibiashara ili zinafanye tathimini ya na kubaini vyanzo vyote mbadala vya mapato na fursa zaidi ya uwekezaji kwa lengo la kuongeza ukwasi wa taasisi na faida ya Serikali.

**3.2.10 Kutokukamilika kwa Miradi ya Uwekezaji kwa Wakati**

**KWA KUWA**, Utekelezaji wa miradi katika Taasisi zinazotumia Mtaji wa Umma unalenga kuongeza faida katika uwekezaji, lakini zipo Taasisi za umma ambazo zinatekeleza miradi ya uwekezaji kwa kuchelewa kuikamilisha na kusababisha ongezeko la gharama za miradi;

**NA KWA KUWA**, Gharama kubwa inayosababishwa na kuchelewesha ukamilikaji wa miradi zinaathiri mtaji kutokana na Fedha za Serikali kutumika bila kupata chumo kwa wakati,

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba, Serikali kupitia Msajili wa Hazina iongeze usimamizi wa karibu kwa taasisi zinazotekeleza Miradi ili zikamilishe miradi ndani ya muda wa mkataba bila gharama za ziada.

**3.2.11 Udhibiti wa Upotevu wa maji yaliyotibiwa (Mamlaka za Maji)**

**KWA KUWA**, mamlaka za maji hutumia mitaji wa umma katika kutibu maji hivyo zinawajibika kudhibiti upotevu wa Maji yaliyotibiwa hadi kufikia sawa au chini ya asilimia 25;

**NA KWA KUWA,** taarifa za uwekezaji za Mamlaka za Maji zimebainisha kuwepo kwa tatizo katika udhibiti wa maji yaliyotibiwa kwa kiasi cha kusababisha hasara ya jumla ya **shilingi Bilioni 162.14**;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba, Serikali ihakikishe;

(a) Mamlaka za maji kwa kushirikiana na Serikali za Mitaa na Serikali za Vijiji iweke mfumo madhubuti wa utoaji wa taarifa kuhusu uharibifu wa miundombinu ya maji pale unapotokea; na

(b) Ukaguzi unafanyika mara kwa mara wa miundombinu ya maji na kuboresha maeneo chakavu.

**3.2.12 Kuimarisha Mfuko wa Taifa Bima ya Afya wa Taifa NHIF**

**KWA KUWA**, Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya unatumia mtaji wa Umma unakabiliwa na mzigo wa gharama kubwa za uendeshaji kutokana na:

(a) Baadhi ya watoa huduma kuwasilisha madai yasiyo na uhalisia kutokana na Mfuko huo kukosa mifumo madhubuti ya kudhibiti uhalisia wa madai;

(b) Baadhi ya vifurushi vya Bima ya Afya kutoendana na gharama halisi; na

(c) Mifumo ya TEHAMA isiyokuwa madhubuti kwa ajili ya udhibiti wa madai na wapokeaji wa huduma

**NA KWA KUWA**, mzigo huo wa gharama kwa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya unavyoendelea kukua unasababisha wasiwasi na mashaka kuhusu uendelevu wake,

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba,

(a) Serikali ifanye tathmini ya kina juu ya uhai na uendelevu wa Mfuko;

(b) Mfuko ufanye mapitio na kuboresha utaratibu wa usajili wa makundi ya wanachama wanaojiunga kwa hiyari;

(c) Mfuko uweke mifumo imara ya TEHAMA kwa ajili ya kutambua wateja halali wanaopata huduma, kama vile matumizi ya *Biometric*;

(d) Mfuko uweke mfumo thabiti wa kutambua madai halali yanayoletwa kwa Mfuko kutoka kwa wakatoa huduma; na

(e) Tathimini ya vifurushi vinavyotolewa na Mfuko ifanyike na kuboreshwa kadiri ya mahitaji ili kuepuka kuumiza upande wowote kati ya mfuko na wanachama;

**3.2.13 Changamoto ya Mtaji kwa Baadhi ya Taasisi**

**KWA KUWA**, Utekelezaji wa majukumu ya mashirika yanayotumia mtaji wa umma unaohusisha mahitaji ya mtaji wa uwekezaji, lakini taasisi na mashirika mengi yamebainika kuwa na mtaji mdogo kutokana na kukosekana kwa mfuko wa uwekezaji na kutokuruhusiwa kokopa kwenye taasisi za kifedha,

**NA KWA KUWA**, Upungufu wa mtaji unaathiri uwezo wa taasisi ya uwekezaji kufanikisha malengo ya kuanzishwa kwake na uwezo wa kuchangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali,

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba,

(a) Serikali ifanye tathimini ya kina juu ya mahitaji ya Mtaji kwa baadhi ya mashirika/taasisi zinazojiendesha kibiashara na kuziruhusu kukopa kwa ajili ya kuongeza mtaji na ufanisi katika uwekezaji;

(b) Serikali iharakishe mchakato wa kuanzisha mfuko wa uwekezaji kwa ajili ya kuyawezesha mashirika ambayo yanafanya vizuri lakini yanachangamoto ya mtaji.

**3.2.14 Mchakato wa Utungwaji wa Sheria ya Msajili wa Hazina**

**KWA KUWA**, Msingi wa utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Msajili wa Hazina na Taasisi mbalimbali zinazotumia mtaji wa umma katika uwekezaji ni Sheria;

**NA KWA KUWA**, Tathminini iliyofanywa na Ofisi ya Msajili wa Hazina inaonesha mambo yanayohitaji kurekebishwa kwa Sheria ya Msajili wa Hazina (Madaraka na Majukumu) Sura ya 370, lakini kasi ya marekebisho haiendani na umuhimu wa kusahihisha dosari zinazosababishwa na sheria hiyo,

**KWA HIYO BASI**, Bunge liaazimia kwamba, Serikali ikamilishe mchakato wa Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Msajili wa Hazina (Madaraka na Majukumu) Sura ya 370 na kuiwasilisha Bungeni kwa uamuzi ili kuweka mazingira ya kisheria yanayoongeza ufanisi katika usimamizi wa mitaji ya umma.

## SEHEMU YA NNE

## 4.0 HITIMISHO

### 4.1 Shukurani

**Mheshimiwa Spika**, napenda kutumia fursa hii kukupongeza kwa ushindi wa kishindo ulioupata kwenye kinyang'anyiro cha kuwania nafasi ya Urais wa Umoja wa mabunge Duniani, tunaimani na wewe katika kupeperusha bendera la Tanzania na kutangaza sifa njema ya Tanzania katika nafasi ya Uongozi. Aidha, napenda kukushukuru kwa uongozi wako na miongozo mbalimbali uliyoipatia Kamati wakati wa kutekeleza majukumu yake mpaka leo taarifa hii inaposomwa.

**Mheshimiwa Spika,** napenda kumpongeza Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wa Bunge kwa weredi waliouonyesha katika kukusaidia kutekeleza jukumu la kuliongoza Bunge. Utekelezaji wa majukumu ya Kamati umefanikiwa kwa kiasi kikubwa kutokana na maelekezo, ushauri na miongozo ya kiti chako kwa kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu ya Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, kipekee napenda kumshukuru na kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuhakikisha kwamba, kunakuwa na usimamizi bora katika Taasisi na Mashirika ya Umma na kuweka msukumo wa hali ya juu katika uwekezaji wenye tija kwa Taifa ikiwa ni pamoja na kutoa fedha za uwekezaji.

**Mheshimiwa Spika,** napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma kwa kutekeleza majukumu ya Kamati hii kwa moyo na uadilifu mkubwa. Aidha nawapongeza kwa kushiriki kikamilifu katika kuboresha

mijadala, maoni na mapendekezo ya kamati na kunipa heshima ya kuiwasilisha Taarifa hii mbele ya Bunge lako Tukufu. Naomba kuwatambua Wajumbe hao kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Deus Clement Sangu – Mwenyekiti
2. Mhe. Augustine Vumma Hole, Mb – Makamu Mwenyekiti
3. Mhe. Abbas Gulam Tarimba, Mb
4. Mhe. Aeshi Alfan Hillary, Mb
5. Mhe. Aida Joseph Kenani, Mb
6. Mhe. Amina Daud Hassan, Mb
7. Mhe. Assa Nelson Makanika, Mb
8. Mhe. Bonah Ladislaus Kamoli, Mb
9. Mhe. Catherine Valentine Magige, Mb
10. Mhe. Charles Muguta Kajege, Mb
11. Mhe. Dkt. John Danielson Pallangyo, Mb-
12. Mhe. Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo, Mb-
13. Mhe. Dkt. Pius Stephen Chaya, Mb
14. Mhe. Francis Kumba Ndulane, Mb
15. Mhe. Fratey Gregory Massay Mb
16. Mhe. George Natany Malima, Mb
17. Mhe. Haji Amour Haji , Mb
18. Mhe. Maryam Azan Mwinyi, Mb
19. Mhe. Matha Nehemia Gwau, Mb
20. Mhe. Mary Masanya, Mb
21. Mhe. Nora Waziri Mzeru, Mb
22. Mhe. Zuena Athumani Bushiri, Mb

**Mheshimiwa Spika**, Vilevile, napenda kuishukuru Ofisi ya Msajili wa Hazina inayoongozwa na Ndugu Nehemia Mchechu kwa ushirikiano wake wa dhati mlioutoa kwa Kamati na kushauri namna bora ya kuzifanya Taasisi na Mashirika ya Umma kuwa na ufanisi katika utendaji na uwekezaji wake kwa lengo la kuleta tija kwa Taifa na kupata chumo lililokusudiwa.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kuwashukuru watumishi wote wa Ofisi ya Bunge wakiongozwa na Katibu wa Bunge Ndugu Nenelwa J. Mwihambi, *ndc* kwa ushirikiano wa hali ya juu walioutoa ikiwa ni

pamoja na kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kikamilifu na kwa wakati mpaka sasa ninapowasilisha taarifa hii ya Kamati.

**4.2 Hoja**

**Mheshimiwa Spika**, taarifa hii ni matokeo ya uchambuzi wa kina kuhusu Uwekezaji wa Mitaji ya Umma unaofanywa na Taasisi na Mashirika ya Umma, maoni na mapendekezo yanayotokana na uchambuzi uliofanywa na Kamati yanalenga kuishauri Serikali katika eneo la Uwekezaji wa Mitaji ya Umma ili uwekezaji huo uwe wa ufanisi na ulete tija kwa Taifa.

**Mheshimiwa Spika**, Naomba kutoa hoja kwamba, Bunge sasa likubali kuipokea na kuijadili Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma, kuhusu uchambuzi wa uwekezaji wa Mitaji ya Umma kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, ili hatimaye kupitisha mapendekezo ili yawe maazimio ya Bunge.

**Mheshimiwa Spika,** Naomba kutoa hoja.

**Deus Clement Sangu, Mb.**
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA**
**UWEKEZAJI WA MITAJI YA UMMA (PIC)**
2 Novemba, 2023

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Mwenyekiti ahsante sana kwa uwasilishaji huu wa Taarifa ya Kamati, ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge tumezisikia Taarifa za Kamati zetu tatu na kama ilivyoada tutanza uchangiaji. Hapa Taarifa ya *PAC* imebainisha mambo mengi kwa upande wa Serikali Kuu.

Kwanza, sehemu ya kwanza kutotekeleza maazimio ya bunge na sehemu ya pili yale mapungufu mapya ambayo yamejitokeza. Kwa upande wa *LAAC* sisi Wabunge wote ni Madiwani kwenye

halmashauri zetu. Kwa hivyo, taarifa iliyosomwa hapa na *LAAC* ni muhimu sana kila Mbunge kuipitia kwa ajili ya kutazama madhaifu yaliyoko kwenye halmashauri yake, ili ajitazame yeye kama sehemu ya hiyo halmashauri na yale ambayo yanatajwa huku.

Sasa, kuna kupata hati safi na bado halmashauri ikawa na changamoto, maana wakati mwingine tunaonesha zile hati safi kama vile basi mambo yote yapo sawa. Kuna hati safi lakini kuna changamoto kwenye halmashauri zetu. Kwa hiyo, nafikiri sote tunakumbuka mjadala ulivyokuwa mzito sana kipindi cha Mwezi wa Tatu, ilipotolewa taarifa hii na *CAG*. Kwa hivyo, ni muhimu sana Waheshimiwa Wabunge tufanye kazi yetu ya kuisimamia Serikali. *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo Waheshimiwa Wabunge, sasa ninayo majina hapa ya Wabunge ambao wameomba kuanza kuchangia na wengine wataendelea kuchangia tutakapokutana wakati wa mchana. Kwa hivyo tutaanza na wachache tunatavyokutana alasiri ama jioni.

Ninayo majina hapa, tutaanza na Mheshimiwa Abdul-Hafar Idrissa Juma, atafuatiwa na Mheshimiwa Issa Ally Mchungahela, Mheshimiwa Suma Ikenda Fyandomo ajiandae.

**MHE. ABDUL-HAFAR IDRASSA JUMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na kuwa mchangiaji wa mwanzo katika hoja hizi zilizokuwa mezani.

Mheshimiwa Spika, ningeomba nijielekeze sana katika hoja iliyowasilishwa na Kamati ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali za Mitaa, kwa sababu ni sehemu ya Wajumbe wa Kamati hiyo.

Mheshimiwa Spika, Fedha za Maendeleo kwa kiwango kikubwa Serikali Kuu imekuwa ikitimiza wajibu wake. Hakuna halmashauri ambayo haijapelekewa kabisa Fedha za Maendeleo, lakini nini kilichopo katika halmashauri zetu kikubwa? Ni usimamizi

usioridhisha wa Fedha za Maendeleo wa Wakurugenzi na wasaidizi wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika…

**SPIKA:** Samahani kidogo Mheshimiwa Mbunge.

Waheshimiwa Wabunge tunaposimama tutazame mchangiaji yuko wapi. Usimkate mchangiaji kwa sababu anapozungumza, anazungumza na mimi. Tuzingatie sana hilo ni la muhimu kwa sababu pia haitaleta picha nzuri kukwambia rudi kwenye kiti chako.

Mheshimiwa Juma.

**MHE. ABDUL-HAFAR IDRISSA JUMA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Kwa hiyo, fedha za maendeleo Serikali Kuu inapeleka, lakini usimamizi wa halmashauri zetu katika fedha za maendeleo hauridhishi kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wapo wanaopelekewa takribani milioni 500 mfano. Halmashauri zote zikapelekewa milioni 500 zikafanye jambo fulani, labda kujenga kituo cha afya ama kiwango fulani cha fedha kwa ajili ya kujenga skuli mpya, lakini nini kinachotokea? Wapo wanaokamilisha, wapo wasio kamilisha, wapo ambao hawafanyi kabisa, wako wengine mpaka leo wamejenga robo na fedha imekwisha.

Mheshimiwa Spika, sasa usimamizi wa fedha zinazopelekwa kwa maafisa wetu masuuli bado hauridhishi, lakini fedha kwa maendeleo zinazotengwa na wao wenyewe kutoka fedha zao za ndani hizo ndizo kabisa. Wapo wengine fedha wanazipata, sheria inawataka wapeleke asilimia 40, wanapeleka kiwango wanachotaka. Sasa nini maana ya sheria zilizotungwa na Bunge?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nadhani Halmashauri zetu Serikali iongeze umakini wa kuzisimamia ili ziweze kutimiza wajibu wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu asilimia 10. Kwanza nimpongeze Mheshimiwa Rais, Samia Suluhu Hassan kwa kuelekeza utaratibu mpya wa usimamizi wa fedha za asilimia 10 ya halmashauri. Lakini katika bajeti ya mwaka 2021/2022 ambayo taarifa yake ndio imewasilishwa hapa mbele bilioni tano haikupelekwa katika mfuko wa asilimia 10. Si kwamba ikatafutwe, fedha ilishakusanywa, lakini Wakurugenzi na maafisa masuuli wenzao waliamua tu kutokupeleka bilioni tano za vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii inamaanisha kwamba, kwa kutokupeleka bilioni tano katika mwaka 2021/2022 vijana katika Taifa hili wamenyimwa shilingi bilioni mbili ya kujiendeleza kiuchumi; wanawake katika Taifa hili wamenyimwa shilingi bilioni mbili ya kujiendeleza kiuchumi, na watu wenye ulemavu wamenyimwa shilingi bilioni moja ambayo ilipatikana na sheria tumeitunga Bunge ilitaka wakapewe.

Mheshimiwa Spika, kama tungeamua kuwa na vikundi 50 tu nchi nzima, kila kimoja kikapewa shilingi milioni 100, fedha ambayo ilikuwa imeshapatikana, leo tungekuwa tumesaidia Watanzania wangapi? Lakini Wakurugenzi na maafisa wao masuuli hawakupeleka fedha hizi.

Mheshimiwa Spika, Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali katika mwaka huohuo amebainisha takribani bilioni 88.4 zimekopeshwa hazijarejeshwa. Hivi ni wazimu wa aina gani ukampe mtu fedha halafu ushindwe kurejesha fedha yako ilhali ulimpa ya mkopo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa ni nini ambacho kamati tuliona? Na mimi kama Mbunge ninashauri kwamba, japo Mheshimiwa Rais ameelekeza mfumo mpya wa utoaji wa utoaji wa fedha hizi ambao Serikali inaendelea kuufanyia kazi lakini zile ambazo zimeshatoka lazima zipatikane kwa sababu, amewapa watu. Vikundi hewa vilikuwepo, wametengeneza vikundi hewa, kikundi kimepewa fedha eti mtu aliandika namba yake ya simu, leo simu haipatikani, ulimpaje

mtu fedha kwa namba ya simu? Inawezekana vipi kama maafisa masuuli hawapo katika sehemu ya mchezo huu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nini ushauri wangu wa jumla ni kwamba; pamoja na Maazimio ya Kamati, kuna umuhimu sasa wa kufanyika tathmini ya jumla ya Halmashauri moja baada ya nyingine kupima uwezo wake wa kifedha, kupima uwezo wake wa kutoa huduma kwa wananchi na kupima umuhimu wa uwepo ama kutokuwepo kwake.

Mheshimiwa Spika, ingekuwa biashara Serikali Kuu katika fedha za matumizi ya kawaida kwa mwaka 2021/2022 Halmashauri ya Kigoma, fedha za matumizi ya kawaida, mshahara, *OC* na mambo mengine, kununua *stationaries,* wamepewa shilingi bilioni 16.3. Fedha walizikusanya wao ni milioni 700. Japo wamezidi bajeti yao kwa asilimia 3, lakini ingekuwa biashara ya kawaida hebu tutathmini jamani; unachukua bilioni 16 unakwenda kukusanya bilioni tatu?

Mheshimiwa Spika, sasa narudia tena ushauri wangu, tufanye tathmini. Muundo huu wa Serikali za Mitaa tulionao ulikuwepo tangu hakujawa na *WhatsApp,* tangu Mheshimiwa Nape hajasambaza minara katika maeneo mengi ya nchi hii. Sasa tufanye tathmini basi tuone Halmashauri tulizonazo tuna umuhimu wa kuendelea kuwanazo katika muundo huu? Tuzibadilishe kulingana na mahitaji ya sasa ama tuone namna gani vizuri zaidi vya kufanya? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningetamani pia kuona Serikali inaboresha hatua za kinidhamu kwa watu ambao wanakuwa wamehusika kabla ya kupeleka katika hatua za kisheria. Wanaosababisha upotevu wa fedha, wakishafanya utafiti wao wanawapeleka TAKUKURU. Kule TAKUKURU mambo yanakwenda yanaenda Mahakamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, labda tu nikwambie; yupo Mkurugenzi ana kesi ya jinai kwa matendo aliyoyafanya kutoka katika halmashauri moja. Sasa hivi ni Mkurugenzi katika Halmashauri nyingine anatoka

na gari la Serikali anakwenda kuhudhuria katika kesi yake ambayo ametenda makosa katika halmashauri fulani.

Mheshimiwa Spika, sasa utaratibu wa kinidhamu nadhani pia Serikali iuboreshe kwa Wakurugenzi wa Halmashauri, kwa wakuu wa idara na watumishi wengine kabla ya kufika katika utatuzi wa kisheria. Wapo Wakurugenzi wamebainika ndugu zao ndio walikuwa wana *POS machine,* wamekusanya fedha, fedha haijapelekwa, ndugu huyu hajulikani yuko wapi, Mkurugenzi yule kahamishwa, wanasema taratibu za kisheria zinaendelea, taratibu za kinidhamu ziko wapi?

Mheshimiwa Spika, fedha hizi ni za Watanzania na ninaomba, pamoja na Maazimio ya Kamati, lakini Serikali ijiangalie katika uchukuaji wa hatua za kinidhamu kwa watu wanaohusika na ubadhirifu katika masuala ya halmashauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia kabisa katika hoja yangu ileile ya ushauri mkuu wa kufanya tathmini. Wenyeviti wa Halmashauri ni Madiwani na sisi Wabunge kwa wale ambao sheria inawaruhusu ni Madiwani katika halmashauri zetu. Tumebaini, yapo maeneo Madiwani ambao wengine ni Wenyeviti wa Halmashauri kwa kushirikiana na watendaji wetu katika Halmashauri wanafanya makusudi kumharibia Mbunge aliyekuwa madarakani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nini ushauri wangu katika tathmini hiyo. Ningetamani tathmini hiyo pia, iangalie je, hakuna uwezekano Mbunge wa jimbo akawa ndiye Mwenyekiti wa Halmashauri? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali Kuu mwaka 2021/2022 imepeleka shilingi trilioni 5.9 katika Halmashauri, za maendeleo pamoja na masuala mengine ya matumizi, lakini Halmashauri zote zimekusanya bilioni 800. Kuna Mheshimiwa Diwani mmoja pale ambaye labda hamtaki na yeye anautaka Ubunge kwa sababu ndiye ameshika zile nafasi na labda kwa sababu mahusiano ya Mkurugenzi na Mbunge hayako vizuri, wanatumia nafasi hiyo kumuharibia.

Mheshimiwa Spika, sasa ile tathmini ikifanyika tuangalie nini kinachowezekana, kama mambo haya yalipitishwa muda mrefu, kama nilivyosema, tangu *WhatsApp* na *Facebook* tunatumia sana *Yahoo,* sasa tuko katika *Gmail* na mengine. Sasa tuangalie ikiwezekana basi tufuate utaratibu ambapo Mbunge wa jimbo ikiwa halmashauri ina Mbunge zaidi ya mmoja itafutwe namna, lakini Mbunge akawe Mwenyekiti wa Halmashauri, ili kujaribu kuunganisha uwajibikaji wa pamoja.

Mheshimiwa Spika, nashukuru. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya. Mheshimiwa Issa Ally Mchungahela, atafuatiwa na Mheshimiwa Suma Ikenda Fyandomo. Mheshimiwa Simon Songe Lusengekile ajiandae.

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehma, lakini pia nikushukuru wewe kwa nafasi.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu utakapoanza nimeamua moja kwa moja kuondoa takwimu, kwa maana ya kuhakikisha kwamba mchango huu unaishi kwa muda mrefu miongoni mwetu.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyowahi kuzungumza hapo mwanzo, siku za nyuma, kwamba Taifa hili linakosa uzalendo. Tatizo hili limekuwa ni changamoto kubwa ambayo nafikiri tunahitaji kujitathmini na kuangalia jinsi gani ya kuenenda ili kuhakikisha kwamba, uzalendo unapatikana na mambo yanakwenda kama vile tunavyotarajia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, licha ya kuaminiwa tulikoaminiwa na wananchi, lakini pia wale walioteuliwa na Mheshimiwa Rais au na watu mbalimbali bado kumekuwa na changamoto, kwamba hatuzitendei haki teuzi hizo, wala hatutendei haki kuchaguliwa huko. Kumekuwa na shida ambayo ni ya wazi inayoonesha upotevu wa maadili, hususan katika taasisi mbalimbali ambazo zinafanya kazi

zilizopewa mamlaka ya kutenda kwa niaba ya wananchi au kutenda kwa ajili ya Taifa hili.

Mheshimiwa Spika, hoja yangu itajielekeza katika taasisi mbalimbali, hizi zikiwapo pamoja na taasisi za halmashauri, lakini na taasisi nyingine za kiserikali. Lengo kubwa ni kuwagusa maafisa masuuli ambao wao ndio wamepewa jukumu la kuendesha taasisi hizi kwa ajili ya ustawi wa nchi na ustawi wa wananchi pia.

Mheshimiwa Spika, uzoefu wangu nilioupata baada ya kujadiliana na kuhoji taasisi mbalimbali, kwa maana ya halmashauri tulizohojiananazo katika kipindi hiki kumeonesha kwamba, maafisa masuuli walio wengi aidha hawajui majukumu yao au kwa makusudi kabisa wameamua kukaidi kutoyatekeleza. Hali hii inasababisha athari nyingi sana, athari ambazo zinajitokeza katika sekta nyingi zilizoko hapa nchini, lakini katika taasisi hizo.

Mheshimiwa Spika, miongoni mwa majukumu waliyopewa maafisa masuuli ambao wao ndio wanaendesha hizo taasisi, majukumu makubwa sana. Majukumu hayo mojawapo kwanza ni kutafuta fedha popote ilipo. Lakini jukumu jingine ambalo afisa masuuli analo ni kuhakikisha kuwa fedha hii aliyoitafuta kwa maana ya aliyoikusanya katika maeneo husika, lakini pia fedha ambayo ameipata kupitia Serikali Kuu na vyanzo vya wafadhili mbalimbali kwamba, fedha hizi zinatumika kama inavyostahiki na matarajio ya walio wengi.

Mheshimiwa Spika, lakini pia, afisa masuuli anahakikisha kuwa anapata mapato kwa kadiri ya jinsi alivyojipangia, kwa maana ya bajeti. Afisa masuuli ahakikishe kwamba, bajeti yake amepata kiasi kinachostahili kwa ajili ya kuiendesha halmashauri au taasisi yake kwa ajili ya ustawi wa wananchi na nchi kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, afisa masuuli yeye ni msimamizi wa fedha alizokasimiwa kutoka Serikali Kuu au wafadhili mbalimbali; kuhakikisha kwamba fedha hizi zinatumika ipasavyo, lakini pia hazitumiwi isivyokuwa sahihi. Kutokana na uhalisia ulioko sasahivi ni

kwamba, maafisa masuuli walio wengi wanalipuuza jukumu hili au tuseme kwamba hawajui kabisa jukumu hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maafisa masuuli wamepewa nyenzo nyingi sana, bora na muhimu sana katika kutekeleza majukumu yake. Hata hivyo, inashangaza kwa jinsi gani wanashindwa kutekeleza majukumu haya. Kwa mfano, maafisa masuuli wamepewa mitaji, kwa maana ya nguvu kazi na vyanzo vya kukusanyia mapato hayo. Maafisa masuuli pia wamepewa wasaidizi, kwa maana ya wakuu wa vitengo na wakuu wa idara.

Mheshimiwa Spika, lakini afisa masuuli pia, amepewa mifumo mbalimbali wezeshi ambayo itamuewezsha yeye kufanya kazi kwa umakini na kufanya kazi kwa jinsi anavyotakiwa. Afisa masuuli anacho kitengo cha ukaguzi wa ndani, pia kamati ya ukaguzi wa ndani, anayo pia bodi ambayo inampa ushauri jinsi gani ya kufanya kazi zake. Halikadhalika afisa masuuli kupitia *RAS* anacho kitengo cha ukaguzi, ufuatiliaji pamoja na tathmini.

Mheshimiwa Spika, hivi vyote vimewekwa kwa ajili ya kumuwezesha afisa masuuli kufanya kazi yake kwa weledi, kama nilivyosema hapo mwanzo. Hivyo, inashangaza kwa nini afisa masuuli anashindwa kuwajibika na kufanya kazi kwa weledi kama si kukosa uzalendo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivi kama ni yule mwakilishi aliyepita, yule aliyetoa ushauri hapa, kwa maana ya mchangiaji aliyepita alivyouliza kwamba, kama ingekuwa ni biashara binafsi ambayo mtu anayo kwa *resources* hizi zote alizopewa afisa masuuli kweli angeweza kushindwa kuifaya kazi yake kwa kiwango hiki? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hapa ndipo tunapozungumza kwamba, uzalendo katika nchi hii haupo. Sasa, tunayo kila sababu kuhakikisha kwamba tunapambana kurudisha uzalendo.

Mheshimiwa Spika, hali hii ipo katika kila mahali, miongoni mwa wengi waliochaguliwa wanahisi kwamba wakishachaguliwa tu basi

kazi yao imekwisha. Wengi hawafikiri kwa niaba ya nchi hii au kwa maslahi ya nchi hii. Walio wengi wanafikiri juu ya maslahi yao binafsi. Wengi tunaendekeza matumbo yetu kwa kweli. kweli tunahitaji kujirekebisha na kubadilika kama kweli tunaitakia mema nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama nilivyowahi kusema huko nyuma kwamba, nchi bila wananchi walio bora haiwezi kwenda popote, nchi bila wafia nchi haiwezi kwenda popote. Basi sisi tuliopewa majukumu na madaraka kwa namna yoyote ile tunatakiwa tufikirie jinsi gani ya kufia nchi, na huo ndio uwananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, malalamiko ya ufujaji wa fedha ambazo zinatoka aidha kutoka Serikali Kuu au maafisa masuuli wanazikusanya wenyewe katika maduhuli yao ni mengi sana. Takribani kila halmashauri katika nchi hii ina changamoto hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mfano nilkitolea kwangu kabisa, kwenye halmashauri yangu maana mimi si Malaika na kwamba halmashauri yangu haina shida hiyo; nataka niseme kwamba, ni miongoni mwa halmashauri zenye shida hiyo, tena kubwa. Hivi ninavyosema Mkuu wa Wilaya ametoa maelekezo kwa TAKUKURU kuichunguza Halmashauri ya Masasi *DC* kwa madai na malalamiko mbalimbali ya ubadhirifu yanayohusiana na fedha za maendeleo ya walizozikusanya, halikadhalika fedha wanazozipata kutoka kwenye vyanzo vingine.

Mheshimiwa Spika, jambo hili si jema. Na ninafanya hivi kwa nia ya kufanya nini, kwamba, tujirekebishe na mimi nikiwapo miongoni mwa hao wanaotakiwa kujirekebisha…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Kengele ya pili imeshagonga Mheshimiwa. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba kuunga mkono hoja. Nakubaliana na maazimio yote ya kamati zote zilizokuja kuwasilisha hapa. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Suma Ikenda Fyandomo, atafuatiwa na Mheshimiwa Simon Songe Lusengekile. Mheshimiwa Kasalali Emmanuel Mageni ajiandae.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia. Kipekee nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema na kunitia nguvu ili niweze kuchangia kwenye Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuchangia kwa namna ambavyo mwenendo wa halmashauri zetu. Halmashauri zetu zina Wakurugenzi ambao ni wachapakazi kwelikweli na vile vile zina Wakurugenzi ambao sio waaminifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali ilianzisha utaratibu wa *force account,* kwa nia njema kabisa, lakini utaratibu huo kwa upande mwingine Wakurugenzi wanaosimamia hayo wanafanya vizuri sana, lakini kwa upande mwingine Halmashauri nyingine zinafanya vibaya sana. Hizi fedha ni za walipakodi masikini kabisa wa Taifa hili la Tanzania.

Mheshimiwa Spika, utakuta Mkurugenzi anakutwa na *CAG* kwenye ripoti zake, *CAG* anavyokwenda kukagua pale majengo ambayo yamejengwa kwa *force account*. Hayo majengo ni mapya, hayajaanza kutumika lakini wakati wa yalipokaguliwa yalikutwa na nyufa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, majengo hayo milango inadondoka yenyewe, hayajaanza kutumika, lakini Mkurugenzi alikuwepo kuangalia na kuhakikisha, maana yeye ndiye msimamizi mkuu wa hiyo halmashauri, lakini anakuwa yupo kama hayupo. Inatia uchungu sana na inasikitisha sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa majengo ya Serikali; yanatakiwa kujengewa vifaa ama hivi vifaa vya ujenzi ambavyo ni *standard,* ni imara kabisa. Kabla ya *Force Account*, mzabuni aki-*supply* ama mkandarasi ambaye anapewa jengo kulijenga, kama hajafanya vizuri, ukaguzi ukipita basi mzabuni ama mkandarasi huyo anawajibika kufanya ujenzi mwanzo mwisho ili kuhakikisha anakabidhi jengo hilo likiwa katika hali inayotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa, ujenzi huu wa *Force Account* jengo ni bovu, unakuta fedha shilingi milioni 800,000/= ama shilingi bilioni 1.2, jengo ni bovu, lina nyufa nyingi. Analaumiwa nani? Matokeo yake ni hasara.

Mheshimiwa Spika, Mtendaji Mkuu wa *PPRA* alipotutembelea kwenye Kamati yetu, nilivyokuwa nikichangia juu ya *Force Account*, namna ambavyo majengo mengi yanakuwa mabovu mapema kabisa kabla ya kuanza kutumika, nilivyokuwa namhoji kwamba moja ya halmashauri imepewa fedha zaidi ya shilingi bilioni 3.0, lakini jengo sio imara. Jengo wakati fulani limeshaanza kujengwa, fedha zimeisha jengo halijakamilika na fedha hazijulikani zimekimbilia wapi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, inasikitisha sana. Mtendaji Mkuu yule wa *PPRA* akanijibu akasema, Mheshimiwa Mbunge, unachoongea kuhusu *Force Account* ni tatizo kubwa. Anasema mahali pengine wamepita wamepewa fedha shilingi bilioni 8.0, jengo halijakamilika. Shilingi bilioni 8.0 jengo halijakamilika, tunakwenda wapi? Watanzania tunatakiwa tufike mahali uzalendo ujae ndani ya mioyo yetu. Hizi fedha zinalipwa na mlipakodi. Kwenye halmashauri kuna matatizo makubwa sana. Kwa kweli matatizo ni makubwa, ni makubwa, ni makubwa, sijui ni namna gani tufanye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hizo fedha nyingi sana zinakwenda mabilioni kwenye *Force Account*. Sioni kama inatusaidia. Natamani sana kuishauri Serikali, fedha za *Force Account* angalau basi tuweke *limit*. Kama ni mambo ya *Force Account*, basi isizidi shilingi milioni 100, lakini kwa mabilioni eti *Force Account,* usimamizi unakuwa sifuri

kabisa. Hilo linakuwa ni tatizo kubwa sana, mioyo inauma. Tunatakiwa tuwaonee huruma hawa walipakodi.

Mheshimiwa Spika, nakwenda kuchangia eneo la madeni ya wazabuni na wakandarasi…

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Spika Taarifa.

**TAARIFA**

**SPIKA:** Mheshimiwa Suma Fyandomo, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Charles Kajege.

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Nataka nimuunge mkono msemaji. *Force Account* siyo kwamba tu miradi haikamiliki lakini hata ubora wake. Sehemu nyingi unakuta majengo yameshaharibika *within* mwaka mmoja. Kwa hiyo, nashauri kwamba ikiwezekana tuondoe kabisa mambo ya *Force Account*. *(Makofi)*

**SPIKA:** Sawa. Sasa, mwenye hoja yake alikuwa ameshatoa ushauri wake. Naona na wewe umeongeza wa kwako. Mheshimiwa Suma Fyandomo, endelea na mchango wako.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

**NAIBU WAZIRI OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Inatokea wapi taarifa.

**NAIBU WAZIRI OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, hapa.

**SPIKA:** Sasa, Mheshimiwa Waziri, ili nielewe taarifa unampa Mheshimiwa Kajege au Mheshimiwa Suma?

**NAIBU WAZIRI OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, wote wawili. *(Kicheko/Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa TAMISEMI, wote wawili! Haya.

**NAIBU WAZIRI OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kuwapa taarifa Waheshimiwa wachangiaji kwamba, kimsingi ukifanya tathmini ya utekelezaji wa miradi kwa kutumia Mfumo wa *Force Account*, kuna faida kubwa zaidi kuliko hasara. Kwa mfano, zahanati ambazo tunajenga kwa takribani shilingi milioni 100, ukichukua nguvu za wananchi na shilingi milioni 50 inaongezwa na Serikali, ukipeleka kwa mkandarasi zahanati ile siyo chini ya shilingi milioni 250 hadi shilingi milioni 300. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vituo vya afya ambavyo tunajenga kwa shilingi milioni 500, ukipeleka kwa mkandarasi si chini ya shilingi bilioni 2.0 hadi shilingi 2.1/=. Sasa, kuhusu udhaifu wa ubora wa miradi inategemea. Si kwa sababu ya *Force Account*, ni udhaifu wa usimamizi ambayo lingeweza kutokea pia, hata mkandarasi asiposimamiwa kuna miradi inakuwa na udhaifu wa aina hiyo. Kwa hiyo, naomba niwape taarifa Waheshimiwa Wazungumzaji kwamba, jambo la msingi ni usimamizi wa wataalam wanaokuwa katika maeneo yale badala ya mfumo kuwa *Force Account* au kuwa *Contractor*. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tutatamani baada ya huo uzembe au udhaifu wa usimamizi, ni hatua gani zinachukuliwa ili wengine sasa wasiendelee na huo uzembe. Kwa sababu, haya yanayosemwa ya mabilioni hakuna mtu anayefurahi pesa iende halafu jengo lisikamilike. Pesa iende halafu jengo liwe halina viwango. Kwa hiyo, lazima tuone Serikali inachukua hatua gani kwa hao waliozembea ili huu mfumo uzuri wake uendelee na ule ubaya wake uondolewe kwa kuondoa hawa watu ambao wanaufanya mfumo mzima uonekane uko vibaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Suma Fyandomo, endelea na mchango wako.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Spika, nilidhani kwamba unaniuliza kama napokea taarifa ama sipokei, ama maamuzi yameshatolewa. *(Kichecho)*

**SPIKA:** Nimeshindwa kukuuliza hilo swali, kwa sababu taarifa ya kwanza iliyotolewa ulikuwa umeshaingia kwenye hoja nyingine. Halafu Mheshimiwa Naibu Waziri amekuja baada ya ile taarifa nyingine na ushauri wa yule mwingine lakini naona kama wewe unakusudia kuipokea, basi nikuulize. Mheshimiwa Suma Fyandomo, unaipokea taarifa ya Mheshimiwa Naibu Waziri Kwa sababu, mchango ulikuwa wa kwako? Ahsante sana. *(Kicheko)*

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Spika, naongea kwa uchungu mkubwa kwenye hili Taifa, nina uchungu moyoni. Siwezi kuipokea taarifa hii. Siwezi kuipokea kwa namna ambavyo Mheshimiwa Naibu Waziri, ni kaka yangu, namheshimu sana, ameongea anasema inatakiwa utafutwe utaratibu wa watu wa kwenda kusimamia fedha hizi. Utafutwe na nani na lini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunatakiwa tuwe makini sana na hizi fedha, tuwe na uchungu. Natamani sana na natamani wanaonipa taarifa, kwa maana wanaguswa na ninachokisema, wajiorodheshe na wenyewe waingie kwenye michango, ilikuwa njema sana. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**TAARIFA**

**SPIKA:** Mheshimiwa Fyandomo, kwa utaratibu wetu hii itakuwa ni taarifa ya mwisho. Mheshimiwa Mwanaisha, nimesikia kama sauti ya Mheshimiwa Mwanaisha Ulenge.

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba nimpe taarifa dada yangu Mheshimiwa Suma

Fyandomo kwamba, maneno anayoyasema ni sahihi na ni kwa mujibu wa tafiti. Aliyoyazungumza hapa Mheshimiwa Naibu Waziri, atuletee tafiti. Tafiti zimefanywa na *PPRA* ambaye ndiyo mwenye dhamana ya kusimamia manunuzi ya umma. Tafiti zimefanywa na Bodi ya Wahandisi. Tafiti zimefanywa na Baraza la Ujenzi Nchini kwamba, *Force Account* hazina tija kwa Taifa hili. Kwa nini tunaendelea kung'ang'ania? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hiyo ndiyo taarifa ambayo nataka kumwongezea dada yangu Mheshimiwa Suma. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Haya. Mheshimiwa Waziri kaa kidogo. Mheshimiwa Suma Fyandomo, unaipokea taarifa hiyo ya Mheshimiwa Mwanaisha?

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Spika, ndiyo, naipokea kwa mikono miwili kabisa.

**SPIKA:** Ahsante sana. Sasa, kaa kidogo, nakulindia muda wako. Mheshimiwa Waziri wa Fedha naona umesimama, sijui umesimama kwa taarifa, utaratibu ama?

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, nilitaka kutoa taarifa na ufafanuzi. Pamoja na kuheshimu…

**SPIKA:** Sasa, ngoja tuliweke vizuri. Ufafanuzi utapata nafasi ya wewe kuchangia, ila kama unatoa taarifa, unaruhusiwa kuitoa sasa. *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, natoa taarifa.

**TAARIFA**

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na maoni haya yanayotolewa na Waheshimiwa Wabunge, kuanzia mtoa hoja pamoja na *Engineer* ambayo yanalenga kusimamia rasilimali fedha za walipa kodi na *value for money*. Naomba tu kutoa taarifa

kwamba, si kweli kwamba jambo hili halina tija yoyote. *PPRA* pamoja na Bodi ya Wahandisi waliishauri Serikali kuendelea kulifanyia maboresho na hicho ndicho tulichofanya, hata kwenye sheria tuliyoipitisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge, utaratibu huu wa *Force Account* unatusaidia kujengea uwezo wananchi wetu kule majimboni. Utaratibu wa kutumia wakandarasi hata kwenye shughuli zinazotokea kwenye *grassroot*, unawafanya wananchi wetu wa kawaida wakose kazi. Utaona tulivyotumia *Force Account* kwenye fedha zile takribani shilingi trilioni moja, tuliweza kutengeneza mgawanyo wa fedha ziende kwenye kila wilaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kutumia wakandarasi, kuna baadhi ya maeneo huwa inaweza ikatokea mkoa mzima, wakandarasi wanaofanya shughuli hata za kujenga vyoo, hata za kujenga madarasa wanatoka mikoa mingine. Ni lini utajenga nguvu ya kazi na sasa hivi tumeshasomesha vijana karibu kila kata? Kwa hiyo, tutaendelea kuboresha na kusimamia mapungufu, lakini tutaendelea kuwatumia pia mafundi kujenga majengo yanayopatikana katika maeneo kule wanakoishi. *(Makofi)*

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Tabasamu, Mheshimiwa Mwigulu Nchemba alikuwa anatoa taarifa. Kwa hiyo, taarifa haiwezi kuwa juu ya taarifa nyingine. Muda wako Mheshimiwa Suma naulinda. Taarifa ya *LAAC* ukurasa wa 38 mpaka 39 unaonesha changamoto za matumizi ya *Force Account* na huku mbele umeeleza kuhusu maazimio, wanapendekeza nini kwa Bunge. Kwa hiyo, tunaweza kupitia hayo maeneo halafu tuone nini tunataka kufanya. Kwa sababu, ni kweli kwa upande mmoja kama alivyosema mchangiaji, inafanya vizuri. Kwa upande mwingine kuna changamoto. *(Makofi)*

Hizi changamoto siyo kwamba ni ndogo, ndiyo maana zinasemwa ili zifanyiwe kazi. Hakuna namna itaonekana huu mfumo

uko vizuri kwa sababu tu maeneo yetu yale kuna watu wanaguswa, hapana. Tunataka tija kwenye matumizi ya huu mfumo. Nadhani ndicho ambacho Kamati inajaribu kusema kwenye hii taarifa yake. Kwa hiyo tupitie hayo maeneo ambayo taarifa ya Kamati imeyasema ili tuweze na sisi kujielekeza vizuri kwenye yale mapendekezo yetu kwa Serikali. *(Makofi)*

Kwa sababu, maeneo mengine inajengwa shule, Mwalimu Mkuu sijui Mkuu wa Shule ndiyo msimamizi. Sasa, yule siyo mtaalam. Kwa hiyo, mazingira kama hayo kidogo ni changamoto kubwa, kwa sababu, hata yeye ukisema unataka kumwajibisha unamwajibisha vipi? Yeye siyo mtaalam wa hilo jambo. Yeye kazi yake ni kufundisha lakini umempa kazi ya ziada. Kwa hiyo, kidogo inakuja hiyo changamoto kwa sura hiyo. *(Makofi)*

Kwa hiyo, katika yale maboresho itazamwe kwa sura hiyo pana anayochangia Mheshimiwa Mbunge. Mheshimiwa Suma Fyandomo, malizia mchango wako. Kwa maana ya kwamba muda wako ulikuwa umelindwa. Kwa hiyo, endelea kwenye hoja yako nyingine. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Mheshimiwa Waziri wa Fedha Mwigulu Nchemba, ilitosha kabisa ile aliyoniambia kwamba wanafanya maboresho. Sasa, kwa sababu amejazia kitu kingine kaka yangu Mheshimiwa, basi naomba nimwambie. Unajua vifaa mfano vifaa vya bomba, inatakiwa kama ni koki ile ya bomba inunuliwe kifaa halisi. Sasa, hawa watu wakitumia *Force Account* kwenda kununua vifaa vya bomba, wananunua *local* kabisa, kiasi kwamba maji yanaanza kumwagika hovyo, mipira inapasuka na kila kitu. Ndiyo maana ya msisitizo kwamba, kwa sababu umesema maboresho boresheni kwa uhakika na kwa uhalisia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili suala lichukuliwe kwa uharaka sana na kwa umakini. Lichukuliwe kwa uharaka kwa sababu, kama ni maboresho watuambie ni lini ukomo wake wa maboresho kwamba,

kufika kipindi fulani tutakuwa tumeshakamilisha maboresho, kila kitu kitakuwa sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna upande wa madeni ambayo wazabuni wanadai. Inasikitisha sana na inatia uchungu sana. Kuna wazabuni ambao wali-*supply* vifaa vya ujenzi ama makandarasi kwa miaka mingi. Wengine miaka 10, miaka mitano na miaka 15, fedha zao mpaka sasa hawajalipwa. Ukimuuliza Mkurugenzi, kwa nini unadaiwa mpaka shilingi bilioni 4.0 na wazabuni pamoja na wakandarasi, tatizo ni nini? Kwa nini usilipe fedha zao na ni muda mrefu umepita? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, anakujibu kirahisi kabisa anasema mimi sikuwepo kipindi hicho. Sasa kama ulikuwa haupo kipindi hicho, wanavyokabidhiana ofisi wanakabidhianaje? Yaani kwamba hawakai wakakabidhiana haya madeni wanadai hawa, haya wanadai hawa, haya anadai huyu? Siyo tu madeni, kwa utaratibu mzima wa kila kitu kilichoko pale. Kukabidhiana kwao ni kama vile, akifika Mkurugenzi mwingine anamwambia hii ndiyo ofisi karibu, kwa heri naondoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haya madeni, hawa wazabuni wa Taifa letu la Tanzania wataendelea kuwa maskini, maskini, mpaka kwa sababu fedha zao hawalipwi. Halafu Mkurugenzi anakujibu swali lingine ukimuuliza. Kwa nini imefikia hapa shilingi bilioni tano au shilingi bilioni tatu? Anasema, unajua hapa Mheshimiwa Mbunge, mimi hapa upande wa hizi fedha shilingi bilioni tatu kama halmashauri, natakiwa nilipe shilingi bilioni mbili ama shilingi bilioni moja, shilingi bilioni mbili inatakiwa illipe Serikali ama Wizara husika. Huyu mkandarasi au mzabuni anajua wapi pa kuingilia Wizarani au huko kwenye ofisi anakosema kwamba, wafuate kwenye Serikali, anafuta wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba tuokoe maisha ya wazabuni na wakandarasi, kwa sababu fedha hizo wanakuwa wamekopa, fedha hizo mwisho wa siku wanauziwa nyumba zao, wanakuwa hawajui wataishi vipi, hela za kwenda kupanga hawana, wanabaki

wanapigwa *stroke*, wanabaki wana presha, mwisho wake unakuwa ni kifo. Tuwanyanyue hawa wakandarasi wa Taifa hili la Tanzania lakini tuwanyanyue hawa wazabuni ma-*supplier*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja, lakini naomba haya wayatendee kazi. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya, ahsante sana. Mheshimiwa Simon Songe Lusengekile, atafuatiwa na Mheshimiwa Kasalali Emmanuel Mageni. Tutamalizia na Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza.

**MHE. SIMON S. LUSENGEKILE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nichangie taarifa ya Kamati zetu zote tatu. Kitu ambacho nimejifunza kwa Serikali kwa wakati huu, kidogo sana, uandaaji wa hesabu ufanisi umeongezeka. Kwa kweli tunawapongeza Serikali kwa kuongeza ufanisi katika suala zima la uandaji wa hesabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, kuna changamoto ambazo zimeonekana na bahati nzuri Kamati zetu zimetoa hapa. Nitachangia maeneo matatu. Eneo la kwanza, ni eneo la Mfuko wa Pembejeo; limesemwa na Kamati ya *PAC* lakini pia limesemwa na Kamati ya *PIC*. Haiwezekani kwa akili ya kawaida. Haiwezekani kabisa mnakopesha shilingi bilioni 26, halafu katika zile shilingi bilioni 26, shilingi bilioni 21 zinakuwa na *indication* ya kutokukusanyika. Hii haiwezekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi naona hapa ufanisi wakati wa utoaji wa mikopo hii haukuwa vizuri, kwa sababu kama tungefanya *due diligence* vizuri katika utoaji wa mikopo hii isingewezekana leo tunazungumza shilingi bilioni 21 ni mikopo chechefu yaani *NPL*, tunaweza kuzungumza mikopo mmetoa shilingi bilioni 26 katika zile shilingi bilioni 26, shilingi bilioni 21 hazikusanyiki hii haiwezekani! Nimeona Kamati ya *PIC* wametoa pendekezo la kufuta mikopo hii, mimi nitakuwa wa mwisho kukubaliana na hili, watu hawawezi kukopeshwa shilingi bilioni 21halafu leo tupitishe tufute eti tu-*write off*

kwenye vitabu vya hesabu, fedha za Serikali ziwe zimekufa kiasi hicho, haiwezekani tufanye suala kama hilo. Watu waliokopeshwa wafuatiliwe, fedha zetu za Serikali zirudi tukopeshe watu wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mfano 2003 mpaka 2017 kuna *bank* zilikopeshwa zaidi ya shilingi milioni 800 zikafungwa na mikopo hii ikafia huko. Mfano, kulikuwa na Benki inaitwa Kagera *Cooperative Bank*, ilikopeshwa shilingi milioni 294, kulikuwa na Benki inaitwa Mbinga *Community Bank* ilikopeshwa shilingi milioni 286. Kulikuwa na Benki inaitwa *Meru Community Bank* ilikopeshwa shilingi milioni 150, kulikuwa na Benki inaitwa Njombe *Community Bank* ilikopeshwa shilingi bilioni 76. Hawa wote hawakurejesha fedha hizi! Pamoja na hayo nini kifanyike? Leo hatuwezi kupitisha eti tufute madeni haya Hapana! Maafisa Masuuli wahakikishe fedha hizi za walipa kodi, fedha hizi za nchi yetu ya Tanzania zinarejeshwa ili watu wengine waweze kukopeshwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *benchmark* ya mikopo inasema "mikopo chechefu walau iwe asilimia tano" yaani mikopo ambayo inaweza isikusanyike walau iwe asilimia tano. Kwa Mfuko wa Pembejeo ni asilimia 81, sasa asilimia 81 na sisi tuunge mkono eti tu-*write off* kwenye vitabu vyao vya hesabu, haiwezekani! Tunaomba sasa Wizara pamoja na Mfuko wetu wa Pembejeo, wahakikishe fedha hizi zinarejeshwa. Pia wafanye *due diligence* wakati wanatoa mikopo kwa Watanzania, inawezekana wanatoa mikopo halafu wanaenda kuzichukua zile fedha, halafu waliopewa wanashindwa kurejesha na tunafika kwenye hali ambayo leo tumefika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia lazima tuimarishe mfumo wa ndani wa ukusanyaji. Tulipowahoji hao watu walisema mfumo wa ndani wa ukusanyaji wa hizi fedha siyo mzuri, pia wanasema *staff* ni watu wachache. Sasa kama *staff* ni watu wachache inakuwaje tunakopesha? Kwa hiyo, tanakopesha halafu tunakuja kusakizia eti hatuna watu wa kufuatilia hiyo mikopo, kweli? Haiwezekani ni lazima tuhurumie fedha za walipa kodi, ni lazima tuhurumie fedha anazotupatia Mama yetu kipenzi Mama Samia Suluhu Hassan,

analeta fedha nyingi lazima sisi tuwe mfano wa watu ambao tunakusanya fedha hizi ili kusudi ziweze kuzunguka kwenye maeneo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la pili ni eneo la *TANOIL*, Shirika letu la Mafuta. Hapa sasa ndiyo kuna *issue*, kilichofanyika nini hapa? Tumepata hasara ya shilingi bilioni saba na milioni mia nane. Hasara hii imetokana na nini, hasara hii imetokana na watendaji kujichukulia uamuzi ambao haupo katika kanuni ambazo zinawaongoza. Kanuni zinataka uuze kwa bei hii, lakini wao wanajichukulia maamuzi yao binafsi kupunguza bei ya mafuta kwa lita ambayo haipo kwenye kanuni. Pale *TANOIL* wanakanuni kwamba, ile *margin* wanaweza kupunguza kwa asilimia 30, lakini imefika sehemu mpaka wanapunguza zaidi kwa shilingi 78 mpaka kupelekea kupata hasara ya shilingi bilioni 7.8.

Mheshimiwa Spika, tulipowauliza walipata wapi kibali, hawana kibali. Waziri wa Nishati, hakuwapa kibali, *TPDC* hakuwapa kibali. Wakajichukulia tu wenyewe, Bodi haikuruhusu lakini wao wakaamua tu kupunguza bei ya mafuta, haiwezekani, *implication* yake ni nini? *Implication* yake hii kwa wale ambao sasa wanawauzia mafuta, wanawauzia kwa kuwapunguzia kwa sababu wao wameamua halafu wanatuzunguka wanaenda kuchukua cha juu, *business as usual*. Lazima tuangalie hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bahati nzuri, Waziri wa Nishati yupo hapa, naomba akaanze na hili, ni lazima tukubaliane na pendekezo la Kamati, Mkaguzi Mkuu akafanye ukaguzi wa kiuchunguzi yaani *Forensic Audit* kuona wale wote waliosababisha hasara kwa Taifa ya shilingi bilioni 7.8 wachukuliwe hatua za kinidhamu, bila hivyo tutakuwa tunapeleka fedha, tunafanya biashara lakini hatupati faida, tunafanyeje sasa, tunakuwaje na kampuni ambayo leo imetuingiza hasara ya shilingi bilioni 7.8 halafu bado ipo. Haiwezekani lazima tuchukuwe maamuzi ya kuwasaidia Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la tatu na la mwisho. Kampuni ya Mbolea, yaani hawa watu wanafanya biashara ya mbolea katika mwaka ambao tunauzungumza 2021/2022, Serikali ilipeleka ruzuku kwa kampuni ya mbolea ya shilingi bilioni 10 kwa ajili ya kulipa mishahara pamoja na *operating expenses*. Katika biashara waliyofanya, hawakufanaya biashara yoyote wakapata *sales* sifuri. Yaani tumepeleka fedha watu wamekaa ofisini, wamelipwa mishahara shilingi bilioni 10.2, mishahara imelipwa kwa watu, matumizi ya mafuta tumewapa, sasa walikuwa wanafanya nini? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, yaani *sales* ni sifuri, wanafanya nini, si tuwapeleke wakafanye kazi zingine? Tuwapeleke hata huko Busega wakatusaidie kazi zingine? Kwa hiyo tuyaangalie maeneo haya. Hatuwezi tukawa tunapeleka fedha za Serikali, tunalipa watu mishahara halafu wanasoma magazeti, haiwezekani ni lazima mishahara ilete tija kwa Taifa. Sisi Wahasibu tunaita *this is nugatory expenditure, you incur some expenditure that cannot generate any benefit*! Ndiyo hawa wa mbolea, tumegharamika shilingi bilioni 10 hakuna walichotuingizia Serikalini. Yupo Mkurugenzi Mkuu, yupo sijui Afisa nini wanaitwa, yupo Afisa Masoko, Afisa sijui nani, sasa hawa wanafanya nini huko? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kampuni ambazo tunazianzisha ni lazima zilete tija, zilete matokeo kwa Watanzania. Kama kuna kampuni, kama kuna Mfuko hauleti matokeo chanya kwa Watanzania, kama hauleti matokeo chanya kwa Taifa ni heri ufutwe kuliko kuendelea kutuingizia hasara bila sababu za msingi. Mfuko wa Mbolea umetuingizia hasara bila sababu za msingi, futeni pelekeni Wizarani watagawa mbolea, kuliko kupeleka fedha shilingi bilioni 10.2 halafu mwisho wa siku hamna mapato ambayo tunapata kama nchi, hamna biashara wanayofanya, tumewapa mafuta, tumewalipa posho halafu kwenye hizi kuna posho nyingi, karibu shilingi milioni 800, tulipowauliza za nini sijui walikuwa wanafuatilia! Sasa unafuatilia nini wakati hakuna ulichouza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasikia kengele ya pili naomba kuunga mkono hoja mapendekezo yote ya Kamati yachukuliwe kama yalivyo, *Forensic Audit kwa TANOIL* lazima ifanyike. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Kasalali Emmanuel Mageni, tutamalizia na Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza.

**MHE. KASALALI E. MAGENI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

Mheshimiwa Spika, kwanza nikushukuru Mwenyezi Mungu kwa uhai na uzima, lakini kabla sijazungumza sana naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa namna ambavyo anatupelekea pesa nyingi sana za miradi ya maendeleo kwenye majimbo yetu. Pia ninampongeza Rais kwa namna ambavyo amekuwa akipeleka miradi hii kwa asilimia kubwa bila kubagua, hata sasa hivi sisi wa vijijini tumeanza kupata miradi ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitaelezea mfano mmoja wa mradi wa ujenzi kwa Kiingereza au tuseme Kisukuma ni *Construction of Sports Center of Excellence* katika Mji wa Malya katika Jimbo la Sumve. Mheshimiwa Rais alitupatia shilingi bilioni 31 kwa ajili ya mradi huo, Mheshimiwa Rais akiwa anaipokea timu ya Yanga alisisitiza kuhusu mradi huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niseme kwamba nimezungumza mradi huo kwa kusudi moja, kila tunapokutana hapa kujadili ripoti ya *CAG* kazi yetu sisi hapa mara nyingi tumejikuta tukijadili madudu ambayo yamefanywa na watu tuliowaamini kusimamia mambo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haya madudu yaliyosemwa na Kamati zote tatu, huwa yanatokana na mchakato, yaani watu huwa wanaanza kuzembea siku ya kwanza, siku ya pili, siku ya tatu mpaka linakuwa dudu, mwisho wa siku inakuwa hoja ya *CAG* tunakuja kujadili hapa.

Mheshimiwa Spika, nilitamani leo nitumie mradi huu kutengeneza utaratibu na kutengeneza mstari wa kuzuia hoja mpya za *CAG*. Ninazo *documents* hapa ambazo nilitamani niziweke mezani ambazo zitasaidia mimi katika kuchangia.

Mheshimiwa Spika, tarehe 06 Julai, 2023 Katibu Mkuu wa Wizara ya Sanaa, Utamaduni na Michezo, alisaini mkataba na kampuni ya *CRJE East Africa* wenye thamani ya shilingi bilioni 31 kwa ajili ya kujenga hiyo inaitwa *Proposed Construction of Sports Center of Excellence to be building on plot Number 30, 31 and 32 at Malya Kwimba District*. Katibu Mkuu akiwa hajafungwa pingu, akiwa na akili timamu na baada ya Serikali kupitia *organs* zake zote kufanya kila kilichotakiwa kufanyika alisaini huu mkataba.

Mheshimiwa Spika, tarehe 27, siku 21 baada ya kusaini huu mkataba Halmashauri ya Wilaya ya Ilemela ikamwandikia Katibu Mkuu wa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo ikimwambia kwamba; "Tunajibu barua yako ya tarehe 02 Juni, 2023 ya kutuomba eneo kwa ajili ya ujenzi wa hii *sports*…" mimi Kiingereza nilisoma mpaka Chuo Kikuu lakini kinanisumbuwa, yaani hii... *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, elimu yetu huko sisi tumesoma shule za ngumbaru, kwa hiyo… *(Makofi)*

**SPIKA:** Sema tu mradi.

**MHE. KASALALI E. MAGENI:** Mheshimiwa Spika, huu mradi wakieleza kwamba tunajibu barua yako ya tarehe 02 Juni, 2023 ya kutuomba eneo kwa ajili ya ujenzi wa huu mradi ambao siku 21 zilizopita Katibu Mkuu ameusaini kuujenga Malya - Sumve na Mheshimiwa Rais aliusema unajengwa Malya Sumve, Mheshimiwa Waziri aliyekuwepo Mchengerwa aliusema na Katibu Mkuu aliyekuwepo Dkt. Abbas alisema, lakini siku 21 baada ya kusaini, Ilemela inajibu barua iliyoandikwa kabla mradi haujasainiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiangalia milolongo hii baadaye kuna barua nimeiweka humu ya *consultant*, Kampuni ya *ABE*, akimuandikia Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo akimwambia kwamba; Ninarejea barua yako ya Tarehe 07 Septemba ya kuniomba ushauri kuhusu kubadilisha eneo la mradi. Yaani wameomba eneo kabla hata *consultant* hawajamshirikisha. Baada ya kuomba eneo na wameshasaini mkataba, wanamuomba *consultant* sasa awashauri. *Consultant* yeye hakukaa muda na hiyo barua, alikaa nayo kama siku tano akawaambia hili jambo haliwezekani, hili jambo mnaenda kuongeza gharama ya mradi, kubadilisha *site* ni ku-*complicate* mradi.. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *movement* zote hizi zisizofuata utaratibu ndizo huwa zinazaa hoja za *CAG*, watu wanawekwa kwenye ofisi za Serikali badala ya kumsaidia Mheshimiwa Rais, alichowaambia wakafanye, wanaenda kufanya wanayofikiria kichwani kwao.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais amewaambia wapiga kura wake wa Sumve kwenye *TV live* kwamba tunajenga Malya, Serikali imesaini, mradi umeanza, Wizara ipo *serious* kuhamisha mradi huu kuliko walivyo *serious* kuhakikisha tunashiriki Kombe la Afrika. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, nimeongea na Mheshimiwa Waziri kwa simu, nimeongea na Naibu Waziri na Katibu Mkuu wababe vibaya, wanazingua. Watu wa Sumve wanataka kuhamishiwa mradi wao majibu yao ni kwamba eti sisi tunakaa kijijini, mradi kama huu hauwezi kwenda kijijini. Malya kuna Chuo cha Michezo cha muda mrefu, unajenga chuo cha michezo bila kuweka shule ya mazoezi, ile ni shule ya mazoezi na Mheshimiwa Rais alitumia akili kuweka ule mradi, lakini wapo *busy* kuuhamisha. Wanaangaika na *consultant* aongeze gharama za mradi ilimradi watu wa Sumve wakose mradi waupeleke Ilemela. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hivi kule Sumve, mimi naingia kwenye kashfa kwa ajili ya hawa jamaa…

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**MHE. KASALALI E. MAGENI:** Mheshimiwa Spika, ninaanza kuonekana kwamba lile eneo la Ilemela ni eneo la Kasalali, ameuza, anatafuta hela za kampeni! Watu lazima waseme pembeni, kwa nini mradi uhamishwe kihuni namna hii!

**SPIKA:** Mheshimiwa Kasalali, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Tabasam.

**TAARIFA**

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Spika, nampa taarifa msemaji kwamba mradi huo kuhamishwa kwake tu, kupelekwa Ilemela unahitaji uongezewe shilingi bilioni 13! Yaani ni upigaji wa dhahiri wa mchana kweupe. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Kasalali Mageni, unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. KASALALI E. MAGENI:** Mheshimiwa Spika, naipokea kwa mikono miwili, na nilikuwa hapa *busy* natafuta ukubwa wa eneo la Malya.

Mheshimiwa Spika, eneo ambalo sasa mradi unatakiwa uhamishwe lina *square meter* zaidi ya 100,000, unakopelekwa ni *square meter* 67,000 yaani haliruhusu hata uendelezaji.

Mheshimiwa Spika, Kamati yako ya Bunge inayoshughulika na mambo haya ilikuja mpaka Sumve na ikaona mradi huu una maana na ikatuambia kwamba tuendelee, ikaiambia Serikali mnafanya vizuri endeleeni, leo Kamati ya Bunge inataka ionekane imesema uwongo kwa sababu kuna Waziri tu jeuri anataka awaoneshe yeye ni jeuri, anajua kufanya mambo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hatuwezi kuendelea namna hii, Kamati ya Bunge imekuja, Mheshimiwa Rais amesema, Mheshimiwa Waziri aliyekuwepo na Katibu Mkuu wamesema na sisi Wabunge

tumezunguka tunawaambia watu kwamba hiki kinafanyika, halafu mtu mmoja anakuja anasema kule ni kijijini, hawawezi kuwekewa mradi, ifike wakati muelewe nchi hii tuna usawa, watu wa Sumve hatuna lami sawa, hatuna hata milimita moja ya lami sawa, tumekubali. Maji ya Ziwa Victoria yapo Mwanza lakini Sumve hayajafika, sawa tumekubali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuna Kituo cha Michezo na chenyewe mnakipeleka Ilemela, *this is not fair,* haiwezekani! Kwa utashi wa mtu mmoja wanajifanya hapa wanashauriana na *consultant,* sijui kulikuwa kuna *consultation team* na nini, ni ujanja ujanja tu huu. Ndiyo mambo aliyokuwa anasema Mheshimiwa Waziri Mkuu wakati anapokea Ripoti ya Ardhi Mwanza. Barua zina *backdate* watu wana-*backdate* barua ili kuweka mambo yasiyoeleweka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naunga mkono hoja za Kamati zote tatu na naomba niongeze Azimio la kwamba hawa wanaotaka kuhamisha miradi na kutengeneza hoja za *CAG*, washughulikiwe kama wahalifu wengine na nipo tayari kuonesha ushirikiano kwenye hili. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, naomba kushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge. Siyo utaratibu wa kawaida, lakini nimeletewa hapa nyaraka anazozisema Mheshimiwa Mbunge na kwa namna alivyoitengeneza hoja yake inakuwa ngumu kidogo kuitoa kwenye hoja iliyopo mezani. Kwa sababu ni kweli mambo mengi anayoyazungumza *CAG*, saa nyingine inakuwa ni kutofuata utaratibu au kwamba maamuzi fulani yalipelekea matumizi ya pesa yawe makubwa zaidi kuliko yalivyosemwa mwanzo. Kwa hiyo, inaniwia ngumu kuitoa hapa, lakini kwa sababu ndiyo ameisema na ameleta vielelezo, mimi naikabidhi Serikali, siku ya Jumamosi wakati wa kuhitimisha hoja hii, Serikali iandae majibu kwa ajili ya hoja ya Mheshimiwa. *(Makofi)*

Ahsante sana. Tunamalizia na Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza.

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii nami niweze kuchangia machache kuhusu hoja zilizopo hapa za Taarifa za Kamati zetu za kusimamia fedha. Mimi ni Mjumbe wa *LAAC,* kwa hiyo, nitajaribu kusema machache tu niliyonayo ambayo tumeyaona wakati tunachambua Taarifa ya *CAG*. Nikuhakikishie kwamba Kamati yako tunafanya kazi mpaka wakati mwingine mpaka saa sita usiku. Tulikuwa tunakuunga mkono wakati tulikuwa tunajua na wewe unakesha huko kutafuta kura, nasi *LAAC* tukasema mpaka saa sita, saba usiku, ili wewe ukipata usingizi naisi tumalize kazi yetu. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mwenyekiti wetu Mheshimiwa Halima Mdee ametuambia akasema tutafika, lakini tutafika tumechoka sana. Nina uhakika nchi yetu tutafika, lakini tutafika tumekuwa wachovu kweli kweli. Nianzie nyuma kidogo; wakati Bunge hili linaanzisha Kamati ya *LAAC* nilipata nafasi ya kuwa mwanzilishi wa Kamati hii. *By then,* Mwenyekiti wetu alikuwa Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla. Baada ya kupitia mambo mbalimbali, tukagundua kwamba Halmashauri zinakusanya mapato lakini zinatumia pesa ovyo ovyo, hazichangii miradi, hazi-*support* chochote. Kwa hiyo, tukapendekeza kwamba Halmashauri hizi zitoe *percentage* kwa ajili ya ku-*support* miradi ndani ya Halmashauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuwepo kwa Halmashauri ni kutoa *services,* kuhakikisha zinasaidia wananchi wake ambao wanachangia katika mapato haya kuweza kufaidi sehemu ya kodi zao. Kwa hiyo, ikakubalika ndani ya Bunge hapa, kwamba zipo Halmashauri ambazo zina mapato kidogo, zitachangia asilimia 40 kwenye mapato yake kusaidia maendeleo katika Halmashuri zao, nyingine zitatoa asilimia 60. Kwa kweli sera hii, sijui niite sera, ilifanikiwa kwa sababu Halmashauri zilianza kuwajibika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hii sera Serikali imeenda kuibadilisha kimya kimya. Wamerudisha Halmashauri kwa *20 percent and 30*

*percent* katika kuchangia Halimashauri. Jambo hili halikubaliki, hakuna Halmashauri maskini, ni ule uzembe wa kutokuwa na ubunifu kwa Wakurugenzi. *( Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi natumikia katika Halmashauri ya Bukoba *DC*. Tulikuwa tunakusanya mapato ya shilingi milioni 800, sasa hivi tumekwenda kwenye *three billion.* Tumechambua, tumeangalia sehemu kubwa ya Halmashauri za Mkoa wa Kigoma, wanakusanya shilingi milioni 700, shilingi milioni 600, wanaendeshaje Halmashauri hizi? Ukiangalia ni uzembe na ukosefu wa ubunifu wa Wakurugenzi. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** *Yes!*

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Serikali Kuu haiwezi kubeba mzigo wote. Kuwepo kwa Halmashauri hizi, zinapaswa kusaidia maana yake hatuwezi kuendesha Serikali hii kutoka *Central Government*. Nchi hii ni kubwa, ni lazima Halmashauri ziwepo, lazima ziwezeshwe na zijiwezeshe zenyewe, zisimamiwe ili kuweza kusaidia maendeleo.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama Kamati hatukukubaliana na jambo hili. Najua na wengine mpo, mtuunge mkono, hakuna Halmashauri maskini. Halmashauri ziendelee na ile *30 percent*, hatuwezi kufanya Wakurugenzi kubweteka. Lazima wawe wabunifu, watengeneze vyanzo vipya. Vyanzo vipo; kilimo, biashara na kadhalika. Najua Watanzania wanapenda ile *copy and paste*. Ukitengeneza stendi na Halmashauri nyingine stendi, na nyingine stendi; ukitengeneza soko na nyingine soko, na nyingine soko; kwa sababu watu *they can't think beyond the box. (Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** *Yes!*

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Mheshimiwa Spika, hatuwezi. Ni lazima kusaidia nchi hii, tuhakikishe Halmashauri zinafanya kazi, zinasaidia ku-*support* Serikali Kuu katika kuleta maendeleo. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kingine nitakachoongelea ni *ceilling,* yaani ule Ukomo wa Bajeti. *Ceiling* hizi namwambia Waziri wa Fedha, asitumie *ceiiling* hivyo kuleta umaskini na kufanya watu wabweteke. Kwa mfano, Halmashauri ya Temeke, (natoa mfano wa Halmashauri moja, lakini zipo nyingi) ilisema itakusanya shilingi bilioni 60 na zaidi. Halafu Wizara ya Fedha ikawaambia mkusanye shilingi bilioni 42. Wapi na wapi? Wao ndio unakusanya? Sasa kinachotokea, wanakwenda wanakusanya fedha zaidi ya ile *ceilling,* wanaanza kutafuta mafungu namna ya kuzitumia. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tulipowauliza, kwa nini mnafanya hivyo? Wakasema kuna miongozo ya *IMF (International Monetary Fund)*. Sasa nikawauliza, *What is this International Monetary Fund*? Yaani inakuja kuchungulia mpaka kwenye vyungu vyetu. Wanatufanya tuendelee kukopa na kukopa mpaka tufe. Wanafurahia nini? Wanachofurahia, ni kwamba sisi tukusanye mapato, tuendeleze nchi yetu, tupunguze mikopo! Hawatakubali na Wizara ya Fedha msikubaliane na hayo. Mhakikishe *ceilling* zinaenda kwenye Halmashauri kwa Halmashauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, zipo Halmashauri ambazo zina uwezo hasa zile za Majiji. Zile sasa zikusanye zi-*support* zile za Buhigwe. Kule Halmashauri ya Buhigwe wanakusanya shilingi milioni 600, halafu hawana mradi hata mmoja, yaani wana Mradi wa Lishe tu. Kwa hiyo, zile tuwape uwezo wa kukusanya na kuhakikisha yale makusanyo yanasaidia zile Halmashauri nyingine ambazo zimekaa; Kigoma *DC,* Buhigwe sijui na nyingine zipi?

**MBUNGE FULANI:** Kasulu

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Kasulu, zote hizo zinakusanya shilingi milioni 700, shilingi milioni 800. Afadhali Uvinza wanajitaji huko. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yaani hata Serikali inahangaika na mawese kutengeneza mafuta, yenyewe yote hiyo haina chochote! Mimi nashanga sana! Mheshimiwa Ndalichako Halmashauri yako,

mwende mwangalie. Waheshimiwa Wabunge, muwe mnakuja kwenye Kamati ya *LAAC* mnasikiliza mambo yaliyopo huko. Muhudhurie kwenye Kamati ya *LAAC* ndiyo mtajua kinachoendelea ndani ya Halmashauri zetu kule, kuna mambo siyo mazuri. Nanyi msaidie kutoa mchango, siyo kudumaza kwamba mrudi kwenye *20 percent*. Yaani badala ya kwenda mbele, tunarudi nyuma!

**MBUNGE FULANI:** Haiwezekani. *(Kicheko/ Makofi)*

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Haiwezekani.

Mheshimiwa Spika, baada ya kumaliza habari ya *cealing*, sasa niongee kidogo kuhusu kulipa pesa za Makandarasi na Wazabuni. Kwa Kiswahili wanaita Wazabauni, ndio *suppliers,* lakini ukitaka kufa maskini katika nchi hii, fanya kazi na Halmashauri. Yaani kama ukitaka kufa maskini na kufilisika, fanya kazi na Halmashauri, unatembea kudai mpaka visigino vikatike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa taarifa ambazo siyo rasmi, huko chini *(underground)* wanasema kama hujatoa chochote hulipwi.

**WABUNGE FULANI:** Hulipwi, ndiyo! *(Makofi)*

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Mheshimiwa Spika, tunaomba, acheni kuziambia Halimashauri hizi hazitakuwa na roho mbaya. Lipeni Wazabuni wenu, lipeni Wakandarasi walio katika uwezo wao ili mwaokoe. Serikali iliyokuwa ikisema kwamba wanalea wakandarasi na wazabuni ili kuwainua kiuchumi, hawa watu wanakopa mikopo, lakini mtu ana-*supply,* anadai mpaka anakufa. *This is too bad*. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ni kuhusu usimamizi. Namshukuru sana Naibu Waziri, kwa kweli tunafanyanaye kazi mpaka saa sita na yeye. Amekaa huyu, amekomaa kweli kweli. Amekomaa, tusingekomaa tusingeweza kupitia Halmashauri zote hizo sabini na kitu. Kwa kweli *it was a big job*. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, usimamizi wa hapa kwenye Sekretatrieti za Mikoa ambazo zipo nchi ya TAMISEMI, hazisimamii. Wana kitu kinaitwa *M & E (Monitoring and Evaluation)*, sasa hivi wameajiri watu mkoani siyo chini ya wawili na wana bajeti, bado hawatoki Ofisini. Miradi yote ya *Force Account* inakufa, na yenyewe labda ingekuwa inakwenda vizuri kama ingekuwa inapata usimamizi unaotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, TAMISEMI watoke Ofisini, Sekretarieti za Mikoa zitoke Ofisini. Wanatufanyisha kazi kubwa; *LAAC* tunafanya kazi kama ya Waziri wakati mwingine na kama Wakurugenzi. Yaani tunajiuliza, sasa tumekuwa Wakurugenzi sisi mwenyewe! Haiwezekani. Tuwajibike. Serikali za Mkoa chini ya hicho Kitengo mlichoweka, mnawawekea wafanyakazi wako wawili, wanalipwa pesa nzuri, wana mafungu, ni kwa nini hawatoki Ofisini? Watoke waende kuangalia hii miradi ili fedha za wananchi ziweze kutumika ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nisiseme mengi leo, niwachie na wengine, ila naunga mkono hoja.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Mheshimiwa, kengele ya pili tayari. Ahsante sana.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa sehemu ya kwanza ya Kikao chetu cha leo. Nitataja baadhi ya Waheshimiwa Wabunge ambao tutaanza nao alasiri, halafu wengine wataendelea kutajwa kwa kadiri michango inatavyokuwa inaendelea.

Tunao Mheshimiwa Bonnah Ladislaus Kamoli, Mheshimiwa Joseph George Kakunda, Mheshimiwa Dkt. Charles Stephen Kimei, Mheshimiwa Bakar Hamad Bakar, Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate, Mheshimiwa Anatropia Theonest na wengine wataendelea kutajwa kadiri uchangiaji utakavyoendelea.

Waheshimiwa Wabunge, ninalo tangazo moja kutoka kwa Katibu wa Bunge, anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote, kuwa Semina ya Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma kuhusu Mfumo wa Uwasilishaji Tamko kwa Njia ya Mtandao *(Online Declaration System (ODS),* iliyokuwa ifanyike leo Siku ya Alhamisi, tarehe 2 Novemba, 2023 imeahirishwa mpaka mtakapotangaziwa tena. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema Tangazo hilo. Nasitisha Shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni leo.

*(Saa 7.30 Mchana Bunge lilisitishwa Hadi Saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirudia)*

*Hapa (Mhe. Najma Murtaza Giga) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tukae.

Katibu.

**NDG. PILI OMARI - KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA KAMATI**

**Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali kuhusu Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa hesabu zilizokaguliwa na Serikali Kuu, Mashirika ya Umma na Kaguzi za Ufanisi kwa Mwaka wa Fedha uliuoishia tarehe 30 Juni, 2022**

**Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa kuhusu Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa hesabu zilizokaguliwa za Mamlaka za Seriakli za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha ulioishi tarehe 30 Juni, 2022**

**Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezajiwa wa Mitaji ya Umma kuhusu uwekezaji wa mitaji ya umma kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na majadiliano yetu na tutaanza na Mheshimiwa. Bonnah Ladislaus Kamoli, na Mheshimiwa Joseph George Kakunda ajiandae.

**MHE. BONNAH L. KAMOLI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kutoa mchango wangu kama ilivyoelezwa kwenye Taarifa ya Kamati yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninapenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa ambayo anaifanya katika kuhakikisha kuwa wananchi wake wa Tanzania tunaweza kupata maji safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Taarifa ya *PAC* Mwenyekiti wangu ameongelea kuhusiana na *DAWASA*. *DAWASA* kumekuwa kuna Taasisi nyingi za Serikali ambazo zinadaiwa na *DAWASA*. Kama unavyojua, kuna sehemu nyingi kwenye majimbo mengi bado watu hawajaunganishiwa maji kutokana na uchache wa fedha. Hizi fedha shilingi bilioni 13.5 zipo katika Taasisi za Serikali, kwa hiyo, nilikuwa ninaomba nichukue nafasi hii kuziomba hizi taasisi ziweze kuwalipa *DAWASA* ili wananchi waweze kuunganishiwa maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama unavyojua, mwananchi wa kawaida asipolipa maji tu kwa miezi miwili anakatiwa maji lakini hizi taasisi zimekaa muda mrefu sana hazijawahi kulipa bili zao wala hazijawahi kukatiwa. Tunajua kwamba hizi ni taasisi muhimu na tunajua hawapati asilimia 100 ya bajeti lakini wajaribu kuangalia. Katika bajeti ambayo wanaipata waweze kuwalipa *DAWASA* ili na wao waweze kufanya shughuli zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nilikuwa ninataka kuliongelea ni jambo la kumuomba Mheshimiwa Waziri wa Maji aweze kuangalia bili. Bili zetu ambazo tunazipata au wananchi wanazozipata hazina uwiano na matumizi ya maji. Unakuta mwananchi ambaye ana familia ya watu watatu anapata bili sawa na mwenye familia ya watu 10 na hizi bili zinakuja, kila bili zinapokuja unaweza ukuta kwa muda wa miezi mitatu iliyoongozana mtu anapata bili ambazo, mfano kama alipata shilingi 220,000 mwezi uliopita basi atapata shilingi 220,000 kwa muda wa miezi mitatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tuangalie ni jinsi gani usomaji wa bili unaonekana kuna tatizo kidogo. Waangalie ni jinsi gani wanaweza kutofautisha familia ya watu wengi na familia ya watu wachache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuhusiana na miundombinu mibovu ya maji. Maji ambayo yanatoka *DAWASA* ambayo tayari yameshatengenezwa asilimia 37 maji yote yanapotelea njiani na ni kwa sababu ya miundombinu mibovu. Kingine, mfano bomba limepasuka, unaweza ukawaita watu wa *DAWASA* waje kutengeneza lile bomba kwa sababu bomba linapopasuka maji yanatoka inawezekana hata kwa siku tano mfululizo lakini hawa watu hawaji na ndiyo maana hawa watu wa *DAWASA* wanaendelea kupata hasara kwa sababu miundombinu yao mingi ni mibovu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana wananchi wengi mfano Mkoa wa Dar es Salaam, Jimbo la Segerea kuna kata zangu, Kata ya Kinyerezi, Kata ya Bunyokwa, lakini pia na Kata ya Segerea, maji yanatoka kwa mgao kwa sababu maji mengi ambayo yanakuja ili yaende kwa wananchi yanaishia njiani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tulikuwa tunawaomba. Pamoja na kazi kubwa ambayo anaifanya Mheshimiwa Rais, pamoja na kazi kubwa anayoifanya Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri lakini kama huku chini kutakuwa hakuna

watu ambao wanaweza kufanya kazi kuziba haya mapengo basi wananchi wataendelea kukosa maji muda wote kwa sababu maji ambayo yanakuja yanaishia njiani. Na haya maji yamekuwa yakileta hasara kubwa kwenye barabara, watu wametengeneza barabara, bomba likipasuka barabara yote inaharibika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyoy, tulikuwa tunaomba watu wa *DAWASA*, kwa kweli watu wa *DAWASA* wamekuwa ni wavivu sana hawa watu wa chini kuja kushughulikia haya mabomba machakavu. Na haya mabomba kama ninavyosema yanaleta usumbufu katika barabara lakini pia kwa wananchi. Unaweza ukakuta bomba limepasuka maji yanaingia kwa wananchi. Nilikuwa ninaomba haya mambo yaweze kufuatiliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nililokuwa ninataka kumuomba Mheshimiwa Waziri ni kuhusiana na jumuiya ya watumia maji. Tulikuwa na visima ambavyo vilikuwa vinaendeshwa na jumuiya ya watumia maji, *DAWASA* wakavichukua hivi visima, lakini sasa hivi hawavihudumii. Visima vyenyewe pampu zilishakufa siku nyingi. Kwa hiyo, nilikuwa ninaomba kama wenyewe wameshindwa kuviendeleza au kuvifanyia *service* ili viendelee kutoa maji, basi wawarudishie watumia maji kwa sababu kwa muda mrefu hivi visima vimekuwa vikiangaliwa na jumuiya ya watumia maji na vilikuwa vizuri tu. Tangu walivyovichukua *DAWASA*, visima vimekuwa havitoi maji, vingine vimekufa, vingine havifanyi kazi. Yaani tuna shida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi kata zangu ambazo nimekuambia kata tatu au tano zina visima vya watumia maji lakini kwa sababu pampu zake zimekufa na *DAWASA* hawajaenda kutengeneza, inabidi wanunue maji na wakati vile visima vipo pale. Kwa hiyo, tunamuomba sana Mhehimiwa Waziri aangalie ni jinsi gani anaweza akavirudisha hivi visima kwa wananchi ili waweze kufanya kazi ya kuviendeleza na wananchi waweze kupata maji. Kwa sababu, kwa kawaida sisi tunapata maji ya mgao, Bonyokwa, Segerea, Kimanga pamoja na Kinyerezi wanapata maji ya mgao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama wanapata maji ya mgao, hivi visima ndiyo vingekuwa vinatusaidia lakini *DAWASA* visima wanavyo, lakini pia maji hayatoki. Waturudishie hivi visima vya watumia maji ili wananchi waweze kutumia hivi visima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nililokuwa ninataka kuongelea ni kuhusiana na vyanzo vya maji. Vyanzo vya maji vimekuwa ni tatizo kubwa kwa sababu kwenye vyanzo vya maji kumekuwa kuna shughuli za kibinadamu na ndiyo maana sisi tunapata maji ya mgao. Pamoja na kwamba, Mheshimiwa Rais anaanzisha miradi mingi na tunamshukuru pamoja na Mheshimiwa waziri, tunamshukuru hasa kwa miradi hii ya kimkakati ambayo imeanzishwa katika Mkoa wa Dar es Salaam kwa jina la Dar es Salaam ya Kusini, tunashukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba sana sana viangaliwe hivi vyanzo vya maji. Kwa sababu, kwenye hivi vyanzo vya maji kama kutaendelea kuwa na shughuli za kibinadamu maji hayatakuwa yanatoka. Tutaendelea kupata mgao wa maji na tutaendelea kupata mgao wa umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuwapunguzie wananchi wetu ili waweze kupata mgao mmoja, wapate tu hata huo mgao wa maji, lakini visima hivi ambavyo tulikuwa tunaviendesha wenyewe tuweze kuvitumia. Visima hivyo wanavyo, pamoja na maji yao yanatoka kwa mgao. Tunaomba sana, tunajua Mheshimiwa Waziri pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri wanafanya kazi kubwa sana, Mkurugenzi wangu wa *DAWASA* Dar es Salaam, anafanya kazi kubwa sana lakini wasipoangalia huku chini maji yanakopotea itakuwa ni shida sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumetoka Mwaka 2015 mpaka Mwaka 2020, tulikuwa hatuna tatizo la maji mpaka Mwaka 2021, lakini sasa hivi linaanza kurudi tatizo la maji. Ukiangalia tatizo kubwa la maji linasababishwa na miundombinu. Mabomba yanapasuka. Hata hapa hapa Dodoma ukiangalia mabomba yanapasuka lakini ukiwapigia simu wahusika hawaji kwa wakati. Maji yanaendelea

kupotea na wakija kwenye taarifa wanasema kwamba wana hasara, upotevu wa maji asilimia 37 na haya maji yanayopotea tayari yameshawekewa dawa kwa hiyo, wanaendelea kupata hasara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba hawa watu wanatakiwa wawalipe, *DAWASA* kutokana na hizi kazi zao pamoja na changamoto zao lakini pia waweze kurekebisha miundombinu yao ya maji. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Bonnah Kamoli.

**MHE. BONNAH L. KAMOLI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, nilimtaja Mheshimiwa Joseph Kakunda, Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei na Mheshimiwa Bakar Hamad Bakar wajiandae.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. Uchambuzi wa Taarifa ya *CAG* ambao umewasilishwa hapa na Kamati zetu za *PAC*, *LAAC* na *PIC,* umethibitisha ukiukwaji wa kanuni, sheria, taratibu na miongozo kwenye ukusanyaji wa mapato, usimamizi wa mikataba, ufanyaji wa malipo mbalimbali na hata utunzaji wa Mali za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa ya *CAG* imeweka bayana udhaifu ambao umeonekana kwenye ukusanyaji wa mapato hususani kwa mfano, *TRA* kutokusanya shilingi karibu bilioni 890. Kwa kweli hili ni jambo ambalo ni kubwa na Bunge linatakiwa ku-*note* na kufanyia kazi. Vilevile umebainika udhaifu mkubwa katika usimamizi wa mikataba. Kwa mfano, eneo moja tu ukilitaja la ucheleweshaji wa malipo ya wakandarasi na wataalamu washauri ambao kwa mara nyingine umesababisha riba ya zaidi shilingi bilioni 36. Hii ni

eneo mojawapo ambalo kwa kweli linatia ukakasi uendeshaji wetu wa kazi zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu, taarifa ile imeonesha udhaifu mkubwa katika utekelezaji wa masharti ya sehemu ya 17 ya viwango vya uhasibu vya kimataifa (*IPSAS)*. Katika baadhi ya taasisi unaona kabisa kwamba, watu wanakuja pale kwenye Kamati hawajajiandaa kujibu maswali ya Kamati, wanaonesha kabisa kuna upungufu wa watumishi kwenye kada hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, kwa nini ije kubinika upungufu wa watumishi kwenye hizo kada mpaka watu wengine wanasema tutatafuta mtaalamu mshauri *(consultant)* wa kuja kufanya *review* ya *asset*. Yaani, ni kazi ndogo ambayo inaweza ikafanywa na mhasibu mdogo tu ambaye ametoka shule, haijafanyika. Kwa hiyo, kuna udhaifu mkubwa sana kwenye eneo la utunzaji wa mali za Serikali kwa sababu tu ya kutokufuatiliwa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo kama hayo ndiyo yamesababisha Kamati hizi zije na maazimio na mapendekezo ambayo mimi kama Mbunge wa Sikonge ninayaunga mkono na ninaomba Wabunge wote tuyaunge mkono ili tuweze kuwezesha Serikali kufanya maboresho na marekebisho mbalimbali ambayo yatasaidia na kuwa tija katika uendeshaji wa kazi zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatoa mfano halisi, kwamba yamefanyika kwa bahati mbaya, sikubali kama yamefanyika kwa bahati mbaya. Mengi yamefanyika kwa makusudi, mengi yaliyoonekana, yamefanyika kwa makusudi. Haiwezekani wewe kutojua sheria, kanuni, taratibu na miongozo kwa sababu miongozo hiyo ukiwauliza wanasema tunafahamu miongozo hiyo ila tutarekebisha. Kwa hiyo, maana yake wengi wamefanya kwa makusudi, na kufanya kwa makusudi inasababisha hasara kwa Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana, haya yafanyie kazi na Bunge likubali maazimio na mapendekezo ambayo

yamewasilishwa na Wenyeviti wetu watatu wa Kamati zetu tatu za usimamizi ili kuweza kufanya maboresho. Nitatoa mfano halisi mmoja tu wa hasara ya shilingi bilioni 7.840 katika kampuni ta *TANOIL*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kampuni ya *TANOIL* ni kampuni tanzu ya shirika la maendeleo ya *petrol* Tanzania (*TPDC)*. Kampuni hii imepewa kazi ya kuagiza na kusambaza mafuta. Sasa kilitokea nini mpaka kampuni hii ikapata hasara hii? Kabla hatujaingia kwenye hizi *point* kuwa kilitokea nini, tushangae kwamba haiwezekani kwamba hasara ya Mwaka 2020/2021 ilikuwa shilingi milioni 166 tu. Sasa ime-*jump* kutoka shilingi milioni 166 mpaka shilingi bilioni 7.840 kwa mwaka mmoja tu. Ina maana hapo kuna watu waliona pengine labda kuna fursa labda ya *transition*, wakaona pengine labda hawatathibitiwa na mambo kama yale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya tunayoyasema hapa mengine yanasaidia Serikali kuweza kuangalia kwa kina. Hivi kwa nini hasara ipande kutoka shilingi milioni 166 hadi shilingi bilioni 7.840 kwa tofauti ya mwaka mmoja tu. Hilo ni jambo ambalo liweke *alarm* kwa kila mtu. Ukizichunguza sababu kwa nini ilipatikana hasara hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu ya kwanza, Menejimenti ya *TANOIL* kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ilikuwa haifanyi usuluhisho wa kila mwezi wa mafuta yaliyokuwa yananunuliwa na kusambazwa. Matokeo yake ilipata mafuta yenye thamani ya shilingi bilioni 1.8, hayakufanyiwa *reconciliation* na hiyo kusababisha hasara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, menejimenti haiwezekani isisimamie *reconciliation*. Lazima kulikuwa na sababu za makusudi. Sasa, Serikali huko watakapokaa wafanye uchambuzi kwa kina, kwa nini hawakufanya *reconciliation*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu ya pili, Menejimenti ilikuwa hainakili mapato yatokanayo na bishara ya mafuta kwenye vitabu. Kwa mfano, shehena mbili za mafuta zenye thamani ya shilingi bilioni 16.2 yaliyopokelewa mwezi Juni, 2022 hadi Mwaka wa Fedha

unaisha, tarehe 30 Juni, 2022 yalikuwa hayajaingizwa kwenye vitabu vya hesabu. Maana yake ni nini? Haya yalikuwa ni makusudi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu ya tatu. Menejimenti ya *TANOIL* iliamua kuuza mafuta kwa makampuni ya ndani kwa bei ya chini kulinganisha na bei elekezi. Maana yake ni nini? Vilevile nyaraka za malipo za makampuni zilipopitiwa na *CAG*, aligundua malipo yenyewe halisi, yaliyofanyika yalikuwa na bei ndogo kuliko hata bei ambayo ilikuwa imeidhinishwa na menejimenti ya *TANOIL*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa maana yake ni nini? Hasara hii ambayo ilisababishwa na kutokuwa na kutonakili kwenye vitabu vya hesabu, hasara iliyosababishwa ilikuwa shilingi bilioni 53.7 na hasara ya kwenye nyaraka ambayo inaonesha bei ya chini kuliko hata ile ya menejimenti, shilingi bilioni 30.9. Huu ni upotevu mkubwa sana wa mapato ya Serikali na hii umetokana na ukiukwaji wa makusudi wa sheria, kanuni, miongozo, na taratibu za Serikali. Wale mabwana ni watu wadogo sana lakini waliamua kusababisha hasara kama hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo ndiyo sababu Kamati zimekuja na mapendekezo. Kwa mfano, kwenye hiyo ya *TANOIL*, Kamati imependekeza kwamba tufanye ukaguzi wa kiuchunguzi. *CAG* afanye ukaguzi wa kiuchunguzi (*forensic audit*) ambayo itabaini nani alifanya nini kwa jina na makusudi gani. Ikiwa ni kwa makusudi basi hatua zitachukuliwa kipindi hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli lazima sababu za kina zibainike kupitia uchunguzi huu utakaofanyika kwa hao ambao wamehusika, lakini kuna mambo madogo madogo ambayo yanatakiwa yaangaliwe. Hivi kulikuwa na sababu yeyote ya kuanzisha *TANOIL* wakati tuna *TIPER?* Pengine TIPER angeweza kupewa kazi hiyo akaifanya vizuri, na pengine tusingeweza kuingia kwenye hasara; au pengine labda Idara ya Serikali ingeweza kufanya kazi hizo. Yaani huu uchungzi utatusaidia kubaini mambo mengi, si haya tu yaliyobainika kwenye hesabu, mambo mengi ili

kuwea kuisaidia nchi na kuweza kupata tija ambayo ilitarajiwa kutokana na kuanzishwa kwa hii kampuni ya *TANOIL*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kwa kweli naliomba Bunge, kwa sababu mimi kama Mbunge wa Sikonge naunga mkono mapendekezo yote na maazimio ambayo yamelewa hapa na Kamati zote tatu. Basi naliomba Bunge nalo katika *deliberations* zake liunge mkono ili tuweze kuisaidia nchi kusonga mbele. Tumsaidie Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan. Hawa ambao wanafanya mambo kama haya ni watu tu ambao kwa kweli wameaminiwa kwenye ofisi. Inawezekana asiwe hata afisa masuhuli, lakini wamefanya haya na yanonekana kwenye hesabu ambayo inasababisha hasara kwa nchi. Kwa hiyo ni jambo ambalo ni lazima tuchukue hatua za makusudi ili kuweza kujanga tija katika nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa nafasi hii.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Joseph Kakunda. Nilimtaja Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei. Mheshimiwa Bakar Hamad Bakar na Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate, ujiandae.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa fursa hii. Mimi naanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais na Amiri Jeshi wetu Mkuu kwa mambo mengi anayofanya. Pamoja na kumwaga fedha nyingi kwenye Jimbo langu la Vunjo; papo tu na mimi inabidi nimpe maua ya Vunjo. Lakini zaidi kwa namna ambavyo alichukua hoja zilizoletwa kwake na *CAG* na akaweza kuzifanyia kazi. Kwa wale wanaofuatilia watajua kwamba Mheshimiwa Rais ameshafanyia kazi hoja nyingi, ikiwemo kubadilisha watendaji kwenye taasisi fulani fulani ambazo zilionekana kwamba zina udhaifu. Pamoja na miongozo mingine ya kutekeleza zile hoja, nampongeza sana kusema kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza *CAG* mwenyewe kwa namna ambavyo ameweza kutuletea hoja nzuri na amechambua vizuri hesabu hizi na akatoa ushauri ambao kweli umeweza

kuongoza mjadala kwenye Bunge hili kuhusiana na utendaji wa Serikali katika kusimamia fedha za umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, nawapongeza wanakamati wa *PAC, PIC* na *LAAC* kwa kazi nzuri na maazimo mazuri ambayo wameyaleta, na ninasema kwamba mimi nayaunga mkono kwa asilimia 100. Kuna moja tu ambalo sitaliunga mkono sana, kwa sababu lile la taasisi za umma au mashirika ya umma kupeleka asilimia 15 ya mapato yao ghafi Serikalini kabla ya kufanya hesabu kwamba wanapata hasara au faida, hilo mimi nafikiri kwamba linapunguza sana uwezo wa mashirika ya umma yaweze kuendelea kufanya kazi kibiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba niwasilishe hoja moja, na nitajikita zaidi kwenye mashirika ya umma. Endapo mashirika ya umma yataendelea kufanya kazi kwa namna tulivyoona kwenye hoja zilizoibuliwa na Mheshimiwa *CAG* ninaamini kwamba hatutaweza kuwa na uhakika wa *prudence of fiscal stability*; yaani utulivu wa fedha za kibajeti kwa miaka inayokuja. Kwa sababu *issue* ni hii; kwenye sheria ya bajeti tunaambiwa kwamba msingi ni mmoja; ni kwamba Serikali ijiendeshe na ijiendeshe kwa *fiscal policy* yake kwa kuhakikisha kwamba kuna utulivu endelevu kwa vizazi vijavyo; kusije kukawa na madeni yameji-*accumulate* kila mahali halafu wewe huyajui, huyatambui, halafu yakiibuka hapa unaambiwa ulipe. Kwa sababu hii unakuwa unaingiza bajeti kwenye *stress* kubwa na hii inakuwa ni *fiscal risk* kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nasema kwamba, kwanza cha msingi ni lazima tuchukue hatua za kuhakikisha kwamba mashirika ya umma yanabadilika kwa namna yanavyojiendesha. Tumeambiwa kwamba mashirika ya umma yanajiendesha kwa hasara. Hasara iliyofanywa na mashirika 14 yaliyo kwenye ripoti ya *CAG* kwa mwaka 2020/2021 na 2021/2022 ni shilingi bilioni 217. Hasara ya mashirika 14 tu. Hatujayaweka mashirika mengine yote kwa sababu na yeye ametupa *sample* tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kitu cha ajabu. Utaona kwamba kwa mfano, Shirika la *ATCL*, limefanya hasara ya shilingi bilioni 105, ukijumuisha fedha ya ruzuku ambayo walipewa. Kama wasingalipewa ruzuku ya shilingi bilioni 30.6 wangefanya hasara ya jumla ya bilioni 105 kwa hiyo miaka hiyo miwili, ni fedha nyingi. Ukiangalia Shirika la *TRC* limefanya hasara ya shilingi bilioni 54, *NDC* imefanya hasara bilioni 38, ukiangalia *Mkulazi Holding* imefanya hasara ya bilioni 20, *Kilimanjaro Lather* bilioni saba. Vyote hivi vinakula ndani *either* ni ruzuku au wamechukua mkopo au sijui wame-*finance* namna gani hiyo hasara, lakini ni kwamba inaingiza bajeti yetu kwenye kutokuwa na *sustainability* ya uhimilivu wake kwa miaka ile inayokuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachosikitisha ni kwamba mashirika haya yanayofanya hasara hamna mkakati ambao wamejijengea ya kuweza kujinasua kwenye kufanya hasara hizi, na hawalazimishwi kutengeneza hizo *business plan* za kuhakikisha kwamba baada ya miaka miwili au mitatu wanajiondoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nafurahi kwamba *TTCL* walikuja kwetu kwenye Kamati ya Bajeti; wakaonyesha kwamba wamefanya hasara kubwa lakini ndani ya mwaka huu na mwaka ujao watakuwa wamekuwa *sustainable*. Kule tunaona kwamba Mkurugenzi Mtendaji naye alibadilishwa na Mheshimiwa Rais. Lakini kwa kweli ni tatizo kubwa kwa sababu hatuwezi kujua mbeleni ni wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, Shirika la *ATCL,* Mkaguzi Mkuu anasema kwamba ilipata hasara kwa sababu ndege zilikuwa *grounded*. Mimi Nakasema niseme kwamba kama ndege zisingekuwa *grounded* basi hasara ya *ATCL* ingekuwa kubwa zaidi; kwa sababu mashirika mengi ya ndege duniani yamepata hasara kubwa tu. Kwa hiyo, ni kwamba pengine lingepata hasara kubwa zaidi kwa sababu haya mashirika hayako *proactive* katika ku-*adjust to market changes.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi niseme hiki, hata nasikitika kwamba kuna kiongozi mmoja alisema kwamba anasikitika kwamba alibinafsishwa. Lakini kama asingebinafsisha tungekuwa wapi kama mashirika ndiyo yanajiendesha hivi? *TANOIL* tumesikia imefanya hasara ya bilioni saba. Kwa hiyo, takribani kila shirika ambalo linajiendesha kwa kusimamiwa na Serikali linamatatizo. Kwa nini Serikali isiingie ubia ikawezesha *private sector* kwa *management contract* kuendesha mashirika haya na wakaachana na haya mambo ya kufanya hasara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo linasumbua kwenye mashirika ya umma ni madeni. Mashirika ya umma yana madeni ya ajabu. Nilishangaa mimi, kwanza nilisoma nikasema ni bilioni au trilioni. Mashirika 11 ya umma ukichanganya yana madeni yanafikia jumla ya trilioni 27.5. Ni trilioni 27 siyo bilioni. Na haya ni yale mashirika yanayosemekana ni ya kibiashara. Sasa ukiongeza taasisi za Serikali ambazo hazitakiwi kufanya biashara na kupata faida, jumla ya madeni ni trilioni 5.2. Ukijumuisha inakuwa ni trilioni 32 kwenye mashirika ya umma, imekaa kwenye vitabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo tunalojiuliza ni hivi, ukichanganya hilo kwa sababu hata *extended public sector debt* unajumuisha ile ya Serikali ya *about 8 trillion* inakuwa ni *112 trillion*. Sasa hilo ni deni kubwa sana kwa sababu huwezi kusema kwamba madeni ya mashirika ya umma hayatalipwa *unless* kuna namna nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninachoshauri na ninaomba Bunge likubaliane ni kwamba, haya madeni ya mashirika ya umma yafanyiwe uchambuzi, tujue yametoka wapi na nani Aliya-*finance*. Je, kuna *transactions* au miamala ambayo imefanyika na Serikali Kuu? Kama ipo, je, kuna uwezekano gani wa kugeuza madeni haya kuwa ni mtaji wa hisa? Halafu vile vitabu vya mashirika haya vikawa angalau *a little bit clean*, na vikiwa vimesafishwa, hiyo *balance sheet* ikiwa imesafishwa ina maana kwamba mashirika haya kama yatakuwa yamegeuka kuwa mashirika ambayo siyo mabaya, basi pengine hata yanaweza kukopa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kimoja ambacho naomba tu-*encourage* mashirika ya umma yaweze kuchukua mikopo ya biashara, *overdraft* ili kuendesha biashara zao kwa gharama nafuu.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mimi naomba hiyo ifanyiwe kazi, na kama isipofanyiwa kazi tujue kwamba tunaweka mrundiko wa matatizo kwenye bajeti ya Serikali kwenye miaka hiyo inayokuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili la Mkulazi ni tatizo sana. Mkulazi imefanya *accumulative growth* kati ya 2020/2021 na 2021/2022 ya bilioni 20. *Astaghafiru-llah*, sasa inakuwaje? wenzake wamekuja nyuma, *Bagamoyo Sugar* imekuja wanaanza kufanya faida, hawa wanaendelea kupata hasara, hawajaanza hata biashara wanafanya mahasara. Mimi ninaomba Serikali iangalie namna gani ifanyike. Kama ambavyo nimeshauri, kwamba tuendelee sasa kuona namna. Kwa mfano, kampuni kama hiyo *immideately* ipewe *private sector* aiendeshe ili tuweze kuepukana na matatizo. *(Makofi/Vicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti,…

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa kengele imelia ya pili. *(Makofi)*

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, haya kumbe imelia ya pili. Naomba tu nitoe kahoja kamoja, yaani *one minute.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni mambo ya mifuko ya *pension.* Mifuko ya *pension return investment* yake iliyofanya ya *604 billion* kwa miaka hii miwili inayozungumzwa, imekuwa ni *0.4 percent*. Sasa *0.4 percent* ni kidogo sana ukilinganisha na *average return* kwa mifuko hiyo ambayo inatakiwa iwe *5 percent.* Kwa hiyo iko *4 percent ten times.* Sasa kama wangefanya biashara yao ya

uwekezaji sawa sawa hata wasingelia kwamba sasa ukwasi umepungua kwa sababu Serikali haitoi michango yake na kadharika; wangepata fedha za kutosha kwenye uwekezaji. Kwa hiyo, mimi nasema kweli, nawaomba wale wanaosimamia mifuko hii wajiangalie upya kwa sababu *0.5 percent* kwenye *return on asset* ni haiwezekani *(Makofi/Vicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, basi naunga mkono tena na Mungu atujalie wote tuishi na mashirika haya. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei. Nilimtaja Mheshimiwa Bakar Hamad Bakar, Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate na Mheshimiwa Haji Amour Haji, ajiandae.

**MHE. BAKAR HAMAD BAKAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili kuweza kuchangia ripoti hizi za Kamati tatu ambazo zimewasilishwa ndani ya Bunge letu leo asubuhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehma; ambaye ametuwezesha kuwa wazima na afya njema na kuweza kukutana hapa katika kutekeleza majukumu yetu mbali mbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ripoti hizi ambazo zinasomwa na hoja hizi ambazo tangu asubuhi leo zinaendelea kutolewa hapa zinaonyesha mapungufu mbalimbali yaliyomo ndani ya Serikali yetu. Si kwamba Serikali yetu haifanyi kazi, tunaamini kwamba Serikali yetu inafanya kazi nzuri na mama yetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anafanya kazi nzuri sana. Tunaendelea kumpongeza na kumtakia afya njema ili anendelee kuwatumika Watanzania kwa umakini sana na kuendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazungumzia dosari hizi ili Serikali yetu iendelee kufanya kazi vizuri zaidi; iendelee ku-*perform* na iendelee kukusanya fedha za umma na kusimamia fedha za umma

ili kuweza kutekeleza miradi kwa kasi na pia, kuwatumikia Watanzania kwa weledi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yako mapungufu mbalimbali ambayo yamebainishwa na ripoti za *CAG*; nami nitazungumzia machache. Kwanza nitaanza kwenye bohari ya dawa *(MSD)*. Tarehe 12 Oktoba, ya mwaka 2021 *MSD* iliingia mkataba na kampuni ya Misri ya Alhandasya. Mkataba na kampuni hii ulikuwa ni kwa ajili ya kusambaza dawa na vifaa tiba kwa *items* 75.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkataba uliingiwa tarehe 12 mwezi wa kumi, lakini malipo kwa ajili ya kazi hiyo yalifanyika siku moja kabla ya mkataba kuingiwa. Kwa maana tarehe 11 Oktoba *MSD* walimlipa Alhandasya bilioni 3.4 *advance payment* kwa ajili ya kazi hiyo. Tunaona hapa kwanza tu kuna jambo huko mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Alhandasya Kampuni ya Misri, kampuni hii ilishindwa kutekeleza jukumu lake wakati tayari imeshalipwa 3.4 bilioni, na ikatoweka na fedha hizo mpaka leo fedha hizi hazijulikani ziko wapi na hawa Alhandasya hawajulikani hata walipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *MSD* walipofuatilia, Alhandasya kule Misri kupitia mabalozi wetu kule walishindwa kuipata kampuni hii. Kwa maneno mengine ni kusema kwamba kampuni hii ilikuwa ni kampuni hewa; kwa maana haipo na fedha hizi za umma zaidi ya bilioni 3.4 zimelipwa na zimepigwa, hazipo tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchato huo na Alhandasya kushindwa kutekeleza majukumu yake *MSD* walimpata mkandarasi mwingine; kampuni nyingine ambayo inaitwa *EIPICO* ambapo yeye alikubali kuweza kusambaza vifaa tiba na kupewa mkataba mwingine wa kuweza kufanya kazi na *MSD*. Hapo ndipo na yeye alipopewa mkataba wa bilioni 10.8 kuweza kusambaza vifaa mbalimbali kwa makubaliano kwamba ataanza kusambaza vifaa ambavyo alipewa Alhandasya; ambazo zilikuwa ni *item* 75. Ndani ya

*item* hizo 75 kwa mkataba huo, pia na yeye huyo *EIPICO* alisambaza *item* 12 kwa fedha ileile ya 3.4 bilioni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaona haya ni mapungufu makubwa na madhaifu makubwa ndani ya Serikali yetu. Tunaiomba sana Serikali iweze kusimamia mikataba hii na iweze kufanya kazi hizi kwa ufanisi mkubwa. Hizi fedha ni nyingi sana kwa ajili ya kuweza kuwatumikia Watanzania. Tunazo shida na changamoto nyingi sana, sasa unapoona mambo haya yanatokea ndani ya Serikali, ni kuitia doa Serikali yetu na ni kumtia doa Mheshimiwa Rais wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais wetu ana nia ya dhati ya kuwatumikia Watanzania lakini mambo haya ambayo yanatokea ni mambo ambayo yanendelea kumtia doa Mheshimiwa Rais wetu. Tunaiomba sana Serikali isimamie mikataba, isimamie fedha za umma kama vile Bunge linavyotaka, kama vile Bunge lilivyoidhinisha fedha hizi ndani ya bajeti ambayo inaendelea na tumeipitisha hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizi ambazo zililipwa, zililipwa kinyume na taratibu. Kwanza, hakukuwa na dhamana kutoka kwa benki ambayo ililipwa lakini pia, hakukuwa na dhamana ya utendaji kazi wa hizo kampuni ambazo zimelipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya mambo yanatokea hapa hapa Tanzania na hawa hawa Watanzania ambao wanalalamika ndio hao hao ambao wanamkwamisha Mheshimiwa Rais wetu. Kwa hiyo, tunaomba sana kuweza kufanyika marekebisho makubwa ndani na kusimamia fedha hizi za umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye jambo lingine. Kuna nakisi ya ukusanyaji wa kodi wa zaidi ya bilioni 887 ambazo hazikukusanywa kutokana na mambo mbalimbali na changamoto mbalimbali zilizoko pale *TRA* na kila siku tunakuwa tunapiga kelele kuhusiana na mifumo ya ukusanyaji na usimamizi wa fedha za umma zilizopo pale *TRA*…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. BAKAR HAMAD BAKAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaiomba sana Serikali, fedha hizi ni nyingi sana. Kwa mfano kuna mafuta ambayo yaliingizwa nchini kwa ajili ya kusafirishwa kwenda nchi nyingine lakini mafuta hayo hayakusafirishwa kwenda nchi nyingine na badala yake yalitumika ndani ya nchi na kuisababishia Serikali kukosa kodi stahiki kwenye mafuta hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya mambo yanatokea hapa na sisi tupo na wasimamizi wa mambo haya Maafisa Masuuli wapo. Kwa hiyo tunaiomba sana Serikali iweze kurekebisha mifumo ya ukusanyaji wa mapato na kuweza kusimamia zaidi ukusanyaji wa mapato ndani ya nchi yetu ili kuweza kufanikiwa zaidi kwenye utekelezaji wa majukumu yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mchakato wa ajira *BOT*. Pia ni moja kati ya mambo ambayo *CAG* alibainisha, *BOT* walitangaza ajira kwa utaratibu wa kawaida na Watanzania walio wengi ambao wana sifa ya kuomba ajira zile, waliomba, lakini cha kushangaza ni kwamba baadaye katika mchakato baada ya Watanzania kuomba, katikati ya mchakato walibadilisha sifa huko ndani kinyume na utaratibu, kinyume na sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu na sheria inasema kwamba, ajira kwa maana ya Watanzania wanatakiwa kuajiriwa chini ya miaka 45, lakini *BOT* walikwenda kubadilisha hiki kipengele cha umri kutoka miaka 45 wakasema mwisho miaka 30. Tunajiuliza ni kwa nini kipengele hiki cha umri kisiingizwe kabla ya mchakato wa ajira kuanza, kwa nini hakikuwemo ndani ya zile sifa ambazo zilibainishwa pale awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwenye hili tunaona kulikuwa na mkakati makusudi wa kuwakosesha baadhi ya Watanzania fursa hizi za ajira na kuweza kuwanufaisha baadhi ya watu ambao inawezekana wanajulikana. Haya ni malalamiko na changamoto hizi zipo kwa muda mrefu kwamba *BOT* na taasisi

zinazofanana na hizi kuwa watu wanaoajiriwa ni watu ni wa wakubwa ambao wanajulikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapungufu haya ni makubwa ambayo yanaisababishia Serikali yetu doa kubwa na tunaiomba sana Serikali iweze kujirekebisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naunga mkono mapendekezo yote ambayo yametolewa na Wenyeviti wetu hapa kwenye Kamati zetu tatu. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Bakar Hamad Bakar. Nilimtaja Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate, Mheshimiwa Haji Amour Haji na Mheshimiwa Condester Michael Sichalwe, ajiandae.

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi jioni hii kuchangia hoja iliyoko mezani. Kwanza naunga mkono hoja zote tatu, naomba Serikali ichukue hatua kwa sababu mengi yaliyoainishwa na Kamati zote ni ukiukwaji wa Sheria za Manunuzi na ukiukwaji wa taratibu za fedha kwa makusudi ili kujinufaisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye suala hili, nitaenda moja kwa moja kwenye Manunuzi ya Umma Sheria, Sheria Na. 410 ambayo kwa taarifa ya *LAAC* imeonesha Serikali kupata hasara ya zaidi ya shilingi 106,799,578,781. Ukitaka *details* nenda kwenye ukurasa wa 19 wa taarifa hii mpaka ukurasa wa 20. Kurasa hizo zinaeleza namna ya Serikali ilivyopoteza fedha hizi ambazo Dkt. Mama Samia Suluhu Hassan, ambaye ndiye Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ametoa fedha nyingi kupeleka kwa ajili ya miradi mbalimbali kwenye Halmashauri zetu, lakini watumishi ambao sio waadilifu wanataka kumuangusha kwa kuzitumia fedha hizi nje ya utaratibu na kazi zake nyingi hazijakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye suala hili hatuwezi kukwepa kwa kulaumu *force account*. *Force Account* kwenye maeneo mengi ya Halmashauri yetu imeshindwa kukidhi haja ya matumizi kwa

makusudi na sio kwa bahati mbaya. Mwongozo unaeleza wazi kabisa namna *force account* inavyotakiwa kutumika; moja lazima Kamati ziundwe, Kamati zile na wataalam wapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati mbaya zile Kamati zimekuwa kama kiini macho katika maeneo mengi ambayo tumepita, kwa sababu majukumu yao hawafanyi kama ilivyoelekezwa kwenye mwongozo, kwa mfano, Serikali imepoteza zaidi ya shilingi 1,510,000,000 kwenye Halmashauri zetu kwa sababu ya kufanya malipo ya pesa taslimu kwenye mfumo huu wa *force account* bila kufuata utaratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili jambo sio kwamba la bahati mbaya ni la makusudi kwa sababu Sheria ya Fedha inataka fedha yote ilipwe kupitia akaunti za wazabuni, lakini kwa kuwa wamekusudia kufanya hivyo basi wamelipa kwa taslimu ili kuepusha kutokupatikana fedha hizo kwa njia za vichochoroni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye *force account* wataalam wetu wanahusika na mara nyingi wanakwepa Kamati hizi ambazo zinahusishwa na wananchi wenyewe chini bila kufanya vikao ambavyo vinatakiwa kwa mujibu wa muongozo. Wakati mwingine wananchi Kamati zile wanaletewa bidhaa ambazo zimenunuliwa juu kwa juu, maana yake juu kwa juu wao wanaandika *cheque* huko huko, wanaandika muhtasari huko huko, wanasaini wenyewe kama Wajumbe wa Kamati, wananunua *then* wanaenda chini ambako ndiko waliko watekelezaji wa miradi wanawaambia andika *check* tunamlipa mtu fulani bila wao kuhusishwa kwenye mchakato mzima wa manunuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili jambo limesababishia Serikali hasara kubwa sana kwenye *force account* kwa maana ya kwamba ukamilifu wa miradi hii matokeo yake haikamiliki kwa ukamilifu na utakuta miradi mingi imeacha bidhaa nyingi ambazo hazina matumizi. Cha ajabu TAMISEMI wanatoa muongozo wa namna ambavyo miradi ile inatakiwa kutekelezwa kwa maana ya *BOQ*

ambayo imeandaliwa na TAMISEMI, ambako kuna ma-*engineer* na ma-*professor*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda chini kwa watu wetu wa chini kuna Wahandisi ambao wamesoma zaidi, ambao wana-*crush,* wanaweka makisio ambayo yanazidi yale ambayo yametengenezwa na Wizara. Mfano mdogo sana, kwenye jimbo letu la Tunduru Kusini tukitumia mapato ya ndani, darasa moja tunajenga kwa milioni 12.5 pamoja na madawati, lakini Serikali inapeleka milioni 24. Darasa lile utakuta linafanana na lile la milioni 12.5, hakuna marumaru, hakuna kitu chochote. Hili jambo linafanya kwamba wenzetu Wahandisi wanaona kwamba pesa zinazoletwa na Mama ni kama zawadi kwa upande wao kwa kujinufaisha badala ya kuwanufaisha wananchi wetu kule chini ambao ndiyo wana shida kubwa ya madarasa, madawati, zahanati pamoja na vituo vya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hili jambo, Halmashauri nyingi sana zimepata hasara katika mfumo wa ununuzi wa magari. Halmashauri zinaomba ununuzi wa magari *GPSA*, wanalipa pesa ambayo *invoice* yake inasoma kutoka *original* ya gari ni kutoka Japan, pesa wakilipa wanakaa zaidi ya mwaka mmoja au miaka miwili. *CAG* ameona namna ambavyo Halmashauri zinapata hasara, pesa ile inakaa kule haina riba lakini wanaenda kule kuletewa magari, magari yale badala ya kuwa *original* Japan, gari hili linakuwa *original South Africa* ambapo sisi wote tunanunua magari humu ndani, gari lililotengenezwa *South Africa* hata liwe Toyota na lililotengenezwa Japan bei zake ni tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati mbaya zaidi katika utofauti wa bei, hakuna Halmashauri yoyote ambayo imerejeshewa zile tofauti. Jambo hili Serikali iliangalie kuna jipu kwenye *GPSA*, kwa sababu ya manunuzi ya magari ya Halmashauri ambayo yanakaa kwa muda mrefu bila kurejeshewa na kupelekewa magari ambayo ni tofauti na ile *invoice* ambayo wameipeleka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine matumizi ya *POS*. *POS* ni nzuri sana katika kukusanya pesa bahati mbaya katika taarifa iliyotolewa na *CAG,* pesa nyingi zinakusanywa lakini hawazipeleki benki. Hili halifanywi kwa bahati mbaya, hawa wengi ni mawakala na wengine ni watumishi wa Halmashauri, lakini hawapeleki benki. Hili matokeo yake Wakurugenzi wanatumia kichaka hiki kuwapeleka *PCCB* hawa watu wanaokusanya hizi pesa ili kuendelea na mtindo wa kuchukua pesa bila kupeleka benki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatakiwa ichukue hatua kwenye jambo hili, kwa sababu limekuwa ni donda ndugu, sisi wataalam tunasema wanakula pesa mbichi. Matokeo yake Halmashauri inakusanya pesa nyingi, zinaishia mifukoni mwa watu na hazifanyi kazi zilizokusudiwa kwa ajili ya maendeleao ya watu wetu tunaowahudumia. Kwenye hili nalo Halmashauri zetu zimeshindwa kukusanya zaidi ya bilioni 37.34 kutokana na vyanzo vyao vya kila siku na vyanzo hivi vinaeleweka, kuna kodi ya vibanda vya masoko, stendi hizi zote zinakusanywa, lakini haziendi benki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mwingine hata mikataba ya hivyo vibanda vya Halmashauri hawana na wakati mwingine mikataba hii imeisha na wakati mwingine mwenye leseni na mwenye mkataba kwenye vibanda hawaeleweki, kumbe wakati mwingine wafanyakazi pamoja na Madiwani wetu ndiyo wanaomiliki hivi vibanda, matokeo yake anapangishwa mtu mwingine, Halmashauri inapata hela kidogo. Mbaya zaidi kuna Halmashauri zimekosa hata rekodi ya vibanda walivyokuwa navyo, kwamba wana vibanda 100 wanatakiwa kukusanya Sh.50,000 kwa mwezi utapata milioni tano, lakini wao hizo taarifa hawana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa *CAG* ameliona hili, Serikali kwa maana ya TAMISEMI tulichukulie *very serious* kwa kuwachukulia hatua hawa wote ambao wanafanya mitindo hii, sio kwa bahati mbaya ni kwa makusudi ili wajinufaishe na Halmashauri zetu zinabaki kuwa tegemezi kutokana na mapato yao kuliwa na watu ambao sio watarajiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache naunga mkono hoja na naiomba Serikali, *wote waliohusika kwenye hizi takataka zinazoonekana huku ndani* **[Maneno haya siyo sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

...wachukuliwe hatua, hiki kitendo cha kutokuwachukulia hatua ndiyo maana kila siku *CAG* anaandika yaleyale.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Daimu, naomba ufute maneno ya takataka.

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nafuta kauli hiyo, ni kwamba hivi vitu ambavyo vinafanyika vya hovyo. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Malizia, muda wako umeisha.

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, aAhsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Sasa ni zamu ya Mheshimiwa Anatropia Theonest, Mheshimiwa Haji Amour Haji, Mheshimiwa Condester Michael Sichalwe, ajiandae.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nami niongeze machache ambayo Kamati yetu imeweza kuyaona wakati tukipitia hizi ripoti. Nitaanza kwa kuvuta kumbukumbu ya taswira ya Mheshimiwa Rais, siku napokea Ripoti ya *CAG* nitaenda kunukuu maneno aliyoyasema na kila mmoja aliyasikia na vyombo vyote vya habari viliandika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaanza kusoma, anasema; "*Invoice* imekuja tunatakiwa kulipa dola milioni 88 unaliza mkataba ulisemaje, hii imetokea wapi? Unaambiwa vifaa vimepanda. Nauliza Mkataba wenu ulisemaje? Mtu anapopokea bila kuuliza, anailetea Serikali ilipe, *stupid!*"

Mheshimiwa Mwenyekiti, aliendelea kati ya maneno mengine aliyoyasema; "Miradi mingine ambayo tunaifanya inakuwa ni mikubwa ambayo matazamio yake yanajulikana." Akauliza maneno na akasema; "oneni uchungu na fedha za Serikali, na hivyo vinafanyika kwa sababu kuna watu wanafaidika." Akaenda mbele zaidi akasema; "Kuna sehemu tumezubaa, pengine kwenye *primitive measures,* hatuchukui hatua." Mwisho wa kunukuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeanza na hayo maneno kwa sababu siku hiyo Mheshimiwa Rais, anawasilisha hotuba niliangalia vizuri na nilimwangalia. Nikaona picha ya mama akionyesha machungu ambavyo anatambua ukubwa, utajiri wa rasilimali zilizopo kwenye nchi lakini zinapigwa na watu wachache. Kamati yetu ya *PAC* kama ilivyopitia *LAAC*, tumechukua masaa ya kutosha kukaa, kujadili zile ripoti na baadaye tunajiuliza tuweke nini, tuache nini, kwa sababu ni madudu bandika bandua. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya waliyoyataja wenzetu ni baadhi tu, lakini changamoto yetu kubwa haijawahi kuwa kwenye mifumo, haijawahi kuwa kwenye utaratibu, imekuwa kwenye kitu kimoja ambacho nimekitaja na kukiandika mara tatu, nikasema kutekeleza, kutekeleza kutekeleza. Utaratibu umeandikwa na umeainishwa vizuri, utaratibu wa kuingia, kuhama, kuheshimu na kutimiza matakwa ya Mikataba, tumekuwa hatufanyi hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu umeainisha nini cha kufanya, lakini Watendaji wetu wameacha kufanya yote tunayoyasema. Msemaji mmoja hapa ametueleza kilichotokea katika *MSD* nitatoa mfano na nitaueleza vizuri. Mtendaji na baadhi ya waliohusika kwenye *MSD* waliingia kwenye Mkataba na Kampuni moja ya kutoka Misri, ameitaja mwenzangu inaitwa *Alhandasia* ya kunua vifaa tiba. Ikatanguliza fedha zaidi ya bilioni 3.4 ika-deposit kwenye akaunti, akaunti inajulikana ambayo naweza nikakutajia hapa, ambayo jina la Akaunti inaitwa *ASM e-trade*, akaunti namba iko hapo 0045609416002 iko kwenye Benki ya *Egypt Gulf*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya ku-*deposit* hizo fedha akijua moja ana-*deposit* hizo fedha bila ya kuona, ameshinda kandarasi, anapaswa kuonyesha *at list* uwezo wa ku-*perform* hizi *contract,* hajafanya hicho kitu, lakini pia hajafanya utafiti kuja kama ana-*exist* au ha-*exist* kwa maana hapati *assurance* ya benki, lakini ame-*deposit* zaidi ya bilioni tatu kwenye akaunti ya mtu. Wakasubiri zaidi ya miezi mitatu madawa hayaletwi. Wakaanza kui-*consult* hiyo kampuni inapatikana wapi, wakamtumia taarifa balozi wetu Misri, akatafuta hiyo kampuni haikujulikana kampuni iko wapi. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo kampuni kwa fedha ambayo wali-*deposit* ambayo ni bilioni 3.4, tulipaswa kupata aina 75 za madawa tofauti tofauti. Baada ya mkataba kushindikana ikabidi wa-*recall* kampuni nyingine na hiyo kampuni wakaiambia sasa tusaidie kuchukua hata yale madawa ambayo alipaswa kuleta huyu *Alhandasia*, tukuongezee kwenye Mkataba uweze ku-*delivery* akakubali kufanya hivyo. Sasa wakampa mkataba wa bilioni 10, lakini katika ku-*delivery* akaonyesha katika zile *product* ambazo alipaswa ku-*delivery* 75 katika hizo ame-*delivery product* 29 tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa unaweza ukaona nini changamoto ambayo ameieleza mwenzangu. Tulifanya nini, tulifanya *due diligence* kujihakikishia kwamba hiyo kampuni ina-*exist*, tulikuwa na *assurance performance* ya *contract* na wale watu, hayo ndiyo yanafanyika katika kila item ambayo naigusa hapa. Changamoto ya hii nchi siyo fedha wala siyo uchumi, changamoto ni watendaji ambao wameamua kwa makusudi mazima bila kufuata kanuni na taratibu. Mheshimiwa Rais, akasema tumewanyamazia pengine tuchukue *primitive measures,* tuweze kuwawajibisha na nataka niulize hapa ni wangapi wamewajibishwa kwa kuisababishia Serikali hasara ya mabilioni ya fedha yanayoongelewa leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa tukiona kwenye vyombo vya Habari, mtu ameiba zaidi ya bilioni kadhaa, trilioni kadhaa, lakini faini anayokuja kutozwa ni milioni kadhaa na umeshakuwa mtindo wa kawaida tu, iba bilioni utaenda kulipa faini ya milioni, hauwezi

kuwa ndiyo mtindo wa maisha na tukaenda, hatutofika kokote kwa mtindo huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hiyo haitoshi wakagundua chaka lingine na Mheshimiwa Mwenyekiti wa *LAAC*, ameieleza vizuri, kuna chaka linaitwa TAKUKURU. Sasa siwezi kueleza chochote kwa sababu sijui, lakini kwa mazingira yanayoonekana TAKUKURU ndiyo namna pekee ya watu kuficha madudu yao kwa sababu wanajua tutakagua kwa zaidi ya miaka 10, 15 na baadaye ushahidi utakosa na faili litafungwa na *business as usually*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hiyo tu, miradi mingine ambayo imekuwa kwa Watumishi wa Umma ambayo wameisababishia Serikali hasara ni kuhamishwa katika hiyo idara hata haya tunayoyaongelea leo kwenye *MSD* wamehamishwa kutoka *MSD* wakapelekwa kwenye idara nyingine, hivi hilo lengo ni nini? kupeleka hasara kwenye maeneo mengine au kuendeleza kutuliza kila sekta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais, anazunguka kila sehemu kutafuta fedha, anahangaika na tozo kila maeneo, lakini kinachofanyika leo ni nini? Ni mifuko yote inavuja asubuhi, mchana na jioni, hatuwezi kwenda namna hiyo. Hivyo naungana na Hotuba ya Kamati zote tatu, pamoja na Kamati yangu hususani juu ya pendekezo la *MSD*, moja TAKUKURU kukamilisha uchunguzi, lakini pia ni lazima kuwepo na *action* za kimaadili kama kuna watu wamefanya makosa kwenye Serikali…

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**TAARIFA**

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana mchangiaji lakini naomba nimpe taarifa kwamba, wahusika waliohusika na ubadhirifu au uvunjaji wa taratibu za manunuzi chini

ya *MSD* wameondolewa kabisa *MSD* Tarehe 22 Aprili, 2022. Mheshimiwa Rais aliteua Mkurugenzi mpya na sasa hivi mambo yanaendelea vizuri taratibu zilizobaki ni za kiuchunguzi wa TAKUKURU na vyombo vingine vya uchunguzi. Hatua zimeshachukuliwa tangu Aprili, 2022.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Anatropia unaipokea hiyo taarifa?

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Bahati mbaya sana kwenye Kamati ambayo Mheshimiwa Spika alinipanga tunaongelea *value for money*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukimwondoa katika nafasi yake ume-*save* shilingi ngapi, nadhani hoja ziwe baada ya ule ubadhirifu alivyovifanya tumeweza kuangalia alikuwa ana kiwango gani ambacho tumekiweka wakati kesi zikishughulikiwa, fedha za walipa kodi ziweze kuwa zimeokolewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nadhani hiyo iwe *spirit* kwa sababu lengo ni kusaidia Taifa na lengo la Mheshimiwa Rais ni kuhakikisha anapata fedha za kuendesha nchi. Pia watu wanauliza alipelekwa wapi, karudishwa Jeshini kuendelea kufanya kazi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee pia suala la *KADCO* najua muda wangu utakuwa mchache lakini nilikumbushe Bunge lako tarehe 2 Novemba hapa mwaka jana iliongelea suala la *KADCO* pamoja na kutoa maazimio ambayo maazimio ya *KADCO* ni pamoja na *KADCO* kuwa chini ya Mamlaka ya *TAA* lakini hilo suala mpaka leo halijaweza kufanyiwa kazi, lakini hiyo haitoshi Baraza la Mawaziri lililokaa katika Kikao Namba 15 cha mwaka 2009 liliwahi kutoa maazimio ya kiwanja cha ndege cha Kilimanjaro kuwa chini ya *TAA* lakini mpaka leo tunavyoongea miaka 14 baadae hakuna chochote kilichofanyika. *Call* yetu tunayoitoa ni lazima *KADCO* sasa iende kwa mujibu wa utaratibu unavyosema kwamba viwanja vya Serikali vitaendeshwa chini ya mamlaka ambazo zimeanzishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niishie hapo kwa hayo machache. Ninaunga mkono maazimio yote yaliyotolewa na Kamati yetu Tukufu. Nakushukuru sana *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Anatropia Theonest. Nilimtaja Mheshimiwa Haji Amour Haji, Mheshimiwa Condester Michael Sichalwe na Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane ajiandae.

**MHE. HAJI AMOUR HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii ya kuweza kutoa yangu ambayo yapo katika uchambuzi wa Taarifa zetu ambazo tunazijadili leo kuanzia asubuhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja katika taarifa ambazo tulizonazo tuna taarifa ya Mahesabu ya Umma, Taarifa ya *LAAC* na kuna Taarifa ya *PAC*. Mimi nadhani kwamba nijielekeze zaidi kwenye taarifa inayohusiana na Kamati ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Mjumbe ambae nipo katika Kamati ile ambayo moja kabla ya yote hayo nipende kumshukuru Mheshimiwa Rais, Mama Samia Suluhu Hassan kwa kuweza kuyajali mashirika yetu haya na kuweza kukaa nayo kwa pamoja kutafuta namna ya ufanisi na tija ya mashirika yetu alikaa nayo katika kikao kimoja pale Arusha, ambapo pale kulikuwa na mazungumzo mengi na kuweza kuyajenga yale mashirika kama ni semina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja katika shughuli ambayo tunaifanya katika Kamati ya Uwekezaji na Mitaji ya Umma ni kwamba kuangalia ufanisi wa mashirika yetu ya umma pamoja na tija yake. Tunavyojua kwamba moja katika vitu viwili hivi lazima kwamba vinakuwa vinaendana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye ufanisi au kukosekana kwa ufanisi maana yake kutakuwa kutakosekana kwa tija katika mashirika yetu. Katika taarifa zetu tulizozipitia katika mashirika yetu ya umma tumejaribu kuangalia mashirika mengi sana kwa sababu kwenye Kamati yetu ya Mitaji ya Umma tuna mashirika karibu 287

ambayo ndiyo tunatakiwa kuyajadili na kuyajengea hoja katika ufanisi na tija katika mashirika hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja kati ya mambo ambayo yalikuwemo katika mashirika yetu tumejaribu kuangalia tija pamoja na ufanisi wa mashirika yale, katika mashirika na tija ambayo ipo katika mashirika yetu yamejigawa katika makundi matatu. Kuna kundi la mashirika ya umma ambayo yanatoa gawio na kwa mujibu wa sheria, kuna makundi na kundi la mashirika ya umma ambayo yanatoa asilimia 15 na kuna kundi la mashirika ambayo yanatoa ziada na kuna kundi la mashirika ya umma yanatoa kwa mujibu wa vile ambavyo wanajihisi namna ya kutoa katika Serikali, ndicho ambacho tulikibaini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukilinganisha mlingano wa takwimu ya mwaka jana na mwaka huu wa fedha maana yake ukitizama katika mashirika yenye kutoa gawio kuna mashirika 66. Kwa mujibu wa taarifa ya Mwenyekiti wangu wa Kamati ya Uwekezaji wa Mitaji wa Umma, alitaja mashirika 66 ambayo kati ya mashirika 66, mashirika 25 tu ndiyo yaliyotoa gawio. Hiki ni kitu ambacho ukiangalia upande mwingine ukiangalia kwamba, ule ufanisi na ile azma ya kuweza kuyajenga yale mashirika yetu maana yake maana yake hayajafikiwa katika hali nzuri. Pamoja na kwamba mashirika 25 ndiyo yaliyotoa gawio na kupata shilingi 37,528.000.000 na kuendelea bado ukiangalia mashirika yote 66 yenye kutoa gawio maana yake hapo tungekuwa tuna fedha nyingi sana katika ukusanyaji wa mapato yetu. Kimsingi nitasema kwamba kazi bado tunayo ya kuweza kuifanya, maana yake hili ambalo tutasema kwamba mashirika 25 waliotoa na ukilinganisha mwaka jana maana yake mashirika haya kidogo tumejitutumua kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa mashirika yale yanayotoa asilimia 15 kwa kiasi fulani nayo si haba maana yake kwa sasa hivi yametoa karibu asilimia 70. Lakini kuna tatizo ambalo ni la kiutendaji na kiufanisi katika haya mashirika yetu, kwanza tulichokigundua katika mashirika yetu kuna kitu ambacho kimekuwa kinagomba kwa mashirika yetu. Kwanza hawaangalii namna ambavyo zile K.P.I

zilizowekwa na Msajili wa Hazina hawazizingatii ipasavyo, kwa sababu utakuta kwa mfano kama taasisi ya maji kwamba kigezo walichowekewa kwa mfano kama upungufu wa maji maana yake usizidi au katika umwagikaji wa maji maana yake usizidi asilimia 25. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, utakuta kwamba katika K.P.I zao maana yake wapo zaidi ya hapo. Kuna baadhi ya mashirika mengine maana yake hata ule utendaji wao unaonekana dhahiri kwamba hauko vizuri na kwa sababu kuna baadhi ya mashirika tumeyakuta katika hata ule mpango mkakati wao hauko vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tumelikuta hata shirika, kuna baadhi ya mashirika ambayo tumekuwa nayo tumelikuta hata ule mpango mkakati hakuna. Sasa katika kupima zile K. P.I maana yake utakuta shirika lile hujui hata ulipime namna gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niweze kumpongeza Msajili wa Hazina kwa jitihada zake kubwa ambazo anazozichukua katika namna ya kuweza kutafuta mwarobaini wa kuyafanya mashirika yetu yawe ya kibiashara, kwa sababu pamoja na yote hayo maana yake kuna mashirika ambayo wakati mwingine yanapatiwa ruzuku, lakini ile ruzuku wanayopatiwa maana yake hakuna tija yoyote inayorudi katika Serikali. Kuna mashirika yale ya kibiashara moja kwa moja maana yake yanafanya biashara zaidi ya zile ruzuku wanazopewa na Serikali yake hakuna kitu chochote. Ufanisi pale unakuwa unakosa na tija inakuwa haipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumegundua kwamba kuna baadhi ya mashirika hata wale Watendaji wake wa Bodi ukiwapima hawawezi kupimika. Mimi ninaiomba Serikali pamoja na yote hayo lakini kuna haja kubwa sana ya Msajili wa Hazina kuweza kukamilisha mchakato wake wa sheria ili waweze kuja hapa Bungeni lengo kubwa ni kuweza kuwahakikishia kwamba mashirika yetu ya umma yanafanya vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na yote hayo nasema kwamba nampongeza sana *TR* kwa kazi yake kubwa anayoifanya, nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kuweza kuyajali mashirika yetu na kwa namna ambavyo anavyokusudia kuyafanya kwamba yaweze kuleta ufanisi na tija. Natumai kwamba mabadiliko yoyote yatakayokuja ya sheria yatakayotoka kwa Msajili wa Hazina yatakuwa ni mabadiliko yenye kuleta tija na ufanisi kwa mashirika yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo naunga mkono hoja taarifa za Kamati zetu zote tatu ambazo zimewasilisha taarifa zao hapa,  Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Haji Amour Haji, nilimtaja Mheshimiwa Condester Michael Sichalwe, Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane na Mheshimiwa Venant Daud Protas ajiandae.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi. Kwanza nianze kabisa kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu wa nchi hii kwa namna ambavyo anafanya kazi vizuri na kwa namna ambavyo anaendelea kupambana kuhakikisha hata sisi ambao tunatoka Majimbo ya Vijijini tunapata pesa. Tunapata pesa kwenye miradi ya maendeleo, tunapata pesa ambazo zinaendelea kuwasaidia wananchi kwenye shughuli mbalimbali, hata wananchi wa Momba nitumie fursa hii kusema tulivyokuwa jana si ndivyo tulivyo leo.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya *PAC* ambayo kwenye kitabu hiki kimesheheni mambo mengi sana. Katika kipindi ambapo nilipata nafasi ya kusikiliza uwasilishaji wa *CAG* katika Taasisi mbalimbali ambazo zilikuja kututembelea kuna baadhi ya mambo nikajifunza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimegundua kwamba Mheshimiwa Rais anafanya kazi kubwa sana kwa kujitoa kwa huruma, kwa weledi na kutamani kuisaidia jamii yake na kama Mama amedhamiria

kuona ule uchungu wa Mama kwa ajili ya kuwasidia Watanzania, lakini kuna baadhi ya mambo nikaona kwamba mimi ni Mbunge natokana na Chama cha Mapinduzi, Serikali ya Chama cha Mapinduzi haina wapinzani, wapinzani ni baadhi ya watendaji wa Serikali ambao siyo waaminifu kwa dhamana ambayo wamepewa ndani ya Serikali, wao ndiyo wanawaumiza Watanzania wenzao kwa nafasi ambazo wamepewa lakini wao ndiyo wanamfanya Mheshimiwa Rais apate do ana Watanzania wakati mwingine wamlaumu ilihali walipaswa kulaumiwa wao.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaanza kuchangia ripoti ya Kamati yangu ya *PAC* nikaangalia kwenye ripoti ya Kamati ya watu wa *LAAC*, asilimia 10 ya Halmashauri, Serikali ilidhamiria kuwasaidia wananchi wa kawaida vijana ambao hawawezi wakakopesheka, wakina mama na maskini watu wenye ulemavu ili waweze kusaidika, lakini angalia shilingi bilioni 5.6 hazikuweza kupelekwa kwenye huo Mfuko, shilingi bilioni 1.7 hazikuweza kupelekwa kwenye huo Mfuko kwenye baadhi ya Halmashauri. Jambo la kusikitisha shilingi bilioni 88.42 hazikuweza kurejeshwa kwenye huo Mfuko! Bilioni 88 hivi kwanini hizi pesa hata zisingepelekwa hata kwenye zahanati? Watanzania wanakufa huko vijijini, kuna vijiji havina zahanati, hakuna vituo vya afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumemsikia jana Waziri wa Afya akiwa anaongelea vyanzo vya kupata pesa kwa ajili ya kuwezesha Mfuko wa Bima kwa Wote, hizo pesa si zingeweza kuwasaidia Watanzania. Kwa hiyo, nikagundua Serikali ya Chama cha Mapinduzi haina mpinzani wapinzani ni baadhi ya watu waliopo ndani ya Serikali wameshindwa kutumia nafasi zao vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais wakati anapokea hotuba ya *CAG* kama ambavyo ameongea Mjumbe mwenzangu wa Kamati, aliongea kwa uchungu sana. Nae kama Kiongozi wa *State* na yeye kama Mheshimiwa Rais wetu yeye mwenyewe alionyesha kuchukizwa na baadhi ya mikataba ambayo inafanywa na watu wasiokuwa waaminifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende kwenye shirika moja hapa la *TRC* kwenye *SGR,* naomba nisome kidogo tu. Kwenye *SGR* kwenye kipengele kidogo ambacho kinasema dosari mbalimbali zilizobainishwa katika ununuzi wa vichwa na mabehewa ya treni. *TRC* ilikataa zabuni mara mbili kwa ajili ya manunuzi ya vichwa vya treni ya umeme na mabehewa ya abiria ambapo mzabuni aliye na bei ya dola za Kimarekani 263,460,514 alikataliwa kufanya manunuzi yasiyo na ushindani kwa dola za kimarekani ikapelekea kufika dola za Kimarekani 478,507,468 iliyosababisha ongezeko la gharama dola za Kimarekani 215,046 ambapo ni sawa na pesa za Kitanzania bilioni 550.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa na-*convert* hapa kwenye vituo vya afya ni vituo vya afya 1,100 maana yake Jimbo langu lote la Momba lingekuwa limeshapata vituo vyote vya afya, Mkoa mzima wa Songwe na Mikoa mingine yote ambayo ipo hapa Tanzania ingekuwa imepata kwa sababu tu kuna mtu hakufuata utaratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa najiuliza swali huu utaratibu je, ni Mheshimiwa Rais ndiyo anawatuma wafanye hivi? hawa ni watu wasio waaminifu ambao wamepewa dhamana, wameaminiwa na wanajificha kwenye kichaka cha dhamana ambazo wamepewa wanasahau kwamba wanaumiza Watanzania wenzao. Kwa nini wasifuate utaratibu, Kanuni na Miongozo kama ambavyo *CAG* mwenyewe anasema kwamba yapo baadhi ya mambo ambayo tunayapata ni watu kwa kutokufuata utaratibu, Kanuni na maagizo ndiyo yanatupelekea hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea hapo hapo kwa *SGR*, katika mkataba wa manunuzi wa *locomotive* na mabehewa ya abiria yaliyotumika, *TRC* ilitelekeza mkataba wa bila dhamana ya tendaji kazi hali iliyosababisha hasara ya *Euro* 5,520,400 ambayo ni sawa sawa na bilioni 13.7 za Kitanzania, nikaweka kwenye vituo vya afya ni vituo vya afya 28.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ilitokana na Mkandarasi kushindwa kutekeleza mkataba na *TRC* kushindwa kutoza gharama zilizotokana na uvunjifu wa masharti ya mkataba. Anaendelea anasema Mkandarasi alidai sababu hizo zilikiuka kanuni hivyo vitu kama hivyo. Mheshimiwa Rais siku anapokea hotuba yake ya *CAG* aliongelea mambo kama haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea tena…

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. CONDESTER MICHAEL SICHALWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Reli *TRC,* Mheshimiwa Waziri utapewa nafasi ya kujibu, shirika la Reli la Tanzania …..

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Condester naomba usubiri kuna taarifa usuburi, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**TAARIFA**

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka tu kumkumbusha msemaji Dada yangu ambae anaongea vizuri sana, kwanza kwa hoja ya kwanza aliyoizungumza na *cancellation* kwamba unapobadilisha Mkandarasi wa kwanza na wa pili na bei ikitofautiana kuna *factor* nyingi. Moja kuna teknolojia, mbili kuna wakati ulipofikia awamu ya kwanza na awamu ya pili. Pia kwenye hoja yake hii ya pili anayoizungumza sasa hivi ambayo kimsingi alikuwa ameshaanza kuizungumza vizuri, tunazungumza hapa tulikuwa tumeshazunzumza haikufanyika ni kwa sababu hakukuwa na *performance* iliyo-*guarantee* ndiyo maana hakupewa, kwa hiyo hakukuwa na hasara iliyotokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri Taifa likafahamu kwa sababu isije ikajengeka hoja kwamba ilifanyika manunuzi tukapata hasara bilioni 13, haikufanyika na sababu mojawapo kwa nini haikufanyika

na haikufika mwishoni ni kwa sababu hapakuwa na hiyo *performance guarantee,* kwa hiyo nilitaka kuiweka vizuri hiyo *statement*. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Condester unaipokea hiyo taarifa?

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, siipokei. Mimi ni Mjumbe wa Kamati na *Management* ya *TRC* ilikuja ikahojiwa nilikuwepo kwenye Kamati na *Hansard* zipo, kwa hiyo najua ninachokifanya na hiki ninachokisoma mimi ni taarifa ya *CAG* siyo mimi, siyo taarifa yangu kutoka Momba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea. Shirika la Reli Tanzania - *TRC* lilimwomba Balozi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Nchini Uturuki kufanya uchunguzi wa kina *due diligence* kuhusiana na kampuni ya *Eurowagon* juu ya ununuzi wa vichwa viwili na mabehewa 30 ya abiria ili waendelee kufanya hii shughuli. Jambo la kusikitisha ni *TRC* waliendelea na shughuli hii pamoja na Mheshimiwa Balozi kuwafanyia *due diligence* kuwaambia kwamba kampuni hii haifai lakini wakaendelea kufanya. Sasa swali tunajiuliza Mheshimiwa Balozi yupo nchini kule, anatumia pesa zetu za kodi na yupo kwa ajili ya hiyo kazi, anataka kulisadia Taifa lakini bado waliokuwa wamemwomba wakakataa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *imagine* tunaenda wapi, *imagine* yaani mtu kateuliwa na Mheshimiwa Rais, halafu hawataki, hawa ndiyo wapinzani wa Serikali ya Chama cha Mapinduzi. Ninaendelea anasema kampuni hao *Eurowagon* haikuwasilisha dhamana ya utendaji kazi *(performance security)* licha ya kukumbushwa mara kadhaa na Shirika la Reli Tanzania *(TRC)*, Shirika la Reli Tanzania liliendelea kutekeleza mkataba huo pasipokuwa na dhamana ya utendaji *imagine* na hivyo kupelekea hasara, anasema Shirika la Reli Tanzania *TRC* haikutoza *Euro* 2,260,000 hivyo kupelekea hasara ya *Euro* 5,520,400 hapa nime-*convert* ni bilioni 14 za kitanzania sawa na vituo 24 ya afya Watanzania wangekuwa wamevipata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kusema nini, wapo viongozi wa juu ambao nia yao ni njema wanataka kulisaidia Taifa, mpango wao ni mzuri ndiyo huo ambao Mheshimiwa Rais alionao mzuri. Lakini wapo wachache ambao wameaminiwa ni wataalam Mheshimiwa Rais amewaamini, ni wabobezi wa kufanya hayo mambo, badala watumie utaalam wao kulisaidia Taifa, kutusaidia Watanzania ambao labda sisi hatujui, wanatumia dhamana yao na utaalam wao vibaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, inawezekana hawa watu pia wamesomeshwa kwa mkopo wa Serikali, hawa nikuambie ni wahujumu uchumi kama wahujumu wengine tu ambapo zipo sheria ambazo watu wakikosa makosa kidogo tu wanachukuliwa hatua, kwanini hawa hawachukuliwi hatua, kwa nini? *CAG* kwa nini kaandika hiki? Kwa nini alileta kwenye Kamati jambo kama hili? Walikuja kwenye Kamati kwanza taarifa yao yenyewe ambayo ilikuwa imeletwa na *CAG* walikuwa wanaikataa, na *GAG* mwenyewe alikuwa anawashangaa, *as if* hawakuwa na *exit meeting* walipokutana na *CAG*! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hilo inatosha kwamba watu wasiendelee kumwangusha Mheshimiwa Rais anapowaamini kwenye mikataba na wasifikirie Watanzania ni wajinga sana, wasiendelee kutuhujumu sana maana wanalitesa sana Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo kwamba Taifa hili halina fedha, hicho kidogo tunachopata tungeweza kuki-*utilize* vizuri, tukakifanyia kazi vizuri, tungefika mbali, lakini watu wachache wasiokuwa na nia njema na mapenzi ya Taifa hili wanaendelea kulihujumu Taifa hili, kujinufaisha peke yao, kwa manufaa yao peke yao na kuendelea kututesa jambo ambalo siyo sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais ana nia njema ya kutumikia Taifa hili. Yule mama ni mtu mzima, anapambana na hata unaiona sura yake ya kusaidia watu. Hata siku moja mwanamke hajawahi kuwa tapeli, mwanamke hajawahi kuacha kuwasaidia

watu kwenye nyumba yake, lakini hawa aliowaamini ndio wanaomfanya Mheshimiwa Rais apate doa na Mheshimiwa Rais ana…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Condester, ahsante sana, kengele ya pili imelia.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, muda wangu umeisha?

**MWENYEKITI:** Ndiyo, ni kengele ya pili.

**MHE.CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia tu hoja moja, kuhusiana na suala la *BoT,* kama ambavyo wameongea wenzangu; aliongea Mjumbe mwenzangu wa Kamati. *BoT* ni taasisi kubwa, sisi wote ni Watanzania, na kila mtoto wa kawaida wa Tanzania anatamani afanye kazi kwenye sehemu nzuri. *BoT* wanapaswa kurejea ile *procedure* yote ambayo walipatikana wale watu, kwa sababu kila mtoto aliyepo Tanzania ana haki ya kupata kazi kwenye taasisi kubwa kama zile. *BoT* wamevunja sheria, wao kwa ajili ya kujinufaisha wenyewe, baadhi ya watu wameona watoto wao ndio wanaofaa sana kwenye hii nchi na ndiyo maana wakavunja utaratibu na wakaenda ndivyo sivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaomba Watanzania watendewe haki sawa na Watanzania wote. Sisi fahari yetu ni Utanzania wetu. Babu zetu waliokufa kwenye ardhi hii, sisi wote lazima tunufaike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Condester Sichalwe. Nilimtaja Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane, Mheshimiwa Venant Daud Protas na Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo ajiandae.

**MHE.FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia katika taarifa ambazo zimetolewa leo katika Kamati zetu tatu za *PAC, LAAC* na *PIC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mwenyezi Mungu, tangu nimeingia hapa Bungeni nimeweza kutumika katika kamati hizi zote tatu. Kwa hiyo, ninao uelewa wa kutosha na nimezielewa vizuri taarifa ambazo zimetolewa leo, lakini kwenye taarifa zao zilizotolewa, nitachangia kidogo kwenye Kamati ya *LAAC* na nitachangia kwa upana zaidi kwenye Kamati ya *PIC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kujikita kwenye eneo lile la matumizi yasiyo sahihi ya *Force Account*. Ni ukweli kwamba taratibu, kanuni na sheria zimekuwa hazizingatiwi katika matumizi ya *Force Account*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna zile kamati ambazo huwa zinahusika na fedha, manunuzi na mapokezi ya vifaa. Zile Kamati zimekuwa *dormant,* hazifanyi kazi yake sawa sawa kama ambavyo Mheshimiwa Mpakate amezungumza muda mfupi uliopita. Kwa hiyo, zinatumika tu kuhalalisha mambo, lakini kazi yenyewe inafanywa kule Makao Makuu ya Halmashauri zetu. Kwa hiyo, kuna jambo hapa ambalo tunatakiwa tulifanye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na ushauri uliotolewa na Kamati ya *LAAC*, nilikuwa nashauri kuwa Serikali yetu iangalie uwezekano wa kupanga viwango vya fedha zinazowekezwa kwenye mradi ambazo zitatumia aidha *Force Account* au wazabuni. Leo tumeona hata majengo ya Ofisi za Halmashauri zetu zenye thamani ya shilingi bilioni mbili, shilingi bilioni tatu na miradi mingine inaongezewa fedha, inakwenda mpaka shilingi bilioni nne hadi tano bado zinatumia *Force Account*. Hii ni hatari kweli kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa napendekeza, mradi ambao unazidi shilingi milioni 200, usitumie utaratibu wa *Force Account,* kwa sababu zile fedha ni nyingi. Hizi fedha zikifika kule, fuatilieni tu, nakuomba Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI na Waziri

wa Fedha mweke utaratibu mzuri wa kuwa na zile *technical audit* kutoka Wizarani, mtashuhudia haya mambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zile shilingi milioni 470 ambazo tuliletewa kwenye miradi hii ya *SEQUIP* hazikumaliza ile miradi, na hata hizi zilizoletwa juzi za miradi ya *BOOST* shilingi milioni 331 kila jimbo hazijamaliza ile miradi. Unakuta mradi unatekelezwa asilimia 80 au 85 na ukizidi sana 95. Mwisho hii imekuwa ikitusumbua. Kipindi unapoenda kupanga matumizi ya fedha za Mfuko wa Jimbo, unakuta Mkurugenzi naye anakusogelea, analeta *request* ili akamalizie vyoo na huduma nyingine katika ile miradi. Kwa hiyo, imekuwa shida kweli kweli. Kwa hiyo, hapa tunapaswa kupaangalia vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika yale marekebisho au maboresho ya utekelezaji wa miradi kupitia *Force Account,* nashauri kwamba tuzingatie viwango vya pesa vinavyowekezwa kwenye mradi, ikizidi shilingi milioni 200 tupeleke kwenye zabuni, na ikiwa chini ya hapo, kama ni kujenga madarasa, sijui kujenga ofisi za shule na vitu kama hivyo, hizo tunaweza kupeleka. Kujenga zahanati, tunaweza kutumia *Force Account,* lakini siyo miradi ambayo inagharimu fedha nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, nije kwenye taarifa iliyotolewa na Kamati ya *PAC*. Nakwenda moja kwa moja kwenye ukurasa wa 31 na 46 kwenye kipengele Na. 2.4.7 na 3.2.10. Pale Kamati yetu ilizungumzia kutokamilika kwa miradi katika taasisi ambazo zinatumia mtaji wa umma kwa wakati. Jambo hili limejitokeza katika maeneo mengi na pale wame-*cite* mifano ya *NSSF*, katika ule mradi wa pale Mkulazi wamelazimika kuongeza fedha kiasi cha dola milioni 32, lakini kuna miradi ya *RUWASA* hasa ile inayotumia fedha za *National Water Fund*, imekuwa ni shida kweli kweli kumaliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na shida kubwa na wakati mwingine fedha zinachelewa kuja na wakati mwingine mlolongo wa malipo unakuwa ni mrefu sana, hasa hizi fedha za wafadhili wa nje.

Matokeo yake sasa mradi ukichelewa, unakuta bei ya vifaa inaongezeka, *inflation* inatokea, na riba inazaliwa kutoka kwa wakandarasi hasa wanapokuwa ni wa kutoka nje. Kwa hiyo, imekuwa ikileta shida kweli kweli na kufanya lile kusudio la Serikali la kuwekeza mitaji katika hizo taasisi kuwa halitekelezwi na mwisho wa siku ziada haizalishwi mapema kama ilivyokusudiwa, na mwisho wa siku kunakuwa na ufanisi mdogo katika utekelezaji wa ile miradi na vile vile tija inakuwa haipatikani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Serikali iliangalie hili eneo ili tuweze kunasuka na hii hali ambayo imejitokeza. Pia naomba Serikali iongeze usimamizi wa hiyo miradi, lakini pale inapohitajika kupeleka fedha, basi zifike kwa wakati kwenye zile taasisi ili waweze kutekeleza hiyo miradi iliyokusudiwa ili ufanisi na tija viweze kupatikana katika uwekezaji wa hayo maeneo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu ambalo napenda kulizungumza ni suala la ongezeko la riba itokanayo na ucheleweshaji wa kulipa wakandarasi au wazabuni. Hili limekuwa jambo ambalo kama limezoeleka. Nataka nikwambie, jumla ya shilingi bilioni 63.77 ambazo zimeainishwa kwenye ukurasa wa 28 na 29 kwenye taarifa ya Kamati ya *PIC,* kama tungezinusuru kulipwa riba au tusingezigharamia kulipia riba, tungeweza kujenga vituo vya afya visivyopungua 127 kwa fedha zile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, tungeweza kujenga zahanati zisizopungua 318 kwa thamani ya ile pesa ambayo inakwenda kutumika kwa ajili ya kulipa riba; tungeweza kujenga madarasa ya kisasa yenye thamani ya shilingi milioni 24 kila moja yasiyopungua 2,600; na pia tungeweza kujenga mabweni au maabara katika shule zetu za sekondari zisizopungua 1,822.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni fedha nyingi, lakini mwisho wa siku tumejikuta tunarudi nyuma kwa sababu tunatumia fedha nyingi kuwekeza katika maeneo ambayo tayari uwekezaji ulishafanyika kwa kuokoa hizo riba zinazotakiwa zilipwe na hazilipwi sasa. Kama tulikopa, unakuta hazilipwi na *donors,* inabidi tutafute

chanzo kingine cha pesa kwa ajili ya kugharamia hayo malipo ya hao wakandarasi kutokana na kuchelewesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na sababu nyingi za ucheleweshaji, lakini leo hapa napenda nitanabahishe, niliwahi kufuatilia baada ya kuona ile hoja ya *CAG* na nikakuta kuna utaratibu ambao huwa unatumika katika malipo hasa kule kwenye upande wa barabara. *TANROADS,* wanatumia mfumo unaoitwa *FIDIC,* ule mfumo unataka malipo yakamilike ndani ya siku 56. *Consultant* na Mkandarasi wanatakiwa wafanye mambo yao ndani ya siku 28 na siku 28 inatakiwa taasisi zetu za Serikali kuanzia *TANROADS* pamoja na Wizara ya Kisekta, Wizara ya Ujenzi pamoja na Wizara ya Fedha waweze kufanya kazi zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TANROADS* ina mfumo wake mzuri wa malipo na udhibiti wa fedha na umekamilika kabisa, lakini utakuta *TANROADS* wanafanya *procedure* zao, lakini lazima iende Wizara ya Kisekta, Wizara ya Ujenzi. Pale kuna maafisa wasiopungua wawili, lazima wacheze na ule mfumo wa malipo. Ukienda Wizara ya Fedha utakuta zile *transactions* zinatakiwa zipite kwa Mkaguzi Mkuu wa Ndani, naye ana wasaidizi wasiopungua wawili; pia inatakiwa ipite kwa Kamishna wa Fedha za nje, naye ana wasaidizi wasiopungua watatu lazima wapitie hiyo *transaction* ya fedha; vile vile Kamishna wa bajeti naye lazima apitie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa nasema hii milolongo imekuwa mirefu, naishauri Serikali ipunguze milolongo ya malipo ili tulipe kwa wakati, tupunguze hizi riba. Kama haitoshi, pia tuwe na mfumo wa kufuatilia kuona ni wapi kuna *laxity* katika kulipa haya malipo ambayo yanazalisha riba ili hizo fedha tuweze kuzi-*save* ziende zikafanye kazi nyingine kwa ajili ya maendeleo ya Taifa na ni fedha ambazo zinatokana na jasho la walipa kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja zote na taarifa zote zilizotolewa na Kamati zetu zote tatu za *PIC, PAC* pamoja na *LAAC*, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane. Tunaendelea na Mheshimiwa Abbas Tarimba, Mheshimiwa Venant Daud Protas na Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo, ajiandae.

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Nami naomba kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kutujali sana wana-Kinondoni. Tulikuwa na shida ya *secondary schools* mbili katika Kata ya Kinondoni ambayo imeshajengwa, ilibakia Kata ya Tandale nayo kwa sasa tumepata *secondary school.* Hivi tunavyozungumza, wananchi wanaopisha Mradi wa Bonde la Mto Msimbazi wameshaanza kulipwa fidia na wengine ambao walikuwa wameomba tathmini upya, wanafanyiwa tathmini. Hivyo, Serikali mambo ni *bulibuli.* Namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anayoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilichobakia ni kwamba nilikuwa nimeomba *high school* na nilizungumza pia na Mheshimiwa Waziri Mkuu, mapendekezo hayo na maombi yangu nimeyapeleka Serikalini ili Kinondoni iweze kupata *high school* kwa maana ya *form five* na *six.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nataka niangalie dhamira ya Serikali katika uwekezaji kwa umma. Hapa inanipeleka kuona kwamba Serikali inawekeza fedha nyingi kwa madhumuni ya kuimarisha sekta za kibiashara, sekta za utoaji huduma, na vile vile, kuchochea uchumi mpana ili hatimaye fedha ziweze kupatikana, zichangie katika Mfuko Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano na kustawisha Watanzania wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo unaiona kwenye dhamira ya Serikali, kwa sababu mwaka 2017/2018 uwekezaji katika sekta ya umma ulikuwa ni shilingi trilioni 55.76. Sasa katika kipindi cha miaka mitano, uwekezaji umekua na kufikia shilingi trilioni 73,37. Hii inaonesha dhamira ya Serikali. Sasa mtu yeyote anayewekeza, madhumuni yake ni kupata *returns.* Sasa hapa ndipo kwenye matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nimpongeze sana *TR*, Bwana Nehemia Mchechu pamoja na timu yake, kwa kuleta mageuzi makubwa katika Ofisi ya *TR*, kiasi kwamba gawio limeweza kupanda na kufikia shilingi bilioni 850. Hii yote inaonesha *seriousness* ya Ofisi ya *TR*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile kuna matatizo katika ulipaji wa ile asilimia 15. Nataka niwaambie Waheshimiwa Wabunge, mimi nimewahi kubahatika kufanya kazi kama Mkurugenzi Mkuu wa *Gambling Board of Tanzania*, taasisi ambayo haikuwa imetakiwa ilipe gawio wala mchango, lakini iliweza kufanya kazi ya kutoa mchango kwa hiari mapema kabla ya sheria. Maana yake ni kwamba baada ya ujio wa sheria, matakwa ya kulipia asilimia 15 ni lazima yatekelezwe na hakuna *option* katika hiyo. Utaona taasisi nyingi mpaka sasa hivi zinategemea ruzuku, hata kama taasisi imekaa miaka 10 au 15, bado inategemea ruzuku. Hii inafanya watu wabweteke, wasifanye kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata Mwenyekiti wa *LAAC* alipokuwa anazungumza, anawataka halmashauri na taasisi za umma ziache fikra za kuendelea kupata ruzuku. Hili jambo ni lazima *TR* aelekezwe, afanye uchambuzi; awape muda wakuu wa taasisi wanaotegemea ruzuku, wafanye kazi, waondokane na tabia ya kutegemea ruzuku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utashangaa hao ambao wanategemea ruzuku, mwisho wa siku wana-*post* ziada. Sasa kama wewe ulikuwa unahitaji ruzuku, ziada unaipata kutoka wapi? Maana yake ni kwamba sisi tunataka zile fedha ambazo zingepelekwa kama ziada zibakie katika Mfuko Mkuu wa Serikali ili zisaidie katika maeneo mengine. Maana yake ni kwamba *failure* ya kuweza kutengeneza ziada, *failure* ya kushindwa kulipa asilimia 15, watu wawajibishwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nitoe mifano ya taasisi mbili; moja *DAWASA* mwaka 2019/2020 walichangia lakini mwaka 2020/2021 hawakuchangia, mwaka 2021/2022 walichangia. *TCCA* mwaka 2019/2020 alichangia, 2020/2021 hakuchangia, 2021/2022

amechangia; na wengine wanachangia wakijisikia siyo kwa matakwa ya sheria, ila wakijisikia ndiyo wanatoa mchango, lakini siyo asilimia 15 kama sheria inavyotaka. Unaweza ukashangaa kuna taasisi moja ambayo ni Mamlaka ya Chai, katika kipindi cha miaka mitatu wamechangia shilingi milioni mbili, kama siyo mzaha ni nini? Taasisi ya Umma unachangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali shilingi milioni mbili, kwangu mimi naona ni mzaha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi, naomba kuwepo na utaratibu kwamba kila mahali ambapo Serikali imechangia, ni lazima watu walete malipo yanayotakiwa kwa mujibu wa sheria. Kushindwa kufanya vile, nashauri Bodi husika pamoja na Mamlaka zile za Menejimenti ziweze kuchukuliwa hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo ambalo kila Mbunge aliyesimama amelilalamikia. Jambo hili linahusiana na Ripoti ya *LAAC, PAC* na hata Ripoti yetu ya *PIC*, zote zinaongelea kwa uchungu kabisa jambo linalohusiana na matumizi mabaya ya fedha za Serikali, ubadhirifu na upotevu wa fedha, lakini mbona hatuoni hatua zikichukuliwa? Hapa nashauri Serikali ilete taarifa Bungeni kila baada ya kipindi fulani; kama ni miezi mitatu, watuletee taarifa ni nani amechukuliwa hatua za kinidhamu, nani amechukuliwa hatua za kisheria? Tusikae kimya kwa kuzungumza tu. Tukikaa kimya kwa kuzungumza, hawa jamaa wanaofanya mambo haya wanatusahaulisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niulize, ni nani mwenye biashara? Mfano binafsi, halafu mtu achukue zile fedha azitumie, wewe ubaki kulalamika, mimi sikubali. Mimi ukichukua fedha yangu, kama sikuwezi, hata kukuloga nakwenda zangu kwetu Tanga, kukupiga hata jini. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Serikali inakaa tunaletewa Taarifa ya *CAG*, watu wanachukua pesa na ukienda huko mjini *lifestyle* yao ni nzuri, hawana kipato cha kutosha, pesa wanatoa wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Marekani wana *theory* yao moja inaitwa *Follow the Money*. Hakuna pesa ya Serikali inayopotea. Hela ya Serikali lazima ipitie katika muamala. Ndiyo maana mwaka 1997 kulikuwa na *film* inaitwa *All the President's Men* walikuwa wanazungumzia hiyo *theory* kwamba fedha ya Serikali haipotei. Ukifanya *investigations* utawakamata. Fanyeni *investigations* muwakamate wanaoiba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo michongo basi ifikie mwisho. Hivi tuibiwe mpaka kiasi gani halafu mwisho tukasirike ndiyo tuoneshe kukasirika? Mimi ningeomba Serikali iwe na ukali katika suala hili ili ile *theory* nyingine ya *Deterrence Theory*, mtu anapoadhibiwa na mwingine aone kwamba kumbe nikifanya hivi naweza nikaadhibiwa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusiwe na huruma na wala tusiwabadilishe wafanyakazi kutoka mahali walipoharibu kuwapeleka mahali pengine. Hicho siyo jambo jema. Tunatoa picha ambayo siyo sahihi kwa watanzania. Anayeharibu aharibiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi jamani hamkumbuki, kwa wale ambao tunasoma Biblia Zaburi 119 hadi 195 anasema hivi "wana amani nyingi waipendayo sheria yako wala hawana la kuwakwaza". Hawa watu wanatuikwaza sisi wanaoiba, wanamkwaza na Mungu, Mungu anakwazika katika hili ndiyo maana ukisoma Zaburi anasema hivyo. Kama wao hawatupatii amani sisi na sisi tusiwape amani, huo ndiyo utaratibu, *Tit for tat*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe unatuibia, unatufanya tunapoteza muda, tunapoteza fedha za watanzania kujadili mambo ambayo umeyasababisha wewe mwizi, halafu wewe tukupe amani, sisi unatupa tabu, unatukwaza. Huo utaratibu haupo. Ifike mahali tuseme jamani hawa wahusika wote kaeni pembeni. Tena hata mkiwapeleka TAKUKURU, tuletewe taarifa ili tujue nini kinaendelea kule, isibakie kama ni kichaka. *(Makofi)*

*(Hapa Kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Ninaamini bado nina dakika tano, au nimemaliza?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa muda wako umekwisha lakini malizia kwa dakika moja tu.

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nataka nimalizie kwa kusema naunga mkono hoja zote tatu lakini naomba ikubaliwe kwamba, Kila Taarifa ya Kamati inayokuja hapa ielezee ni hatua gani zinachukuliwa ili mapendekezo ya kutaka kuongelea ruzuku kwenye Taasisi za Umma iweze kukamilika na iachwe kabisa, kusiwe na ruzuku, watu wajitahidi kutengeneza fedha na kuiletea Serikali mapato. Siyo wao kupelekewa fedha. Nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Abbas Tarimba, ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Venant Protas, Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma, Mheshimiwa George Malima na Mheshimiwa Riziki Lulida wajiandae.

**MHE. VENANT D. PROTAS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia Kamati hizi tatu. Kwanza, nianze kwa kuunga mkono kazi kubwa ambayo imefanywa na Kamati hizi tatu kwa niaba ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa na hoja ndogo yenye masilahi kwa Taifa letu. Nilikuwa nataka niseme jambo moja, kazi ya Bunge ni kuisimamia Serikali, lazima sisi kama wawakilishi wa wananchi tulinde haki zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa nataka nitangulize hivyo kwa sababu gani; nchi hii imekuwa inaibiwa siyo kwa mitutu ya bunduki. Nataka Mheshimiwa Waziri wa Fedha (Mchumi aliyebobea), juzi alisema, namnukuu "Fedha hazipotei, kwa sababu Serikali inalinda mianya ya fedha kupotea".

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimwambie kwamba, hatuibiwi kwa kwenda kuvunja nyumba, tunaibiwa kwa kutumia akili, tunaibiwa kwa kuingia mikataba mibovu. Lile suala la kuingia mikataba ndilo limeingiza Taifa letu hasara na tusipokuwa makini tutaendelea kuwa na hasara. Hapa ndio nashindwa kuelewa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu inafanya kazi gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii ndiyo maana Mheshimiwa Rais siku moja alisema, sijui hicho cheo cha Mheshimiwa Kabudi (Mzee wa mikataba) kipo? Kwa sababu, tumekuwa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu ambayo inakwenda inakula huku na huku. Kwa sababu gani, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu inatakiwa isaidie Serikali katika kuingia mikataba mbalimbali. Sijawahi kuona Serikali inakwenda kushinda kesi, Serikali inakwenda kutetea mkataba ulioingia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakutolea mfano mwaka 2013/2014 ilikuja hoja hapa ya Tegeta *Escrow* mnaikumbuka. Mwanasheria Mkuu aliyekuwepo wakati ule alisema zile fedha siyo za Serikali. Wakasema fedha ni za watu binafsi. Kwa kuwa siku hazigandi, hilo jambo limerudi tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme jambo moja ndiyo useme Ofisi ya Mwanasheria Mkuu na yenyewe inatakiwa iendewe na *CAG* huko. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliingia mkataba na *APTL,* tukatengeneza akaunti ya pamoja, tukasema fedha zetu tuziweke mahala fulani, Serikali ikatimiza wajibu wake ikaweka fedha. Wakatokea wajanja wakaenda kuzipakua. Tukaanza kuuliza humu za umma au siyo za umma si za umma? Mwanasheria Mkuu akasema siyo za umma, leo anaumbuka huku zile fedha zilikuwa za Serikali. *(Makofi na Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo kuna mashtaka yamekwishakuja tunadaiwa zaidi ya dola za kimarekani bilioni 148. Tunatakiwa tulipe dola za kimarekani milioni 148 sawa sawa na bilioni mia tatu na

ushee. Sasa, huyu Mwanasheria Mkuu hakuliona hili toka zamani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo hapo nakuja kusema kwamba, kwa nini Ofisi ya Mwanasheria Mkuu haitusaidii? Cha ajabu, yule *APTL* wakati wanakwenda kutoa hizi fedha wakisema za kwao akasema, likitokea lolote linalohusu Serikali, Serikali haitohusika nitahusika mimi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo inakwenda kudaiwa Serikali na Serikali imekwishajiandaa kuanza kulipa. Mimi ninawambia msilipe, kalipeni hela zenu huko. Mwaka 2018 Mwanasheria Mkuu akapeleka kesi mahakamni kumshtaki huyu *IPTL* kwa nini ametutelekeza, sijui imekuwaje, mbona tulikuwa wote pamoja, ameingilia wapi? *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mahakama Kuu ikatoa uamuzi wa kwamba, *IPTL* iilipe Serikali hizo fedha ili likitokea la kutokea iweze kuwalipa wale wanaodai ambao waliikopesha *IPTL*. Lakini mpaka kufikia tarehe 1 Machi, 2021 ilitakiwa zile fedha ziwe zimwkeishalipwa lakini hadi kufikia Desemba 2022 fedha hizo bado hazijalipwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Serikali inaanza kuandaa eti kwa sababu tutakamatiwa ndege, *image* ya nchi itaharibika. Mimi niwambie hivi, kwa kulinda wezi, wabadhilifu, mlikuja hapa na hoja ya kusema fedha siyo za Serikali kumbe ni za Serikali. Mlikuwa mnajizunguka wenyewe leo mnaumbuka. Mimi niwambie na Kamati imependekeza fedha hiyo isilipwe, watakwenda kuchukua fedha za walipa kodi wa Tanzania kwenda kuhalalisha hela walizokuwa wamezitoa wakati ule kwenda kugawana kwenye viroba na leo hii hatuwajui waliogawana wako wapi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niombe, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu ulikubaliana na *IPTL* fedha ilipwe, nenda ukasimamie hilo jambo. Bunge hili hatutapitisha fedha kwenda kulipwa kwa sababu ya uzembe wa watu. Kwa hiyo, nilikuwa nataka

niikumbushe Serikali kwamba, hatuibiwi kwa mitutu ya bunduki kwa sababu hata hao wenyewe wenye mitutu ya bunduki na wenyewe wameshaibiana huko tozo unatozwa polisi wenyewe wameibiana. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hii nchi kila mtu ni mpiga *deal*. Mlinzi wa amani mpiga *deal*, ukienda TAKUKURU unakwenda kupumzishwa na hakuna kitu kinachoendelea. Kwa hiyo, haya mambo yaweze kusaidika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ni la kusikitisha, Serikali imekwenda kuanzisha vitaasisi vya kufanya biashara halafu hamuwezi kufanya biashara. Leo *TANOIL* imeleta hasara duniani sijawahi kuona, Serikali ilipeleka bilioni 128 kuusaidia mfuko wa *TANOIL* ili ifanye biashara ya mafuta. Leo hata bilioni 20 haifiki, hela zote wamekula, tunaanza hapa kuzungushana, tumewafukuza. Umewafukuza wamekwedna wapi? Au ninyi wenyewe mlijitangulizia pasi ili mwende mkafunge? *(Makofi/Kicheko)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Venant, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Mwigulu.

**TAARIFA**

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa mchangiaji. Pamoja na mchango mzuri anaochangia naomba nimpe taarifa kwamba, hizi taarifa tunazojadiliana ni moja ya sehemu ya kazi nzuri zinazofanywa na taasisi zetu ikiwepo TAKUKURU pamoja na *CAG*. Inawezekana katika utendaji wa kazi na taasisi akawepo mtu mmoja mmoja. Hata hivyo, ningeomba hiki chombo chako ambacho ndiyo mtungaji wa Sheria, kiepuke ku-*generalize* taasisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu inaheshimika kwa taasisi. Inaweza ikawa na mtu mmoja mmoja akafanya hivyo lakini taasisi

zetu ni moja ya nchi ambayo inaheshimika sana. Pia, TAKUKURU ni moja ya taasisi yetu ambayo inaheshimika kama taasisi. Kwa hiyo, nilitaka nikubaliane na michango yake na hisia aliyonayo lakini nimuombe asi-*generalize* taasisi kama taasisi, bali twende kwenye maeneo moja moja ambalo tunaona mapungufu. Pia, Serikali iko kwa ajili hiyo na huo ndio utawala wa Sheria unavyotaka. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Venant, unapokea hiyo taarifa?

**MHE. VENANT D. PROTAS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza amekula dakika zangu tatu, zilindwe. *CAG* alisema, Jeshi la polisi fedha zilizopotea za tuzo na tozo na hajamtaja mtu mmoja mmoja. Sasa, kama kuna mtu mmoja mmoja mtuletee tuwashughulikie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, *CAG* yeye alifanya Jeshi la polisi, sasa kumbe mnawafahamu mtu mmoja mmoja. Mtusaidie hilo jambo...

**MHE. CHISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, Taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimpe taarifa mzungumzaji makini anayezungumza jambo hili kwa uchungu unaostahili. Jambo la msingi na namna bora ya Bunge hili kujiheshimisha kwa wale waliotuleta hapa, kuhitimisha hoja hizi kubwa tatu, ni kwa Bunge hili kuweka Azimio madhubuti na kuhakikisha kwamba Wizara zote ambazo ufisadi umetokea wa matrilioni ya fedha hizi, Mawaziri wanaohusika, narudia kusema Mawaziri walioshindwa kusimamia taasisi zilizoko chini ya Wizara zao wawajibike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hawatowajibika hakuna namna nyingine. Kama hawatowajibika wao, twende na shingo ya yule ambaye tuna mamlaka naye ili boti letu lililotobolewa leo na mafisadi wasiendelee kwenda kushangilia kula hela ya umma huko halafu tunalijadili jina la jambo hili kwa wepesi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima Bunge hili lilinde heshima ya Bunge kwa kuwachukulia Mafisadi hatua na kuwachukulia wale walioshindwa kuwawajibisha. Nataka kumuunga mkono kwa kusema hivyo, acheni masihara. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Venant, unapokea taarifa ya Mheshimiwa Olesendeka?

**MHE. VENANT D. PROTAS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipokea. Kwa kuongezea kuweka msisitizo wa mtoa taarifa, nilikuwa nagusia Taasisi ya *TANOIL* ambayo imetupotezea zaidi ya bilioni mia moja na kidogo. Yaani hatua, Serikali inasema tumewaweka pembeni. Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu na pia ni Waziri wa Nishati, ninakuheshimu sana. Nikuombe, nenda pale *TANOIL* na Kalandinga, ukamuache mhudumu tu. Wengine wote kamata mwende mkawaweke huko. Aliyehusika akae huko, hajahusika mumtoe kwa utaratibu uliopo. Lakini pale *TANOIL* kuna uozo mkubwa na sisi huku tumetoa mapendekezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe kupitia Bunge lako, tunapigwa ndani na nje, tusipodhibiti sisi wenyewe, hakuna baba ambaye atakuja kutuokoana haya yatakuwa watendaji wa Serikali...

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jenista.

**TAARIFA**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Kwanza kabisa naomba niendelee kumpongeza mchangiaji kwa kazi nzuri anayoifanya ya kuendelea kutoa ushauri na kuungana na ripoti ya CAG kupitia kwenye Kamati husika. Lakini naomba tu nikumbushe maneno mengine ambayo mchangiaji amekuwa akiyatumia mara kadhaa leo kwamba, tunapigwa, tunapigwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tunapigwa, naomba tu nikumbushe Bunge lako Tukufu kwamba, yako makosa na baadhi ya watumishi kweli wanatukosea na wanafanya isivyo haki. Lakini bado Serikali yetu ya Awamu ya Sita imeendelea kufanya kazi nzuri katika miradi mingi na maeneo mengi. Kwa hiyo, ninachotaka kutoa taarifa, makosa haya yatachukuliwa na kufanyiwa kazi kwa uzito wake kwa idadi ya makosa yaliyopo. Lakini hayatochukua nafasi ya kazi nzuri sana ambayo imefanywa na Serikali ya Awamu ya Sita katika kuwahudumia wananchi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Venant, malizia.

**MHE, VENANT D. PROTAS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inafanya kazi vizuri, hatujakataa. Hao mnaowasema mmoja mmoja kwa nini mnawacheleweshsha huku mtaani wanaendelea kutusumbua? Wachukulieni hatua mapema. Hapa mnapokuja, hapa CAG mlikwishashindana huko ndiyo maana mmekuja humu Bungeni. Tunachokisema, tumekwishawaita kwenye Kamati wamejitetea na hakuna utetezi zaidi ya kuchukua hatua… *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, muda wake umekwisha nilimpa dakika moja tu amalizie.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, basi.

**MHE. VENANT D. PROTAS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wamenilia dakika zangu lakini yote kwa yote, Bunge hili tusilete ushabiki. Ni lazima tuisaidie nchi, lazima tumsaidie Mheshimiwa Rais. Mheshimiwa Rais amesema tumsaidie. Inaweza kuwa ninyi Mawaziri hamjui huko ni nini kinachoendelea. Sisi tukijua mkayafanyie kazi, msianze kukinga kinga hapa mtakuwa hamtusaidii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Venant, ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo, Mheshimiwa George Natany Malima na Mheshimiwa Riziki Lulida ajiandae.

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia hoja ambayo iko mbele yetu. Mimi natokea Kamati ya *PIC*. Nitaongelea ufanisi…

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa, naomba tupunguze sauti tuwasikilize wachangiaji wetu.

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaongelea ufanisi wa mashirika yetu ya umma. Kamati imepitia mashirika ambayo Serikali yetu imewekeza zaidi ya trilioni 73.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukuaji wa mitaji katika mashirika yetu, pamoja na uwekezaji mkubwa ambao Serikali imeweka lakini ukuaji wa mitaji unatia shaka na wasiwasi. Kwa kipindi cha miaka mitatu, ukuaji wa mitaji katika mashirika yetu ya umma ni asilimia nane tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama watangulizi waliochangia walivyosema, Serikali imewekeza fedha nyingi katika mashirika yetu ya umma lakini *return* katika uwekezaji ni mdogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Serikali kuwekeza trilioni 73 katika mashirika ya umma hayo mashirika ya umma yanayo matobo mengi sana. Asubuhi tumesikiliza ripoti tatu ambazo

zimesomwa na Kamati tatu, kwa kweli inahitaji moyo mgumu kuzipokea na kuzikubali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na uwekezaji katika mashirika yetu ya umma; mashrika yetu mengi yanasuasua. Serikali inawekeza fedha ya walipakodi lakini mapato yanayotokana na uwekezaji huo ni madogo. Tunayo kazi kubwa mbele yetu ya kufanya ili kuhakikisha kwamba uwekezaji unaendana sambamba na mapato tunayoyapata kutokana na uwekezaji huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya *PAC* imetoa taarifa yake asubuhi, kati ya mashirika 66 ambayo yalipaswa kutoa gawio ni mashirika 25 ambayo yametoa gawio, mashirika 41 hayajachangia chochote. Ni kana kwamba Serikali kwa kipindi cha miaka mitatu haijawahi kuwekeza fedha yoyote ya walipakodi; lakini tunajua Serikali imewekeza fedha nyingi lakini mashirika yanafanya vibaya na tumenyamaza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo mashirika 25 ambayo yamesema yamechangia mfuko mkuu wa Serikali ni mashirika matatu tu ambayo yamechangia zaidi ya asilimia 38, na hayo yametajwa hapa; ni *BOT* imechangia bilioni 200, *Airtel* imechangia bilioni ishirini na kitu na *NMB;* mashirika mengine yote yanasuasua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimenangalia hata kwenye mchango wa *GDP* mashirika yetu haya ambayo tumewekeza zaidi ya trilioni 73 kwa kipindi cha miaka mitatu mwaka 2019/2020 kwenye *GDP* yamechangia 0.6, yaani hata asilimia moja haifiki. Tumewekeza fedha nyingi lakini tunachokipata kama Taifa ni kidogo mno. 2020/2021 yamechangia 0.5, 2021/2022 ni 0.6 kwenye *GDP*, 2022/2023 0.6; kwenye bajeti yanachangia asilimia tatu kwa miaka mitatu mfululizo. Sasa tunajiuliza tunawekeza ili iweje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapowekeza kwenye kitu chochote; amesema mchangiaji wa mwisho kwenye *TANOIL;* tunapowekeza fedha ya walipa kodi tunatarajia baada ya mwaka mmoja au miwili

tuweze kuvuna; na kama tunawekeza bila kuvuna haina maana yoyote ya kuwekeza kwenye haya Mashirika ya Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeangalia gawio, haya Mashirika ambayo hayakuleta gawio ni hatua gani zinachukuliwa na Serikali? Lakini kwa kipindi cha miaka mitatu hakuna hatua yoyote imechukuliwa dhidi ya mashirika ambayo hayakutoa gawio. Tunachokisikia ni Mkurugenzi anahamishwa anatolewa shirika moja anapelekwa shirika jingine na anapopelekwa kwenye shirika jingine ni *business as usual*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo tunalijua, mwaka jana nilichangia hapa, kwamba tatizo la mashirika yetu ni sheria ambayo tunayo ambayo inaongoza mashirika haya. Mwaka jana nilisema na nikashauri, kwamba kama tunataka ufanisi kwenye mashirika ya umma lazima twende kubadilisha sheria ambayo ni kongwe sheria ambayo haimpi pia uwezo wa kuyasimamia mashirika haya ya mmma…

**MWENYEKITI:** Taarifa, Mheshimiwa Oscar kuna taarifa.

**TAARIFA**

**WAZIRI WA MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mchango mzuri wa Mheshimiwa anayechangia nataka tu nimpe taarifa kwamba siyo sahihi kusema kwamba hakuna hatua yoyote inayochukuliwa kuhusu mashirika ya umma ambayo hayafanyi vizuri. Mnafahamu mwaka jana na mwaka huu Mheshimiwa Rais aliagiza mashirika ambayo yanasuasua yachukuliwe hatua na mnafahamu mwaka huu Msajili wa Hazina ametangaza hadharani kwamba yapo Mashirka ambayo yanakwenda kufutwa, yapo ambayo yanakwenda kuunganishwa. Lakini muhimu zaidi tumetangaza hadharani kwamba tunaanzisha sheria mpya ya kuyaangalia mashrika haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nakubaliana naye kwamba kuna Mashirika yana changamoto lakini siyo sahihi kusema kwamba

hakuna hatua zozote ambazo zimechukuliwa. Kuna hatua zipo zinachukuliwa, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma, unaipokea hiyo taarifa?

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana nilitoa ushauri huo kama umechukuliwa na kama hatua zimechukuliwa tumshukuru Mungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ku-*merge* mashirika au kuunganisha mashirika bila kutibu ugonjwa unaotafuna mashirika yetu ni kazi bure.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria iiliyopo ya sasa ambayo wanasema wanakwenda kuifanyia marejeo kimsingi hatupaswi kufanya marejeo kwenye sheria iliyopo tunapaswa kutunga sheria mpya. Mwaka jana nilisema, kama Maandiko Matakatifu yasemavyo huchukui wine mpya ukaweka kwenye viriba vya zamani. Sheria iliyopo haifai, sheria iliyopo ni ya mwaka 1959, kipindi ambacho Taifa hili lilikuwa halijapata uhuru mpaka sasa bado tunatembea na sheria kongwe ya namna hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashuri na kupendekeza kwenye Sheria itakayotungwa ihakikishe inampatia uwezo *TR* kuyasimamia mashirika haya ikiwa ni pamoja na kutoa ushauri au kupewa uwezo wa kuteua bodi kuzisimamia bodi na kuwasimamia watendaji wakuu wa hayo. Kama tunataka kufanya biashara tuondokane na tabia ya uteuzi wa Wakurugenzi kwenye mashirika yanayofanya biashara. Kama tunataka kwenda kufanya biashara kufanye biashara kama kampuni nyingine zinavyofanya; kwamba watendaji wakuu wapatikane kwa njia ya ushindani badala ya uteuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini haya mashirika yenyewe haya *TR* mpaka wakati huu tunapoongea hana mfuko wa kuyasaidia haya mashirika katika mizania ya uwekezaji. Tumeona mashirika mengi yanapotokea matatizo yanakosa uwezo wa kukabiliana na

matatizo ya kibiashara; *TR* hana uwezo wa kifedha kuyasimamia wanabaki kusubiri Serikali iwapatie fedha na wakati mwingine fedha ya Serikali inaendana na bajeti ambayo Bunge lako limeipitisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Kamati yetu tumebaini baadhi ya matatizo ambayo mashirika yetu yanakabiliana nayo; mojawapo ni kuchelewesha kumaliza miradi ya maendeleo. Tumeangalia kipande cha *SGR* kutoka Dar es salaam mpaka Morogoro kwa kipindi cha miaka mitatu tumeongelea hili tatizo tunasubiri nini? Tunaambiwa kipande kimekamilika asilimi 98.9 lakini kwa kipindi cha miaka mitatu tumekuwa tukisikiliza maneno yaleyale kutoka kwa watu walewale, hakuna kinachoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna miradi mingine ya *TANROADS;* tuna Mradi wa Nyakanazi *stopover* tulikuwa na mradi wa kusuka magari pale Nyakanazi na mwingine upo pale Manyoni, hii miradi imesimama tangu mwaka 2016. Serikali imewekeza fedha yake pale ya walipakodi lakini hakuna kinachoendelea. Tunajiuliza, hivi wakati tunakwenda kuwekeza pale tulifanya upembuzi yakinifu au tulifanya *due diligence* au watu waliamua tu wakaamka wakaenda kufanya uwekezaji pale? Fedha ya walipa kodi imesimama, fedha ya walipa kodi imetumika na hakuna tija katika uwekezaji huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi napenda nishauri Serikali, tunapoamua kutekeleza miradi ya maendeleo, tunapoamua kuwekeza katika sekta yoyote kwanza tumalizie miradi viporo ndio twende kwenye miradi mipya vinginevyo miradi ya zamani haikamiliki na tunayoendea mipya haikamiliki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hili la mwisho tumeongelea miradi ya maji; Serikali hususani Wizara ya Maji ilishatoa kiwango cha upotevu wa maji hapa nchini isizidi asilimia 25, wengi wamelisema hili, nitaomba nimalizie na hilo. Lakini ukiangalia mamlaka zetu za maji, mamlaka nyingi upotevu wa maji unakwenda zaidi ya asilimia 38 na tusipochukua hatua mapema, na muona Mheshimiwa Waziri wa Maji yupo, tusipochukua hatua mapema kwa uzembe ambao

nauona watu mamlaka zinaanchaia mabomba hata leo nyumbani kwangu pale maji yanamwagika siku saba…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO:** …tusipochukua hatua mapema maji tunayozalisha asilimia 50 yatapotea na tutakuwa tumewekeza fedha lakini wananchi hawapati maji kadri inavyotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma. Tunaendelea na Mheshimiwa George Natany Malima na Mheshimiwa Riziki Lulida, ajiandae.

**MHE. GEORGE N. MALIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi kuchangia hoja iliyopo mezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze na kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuonyesha nia ya dhati kabisa ya kufanya uwekezaji katika nchi yetu. Shilingi trilioni 73 ambayo yote imeenda kwa ajili ya uwekezaji si fedha kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Uwekezaji Mitaji ya Umma, nimepata nafasi ya kupitia mashirika mbalimbali. Zipo changamoto nyingi. Changamoto moja wapo ambayo ningependa kuizungumzia hapa ni mzigo mkubwa wa madeni ambayo taasisi hizi zinayo. Taasisi nyingi zinaendeshwa kwa hasara kwa sababu zina madeni mengi sana, lakini pia hata unapokutana nazo huwezi kuona mikakati ya dhati kabisa ya kulipa hayo madeni. Kwa hiyo taasisi kama hizi zinazoendeshwa kwa madeni huwezi kutegemea utapata tija ile iliyokusudiwa wakati wazo la uwekezaji lilipoanzishwa. Kwa hiyo ndiyo maana unaona Mashirika haya yanashindwa hata kutoa gawio katika Mfuko Mkuu

wa Serikali kwa sababu wanadaiwa lakini pia hawana mikakati ya kulipa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningetoa mifano tu kidogo ya Mashirika kama mawili au matatu, kwa mfano Taasisi ya *NSSSF* mwaka 2019/2020 ilikuwa inadaiwa shilingi bilioni 239.58 lakini mwaka 2020/2021 ikawa inadaiwa shilingi bilioni 256.43 na 2021/2022 inadaiwa shilingi bilioni 306.29. Sasa taasisi kama hii inahusika na kulipa mafao ya watumishi wale wanaostaafu. Nataka kujiuliza taasisi yenye madeni kama haya inaweza kuendelea kuwa na uwezo wa kulipa michango ya wastaafu, au ndiyo kama zile tunazoona mtaani kila siku wastaafu wanazunguka mtaani Kwenda na kurudi kwa sababu mashirika haya hayafanyi vizuri? Mimi ningeshauri sana Serikali lazima tujikite kutafuta sababu kubwa ambayo inasababisha mashirika haya yasifanye vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni hili la uendeshaji mbovu. Wale wanoendesha, kama ambavyo wamesema wengine, kuna wafanyakazi ambao siyo waaminifu, hawatumii vizuri michango hii ya watumishi; kwa hiyo lazima tuwamulike na tuwachukulie hatua. Nimeona baadhi ya Mawaziri wameonyesha *commitment* kwamba Serikali itaendelea kuchunguza wale wote ambao hawafanyi vizuri kwenye mashirika ya umma wachukuliwe hatua. Mimi ningependa sana kusikia siku moja watendaji wabovu wanachukuliwa hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwenye Shirika la Michezo ya Kubahatisha nalo kwa miaka mitatu mfululizo limeendelea kupata madeni huku madeni yakiendelea kukua. Kwa mfano, mwaka 2019/2020 lilikuwa na deni ya shilingi milioni 742.5, lakini mwaka 2020/2021 likawa linadaiwa shilingi bilioni 2.8. Hata wao tulipokutana nao hawaonyeshi nia ya dhati kwamba wana mikakati gani ya kuhakikisha kwamba deni hili linalipika na linapungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taasisi nyingine ni Baraza la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira *(NEMC)*, nalo pia ni Shrika ambalo lina mzigo mkubwa sana wa madeni. Mwaka 2019/2020 lilikuwa

linadaiwa shilingi bilioni 1.36, lakini hadi 2021/2022 likawa linadaiwa shilingi bilioni 5.9. Mashirika haya yote usitegemee kwamba yanaweza kutoa mchango katika Mfuko Mkuu wa Serikali, lengo ambalo kwa kweli ndilo kubwa. Unapowekeza hata kwenye biashara yako binafsi unategemea upate faida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama unawekeza halafu hupati faida kila mwaka, na kila unapokwenda kuangalia hesabu zake hazionyeshi matumaini maana yake huwezi kupata faida; na ndiyo maana tunashauri kwamba Serikali ijaribu kupita upya mashirika haya; hebu tuone yale ambayo yako kabisa yana dhamira ya kufanya biashara na kuleta tija iliyokusudiwa yaendelee na yapewe uwezo; lakini yale ambayo hayafanyi vizuri ama menejimenti zibadilishwe na bodi ama mashirika hayo yaunganishwe na mashirika mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo jingine ambalo ningependa kulizungumzia kidogo hapa ni utegemezi wa ruzuku. Yapo mashirika mengi yanategemea sana ruzuku; na ukishangaa shirika ambalo linapewa ruzuku ya Serikali bado linaendeshwa kwa hasara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ningeomba hapa kwamba Serikali iangalie vizuri, kwamba, kama shirika halifanyi vizuri hakuna sababu ya kupeleka fedha pale, ni afadhali tuwapeleke wale wanaofanya vizuri. Mashirika mengi yanategemea ruzuku, ni pamoja na *NEMC* pia. Mwaka 2022 ilipata shilingi bilioni nne zilikopwa kutoka Serikalini. Sasa ukiangalia bado halifanyi vizuri, bado lina mzigo wa madeni na bado Serikali inapeleka fedha nyingi mahali pale; nadhani tuangalie vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia shirika lingine ni Mamlaka ya Ufundi Stadi *(VETA)*, pia linapata ruzuku nyingi sana. Na hata ile ziada ambayo wana-*register* kila mwaka inatokana na fedha kutoka ruzuku ya Serikali sisi tungetegemea tuone ziada inayozalishwa na wao wenyewe na kwa ruzuku hii kwa mfano *VETA* mwaka 2020/2021 walipata ruzuku ya shilingi bilioni 62 kutoka Serikalini. Na ndiyo maana ukiangalia kwenye hesabu zao kuna ziada kwa miaka

mitatu mfululizo, ni kwa sababu fedha nyingi inatoka Serikalini lakini wao wenyewe hatujaona kama kuna kitu wanajaribu kufanya…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. GEORGE N. MALIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa kuzungumza ni uzingatiaji wa vigezo vya Msajili wa Hazina; vigezo vinavyohusu utendaji wa kifedha na utendaji wa ujumla. Msajili wa Hazina amepewa mamlaka ya kuweka vigezo *(KPIs)* kwa ajili ya kuendesha mashirika, lakini yako mashirika ambayo hayafuati hata kimoja, je mfano tu Bodi ya Chai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi ya Chai ni kati ya mashirika ambayo hayafuati vigezo vya Msajili wa Hazina. Kwa mfano ukiangalia kwenye gharama za watumishi kwa matumizi ukomo wa *TR* ni asilimia 40 lakini wao wanaendesha kwa asilimia 64. Kwa utegemezi wa ruzuku *TR* anazungumzia hoja ya kupunguza kutegemea ruzuku lakini wao wanategemea ruzuku kwa asilimia 86. Uwiano wa matumizi kwa mapato, ukomo wa *TR* ni asilimia 50 lakini Bodi ya Chai wao wanaendesha kwa asilimia 116 lakini unaona kwamba hawaendi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na yapo mashirika mengine, kwa mfano Mfuko wa Pembejeo wa Taifa na *NHIF;* yote haya hayafuati vigezo vile ambavyo vimewekwa na Msajili wa Hazina lakini unaangalia unaona kwamba Msajili wa Hazina hana meno, hana namna ya kuwachukulia hatua watu kama hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nashauri muswada uletwe turekebishe sheria. Msajili wa Hazina awe na Sheria, awe na nguvu ya kuyawajibisha Mashirika kama haya ambayo hayafuati taratibu hizi. Taratibu hizi zimewekwa maalum kwa ajili ya kusaidia mashirika yetu yaweze kufanya vizuri. Sasa kama hakuna kitu cha kuwasukuma wafanye hivyo ndiyo maana tunaona mashirika mengi sana hapa hayafuati na yanafanya yanavyotaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni tatizo la kucheleweshа kuwalipa wakandarasi na wale watoa huduma. Tatizo hili limeleta hasara kubwa sana serikalini. Unapochelewesha kumlipa mkandarasi au mtoa huduma maana yake kunakuwa na *penalty,* kunakuwa riba, baadaye unapokuja kulipa lazima ulipe na riba. Tumeona kwenye ripoti kwamba kwenye mashirika 12 ambayo yalichelewesha kuwalipa wakandarasi na watoa huduma, walilazilika kulipa zaidi shilingi bilioni 63. Hizi fedha ni nyingi sana na zingeweza kufanya kazi nyingine ya kuwaletea wananchi Watanzania maendeleo lakini zinalipwa kwa ajili ya riba na wale waliofanya hivyo, waliochelewesha kuwalipa wakandarasi au watoa huduma wanaendelea kuwa ofisini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana, jambo hili ni jambo ambalo linatia aibu, kwa nini tucheleweshe kuwalipa halafu tuingie kwenye *penalty* kubwa kama hii, shilingi bilioni 63.7. Mimi nadhani watu kama hawa Serikali lazima iwachukulie hatua, kwa sababu wanatuingiza kwenye hasara kubwa na fedha hizi ni za walipakodi na wakati mwingine walipakodi wa chini kabisa ndio wanaolipa hizi fedha. Sasa zinatumika vibaya na bado tunaendelea kusema waendelee kuwa ofisini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani hatua lazima zichukuliwe, tumpe meno Msajili wa Hazina, anaposimamia mashirika haya awe na nguvu ya kumwajibisha Mtendaji au kuiwajibisha Bodi ya hiyo taasisi. Hii itatusaidia kupunguza gharama kama hizi ambazo zimekuwa zikitokea, ni kama hakuna mtu wa kuangalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuchelewa kukamilika kwa miradi ya maendeleo na hii imetuletea shida pia. Unapochelewa kukamilisha mradi gharama zinapanda kwa sababu bei za vifaa zinabadilika, lakini pia kuna zile gharama za kimkataba. Mkandarasi mlikubaliana ujenzi kwa miaka mitatu, inafika miaka saba, lazima kuwe na *penalty,* ndio haya mambo ambayo tunayasema. Kwa nini tunachelewesha miradi ya maendeleo? Kwa nini haikamiliki kwa wakati?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kuna watu wanahusika, Serikali ichukue hatua kuliko kusubiri mpaka tulipe gharama hizi, tunasubiri mpaka vifaa vinapanda bei. Kwa hiyo, gharama iliyokuwa imekusudiwa kulipwa kwa huo mradi mmoja, unapokuja kukamilika tunalipa mara tatu zaidi, pamoja na *penalty,* pamoja na gharama za kimkataba. Kwa hiyo nafikiri na hili jambo ni muhimu sana, ningependa pia nilizungumzie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nikubaliane na wenzangu wote kuunga mkono hoja. Tuendelee kum-*support* Mheshimiwa Rais kwa kumsaidia katika maeneo kama haya ambayo yameonekana yanaleta shida katika uwekezaji. Fedha hizi amezitoa kwa wingi, shilingi trillioni 73, sisi kumuonesha kwamba tunamuunga mkono lazima tusimamie haya mashirika kwa uhakika na kwa usahihi mkubwa sana. Bila hivyo hizo fedha zitakuwa zinatolewa, tija haipatikani na tunaendelea kusema tuna uwekezaji hapa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa George Malima. Tunamalizia na Mheshimiwa Riziki Lulida.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru na kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetujalia kuwepo katika siku ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru pia Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anayoifanya kuhakikisha halali na wala hapumziki akihakikisha ana nia nzuri ya kutaka kuleta maendeleo ya Tanzania. Wabunge wote tuungane tumsaidie Mheshimiwa Rais, kwenye mapungufu tuyaongee tusiyanyamazie. Tumefikia mahali ambapo unaona Mheshimiwa Rais anakimbia na anataka Tanzania iwe na maendeleo na mabadiliko makubwa yaonekane lakini anakwamishwa na makundi machache ambayo yamejificha wanataka kujiona wao wanafanya kazi lakini bado unaona kuna mapungufu makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza; ukikwaji wa Sheria za Manunuzi ni mojawapo ya hoja ngumu ambayo sasa hivi tunakwenda nayo kama mwiba wa nchi. Nikupe mfano, Mheshimiwa Rais alikwenda kutafuta fedha za mikopo katika upande wa *Covid* zikapelekwa halmashauri. Cha kusikitisha muda ule ule tu sementi ilipanda kutoka shilingi 14,000, shilingi 15,000 mpaka shilingi 30,000 baadhi ya mikoa. Bati zilipanda kutoka shilingi 15,000 mpaka shilingi 30,000, hali ya manunuzi ilikuwa ni mbovu, unajiuliza alipita mdudu gani mpaka kufikia katika mazingira yale. Maana yake kuwa watu wanangojea ahangaike kutafuta pesa wao watumie zile pesa kwa wanavyotaka, ukikwaji huu ni dosari kwa nchi yetu

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitazungumzia mifumo, kila Wizara sasa hivi kuna mifumo ya kidijitali, mifumo hii haiongei. Kama mfumo hauongei maana yake bado tunaendelea kujikuta tunakwenda katika kianalogia badala ya kwenda kidigitali. Nikupe mfano, leo katika baadhi ya Wizara, wana uwezo wa kupata fedha za ndani za kutosha za kuifanya Wizara ile isiwe tegemezi tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe mfano, tulisema tutaanzisha vitambulisho vya wafanyabiashara ndogondogo, tukasema tutawafanyia nini? Walipe shilingi 20,000 ile Sh.20,000 ambayo wangetoa ukizidisha kwa wafanyabiashara ndogondogo iwe 30,000 tu, unaweza kupata shilingi trilioni sita. Naomba chukueni *calculator* zenu halafu mfanye hesabu hizi, lakini jiulizeni mfumo ule umekwenda wapi? Umeachwa. Tumerudia mfumo wa kila siku tunatoa Sh.1,000. Sh.1,000 kwa siku 30 inakuwa ni shilingi 30,000, 30,000 kwa mwaka mmoja mfanyabiashara ndogondogo analipa shilingi 360,000, hivyo tukiwa na wafanyabiashara ndogondogo wachache tu, nikupe mfano 7,500, tuna uwezo wa kukusanya zaidi ya shilingi trilioni 3.6.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tujiulize, sisi na usomi tuliokuwa nao, wasomi wanamsaidiaje Mheshimiwa Rais kutafuta hela za ndani zikafanya kazi, matokeo yake wanangoja ziingie pesa za *OC* wazitapakanye, wazitumie wanavyotaka wao, matokeo yake miradi

mingi inakuwa imesimama. Siyo imesimama hivi hivi tu, ni mifumo tu haiongei. Baadhi ya watu kuisimamisha mifumo kutoongea ni kikwazo cha maendeleo ya uchumi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hali kama hii tusingekuwa tena tunakwenda kukopa, tunakopa nini wakati tuna hela yetu ya ndani? Shilingi bilioni 3.6 zikienda katika kukopesheka kwa wafanyabiashara ndogondogo tunakwenda kukopa tena hela za nje, tunazo hela zetu zinazokwenda katika mabenki, watu wangekopeshwa tusingekuwa hivi, lakini tumesimama hivi kwa ajili ya nini? Kwanza sisi si wabunifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi za jirani wanatupita kwa kila upande maana yake tuna uwekezaji, tuna maeneo mazuri, lakini kwa vile wenzetu ni wabunifu, wametupita vibaya sana, hapa Rwanda tu wanatupita. Sasa Mheshimiwa Rais anahangaika, Mheshimiwa Rais halali, nchi una uchumi mkubwa sana, nenda kwenye madini tupo sisi. Madini sasa hivi yamekuwa ni katika kila mkoa, leo Lindi ni *kuchele* madini tupu, lakini jiulize mifumo inaongea? Kama haiongei itakuwa tunacheza nini? Tunaimba lakini bado tunaifanya nchi kuwa imesimama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kushindwa kulipa madeni; wakandarasi, mimi wananijua wakandarasi kunishtakia mpaka najiuliza mimi sina uwezo, mkandarasi anajikuta toka mwaka 2013, alifanya kazi Serikalini anaambiwa tutakulipa mwakani, ikija mwakani, mwakani, mpaka sasa hivi wale watu wanadai mabilioni, *billions of monies*. Tunajiuliza hivi yeye huyu mtu alichukua mkopo benki, anauziwa majumba yake, mali zake zinakuwa *confiscated*. Je, tumefikia wapi? Hii ni dhuluma, dhuluma kubwa sana kwa makandarasi na wafanyabiashara ambao wamekopa wakafanya kazi kubwa lakini …

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Riziki kuna taarifa. Mheshimiwa Waziri.

**TAARIFA**

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mama yangu, Mheshimiwa Lulida kwa mchango mzuri, lakini ningependa kumhakikisha kwenye upande wa makandarasi, Serikali sasa hivi tuna mkakati mzuri. Kuanzia mwezi Agosti tumeanza kulipa makandarasi shilingi bilioni 70 kila mwezi. Kwenye shilingi bilioni hizi 70 tumeanza kuwapa vipaumbele wakandarasi wazawa, shilingi bilioni 50 kila mwezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumelipa shilingi bilioni 50 mwezi Agosti, tumelipa bilioni 50 mwezi Septemba, tumelipa shilingi bilioni 50 mwezi Oktoba na bado kuna shilingi bilioni 17 kwa wakandarasi wazawa ambao wanadai mpaka tarehe 30 Juni, 2023, tutawalipa hizi shilingi bilioni 17 mwezi huu Novemba. Kwa hiyo, Mama yangu Mheshimiwa Lulida kwa upande wa Serikali tumejipanga vizuri lakini nimhakikishie hata makandarasi wa nje zile shilingi bilioni 70, kuna shilingi bilioni 20 ambayo tunawalipa kila mwezi na tukishamaliza wakandarasi wa ndani, basi tunaanza kuwalipa shilingi bilioni 70 wakandarasi wa nje, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Riziki umeipokea hiyo taarifa?

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza katika kijana msikivu, mnyenyekevu, hii ni mara ya pili nampongeza. Nakupongeza ndani ya moyo kuwa ni msikivu, lakini naanza na wewe, nina wafanyakazi wa *TAZARA* wamestaafu huu ni karibia mwaka wa 10 wametembea katika Kamati zote mpaka Wizara, mpaka Wizara ya Fedha nimekwenda nao hawajalipwa mpaka leo haki zao. Nina Wafanyakazi wa *ATCL* nao wamehangaika, wale mpaka wengine, kwa mfano *TAZARA* walikuwa watu 473 karibu wastaafu 73 wameshapoteza maisha yao, wamekufa kutokana na Mwenyezi Mungu kuwachukua, wao wanadai madai yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafanyakazi wa *ATCL*, kwa vile umeshaniambia hivyo, nimetulia ila nakwambia nakuletea watu

wangu, tena mimi nitakuwa mwakilishi wao. Kwa vile wananifuata mimi, wameona tunapeleka kwa Mama Lulida, hili nawaambia kabisa, waliko huko wananisikia, nakuja kwako wewe ili uweze kuwasaidia hawa watu kwa vile hali ya watu hawa ni ngumu hasa *TAZARA, ATCL* Makandarasi wananifuata. Nikupongeze sana, nilikuwa nataka kuongea mengi, lakini kutokana na hilo ulilioniambia hapo kwa upande wako nimeacha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Mawakala, tumefanya kazi nyingi sana kwa kupitia Mawakala, hawa Mawakala waliopewa kazi nyingi sana za kandarasi wamekuwa mwiba wa nchi. Makusanyo yanayopitia kwao hayafiki katika Serikali Kuu. Hivyo ningeomba kwa hawa Mawakala ambao tunaona kabisa, tunaona humu ndani, wewe umeshapewa kazi, lakini kwa nini unaukwepa mfumo, anau-*by pass* mfumo. Mfumo anauzima unakuwa haufanyi kazi, matokeo yake zile hela ambazo zilibidi ziingie Serikali Kuu zinaingia katika mikono ambayo siyo sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo nasema na hili nalo tulifanyie kazi. Nasema tena kwanza Mheshimiwa Waziri amenipoteza katika reli, hapa leo naondoka na furaha kubwa sana, yote yale niliyotaka kuzungumza leo nimeishia hapa. Nasema Mwenyezi Mungu awabariki tupate viongozi kama Mheshimiwa Innocent Bashungwa, anayetaka kusikiliza vilio vya Watanzania, yuko tayari kusikiliza kero za Watanzania. Waheshimiwa Mawaziri wajifunze kwa Mheshimiwa Bashungwa kutoka hapo migogoro mingine mingine itapotea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine la mwisho, uwakala wa upimaji wa viwanja katika halmashauri imekuwa ni mwiba na hii inaonekana Wizara ya Kisekta haiko pamoja na halmashauri. Mtu wa halmashauri anapima kivyake na Wizara inafanya kazi yake, matokeo yake mfumo huu wa upimaji wa viwanja umesabisha migogoro Tanzania nzima. Ningeomba tukae chini tuangalie hii mifumo isiyoongea tutaisaidiaje. Kwa mfano, mfumo wa ardhi hauongei na wa halmashauri, lakini vilevile pesa za majengo

ambazo zinatolewa katika baadhi ya taasisi ikiwa katika Wizara zingine kama Kazi …

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Riziki kuna taarifa nyingine kutoka kwa Mheshimiwa Jerry Silaa, Mheshimiwa Waziri.

**TAARIFA**

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Mama Riziki Lulida, ni kweli kumekuwa na matatizo mengi kwenye upimaji wa ardhi kwenye maeneo mengi nchi nzima lakini hatua zimeanza kuchukuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mosi, Serikali imesha-*centralize* utendaji kazi wa watumishi wa ardhi nchi nzima kwa ngazi ya wilaya, mikoa na Wizara ya Ardhi. Hivi ninavyozungumza tumeendelea kutoa maelekezo na kupitia Bunge lako Tukufu, watumishi wote wa ardhi wa ngazi za wilaya wazingatie taaluma zao wanapofanya kazi za ardhi; lakini maeneo mengi yenye mkwamo ikiwemo Mkoa wa Dar es Salaam ambapo zoezi la urasimishaji lilikuwa na mkwamo, tayari kupitia mradi wa *Land Tenure Improvement Project (LTIP)* tumeanza kuukwamua. Nilithibitishie Bunge lako kwamba kufikia Disemba 31 maeneo mengi matatizo haya yatakuwa yamekwisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Riziki unaipokea hiyo taarifa?

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea hiyo taarifa na yeye vile vile nina msururu wa watu ambao nitakwenda nao kwake Mheshimiwa Silaa kwa heshima na taadhima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima alionionesha nakwenda kwake na ma-*file* ya watu ambao wanadai kihalali, wamenyang'anywa maeneo yao lakini bado kuna usumbufu mkubwa wanakutana nao. Vile vile na yeye ni Waziri wa pili nasema Mwenyezi Mungu ambariki. Tunataka Mawaziri wenye kusimamia, kuleta heshima kwa Mheshimiwa Rais. Mheshimiwa Rais anataka mambo kama haya, majibu ambayo hayana kando kando, majibu ambayo hayana ulinzi, kwenda kuwalinda watu ambao wanatufanyia vurugu, tunataka vitu vilivyonyooka. Mimi na Mheshimiwa Waziri tunataka twende kwenye rula, Mheshimiwa Innocent Bashungwa twende kwenye rula. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nasema nikushukuru sana na Mwenyezi Mungu awabariki sana. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Riziki Lulida kwa kutumalizia na kuwa mchangiaji wetu wa mwisho kwa siku hii ya leo. Nami niwapongeze wote kwa kazi nzuri mliyofanya na kuwajibika ipasavyo kwa siku nzima ya leo, naamini kabisa michango yote ya Wabunge ni kwa nia njema kabisa ya kutaka kuliendeleza na kujenga Taifa letu.

Baada ya kusema hayo, niwatakie jioni njema na naahirisha shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu kamili asubuhi.

*(Saa 1.33 Usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Ijumaa, Tarehe 3 Novemba, 2023 Saa Tatu Asubuhi)*